Mtuma Mteule

Muhammad Mustafa

صلى الله عليه وسلم

Othman Nuri Topbash

2

ERKAM PUBLICATIONS

Istanbul / 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

Mtume Mteule Muhammad Mustafa ﷺ

- 2 -

Othman Nuri Topbash

Jina la Asili: Hazret-i Muhammed Mustafâ -Sallâllâhu Aleyhi ve Sellem- 2
Mwandishi: Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu: Abdi Mohamed Adam
Mfasiri: Juma Mwakimatu
Mhariri: Madaila Dalidali
Msanifu jalada: Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na: Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov
ISBN: 978-9944-83-681-4
Mchapaji: Erkam Printhouse
Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey
Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748
Barua pepe: info@islamicpublishing.org
Tovuti: www.islamicpublishing.org
Language: Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

Mtume Mteule Muhammad Mustafa

ﷺ

- 2 -

Othman Nuri Topbash

ERKAM PUBLICATIONS

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote." (al-Anbiya, 107)

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ

"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma." (at-Tawbah, 128)

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْلَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu." (Al-i Imran, 31)

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا

"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu." (al-Ahzab, 40)

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَآمَنُوا بِمَا نُزِّلَ عَلَى مُحَمَّدٍ وَهُوَ الْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ بَالَهُمْ

"Na walio amini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyo teremshiwa Muhammad - nayo ni Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi - atawafutia makosa yao na ataitengeneza hali yao." (Muhammad, 2)

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Nitakuwa wa kwanza kufika kwenye Birika la Kawthar na nitakutana nanyi huko! Makutano yetu na kwenye Birika. Ninaliona sasa hivi! Nitatoa ushuhuda kwa niaba yenu! Wakati huu, nimepewa hazina za ardhi na funguo zake. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, sihofii kuwa mtarejea kuwa makafiri baada ya kuondoka kwangu! Bali ninahofia kwamba utasukumwa katika tamaa za dunia na kuoneana husda, mkiuana nyinyi kwa nyinyi na kuangamia kama walivyoangamiwa wale waliokuwa kabla yenu!" (Bukhari, Janaiz, 73; Muslim, Fadail, 31)

"Hakika, nitaenda kabla yenu na kuwasubiri! Tambueni kuwa makutano yetu Siku ya Kiyama ni kwenye Birika la Kawthar. Atakaye kukutana na mimi kesho basin a aiepushe mikono na ulimi wake dhidi ya dhambi." (Bukhari, Salat, 80; Ibn Saad, II, 227)

Chochote ambacho ulimwengu unacho, nia zawadi Yake,
Jamii ni wadeni Wake, kila mtu ni mdeni wake,
Wanadamu wote ni wadeni wa Mtu huyo Mtakatifu,
Mola wangu, tufufue siku ya Kiyama tukiwa na fikra hizi akilini mwetu!

Mehmet Akif Ersoy

MWAKA WA KWANZA WA HIJRA

Maisha ya Mtume Aliyebarikiwa ﷺ Katika Mji wa Madina

Kuhama kwa Mtume ﷺ kwenda Madina kuliashiria zama mpya na kuleta ukurasa mpya kabisa katika historia ya Uislamu na Waislamu.

Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa mkimbizi katika mji wa Madina. Bali, alikuwa mhandisi mkuu wa ulimwengu wa baadaye, dira yake, kiongozi wa dola mpya ya Kiislamu, kwa mukhtasari, alikuwa ndio uhai wake na roho yake. Kwa kuwasili kwake mjini Madina, vugu-vugu la Uislamu na usambaaji wake ulimwenguni vilipata nguvu na msukumo wa ajabu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliendelea kuwa mgeni katika nyumba ya Abu Ayyub al-Ansari ؓ kwa kipindi cha miezi saba mpaka ujenzı wa Msikiti wa Madina, Masjidun-Nabi, ulipokamilika. Lakini ugeni wake katika nyumba ya Abu Ayyub, mbeba bendera ya Mtume ﷺ, ulikuwa na historia inayoanzia karne kadhaa nyuma.

Miaka mia saba kabla, *Tubba' Abu Karib*, mmoja wa wafalme wa Yemen, alikuja Madina, wakati huo ikijulikana kama Yathrib. Baada ya kupata taarifa kutoka kwa wanzuoni wa Kiyahudi kuwa atadhihiri Mtume kutoka Makka ambaye atahamia Madina, aliamua kujenga nyumba katika mji huo. Kisha alikabidhi barua iliyogongwa muhuri wa dhahabu kwa mwanachuoni mkubwa kabisa

wa Kiyahudi katika mji wa Madina, akamuomba kuwa, iwapo hatadiriki zama za Mtume huyo, aikabidhi barua hiyo kwa kizazi cha baada yake na ikabidhiwe kwa Mtume huyo anayengojewa.[1]

Baada ya kufanya hivyo, Tubba' akatangaza mapema kabisa imani yake kwa Mtume ﷺ na kusilimu.[2]

Baada ya kupita miaka mingi, hatimaye nyumba hiyo, iliyo mashariki mwa Msikiti wa Mtume ﷺ, ilikabidhiwa kwa Abu Ayyub Khalid ibn Zayd رضي الله عنه, ambaye alijulikana kuwa miongoni mwa kizazi cha mwanachuoni huyo tuliyemueleza hapo juu.

Wale waliokuwa wameitunza barua ya *Tubba'* walimtuma Abu Layla, mtu mwaminifu wa kabila la Sulaym, kwenda na barua hiyo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, baada ya kusikia kuwa anakaribia kufika Madina. Abu Layla alikutana na Mtume ﷺ katika njia ielekeayo Makka; japokuwa Mtukufu Mtume ﷺ ndiye aliyeanza kumuita:

"Wewe ndiwe Abu Layla?"

"Ndiyo", alijibu.

"Ninaamini unayo barua ya Tubba'. Naweza kuiona?"

Abu Layla hakuwa amewahi kumuona Mtume ﷺ kabla ya siku hiyo. Alishtuka na kushikwa na mshangao.

"Wewe ni nani? Kwa hakika huonekani kuwa kama kuhani… lakini ulijuaje kuwa ninayo hiyo barua?" aliuliza kwa mshangao.

"Utulize moyo wako, kwani mimi ndiye Muhammad. Tafadhali nikabidhi barua", alisema.

1. Ibn Asakir, III, 334-335; Samhûdî, I, 188-189.
2. Ahmad, V, 340.

Abu Layla aliitoa barua na kuikabidhi kwa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ. Baada ya Abu Bakr ؓ kuisoma barua hiyo kwa sauti, Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, mara tatu:

"Salaam kwa ndugu yetu mwema, *Tubba*!"

Baada ya kukabidhi barua, Abu Layla alishauriwa kurejea Madina, naye akafanya hivyo na kurejea akiwa amebeba habari njema za ujio wa Mtume ﷺ, ambapo alipewa kiapo cha utii na kila mkazi wa Madina kama sehemu ya kuonesha shukrani zao kwake.[3]

Abu Ayyub al-Ansari:
Mbeba bendera wa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ

Akiwa amebarikiwa kupata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mtume Bora ﷺ kwa kipindi cha miezi saba katika nyumba yake adhimu yenye ghorofa, mwanzo Abu Ayyub ؓ alimuomba sana Mtume ﷺ akae sehemu ya juu ya nyumba hiyo, lakini mara zote alikuwa akipata jibu lifuatalo:

"Ewe Abu Ayyub! Usiwe na wasiwasi wowote… sehemu ya chini ni bora na ni nzuri zaidi kwetu." Hivyo, sehemu ya chini ndipo ambapo Mtukufu Mtume ﷺ alianza kuishi.

Katika kumhudumia mgeni wao wa heshima, Mtume ﷺ, kwa upendo na heshima ya kipekee, Abu Ayyub ؓ na familia yake walifikia hatua ya kujibana ukutani, wakitaka kulala usawa wa mahali alipolala Mtukufu Mtume ﷺ.

Siku moja jagi lilivunjika na kumwaga maji yote sakafuni. Kwa hofu ya kuwa maji hayo yanaweza kumdondokea mgeni wao mtukufu, mara moja Abu Ayyub alichukua shuka lao moja na la pekee, na kuanza kuyakausha maji hayo akiwa na wasiwasi mkubwa.

3. Ibn Asakir, III, 335; Aynî, IV, 176.

Japokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliendelea kumhakikishia Abu Ayyub kuwa alifurahia kuishi upande wa chini wa nyumba hiyo, lakini Abu Ayyub ؓ alimsisitizia na kumuomba kwa upole akisema:

"Hatuwezi kwenda ghorofani mpaka uende!" Hapo ndipo Mtume ﷺ akabadilisha malazi na kwenda upande wa juu.[4]

Katika kipindi hicho cha ugeni wa Mtukufu Mtume ﷺ katika nyumba hiyo, Abu Ayyub al-Ansari na familia yake walikuwa wakimpa chakula walichokiandaa wenyewe. Pindi mabaki ya chakula yanaporudishwa, Abu Ayyub alikuwa akiangalia mahali palipoguswa na Mtume ﷺ wakati wakula na kula sehemu hiyo kwa ajili ya *tabarruk*, yaani kwa ajili ya kupata Baraka. Siku moja alimpelekea Mtukufu Mtume ﷺ sahani iliyojaa vitunguu vya maji na vitunguu thaumu, vikarejeshwa bilakuguswa. Abu Ayyub ؓ baada ya kutoona alama ya vidole vya Mtume ﷺ kwenye chakula hicho, akawa na wasiwasi na kuenda kumuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, je chakula hiki ni haramu kuliwa?"

"Hapana, sio haramu", Mtume ﷺ alijibu. "Bali si mpenzi wa chakula hicho, kwa maana ni mtu ninayezungumza na malaika."

"Kama hukipendi, nami pia sikipendi," alisema Abu Ayyub ؓ.

Lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamshauri: "Lakini waweza kula chakula hicho."

Hata hivyo, huo ndio ukawa mwisho wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kupikiwa chakula hicho.[5]

4. Muslim, Ashriba, 171; Ibn Hisham, II, 116.
5. Muslim, Ash ri ba, 170-171; Ibn Hisham, II, 116.

Tukio hili linaonesha kiwango cha umakini wa Mtukufu Mtume ﷺ katika kujizuia kusababisha hata karaha ndogo kwa viumbe wote, binadamu na malaika pia. Hakika hii ni ajabu!

Heshima na upendo wa Abu Ayyub رضي الله عنه kwa Mtukufu Mtume ﷺ havikubadilika hata baada ya mgeni huyu kuondoka.

Miaka mingi baadaye, japokuwa alikuwa ameshakuwa na umri wa miaka themanini, alitaka kupata heshima ya kuwa miongoni mwa wale waliochuma Baraka kama walivyotabiriwa na Mtume ﷺ katika maneno yake yafuatayo:

"Hakika Constantinople itafunguliwa…kamanda wake ni kamanda mwenye kheri; na askari wake ni askari wenye kheri," (Ahmad, IV, 335; Hakim, IV, 468/8300). Pamoja na kuwa na umri mkubwa, Abu Ayyub alishiriki katika kampeni mbili za kuufungua mji huo, na ikiwa kama maandalizi ya ufunguzi wa kweli ambao ungetokea karne nyingi baadaye, aliyatoa maisha yake kwa ajili ya tukio hilo adhimu. Muda mfupi kabla ya kufariki dunia, katika kuifanya maiti yake kuwa kichocheo cha wanajeshi wa Kiislamu kuutwaa mji huo baada ya kake, aliwaambia wale waliokuwa karibu yake:

"Mtanizika sehemu ya mwisho kabisa mtakayokanyaga…"[6]

Anas ibn Malik: Mtumishi wa Mtukufu Mtume ﷺ

Anas رضي الله عنه anasimulia:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowasili Madina, baba yangu wa kufikia, Abu Talha, alinichukua kwa mkono na kunipeleka mbele yake.

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Anas ni mtoto maridadi', alisema. 'Mpe nafasi ya kukutumikia!' na hivyo ndivyo nilivyokuja kuwa mhudumu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Nilimtu-

6. Tazama: Ibn Saad, III, 484-485.

mikia kwa muda wa miaka kumi, wakati wa vita na amani. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, sikumsikia akinifokea kwa kufanya kitu ambacho sikutakiwa kukifanya wala kwa jambo ambalo nilishindwa kulifanya." (Muslim, Fadhaail, 52)

Kwa mujibu wa maelezo mengine, tukio la Anas kuwa mhudumu wa Mtukufu Mtume ﷺ lilitokea kama ifuatavyo:

Mtukufu Mtume ﷺ alipowasili Madina, wanaume na wanawake wa Kiansari walimpokea kwa zawadi mbalimbali. Kwa upande mwingine, Ummu Sulaym alijawa na simanzi kwa kutokuwa na chochote cha kumzawadia. Baadaye alimchukua mwanaye, Anas, na kumpeleka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Alimuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, je itafaa ukimruhusu Anas akutumikie?" Mtukufu Mtume ﷺ akamkubalia. (Samhudi, I, 271)

Anas رضي الله عنه anaeleza:

"Siku mojaMjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitaka kunituma mahali fulani.Ingawa nilionekana kukataa, nikisema 'Sitakwenda', ndani ya moyo wangu nilikuwa nimeshakubali kuwa nitakwenda; hasa ikizingatiwa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuwa akiniagiza. Hivyo nilikwenda. Njiani niliwaona watoto wakicheza mtaani nikaungana nao kwa muda. Baada ya muda nikahisi mtu akija kutokea nyuma yangu na kunigusa taratibu shingoni. Nilipogeuka, nikakuta ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akitabasamu.

'Ewe mwanangu Anas umeshakwenda mahali nilipokuagiza?' aliuliza.

'Ninakwenda sasa hivi, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!' nilijibu kwa haraka." (Muslim, Fadhaail, 54)

Anas رضي الله عنه anasimulia tukio jengine:

"Siku moja, baada ya kumaliza kazi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ nilienda nje kuungana na watoto, kwa kufikiri kuwa atajipumzisha mchana. Wakati nimemakinika na kuchukuliwa na mchezo wa watoto, ghafla Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitokea. Aliwatolea salamu watoto kisha akaniita na kuniagiza mahali fulani. Hivyo nikaenda. Alikaa na kusubiri chini ya kivuli mpaka nilipore-jea. Mpaka ninamaliza majukumu yangu nilikuwa nimechelewa kurudi kwa mama; nahivyo mama yangualiniuliza:

'Kwanini umechelewa?'

'Mtume wa mwenyezi mungu aliniagiza sehemu fulani kwa ajili ya jambo fulani', nilisema.

'Ni jambo gani hilo?' aliuliza.

'Basi itunze siri ya mwenyezi mungu', aliniusia."

Baadaye, Thabit ambaye ameripoti hadith hii ya Anas رضي الله عنه, alisema:

"Anas aliniambia kwamba 'ewe Thabit kama ningemjuza mtu yeyote, basi mtu huyo angekuwa wewe!'" (Ahmad, III, 195)

Kama tunavyoona, Mtukufu Mtume ﷺ aliamiliana na watoto kama alivyoamiliana na watu wa rika lake nakuwapa baadhi ya siri. Katika kuimarisha upendo na huruma kwao katika hatua ya maisha yake, Mtume wa Rehma ﷺ aliwatambua watoto, akachanganyikana nao kwa kiwango chao, na hatimaye akapenya ndani ya nyoyo zao. Mfano mzuri wa muamala maridhawa aliokuwa nao kwa watoto unapatikana katika hadhith zake kadhaa wa kadhaa,zikiwemo had-ith mbili zifuatazo:

"Ukiwana wototo, kuwa mtoto unapokuwa karibu nao…" (Daylami, III, 513)

"Amilianeni na watoto vizuri na kuyakamilisha malezi yao." (Ibn Majah, Adab, 3)

Vile vile, maisha ya mfano ya Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ yanatupatia muongozo kuhusu malezi ya watoto. Ajabu iliyoje ya malezi aliyompatia Anas kiasi kwamba hakuwahi kuwa na hisia ya kumkasirikia mtoto huyo hata mara moja! Mtume ﷺ aliyekuwa na umri wa miaka hamsini na tatu alipenya katika moyo wa Anas mwenye umri wa miaka kumi, akitaniana naye kama rafiki yake na kumpa siri zake pale inapohitajika; alilelewa na Mtukufu Mtume ﷺ kiasi kwamba, licha ya kuwa mtoto, Anas ؓ alikuwa kama mtu mzima na kuzitunza kwa dhati siri za Mtukufu Mtume ﷺ. Bila shaka, kilichomuinua Anas ؓ kwenye daraja hiyo ya ukomavu ni mbinu adhimu ya malezi iliyotumiwa na Mtukufu Mtume ﷺ.

Maridhiano ya Undugu baina ya *Muhaajiruun* na *Ansaar*: *Muakhaat*.

Tangu alipoanza kazi yake ya kuwalingania watu, bila kujali rangi au makabila yao, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷻ aliwachukulia wale wote walioingia katika Uislamu kuwa watu walio sawa na kuimarisha undugu wa Uislamu baina yao. Alianzisha maridhiano ya*muakhaat*, yaani undugu, mara mbili, mmoja kabla ya Hijra na wa pili baada ya Hijra. Maridhiano ya Undugu mjini Makka yalihusisha kutengeneza undugu baina ya Waislamu wa Kiqurayshi na watumwa walioachwa huru. Kwa mfano, Zayd ibn Harithah na Hamza, walitangazwa kuwa ni 'ndugu', kama ilivyokuwa kwa Salim, aliyewahi kuwa mtumwa wa Abu Hudhayfah na Abu Ubaydah ibn Jarrah, na pia Bilal Habashi na Ubaydah ibn Harith ؓ.[7]

7. Ibn Seyyidinnâs, I, 321; Ibn Habîb, uk.70; Ibn Abdilbar, ad-Durar, uk. 90.

Baada ya mshikano huo ulioanza tokea siku za mwanzo za Uislamu, Waislamu walionesha undugu mwingine baada ya Hijra.

Pindi *Muhajirun* walipokanyaga ardhi ya Madina,mgogoro mkali uliibuka baina ya Ansaar, ambao walikuwa wakishindana kwa shauku na hamasa kubwa kuwakaribisha ndugu zao wapya. Kufuatia mgogogro huo, walilazimika kupiga kura ili kuamua nani atakayekuwa mwenyeji wa nani.[8] Miezi mitano baada ya kuwasili mjini Madina, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimfanya kila *muhajir* kuwa ndugu na mtu katika *Ansar*; maridhiano hayo yalifanyika katika nyumba ya Anas ibn Malik رضي الله عنه.[9]

Miongoni mwa mifano ya undugu huo, Abu Bakr alifanywa kuwa ndugu wa Kharijah ibn Zayd, Omar na Utbah ibn Malik, Abu Ubaydah na Saad ibn Muadh, Othman na Aws ibn Thabit,[10] Bilal Habashi na Abdullah ibn Abdurrahman,[11] Salman na Abu Darda,[12] Salim na Muadh ibn Maiz,[13] na Ammar akawa ndugu wa Hudhayfah رضي الله عنه.[14] Katika kuwaunganisha watu hawa, Mtukufu Mtume ﷺ alizingatia ufanano wa kimaadili baina ya watu husika.

Kila familia ya mhamiaji ilipata makazi katika nyumba ya mwenyeji wa Madina. Hivyo, Maswahaba ambao walitangazwa kuwa ni ndugu walitakiwa kufanya kazi pamoja na kushirikiana kile watakachopata.*Ansar* walijitolea ardhi yao ya ziada kumpa Mtukufu Mtume ﷺ, naye akazigawa kwa *Muhajiruun*. Bado *Ansar*

8. Bukhari, Janaiz, 3; Manaqıbu'l-Ansar, 46.
9. Bukhari, Adab, 67.
10. Ibn Hisham, II, 124-125.
11. Ibn Saad, III, 233, 234.
12. Bukhari, Adab, 67.
13. Ibn Abdilbar, II, 567.
14. Hakim, III, 435/5657.

hawakuishia hapo, wakaenda mbali zaidi kumsisitizia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷻ kuwa:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, yagawe mashamba yetu pia miongoni mwa ndugu zetu *muhajruun*!"

"Hilo haliwezekani," Mtukufu Mtume ﷺ alisema, ambapo Ansar walitoa pendekezo lifuatalo kwa *Muhajiruun*:

"Basi nyinyi mtamwagilia na kuitunza miche ambapo tutagawa mavuno pamoja nanyi!" Mtukufu Mtume ﷺ alipokubali, pande zote zikakubaliana. (Bukhari, Harth, 5)

Undugu huu ulijikita kwenye kuwasaidia kimaada na kimaanawi Waislamu ambao walikuwa wameacha kila kitu chao Makka na kuhamia Madina ili wapate kuanza mwanzo kabisa, ambapo *Ansar* wa Madina waliwakaribisha kwa mikono miwili kwa lengo la kuwafanya *Muhajiruun* wasahau machungu ya kufukuzwa katika mji wao kwa sababu tu ya imani yao na kuwakaribisha kwa ukunjufu mjini Madina, makazi yao mapya, na kuwaunganisha pamoja Waislamu kwa kuimarisha mshikamano baina yao.

Maridhiano hayo yaliyotokana na upendo wa imani na kuepukana na unafiki, yakifika mbali mpaka kwenye haki, usawa na kusaidiana, yakijumuisha pia suala la kurithiana.[15] Kwa wa maridhiano hayo, 'ndugu' hao walikuwa walinzi watakaolindana na kurithiana. Japokuwa maridhiano ya undugu yaliendelea kufanya kazi, kifungu kinachohusu kurithiana kiliondolewa baadaye kwa ufunuo ulioteremka baada ya Vita ya Badr na kulifanya suala la kurithiana kuwahusu ndugu wa damu.[16]

Ibn Abbas ﷺ anaelezea kuhusu suala hilo:

15. Bukhari, Kafala, 2; Adab, 67.
16. See, al-Anfal, 72-75; Bukhari, Faraid, 16.

"kutokana na undugu ulioasisiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu, *Muhajir* (mhamiaji kutoka Makka) alikuwa na haki ya kurithi mali za ndugu yake wa Kiansari, kuliko wale wenye uhusiano naye wa damu. Lakini aya isemayo:

وَلِكُلٍّ جَعَلْنَا مَوَالِيَ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالأَقْرَبُونَ

"Na kila mmoja tumemwekea warithi katika waliyo yaacha wazazi wawili na jamaa", (an-Nisa, 33) iliondosha ada hii. Na kwa kuwekwa kipande hiki cha aya:

وَالَّذِينَ عَقَدَتْ أَيْمَانُكُمْ فَآتُوهُمْ نَصِيبَهُمْ

"…Na mlio fungamana nao ahadi wapeni fungu lao", haki za undugu baina ya *Muhajiruun* na *Ansar* ukaishia kwenye kusaidiana, kuungana mkono na kuombeana kheri. Hivyo mirathi ya kisheria kwa misingi ya undugu huo ikaondolewa. Lakini mtu angeweza kutoa mirathi kwa hiari kwa njia ya wosia ilmradi isizidi theluthi ya mali yake." (Bukhari, Tafsir, 4/7; Abu Dawud, Faraid, 16/2922)

Muakhaat ulisaidia kukomesha mapigano baina ya *Aws* na *Khazraj*, makabilaya Madina, na kuanzisha undugu uliokuwa imara zaidi ya undugu wa damu. Kutokana na ukomavu wa undugu huo, mtu alikuwa akipata shida sana kusubiri mapambazuko ili aweze kumuona ndugu yake. Kama wakıwa hawajaonana kwa mıaka mıngı, pindi wanapokutana huulizana kwa shauku juu ya hali zao. Ingekuwa nadra sana kupita siku tatu bila kutembeleana. Ni undugu uliosifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kupigiwa mfano na Qur'an Tukufu.[17]

17. Tazama, al-Hashr, 9.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiweka misingi ya jamii na dola ya Kiislamu mjini Madina. Hivyo kilichohitajika kwanza ni kutengeneza na kuasisi umoja na mshikamano wa kijamii, na hakuna jambo bora kama kupendana na kusaidiana. Kwa sababu hiyo, maridhiano ya undugu yaliyoasisiwa na Mtume ﷺ baina ya *Muhajirun* na *Ansar* yalikuwa nguzo muhimu zaidi katika kutengeneza jamii isiyo kifani katika historia ya mwanadamu.

Mtukufu Mtume ﷺ aliiasisi jamii changa ya Kiislamu juu ya msingi wa undugu wa Kiislamu, badala ya msingi wa ukabila, rangi au matabaka ya kijamii baina ya watumwa na watwana, matajiri na maskini, na kadhalika. Jamii ya Kiislamu ilijengwa kwa kuwaweka pamoja watu wa aina na silika tofauti tofauti.

Ubora wa *Muhajiruun* na *Ansaar*

Muhajir, kwa maana ya mtu aliyehama kutoka sehemu moja kwenda nyingine, ni jina walilopewa Waislamu wa Makka waliolazimishwa kuhamia Madina kutokana na mateso na manyanyaso mazito waliyokabiliana nayo.

Muhajirun walihamia Madina, wakiwa wameacha nyumba kila kitu walichokuwa nacho isipokuwa kiasi kidogo tu walichoweza kukibeba. Makafiri wa Makka walikuwa wamezizuia na kuzichukua mali zao. Kwa hakika hasara ya kiuchumi ya Waislamu ilikuwa kubwa. Lakini hawakuyakodolea macho yao kwenye mali wala hawakuwa wakitafuta utajiri wa kidunia; walikuwa wamepata ladha ya kilele cha imani. Hivyo, walikuwa tayari kukitoa mhanga chochote walichokuwa nacho katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ombi lolote la Mtukufu Mtume ﷺ walilichukulia kuwa ni amri inayotakiwa kutekelezwa, wakiwa tayari kabisa kumtumikia kwa moyo wote huku wakisalimu amri kwa kusema "wazazi wetu wawe

fidia kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mung", maneno yaliyotoa mwangwi wa hisia za kujitoa kwa moyo walizokuwa nazo ndani ya vifua vyao. Mojawapo ya mifano yenye kusisimua unaelezwa na Suhayb ibn Sinan, almarufu kama Suhayb ar-Rumi ﷺ, ambaye aliwaonesha makafiri mahali alipokuwa ameficha mali zake mjini Makkah pale walipojaribu kumzuia kuhamia Madina. Akiwa ameshapata mateso makali kutoka kwa makafiri wa Makka, Suhayb ﷺ alianza safari ya kuhamia Madina baada tu ya Ali ﷺ. Kundi la makafiri lilimfuata nyuma na kumkuta njiani.

"Ulipokuja Makka ulikuwa dhaifu na maskini", walisema. "Lakini sasa umekuwa tajiri mkubwa na unataka kuondoka pamoja na mali zako? Hilo sio jambo rahisi!"

Suhayb akateremka kutoka juu ya farasi wake, akachukua mishale kwenye mkoba wake na kuwa tayari kwa makabiliano:

"Mnatambua vyema kuwa mımı ni miongoni mwa watupaji hodari zaidi wa mishale. Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba, kama ni lazima kurusha mishale hii niliyonayo na baada ya mishale kuisha nitumie upanga wangu, sitasita kufanya hivyo…na kwa muda ambao nina silaha hizi mkononi mwangu, hamtaweza kunisogelea hata hatua moja. Mtaweza tu kunisogelea kama nitaishiwa kabisa na sialaha hizi. Sasa, kama nikiwaambia mahali mahali zilipo mali zangu mtaniacha niondoke?"

Makafiri walikubaliana na wazo hilo. Hapo Suhayb ﷺ akawaelekeza mahali zilipo mali zake naye akaendelea na safari yake bila kubughudhiwa. Katikati ya mwezi wa Rabiul-awwal aliwasili Quba na kuungana na Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye alikuwa amesuhubiana na Abu Bakr na Omar ﷺ. Mbele yao palikuwa na mkungu wa tende za Umm Jirzan zilizokuwa zimeletwa na Kulthum ibn Khidm. Suhayb ambaye alikuwa amevimba macho na njaa kali alianza kula tende hizo. Omar ﷺ akasema kwautani:

"Mtazame Suhayb, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Macho yake yamevimba lakini hiyo haimzuii kuchukua tende!" Mtukufu Mtume ﷺ, naye akasema kwa utani:

"Unakula tende mbivu japokuwa macho yako yamevimba?"

"Nimeziona tende kupitia sehemu ya macho ambayo haijavimba!" alijibu Shayb ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ alijibu kwa tabasamu na kuonesha jinsi Suhayb alivyotoa mali yake kuwapa Makafiri kama fidia ya uhai wake, akasema:

"Suhayb ndiye mshindi… Suhayb ni mshindi. Ewe Suhayb, hakika biashara yako imekupatia faida!" (Ibn Sad, III, 226-230; Hakim, III, 450, 452)

Wakati Waislamu wa Makka wakitoa mhanga mkubwa chini ya mazingira magumu katika kujaribu kukimbilia Madina, Waislamu wa Madina walikuwa wakiwakaribisha kwa upendo wa *iman*, ambao ulionesha ukubwa wa tabu ambayo wote walikuwa wakikabiliwa nayo. Baadhi ya *Muhajiruun*, kwa kutotaka kuwa mzigo kwa Ansaar ambao hawakuwa na choyo hata kidogo katika kushirikiana walichokuwa nacho pamoja na ndugu zao muhajiruun, hawakuwa wakikubali kupokea vitu wanavyopewa bure, huku wengine walikuwa wakikubali kufanya makubaliano ya kufanya kazi katika mashamba ya Ansaar ili waingize kipato walichokifanyia kazi kwa mikono yao. Baadhi ya Muhaajiruun walipendelea zaidi kujishughulisha na kazi ambayo walikuwa na uzoefu nayo zaidi: biashara. Miongoni mwao ni Abdurrahman ibn Awf ﷺ. Ingawa Saad ibn Rabi ﷺ, ndugu yake wa Kiansar, alikuwa amempa nusu ya mali yake, lakini alikataa na kusema:

"Mwenyezi Mungu aipe Baraka mali yako na kuijalia kheri familia yako. Nioneshe tu mahali lilipo soko la Madina." Hivyo alianza safari yake ya biashara, na ndani ya muda mfupi akawa tajiri.

Muhaajiruun, watu wa mwanzo kuusikia Wahyi, ambao walikabiliana na hatari zote zilizotokana na kumuamini Mjumbe wa Mwenyezi ﷺ na ambao walipitia mateso makali kiasi cha kuyakimbia makazi yao, walipata heshima ya kusifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.Japokuwa hawakuwa wakisubiri manufaa ya kidunia, bado waliviacha vyote walivyokuwa navyo ili tu wapate kuishi kulingana na dini yao. Hivyo, sio tu kwamba Muhajiruun walikuwa wakionesha mfano wa kujitoa kwa moyo, bali pia walikuwa wakitekeleza wajibu wa kidini, kwa sababu Qur'an ilikuwa ikiwalaumu wale waliokuwa wakikataa kufanya Hijra licha ya kuwa na uwezo wa kufanya hivyo.[18]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatoa ahadi ya kuwasamehe Muhaajiruun dhambi zao na kuwaingiza Peponi:

فَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَأُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأُوذُوا فِي سَبِيلِي وَقَاتَلُوا وَقُتِلُوا
لَأُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأُدْخِلَنَّهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ثَوَابًا
مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الثَّوَابِ

"Basi walio hama, na walio tolewa makwao, na wakateswa katika Njia yangu, na wakapigana, na wakauliwa, kwa yakini Mimi nitawafutia makosa yao, na kwa yakini nitawaingiza katika Mabustani yanayo pita mito kati yake. Hayo ndiyo malipo yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu kwake yapo malipo mema kabisa." (Al-i Imran, 195)

18. Tazama: an-Nisa, 97.

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ هَاجَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا فُتِنُوا ثُمَّ جَاهَدُوا وَصَبَرُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ

"Kisha hakika Mola wako Mlezi, kwa wale walio hama makwao baada ya kuteswa, kisha wakapigania Dini na wakasubiri, bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." (an-Nahl, 110)

Kuhusiana na hilo, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Muhaajiruun wataingia Peponi miaka sabini kabla ya watu wengine na kufurahia neema zake… ambapo watu watakuwa wakisubiri kuhesabiwa." (Haythami, X, 15)

Mbali na malipo makubwa watakayopata huko Akhera, vilevile Muhaajiruun walipata baraka nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu hapa hapa duniani, kutokana na kujitoa kwao kwa moyo:

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا ظُلِمُوا لَنُبَوِّئَنَّهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَلَأَجْرُ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ ۚ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

"Na wale walio hama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baada ya kudhulumiwa, bila ya shaka tutawaweka duniani kwa wema; na ujira wa Akhera ni mkubwa zaidi; laiti kuwa wanajua!" (an-Nahl, 41)

Tena, kutokana na tabu walizozipata, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwatengea fungu kubwa la ngawira ikilinganishwa na watu wengine. Qur'an Tukufu inasema kuhusu jambo hilo:

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

"Wapewe mafakiri Wahajiri walio tolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio wa kweli." (al-Hashr, 8)

Mbali na uchungu wa kukumbuka nyumbani ambao uliwashika baada ya kuwasili Madina, kwa muda mrefu Muhajirun pia walishindwa kuizoea hali ya hewa ya Madina, wakashambuliwa na homa na maradhi pia. Bibi Aisha ﵂ alipomshuhudia baba yake Abu Bakr pamoja na Bilal Habashi ﵁ wakiwa wamedhoofika kiafya pamoja na kutamalakiwa na shauku kubwa ya kuukumbuka mji wa Makka, alimtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ juu ya hali hiyo, ambapo aliomba akisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu…ifanye Madina kuwa kipenzi chetu kama ulivyoifanya Makka au zaidi! Yakithirishe mazao yake! Ewe Mwenyezi Mungu…iboreshe hali ya hewa ya Madina na homa na malaria yake ipeleke Juhfah!"[19] (Bukhari, Fadail'ul-Madina, 12; Muslim, Hajj, 480)

Ansaar, yaani wasaidizi, ni jina walilopewa Waislamu shupavu wa Madina waliowakaribisha *Muhaajiruun* kutoka Makka, wakashirikiana nao kwa moyo mmoja katika rasilimali zao, na zaidi wakamuunga mkono Mtukufu Mtume ﷺ katika kazi yake.

Ghaylan ibn Jarir ﵁ anasimulia:

19. Wakati huo, Juhfah ni eneo lililokuwa likikaliwa na Wayahudi na waabudu masanamu, ambao mar azote walikuwa wakiwasaidia maadui wa Uislamu katika kuwakandamiza Waislamu na kupandikiza mbegu za uadui, fitna na uhasama. Mtukufu Mtume ﷺ aliomba hivyo ili kuwafanya washughulishwe na pigo hilo kiasi cha kuwafanya wasifikirie kuwasadia waabudu masanamu wa Makka nakusababisha shari. (Aynî, X, 251)

"Siku moja nilimuuliza Anas ﷺ, 'Je neno Ansaar mlikuwa mkilitumia kabla, au mlipewa jina hilo na Mwenyezi Mungu?' naye akajibu, 'Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupatia jina hilo.'" (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 1)

Jamii ya Ansaar iliundwa na makabila mawili pinzani na ndugu ya mjini Madina, yaani Aws na Khazraj. Mwaka wa 11 baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kuanza rasmi majukumu ya Utume, ujumbe wa watu sita kutoka katika kabila la Khazraj ulikuja Makka kwa lengo la kutaka msaada wa Maqurayshi dhidi ya maadui zao wa Aws, ambao walikuwa na ugomvi mkubwa. Huko walikutana na Mtume ﷺ na daawah yake ya kuwalingania watu kwenye Uislamu, na matokeo yake nao wakasilimu. Waliporudi Madina, Khazraj walifanikiwa kuwalingania Aws kwenye Uislamu, kwa matarajio ya kukomesha uhasama wa muda mrefu baina ya ona kuwaunganisha kama ndugu kwa mara nyingine. Hivyo makovu yaliyokuwa kwenye nyoyo zao kutokana na vita vya muda mrefu yakabadilika na kuwa umoja na nguvu, kutokana na *silm*, yaani amani na utulivu wa Uislamu. Baada ya kuungana kwa mara nyingine, mnamo mwaka wa 12 na wa 13 wa Utume, makabila haya ndugu yalituma wawakilishi wao kwenda Makka, ziara zilizozaa Kiapo cha Utii cha kwanza na cha pili cha Aqabah.

Katika kiapo cha pili cha utii, waliapa kumlinda na kumsaidia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na Waislamu wa Makka iwapo watahamia Madina, na hivyo kutoa mchango mkubwa katika Hijra na mwanzo wa zama mpya za Uislamu.

Pindi Mtukufu Mtume ﷺ walipotengeneza undugu baina ya Muhajiruun na Ansar, kila Ansar alimshirikisha ndugu yake *Muhajir* katika nyumba, kazi, mali na kila alichokuwa nacho, na hivyo kuonesha mfano halisi wa mshikamano ambao mtu hawezi kuupata

hata kutoka kwa ndugu yake wa damu. Ikhlasi na usafi wa moyo wa *Ansar* unaelezwa na Qur'an Tukufu:

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

"Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji." (al-Hashr, 9)

Tukio lifuatalo, ambalo ndio sababu ya kuteremka kwa aya iliyotajwa hapo juu, linaonesha kiwango cha kujitoa kwa moyo walichokuwa nacho Ansaar wa Madina:

Mtu mmoja aliyekuwa na njaa kali alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumtaka msaada.

"Nani atakayemchukua ndugu huyu kuwa mgeni wake?" Mtukufu Mtume ﷺ aliwauliza Maswahaba.

"Nitamchukua mimi, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", alisema Abu Talha ؓ kutoka jamii ya Ansaar na kumchukua masikini yule mpaka nyumbani kwake. Alipowasili nyumbani, alielekea ndani moja kwa moja na kumwabia mkewe, "Tumuandalie chochote mgeni wa Mtume wa Mwenyezi Mungu", kisha akauliza, "Je tuna chakula chochote?"

Mkewe akajibu, "Hatuna kitu zaidi ya chakula kidogo sana kwa ajili ya watoto."

"Basi wabembeleze watoto. Wakitaka chakula wafanye walale. Na mgeni wetu atakapoingia, utaizima taa kwa siri. Kisha tutafanya kana kwamba tunashiriki naye katika mlo."

Hivyo walikaa kwa ajili ya mlo. Mgeni alikula, huku wao wakilala na njaa. Asubuhi Abu Talha alikwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ, alipomuona tu akasema:

"Mwenyezi Mungu alifurahishwa na ulichofanya usiku." (Bukhari, Tafsir, 59/6; Muslim, Ashribah, 172-173)

Mtukufu Mtume ﷺ alipowasili Madina, Muhaajiruun walimwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hatujawahi kuona watu wakarimu na wenye moyo kama hawa. Matajiri wao hutoa kwa wingi na masikini wao husaidia katika kukidhi mahitaji yetu. Wameyaondosha kabisa matatizo yetu ya kiuchumi na wametufanya kuwa washirika katika mali zao. Tunahofu kuwa wanaweza kuchukua thawabu zote kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

"Msiwe na wasiwasi", Mtume ﷺ aliwatuliza. "Madamu mnawaombea kwa Mwenyezi Mungu na kuwashukuru kwa yale wanayowafanyia, nanyi pia mtapata thawabu." (Tirmidhi, Qiyamah, 44/2487)

Jabir ؓ anasimulia tukio lifuatalo:

"Baada ya kukusanya mavuno ya tende, Ansaar walikuwa wakiyagawa katika mafungu mawili. Kisha huweka majani ya tende kwenye fungu dogo ili lionekane kubwa kidogo kuliko jingine, kisha huwaambia Muhaajiruun wachague fungu wanalolipenda. Kwa kuwa walitaka ndugu zao Ansar wapate fungu kubwa, wao walikuwa wakichagua fungu linalodhaniwa kuwa dogo, ambapo kumbe fungu wanalochukua wao ndilo lenye tende nyingi. Hivyo Ansar wanakuwa wametimiza walilolitaka kwa wao kuchukua fungu dogo. Tendo hili la ukarimu liliendelea mpaka baada ya ufunguzi wa Khaybar." (Haythami, X, 40)

Mfano mwingine wa ithaar (uungwana) uliooneshwa na Ansaar kwa ndugu zao kutoka Makka ni huu ufuatao:

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ aliwaita Ansaar ili kuwagawia ardhi ya Bahrain. Lakini Ansaar waliiacha haki yao hiyo wakasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tunakuomba usitupatie chochote mpaka uwape mara mbili ndugu zetu Muhaajiruun!"

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu, "Enyi Ansaar, kwa kuwa mtawatanguliza wengine kabla ya nafsi zenu, basi endeleeni kuwa na subira mpaka mtakapoungana nami kwenye Bwawa la Kawthar…kwa maana baada yangu zitakuja zama ambazo watu wengine watatangulizwa kabla yenu!" (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 8)

Moyo huo wa Ansar ulisifiwa na Mtukufu Mtume ﷺ:

"Mnapoitwa kwenye vita au kumsaidia mwenye shida mnakuja makundi kwa makundi na kuongezeka kwa wingi. Lakini mnapoitwa ili mpatiwe mambo ya kidunia, idadi yenu inapungua na kukataa." (Ali al-Muttaqi, XIV, 66)

Kwa sababu ya uungwana wao waliomuonesha Mtukufu Mtume ﷺ na Muhajiruun waliohamia kwao, Ansaar walipewa zawadi ya Pepo, lakini kubwa zaidi walipewa zawadi ya kuridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hivyo, Qur'an Tukufu inasema:

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ
رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ
خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito

kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (at-Tawba, 100)

Ansaar hawakusita kuyaweka maisha yao hatarini katika kuutetea Uislamu na kumlinda Mtukufu Mtume ﷺ. Walisimama imara katika Vita ya Badr. Katika Vita ya Uhud, wakati Waislamu wakiwa katika wakati mgumu baada ya kushambuliwa na maadui kutokea upande wa nyuma na hali kuwa mbaya dhidi yao, Maswahaba waliomlinda Mtukufu Mtume ﷺ wengi wao walikuwa Ansar, ambao walitengeneza ukuta kwa miili yao kumlinda na kumkinga dhidi ya mashambulizi ya maadui. Walishikamana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ kwa upendo na utii usiomithilika. Kisa kifuatacho kilichosimuliwa na Anas ؓ ni mfano hai:

"Nilikuwa safarini pamoja na Jarir ibn Abdullah.[20] Licha ya kunizidi umri, alikuwa akinihudumia; na nilipomwambia aache kufanya hivyo alisema, 'Niliishuhudia huduma kubwa iliyotolewa na Ansaar kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nami nikaahidi kuwa kama nikisuhubiana nam tu wa jamii ya Ansaar nitamhudumia." (Bukhari. Jihad, 71; Muslim, Fadhail'us-Sahaba, 181)

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alisema, "Kama Hijrah isingekuwepo, nami ningekuwa Ansaar", alikuwa akielezea thamani na hadhi waliyokuwa nayo machoni mwake. (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 2)

Yafuatayo ni baadhi ya maneno yaliyotamkwa na Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu ubora wa Ansaar:

---

20. Jarir ibn Abdillah ؓ alikuwa kiongozi wa kabila la Bajila la Yemen. Akiwa ameandamana na watu 150, alikuja mjini Madina katika mwezi wa Ramadhan na kusilimu. Ilikuwa mwaka wa 10 wa Hijrah, miezi mitatu kabla ya kifo cha Mtukufu Mtume ﷺ. Alikuwa akimpenda mno Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Hata Mtukufu Mtume ﷺ naye alikuwa akimpenda na mara anapomuona Jarir alikuwa akitabasamu.

"Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho basi asiwatendee vibaya Ansaar." (Tirmidhi, Manaqib, 25/3906)

"Waumini ndio watakaowapenda na wanafiki ndio wanaowachukia. Mwenyezi Mungu huwapenda wale wenye kuwapenda Ansaar na huwachukia wale wenye kuwachukia." (Tirmidhi, Manaqib, 25/3900)

"Watu wengine wanaongezeka lakini Ansaar wanapungua; wataendelea kupungua, kama chumvi inavyoyeyuka katika chakula." (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 11)

"Ninakuusieni kuwatendea wema Ansaar. Hakika wao ni watu wangu, wasiri wangu na waumini wangu. Wametekeleza kikamilifu wajibu wao. Bado hawajalipwa kwautumishi wao (watalipwa kwa wingi huko Akhera). Hivyo, amilianeni kwa wema na wale walio wema miongoni mwao na muwasamehe wakosefu wao." (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 11)

Upendo wa hali ya juu aliokuwa nao Mtukufu Mtume ﷺ kwa Muhaajiruun na Ansaar ulitambaa mpaka kwa Maswahaba zake wote; kiasi kwamba kila Swahaba aliamini kuwa alikuwa anapendwa zaidi na Mtume ﷺ kuliko mtu mwingine.

Ka'b ibn Ujra رضي الله عنه anasimulia tukio lenye kusisimua:

"Tulikuwa tumekaa mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika Msikiti wa Madina. Waliokuwa wamekaa hapo ni kundi dogo la Ansaar, Muhajirun na bani Hashim. Tulikuwa tukiulizana baina yetu ni kundi lipi ambalo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alilipenda zaidi.

Sisi, Ansar tukasema:

'Tulimuamini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tukamtii na kupambana dhidi ya maadui zake. Hivyo, kwa sababu hizo, anatupenda zaidi!'

Ndugu zetu wa Muhajirun wakajibu:

'Tulihama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, tukaziacha familia na mali zetu katika njia Yake. Aidha, tulishiriki katika mapambano yote mliyoshiriki. Hivyo, Mtume anatupenda zaidi sisi!'

Kisha bani Hashim nao wakasema:

'Sisi ni ndugu wa Mtume, ambao tumeshiriki katika vita vyote mlivyoshiriki. Hivyo, bila shaka Mtume atakuwa na mapenzi makubwa zaidi kwetu!'

Mara Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitokea na kuuliza:

'Ni jambo gani hilo mlilokuwa mkilizungumzia?'

Kila mmoja wetu alirejea kueleza kile alichokisema, ambapo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

'Nyote mmesema kweli…nani anayeweza kuwa na mawazo tofauti na hayo?' Kisha baada ya kusita kidogo, aliuliza, 'Je mnge-penda nilitatue suala hili?'

Tukajibi, 'Bila shaka.' Hapo Mtume ﷺ akasema, 'Enyi Ansaar… Mimi ni ndugu yenu!'

'Allah Akbar!, tunaapa kwa Mola wa Kaabah, tumeshinda!' Ansaar walilipuka kwa furaha.

Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, 'Enyi Muha-ajiruun, mimi ninatokana nanyi!'

Muhajirun nao wakaripuka kwa furaha, 'Allah Akbar! Tunaapa kwa Mola wa Kaabha, tumeshinda!'

Mtume wa Mwenyezi Mungu akaendelea, 'Enyi bani Hashim, nyinyi mnatokana nami na mmekuja kwangu!' Nao pia wakasema:

'*Allah-u Akbar*! Tunaapa kwa Mola wa Kaabah, tumeshinda!' Sote tukaondoka tukiwa tumeridhika. Kila kundi lilifurahishwa na maelezo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ." (Haythami, X, 14)

Mipaka ya mji wa dola ndogo ya Kiislamu iliyoasisiwa Madina, ilikuwa na takriban familia mi anne, na baada tu ya miaka kumi ikafika Iraq na Palestina. Wakati Mtukufu Mtume ﷺ anafariki dunia, Maswahaba walikuwa vitani dhidi ya Warumi na Waajemi, ingawa viwango vyao vya maisha vilikuwa vimebadilika kidogo kulinganisha na miaka kumi kabla. Waliendelea kuishi maisha ya kujizuia na kuridhika. Mambo kama vile israfu, uchoyo, anasa na starehe ni vitu ambavyo Maswahaba hawakuvijua kabisa. Daima walijazwa utambuzi kwamba 'kaburi ndio hatima ya mwili.' Hivyo, daima walijiepusha na muelekeo wa kujilimbikizia na kuzama ndani ya anasa za dunia. Badala yake walizitumia rasilimali za dunia kama nyenzo za kuwaongoza wanadamu kwenye wokovu, kutokana na mwamko na ladha ya imani waliyokuwa nayo. Waliyatengeneza maisha yao katika mwelekeo wa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Bila shaka miongoni mwa sababu kubwa kabisa na za wazi za kuenea Uislamu kwa kasi miongoni mwa watu wanyonge na waliodhulumiwa, kama miale ya mwanga wa asubuhi, ni ile hali halisi ya kwamba Maswahaba walionesha tabia halisi ya Muislamu kila walipokwenda. Wanafunzi hao mahiri wa Mtukufu Mtume ﷺ, yaani Maswahaba, walikuwa waumini bora, waaminifu na waadilifu, waliobeba hazina za maadili ndani ya nyoyo zao zilizoangazwa kwa nuru ya Mtume, ambao waliwatazama wanadamu wenzao kwa jicho la huruma.

Madinat'un-Nabi na Mkataba wa Madina

Mji wa Madina uko upande wa kaskazini na umezungukwa na milima kwenye pande tat una eneo la wazi upande wa kusini. Ni

mji mzuri wenye mandhari ya kijani yenye wingi wa mabustani ya mitende, ardhi yenye rutuba na hali ya hewa maridhawa.

Wakati wa Hijrah, wakazi wa mji huu walikuwa ni makabila mawili ya Kiarabu, yaani Aws na Khazraj, pamoja na makabila matatu ya Kiyahudi, ambayo ni Banu Qaynuqa, Banu Nadhir na Banu Quraydhah. Waarabu walikuja Madina wakitokea Yemen kufuatia mafuriko makubwa yajulikanayo kama *Sayl'ul-Arim*, huku Wayahudi kwa asili wakiwa ni wakimbizi kutoka Jerusalem, waliokimbia ukandamizaji wa Warumi waliouvamia mji huo.

Kwa muda mrefu, kulikuwa na uhasama baina ya Waarabu na Wayahudi uliotokana na Wayahudi walishindwa na Waarabu na kuwa na nguvu katika mji wa Madina. Lakini muda mfupi baadaye Wayahudi walipandikiza mbegu za uadui baina ya Waarabu, Aws na Khazraj walijikuta katika vita visivyokwisha baina yao, vita ya mwisho ikiwa ni Vita ya Buath. Vifo na majeruhi kutoka pande zote mbili, katika vita vilivyodumu zaidi ya miaka mia moja na ishirini na kufikia kikomo miaka mitano tu kabla ya Hijrah, vvilikuwa vimeyadhoofisha makabila yote mawili. Hivyo, wakati wa Hijrah, Wayahud wakawa na uwezo mkubwa kiuchumi katika mji huo.

Hivyo, kuwasili kwa Mtukufu Mtume ﷺ mjini Madina kulimaanisha kuwa uhasama na uadui baina ya makabila hayo ndugu ulikuwa umefikia kikomo kwa neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۚ وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ
كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنْتُمْ عَلَىٰ شَفَا
حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ مِنْهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

"Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Ishara zake ili mpate kuongoka." (Al Imran, 103)

Muda mfupi baada ya Hijrah, Makafiri wa Makka waliandika barua za vitisho na kuwahamasiha waabudu masanamu na Wayahudi wa Madina, kwa matarajio ya kuwazuia Waislamu wasiweze kutulia na kupata nguvu katika mji huo. Vitisho katika mojawapo ya barua hizo vilielekezwa kwa Abdullah ibn Ubayy na waabudu masanamu kutoka katika makabila ya Aws na Kkhazraj ambao walikuwa upande wake, vilisema:

"Huko kwenu kuna mtu wetu. İma umuue au umfukuze, la sivyo tutakuja na jeshi la makabila yote ya Arabia, tutawaua na kuwachukua wanawake wenu kama mateka watakaotustarehesha!"

Abdullah ibn Ubayy, akiungwa mkono na waabudu masanamu wa Madina waliazimia kukabiliana na Mtukufu Mtume ﷺ. Mtukufu Mtume ﷺ alipata taarifa ya hali hiyo kabla,na hivyo akaamua kuwaendea kabla hawajafanya hivyo:

"Inaonekana kuwa vitisho ulivyopewa na Maqurayshi vimekupata. Tambua kuwa madhara watakayokusababishia sio makubwa kama madhara utatakayoyapata kwa kupambana naşi!au mnakusudia kupigana na watoto na ndugu zenu wenyewe na kuwaua?"

Hatimaye walitawanyika. (Abu Dawud, Kharaj, 22-23/3004; Abdurrazzaq, V, 358-359)

Vitisho na uchochezi kutoka Makka havikufua dafu. Lakini kulikuwa na uwezekano kuwa Maqurayshi waliokuwa na hasira

wangeishambulia Madina muda wowote na kuwaua Waislamu, Wayahudi na waabudu masanamu bila kubagua. Kitisho hiki kilichokuwa kikiwakabili watu wote wa Madina kiliwaleta pamoja Waislamu na wale wasiokuwa Waislamu chini ya uongozi wa Mtukufu Mtume ﷺ.

Kwa upande mwingine, tokea zamani, makabila ya Aws, Khazraj na Wayahudi walikuwa wakishindana kuwa mamlaka pekee katika mji huo. Kwa mfano, watu wa kabila la Khazraj walikuwa wakijianda kumtangaza kiongozi wao Abdullah ibn Ubayy kuwa mtawala wa Madina, licha ya ukweli kwamba mtu kutoka Aws au Khazraj asingekubalika kwa kabila pinzani. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alionekana kuwa kiongozi anayeweza kuwaunganisha wakazi wote wa Madina.

Kwa hali hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alishika uongozi wa mji wa Madina. Akiwa amekwishaasisi undugu baina ya Aws na Khazraj na hivyo kutengeneza nidhamu ya kijamii baina ya Waumini kupitia *muakhat*, bila kuchelewa aliwajumuisha Wayahudi kama raia wa Madina kwa hati maalumu. Mkataba huo uliweka kanuni ambazo zilichukuliwa kama katiba ya Mji wa Dola ya Madina. İfuatayo ni miongoni mwa kanuni na misingi iliyokuwa ndani ya hati hiyo inayojulikana kama Mkataba wa Madina, ambao ni waraka rasmi wa uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu:

"Bismillahi'r-Rahmani'r-Rahim,

1. Waislamu kutoka Makka na Yathrib (Madina), wategemezi wao na wale walio bega kwa bega ni *ummah* uliotolewa katika jamii nyingine.

2. Hakutakuwa na uovu na shari. Waislamu wema wataunganana dhidi ya dhalimu anayetaka kuminya na kudhulumu haki za wengine, anayetenda dhambi, anayependikiza uadui, chuki na shari

kati ya Waumini. Hata kama mtu huyo atakuwa ndugu yao, watasimama kama kitu kimoja dhidi yake.

3. Mauaji hayataruhusiwa. Iwapo utatokea, pande zote mbili za Muhaajiruun na kila familia ya Madina kwa pamoja watalipana fidia, kwa mujibu wa desturi zao. Kila upande utalipa kikomboleo kwa mateka wao kwa pamoja, kulingana na misingi na kanuni za uadilifu na haki zilizopo baina ya Waislamu.

4. Waislamu hawatawaacha wale wenye familia kubwa au wenye madeni katika kuwashughulikia matatizo yao wenyewe, bali watawasaidia na kuwalipia vikomboleo au fidia yao, ndani ya taratibu za haki na uadilifu zitakazokubalika kwa pande zote mbili.

5. Usalama utadumishwa ndani na nje ya Madina. Wakazi wote na wageni pia watakuwa katika hali ya usalama na amani. Isipokuwa wale watakaofanya dhulma, uonevu au kufanya uhalifu.

6. Wayahudi watakuwa na uhuru wa imani na watabaki katika dini yao kwa uhuru, kama ambavyo Waislamu wataendelea na dini yao. Raia wetu wa Kiyahudi watapata msaada wa bure wa haki na kuwasaidia kukabiliana na tishio lolote dhidi yao. Vita ikitokea, basi pande zote zitashirikiana. Kwa muda ambao wataendelea kushiriki mapambano bega kwa bega na Waislamu, Wayahudi watashiriki katika gharama za vita.

7. Hakuna upande utakaoshirikiana na makafiri wa Makka. Kwa vyovyote vile, hawatawapatia hifadhi Maqurayshi na washirika wao.

8. Vita ndani ya Madina havitaruhusiwa. Ndani ya Bonde la Madina ni eneo salama kwa wote wanaowajibika chini ya mkataba huu. Iwapo patatokea uvamizi kutoka nje, hivyo kila upande utalilinda eneo lake. Makubaliano ya amani yatakayofanywa na upande wowote yatakubaliwa na kuheshimiwa na pande zote. Wakati

wote wa vita, Wayahudi watajigharamia na Waislamu pia watajigharamia; japokuwa watasaidiana na kufanya mambo yanayofaa dhidi ya mvamizi na wema utatawala katika kusaidiana. Hakuna upande utakaoufanyia madhara upande mwingine na wanatakiwa kumsaidia anayeonewa kwa hali yoyote ile.

9. Iwapo mgogoro utaibuka, basi suala hilo litapelekwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, ambapo hukmu yao itakuwa ya mwisho.

10. Ahadi na hakikisho la Mwenyezi Mungu ni kwa watu wote hata wale walio dhaifu kabisa; kwa maana Waislamu ni tofauti na watu wengine katika kuimarisha undugu na kusuhubiana wao kwa wao.

11. Hakuna Yahudi atakayeshiriki katika safari ya kivita (ya Waislamu) bila ridhaa ya Muhammad ﷺ.

Bila shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuwa radhi na wale wenye moyo wa kujizuia kwenda kinyume na vifungu vilivyoainishwa katika hati hii, wale wenye kushikamana na wema na haki. Vifungu hivi havitazuia utekelezaji wa adhabu dhidi ya dhalimu au mhalifu aliyetiwa hatiani.

Mwenyezi Mungu atawalinda wale wenye kutenda mema na kujizuia na maovu. Muhammad ﷺ ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." (Ibn Hisham, II, 119-123; Ibn Kathir, al-Bidaya, III, 263-264; Hamidullah, al-Wasaiq, uk. 57-64)

Ni dhahiri kuwa vifungu hivi ni muhimu sana katika utekelezaji wa sheria za Kiislamu katika jamii. Mkataba wa Madina, msingi wa uraia, ni jibu la wazi kabisa dhidi ya tuhuma kwamba Uislamu ni dini isiyokuwa na taratibu za kisheria na za kijamii, kwamba ni dini tu yenye kushughulikia masuala ya ibada.

Makubaliano hayo yaliyobeba maelekezo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii n akidini, yanauonesha Uislamu kama mfumo pekee unaotoa umoja baina ya Waislamu ambao wanatakiwa kusaidiana, kusimamisha haki na uadilifu katika miamala yao yote na watafute suluhisho kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake pindi migogoro inapotokea.

Mkataba huo unaweka kikomo na kuondosha mshikamano wa kikabila uliokuwepo baina ya Waarabu kwa kuweka kanuni ya uadilifu, inaagiza kumuadhibu mhalifu hata kama atakuwa ndugu. Vilevile, kwa kuwapa Wayahudi haki ya kumiliki mali na haki kutekeleza dini yao, Mkataba huo unathibitisha kiwango cha uadilifu wa hali ya juu alichokuwa nacho Mtukufu Mtume ﷺ. Kama Wayahudi wenyewe wasingekiuka mkataba huo, ungeendelea kuwapatia uadilifu kwa muda mrefu.

Tangazo la mji wa Madina kuwa Eneo Takatifu

Mkataba huo ulifuatiwa na uainishaji wa mipaka ya *Haram*, yaani eneo takatifu, katika mji wa Madina. Mtukufu Mtume ﷺ alilitangaza hilo kwa kusema:

"Ibrahimu عليه السلام aliitangaza Makka kuwa *haram*, nami nalitangaza eneo la baina ya vilima viwili vya Madina kuwa *haram*." (Ahmad, IV, 141)

Mipaka ya eneo takatifu la Madina iliwekwa kwa kusimika mawe katika vilima hivyo vilivyoelezwa. Baada ya kuwekwa mipaka hiyo, Madina ikaitwa *al-Haram'ur-Rasul*, yaani Eneo Takatifu la Mtume ﷺ. Kila pembe ya eneo la *farsah* tatu baina ya vilima vya Ayr na Thawr ilifanywa kuwa shamba.[21](Bukhari, Fadhail'ul-Madina, 1; Muslim, Hajj, 471-472)

21. Hili ni eneo lilipo baina yam lima Ayr jirani na Dhulhulayfah na Thawr, kilima

Baada ya kuitangaza Madina kuwa eneo Takatifu, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaongezea kwa kusema:

"Miti haitaruhusiwa kukatwa wala dhambi kutendeka ndani ya mipaka hii. Atakayefanya jambo linalokwenda kinyume na Kitabu na Sunnah atathibitikiwa na laana ya Mwenyezi Mungu, Malaika na watu wote." (Bukhari, Fadhail'ul-Madina, 1)

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliinyanyua mikono yake juu na kuuombea kheri mji huo, ambapo tokea kipindi hicho mji huo umekuwa eneo lenye amani, utulivu, rehma na furaha kwa Waumini wote na ulimwengu wote wa Kiislamu kwa ujumla.

Muda wote Maswahaba walizingatia na kuilinda hadhi ya mji wa Madina, kama inavyothibitishwa na Abu Hurayrah رضي الله عنه:

"Nikimuona swala akila katika malisho ya Madina, nilikuwa simbughudhi, kwa maana nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akilitangaza eneo baina ya sehemu zilizowekewa mawe katika mji wa Madina kuwa ni Takatifu." (Muslim, Hajj, 471)

Sio hivyo tu, bali pia Maswahaba hawakuwa wakiwavumilia watoto wao kuonesho mwenendo mbaya kwenye eneo hilo tukufu, kama inavyosimuliwa na Abdullah ibn Ubada رضي الله عنه:

"Siku moja nilikuwa nikiwinda ndege jirani na Kisima cha Abu Ihab. Baba yangu aliniona na haraka sana akaniamuru nimuachie ndege niliyekuwa nimemkamata, akaniambia, 'Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilitangaza eneo lililopo baina ya mawe haya kuwa eneo Takatifu, kama ambavyo Ibrahimu عليه السلام alivyoitangaza Makka (kuwa eneo Takatifu).'" (Ibn Athir, Usdu'l-Ghaba, III, 159)

---

kidogo kilichopo upande wa kasikazini wa Uhud. Kilima hiki cha Thawr ni tofauti na Mlima Thawr wa Makka.

Soko la Madina na Udhibiti wa Shughuli za Kibiashara

Baada ya kuwasili Madina, Mtukufu Mtume ﷺ aliteua eneo maalumu la soko tofauti na lile la Mayahudi, na kuwasisitiza Waislamu wafanye biashara zao huko. Ni ukweli unaojulikana vyema kwamba, maeneo tofauti ya masoko ni muhimu sana ili kuwa na uhuru na kujitegemea kibiashara na kiuchumi.

Mtukufu Mtume ﷺ alilifuatilia kwa karibu soko hilo na shughuli za kibiashara za Madina, akizizungukia bidhaa na hata wafanybiashara wenyewe.

Siku moja, alikwenda kwa mfanya biashara mmoja sokoni. Aliingiza mkono wake ndani ya fungu la ngano, akahisi unyevunyevu na ubichi chini ya ngano hiyo, akauliza sababu.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ilitokana na mvua," mfanyabiashara huyo alifafanua.

"Kwa nini sehemu yenye ubichi usiiweke juu ili kila mtu aione?" Mtukufu Mtume ﷺ alishauri, akaongeza kusema, "Mdanganyifu hana nafasi kwangu!"

Qays ibn Abi Garaza ﷺ anasema:

"Wakati wa zam aza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ bado tulikuwa tukiitwa 'madalali', mpaka alipokuja sokoni na kutupatia jina zuri la 'wafanyabiashara' na kutuusia, 'Wafanyabiashara wanajua kuwa uongo na viapo hupamba biashara zao, hivyo changanyeni sadaka katika biashara zenu!'" (Ahmad, IV, 6; Abu Dawud, Buyu', 1/3326)

Licha ya umakini mkubwa ambao mtu anaweza kuwa nao, usahaulifu na ujinga lazima vitajitokeza katika miamala mbalimbali na kusababisha ukosefu wa uadilifu na dhulma. Hivyo, yampasa mtu kuchukua hatua ya tahadhari kwa kutoa sadaka kutokana na chumo

lake, kitu ambacho kimegusiwa na Mtukufu Mtume ﷺ katika hadith iliyotangulia hapo juu.

Rifaa ibn Rafi ﷺ anasema:

"Siku moja tulikuwa tukienda kwenye *Musalla*[22] pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Njiani aliona kundi la watu wakifanya biashara. Akawaita nao wakaitika na kumsikiliza. 'Enyi wafanyabiashara, siku ya Kiyama wafanyabiashara wengi watafufuliwa kama waovu…isipokuwa wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu, wakatenda mema na kutoa sadaka.'" (Tirmidhi, Buyu, 4/1210)

Kuhusu maadili yanayotakiwa kutawala katika biashara, Mtukufu Mtume ﷺ anaelezea kisa kilichotokea huko nyuma baina ya watu wawili wema wa Bani Israeli:

"Siku moja, mtu mmoja kabla yenu, alinunua ardhi kutoka kwa mtu, na baadaye akakuta chungu cha dhahabu katika ardhi hiyo. Alikichukua chungu hicho kwa mikono yake na kukirudisha kwa yule aliyemuuzia ardhi, akasema:

'Chukua dhahabu yako, nilichonunua kwako ni ardhi tu, sio dhahabu iliyokuwa ndani yake!'

'hapana; kwa maana nilikuuzia ardhi pamoja na vyote vilivyomo!' alijibu.

Waliposhindwa kulitatua suala hilo, walimteua mtu mwingine awasuluhishe. Baada ya kuwasikiliza akawauliza:

---

22. *Musalla* ni eneo kubwa ambalo limetengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile swala za Ijumaa, Eid au swala za jeneza ambazo huswaliwa kwa jamaa katika jamii husika. Kwa asili maeneo ya *Musalla* yalikuwa yakitengwa nje kidogo ya miji kwa ajili ya swala mbalimbali za jamaa, kama vile swala za Ijumaa au Eid, badala ya misikitini. Hivyo ni eneo ambalo wakazi wote wa mji fulani walikuwa wakikusanyika kwa mikusanyiko ya kila wiki.

'Je mna watoto?' Ikabainika kuwa mmoja wao alikuwa na mtoto wakiume na mwingine akawa na mtoto wa kike.

Msuluhishi akashauri, 'Basi waozesheni, sehemu ya dhahabu muitumie kwa ajili ya ona iliyobaki muitoe sadaka.'" (Bukhari, Anbiya, 54; Muslim, Aqdiyya, 21; Ibn Maja, Luqata, 4)

Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye aliwahi kufanya safari nyingi za kibiashara na kuwa na uzoefu mkubwa, miongoni mwa miongozo ya kibishara aliyoitoa alipowasilia Madina ni:

"Tisa ya kumi ya mapato ni katika biashara." (Suyuti, I, 113)

"Chakula bora na cha halali kuliko vyakula vyote ni kile ambacho mtu hukipata kwa jasho lake." (Ibn Maja, Ticarat, 1)

Hakika, mbalina taathira ya kimwili, chakula pia kina taathira ya kiroho kwamtu husika. Kila tonge tunalokula, liwe na halali, laharamu au hata lenye kutia shaka, huwa na nafasi na taathira kubwa kwenye nyoyo zetu. Kile tunachokula kinaziathiri hisia na umakini wetu. Hadith ifuatayo inaelezea umuhimu wa uhalali wa pesa tunazotumia katika ibada mbalimbali, kama vile hijja na kadhalika:

"Mwenye kwenda kuhijji kwenye Nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa pesa alizozipata kwa njia za haramu atakuwa amejitoa katika utii wa kumtii Mwenyezi Mungu. Mtu huyo anapovaa vazi la *ihram*, akampanda ngamia wake na kusema'*labbayk Allahumma labbayk*', huitikiwa na sauti kutoka Mbinguni, '*la labbayk, walaa sa'dayk*, kwa maana mapato yako, maandalizi yak ona hata ngamia wako ni vya haramu; hivyo utarudi ukiwa huna thawabu yoyote na huzuni itakuandama kwa masaibu yatakayokupata.'

Lakini mja anapokwenda hijja kwa pesa aliyoichuma kihalali na kumpanda farasi wake na kusema *'labbayk Allahumma lab-*

bayk', huitikiwa kutoka Mbinguni, '*labbayk wa sa'dayka*… yaani, Ninakuitikia, kwa maana ngamia wako, mavazi yako na matumizi yako ni ya halali. Hivyo utarudi ukiwa na wingi wa thawabu, zisizokuwa na kasoro ya dhambi; na furahi kwa maana utapata furaha na neema!'" (Haythami, III, 209-210)

Kutokana na umuhimu na unyeti wake, mlango wa mapato ya haramu umefungwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika surat al-Baqara, mara tu baada ya kuufunga mlango wa *shirk*, yaani kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata surah al-An'am, Al-A'raf, Yunus na an-Nahl, zilizoteremka katika kipindi cha Makka na ambazo hazikuwa na kiwango kikubwa cha hukmu za kisheria, zimeainisha mambo ya halali na ya haram umara tu baada ya aya zinazohusu kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.[23]

Katika kusisitiza haja ya ujasiri na uaminifu katika biashara, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Amerehemewa mfanyabiashara jasiri mwenye kuzitoa bidhaa zake kwa ajili ya kuziuza, amelaaniwa mwenye kuzilimbikiza bidhaa zake." (Ibn Majah, Tijarat, 6)

"Mfanyabiashara mwoga ni mwenye kunyimwa, na mfanyabiashara jasiri ni mwenye kuruzukiwa." (Daylami, II, 79)

Katika hadith zifuatazo kuna kanuni kadhaa nyingine za kibiashara zilizoelezwa na Mtume wa Allah ﷺ:

"Muuzaji na mnunuzi wana uhuru wa kubadilisha mawazo, madamu mmoja wao hajaondoka (hawajaachana). Iwapo watawekeana mkataba wenye uaminifu na kila kitu kikawekwa wazi kama kilivyo, biashara yao itakuwa yenye ustawi na neema. Lakini

23. al-Anâm, 136-152; al-Arâf, 32-33, 169; Yûnus, 59-60; an-Nahl, 95, 115-116. Tazama, Draz, an-Nabau'l-Adhîm, uk. 193.

kama wataficha baadhi ya mambo na kuongopa, basi biashara yao hukosa ustawi." (Bukhari, Buyu, 19; Muslim, Buyu)

"Viapo huvutia biashara, japokuwa vinaondosha baraka katika biashara." (Bukhari, Buyu, 26; Muslim, Musaqat, 13)

Mtukufu Mtume ﷺ alipiga marufuku mambo kama vile kulangua bidhaa kabla hazijafika sokoni, kupatana kila kitu kabla bidhaa hazijawafikia wenye nazo, kuuza bidhaa kabla hazijawa zako, kuzuia bidhaa ambazo zimeshauzwa na kuwa kikwazo baina ya wateja.[24]

Katika kusisitiza juu ya haja ya kurahisiha mambo katika biashara, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Mwenyezi Mungu amrehemu mja karimu na mwepesi katika kununua, kuuza na kukubali deni halali." (Bukhari, Buyu, 16)

"Mwenyezi Mungu alimrehemu mja kabla yenu kwa sababu mja huyo alikuwa akionesha ulaini na wepesi katika kununua, kuuza na kurejesha anayodaiwa." (Tirmidhi, Buyu', 75/1320)

Kuingia katika mtego, kuhadaiwa na tama aza dunia na kudhani kuwa unaweza kujiingizia mapato kwa kutotii miongozo iliyowekwa na Mtukufu Mtume ﷺ itakuingiza katika hatari ya kuwa maskini huko Akhera. Kwa upande mwisngine, wafanyabiashara waaminifu wanafanya juhudi ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kufanya maandalizi kwa ajili ya Akhera, wamebashiriwa habari njema na Mtukufu Mtume ﷺ:

"Mfanyabiashara Muislamu, mwaminifu na mkweli, siku ya Kiyama atakuwa katika kundi la mashahidi (waliokufa wakipigania dini ya Mwenyezi Mungu)." (Ibn Maja, Tijarat, 1)

24. Tazama; Bukhari, Buyû, 70-72; Muslim, Buyû, 29.

Masjid'un-Nabi na Ujenzi wa Nyumba ya Mtume ﷺ

Mwanzo hapakuwepo masikiti katika Mji wa Madina na Mtukufuu Mtume ﷺ alikuwa akiswali popote alipoona panafaa. Haukupita muda mrefu*Masjid'un-Nabi* ikajengwa baada ya ule wa Quba.

Wakati akiwasili mjini Madina, ngamia wa Mtukufu Mtume ﷺ, aitwaye Qaswa, alipiga magoti kwenye eneo la kiwanja kilichokuwa jirani na makazi ya Bani Najjar, ambalo lilitumika kukaushia tende. Eneo hilo lilikuwa likimilikiwa na yatima wawili wa ukoo huo, Sahl na Suhayl. Mtume ﷺ aliteremka juu ya ngamia wake na kusema:

"Mwenyezi Mungu akipenda, hapa patakuwa makazi yetu!" Alipouliza kuhusu wamiliki wa ardhi hiyo, Muadh ibn Afra ؓ akamweleza. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaitisha Sahl na Suhayl na kuzungumza nao kuhusu bei ya ardhi hiyo ili aweze kuinunua.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hatutakuuzia bali tutakupa kama zawadi ili tupate malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu!"

Lakini Mtukufu Mtume ﷺ hakulikubali wazo lao, badala yake aliinunua ardhi hiyo. (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 45, Salat 48; Muslim, Masajid, 9)

Eneo hilo lilikuwa na makaburi kadhaa ya waabudu masanamu, vichuguu hapa na pale na mitende. Makaburi yalifukuliwa na mifupa ikawekwa mahali pengine, vichuguu vikasawazishwa na mitende ikasawazishwa.[25] Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza yatengenezwe matofali ya udongo kwa ajili ya ujenzi.[26]

Wakati wa ujenzi, Mtukufu Mtume ﷺ alifanya kazi ya kubeba matofali pamoja na Maswahaba zake huku akisema:

25. Muslim, Masajid, 9.
26. Ibn Saad, I, 239.

"Mzigo huu sio mzigo wa Khaybar, bali kazi bora na safi zaidi ni ile ya kumtumikia Mwenyezi Mungu." (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 45)

Kwa maneno haya, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiashiria kwamba kazi waliyokuwa wakiifanya haikuwa na manufaa ya kidunia, ilikuwa na faida na manufaa makubwa kuliko bidhaa za tende na zabibu ambazo watu walikuwa wakizibeba kutoka Khaybar kwa ajili ya biashara.

Swahaba mmoja aliyekuwa amebeba tofali alimuona Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amebeba tofali akaenda na kumtaka abebe kwa niaba yake, Mtume ﷺ akamwambia:

"Nenda kachukue tofali jingine, kwa maana hata mimi ninazihitajia thawabu za Mwenyezi Mungu kuliko hata wewe!" (Samhudi, I, 333)

Uwajibikaji kiroho na hatua ya motisha iliyofanywa na Mtukufu Mtume ﷺ kuwahamasisha Waislamu wenzake kufanya kazi kwa yeye mwenyewe kushiriki katikakufanya kazi wakati wa ujenzi[27]

27. Mwenendo wa Mtukufu Mtume ﷺ ni mwenendo wenye kupigiwa mfano na unaotakiwa kuigwa na wale walio katika nafasi za uongozi. Wakati wote alikuwa msitari wa mbele katika kutekeleza majukumu yote na kuepuka kiburi cha kutoyapa uzito majukumu, hata kama yatakuwa kidogo kiasi gani. Mfano huo wa Mtukufu Mtume ﷺ tunauona kwa Sultan Ahmad I wakati wa ujenzi wa Msikiti Mkubwa Sultan Ahmad. Sultan Ahmad I alikuwa akifanya kazi kama kibarua akiwa na koleo mkononi. Baada ya kifo chake, binti yake, Jawhar Nasibah Hatun aliota ndoto na kumuona akiwa katika kasri zuri peponi, akamuuliza, 'Baba yangu, ni matendo gani yaliyokupatia faraja hiyo?', akajibu, 'Nilibeba matofali mgongoni mwangu wakati wa ujenzi wa msikiti, na hiyo ndiyo sababu ya kupata daraja hii ya juu'.
Fikiria, wakati Sultan Ahmad I akibeba mawe mgongoni mwake, katika kuonesha maadili ya Kiislamu, Dola ya Uthmaniyailikuwa katika kilele cha juu kabisa, ikitawala maeneo mengi na makubwa sana. Wafalme walikuwa wakiiheshimu na walikuwa wakitetemeshwa na mawaziri wake.

viliwahamasisha Maswahaba kiasi cha kusema, "…kutulia huku Mtume akifanya kazi kutatupeleka kwenye upotevu." (Ibn Hisham, II, 114)

Wakati wa ujenzi alikuwepo mwanaume mmoja kutoka Hadhramawt, mwenye ustadi wa kuchanganya na kutengeneza matofali ya udongo. Mtukufu Mtume ﷺ alimsifu kwa kusema:

"Mwenyezi Mungu amrehemu yule anayetumia ujuzi wake kwa ubora na ukamilifu. Endelea kufanya kazi yako, kwani ninakuona na ustadi katika kazi hiyo!" (Samhudi, I, 333; Diyarbakri, I, 344)

Vilevile Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka Waumini wafanye mambo yao yote kwa ustadi. Anasema katika aya tukufu وَأَحْسِنُوا, "…fanyeni kwa uzuri na ubora", kisha anafuatisha kwa kusema "…hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaofanya (mambo yao) kwa ukamilifu na ubora." (al-Baqara, 195)

Wakati akibeba matofali akiwa bega kwa bega na Maswahaba zake, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akirudiarudia maneno yafuatayo:

"Hakuna maisha isipokuwa maisha ya Akhera. Ewe Mwenyezi Mungu wape rehma Zako Muhajiruun na Ansaar!" (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar, 45)

Wakati watu wote walikuwa wakibeba tofali moja moja, Ammar ibn Yasir ؓ alikuwa akibeba matofali mawili kwa wakati mmoja, moja kwa ajili yake na jingine kwa ajili ya Mtukufu Mtume ﷺ. Mtukufu Mtume ﷺ alipoiona juhudi yake kubwa, alimuuliza huku akimfuta vumbi:

"Ewe Ammar, kwani hubebi tofali moja moja?"

"Ninafanya hivyo kwa matarajio ya kupata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu", alijibu. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akampiga kikofi mgongoni, kama ishara ya upendo, na kusema, "Ewe

Ammar, wengine wana thawabu moja, lakini wewe una thawabu mbili!" (Ahmad, III, 91; Ibn Kathir, al-Bidaya, III, 256)

Simulizi ifuatayo inathibitisha ukweli kuwa wanaume na wanawake wote walifanya kazi kwa hamasa na shauku kubwa wakati wa ujenzi wa Msikiti huo:

"Abdullah ibn Awfa ﵁ alipofiwa na mkewe, aliwataka watu 'kulibeba jeneza lake kwa hamasa. Kwa maana wakati wa usiku, yeye na wajakazi wake walikuwa wakibeba mawe ya msikiti wa Mtume, ambao umejengwa juu ya msingi wa uchamungu. Naşi wanaume tulikuwa tukiyabeba wakati wa mchana." (Haythami, II, 10)

Msikiti huo wenye pembe nne, ulikuwa na urefu na upana wa takriban ziraa[28] mia moja, na ziraa tano mpaka saba kwa urefu wa kwenda juu, tatu za mwanzo zikiwa kwenye msingi wa mawe na zilizobaki zikiwa za tofali za udongo.[29] Tope lilitumika kama chokaa ya jengo.[30] Magogo ya mitende yalifungwa pamoja kama nguzo za wima upande wa qibla, huku majani na matawi ya miti hiyo ikitumika kwa ajili ya paa.[31] Kulikuwa na *mihrab* iliyoelekea upande wa *Masjidul-Aqsa*, Palestina, na milango mitatu. Pindi qibla ilipobadilishwa kutoka upande wa Masjidul-Aqsa, Palestina, kuelekea upande wa Kaabah, Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza mlango wa kwanza ufungwe, na badala yake mlango wa pili uliokuwa upande wa Damascus ukafunguliwa.[32]

28. Ziraa moja ni cm 75.
29. Ibn Saad, I, 239.
30. Diyarbakri, I, 344.
31. Bukhari, Salat, 62.
32. Diyarbakri, I, 346.

Vyumba viwili vya ziada viliongezwa kando ya msikiti kwa ajili ya makazi ya Mtukufu Mtume ﷺ na familia yake;[33] na idadi yake iliendelea kuongezeka.

Hasan Basri, ambaye wakati wa utoto wake alivuta hewa ya nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ kutokana na mama yake kuwa msaidizi wa Umm Salama, anasimulia jinsi mtu angeweza kuligusa paa la vyumba hivi,[34] hii ikionesha kuwa vyumba hivyo havikuwa na urefu sana kwenda juu. Milango ya vyumba ilikuwa na mapazia yaliyotengenezwa kwa ngozi nyeusi.[35]

Said ibn Musayyab, mmoja katika maimamu wakubwa wa kizazi cha *Tabiuun*, anaelezea masikitiko yake kuhusu kubomolewa vyumba hivi wakati wa utawala wa bani Umayyah na kuvitenganisha na Msikiti:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, ninatamani lau kama vyumba hivi vingeachwa kaama vilivyokuwa, ili kizazi cha sasa na wale watakaokuja baadaye watembelee eneo hilo na kujionea jinsi Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyokuwa ameridhika na maisha na hivyo kuacha kushindana katika kuhodhi na kujilimbikizia mali!" (Ibn Sad, I, 499-500)

Kwa kuwa Msikiti ulikuwa umefunikwa na matawi na majani ya mtende, mvua inaponyesha, sakafu yake ilikuwa ikibadilika kuwa tope. Siku moja wakati wa mwezi wa Ramadhan, wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiwa katika *itikaaf*, mvua ilinyesha na kuilowesha sakafu ya msikiti na athari ya tope ilionekana usoni mwa Mtukufu Mtume ﷺ baada ya kumaliza kuswalisha swala ya alfajiri.[36]

33. Ibn Saad, I, 240.
34. Ibn Saad, VII, 161; Suhayli, I, 248.
35. Ibn Saad, I, 499.
36. Bukhari, Itiqaf, 1.

Siku nyingine mvua ilinyesha na kulowanisha sakafu. Mtu mmoja alikuja na mchanga kwenye nguo yake na kuumwaga sakafuni ili kuikausha. Mtume ﷺ alivutiwa sana na kitendo hicho, na baada ya swala akaelezea kurishwa kwake kwa kusema:

"Ni hatua ya ajabu na yenye kupendeza!" (Abu Dawud, Salat, 15/458)

Siku moja Tamim'u-Dari ؓ, katika safari yake kutoka Damscus, alileta kiwango kikubwa cha taa, mafuta na vishikio. Siku ya Ijumaa aliingia Msikitini. Alimuagiza mtumishi wake, Abul-Barrad kuweka kiasi cha mafuta na maji ndani ya taa hizo, azitungike ndani ya Msikiti na kuziwasha baada ya jua kuzama. Mtukufu Mtume ﷺ alipoingia msikitini na kukuta msikiti uking'ara kwa taa, aliuliza nani aliyeleta wazo hilo.

Akajibiwa: "Ni wazo la Tamim ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Mtukufu Mtume ﷺ akionekana kuwa mwenye furaha alimwambia Tamim:

"Umeuangaza Uislamu na kuupamba Msikiti wake, Mwenyezi Mungu akupe nuru duniani na Akhera!" (Samhudi, II, 596-597; Ibn Hajar, al-Isaba, II, 18)

Mtukufu Mtume ﷺ alibainisha kuwa *Masjid'un-Nabawi* ni moja kati ya misikiti mitatu bora inayofaa kutembelewa na kuswali ndani yake. (Bukhari, Fadl'us-Salat, 1; Muslim, Hajj, 505-510) Katika *hadith* moja anasema:

"Eneo la baina ya nyumba yangu na *minbar* yangu ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi. *Mimbar* yangu ipo juu ya Bwawa (Kawthar)." (Bukhari, Fadhl'us-Salat, 5; Fadhail'ul-Mdina 11; Muslim, Hajj, 502)

Kwa mujibu wa maneno ya Mtume ﷺ, swala moja inayoswaliwa katika Msikiti wake thawabu zake ni mara elfu moja ya thawabu za swala inayoswaliwa sehemu nyingine, isipokuwa inayo-

swaliwa katika Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu, yaani Kaabah. (Bukhari, Fadl'us-Salat, 1; Muslim, Hajj, 505-510)

Kwa mujibu wa maelezo ya Anas ﷺ, Mtukufu Mtume ﷺ anapozungumza na Waumini ndani ya Msikiti alikuwa akiegemea gogo la mtende. Pakawa na haja ya kutengeneza *mimbar*, hivyo ilipotengenezwa akawa anatolea *khutbah* yake hapo. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ alipopanda kwenye *mimbar* hiyo kwa mara ya kwanza, sauti ya kuugulia mfano wa sauti ya ngamia ilisikika kutoka kwenye gogo hilo kama shara ya maumivu ya kutengwa. Muda huohuo Mtume ﷺ aliteremka juu ya mimbar na kulipiga taratibu gogo hilo. Ni baada ya hatua hiyo ndipo gogo lilipotulia na kuacha kuugulia. (Bukhari, Juma, 26; Tirmidhi, Manaqib, 6/3627)

"Gogo hilo lililia kwa kushindwa kuvumilia hali ya kuwa mbali na *dhikr* ambayo ilikuwa ikisomwa jirani yake", alisema Mtukufu Mtume ﷺ. (Bukhari, Manaqib, 25; Ahmad, III, 300)

Ripoti zimetofautiana kuhusu mahali gogo hilo lilipowekwa baada ya tukio hilo. Taarifa moja inasema kuwa lilifukiwa chini ya *mimbar*, huku taarifa nyingine ikisema kuwa liliwekwa darini. Popote litakapokuwa limewekwa, kuna jambo moja linafahamika vyema. Wakati wa kuujenga upya Msikiti huo wakati wa zama za Ukhalifa wa Othman ﷺ, gogo hilo lilichukuliwa na Ubayy ibn Kaab ﷺ na kuliweka nyumbani kwake mpaka lilipoliwa kabisa na wadudu.[37]

Maulana Rumi katika kitabu chake cha Mathnawi, ametengeneza taswira ya gogo hilo likizungumza katika lugha ya kimaanawi:

"Mtume ﷺ aliteremka kutoka juu ya minbar, akalipigapiga gogo kwa mikono yake mitukufu, akauliza kwa utambuzi wa hali ya juu:

37. Ibn Saad, I, 251-252.

'Unataka nini, ewe gogo? Kwa nini walia? Kuna tatizo gani?" Gogo la mtende likaanza kuzungumza kwa lugha yake lenyewe, likatoa machezo ya upendo na kusema:

'Kuwa mbali nawe, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kumeniungaza na kuwa majivu…kumenijaza huzuni na maumivu yasiyoelezeka. Mimi ndio nguzo yenye bahati na furaha ambayo ulikuwa ukiiegemea wakati wa kutoa hotuba. Lakini sasa umeniacha na kupanda juu ya *minbar*. Sasa minbar ndio egemeo lako. Lakini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ninakuomba uyatambue maumivu yangu, kwa maana ni kiumbe gani Ardhini anayeweza kustahmili kutengana nawe?'

Katika kujibu kilio na ombi la upendo lililotolewa na gogo hilo, Mtume ﷺ, kwa huruma akasema:

'Kwa kuwa walalama kutokana na maumivu ya kutengwa, niambie unachotaka! Je nimuombe Mwenyezi Mungu akubadilishe kuwa mti wa kijani imara na wenye kupendeza, uatakaotoa matunda kwa watu wote, Mashariki na Magharibi? Au nimuombe akufanye kuwa mberoshi mchanga wa Peponi ambapo milele utaendelea kuwa mchanga na maridhawa, kama miti mingine mizuri?'

Baada ya kupokea maneno haya mazuri, mtende ule ukatoa ombi lifuatalo, ukionesha upendo wake uliokuwa ukiwaka ndani ya kina chake kirefu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sitaki chochote kati ya hivyo. Ninachotaka ni kuingia ndani ya maisha yako…hivyo ninakuomba unifukie na kunizika ili nitoweke katika mwili huu wenye kufa. Kwa maana, mti wowote mzuri wenye kumea hupata virutubisho vyake kutoka kwenye jua na maji. Lakini maisha yangu yalipata virutubisho kutoka katika nuru yako. Maisha yangu yameonja ladha ya kuwa jirani yako, kupata joto lak ona kuungua ndani

ya upendo wako. Sitapenda kutenganishwa na ladha hiyo nzuri na tamu. Ninataka kitu cha milele. Nizike ili nipate kufufuliwa pamoja na nuru yak ona kuwa wa milele.'

Hivyo, gogo hilo lilizikwa ili lipate kufufuliwa Siku ya Kiyama likiwa kama mwanadamu."

Mara baada tu ya kuwasili mjini Madina, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Mtukufu Mtume ﷺ katika kutengeneza jamii imara ya Kiislamu ni kujenga Msikiti. Bila shaka kutupilia mbali tofauti za mali na cheo na kukusanyika ndani ya nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu mara tano kwa siku, kuna mchango mkubwa sana katika kuimarisha undugu miongoni mwa Waumini. Ni kwa sababu hiyo kwamba miji ya Kiislamu, kwa ujumla wake, imejengwa kuzunguka misikiti, ambayo imekuwa kama vitovu kwa jamii zinazoizunguka, kiasi kwamba makazi huanza kujengwa kutokea hapo na kupanuka kwenda kwengine.

Wakati wa Zama za Neema, mbali na kuwa nyumba ya ibada, Msikiti pia ulikuwa shule, baraza la kuamua mambo yanayojitokea, kituo cha kujadilia masuala ya kiuongozi na kijeshi, hospitali na sehemu ya kufurahika. Vilevile Msikiti ulikuwa ukitoa malazi kwa Maswahaba wasiokuwa na wake au wasiokuwa na makazi, ambao mara zote walihudhuria masomo, vikao vya mijadala na *dhikr* vilivyokuwa vikifanyika huko, na pia ilikuwa ikitumika kama nyumba ya wageni.



Kuhamasisha Swala ya Jamaah

Mafunzo ya kijamii ni mojawapo ya misingi muhimu sana ya Uislamu. Hatua ya mwanzo kabisa ya mafunzo ya kijamii anayopewa Muislamu ni kupitia kujumuika katika swala ya pamoja, yaani swala ya jamaah, ambayo ni nguzo muhimu sana inayoifanya jamii ya

Kiislamu iendelee kuwa imara na madhubuti. Mahali popote pale, swala ya jamaah hudhihirisha na kuonesha kielelezo cha moyo wa kijamii na umoja wa Uislamu.Hivyo, katika kuweka na kuasisi umoja na mshikamano baina ya wafuasi wake, Uislamu ulilifanya suala la kutekeleza ibada ya swala ya jamaah kuwa alama ya Muislamu, na kwamba ushahidi wa kwamba mtu husika ni Muumini huangaliwa kama anaingia msikitini au la. Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Mtakapomuona mtu akiwa na mazoea ya kuhudhuria msikitini basi shuhudieni kuwa ni muumini, kwa maana Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسَاجِدَ اللَّهِ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ

'Hakika wanao amirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala…'" (at-Tawba, 18) (Ibn Majah, Masajid, 19)

Umuhimu wa kuiimarisha misikiti kimwili ni sawa na kuiimarisha kiroho na kimaanawi kwa kuhudhuria na kushiriki swala za jamaah, ambalo ni jukumu nyeti kwa mja. Maneno yafuatayo yaliyosimuliwa kupitia kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, yanasema:

"Hakika vitu vinne ndio vigeni ardhini: Qur'an iliyohifadhiwa akilini mwa dhalimu, msikiti ambao hauswaliwi swala ya jamaah licha ya kuwa katika ardhi ya Waislamu, Qur'an isiyosomwa licha ya kuning'inia ukutani ndani ya nyumba na mtu mwema anayeishi ndani ya watu waliofisidika." (Daylami, III, 108/4301)

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka msisitizo mkubwa sana kwenye swala ya jamaah kiasi kwamba ndani ya Qur'an anaamrisha iswaliwe hata wakati wa vita na kufundisha jinsi inavyotakiwa kuswaliwa katika mazingira hayo.

Abu Hurayra ﵁ anasema:

"Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa safarini akapumzika katika eneo la baina ya Dajnan na Usfan. Waabudu masanamu wakapanga njama wakisema:

'…tujiandae na tuwashambulie Waislamu wakati wa swala ya alasiri, kwa maana hiyo ndiyo swala wanayoipenda zaidi kuliko hata watoto na wazazi wao!' Hapo Jibril ﵇ akaja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akiwa na aya ya 102 ya surat Nisa inayoelezea jinsi swala inavyotakiwa kuswaliwa wakati wa vita." (Tirmidhi, Tafsir, 4/21)

Vyovyote mazingira yatakavyokuwa, Muislamu anatakiwa kuakhirsha swala yake na kuiswali kuiswali katika jamaah.

Baadhi ya *hadith* za Mtukufu Mtume ﷺ zinazohamasisha na kushajiisha mno swala ya jamaa ni pamoja na:

"Swala iliyoswaliwa katika jamaah ni bora mara ishirini na tano kuliko swala iliyoswaliwa na mtu pekee yake." (Bukhari, Adhan, 30)

"Mwenye kuhudhuria msikitini usiku na mchana, Mwenyezi Mungu humuandikia pepo kila anapokwenda na kurudi." (Bukhari, Adhan, 37)

"Mwenye kuchukua wudhu kisha akaenda kuswali, Mwenyezi Mungu humpa thawabu kila anaponyanyua mguu wake wa kulia na humfutia madhambi kila anaponyanyua mkono wake wa kushoto, hata kama msikiti utakuwa karibu au mbali. Akienda msikitini na kuswali jamaah, husamehewa dhambi zake, hata kama atakuta wameswali sehemu ya swala, akaungana nao na kisha akamaliza sehemu iliyobaki. Vilevile hata kama atakuta wameshamaliza kuswali na hivyo akaswali peke yake." (Abu Dawud, Salat, 50/563)

"Mwenye kusubiri msikitini ili swala ianze huhesabiwa kuwa yuko katika swala." (Ibn Majah, Masajid, 14)

Abu Hurayra ﵁ anasimulia:

"Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuliza, 'Je nikujulisheni matendo yenye kufuta dhambi zen una kuongeza daraja zenu?'

'Ndiyo, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', tulijibu.

'Kuchukua wudhu licha ya tabu zote, kuongeza hatua kuelekea msikitini na kusubiri swala nyingine baada ya kuisha kwa swala aya awali…Hizo ndizo *ribat*[38] za kweli." (Muslim, Taharat, 41)

Yazid ibn Amir ﵁ anasimulia tukio jingine:

"Siku moja niliwasili kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati akiswali. Nilisubiri nikawa sijaungana naye katika jamaah. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipotugeukia baada ya kumaliza kuswali, aliniona nikiwa nimekaa pembeni. Akauliza:

'Ewe Yazi, bado hujawa Muislamu?'

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakuna shaka mimi ni Muislamu', nilijibu.

'Sasa kitu gani kimekuzuia usiswali jamaah?' aliuliza.

Nikamjibu, 'Niliswali nyumbani kwa kuwa nilidhani kuwa mtakuwa mmeshaswali.' Hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaniusia:

'Unapofika msikitini ukakuta watu wanaswali, ungana nao. Kama utakuwa umeshaswali, hiyo itahesabiwa kama sunna; na ile uliyoswali mwanzo itahesabiwa kuwa ni faradhi.'" (Abu Dawud, Salat, 56/577)

---

38. *Ribat* ina maana nyingi kama vile kuidhibiti nafsi na kuilazimisha kuwa na utiifu, kushiriki katika ulinzi wa mipaka (ya dola ya Kiislamu) au kushiriki katika vita katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. *Ribat* ambayo ni chanzo cha thawabu nyingi, imesifiwa kwa misisitizo mkubwa ndani ya Qur'an na Sunnah.

Katika kuonesha kuwa hakuna udhuru wowote wa kutoshiriki swala ya *jamaah*, Mtukufu Mtume ﷺ aliwataka Waislamu kuratibu na kupanga shughuli zao kulingana na adhana tano za kila siku. Mfano hatua hiyo ni pale Abdullah ibn Umm Maqtum ؓ alipokuja kwa Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ na kumuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kama unavyojua, mimi ni kipofu, na nyumba yangu iko mbali na msikiti. Nina mtu wa kuniongoza lakini anashindwa kunisaidia. Je, ninaweza kuruhusiwa kuswali nyumbani?"

"Je, unaisikia adhana?" Mtukufu Mtume ﷺ alimuuliza Ibn Maqtum ambaye alikubali kuwa anaisikia adhana.

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia, 'Sioni udhuru wowote wa wewe kutoshiriki swala ya jamaah." (Abu Dawud, Salat, 46/552)

Aidha, kuhusu kwenda kuswali kwenye msikiti wa mbali, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Wenye kupata thawabu nyingi za swala ni wale waokuja kuswali wakitembea kutoka mbali…na yule anayesubiri kuswali jamaah nyuma ya imam ana thawabu nyingi kuliko yule anayeswali haraka haraka nyumbani kisha akalala." (Bukhari, Adhan, 31)

"Kadiri nyumba inavyokuwa mbali zaidi na msikiti ndivyo anavyopata thawabu nyingi wakati wa kuja kuswali." (Abu Dawud, Salat, 48/556)

Mtukufu Mtume ﷺ alitoa maonyo mbalimbali kwa wale wanashindwa kuhudhuria swala ya jamaah. Ubayy ibn Kaab ؓ anasimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituswalisha swala ya alfajiri, kisha akageuka na kuuliza kama mtu fulani alikuwepo. İkabainika kuwa hakuwepo. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi

Mungu ﷻ akauliza kama mtu mwingine alikuwepo. Naye ikabainika kuwa hakuwepo. Hapo Mtume ﷺ akasema:

'Hizi swala mbili (alfajiri na ishaa) ndizo swala ngumu zaidi kwa wanafiki. Kama mngejua thawabu zinazopatikana katika swala hizi, mngehudhuria jamaah hata kwa kutambaa. Safu ya kwanza ni mfano wa safu ya malaika. Kama mngelijua ubora wa safu hii, mngeshindana kusimama mahalihapo. Swala ambayo mtu huiswali akiwa pamoja na mwenzake ni bora na ina thawabu na malipo mengi kuliko ile anayoswali akiwa peke yake. Swala ambayo mtu huiswali akiwa na watu wawili ni bora na ina thawabu nyingi kuliko anayoswali wakiwa na mtu mmoja. Kadiri idadi inavyoongezeka ndivyo Allah anavyozidi kufurahi.'" (Abu Dawud, Salat, 47/554)

Katika *hadith* nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Swala ya mtu aliye jirani na msikiti hukamilika anapoiswali msikitini." (Ibn Abi Shayba, I, 303)

Ali ؓ alipoulizwa kuhusu 'jirani wa mskiti' aliyekusudiwa katika maneno hayo ya Mtume ﷺ alijibu:

"Kila anayeisikia sauti ya adhana." (Bayhaki, as-Sunanu'l-Kubra, III, 57)

Maneno yafuatayo ya Mtukufu Mtume ﷺ yana maonyo makali kwa wale wanaoacha kuswali jamaah:

"Kama katika kijiji au kundi fulani kuna watu watatu wasioswali jamaah, shetani huwazingira na kuwashinda. Hivyo, endeleeni kuswali jamaah, kwa maana kondoo anayejitenga na wenzake ndiye anayeliwa na mbwa mwitu." (Abu Dawud, Salat, 46/547)

"Watu watakapoiacha jamaah, Mwenyezi Mungu ataipiga mihuri mioyo yao na kuwaweka katika kundi la walioghafilika." (Ibn Majah, Masajid, 17)

Adhana ya Kwanza

Mwanzo, maneno ya 'salaa, salaa'ndiyo yaliyokuwa yakitumiwa na Waislamu kujulishana muda wa swala. Neema ya adhana ilikuja baadaye.

Wakati huo huo, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akishauriana na Maswahaba zake kuhusu njia nzuri inayofaa kutumika wakati wa kuwaita Waislamu kwenye swala. Baadhi walisema, "Muda wa swala unapofika tupandishe bendera ili Waislamu wanapoiona waambizane." Lakini Mtukufu Mtume ﷺ hakulipenda wazo hilo, pia hakulipenda wazo la kupuliza tarumbeta, kwa sababu ni "kifaa kilichokuwa kikitumiwa na Mayahudi." Vile vile, Mtukufu Mtume ﷺ hakulipenda wazo la kugonga kengele, ambalo lililetwa kwenye meza ya mjadala, kwa kuwa ni zana "iliyokuwa ikitumiwa na Manaswara." Abdullah ibn Zayd رضي الله عنه[39], ambaye alikuwepo wakati wa majadiliano hay ona kuweza kuzitambua hisia za Mtukufu Mtume ﷺ, alirejea nyumbani. Akiwa amejilaza na akiwa hali ya baina ya kusinzia na kuwamacho, aliota ndoto ya adhana. Haraka sana akarudi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akamweleza jinsi alivyokuwa "amefundishwa adhana alipokuwa amelala."

39. Abdullah ibn Zayd ibn Asim al-Ansari رضي الله عنه alisifiwa na Mtukufu Mtume ﷺ kwa kumlinda kwa karibu wakati wa vita ya Uhud. Abdullah hakuwa mtu pekee aliyeonesha ushujaa katika vita hiyo; wakati wote wa vita familia yake yote ilionesha ujasiri wa hali ya juu, kiasi kwamba Mtukufu Mtume ﷺ aliwaombea dua ili wapate kuwa jirani naye peponi. Mara kwa mara, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiitembelea nyumba ya Abdullah ibn Zayd, ambapo aliswali swala nyingi hapo. Ibn Zayd al-Ansari رضي الله عنه alikuwa miongoni mwa Maswahaba walikuwa wakipendwa mno na Mtume ﷺ. Abdullah alipopata taarifa za kifo cha Mtukufu Mtume ﷺ aliumia mno, kiasi kwamba alimuomba Mwenyezi Mungu, '…ewe Allah yachukue macho yangu nisipate kumuona yeyote baada ya Muhammad ﷺ!' Dua yake ilipokelewa, na baada ya hapo akaishi maisha yake yote akiwa kipofu. (Qurtubi, V, 271) Baadaye aliuawa kishahidi pamoja na watoto wake wawili katika tukio la Harra.

Baada ya kubaini kuwa hata Omar ﷺ alikuwa ameiona ndoto hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ akamuagiza Bilal ﷺ kuyarudia kwa sauti maneno hayo ambayo Abdullah ibn Zayd ﷺ alikuwa ameyasikia. Hivyo ndivyo sauti ya adhana ilivyosikika kwa mara ya kwanza. (Abu Dawud, Salat, 27/498)

Adhana ikawa sunna yenye nguvu ambayo ilikaribia kuwa wajibu, kwa kuwa ilithibitishwa na ndoto ya kweli, Sunnah ya Mtume ﷺ na Qur'an Tukufu ambayo inasema:

وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ

"Na mnapo adhinia Sala…" (al-Maida, 58)

Lazima ieleweke kuwa, japokuwa Abdullah ibn Zayd ﷺ ndiye aliyekuwa kiunganishi katika kuwepo kwa adhana, daima Mtukufu Mtume ﷺ ndiye aliyekuwa akipokea wahyi na ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ni baada tu ya kuthibitishwa na Mtukufu Mtume ﷺ, ndipo adhana ilianza kutumika kama njia ya kuwaita Waislamu. Bilal Habashi ﷺ alipotoa adhana kwa mara ya kwanza, wito huo wa Kimungu ulifika kila kona ya mji wa Madina, mwangwi wake ukalitetemesha anga na Waislamu wakamiminika Msikitini.

Licha ya mawazo mengi yaliyotolewa kuhusu njia inayofaa kuwaita Waislamu Msikitini, Mtukufu Mtume ﷺ hakuzikubali, isipokuwa adhana ambayo aliipokea kwa shaukukubwa. Hakika adhana ni ufupisho wa mafundisho ya Uislamu kuhusu Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtume Wake, dhana ya ibada na maisha kwa ujumla, ambayo muumini anatakiwa kushikamana nayo. Hivyo, tunaweza kusema kuwa Mtume ﷺ alichagua njia bora ya kuwaita watu kwenye swala.

Adhana ambayo imethibitishwa na Qur'an na Sunnah, kwa zaidi ya miaka 1400, imeendelea kuwapa Waislamu wito kutoka

mbinguni. Ni wito unaotumiwa na Waislamu wote duniani n ani wito wa kimataifa, ndio maana hauwezi kusomwa na kutolewa katika muundo mwingine tofauti na muundo wake wa asili. Wito huu ambao hukaririwa, huwaita watu kwenye uzingatiaji.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Mnaposikia adhana, rudieni kama anavyosema muadhini, neno kwa neno. Kisha nitakieni rehma, kwa maana Mwenyezi Mungu humtakia rehma mara kumi yule anayenitakia rehma. Kisha ombeni dua nipate *wasilah*, daraja maalumu Peponi ambayo atapewa mja mmoja tu. Ninataraji kuwa mtu huyo atakuwa mimi. Nitawajibika kuwaombea wale wanaotaka *wasilah* kutoka kwa Mwenyezi Mungu." (Muslim, Salat; Abu Dawud, Salat, 26/523)

Katika *hadith* nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ anawahakikishia Pepo wale wanaoitikia adhana kwa kufuatisha maneno yanayotamkwa na muadhini.[40] Na kuhusu dua inayosomwa baada ya adhana, anasema:

"Hakika nitamuombea yule anayesoma dua hii baada ya kuisikia adhana: Ewe Mola wa wito huu na swala yenye kusimamishwa! Mpe Muhammad ﷺ *wasilah* na *fadhilah* na umfufue kwenye daraja ya *Mahmud* ambayo ulimuahidi!" (Bukhari, Adhan, 8; Abu Dawud, Salat, 37/529)

Kuna *ahadith* nyingi ambazo zimezungumzida fadhila na ubora wa adhana. Baadhi yake ni hizi zifuatazo:

"Dua mbili kwamwe hazikataliwi: dua inayosomwa baada ya adhana, na ya pili ni ile inayosomwa wakati wa vita, pindi tu pande mbili zinapoanza kushambuliana." (Abu Dawud, Jihad, 39/2540)

40. Muslim, Salat, 12.

"Lau kama watu wangejua thawabu za wale wanaotoa adhana na wale wanaosimama safu ya kwanza katika swala, na wakawa hawana njia nyingine zaidi ya kupiga kura, hakika wangefanya hivyo." (Bukhari, Adhan, 9, 32; Muslim, Salat, 129)

"Adhana inapotolewa kwa ajili ya swala, Shetani hukimbia akipiga kelele kwenda mahali ambapo hawezi kusikia adhana. Adhana inapokwisha hurudi; na hukimbia tena *iqamah* inapoanza. Kisha hurudi tena, akapenya katika njia ielekeayo kwenye moyo wa mtu, humtia wasiwasi akamwambia, 'fikiria hili, kumbuka jambo lile'; mambo ambayo mwanzo hayakuwepo katika fikra za mtu, kiasi kwamba mtu anapochukuliwa na wasiwasi huu husahau alikuwa sehemu gani ya swala anayoswali." (Bukhari, Adhan, 4; Muslim, Salat, 19)

Suffa: Shule ya Maarifa na Hekima

Sehemu moja ya Msikiti wa Madina ilitengwa kwa ajili ya Suffa[41], eneo la kivuli lililofunikwa kwa majani ya mitende na kutumika kwa ajili ya makazi na malazi ya Waislamu masikini au wasiokuwa na familia, wakijulikana kama watu wa *Suffa*[42]. Idadi yao ilikuwa ikitofautiana kutokana na vifo, kuoa au kuondoka kwa sababu mbalimbali kama vile kuhamia sehemu nyingine au kwenda vitani; japokuwa inaelezwa kuwa wakati fulani idadi yao ilifikia watu sabini. Kuna baadhi ya vyanzo vinasema kuwa idadi yao ilifikia mia moja. Mtume ﷺ ndiye aliyekuwa akigaharamia mahitaji ya Maswahaba hao, na wakati mwingine akiwahamasisha Maswahaba wenye kupenda kujitolea na wenye uwezo wawasaidie.

41. *Suffa* ni neno lililokuwa likitumika kumaanisha sehemu ya nyumba za zamani ambayo ilikuwa imeinuliwa, kama makochi, kwa ajili ya kukaa. Neno sofa linalotumika katika lugha ya Kiswahili linatokana na istilahi hii.
42. Ibn Saad, I, 255.

Abu Hurayra ﷺ, ambaye mwenyewe alikuwa miongoni mwa watu wa *Suffa*, anasimulia:

"Watu wa *Suffa* walikuwa ni wageni katika Uislamu. Hawakuwa na familia wala ndugu wa karibu wa kuwahifadhi. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiwapelekea kila msaada uliokuwa ukimfikia, bila hata kujibakishia chochote. Anapoletewa zawadi, alikuwa akichukua sehemu ndogo tu kwa ajili yake, na inayobaki akiwatumia watu wa *Suffa*, akishirikiana nao hata ile sehemu yake ndogo" (Bukhari, Riqaq, 17)

Kwa mara nyingine Abu Hurayra ﷺ anaeleza:

"Mimi mwenyewe niliwaona watu sabini wa *Suffa*. Hakuna yeyote kati yao aliyekuwa na mavazi ya kutisha kujisitiri mwili wote. Ima walikuwa na *izar* ya kujisitri upande wa chini, au *rida* ya kujisitiri upande wa juu; hivyo walikuwa wakifunga mavazi yao kuzunguka shingo zao. Baadhi ya mavazi hayo yalikuwa yakifika kwenye nusu ya mapaja, huku mengine yakifika kwenye nyayo za miguu yao, japokuwa bado walikuwa wakizishikilia nguo zao ili maeneo yao ya siri yasibaki wazi." (Bukhari, Salat, 58)

Maelezo yafuatayo yanatoka kwa Fadala ibn Ubayd ﷺ:

"Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akiswalisha, baadhi ya watu walikuwa wakizimia nyuma yake kutokana na njaa kali. Watu hawa sio wengine bali ni watu wa *Suffa*. Mabedui waliokuwawakiwaona walikuwa wakidhani kuwa ni wendawazimu. Baada ya kumaliza kuswali, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiwaendea wale waliokuwa wamezimia kutokana na njaa na kuwafariji kwa kuwaambia, 'Lau ungejua malipo mtakayopata mbele ya Mwenyezi Mungu, mngetamani kuwa na umaskini na uhitaji zaidi ya huu.'" (Tirmidhi, Zuhd, 39/2368)

Abdurrahman ibn Abi Bakr ﷺ anasimulia tukio lifuatalo:

"Watu wa *Suffa* walikuwa maskini mno. Ninakumbuka siku moja Mtume ﷺ alisema, 'Mwenye chakula cha watu wawili, achukue mtu wa tatu kutoka *Suffa*, na mwenye chakula cha watu wanne, achukue mtu wa sita kutoka *Suffa*.'

Baba yangu, Abu Bakr, alileta watu watatu nyumbani kwetu. Na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akachukua watu kumi. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba chakula kilikuwa kikiongezeka kila tunapokula. Wageni walikuwa mpaka wakatosheka, lakini bado chakula kilibaki kama kilivyokuwa mwanzo. Baba yangu alikiangalia chakula hicho kwa muda kisha akamuuliza mkewe kilichotokea, naye hakuwa na la kufanya zaidi ya kusema, 'Ninaapa kwa nuru ya macho yangu kuwa chakula hiki kimekuwa kingi mara tatu zaidi ya kilivyokuwa mwanzo.'" (Bukhari, Mawaqit, 41; Manaqib, 25; Adab, 87-88; Muslim, Ashriba, 176-177)

Tukio hili ni mfano halisi wa neema na baraka zitokanazo na mtu kuwa na moyo safi na ukarimu.

Watu wa *Suffa* walikuwa wakifanya kaz ipindi fursa inapopatikana na muda uliobaki wakiutumia kwa ajili ya kufanya ibada na kusoma. Wale waliokuwa na nguvu za kutosha walikuwa wakifanya kila linalowezekana, kama vile kubeba viriba vya maji au kuni migongoni mwao kutoka kwenye vilima vya jirani, wakienda kuziuza na kuwanunulia wenzao chakula kutokana na pesa wanayoipata.[43] Kutokana na kuwa na tahadhari katika kuchunga utu na heshima yao, walikuwa wakijiepusha na tabia ambayo inaweza kuondosha kivuli za maadili yao. Hivyo walikuwa wakijiepusha mno kuomba vitu kutoka kwa watu.

Watu wa *Suffa* ni watu waliokuwa karibu zaidi na chanzo cha dini, ndio waliovuta zaidi hewa ya mazingira ya Mtukufu

43. Bukhari, Maghazi 28, Jihad 9; Ibn Saad, III, 514.

Mtume ﷺ kuliko watu wengine. Hivyo walielimika kwaharaka zaidi kuliko Maswahaba wengine. Walimu wao walikuwa ni Maswahaba wakubwa kama vile Ubayy ibn Kaab, Abdullah ibn Masud, Muadh ibn Jabal na Ubada ibn Samit ﷺ, na mwalimu wao mkuu alikuwa Mtukufu Mtume ﷺ.

Maswahaba wa *Suffa* walipewa mafunzo ya hali ya juu na ya haraka. Uthibitisho wa hilo ni kwamba *mukthrun* wote, yaani Maswahab walipokea hadith nyingi, ni Maswahaba wa *Suffa*. Aliyekuwa mashuhuri zaidi miongoni mwao ni Abu Hurayra ﷺ ambaye alisikika akisema:

"Watu wanashangaa kwamba 'Abu Hurayra anasimulia *ahadith* nyingi'. Lakini wakati ndugu zetu wa Muhaajiruun wakiwa wameshughulishwa na kufanya biashara sokoni na Ansaar wakiwa wameshughulishwa na kulima mashamba yao, Abu Hurayra alikuwa pembezoni mwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sio kwa mambo ya kidunia, bali akishuhudia mambo mengi ambayo hawakuweza kuyashuhudiana kujifunza mambo ambayo hawakuweza kujifunza." (Bukhari, Ilm, 42)

Wajumbe mbalimbali ambao walikuwa wakiwasili Madina kwa muda mfupi kwa lengo la kujifunza Uislamu walikuwa wakikutana na Mtukufu Mtume ﷺ na kujifunza yale wasiyoyajua kutoka kwa Maswahaba wa *Suffa*. Kila ilipohitajika kutumwa mwalimu kwenda katika makabila ambayo yalikuwa yameingia katika Uislamu, mara nyingi mwalimu huyo alikuwa akiteuliwa kutoka katika watu wa *Suffa*.

Aidha, Maswahaba wa Suffa wamepewa daraja kubwa baada ya *Khulafa'ur-Rashidin*, yaani Makhalifa Waongofu, baada ya *Asharat'ul-Mubashshara*, yaani Maswahaba waliobashiriwa pepo katika uhai wao, na *As'habul-Badr*, yaani Maswahaba walioshiriki katika Vita ya Badr. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

لِلْفُقَرَاءِ الَّذِينَ أُحْصِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ ضَرْبًا فِي الْأَرْضِ يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ أَغْنِيَاءَ مِنَ التَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُمْ بِسِيمَاهُمْ لَا يَسْأَلُونَ النَّاسَ إِلْحَافًا ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ

"Nawapewe mafakiri walio zuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasio weza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiye wajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang›ang›analii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayo toa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anaijua." (al-Baqara, 273)

Habbab ﷺ anasimulia:

"Siku moja Aqra ibn Habis na Uyayna ibn Hisn, washirikia waliokuwa wakijulikana kwa tabia ya kujiona, walikujwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakamkuta akiwa amekaa pamoja na watu masikini na wanyonge kama vile Bilal, Suhayb, Ammar na mimi mwenyewe. Kutokana na kutudharau, walimwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa majivuno, 'Tunataka ututengee sehemu maalumu ili kwamba Waarabu wengine watakapokuja watambue ubora wetu juu yao. Unajua vyema kuwa wageni wengi kutoka makabila mabalimbali ya Arabia yote huja kututembelea. Hatutajisikia vizuri wakituona tukiwa katika mazingira sawa na hawa watumwa. Hivyo, watakapokuja waondoshe…lakini ukitaka unaweza kukaa nao sisi tukiwa hatupo!'

'Sawa', alisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Wakasema, 'Hatuwezi kuyachukua maneno hayo kama jibu. Iweke ahadi hiyo kwenye maandishi.' Hivyo, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimuitisha Ali ﷺ na kipande cha karatasi ili aandike

makubaliano hayo. Wakati huo huo tulikuwa tumekaa kwenye kona. Hapo Jibril عليه السلام akaja na Ufunuo ufuatao:

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۖ مَا عَلَيْكَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِنْ شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ

"Wala usiwafukuze wanao mwomba Mola Mlezi wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi yake. Si juu yako hisabu yao hata kidogo, wala hisabu yako si juu yao hata kidogo, hata uwafukuze na uwe miongoni mwa wenye kudhulumu." (al-Anam, 52)

وَكَذَٰلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهَٰؤُلَاءِ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ بَيْنِنَا ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ

"Na hivi ndivyo tunavyo wajaribu wao kwa wao, ili waseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu amewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu hawajui wanao shukuru?" (al-Anam, 53)

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ ۖ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

"Na wanapo kujia wanao ziamini Ishara zetu waambie: Assalamu alaikum! Amani iwe juu yenu! Mola wenu Mlezi amejilazimisha rehema…" (al-Anam, 54)

Muda huo huo Mtume ﷺ akaiweka pembeni karatasi ambayo alitaka kuandika makubaliano hayo akatuita. Tulipokwenda tulim-

kuta akisema, Amani iwe juu yenu! Mola wenu Mlezi amejilazimisha rehema…'

Tulikuwa tumekaa karibu naye sana kiasi kwamba magoti yetu yalikuwa yakigusana na magoti yake. Baada ya Ufunuo huo, tuliendelea kukaa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama zamani na alikuwa akiondoka pindi anapotaka kufanya hivyo. Lakini ilipteremka aya isemayo:

وَاصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۖ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

"Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia…" (al-Kahf, 28), akaacha kufanya hivyo pia. Baada ya hapo tulianza kuwa na wasitani katika vikao vyetu. Baada ya kuka ana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa kipindi fulani cha muda tulikuwa tukionesha busara na kuanza kuondoka, ili apate kupumzika." (Ibn Majah, Zuhd, 7; Tabari, Tafsir, VII, 262-263)

Baada ya kuteremka kwa Ufunuo uliotajwa hapo juu, muda huo huo Mtukufu Mtume ﷺ alinyanyuka na kwenda kuwatafuta Masikini Waislamu, akawaona wakiwa sehemu ya nyuma ya msikiti, wakiswali. Macho yake yalipotua kwao, akasema, "Himidi ni za Mwenyezi Mungu aliyeniamrisha kuisubirisha nafsi yangu pamoja na watu hawa katika umma wangu! Sasa, nitakuwa ubavuni mwenu katika kipindi chote cha uhai na umauti wangu!" (Wahidi, uk. 306)

Abu Said رضي الله عنه anasimulia tukio lifuatalo:

"Nilikuwa nimekaa pamoja na kundi la watu masikini katika Muhajirun. Baadhi yao, kutokana na kutokuwa na mavazi ya kutosha

kusitiri miili yao, walikuwa wakijibanza nyuma ya wenzao ili kujisitiri. Mtu mmoja alikuwa akitusomea Qur'an. Mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitokea, akasubiri kwa muda huku akiwa amesimama. Alipowasili, mtu yule aliyekuwa akitusomea Qur'an akaacha kusoma. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatutolea salam una kutuuliza:

'Mnafanya nini?'

Tukasema, 'Mtu huyu ni mwalimu wetu, anatusomea Qur'an naşi tunakisikiliza Kitabu cha Mwenyezi Mungu.'

Mtukufu Mtume ﷺ aliposikiahivyo, akasema, 'Himidi ni za Mwenyezi Mungu ambaye, katika umma wangu, ameumba wale ambao ninatakiwa kuisubirisha nafsi yangu pamoja nao.'[44]

Kisha kwa staha ya hali ya juu, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikaa katikati yetu. Aliashiria kwa mkono wake, akasema:

'Tengenezeni duara kama hivi…'

Tulitengeneza mkao wa duara pembezoni mwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, huku tukiwa tumemuelekea. Ndipo alipotupa habari njema kwa kusema:

'Furahini enyi Maskini wa Muhajiruun…Ninawapa habari njema ya nuru kamili huko Akhera. Mtaingia Peponi nusu siku kabla ya matajiri…nusu siku hiyo ni sawa na miaka mia tano ya duniani!'" (Abu Dawud, Ilm, 13/3666)

44. Maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ yanaashiria aya ya 28 ya Surat Kahf. Katika aya hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anamuamrisha Mtume ﷺ kuisubirisha nafsi yake pamoja na masikini wachache, ambao ndio waliokuwa wa mwanzo kuingia katika Uislamu, pale wanapokabiliwa na shida na kuamiliana nao kwa umakini.

Mtukufu Mtume ﷺ Amuoa Bibi Aisha ؓ

Kwa kweli ndoa baina ya Mtukufu Mtume ﷺ na bibi Aisha ؓ ilifungwa Makka kabla ya Hijra, lakini ikamaliziwa na kuingia katika uhalisia baadaye mjini Madina.

Bibi Aisha ؓ anasimulia tukio hilo kama ifuatavyo:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipohamia Madina, aliwaacha mabinti zake pamoja na mimi mjini Makka. Baadaye, alimtuma Zayd ibn Haritha na Rafi kwenda Makka, akawapa ngamia wawilina dirham 500 kwa ajili ya kugharamia safari yao. Vivyo hivyo, baba yangu Abu Bakr alimtuma Abdullah ibn Urayqit kuja pamoja nao, akampa ngamia wawili au watatu wa ziada, pamoja na ujumbe kwa kaka yangu Abdullah akimwambia afanye maandalizi ya safari ya mama yangu Umm Ruman, dadangu Asma pamoja nami kwenda Madina. Abu Rafi aliandaa ngamia kwa ajili ya Fatma, Umm Kulthum na Sawda bint Zama, naye Zayd akamuandalia Umm Ayman na mwanaye Usama. Hivyo sote tukaanza safari.[45] Tulipofika Bayzar jirani na Mina, ngamia wetu alikimbia, huku mimi na mama yangu tukiyumbayumba ndani ya *hawdaj*[46] yake. Mama yangu alishikwa na hofu; 'maskini mwanangu', nilimsikia akisema. Lakini muda mfupi baadaye, Allah alijaalia ngamia wetu akatulia na hivyo tukaweza kuungana na wenzetu.

Mwishowe tulifika Madina kwa salama na amani. Japokuwa nilikuwa nimeshafunga ndoa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mjini Makka, niliendelea kuishi na familia yangu. Wakati huo, Msikiti na vyumba vinavyouzunguka vilikuwa vimejengwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuhamia katika chumba chake, na

45. Zaynab ؓ alilazimika kubaki Makka kwa muda mrefu kidogo kwa sababu mumewe Abu'l-As ibn Rabi' alikataa kumpa ruhusu.

46. *Hawdaj* ni tandiko dogo lililojengewa juu ya mgongo wa ngamia kwa ajili ya kuwahifadhi wanawake wakati wa safari.

familia yake ikafanya vivyo hivyo. Muda mfupi baadaye, babangu alimuuliza mjumbe wa Mwenyezi Mungu kitu kilichokuwa kinamzuia kukamilisha ndoa yake.

"*Mahr*", alijibu.

Hivyo, baba yangu alimtumia *uqiyya*[47] kumi na mbili na nusu, ambapo mwezi wa Shawwal Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliikamilisha ndoa yetu.[48] Hakuna ngamia wala kondoo aliyechindwa wakati wa harusi; Saad ibn Ubadah[49] ﷺ ndiye aliyetuma chakula ndani ya wekeo kubwa.[50]

47. *Uqiyya* ilikuwa ikitumiwa kama sarafu ya fedha. Vilevile ilitumiwa kama kipimo cha mzani. *Uqiyya* moja inakaribia kuwa sawa na gramu 128.

48. Ibn Saad, VIII, 58, 62-63.

49. Saad ibn Ubadah ﷺ alisilimu katika *Baiyah* ya Pili ya Aqabah. Alikuwa miongoni mwa wawakilishi kumi na mbili waalioteuliwa huko. Utajiri wake uliendana na ukarimu wake. Katika kipindi chote ambacho Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiishi katika nyumba ya Khalid ibn Zayd ﷺ, kila siku Saad alikuwa akiagiza chakula kwa Mtume ﷺ. Hakuna siku ambayo ilipita bila kuandaa chakula na kuwaalika watu wote. Kila siku aliwapa chakula watu wa *Suffa*. Alibeba bendera ya Khazraj katika vita zote. Wakati wa vita ya Dhu Qarad, alijitolea ngamia kumi wakiwa wamebeba mizigo ya tende kuwapelekea wanajeshi. Mtukufu Mtume ﷺ alifurahishwa na kitendo hicho, akamuombea, 'Ewe Mwenyezi Mungu mpe rehma Zako Saad na familia yake!' Walitoa chakula kwa jeshi lote la Kiislamu wakati wa Vita ya Banu Quraydha. Uhai na mali yake alivitumia kama nyenzo ya mapambano katika njia ya Mwenyezi Mungu mpaka alipofariki dunia. Kwa kuwa nyumba yake ilikuwa nje kidogo ya mji wa Madina na kujikuta akiwa mbali na Msikiti wa Mtume ﷺ, ilibidi Saad ajenge msikiti mdogo huko huko. Baada ya Abu Bak ﷺ kuteuliwa kuwa Khalifa, Saad ibn Ubadah ﷺ alihamia Hawra, jirani na Damascus, na huko alifariki dunia mwaka 635. Alizikwa katika mji mdogo wa Ghuta.

50. Ahmad, VI, 211.

Hali ya Mji wa Madina

Zama za Madina, wakati Uislamu na Waislamu waliposhika hatamu, kilikuwa kipindi cha uhai na nishati kilichojaa harakati zenye neema zilizoifanya misingi mikuu ya Uislamu kupata nguvu isiyotetereka; na damu iliyomwagika katika vita zote ilikuwa katika kuimarisha zaidi misingi hiyo.

Mwanzo, hali ya mji wa Madina haikuwa na tashtiti yoyote kabisa, licha ya mji huo kuwakaribisha wahamiaji wapya kwa moyo mkunjufu. Kulikuwa na hatari kadhaa zilizofuata, ambazo mwanzo zilichochewa na wanafiki na Wayahudi, ambao walipandikiza mbegu za uadui bila kuchoka kutokana na msimamo wao pinzani dhidi ya kuibuka kwa Uislamu.

Alama makhsusi ya wanafiki ilikuwa ni kuendelea na imani yao za kuabudu masanamu licha ya kuonesha kwa nje kuwa wameukubali Uislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimzindua Mtume Wake juu ya hatari ya wanafiki na wakati huohuo akatoa onyo na karipio kali dhidi yao:

وَمِمَّنْ حَوْلَكُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ مُنَافِقُونَ ۖ وَمِنْ أَهْلِ الْمَدِينَةِ ۖ مَرَدُوا عَلَى النِّفَاقِ
لَا تَعْلَمُهُمْ ۖ نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ ۚ سَنُعَذِّبُهُمْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ

"Na katika mabedui walio jirani zenu wamo wanaafiki; na katika wenyeji wa Madina pia wapo walio bobea katika unaafiki. Wewe huwajui. Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa." (at-Tawba, 101)

Wanafiki walikuwa mahiri sana katika hila na hadaa zao kiasi kwamba hata Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe hakuweza kûhisi na kuzigundua njia na mbinu zao. Alikuja kugundua baada ya

kuambiwa kupitia wahyi na ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wanafiki walikuwa wakihofia kujiingiza katika tabia ambayo inaweza kuwafanya watiliwe shaka hata kidogo au kutoaminika, hivyo walikuwa wakifanya mambo yao kwa tahadhari na ustadi wa hali ya juu kabisa.

Wakati huo huo washirikina wa Makka, ambao waliwalazimisha Waislamu kuhama, walikuwa wakifanya kazi kubwa ya kuchochea moto wa shari uliokuwa umewashwa na wanafiki wa Madina. Washirikina wa Makka na wanafiki walikuwa na mawazo ya aina moja. Walikuwa wakihofia kuimarika na kustawi kwa Uislamu. Hivyo walikuwa wakiwachochea wenzao wa Madina kuzinyanyua silaha zao dhidi ya Waislamu na kuwafuta kabisa katika uso wa ardhi ya Madina. Uchochezi huu ulikuwa ukitoa sauti ya kitisho; kama wanafiki wa Madina wakishindwa kuwashughulikia Waislamu, basi washirikina wa Makka walikuwa wakiwahakikishia kuwa watakuja wao wenyewe kuifanya kazi hiyo wakiwa wanaungwa mkono na makabila yote ya Peninsula ya Arabia. Lakini kama watakuja hawatabagua nani ni nani, bali watawafyeka wakazi wote wa Madina, Waislamu na wale wasiokuwa Waislamu. Ili kuwaonesha kuwa walikuwa na jukumu sawa, washirikina wa Makka walituma kundi kwenda Madina, likapora mifugo yao iliyokuwa malishoni nje kidogo ya mji.

Hali ilikuwa tete na hatari ilikuwa ikionekana wazi katika anga la Madina. Waislamu wakaanza kuilinda mitaa yao wakati wa usiku na kuchukua kila hatua ya kiulinzi dhidi ya shambulizi ambalo lingeweza kutokea. Katika kazi hiyo ya kukesha hata Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akishiriki. Vikosi vidogo vidogo vilikuwa vikitumwa nje ya mji wa Madina kwa kazi ya kuulinda mji na kutoghafilika pindi watakaposhambulia.

Kwa upande mwingine, yalikuwepo makabila ya Kiyahudi, maadui wakubwa wa Waislamu. Daima walikuwa wakisubiri muda muafaka wa kuanzisha mashambulizi dhidi ya Waislamu. Kutokana na historia yao ya kidini, walijikuta katika hali ya vuta nikuvute na Waislamu na walikuwa wakisababisha usumbufu mkubwa.Ni kwa sababu hiyo kwamba, surah ya kwanza kuteremka Madina, al-Baqara, iliweka msisitizo mkubwa katika kuwaita Wayahudi kwenye Uislamu. Baada ya kulingania na kuwaita watu wote, Surah hiyo inawataja moja kwa moja 'Wana wa Israeli' baina ya aya ya 40 na ya 162, na kuweka mkazo wa kipekee katika aya ya 123, hali inayoonesha kuwa karibu nusu ya surah nzima iliwakusudia wao. Maneno hayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu yamejiepusha kuwataja moja kwa moja Wayahudi na kuwaelezea katika dhamiri ya mtu wa tatu; maelezo hayo yanataka kuwasha upya nuru ya imani ndani ya nyoyo za Wayahudi kwa kuyakanusha madai yao na kuwakumbusha neema walizokuwa wamejaaliwa.[51]

Mshairi wa Kiyahudi, Kaab ibn Ashraf alikuwa na tabia ya kumdhihaki Mtukufu Mtume ﷺ, kuwachochea makafiri wa Makka dhidi yake, ambapo washairi wa Kiqurayshi nao walifuata mfano wake. Hassan ibn Thabit رضي الله عنه, mshairi bingwa katika Ansar, alimuomba ruhusa Mtukufu Mtume ﷺ ya kujibu mapigo. Akaruhusiwa.[52]

Hivyo basi, wakati huo ushairi ulikuwa na nguvu kama ya vyombo vya habari vya sasa. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa ameweka minbar maalumu ndani ya Msikiti kwa ajili ya Hassan ibn Thabit,

51. Tazama, Draz, *an-Nabau'l-adhîm*, p. 178.
52. Bukhari, Manâqıb, 16; Muslim, Fadhailu's-Sahaba, 156-157.

ambaye alikuwa akiyapaza mashairi yake katika kujibu dhihaka alizokuwa akitupiwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akisema, "Madamu Hassan anamtetea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Roho Mtakatifu atakuwa pamoja naye." (Abu Dawud, Adab, 87/5015)

Mtukufu Mtume ﷺ na Waislamu walipokuwa wakikabiliwa na upinzani kutoka kwa Wayahudi na washirikina, Mwenyezi Mungu Mtukufu akimtaka kufanya subira na kusamehe. Siku moja kabla ya Vita ya Badr, Mtukufu Mtume ﷺ alipanda punda wake pamoja na Usama ibn Zayd kwa lengo la kwenda kumtembelea Saad ibn Ubada aliyekuwa mgonjwa. Njiani alikutana na kundi la watu likiwa limekaa kando kando ya njia. Katika kundi hilo alikuwemo Abdullah ibn Ubayy ibn Salul, ambaye 'kwa nje' bado alikuwa hajaukubali Uislamu wake; alikuwa akitangaza waziwazi ukafiri wake. Pamoja naye walikuwpo pia baadhi ya Waislamu, akiwemo Abdullah ibn Rawaha, pamoja na Wayahudi na washirikina. Punda aliyekuwa amepandwa na Mtume ﷺ na Ibn Zayd, alipofika kwenye kundi hilo alitimua vumbi wakati akipita. Abdullah ibn Ubayy alifunga pua yake kwa ncha ya kanzu yake, kisha akang'aka:

"Usitutimulie vumbi!"

Mtukufu Mtume ﷺ aliteremka juu ya punda, akawasalimia na kuwasomea baadhi ya aya za kuwalingania kwenye imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Abdullah ibn Ubayy akang'aka tena, "Kwa nini watuambia mambo haya? Kama unayozungumza yana ukweli, basi tuache.. nenda kawambie wale wanaokuja kukusikiliza!"

Abdullah ibn Rawaha akaingilia kati: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu endelea kutembelea vikao vyetu, kwa maana tunafurahia kukusikiliza!"

Hatua hiyo ilisababisha mabishano makubwa baina ya Waislamu, washirikina na Wayahudi. Walikaribia kupigana lakini Mtukufu Mtume ﷺ aliweza kuwatuliza. Mambo yaliporudi katika hali ya kawaida, Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea na safari yake. Alipofikakwa Saad ibn Ubadah alimsimulia juu ya mgogoro huo.

Saad ibn Ubada akamfariji: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wasamehe. Ninaapa kwa yule aliyekutuma na Kitabu kwamba, kabla ya kuwasili kwako, watu hawa walikuwa wakijiandaa kumtangaza Ibn Ubayy kama kiongozi na kumvika taji kama wafanyavyo kwa wafalme. Lakini, Mwenyezi Mungu alipokuleta kwetu na Dini ya Haki, ndoto zake za kuwa mfalme zilitoweka na kumuacha katika taabu…ilikuwa kana kwamba hatapumua tena. Yumkini chuki inatokana na hilo."

Mtukufu Mtume ﷺ alimsamehe Abdullah ibn Ubayy kwa mwenendo wake. Aya ifuatayo iliteremka kuhusu tukio hilo:

لَتُبْلَوُنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ
وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا ۚ وَإِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذَٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ

"Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutokana na walio pewa Kitabu kabla yenu na wale walio shiriki. Na ikiwa mtasubiri na mkamchamngu basi hakika hayo ni katika mambo ya kuazimia." (Al Imran, 186)

Kabla ya kuteremka kwa aya inayoruhusu kupigana, Mtukufu Mtume ﷺ walikuwa wakisamehe mauddhi waliyokuwa wakitendewa na washirikina na Wayahudi, kwa maana walikuwa wameamriwa kuchukua hatua hiyo ya kusamehe.[53]

53. Bukhari, Tafsîr, 3/15.

Ruhusa ya Kupigana: "Wapigeni wale Wanaokupigeni!"

Mwanzoni, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa amepewa ruhusa ya kupambana na washirikina. Jukumu lake ilikuwa ni kuwaita na kuwalingania kwenye imani ya Mungu Mmoja, na kuvumilia na kustahmili malipizi, mateso na maudhi ambayo yangeweza kutokea. Washirikina wa Kiqurayshi wenye chuki hawakuacha hata kidogo kuwatesa na kuwaadhibu wafuasi wa Mtukufu Mtume ﷺ, kwa matarajio ya kuwarudisha kwenye imani zao za kipagani. Kutokana na kuendelea kutumia aina mbalimbali za mateso na ukatili, walifanikiwa kuwarejesha baadhi, huku wengine wakilazimika kuungama mji wao na kukimbilia Abyssinia (Ethiopia) na Madina kwa lengo la kulinda imani yao.

Mambo yaliendelea kuwa mabaya mno kiasi kwamba isingewezekana tena kutunza amani kupitia sera ya 'subira' na uvumilivu', ambayo mpaka wakati huo ilikuwa ikitekelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Hata njia ya kujilinda haikuweza kuzuia bahari za uchungu, ikamlazimu Mtukufu Mtume ﷺ kumkimbilia Mwenyezi Mungu Mtukufu na kusubiri kupata suluhisho kutoka Kwake.

Hatimaye, wakati washirikina wakiendelea kuzikana neema zote walizopewa na Mwenyezi Mungu na kumkana Mtukufu Mtume ﷺ; na wakati wakiendelea kuwapa Waislamu wasiwasi na shida hata baada ya kuhama, zikateremka aya zinazowaruhusu Waislamu kujibu mapigo, huku zikisisitiza umuhimu wa kujilinda, jambo ambalo sasa lilikuwa likihitajika mno:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَاتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ الَّذِينَ

أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ

النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَهُدِّمَتْ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ

"Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nymba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu." (al-Hajj, 39-40)

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

"Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui." (al-Baqara, 190)

Ama kuhusu sababu na malengo halali ya kupigana, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

"Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu…" (al-Anfal, 39)

Ruhusa ya kupiga ilitolewa kutokana na misimamo ya kiuadui iliyotumiwa dhidi ya Uislamu na Waislamu. Hivyo, Jihadi ilifaradhishwa ili kuyalinda na kuyatetea mambo matano ya dharura, yaani *dharuuraat'ulkhamsa*, ambayo ni tunu muhimu zinazotakiwa kulindwa kwa ajili ya uhai wa jamii. Mambo hayo ni mali, uhai na kizazi cha mwanadamu, akili na dini. Amri hii ya Mwenyezi Mungu inalenga kuwaadhibu wale wanaofanya uhalifu wa kuwazuia wengine wasifikiwe na Ukweli na kuondosha vitu vikwazo vyote vinavyouzuia kuenea kwake.

Mtume Muhammad Mustafa ﷺ, mnara wa mitume wote, aliyetumwa kama rehma kwa walimwengu wote, licha ya kuwa na huruma ya hali ya juu ambayo iliwaenea watu wote, alilazimika kuingia kutokana na hitajio la kujenga amani na uthabiti wa kijamii na kuimarisha mapambano kwa ajili ya *tawhid*. Hivyo hadith yake isemayo, "Mimi ni mtume wa rehma na vita", (Ahmad, IV, 396) inapaswa kueleweka katika muktadha huu.

Sanjari na aya iliyotoa ruhusa ya kujitetea na kupigana kuna aya nyingine zinazomhamisisha Mtume ﷺ na Waumini kutekeleza kwa vitendo ruhusa hiyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَيَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ

"Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na Waumini walio kufuata. Ewe Nabii! Wahimize Waumini wende vitani." (al-Anfal, 64-65)

أَلَا تُقَاتِلُونَ قَوْمًا نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ الرَّسُولِ وَهُمْ بَدَءُوكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۚ أَتَخْشَوْنَهُمْ ۚ فَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ قَاتِلُوهُمْ

يُعَذِّبْهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ
مُؤْمِنِينَوَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ ۗ وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

"Je, hamtapigana na watu walio vunja viapo vyao na wakawa na hamu ya kumfukuza Mtume, nao ndio walio kuanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumwogope, ikiwa nyinyi ni Waumini. Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini, na aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu humkubalia toba ya amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima." (at-Tawba, 13-15)

Sambamba na aya hizo, kuna aya nyingine zinazowaonya wale wanaoacha kushiriki katika jihadi:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا
شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا
وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

"Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." (al-Baqara, 216)

مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ أَنْ يَتَخَلَّفُوا عَنْ رَسُولِ
اللَّهِ وَلَا يَرْغَبُوا بِأَنْفُسِهِمْ عَنْ نَفْسِهِ

"Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume, wala kujipendelea nafsi zao kuliko yeye." (at-Tawba, 120)

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

"Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu." (at-Tawba, 24)

Waumini, wakiongozwa na Mtukufu Mtume ﷺ, walianza operesheni kubwa ya kupambana na washirikina ili kutekeleza amri hizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu

Jihad, kwa maana ya jumla, ni mtu kupambana katika kusafisha na kuitakasa nafsi yake, kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa moyo wote, kujiepusha na mambo ya haramu,[54] kuwaamrisha Waislamu wenzake kutenda mema na kuwaombea kheri, kuitangaza misingi ya Uislamu kwa wasiokuwa Waislamu

54. Nasai, Hajj, 4.

na kuwaonesha njia ya uongofu[55] na kutumia nyenzo zote, iwe uhai, mali au mazungumzo, katika kuilinda dini na mambo yake matukufu na pia kuondosha vizuizi na vikwazo vinavyozuia Ukweli kuonea, kwa kutumia juhudi nzito, bila shaka ikiwa ni pamoja na vita, ingawa hiyo sio njia pekee.[56]

Hivyo, neno *jihad*, ni neno pana linalohusisha na kujumuisha juhudi, mapambano, na hatua binafsi na za pamoja kwa lengo la kuitakasa 'nafsi', na kujenga mfumo wa maisha ya Kiislamu, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, na kwa ajili ya kuinua dini Yake. Hatutakuwa tumekosea tukisema kuwa miaka ishirini na tatu ya utume ililenga kufanikisha lengo hili.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameufanya uhai na mali kuwa sababu ya mitihani, akatahadhirisha katika maeneo mbalimbali kuwa vitumike kama nyenzo ya kupigania njia Yake, kamainavyoelezwa katika aya ifuatayo:

لَٰكِنِ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ جَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ ۚ
وَأُولَٰئِكَ لَهُمُ الْخَيْرَاتُ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

"Lakini Mtume na wale walio amini pamoja naye waliwania Jihadi kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio watakao pata kheri nyingi, na hao ndio wenye kufanikiwa." (at-Tawba, 88)

55. Ahmad, III, 456.

56. Kwa upande wa aya za Qur'an, tazama an-Nisa, 95; al-Anfal, 72; at-Tawba, 20, 41, 44, 81, 88; na kuhusu hadith tazama, Bukhari, Mazalim, 33; Muslim, Iman, 226; Abu Dawud, Sunnah, 28-29.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ تِجَارَةٍ تُنْجِيكُمْ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

"Enyi mlio amini! Nikuonyesheni biashara itakayo kuokoeni na adhabu iliyo chungu? Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganeni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnajua." (as-Saff, 10-11)

Siku moja Maswahaba walimuuliza Mtukufu Mtume ﷺ awaambie mtu bora. Akasema:

"Muumini anayeutumia uhai na mali yake kwa ajili ya *jihad* katika njia ya Mwenyezi Mungu." (Bukhari, Jihad, Muslim, Imarat, 122)

Kushiriki *jihadi* katikanjia ya Mwenyezi Mungu, kama ilivyo-amrishwa na Qur'an na Sunnah, haihusu medani ya vita pekee; kushika silaha ni hatua ya mwisho kabisa, ambayo huchukuliwa pindi inapotokea dharura ya haraka ya kukomesha dhulma na kusi-mamisha haki na uadilifu. *Jihad* halisi ni ile inayolenga kuziteka nyoyo za watu, ambayo huweza kufanyika kupitia njia mbalimbali, ya kwanza na ya muhimu zaidi ikiwa ni kuutangaza ukweli kwa maneno au kwa maandishi.

Waislamu hawakutumia nguvu ya vita katika kipindi cha Makka, licha ya kuwepo kwa aya kadhaa kuhusu *jihad*. Ili kuendana na amri ya Mwenyezi Mungu katika kukabiliana na vitisho vya watu zam aza ujahiliya, Waislamu walikuwa wakionesha mwenendo wa Muislamu wa kweli pamoja na kuonesha mafundisho ya Uislamu

kama vile ukweli, haki na uadilifu. Hatua yao hiyo imesifiwa na Qur'an kama 'jihadi kubwa'.

فَلَا تُطِعِ الْكَافِرِينَ وَجَاهِدْهُمْ بِهِ جِهَادًا كَبِيرًا

"Basi usiwat›ii makafiri. Na pambana nao kwayo kwa Jihadi kubwa." (al-Furqan, 52)

Maneno جِهَادًا كَبِيرًا, 'jihadi kubwa', katika aya iliyotajwa hapo juu, inamaanisha kufikisha neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kauli, tabia na kutumia nyenzo zote kuinyanyua Haki kwa ajili ya kuwaleta pamoja wanadamu kwenye amani ya uongofu na furaha. Bila shaka kufanya jihadi kwa *tabligh*, yaani kueneza neno la Haki, ni jambo kubwa na lenye athari zaidi kuliko kutumia silaha. Katika kipindi cha miaka ya mwanzo, Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe alifanya *jihad* kwa kutumia Qur'an.

Ikiwa na lengo la kuwaongoza wanadamu, Qur'an Tukufu inahamasisha njia mbalimbali za kufanya "*jihad* katika njia ya Mwenyezi Mungu". Njia moja tu, katika hizo njia nyingi, ndiyo inayohusisha *qital*, au medani ya vita. Njia hiyo hutumika tu pale mazingira yanapolazimisha kufanya hivyo.

Vita nyingi ambazo Mtukufu Mtume ﷺ alishiriki zilikuwa vita zakujilinda, kama vila Vita ya badr, Uhud na Khandaq. Harakati nyingine kama vita vya Mu'tah na Tabuk zilifanywa kama tahadhari ya kuzuia mashambulizi yanayoweza kufanywa. Kwa upande mwingine, ufunguzi wa Makka ulitokea tu baada ya washirikina wa Makka kwenda kinyume na mkataba wa amani, na lengo likiwa ni kurejesha haki za Waislamu zilizokiukwa. Hivyo, maana pana ya rehma na haki vilitawala vita zilizofanywa na Mtume ﷺ na kwa hakika zilielezea rehma ya kweli. Katika Uislamu, vita haifanyiki

kwa lengo la kukatisha uhai wa watu,[57] kutwaa ngawira, kufanya uharibifu Ardhini, kujipatika faida na manufaa binafsi au kutoa nafasi ya hisia za kulipiza kisasi; bali hufanyika kwa lengo la kuondosha ukandamizaji, kujenga uhuru wa kuamini, kuwapeleka wanadamu kwenye uongofu na kukomesha aina zote za dhulma.

Tathmini ya vita zote ambazo Mtume ﷺ alishiriki, inaonesha kuwa vita halali hupiganwa tu kwa lengo la kujilinda na *ila'yi kalimatullah*, yaani kuliinua neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vita inayopiganwa kwa lengo kupanua himaya ni fedheha kwa

57. Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye alitumwa kama rehma kwa walimwengu wote, alifuata sera ya huruma katika harakati zake zote 120 za kijeshi – 29 zikiwa vita kubwa (ghazwa) na 91 zikiwa vita ndogo (sariyya)- kiasi kwamba licha ya kuiweka Arabia yote chini ya udhibiti wake, hakuruhusu jeshi lolote la Kiislamu kumwaga tone la damu zaidi ya ilivyohitajika. Kwa mujibu wa ripoti sahihi, idadi ya Waislamu waliouawa katika vita zote 120 zilizopiganwa katika kipindi cha miaka 11, ni 340, na upande wa maadui waliokufa katika vita zote ni 800. Hii ina maana kuwa idadi ya vifo katika vita zote 120 ilikuwa chini ya 1200. Kwa mfano katika vita 29 zilizoongozwa na Mtume ﷺ mwenyewe, 16 hazikuwa na makabiliano ya silaha. 13 zilizobaki zilikuwa na makabiliano ya silaha, ambapo Waislamu 140 na maadui 335 ndio waliouawa.
Kwa kutumia njia muhimu ya kidiplomasia, Mtukufu Mtume ﷺ aliweza kupata kiapo cha utii kutoka kwenye maeneo mbalimbali bila kuhitaji kuingia vitani. Maeneo mengine yalimkubali na kumfuata baada ya kufikishiwa maneno ya uongofu wakayapokea. Kwa kutambua kuwa njia hii ni bora kuliko mapambano, Mtukufu Mtume ﷺ alijiepusha kutumia upanga isipokuwa pale ilipobidi. Katika matukio mengine, kwa kutumia diplomasia pamoja na upelelezi aliweza kuwazuia maadui kuingia vitani, na hivyo kuzia umwagikaji wa damu. Akitaka kupata ushindi katika vita fulani, alikuwa akimteua kamanda ambaye alizaliwa katika eneo husika, au mwenye asili ya kabila pinzani. Daima Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiliusia jeshi kukumbuka maelekezo yake, wasiue watu bila sababu, wasiwakamate watumwa, watoto, wanawake, wazee na watawa walio katika nyumba za ibada, wasiikate miti na kubomoa majengo. (Tazama, Elşad Mahmudov, Sebep ve Sonuçları *İtibâriyle Hazret-i Peygamber'in Savaşları*, 2005, Chuo kikuu cha Marmara, Taasisi ya Sayansi za jamii, tasnifu ya uzamili.)

binadamu. Hivyo, katika Uislamu, vita inatakiwa kupiganwa kwa malengo makuu ya kueneza haki, uadilifu, kutengeneza njia ya watu kufikiwa na uongofu na kuondosha dhulma. Qur'an Tukufu inasema:

مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا

"…aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote." (al-Maida, 32)

Jihadi zote zilizofanywa na Waislamu, iwe kwa nafsi au mali zao, zilifanywa chini ya miongozo hiyo ya Kiislamu, na hivyo kufanywa kwa alengo la kupata neema na Pepo ya Mwenyezi Mungu. Lakini, ikhlasi na nia njema katika jihadi ni muhimu sana kama ilivyo katika mambo mengine. Siku moja Abdullah ibn Amr alimtaka Mtukufu Mtume ﷺ amfahamishe kuhusu *jihad* na medani ya vita.

Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia, "Ewe Abdullah, kama utapigana ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu, Siku ya Kiyama utafufuliwa kama ulivyo. Lakini kama utapambana kwa ajili ya ufakhari na kujionesha, utafufuliwa kama ulivyo." (Abu Dawud, Jihad, 24/2519)

Siku nyingine, Bedui mmoja alitaka maoni ya Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu "mtu anayepigana kwa ajili ya ufakhari na sifa binafsi, ili apate ngawira au kutaka kujionesha." Hapo hapo mtu mwingine akaingilia kati, akitaka Mtume ﷺ amwambie "makusudio na maana ya kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa maana kuna watu wanaopigana ili kuzima hasira zao au kwa lengo la kuonesha ushujaa na ujasiri wao."

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu, "Mwenye kupigana kwa ajili ya kuitukuza na kuiinua dini ya Mwenyezi Mungu, basi atakuwa amepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu." (Bukhari, Ilm, 45; Muslim, Imara, 149-150)

Kisha mtu mwingine akaanza kuuliza, "Unasemaje kuhusu mtu anayetaka kupigana katika njia ya Mweneyzi Mungu na wakati huo huo apate kitu fulani cha kidunia?"

"Hana thawabu", alijibu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Jibu hilo lilionekana kuwa kali kwa Maswahaba, kutokana na ugumu wa kuwa na ikhlasi ya kiwango cha juu kama hicho. Hivyo wakamtaka swahaba aliyekuwa ameuliza, kwamba "Uliza swali lako tena…huwenda hukulielewa jibu vizuri". Walikuwa wakitarajia kupata jibu litakalowapa faraja na wepesi. Lakini waliambulia patupu, kwa maana hata baada ya kuuliza mara tatu, jibu la Mtukufu Mtume ﷺ halikubadilika. (Abu Dawud, Jihad, 24/2516)

Mtukufu Mtume ﷺ mara nyingi alisikika akielezea ubora wa *jihad* katika *ahadith* zake nyingi. Miongoni mwake ni hizi zifuatazo:

"Kusimama mchana na usiku mmoja kulinda mpakani ni bora kuliko mwezi ambao siku zake zimetumika kwa funga na mikesha iliyojaa ibada. Mwenye kufariki akiwa analinda, ataendelea kupokea thawabu mpaka Siku ya Mwisho; atapata baraka na neema za mashahidi na hataulizwa maswali na malaika wenye kuuliza maswali kaburini." (Muslim, Imara, 163)

"Kusimama ukilinda mpaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa siku moja tu ni bora kuliko dunia yote na vilivyomo. Makazi yako Peponi ni bora kuliko dunia na vilivyomo. Jioni au asubuhi moja unayoitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu ni bora kuliko dunia na vilivyomo." (Bukhari, Jihad, 6, 73; Riqaq, 2; Muslim, Imara, 113-114)

"Mwenyezi Mungu Mtukufu husema kuhusu mtu aliyetoka kwa ajili ya kwenda kupigana jihadi katika njia Yake, 'ametoka kwa ajili Yangu tu, moyoni mwake amewaamini na kuwasadikisha manabii wangu', na kuwa mdhamini wake…humhakikishia Pepo kama akiuawa kishahidi, au thawabu na ngawira akibaki hai. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, ambaye nafsi ya Muhammad iko mikononi Mwake, jeraha lililofunguliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, siku ya Kiyama litakuwa katika hali yake ya ubichi na damu lakini litakuwa likinukia harufu nzuri kama ya miski." (Muslim, Imara, 103; Nasai, Iman, 24)

"Kila atakayeingia peponi hatatamani kurudi duniani, kwa maana pepo ina kila kitu ambacho dunia inacho na zaidi. Isipokuwa mtu aliyekufa shahidi, ambaye kwa sababu ya atakayoyapata, atatamani arudi ardhini mara kumi na kutamani kuuawa kishahidi kila mara." (Bukhari, Jihad, 21; Muslim, Imara, 108-109)

Katika hadith ifuatayo, Mtukufu Mtume ﷺ analieleza lengo kuu la mapambano na jihadi alizoshiriki:

"Nimeamrishwa kupambana na watu mpaka washuhudie kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume Wake, wasimamishe swala na kutoa zaka. Wakiyafanya haya, maisha na mali zao vitasalimika, isipokuwa kwa adhabu zilizowekwa na Uislamu." (Bukhari, Iman, 17)

Ni kwa sababu hiyo kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.aw), alikuwa hafanyi mashambulizi wakati wa usiku, bali alikuwa akisubiri mpaka alfajiri ili aone kama atapata kusikia adhana kutoka katika mji husika anaotaka kuushambulia.[58] Anapotuma kikosi cha jeshi alikuwa akikiamuru kuwa, "…msishambulie sehemu mtakay-

58. Bukhari, Adhan, 6; Muslim, Salat, 9.

oona msikiti au kusikia adhana." (Abu Dawud, Jihad, 91/2635; Ahmad, III, 448-449)

Muslimibn Harith ﷺ anasimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituma kikosi, ambacho mimi pia nilikuwemo, kwenda sehemu moja. Tulipofika mahali tulipotakiwa kushambulia, niliongeza mwendo wa farasi wangu na kuwapita wenzangu. Mara nikakutana wanawake na watoto fulani wakilia.

'Je, mngependa kuyaokoa maisha yenu?' niliwauliza. 'Ndiyo', walijibu bila kusita.

'Basi semeni *La ilaha ill'Allah Muhammadun Rasulullah* mtayaokoa maisha yenu', niliwaambia, nao wakafanya hivyo. Lakini wenzangu walianza kunikosoa kwa hoja kwamba nilikuwa nimewafanya wasipate ngawira. Tuliporejea kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, walimtaarifu juu ya kilichotokea. Mtukufu Mtume ﷺ aliniita na kuniambia huku akiwa amefurahi:

"Mwenyezi Mungu amekupa thawabu tele kwa kila mmoja wao (uliyefanikiwa kumuokoa)." (Abu Dawud, Adab, 100-101/5080)

Burayda ﷺ anasema;

"Kabla ya kutuma kikosi chochote kwenda kwenye *jihad*, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimuusia kamanda wa kikosi kujipamba na uchamungu, kuwatendea wema Waislamu wenzake na kuamiliana nao kwa uzuri. Kisha huwaambia:

'Piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa jina Lake dhidi ya wale wanaomkana. Msihadaiwe na ngawira. Msifanye ukatili. Msikate pua au masikio ya watu. Msiwaue watoto. Mkikutana na maadui zenu makafiri, waiteni kwenye mojawapo ya mambo matatu: waiteni kwenye Uislamu, wakikubali waacheni waende.

Wakikataa waambieni watoe kodi ya *jizya*, na waacheni waondoke iwapo watalikubali. Wakilikataa hilo pia, basimtegemeeni Mwenyezi Mungu na pambaneni nao." (Muslim, Jihad, 3; Tirmidhi, Siyar, 48/1617; Ahmad, V, 353, 358)

Baadhi ya Harakati ndogo ndogo za Kijeshi

Sasa Mtukufu Mtume ﷺ alitaka kuikata njia muhimu na inayotumika sana kupitishia biashara za makafiri wa Makka kwenda Syria[59], na hivyo kuwatupa makafiri katika mgogoro kibiashara na kiuchumi pasipo kuatarajia, na kuwazuia wasipate nguvu zaidi dhidi ya Waislamu.[60] Mpaka wakatihuo, makafiri walikuwa wakifanya hujuma mbalimbali dhidi ya Waislamu wa Madina, wakiwazuia kuingia katika miji yao na wakiwachochea wanafiki wa Madina wawaue. Hivyo, miezi saba baada ya Hijra, Mtukufu Mtume ﷺ

59. Hatua ya kwanza aliyoichukua Mtukufu Mtume ﷺ katika kukabiliana na uadui kutoka Makka, alianzisha vikwazo vya kiuchumi na kisiasa, kutengeneza uhusiano wa kidplomasia na makabila ya jirani na kuratibu harakati za kijeshi kuifuatilia misafara ya kibiashara ya Maqurayshi, ambayo ilikuwa moyo wa biashara na uchumi wa makafiri wa Makka. Kuhusu hatua hii, Muhammad Hamidullah anasema, "Mashambulizi yaliyofanywa dhidi ya misafara ya Maqurayshi haipaswi kuchukuliwa kuwa ni uporaji; kwa maana Maqurayshi hawakuwa wasafi, na pia washambuliaji halikuwa kundi lililoanzishwa kwa lengo la kuuvamia msafara wowote. Bali kuna hali ya vita iliyokuwa imeibuka baina ya miji hiyo miwili. Hali na mazingira ya vita hulazimisha kutoa onyo sahihi linaloweza kusababisha hasara ya uhai, mali na maslahi ya upande wa pili. Hivyo kanuni ya vita ilikuwa imetumika kati ya pande hizi mbili. Na kwa hiyo, harakati hizo za kijeshi hazikuwa harakati za uvamizi na uporaji wa misafara." Nukta nyingine inayohitaji kuzingatiwa hapa ni kwamba katika harakati zao zote za kijeshi, Waislamu walikuwa wakiilenga misafara ya Maqurayshi tu. Makabila mengine ya peninsula hiyo yalibaki kuwa salama licha ya kuwa hayakuwa makabila ya Waislamu. (Tazama, *Hamidullah, İslâm Peygamberi*, I, 219; *Hz. Peygamberin Savaşları*, uk.56)

60. Bukhari, Maghazî, 2; Abu Dawud, Kharaj, 22-23/3004.

aliwatuma askari thelathini katika *Muhajirun*, chini ya uongozi wa Hamza ﷺ, kwenda Sif 'ul-Bahr kwa lengo hilo la kuwatia hasara ya kiuchumi makafiri.[61] (Rajab 8/Novemba-Desemba, 623)

Sasa msafara huo wa kibiashara, ambao ulikuwa ukirejea kutoka Damascus kwenda Makka, uliwasili Sif'ul-Bahr, ukiwa chini ya ulinzi wa wapanda farasi mia tatu, akiwemo Abu Jahl. Wakati pande zote zikiwa zimepanga safu tayari kwa ajili ya mapambano ambayo yalionekana kutoepukika, Majdi ibn Amr, ambaye alikuwa mshirika wa pande zote mbili, aliingilia kati na kuwazuia wasipigane. Mtukufu Mtume ﷺ aliposikia habari hiyo, alifurahia hatua ya Majdi kuingilia kati na kuusifu umahiri wake wa kuendesha masikilizano. Katika kutambua hatua yake hiyo alimtumia Majdi zawadi nyingi.[62]

Miezi nane baada ya Hijra, mwanzoni mwa mwezi wa Shawwal, kwa mara nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ alituma kikosi cha Muhajiruun sitini mpaka themanini kwenda Rabigh[63], chini ya uongozi wa Ubayda ibn Harith.

Maqurayshi walikuwa mia mbili, wakiongozwa na Abu Sufyan. Mbali na mvutano na kutupiana mishale kadhaa, pande zote mbili hazikuweka safu wala kuchomoa panga zao kwa ajili ya mapambano. Mtu wa kwanza kutupa mshale alikuwa Saad ibn Abi Waqqas ﷺ. Hivyo, yeye ndiye mtu wa kwanza kabisa kutupa mshale katika Uislamu. Kwa kuhofia kuwa Waislamu wanaweza kuongezewa nguvu kutoka Madina, makafiri walikimbia na hivyo pande zote mbili zikatawanyika.

---

61. Sif 'ul-Bahr, ni eneo katika mkoa wa Iys. Bani Juhayna walikuwa wakiishi mahali hapa. Imeitwa hivyo kwa sababu liko kando kando mwa bahari. (Neno *bahr*lina maana ya bahari)
62. Waqidi, I, 9-10; Ibn Saad, II, 6.
63. Rabigh ni bonde ambalo mahujaji hupitia wakati wa kwenda Makka. Bonde hili lipo kati ya Anwa na Juhfa, takriban umbali wa maili 3 kutoka Juhfa.

Japokuwa Miqdad ibn Amr na Utbah ibn Ghazwan walikuwa wameingia katika Uislamu muda mfupi, mpaka wakati huo hawakuwa wamepata upenyo na uwezo wa kuungana na Mtukufu Mtume ﷺ mjini Madina. Hivyo walikuwa wameungana wamejiunga katika msafara huo wa Maqurayshi ili wapate njia ya kukimbilia upande wa Waislamu na kutimiza azma yao. Mara tu walipowaona askari Kiislamu waliokuwa wamepanda farasi, waliwachomoka washirikina na kukimbilia upande wa Waislamu.[64] Miezi tisa baada ya Hijra, katika mwezi wa Dhilqa'dah, Mtukufu Mtume ﷺ alituma kikosi cha watu nane, (au ishirini kwa mujibu wa vyanzo vingine), kwenda Harrar[65] chini ya uongozi wa Saad ibn Abi Waqqas ؓ. (Dhil'qadah 1/ May, 623)

Saad ؓ mwenyewe anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliniamuru, '…nenda mpaka ufike Harrar, kwa maana msafara wa Maqurayshi utapita hapo.' Hivyo tilikuwa tukisafiri usiku na kupumzika mchana. Tulifika Harrar wakati wa asubuhi, baada ya siku tano. Lakini msafara ulikuwa umepita hapo siku moja kabla. Kama isingekuwa amri ya Mtume kwamba nisiende zaidi ya Harrar, yumkini ningewafikia."

Maswahaba hao walirejea Madina bila kukabiliana na makafiri.[66]

Mwanzoni mwa mwezi wa kumi na moja wa Hijra, katika mwezi wa Safar, Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe aliongoza Safari ya

64. Ibn Hisham, II, 224-225; Waqidi, I, 10; Ibn Saad, II, 7.

65. Harrar ni jina la chemchem huko Hijaz, jirani na Juhfah. Chemchem hiyo iko katika njia itokayo Juhfah kwenda Makka, iko upande wa kushoto wa Mahajja jirani na Ghadir'ul-Khum.

66. Ibn Hisham, II, 238; Waqidi, I, 10; Ibn Saad, II, 7.

Kijeshi ya Abwa (Waddan)[67] (Safar 2/Agosti, 623). Hii ndiyo safari ya kwanza ya kivita ambayo Mtume ﷺ alishiriki. Saad ibn Ubadah ؓ, kutoka jamii ya Ansar, alibaki Madina kama msimamizi wa mambo.

Safari hii haikushuhudia makabiliano yoyote na washirikina wa Makka, ingawa yalifanyika makubaliano ya amani na Ukoo wa Damra wa kabila la Kinanah. Pande mbili zilikubaliana kutoshambuliana, na kabila hilohalikutakiwa kujihusisha na hujuma yoyote dhidi ya Waislamu wala kuwasaidia maadui wa Waislamu. Mtume ﷺ alihakikisha makubaliano hayo yanawekwa katika maandishi na kutamatisha siku kumi na tano za safari hiyo ya Abwa.[68] Huu ni mfano mmoja tu katika mifano mingi inayotoa ushuhuda wa tamaa ya amani aliyokuwa nayo Mtukufu Mtume ﷺ na huruma yake kwa watu wengine.

67. Abwa ni kijiji kilichopo baina ya Furu na Juhfah, karibu maili 23 kutoka Madina. Mahali hapa ndipo alipozikwa bibi Amina, mama wa Mtume ﷺ.
Waddan iko baina ya Makka na Madina, maili 8 kutoka Abwa, na ni sehemu ya ardhi iliyo karibu na Juhfah iliyokuwa ikimilikiwa na makabila ya Damra, Ghifar na Kinanah.

68. Ibn Hisham, II, 223-224; Waqidi, I, 12; Ibn Saad, II, 8.


Bahari
ya Mediterania
Quds
Bahari ya Chumvi
Muta
Ayla
Sina
Dumat'ul-Jandal
Uzra
Kalb ibn Wabra
Tay
Tabuk
Teymâ
Fedek
Dhat'u Thalath 'il Wadi 'il-Qura
Tamim
Qatan
Habat
MADINA
Misri
Idam
Yanbu'
Waddan
Kisima cha Maunah
Qarad
Zab'ul-Irq
Rabigh
Usfan
Batn-u Nakhlah
Makkah
Raji
Taif
Adal – Qara
Hawazin
Bahari Nyekundu
Najran
Hamdan
Sana
Yemen

MWAKA WA PILI WA HIJRA

Batn'u Nakhlah na Harakati nyingine za Kijeshi

Miezi kumi na tatu baada ya Hijra, katika mwezi wa Rabiul-Awwal, Safari ya Kijeshi ya Buwat[69] ilifanyika kwa lengo la kufuatilia msafara wa ngamia 2500 wa Maqurayshi uliokuwa ukisafiri chini ya ulinzi wa askari farasi 100 (2 Rabiulawwal / Septemba, 623). Mtukufu Mtume ﷺ alitoka na jeshi la Waislamu 200 na kumuacha Saad ibn Muadh ؓ, kutoka jamii ya Ansaar, kama naibu wake mjini Madina. Hata hivyo, walirudi bila kuingia katika makabiliano yoyote.[70]

Harakati ya kijeshi ya Safawan[71], inayojulikana pia kama *Badr'ul-Ula*, au Badr ndogo, ilitokea kipindi hicho hicho kwa lengola kumkamata Qurz ibn Jabir. Alikuwa amepora na kukimbia na ngamia na ng'ombe wa eneo hilo walikuwa katika malisho jirani na Mlima Jamma, katika mji mdogo wa Aqiq, karibu maili tatu kutoka Madina. (Rabiulawwal, 2 / Septemba 623). Zayd ibn Haritha ؓ ndiye aliyebaki Madina kama naibu kwa muda mfupi. Licha Mtukufu Mtume ﷺ kufika Safawan, lakini alilazima kurudi Madina, kwa sababu Qurz alikuwa ameshakimbia muda mrefu.

---

69. Buwat ni miongoni mwa milima kadhaa inayopatikana katika eneo ambalo zamani lilikuwa makazi ya Juwaynah. Liko umbali wa maili 36 kutoka Madina.
70. Waqidî, I, 12; Ibn Saad, II, 8-9.
71. Safawan ni bonde lililopo katika viunga vya Badr.

Baadaye Qurz alikuja kuwa Muislamu wa dhati.[72]

Mwezi wa Jamadal-Akhir ulishuhudia harakati ya kijeshi ya Dhul-Ushayra (Jamadilakhir, 2 / Novemba 623) iliyopelekea kusainiwa kwa mkataba wa amani na Bani Mudlij na waitifaki wao.[73]

Kipindi hicho hicho, kikosi kidogo chini ya uongozi wa binamu wa Mtume ﷺ, Abdullah ibn Jahsh ؓ kilichotumwa kwa ajili ya uchunguzi, kilikabiliana na msafara wa Washirikina wa Makka jirani na eneo la Batn'u Nakhlah. Tukio hilo lilitosha kuongeza hisia za washirikina wa Makka, ambao walikuwa wakitafuta sababu na fursa muafaka wa kuivamia Madina.

Tukio hilo likiwa limeshaongeza chuki dhidi ya Uislamu mjini Makka, washirikina hao walizidi kusisitiza kuwa shambulizi hilo dhidi ya msafara wao limefanyika katika mwezi wa Rajab, msimu usioruhusiwa kupigana ndani yake (*haram*). Waling'aka, "Muhammad amekwenda kinyume na kuvunja utukufu wa miezi ya amani… amemwaga damu, amechukua mateka na kuzitwaa mali zetu!"

Kwa kweli, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa ametoa agizo la kuushambulia msafara hu ona alimlaumu Abdullah ؓ kwa kusema:

"Sikukuagizeni kupigana katika miezi mtukufu!"

Mtukufu Mtume ﷺ alikwenda mbali zaidi, akajizuia kuchukua chochote katika ngawira hizo, jambo lililowafanya Maswahaba kuwa katika hali ya utungu na majuto, wakihofu kuwa muda wowote wangefikwa na adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.[74] Lakini makafiri wa Makka katika kulitumia tukio hilo kama propaganda dhidi ya Uislamu walionesha aya ifuatayo:

72. Ibn Hisham, II, 238; Ibn Saad, II, 9; Ibn Athîr, *Usdu'l-Ghaba,* IV, 468.
73. Ibn Saad, II, 9-10.
74. Ibn Hisham, II, 241.

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ۖ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ۖ وَصَدٌّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ بِهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ ۗ وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَنْ دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا

"Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasende katika Njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye, na kuzuilia watu wasende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuwa. Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika Dini yenu kama wakiweza." (al-Baqara, 217)

Abdullah ibn Jahsh na wenzake ndio waliofaraijika zaidi, wakauliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, je tutapata thawabu kama wale waliopigana katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Hapo ikateremka aya ifuatayo:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

"Hakika wale walio amini na wale walio hama na wakapigania Njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanao taraji rehema za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu." (al-Baqara, 218)

Aya hizo zilizokuwa zikiimarisha azma na kuwatinga nguvu Waislamu, wakati huo huo zilikuwa zikiwaghadhibisha makafiri na kuzidisha hamu yao ya kulipiza kisasi, japokuwa hawakuwa na haja sana na Ufunuo huo, kwa maana tayari walikuwa wameshajawa na chuki dhidi ya Waislamu, ambao walikuwa wakiongezeka kila sik una kuzidi kuipa nguvu Dola chipukizi ya Kiislamu. Kwa mujibu wa sensa iliyokuwa imefanywa na Mtukufu Mtume ﷺ, idadi ya Waislamu wanaume iliripotiwa kufikia 1500.[75] Kwa kuzingatia kuwa idadi hiyo ingeendelea kuongezeka, ilitosha kuwapa homa makafiri wa Makka. Zaidi ya hapo, Madina ilikuwa imekaa kwenye njia inayotumika kupitisha biashara za watu wa Makka, biashara ambazo ndio roho ya uhai na maisha yao. Kwa vyovyote vile, washirikina walihitaji kuiondosha hatari kabla haijawa kubwa. Hivyo waliazimia na kuamua kuishambulia Madina.

Hakam ibn Kaysan alikuwa miongoni mwa mateka waliochukuliwa katika shambulizi la Batn'u Nakhlah. Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alimlingania sana kwenye Uislamu, akamfafanulia mara nyingi na kwa ndani njia ya haki, ili kuondoa shaka inayoweza kuibuka akilini mwake. Licha ya juhudi kubwa iliyofanywa na Mtukufu Mtume ﷺ kumlingania, hakukubali. Omar ؓ aliudhika kwa ung'ang'anifu wa Hakam kuendelea kukana ukweli licha ya juhudi iliyokuwa imefanywa na Mtume ﷺ. Alishindwa kuvumilia, akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa nini unasumbuka naye? Wallah, hatasilimu huyu. Niruhusu niikate shingo yake, ili apate kwenda Motoni!" Lakini Mtukufu Mtume ﷺ alikataa na

75. Bukhari, Jihad, 181.

badala yake akaendelea kumfafanulia Hakam kuhusu Uislamu. Mara hii Hakam akasikiliza.

"Umesema Uislamu ni nini?" aliuliza.

"Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu, pasipo kumshirikisha na yeyote, na kushuhudia kuwa Muhammad ni mja na ni Mjumbe Wake."

Ghafla Hakam akasema, "Kama ni hivyo nimekubali kuwa Muislamu."

Mtukufu Mtume ﷺ akawageukia Maswahaba na kusema, "Lau kama ningewasikiliza, Hakam angekuwa Motoni!"

Miaka mingi baadaye, Omar رضي الله عنه alisema kuhusu tukio hilo:

"Nilipomuona Hakam amesilimu ilinifanya nihisi kana kwamba nilikuwa nimeangukiwa na mizigo yote ya zamani na ijayo. Nilijiuliza, 'Nilifikiria nini kumpendekezea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu jambo ambalo alikuwa akilijau zaidi?' Kisha nilijiliwaza na kujifariji, nikisema kuwa nia yangu ilikuwa kupata radhi za Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hakamu aliingia katika Uislamu na kuwa Muislamu mzuri sana. Alipigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu na aliuawa kishahidi katika tukio la Kisima cha Mauna." (Ibn Sad, IV, 137-138; Waqidi, I, 15-16)

Katika tukio hilo tunajifunza kuwa kuna haja ya kuutangaza Uislamu kwa namna ya subira na upole, huku tukiupamba kwa hekma na mawaidha mazuri.

Kubadilisha Uelekeo wa *Qibla*

Mwanzoni Waislamu waliendelea kuswali wakielekea upande wa *Masjid'ul-Aqsa*, Jerusalem, hatua iliyoendelea kwa kipindi cha miezi kumi nas ita au kumi na saba ya Hijra. Wayahudi walikuwa

wakitumia kitendo hicho kama sababu ya kudai kuwa wao ni bora kuliko Waislamu, jambo lililosababisha huzuni kubwa kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Mara zote aliuweka moyo wake kwenye Kaabah iwe *qibla*, ambayo ingekuwa hatua ya kwanza ya kuivuta Makka kwenye Uislamu. Alikuwa na shauku kubwa ya kuteremshiwa Ufunuo kuhusu suala hilo. Na kwa kuwa ruhusu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ilikuwa haijafika, fikra ya Mtukufu Mtume ﷺ ilibaki kuwa raghba tu, huku akiendelea kufanya subira kwa kutarajia kuwa raghba yake itatimizwa. Hatimaye, Siku ya Jumatatu katikati ya mwezi wa Rajab, wakati akiswali swala ya Adhuhuri katika msikiti mdogo kwenye makao ya Bani Salima, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimletea habari njema:

قَدْ نَرَىٰ تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ۖ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا ۚ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۚ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۗ وَإِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ

"Kwa yakini tukiona unavyo geuza geuza uso wako mbinguni. Basi tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu; na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo; na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale wanayo yatenda." (al-Baqara, 144)

Wakati huo akiwa kwenye hatua za mwisho za rakaa ya pili, hapo hapo Mtukufu Mtume ﷺ akageuka kuelekea upande wa kaabah, na Maswahaba nao pia wakafuata. Wote, kwa pamoja wakaan-

za kuelekea *qibla* mpya na rakaa mbili zilizobaki walizikamilisha wakiwa wameelekea al-Kaabah. Hivyo tokea wakati hapo, msikiti huo ukaitwa *Masjid'ul-Qiblatayn*, yaani msikiti wa *qibla* mbili.[76]

Swahaba mmoja ambaye aliswali nyuma ya Mtume ﷺ alikwenda kwenye msikiti mwingine, akawaona watu wakiswali pamoja. Walikuwa wameelekea kwenye rukuu, akawaambia:

"Wallah, tumemaliza kuswali pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tukiwa tumeelekea upande wa Kaabah!" Hapo hapo kundi hilo likageuka kuelekea upande wa Kaabah.

Wakati Waislamu wakiyakaribisha kwa furaha mabadiliko hayo, kwa upande wa washirikina, Wayahudi na wanafiki, yalisababisha kuzusha uvumi na kujifurahisha kwa madai ya uongo. Uzushi na uvumi wao huo ulijibiwa na aya ifuatayo:

سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ مَا وَلَّاهُمْ عَنْ قِبْلَتِهِمُ الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا ۚ قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ۚ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

"WAPUMBAVU miongoni mwa watu watasema: Nini kilicho wageuza kutoka kibla chao walicho kuwa wakikielekea? Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye humwongoa amtakaye kwenye njia iliyo nyooka." (al-Baqara, 142)[77]

İbn Abbas ﵁ anasimulia:

"Qibla ilipobadilishwa kuelekea upande wa Kaaba katika kutekeleza amri ya Qur'an, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikutana na swali kutoka kwa Waislamu:

76. Ibn Saad, I, 241-242.
77. Bukhari, Iman 30, Salat 31; Muslim, Masajid 11.

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, vipi kuhusu ndugu zetu waliswali kwa kuelekea upande wa *Masjidul-Aqsa* nas asa wameshafariki dunia?'

Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ifuatayo:

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا ۗ وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يَتَّبِعُ الرَّسُولَ مِمَّنْ يَنْقَلِبُ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ ۚ وَإِنْ كَانَتْ لَكَبِيرَةً إِلَّا عَلَى الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ

'Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kibla ulicho kuwa nacho ila tupate kumjua yule anaye mfuata Mtume na yule anaye geuka akarejea nyuma. Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu isipo kuwa kwa wale alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza Imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye kuwarehemu.' (al-Baqara, 143)[78]

Kwa hakika, mabadiliko ya qibla ni tukio kubwa. Utenguaji qibla ya awali, ni jambo lililosababisha kuibuka kwa uvumi na uzushi ambao ungeweza kuwapotosha watu kutoka kwenye ukweli. Ndiyo maana amri za Mwenyezi Mungu kuhusu qibla mpya zimekuwa zikirudiwarudiwa mara nyingi, zikizungumza na Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe, kisha Waumini na mwisho pande zote mbili, na kuthibitisha bila shaka kwamba wanatakiwa kushikamana na qibla yao mpya, wakiwa nyumbani na safarini.[79]

78. Tirmidhi, Tafsir, 2/2964.
79. Tazama, al-Baqara, 148-149.

Katika kuelezea na kufafanua hekma inayopatikana katika mabadiliko hayo, ndiyo maana uthibitisho huo umetolewa katika maana ya makhsusi ndani ya aya ifuatayo:

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۚ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي وَلِأُتِمَّ نِعْمَتِي عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

"Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo ili watu wasiwe na hoja juu yenu, isipokuwa wale walio dhulumu miongoni mwao. Basi msiwaogope wao, lakini niogopeni Mimi - na ili nikutimizieni neema yangu, na ili mpate kuongoka." (al-Baqara, 150)

Katika tangazo hilo la Mwenyezi Mungu, kuna hekma mbalimbali:

1. Kwa mujibu wa aya hiyo, hekma ya kwanza ya kubadilisha qibla ni kuwanyima Watu wa Kitabu na washirikina uthibitisho na ushahidi wanaoweza kuutumia dhidi ya Waislamu; kwa sababu ubadilishaji wa qibla kuelekea upande wa Kaaba ni miongoni mwa ishara na alama za Mtume wa Mwisho aliyetabiriwa katika vitabu vya zamani.

Utabiri wa Kitabu cha Isaya katika Agano la Kale kuhusu mustakbali wa Makka unaelezea kwa uwazi kuhusu alama za Mtume huyo. Hivyo hatua ya Mtume wa Mwisho ﷺ bado alikuwa akiswali kuelekea upande wa al-Aqsa wakati alitakiwa kuelekea upande wa Kaabah lingeibua shaka katika akili za Watu wa Kitabu.

Aidha, kwenda kinyume na qibla cha Nabii Ibrahimu عليه السلام kungepingana na hoja ya Mtukufu Mtume ﷺ ya kuuwakilisha Umma wa Ibrahimu, hoja ambayo ingetumiwa na washirikia kama pingamizi la msingi. Lakini baada ya mabadiliko hayo kutokea, pingamizi hilo halikutolewa tena, isipokuwa kwa wale waliojitengenezea mazoea ya kukana ukweli kutokana na ukaidi wao.[80]

2. Hekma nyingine ya kubadilisha qibla ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuwatmizia neema mbalimbali Waislamu. Hivyo, Waislamu walipewa qibla kuwapa nguvu ya kuwafanya wafikie lengo lao la kuelekea kwenye ukamilifu wa njia ya haki. Qibla ni sehemu ya neema hizo.

3. Mojawapo katika hekma za Mtukufu Mtume ﷺ kuanza kuswali akielekea Baytul-Maqdis ni kuonesha kuwa dini zote kutoka mbinguni chanzo chake ni kimoja na hivyo kuzivuta nyoyo za Wayahudi na Wakristo kwenye Uislamu. Hatua hii inachukuliwa kuwa iliweza angalau kupunguza upinzani wa Wayahudi na Wakristo wakati wa kuchipua kwa jamii na dola ya Kiislamu.

Wakati huo huo, pamoja na mambo mengine, tukio hili lilithhibitisha kuwa Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa na mamlaka yoyote ya kuingilia kati au kuiamulia Qur'an Tukufu. Licha ya kwamba alikuwa akitamani sana Kaabah iwe qibla yake mpya, alilazimika kusubiri miezi kumi nas ita baada ya Hijra,ndipo aya husika zikashuka.

Funga, Zakatul-Fitr na Zaka

Wakati Uislamu ukijiimarisha kisiasa kwa kufanya harakati mbalimbali za kijeshi, wakati huo huo uliendelea kuuboresha uhai wake adhimu wa kiroho. Hatua muhimu katika hilo ni pale ilipowataka Waislamu kufunga swaumu wakati wa mwezi wa Ramadhan.

80. Tazama, Elmalılı, I, 537.

Tangazo hilo la kuifaradhisha funga lilitolewa mwezi wa Shaaban, miezi kumi na nane baada ya Hijra, muda mfupi tu baada ya mabadiliko ya qibla.[81]

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliitangaza faradhi ya kufunga swaumu ya mwezi wa Ramadhani kupitia aya hii:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

"Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kucha Mungu." (al-Baqara, 183)

Kuhusu hilo, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Uislamu umejengwa juu ya mambo matano: Kushuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mtume Wake, kudumisha swala, kutoa zaka, kuhiji na kufunga mwezi wa Ramadhan." (Bukhari, Iman, 1, 2; Tafsir, 2/30; Muslim, Iman, 19-22)

Katika hadith ifuatayo, Mtukufu Mtume ﷺ amezielezea kwa uzuri kabisa fadhila na ubora wa funga:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema, 'matendo yote ya mwanadamu ni kwa ajili yake, isipokuwa Funga. Funga ni kwa ajili yangu tu, nami ndiye nitakayeilipa.' Funga ni ngao. Mja anapokuwa amefunga hapaswi kujiingiza katika maneno ya kipuuzi au ugomvi. Iwapo mtu atamtukana au kumkasirisha, amwambie, 'Nimefunga.' Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambye nafsi ya Muhammad iko mikononi Mwake, harufu ya mtu aliyefunga ni nzuri mbele ya

81. Ibn Saad, I, 248.

Mwenyezi Mungu kuliko harufu ya miski. Mtu aliyefunga huwa na furaha katika nyakati mbili: Pale anafuturu, na pale atakapokuna na Mola wake na kupata thawabu kutokana na funga yake." (Bukhari, Sawm, 9; Muslim, Siyam, 163)

"Amali za mwanadamu hulipwa mara dufu; amali moja hulipwa kuanzia mara kumi mpaka mara mia saba. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, 'Isipokuwa funga, Mimi Mwenyewe ndiye nitakayeilipa…kwa maana mtu anayefunga huacha vile anavyovitamani kwa ajili Yangu." (Muslim, Siyam, 164)

"Mwenye kudumu kutoa sadaka katika njia ya Mwenyezi Mungu, ataitwa kutoka kwenye milango mbalimbali ya Pepo, 'Njoo, ewe mja kipenzi wa Mwenyezi Mungu; katika mlango huu kuna neema na baraka tele zinakusubiri!' Wale wenye kudumisha swala wataendelea kuitwa katika mlango wa swala, waliopigana jihadi wataitwa katika mlango wa jihadi, waliofunga watandelea kuitwa katika mlango wa *Rayyan* na wakarimu wataitwa katika mlango wa sadaka." Abu Bakr ؓ akauliza, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kila kitu changu kiwe fidia kwa ajili yako. Hata kama mtu ataitwa katika moja ya milango hii na akawa hana haja ya mlango mwingine, je bado kuna watu watakaoitwa katika milango hii yote?'

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu, "Ndiyo, na ninatarajia kuwa wewe utakuwa miongoni mwa hao watakaopata bahati hiyo." (Bukhari, Sawm, 4 Jihad, 37; Muslim, Zakat, 85, 86)

Funga ambayo hutuwezesha kuzitambua thamani za baraka lukuki tulizojaaliwa, ni ibada inayoziamsha hisia za kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu; na kwa kuiondosha roho katika matamanio na mielekeo ya kihayawani, funga huukomboa moyo kutoka kwenye minyororo ya maada (dunia) na hivyo kumpeleka mja kwenye subira, ambayo ni sifa ya juu kabisa ya kimaadili inayohitajiwa na mwanadamu. Funga ambayo hupandikiza dhamiri ya kuwakum-

buka masikini na wanyonge, huujaza moyo hisia za huruma. Licha ya kupewa cheo cha kuwa msimamizi wa hazina, Nabii Yusufu ﷺ hakuwahi kulijaza tumbo lake hata kidogo, ili asipate kuzisahau taabu zinazowakabili masikini.

Sambamba na hekma zote hizi, funga ni amri ya Mwenyezi Mungu yenye nguvu kubwa ya kuondosha hisia zote mbaya kama vile chuki na husda ambazo huikaba na kuisonga jamii. Katika funga kuna ufunguo wa siri ya kuacha mambo ya kupita kwa ajili ya mambo ya kudumu na ya milele. Ni ngao inayoulinda utu na heshima ya mwanadamu dhidi ya matamanio yasiyokwisha ya nafsi yanayotokana na vyakula na ashki.

Mchana wa mwezi wa Ramadhan huhuishwa kwa funga na usiku hupambwa kwa sala ya *tarawih*, ambayo ni Sunnah ya Mbora wa Viumbe ﷺ.

"Mwenyezi Mungu ameifaradhisha funga ya Ramadhan; nami nimeifanya *tarawih* kuwa Sunnah," alisema. (Ibn Maja, Salat, 173)

Ili kupata faida nyingi za mwezi wa Ramadhan, ni muhimu kuiambatisha swaumu na amali za ibada wakati wa usiku, na kujiepusha na kila aina ya mienendo isiyokuwa na faida, kuutakasa ulimi kwa dua na *dhikr* na kuusafisha moyo kwa machozi ya toba. Kukaa *itikaaf* katika siku kumi za mwisho nayo pi ani Sunnah ya Mtukufu Mtume ﷺ.

Anasema: "Mwenye imani moyoni mwake, akaihusisha mikesha ya mwezi wa Ramadha kwa kutarajia malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu, atasamehewa madhambi yake yote yaliyopita." (Bukhari, Tarawih, 46)

Bibi Aisha رضي الله عنها anasimulia:

"Jioni moja ya mwezi wa Ramadhan, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliswali swala ya Sunnah Msikitini. Watu wengi waliswali nyuma yake. Asubuhi baadhi ya Maswahaba wakaanza kuzungumzia kuhusu 'swala aliyoswali Mtume Msikitini usiku w ajana.'

Usiku uliofuata, Mtume wa Mwenyezi Mungu akaswali tena. Kwa mara nyingine watu wakaizungumzia; idadi ya walioswali nyuma yake ilikuwa imeongezeka zaidi. Katika usiku wa tatu au w anne, watu wakafurika tena Msikitini. Walikuwa wengi mno kiasi kwamba msikiti haukuwatosha. Lakini jioni iliyofuata, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakutokea. Asubuhi akasema:

'Nimeona kile ambacho mmekuwa mkikifanya. Kitu kilichonifanya nisitokee usiku w ajana nilihofia kuwa swala hii inaweza kuja kufanywa kuwa faradhi.'" (Bukhari, Tarawih, 1; Muslim, Musafirin, 177)

Mtukufu Mtume ﷺ hakuswali *tarawih* katika jamaah, aliona ni bora watu waiswali kulingana na vipawa vyao. Wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr ؓ tarawih iliendelea kuswaliwa kwa kila mtu kuiswali peke yake. Ni katika zam aza ukhalifa wa Omar ؓ ndipo ilipoanza kuswaliwa kwa jamaah.

Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alikuwa akikithirisha ibada na amali zake katika mwezi wa Ramadhan, muda ambao huingia katika mazingira ya mawasiliano yasiyokuwa na kikomo ya kuwasiliana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maelezo ya Ibn Abbas ؓ yanalithibitisha hili:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa karimu zaidi kuliko watu wote. Kipindi amabcho ukarimu wake ulikuwa ukiongezeka mno ni pale anapokutana na Jibril ؑ katika mwezi wa Ramadhan. Walikuwa wakikaa wote pamoja kila usiku wa Ramadhan na kusomeana Qur'an. Baada ya kukutana na Jibril ؑ ukarimu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ulikuwa ukiongezeka zaidi kuliko

upepo wa rehma unaondelea kuvuma." (Bukhari, Bad'ul-Wahy, 5, 6; Sawm, 7; Muslim, Fadail, 48, 50)

Muda mfupi baada ya amri ya kufunga ilikuja amri ya swala ya eid na zaka ya fitri. Mtukufu Mtume ﷺ aliweka kiwango maalumu cha fitri ambacho kilitakiwa kutolewa na kila Muislamu, mdogo na mkubwa, mwanamke na mwanaume, mtwana au mtumwa. Kiwango hicho ni *sa'*[82] ya tende au kipimo cha shayiri kilicho sawa na kiwango hicho.[83] Na kuhusu mafukara na masikini, alisema, "Siku ya leo (*eid*) waepusheni wasitembee na tumbo lisilokuwa na kitu." (Ibn Saad, I, 248)

Zaka ya fitri ikitolewa kabla ya swala ya eid huweza kufanikisha malengo yake na hukubaliwa. Lakini ikitolewa baada ya swala, basi ingawa itakubaliwa, haitahesabiwa kuwa ni zaka ya fitri bali kama sadaka tu.[84]

Anas رضي الله عنه anasema:

"Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowasili Madina, wenyeji walikuwa wakiadhimisha sikukuu mbili. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza umuhimu wa sikukuu hizo mbili. Wakajibu, 'Siku hizi mbili ndizo tulizokuwa tukiziadhimisha na kuzisherehekea katika zam aza Ujahiliya'.

Hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, 'Mwenyezi Mungu amewabadilishia sikukuu mbili zilizo bora zaidi kuliko hizo. Nazo ni Adh-ha na Ramadhan!'" (Abu Dawud, Salat, 239/1134; Nasai, Iydayn, 1)

---

82. *Sa'* moja ni ni kipimo ambacho kinakaribia kuwa sawa na uzito wa dirham 1040 za ngano au shayiri. Kwa mujibu wa dirham ya kisheria, *sa'* moja ina uzito wa kilogramu 2,917, na kwa mujibu wa dirhamu ya kawaida ina uzito wa kilogramu 3,333.
83. Bukhari, Zakat, 70-78; Muslim, Zakat, 13.
84. Ibn Maja, Zekât, 21.

Baada ya kuswalisha swala ya eid kwa mara ya kwanza tarehe 10 ya mwezi wa Dhulhajj, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaagiza Waislamu kuchinja wanyama wao kwa ajili ya sadaka. Katika miaka yote kumi aliyokaa Madina, alikuwa akichinja mnyama wa sadaka ya eid kila mwaka.[85] Kila mwaka alikuwa akichinja wanyama wawili; mmoja kwa niaba ya watu wa umma wake wasiokuwa na uwezo wa kufanya hivyo, na mwingine kwa ajili yake na familia yake.[86]

Hanash رضي الله عنه anasimulia akisema:

"Nilimuona Ali رضي الله عنه akichinja wanyama wawili wa sadaka. Nilipomuuliza sababu, akajibu, 'kabla Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hajafariki dunia aliniomba niwe nachinja mnyama mmoja kwa niaba yake pia. Hivyo nimechinja mnyama wa pili katika kutekeleza ombi lake na nitaendelea kufanya hivyo kila mwaka.'" (Abu Dawud, Adahi, 1-2/2790; Ahmad, I, 107)

Kuanzia wakati wa swala ya alfajiri ya kilele cha eidul-Adh-ha mpaka wakati wa swala ya alasiri ya siku ya nne, ambayo ni jumla ya swala ishirini na tatu, Waislamu wote, wake kwa waume, wakazi na wasafiri, wanaoswali kwa jamaah au mmoja mmoja, ni wajibu kwao kusoma takbir'ut-tashriq:[87]

اَللَّهُ أَكْبَرُ اَللَّهُ أَكْبَرُ لَا اِلَهَ اِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ اَللَّهُ أَكْبَرُ وَلِلَّهِ الْحَمْدُ

Baada ya zaka ya fitri, ilikuja amri ya zaka. Qur'an Tukufu inasema:

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ

85. Ibn Saad, I, 248-249.
86. Abû Dawud, Adahi, 3-4/2792; Ibn Saad, I, 249.
87. Muwatta, Hajj, 205.

"Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba." (adh-Dhariyat, 19)

وَالَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ

"…Na ambao wanatoa Zaka" (al-Muminun, 4)

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَهُمْ

"Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao…" (at-Tawba, 103)

Zaka imetajwa mara ishirini na sita ndani ya Qur'an pembezoni mwa swala nam ara nne ikiwa peke yake. Miongoni mwa hizo mara nne ni aya iliyotajwa hapo juu katika surah al-Muminun, ambayo japokuwa haikutajwa pembezoni mwa swala, sura hiyo imeendelea kuwasifu Waumini wanaosimamisha na kudumisha swala. Sababu ya kutajwa pamoja katika aya nyingi ni kuwa, katika matendo yote ya ibada, ya kimwili au ya kimali, hizi ibada mbili ni za msingi na zina umhimu ulio sawa. Kuna hadith moja inasema:

"Hakuna kheri katika swala ya mtu ambaye hatoi zaka licha ya kuwa anaswali." (Haythami, III, 62)

Taasisi, mashirika na/au vyama kama vile shule au hospitali hayawezi kupewa Zaka, haki hiyo inabaki kwa makundi nane ya watu yaliyoainishwa na Mwenyezi Mungu.[88] Ikitokea mashirika hayo yakapokea zaka, basi hayatatakiwa kuitumia kwa mambo

88. Tazama, Tawba, 60.

mengine zaidi ya mahitaji ya msingi ya masikini. Labda wanaweza kuitumia tu kugharamia mahitaji ya wanafunzi au wale wanaotafuta elimu kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hivyo kuwaepusha wanafunzi hao na shughuli nyingine zaidi ya masomo. Miongoni mwa masharti ya zaka ni kuipeleka mahali panapofaa zaidi kukidhi mahitaji ya msingi (*hawaij-i asliyya*) ya masikini ambao hawawezi kukidhi mahitaji yao, na kufanya utafiti wa kina ili kuwapata watu sahihi wenye mazingira hayo. Kwa hali hiyo, mashirika yaliyopewa jukumu la kusimamia na kufikisha Zaka kwa walengwa yanatakiwa kulishughulikia suala hili kwa umakini mkubwa, ili yasije yakawajibika mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Qur'an Tukufu inaainisha watu sahihi wanaostahiki kupata zaka kama ifuatavyo:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

"Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima." (at-Tawba, 60)

Kwa hivyo, mashirika na taasisi zinaweza kupokea Zaka kwa sharti la kuzipeleka kwa kundi lolote katika makundi hayo nane. Hili ni jambo muhimu sana.

Baada ya kupokea tangazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuhusu Zaka, Mtukufu Mtume ﷺ aliandika na kuorodhesha vitu vinavyotakiwa kutolewa zaka, kiwango cha chini cha mali inayopaswa kutolewa zaka, kisha karatasi hiyo akaifunga kwenye upanga wake. Karatasi hiyo aliendelea kuwa nayo mpaka alipofariki dunia, na aliifanyia kazi kwa umakini wa hali ya juu. Abu Bakr na Omar ﷺ nao katika zam aza ukhalifa wao walifuata nyayo za Mtukufu Mtume ﷺ kwa kuufanyia kazi waraka huo.[89]

Kuna sababu na hekma mbalimbali za kijamii na za binafsi za kufaradhishwa zaka. Miongoni mwake ni pamoja na kuweka kizuizi dhidi ya ukandamizaji unaoweza kufanywa na matajiri kwa kutumia nguvu ya mali zao, kuwazuia maskini wasiwe na hisia za chuki dhidi ya matajiri, kutunza mshikamano wa kijamii na kuwafungamanisha pamoja kwa upendo. Katika mfumo wa kijamii wa Kiislamu, zaka na *infaq* ni nguzo muhimu katika kuendeleza uwiano na upendo baina ya matajiri na masikini.

Hekma nyingine ya kuamrishwa kwa Zaka na sadaka ni kuzuia mapema mrundikano wa mali kwa mtu mmoja na hivyo kuwalinda masikini dhidi ya unyonyaji na kuepusha ukuaji mkubwa wa chuki na uhasama. Utajiri unapokuwa chanzo cha ufakhari na kiburi, huwa ni mwanzo wa mwisho mbaya kwa tajiri. Ukweli ni kwamba wanajamii wote, wote wanaosaidia na wale wanaosaidiwa, wanahitajiana kimaada na kimaanawi.

İkumbukwe kuwa, kwa uhalisia, mali ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mamlaka anayokuwa nayo mwanadamu juu ya mali ni mamlaka ya muda yenye kuhama. Kwa maneno mengine, mali ni amana ambayo mwanadamu anakuwa amekabidhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo matumizi yake yanatakiwa

89. Bukhari, Zakat, 38; Ahmad, II, 14.

kufanyika kutokana na maagizo ya Mwenyezi Mungu mwenyewe. Inatakiwa kutumiwa katika namna iliyoagizwa na Mmiliki wake Halisi (yaani Mwenyezi Mungu). Mali inapotumika kinyume na maagizo ya Mwenyezi Mungu hugeuka kuwa chanzo cha kumpeleka mtu kwenye upotevu kwa kuwa hudanganyika na kuzama katika dhulma. Mapenzi ya mali hukita mizizi katika nyoyo za wale wanaoingia katika njia hii hatari. Sababu ya Mwenyezi Mungu kuitaja mali na watoto tu kuwa ndio cha fitna, au mtihani, ni ule ukweli kwamba mali huingia ndani ya moyo wa mtu na kugeuka kuwa sanamu linaloabudiwa na mtu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaonya wale waliozama katika janga hili kuwa:

وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍيَوْمَ يُحْمَىٰ عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ۖ هَٰذَا مَا كَنَزْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْنِزُونَ

"Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu. Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikizia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika." (at-Tawba, 34-35)

Vilevile,Mtukufu Mtume ﷺ amebainisha mwisho mbaya unaowasubiri wale wanaopuuza kutoa zaka:

'"Siku ya Kiyama kila kipande cha dhahabu au fedha ambacho hakikutolewa Zaka kitaletwa kikiwa kimechemshwa katika moto na kuwa kama chuma na kuwababua wahusika mbavu zao, nyusoni na migongoni. Kila wakipoa, wataendelea kuadhibiwa. Adhabu

itaendelea kwa siku moja ambayo ni sawa na miaka elfu hamsini ya duniani, mpaka watu watakapohukumiwa. Mwishowe, mtu huyo ataoneshwa njia yake inayoelekea Peponi au Motoni.'

Maswahaba wakauliza, 'Vipi kuhusu ngamia ambao hawakutolewa Zaka?'

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu, 'Kila mwenye ngamia asiyelipa Zaka – ikiwemo kuwakamua maziwa na kuwapa masikini – ataamrishwa kulala chini akiwa amenyooka, kwenye uwanja mpana, ndama wote watakuja kwa wingi wao wakimkanyaga na kumrarua kwa meno yao. Wakimaliza, watakutafutia ngamia wengine. Hili litaendelea kwa siku nzima ambayo ni sawa na miaka elfu hamsini, mpaka wanadamu watakapohukumiwa. Mwisho, mtu huyo ataoneshwa njia yake ya kuelekea Peponi au Motoni.'

Maswahaba walipouliza swali jingine kuhusu hatima ya wamiliki wa ng'ombe na kondoo, jawabu la Mtukufu Mtume ﷺ halikubadilika." (Muslim, Zakat, 24; Bukhari, Jihad, 48)

Muamala mzuri wakati wa kutoa sadaka na zaka ni jambo muhimu. Anayetoa Sadaka anapaswa kujiepusha na tabia inayoweza kuzibatulisha amali zake zote hizi, kama vile kutoa matusi au kutoa bidhaa zenye viwango vya chini. Mtoaji anatakiwa kumshukuru mpokeaje, kwa maana amempa fursa ya kutekeleza wajibu wake ambao yumkini asingeweza kuutekeleza. Wakati huo huo sadaka ni kinga madhubuti inayomlinda mtoaji dhidi ya maradhi na masaibu. Kwa kweli, watu masikini ni baraka kwa matajiri, kwa maana dua zao wanazowaombea ndizo zinazofungua milango ya Pepo.

Aya ifuatayo imeainisha mwenendo sahihi unaotakiwa wakati wa kutoa sadaka:

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ لَا يُتْبِعُونَ مَا أَنْفَقُوا مَنًّا وَلَا أَذًى ۙ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ۞ قَوْلٌ مَعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِنْ صَدَقَةٍ يَتْبَعُهَا أَذًى ۗ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَلِيمٌ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُبْطِلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَىٰ كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ رِئَاءَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

"Wanao toa mali zao kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii masimbulizi wala udhia kwa walicho toa, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayo fuatiliwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha na Mpole. Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho…" (al-Baqara, 262-264)

Itikafu

Kilugha itikafu inamaana ya kujifungia na kusubiri sehemu fulani, kufunga swaumu na kushughulika na jambo fulani. Lakini, kitaalamu, itikafu ina maana ya kukaa msikitini kwa kipindi fulani cha muda, kwa nia ya kutaka kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa kuwa hakuna ukomo wa muda maalamu uliowekwa, kukaa huko, hata kama itakuwa ni kwa saa moja, itahesabiwa kuwa ni itikafu, kwa kuwa ni sunnah. Hivyo, aya hii:

وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ

"…Wala msichanganyike nao, na hali mnakaa Itikafu msikitini…" (al-Baqara, 187), inaonesha kuwa funga ni sehemu ya lazima katika itikafu. Hivyo, aya hiyo inapendekeza kuwa kipindi cha kukaa itikafu hakiwezi kuwa chini ya siku moja – na hiyo ndiyo itikafu ya kisheria. Kwa hali hiyo, kwa ujumla itikafu hufanywa wakati wa mwezi wa Ramadhan, kwa kukaa ndani ya msikiti huku ukiwa umefunga swaumu. İtikafu ni hali ya mja kuzama katika ibada kwa kufunga mchana na kuutumia usiku msikitini kwa kufanya ibada na kuzama katika *dhikr*.

Itikafu, ambayo hufanywa siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhan, ni Sunnah Muakkadah, (yaani sunnah yenye nguvu ambayo ilikuwa nadra mno kutofanywa na Mtukufu Mtume ﷺ) na wakati huo huo ni *fardhul-Kifayah* (yaani faradhi inaweza kufanywa na baadhi ya watu na waliobaki wakaondokewa na wajibu wa kuifanya). Mtu anapoweka nadhiri ya kukaa itikafu anapaswa kuitimiza. Kukaa itikafu katika siku ambazo sio za mwezi wa Ramadhan huhesabiwa kuwa ni jambo lenye kupendeza (*mustahab*).

Mtu anapokaa itikafu inamlazimu kuwa makini asitoke msikitini isipokuwa kama kutakuwa na haja ya lazima, kama vila kutawadha n.k

Wake wa Mtukufu Mtume ﷺ walikuwa wakikaa itikafu ndani ya vyumba vyao. Awali walikuwa wakiwekewa hema ndani ya msikiti kwa ajili ya kukaa itikafu, baadaye ziliondolewa kwa amri ya Mtume ﷺ. Mahali sahihi kwa ajili ya itikafu ya wanawake wa Kiislamu ni nyumbani.

Bibi Aisha رضي الله عنها anasema:

"Siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhan, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akikesha kwa kufanya ibada; alikuwa akiiamsha familia yake, na kujikita moja kwa moja kwenye ibada

na kutochanganyika na wake zake." (Bukhari, Fadhlu Laylat'il-Qadr, 5; Muslim, Itiqaf, 7)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine iliyotolewa na bibi Aisha ﵂, Mtume ﷺ aliendelea kukaa itikafu katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhan. Aliendelea kufanya hivyo mpaka alipofariki dunia, ambapo katika mwaka wake wa mwisho alizidisha mpaka kufikia siku ishirini. Baada ya kufariki dunia, wakeze waliendelea kufuata nyayo zake.[90]

Tukio lifuatalo linaonesha umuhimu na fadhila za kukaa itikafu, na wakati huo huo linaonesha ulazima wa kuzingatia majukumu binafsi na ya kijamii:

"Siku moja ibn Abbas ﵄ aliingia Msikitini kwa ajili ya kukaa itikafu anamtolea salamu mtu mmoja aliyekuwepo, akamsogelea nakukaa jirani naye.

'Ndugu yangu, unaoneka kuwa umechoka na una huzuni', Ibn Abbas alisema.

Mtu yule akajibu, 'Ndiyo, ewe binamu wa Mtume. Mtu fulani aliniacha huru ambapo ninalazimika kumlipa kiasi fulani…lakini ninaapa kwa cheo cha mtu yule (Mtume) aliyelala katika kaburi lile, nimeshindwa kumlipa.'

'Je ungependa nizungumze naye kwa niaba yako?' aliuliza Ibn Abbas ﵄.

'Ukiweza kufanya hivyo', alijibu mtu yule. Wakati Ibn Abbas ﵄ akichukua viatu vyake na kuanza kutoka msikitini, mtu yle akamuita kwa sauti:

'Umesahau kuwa uko katika itikafu?'

90. Bukhari, Itikaf, 1, 17; Muslim, Itikaf, 5.

'Hapa, sijsahau. Ngoja nikwambie jambo moja nililolisikia kutoka kwa mtu aliyelala ndani ya lile kaburi' Ibn Abbas ﷺ alisema huku akitokwa na machozi:

'Kufuatilia nakutatua shida ya ndugu yako ni bora kuliko itikafu ya miaka kumi…na mwenye kuingia itikafu kwa siku moja tu kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenuezi Mungu, Mwenyezi Mungu huweka mahandaki matatu baina ya mtu huy ona Moto…na upana wa kila handakini zaidi ya umbali uliopo baina ya Mashariki na Maghribi." (Bayhaki, Shuab'ul-Iman, III, 424-425)

Vita ya Badr Kubwa (17 Ramadhan 2/ 13 Machi 624)

Katika mwaka wa pili wa Hijra, Maqurayshi walituma msafara mkubwa wa biashara wenye ngamia imara elfu moja, ukiwa na thamani ya dinar 50,000 kutoka kwa watuwote wa Makka, wanaume kwa wanawake. Msafara huo ulikuwa ukielekea kwenye Maonesha ya Biashara ya Gaza mjini Damascus. Washirikina maarufu thelathini mpaka arobaini walishiriki katika safari hii, maarufu zaidi wakiwa ni Abu Sufyan, Muhammad ibn Nawfal na Amr ibn As.

Washirikina walikuwa wamekwishahisi kuwa Waislamu wangejaribu kuikata njia yao muhimu ya biashara kuelekea Syria katika kulipiza hatua yao ya kuwakatalia kuingia Makka. Walipokuwa wakirejea Damascus walianza kuwa na hofu kubwa. Abu Sufyan alimkodisha Damdam ibn Amr, aliyekuwa sehemu ya msafara huo, akamlipa gramu 85 za dhahabu na kumtuma mara moja kutoka Tabuk kwenda Makka ili kutoa taarifa juu ya hali hiyo ya hatari.[91]

91. Ibn Hisham, II, 244; Waqidi, I, 27-28.

Wakati huo huo, siku tatu kabla Damdam hajawasili Makka, Atiqah, shangazi wa Mtukufu Mtume ﷺ aliota ndoto ya kutisha. Alimsimulia kaka yake, Abbas, juu ya ndoto hiyo.

"Ndoto niliyoiota ilinitisha. Ninahofia kitu kibaya kinaweza kulitokea kabila lako. Nitakachokwambia kifanye kuwa siri; usimwambie mtu yeyote!"

"Endelea…uliona nini?"

"Nilimuona mtu akiwa amepanda ngamia akaja na kusimama Abtah (baina ya Muhassab na Makka) na kutangaza, mara tatu, kwa sauti ya juu, 'Sikilizeni enyi wadanganyifu! Ndani ya siku tatu mripoti kwenye medani ya vita, mhali ambapo mtaangukia!' Watu waliomsikia walikusanyika. Kisha aliingia katika uwanja wa Kaabah na watu wakamfuata. Kwa mara nyingine alirudia kutangaza kwa sauti ya juu huku watu wakiwa wametanda nyuma ya Kaabah. Kisha alipanda juu ya Mlima Abu Qubays na kufanya hivyo tena. Baada ya kutangaza, alichukua jiwe kubwa na kulibiringisha. Lilibiringika kuelekea chini ya mlima, kisha lilipasuka karibu na shina la mlima na hakuna nyumba ya Makka ambayo haikuguswa na vipande vya jiwe hilo."

"Ninaapa, hii yaonekana kuwa ndoto muhimu", alisema Abbas. "Chochote utakachofanya usimwambie mtu yeyote juu ya ndoto hii!"

Baada ya kuachana na Atiqah رضي الله عنها, Abbas رضي الله عنه alikutana na rafiki yake Walid ibn Utbah. Abbas akamwambia kuhusu ndoto hiyo, lakini akamsisitizia kuifanya kuwa siri. Lakini ndoto hiyo ilimuogopesha Walid, akamsimulia baba yake, na muda mfupi tu ndoto hiyo ikawa mdomoni mwa kila mtu katika mji wa Makka.

Abbas رضي الله عنه anasimulia kilichotokea baadaye:

"Abu jahl alikasirika na kuniuliza, 'Tangu lini mmeanza kuwa na nabii mwanamke? Hamkutosheka na nabii mwanaume na mpaka wanawake wenu nao wakaona wanafaa kufanya kazi hiyo? Hakika Atiqah alimsikia mtu katika ndoto yake akiwaambia Maqurayshi wakaripoti mahali watakapoangukia baada ya siku tatu. Tuasubiri siku tatu. Kama alichosikia ni cha kweli, basi kuna kitu kitatokea. Lakini siku tatu zikipita na ikawa hakuna kilichotokea, basi tutaandika kwamba wanawake wenu ndio waongo wakubwa zaidi kuliko wanawake wote wa Arabia!'

Licha ya ugumu wa kuikanusha, nilimwambia kuwa hapakuwa na kitu kama hicho. Asubuhi ya siku ya tatu baada ya ndoto ya Atiqah, nikiwa nimehamaki, nilielekea kwenye Kaabah nikitaraji kumkuta Abu Jahl huko na kumuonesha hasira yangu kwa kuzuia kile ambacho alistahiki kukisikia kuhusu yale aliyoyasema siku tatu kabla. Wakati ninaingia, naye akawa anaondoka haraka kutokea kwenye mlango wa Sahm wa Nyumba Tukufu, na hivyo ikanifanya niwaze, 'huyu muovu amenikwepa kwa sababu alijua kuwa ninataka kumjaribu.' Sikuwa na taarifa kwamba alikuwa ameshaisikia sauti ya Damdam. Lakini muda si mrefu nikaligundua hilo, kwa maana nilimuona Damdam kwa mbali ambaye aliikata pua ya ngamia wake, akaichana kanzu yake na kukigeuza kikalio cha ngamia wake ili kuwashawishi watu na kuwaonesha jinsi hali ilivyokuwa mbaya. Alikuwa katikati ya bönde la Makka, akipiga kelele kwa nguvu zake zote:

'Enyi Maqurayshi! Okoeni msafara wenu! Muhammad na watu wake wamezivamia mali zenu mlizoziweka chini ya ulinzi wa Abu Sufyan! Msipotezi muda wa kuwawahi na kuwadiri… Msaada, msaada!' Sauti na mayowe ya Damdam yalitufanya tuyasahau mambo mengine yote." (Ibn Hisham, II, 244-247; Waqidi, I, 29-31)

Maquraishi hawakupoteza muda katika kujiandaa. Iliwachukua siku mbili au tatu pekee kuwa na silaha na kuwa tayari kwa vita. Wale ambao hawakuwa na silaha walinunuliwa silaha, na matajiri walichukua mzigo mkubwa katika kuwasaidia masikini katika maandalizi yao. Watu mashuhuri kama vile Suhayl ibn Amr, Zama bin Aswad walikuwa wakitangaza hadharani katika mitaa ya mji wa Makka kuwa:

"Ngamia na chakula ni juu yetu, zaidi ya mnavyoweza kudhani! Nyinyi nyote jiandaeni kwa safari! Asibaki mtu yeyote nyuma! Kama Muhammad ataudhibiti msafara wetu, bila ya shaka, atautumia kudhamini kampeni yake ya kivita kuja kuivamia Makka!"

Karibu wanaume wote wa Makka waliungana na jeshi hilo na wale ambao hawakuweza, waliwaajiri watu na kuwatuma badala yao. Ilipofika siku hiyo ambayo Abu Jahl aliwaamuru askari kuchukua vipandwa na kuanza safari, Umayya ibn Khalaf alianza kuburuza miguu yake, akihisi ndani mwake kuwa hiyo ndiyo itakayokuwa safari yake ya mwisho kwenda nje ya mji wa Makka, kwa sababu Mtukufu Mtume ﷺ, Mwaminifu, aliwahi kumtabiria adhabu inayomsubiri. Akaanza kusema huku akiwa ameshikwa na hofu kubwa: "Ninaapa, kamwe Muhammad hasemi uongo". Hatimaye, msisitizo wa kiujanja kutoka kwa Abu Jahl ulimshawishi kushiriki katika safari hiyo.

Wakati Utba na kaka yake Shaybah walipoanza kuziandaa sialaha zao, mtumwa wao Addas aliwauliza iwapo walikuwa wakijiandaa kwa jambo gani.

"Unamkumbua Yule mtu uliyempatia tende katika shamba letu kule Taif?" waliuliza.

'Hakika, ninamkumbuka!'

"Basi tunakwenda kupambana naye!"

Addas aliwaangukia miguuni mwao na kuanza kuwasihi.

"Tafadhalini msiende! Hakika yeye ni Mtume! Itawakumba gharıka!"

Machozi yalikuwa yakitiririka kwenye mashavu yake. Utbah na Shaybah waliendelea kutomsikiliza na hivyo wakaondoka bila kujali.

Idadi ya waabudu - sanamu ilikuwa mia tisa na hamsini. Watu mia moja au mia mbili walikuwa wamepanda farasi huku wengine wapatao mia saba wakiwa juu ya ngamia. Wengi wao walikuwa na ngao. Watu wote mashuhuri miongoni mwa Maqurayshi walikuwepo, wakisindikizwa na watumwa wa kike, ambao walikuwa wakiwapigia ngoma na kuwaimbia mashairi ya kuwaponda Waislamu wakati wakielekea nje ya mji wa Makka.[92]

Ilikuwa mwaka wa pili wa Hijra, tarehe kumi na mbili ya mwezi wa Ramadhan. Mtukufu Mtume ﷺ alimuacha Abdullah ibn Ummi Maqtum رضي الله عنه mjini Madina kama imamu wa swala na kuondoka akiwa na jeshi la Waislamu mia tatu na kumi na tatu, sitini na nne kati yao walikuwa *Muhajirun* na wengine wote walikuwa *Ansar*. Watatu walipanda farasi, sabini wakiwa na ngamia na waliobaki walikuwa wakitembea kwa miguu.[93]

92. Waqidi, I, 31-39; Bukhari, Manaqib, 25; Ibn Kathir, al-Bidayah, III, 294-295.
93. Waqidi, I, 23-24; Ibn Hisham, II, 250-251; Ibn Saad, II, 12.

Mtukufu Mtume ﷺ alilisimamisha jeshi la Waislamu katika eneo la Buyut'us-Suqya, umbali wa maili moja kutoka Madina, na kutoa amri kwa wazee na watoto warudi Madina. Saad ibn Abi Waqqas ؓ anaelezea:

"Muda mfupi kabla ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutoa amri kwa vijana warudi, nilimuona ndugu yangu Umayr akijaribu kujificha.

'Unataka kufanya nini?' Nilimuuliza.

Akasema, ninahofia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaweza kuniona na kuniambia nirudi nyumbani, lakini kwa hakika nina-taka kuja pamoja nanyi kwa matumaini ya kufa kishahidi!'

Kwa hakika, baada ya kumuona, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliona kuwa ni mdogo na kumshauri arudi nyumbani. Lakini Umayr akaanza kulia sana kiasi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ilibidi amruhusu kubaki. Kwa kuwa alikuwa na umbile jembamba, nilimfunga upanga wake mwilini mwake. Umayr ali-kuwa na takriban miaka kumi na sita alipouawa kishahidi katika vita vya Badr." (Waqidi, I, 21; Ibn Sad, III, 149-150)

Kutokana na upungufu wa ngamia waliokuwa nao Waislamu, watu watatu walilazimika kufanya zamu ya kupanda juu ya kila ngamia. Mtukufu Mtume ﷺ alishirikiana na Ali ؓ na Abu Lubabah ؓ. Ilipifika zamu ya Mtume ﷺ kutembea kwa miguu, walimuomba abaki juu ya ngamia na wao watembee kwa miguu badala yake. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ akawaambia: "Nyinyi hamuwezi kustah-mili matatizo ya kutembea zaidi yangu mimi, na mimi pia ni mhitaji wa kupata thawabu zaidi yenu nyinyi!" (Ibn Sad, II, 21; Ahmad, I, 422)

Mwenendo na tabia hii inaonyesha upendo mkubwa aliokuwa nao Mtukufu Mtume ﷺ kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, upendo ambao alionao ndani mwake, na shauku yake ya kuwa karibu zaidi

na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa amali yoyote na wakati wowote. Muda wote anatuelimisha juu ya umuhimu wa kushikamana na uadilifu bila kuangalia mtu huyo ni nani au bila kujali mazingira gani tuliyomo.

Baadaye Mtukufu Mtume ﷺ alimwambia Abu Lubabah ؓ arejee Madina kukaimu nafasi yake mpaka atakaporejea.[94]

Akiwa anatambua kuwa hakuna kimbilio lingine zaidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, akiyapeleka mahitaji yake yote Kwake Mwenyezi Mungu na kutovumilia kuona ummah wake ukidhoofika wakati wa safari yao ya kuelekea Badr, Mtukufu Mtume ﷺ aliomba dua ifuatayo:

"Ewe mwenyezi Mungu…Wape vipandwa kwa maana hawana vipandwa! Wape mavazi kwa maana hawana mavazi! Wape chakula kwa maana wao ni wenye njaa!"

Kwa hakika, baada ya ushindi walioupata katika medani ya vita vya Badr, kila Muislamu alirejea nyumbani akiwa na ngamia mmoja au wawili, mavazi na akiwa ameshiba. (Abu Dawud, Jihad, 145/2747)

Katika nyakati hizo zenye kuhitaji nguvu nyingi ambazo zilisadifiana na mwezi mtukufu wa Ramadhani, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaamuru waislamu wafungue swaumu zao, kwa maana walikuwa wakihitaji nguvu nyingi za kimwili kabla ya kuingia vitani. Hivyo waislamu wote walioshiriki vita vya Badr waliakhrisha funga zao mpaka waliporejea nyumbani.

Jeshi la kwanza la Uislamu lilikuwa njiani kuelekea Badr. Walipofika katika bonde la Aqiq watu wawili, Hubayb ibn Yasaf na Qays ibn Muharris, ambao walitaka kuungana na jeshi hilo kwa madhumuni tu ya kupata sehemu ya ngawira za vita, waliwakuta mahali hapo.

94. Ibn Hisham, II, 251.

"Mlikuwa pamoja nasi tangu mwanzo?" Mtukufu Mtume ﷺ alimuuliza Hubayb.

"Hapana. Bali wewe ni jirani yetu na binamu yetu kwa upande wa mama yako. Hivyo tumeshiriki ili kuwasaidia watu wetu na kupata ngawira!" alijibu.

"Mnamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake?" Mtukufu Mtume ﷺ akauliza. Hubayb alipojibu kwa kukataa, alikutana na jawabu lifuatalo:

"Hivyo rudi nyumbani, kwa maana hatuhitaji msaada kutoka kwa muabudu sanamu!"

Hubayb asingeweza kulikataa jawabu lolote, lakini bado aliendelea kusema: "Kila mtu anajua jinsi nilivyo shujaa katika medani ya vita na kiasi gani ninavyoweza kumtia hasara adui. Je siwezi tu kupigana nikiwa upande wako ili nipate kiasi cha ngawira?"

"Hapana. Silimu kwanza kisha waweza kupigana!" Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijibu, baada ya hapo akaendelea kuliongoza jeshi kuelekea vitani.

Lakini muda mfupi baadaye, Hubayb alikuja tena na kuelezea pendekezo lake kwa mara nyingine. Hata hivyo, jibu halikubadilika. Hubayb alichanganyikiwa. Alikuwa mtu maarufu miongoni mwa waarabu kwa ushujaa wake katika medani ya vita. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ hakumruhusu kujumuika na jeshi lake, kwa sababu tu hakuwa Muislamu. Msimamo adhimu wa Mtukufu Mtume ﷺ, licha ya tofauti kubwa iliyokuwepo baina ya uimara wa jeshi la Waislamu na majeshi ya makafiri, ulimtikisa sana Hubayb. Kwa muda fulani hali hiyo ilimfanya aingie katika kina cha ulimwengu wake wa ndani na akaweza kuona nuru za himaya ya haki ambayo alikuwa hajawahi kuiona hapo kabla. Hapo alinyanyuka na kumkimbilia

Mtukufu Mtume ﷺ. Mara hii alikuwa na kitu kingine kabisa akilini mwake.

"Ndiyo, ninamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!" alitamka kwa upendo na utulivu wa hali ya juu.

Mtukufu Mtume ﷺ alionekana kuwa mwenye furaha. "Sasa unaweza kuungana nasi upendavyo", alisema. (Muslim, Jihad, 150; Tirmidhi, Siyar 10/1558; Waqidi, I, 47; Ibn Sad, III, 535)

Tukio hili linathibitisha kiwango cha imani ambayo, bila kujali mazingira ni magumu kiasi gani, njia au nyenzo batili haipaswi kutumika hata kidogo kulifikia lengo halali. Badala yake mtu anachotakiwa kufanya ni kuchukua tahadhari za lazima na kisha aendelee kumtegemea Mwenyezi Mungu. Kwa kumkatalia Hubayb kujiunga na jeshi la Waislamu kwa sababu ya kutokuwa Muislamu, Mtukufu Mtume ﷺ alitaka kuuonyesha ummah wake wa baadaye msimamo wa mfano unaosukumwa na hisia kubwa ya imani. Mtukufu Mtume ﷺ alitambua vyema kuwa aina yoyote ya msaada na fadhila hutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee, ambaye ndiye aliyekuwa kimbilio lake katika hali zote na ambaye alikuwa akirejea Kwake wakati wote. Hatua hiyo ni mfano wa msingi na dhihirisho hai la *tawakkul*, yaani kumtegemea Mwenyezi Mungu pekee, ambayo imetajwa katika aya ifuatayo:

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

"Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa." (al-i Imran: 173)

Hudhayfah ؓ anasimulia:

"Mimi na baba yangu tulikuwa tumetoka kwa ajili ya kuungana na jeshi. Waabudu - sanamu wa Kiquraishi wakatuzuia wakitutuhumu kuwa '…mnataka kuungana na safu za jeshi la Muhammad'. Lakini tuliwahakikishia kuwa tulikuwa tukienda Madina kwa ajili ya kushughulikia masuala mengine. Hapo wakatulazimisha tuweke kiapo kuwa hatutaungana na Mtume wa Mwenyezi Mungu na kupigana upande wake. Tulipowasilia Madina, tulimueleza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuhusu suala hilo, naye akasema:

'Kama ni hivyo basi rejeeni. Tutachunga ahadi mliyoiweka kwa ajili yenu na kumuomba Mwenyezi Mungu awape nusra dhidi yao!' Hiyo ndiyo sababu iliyonifanya nisiwepo katika vita vya Badr." (Muslim, Jihad, 98). Tukio hili ni ushahidi mwingine wa wazi wa uaminifu wa hali ya juu wa Mtukufu Mtume ﷺ ambao uliwafikia mpaka maadui zake.

Vilevile walikuwepo wanawake ambao walitaka kushiriki katika vita vya Badr. Miongoni mwao ni Umm Waraqa, ambaye alimkimbilia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumsihi:

"Tafadhali, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nakuomba uniruhusu niungane nanyi…nitawatibu majeruhi na wagonjwa, na Mwenyezi Mungu akipenda, niweze kufa kishahidi!"

Badala yake Mtukufu Mtume ﷺ alimshauri kuwa: "Ni bora kwako ukisoma Qur'an nyumbani mwako na kwa hakika Allah atakupa heshima ya kufa shahidi."

Kufuatia mazungumzo haya, Umm Waraqa alikuja kujulikana mingoni mwa Maswahaba kama *'Shaheedah'* (yaani aliyekufa katika njia ya Mwenyezi Mungu). Baadaye, kutokana na kuwa na kiu kubwa ya kufa kishahidi, wakati wa ukhalifa wa Umar رضي الله عنه, watumi-

shi wake walimsonga na blanketi yenye mahameli mpaka akafariki dunia. Umar ﷺ alipopewa taarifa alisema: "Mwenyezi Mungu na Mtume Wake walisema kweli", hapo wale waliohusika na kifo chake wakakamatwa na kupata adhabu inayowastahiki. (Abu Dawud, Salat, 61/591; Ibn Hajar, al-Isaba, IV, 505)

Baada ya kutaarifiwa kuwa Waislamu walikuwa wakielekea upande wa Badr, bila kuchelewa Abu Sufya alibadilisha uelekeo wa msafara wake na kuelekea upande wa pwani, akaiacha Badr upande wake wa kushoto.[95] Alipotambua kuwa ameuokoa msafara wake, alituma mjumbe kwenda kwa jeshi la Maqurasishi akiwa na ujumbe ufuatao:

"Mlitoka kuja kuulinda msafara wenu, watu na mali zenu. Lakini sasa hatari imeondoshwa, mnaweza kurejea nyumbani!"

Kutokana na ujumbe huo wa Abu Sufyan na kwa kuufanyia kazi ushauri wa Ahnas ibn Sharik, wanajeshi kutoka ukoo wa Ibn Zuhra na Ibn Kaab walirejea nyumbani. Lakini Abu Jahl aliendelea kuwa kichwa ngumu. Alisema kwa majivuno:

"Hatutarudi nyumbani mpaka tufike Badr. Huko tutakaa kwa muda wa siku tatu. Tutachinja ngamia na kusherehekea; wanawake watacheza na kuimba. Waarabu walio jirani na eneo hilo watatusikia na kutuogopa kuanzia hapo na kuendelea. Twendeni!"

Abu Sufyan aliposikia kuwa washirikina wa Makka wameamua kusonga mbele bila kujali, alisema, "Nalisikitikia kabila langu… Hili lazima litakuwa ni wazo la Ibn Hisham (Abu Jahl)! Kukataa kwako

95. Ibn Hisham, II, 57.

kurejea kunatokana na tamaa yake ya kuwa kiongozi wa watu… ni uasi! Na uasi ni mkosi!" (Waqidi, I, 43-45; Ibn Hisham, II, 258)

Akiwa mwenye kufuatilia kwa undani hali ya mambo ilivyokuwa ikiendelea, sasa Mtukufu Mtume ﷺ alitambua kuwa walikuwa wakikabiliana na vita vya kufa au kupona. Aliwakusanya Maswahaba wake akawauliza:

"Mnaona jambo gani linalofaa zaidi: kuufutilia msafara au kupambana na jeshi la Maqurayshi?"

Wakizungumza kwa niaba ya *Muhajirun*, Abu bakar na Umar رضي الله عنه walimhakikishia kuwa walikuwa tayari kukabiliana na jeshi la washirikina. Mtukufu Mtume ﷺ akataka kusikia maoni ya *Ansar*; na hapo alisimama Miqdad ibn Aswad رضي الله عنه na kuzungumza yafuatayo:

"Tambua ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwamba kamwe hatutakwambia yale yaliyosemwa na Wayahudi kumwambia Nabii Musa عليه السلام: 'Nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane!' (al-Maida: 24). Kutokana na ahadi tuliyokupa katika eneo la Aqabah, muda wote tupo tayari kupambana na adui kuliani na kushotoni kwako, mbele na nyuma yako, mpaka mwisho!"[96] (Bukhari, Maghazi, 4; Tafsir, 5/4)

Aliyesimama baada ya Miqdad رضي الله عنه ni Saada ibn Muadh رضي الله عنه:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu…tumekuamini na kuusadikisha ukweli wa Qur'an uliyoteremshiwa. Fanya unavyoona kama inafaa! Kwa hakika, kama utaingia baharini tutakufuata. Hakuna hata *Ansar* mmoja atakayesita!"

96. Ibn Masud رضي الله عنه anasimulia: "Nilimshuhudia Miqdad akitamka maneno hayo ya ushuhuda ambayo kama ningetakiwa kusema ningetamka maneno hay ohayo yenye thamani…" (Bukhari, Maghazi, 4; Tafsir, 5/4)

Maneno haya ya utii na kujisalimisha yaliweka tabasamu la faraja usoni mwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na baada ya kuwaombea dua fupi, akasema:

"Hivyo, twendeni mbele kwa Baraka za Allah! Habari njema kwenu…kwa maana Mwenyezi Mungu amewaahidi mojawapo kati ya mambo mawili, bila kuelezea ni jambo gani hilo.[97] Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, ni kana kwamba ninaziona sehemu ambazo Maqurayshi wataangukia katika medani ya vita!" (Muslim, Jihad, 83; Waqidi, I, 48-49; Ibn Hisham, II, 253-254)

Pindi jeshi la Kiislamu lilipowasili Badr, tayari Maqurayshi walikuwa wameweka kambi katika Bonde la Yalyal, nyuma ya kilima fulani cha mchanga,upande wa mbali kabisa na mji wa madina. Visima vya Badr, kwa upande mwingine, vilikuwa upande wa bonde lililo jirani kabisa na Madina.[98] Pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipofika kwenye kisima kilicho jirani kabisa na Badr, alishauriana na Ansar kuhusu sehemu nzuri zaidi ya kuweka kambi. Hubab ibn Mundhir رضي الله عنه alielezea wazi hisia zake:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hili eneo sio muafaka kwa kuweka kambi. Badala yake twende jirani kabisa na jeshi la Maqurayshi na kisha tuyafunge mabaki ya visima vilivyo nyuma yetu, isipokuwa kile kimoja. Kisha tunaweza kuweka Birika jirani na kisima kile ili maji yaweze kukusanyika hapo."

97. Mojawapo ya mambo waliyoahidiwa katika aya ya 7 ya surah Anfal ni ushindi watakaoupata dhidi ya maqurayshi na wengi wao kuangukia mikononi mwa Waislamu kama mateka, ilihali jambo la pili ni msafara mkubwa wa biashara za Maqurayshi uliokuwa ukitoka Damascus.

98. Ibn Hisham, II, 259.

Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ akaafiki.[99] (Ibn Hisham, II, 259-260; Ibn Sad, II, 15)

Kundi la waabudu masanamu ikiwa ni pamoja na Hakim ibn Hizam lilikuja kuchukua maji kutoka kwenye kisima kilichokuwa jirani na kambi ya Waislamu. Japokuwa Maswahaba walitaka kuwazuia wasichukue maji, Mtukufu Mtume ﷺ aliingilia kati na kusema: "Waacheni; wacheni wanywe maji." Siku hiyo Bar Hakim, watu wengine wote waliokuwa katika kundi hilo waliishia kuuawa katika medani ya vita vya Badr; na Hakim, kutokana na tukio hilo akasilimu. Baadaye, kila alipotaka kuweka kiapo katika kuwekea mkazo maneno yake, alikuwa akisema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye aliniokoa na kifo siku ya Badr na akanijaalia neema ya imani…" (Ibn Hisham, II, 261)

Kwa kumruhusu adui kunywa maji hayo, licha ya kutambua kuwa ni adui huyo huyo anayesubiria kuwaua hapo baadaye, Mtukufu Mtume ﷺ alionyesha kiwango cha juu cha tabia na maadili kilichowaenea watu wote. Tabia hiyo adhimu ikapelekea kuzilainisha nyoyo nyingi zilizokuwa ngumu kama jiwe, na hivyo kuzifungulia mlango kuelekea kwenye nuru ya uongofu.

Mara baada ya jeshi la Waislamu kuweka kambi, Saad ibn Muadh رضي الله عنه alisema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu… Ngoja tukiwekee kivuli na kipandwa chako kiwekwe karibu nawe. Kisha sisi tutakwenda kupambana na adui. Iwapo Mwenyezi Mungu atatupatia ushindi, hiyo itakuwa kheri. Lakini iwapo hatutapata ushindi, utampanda farasi wako na kwenda kwa ndugu zetu tuliowaacha nyuma. Ewe

99. Kwa mujibu wa maelezo ya wenyeji wa eneno hilo, japokuwa vilima vingine vya mchanga katika eneo la badr huwa vinahama kila baada ya miaka mitano kutokana na upepo mkali wa mfululizo, kilima ambacho Mtukufu Mtume ﷺ aliweka kambi kimeendelea kuwepo mpaka sasa.

Mtume wa Mwenyezi Mungu..! wanakupenda sana kama tunavyokupenda. Kama wangejua kama utaingia vitani, wangeweza kubaki! Hakika wameshikamana nawe kutoka ndani ya kina cha nyoyo zao na watapambana upande wako bila kujali lolote likakalotokea!"

Mtukufu Mtume ﷺ alimsifu Saad ﷺ na kumuombe kheri. Kisha Saad ﷺ aliuchomoa upanga kutoka kwenye ala yake na kusimama akilinda kwenye kivuli hicho kilichotengenezwa. (Ibn Hisham, II, 260; Waqidi, I, 49)

Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Omar ﷺ kwa mara ya mwisho kuwapelekea Maqurayshi ujumbe ufuatao: "Rejeeni nyumbani… kupambana na watu wengine (wasiokuwa nyinyi) ni bora kwetu!"

Hakim ibn Hizam alikuwa tayari kusikiliza ushauri huo. "Hii ni hatua nzuri; ni bora tuikubali", alisema. "Hatutapewa umuhimu na mtu yeyote baada ya hatua hii!"

Maneno yake yenye dhamira nzuri yalikandamizwa na inda na chuki ya Abu Jahl.

Ninaapa, hatutarejea npaka tulipize kisasi; hususan baada ya Allah[100] kutupatia fursa ya kufanya hivyo. Tutawafundisha somo ambalo litawafanya wasiweze tena kuisogelea na kuizuia misafara yetu!" Maneno haya yaliwahamasisha maqurayshi kuingia vitani. (Waqidi, I, 61-65)

---

100. Waarabu katika zama za Jaahiliya walikuwa wakiukubali uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini walikuwa wakimshirikisha na miungu wengine katika ibada zao, na hivyo wakapotoka kutoka kwenye njia ya *tawahid* wakaangukia katika njia ya *shirk*. Kwa sababu hiyo ilikuwa kawaida yao, kama inavyoonekana katika tukio hili, kulitaja jina la Mwenyezi Mungu na kuutaja Uungu Wake. Jambo lililowapeleka katika shipo la shir ni hatua yao ya kuabuadu masanamu wakisukumwa na tamaa yao ya kutaka kuwa karibu na Mwenyezi Mungu kwa kuyatumia masanamu kuwa waombezi wao na imani yao kwamba wangepata heshima kwa kufanya hivyo. (Tazama al-Ankabut: 61; az-Zumar: 3)

Waabudu masanamu walimtuma Umayr ibn Wahb na askari farasi mkubwa Abu Usama kwenda kulipeleleza jeshi la Waislamu. Baada ya kuizunguka mara moja kambi ya Waislamu, walirudi na kutoa maoni yafuatayo: "Hatukuona farasi au ngamia wenye maziwa na imara… wala hapakuwepo na idadi kubwa ya askari, wala hawana maandalizi makubwa ya vita. Lakini tumeona kikosi ambacho kipo tayari kuuawa kuliko kurejea nyumbani kuungana na familia zao! Hawana mahali pa kukimbilia wala chochote cha kujikinga zaidi ya panga zao!" (Waqidi, I, 62)

Omar رضي الله عنه anasimulia:

"usiku huo, kabla ya vita, Mtume wa Mwenyezi Mungu alituonyesha sehemu ambazo waabudu masanamu maarufu watakapoangukia mmoja baada ya mwingine. Naapa kwa Mwenyezi Mungu aliyemtuma kama Nabii wa haki, wote waliotajwa, hakuna aliyeweza kuponyoka. Baadaye walitupwa shimoni, wakarundikwa mmoja baada ya mwingine." (Muslim, Jannat, 76, Jihad, 83)

Eneo ambalo Waislamu walikuwa wameweka kambi lilikuwa na mchanga mwingi na hivyo kufanya iwe ngumu hata kutembea. Kuendelea kupungu kwa kiwango cha maji kulimaanisha kuwa walikuwa wakikabiliwa na upungufu mkubwa.Walikuwa wakikabiliwa na ugumu wa kupata maji ya kutosha hata kwa ajili ya wudhu. Vikwazo hivi, ikiongezewa na ubora wa jeshi la washirikina kwa upande wa umadhubuti na idadi, vilimpa Shetani hoja ya kutosha ya kujaribu kuingiza hofu dani ya nyoyo za Waislamu.

Lakini usiku huo manyunyu ya mvua yalinyesha kwa kiasi cha kutosha kulijaza bonde la Waislamu. Waislamu walihifadhi maji ya kutosha na kuyatumia kwa ajili ya mahitaji yao nay a wanyama wao. Wakati huo huo, mvua hiyo iliondosha vumbi na kuifanya ardhi iwe ngumu na madhubuti. Kwa upande mwingine, iliwalazimisha Washirikina kubaki mahali walipokuwa; hawakuweza kutoka

kwenye kambi zao. Aidha, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaaliwa Waislamu hali ya usingizi mwanana,[101] na yote hayo yameelezwa katika aya ifuatayo:

إِذْ يُغَشِّيكُمُ النُّعَاسَ أَمَنَةً مِّنْهُ وَيُنَزِّلُ عَلَيْكُم مِّن السَّمَاءِ مَاءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِ وَيُذْهِبَ عَنكُمْ رِجْزَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الأَقْدَامَ

"Alipokufunikeni kwa usingizi uwe ni uaminisho kutoka kwake, na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni ili kukusafisheni kwayo na kukuondoleeni uchafu wa Shet›ani, na kuzipa nguvu nyoyo zenu, na kuitia imara miguu yenu." (a-Anfal: 11)

Mtukufu Mtume ﷺ aliswali usiku mzima na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa maombi mbalimbali, kama inavyothibitishwa na Sayyidna Ali رضي الله عنه:

"Ninayakumbuka yote kwa uwazi kabisa kwamba usiku wa Badr sisi wote tulikuwa tumelala, isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali na kulia mpaka asubuhi." (Ibn Huzayma, II, 52)

Ilipofika wakati wa alfajiri, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliita kwa sauti: "Salat, enyi waja wa Mwenyezi Mungu." Baada ya kuswalisha swala ya alfajiri, aliwahamasisha Waumini kwa ajili ya *jihad*. (Ahmad, I, 117)

Kabla ya waabudu masanamu kuzipanga safu zao kwa ajili ya kupambana na Waislamu, Mtukufu Mtume ﷺ, akiwa na mshale mkononi mwake, alipita katika safu za jeshi la Waislamu na kumfanya kila mwanajeshi ajipange vizuri katika safu yake, na Kisha akawahesabu.Wakati akiendelea kukagua safu za Waislamu, Mtume

101. Tabari, *Tafsir*, IX, 256-261.

ﷺ alilisukuma kidogo tumbo la Sawad Ghaziyaa, ambaye alikuwa ametoka kidogo nje ya msitari, akamwambia arudi nyuma.

"Umeniumiza ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu", alisema Sawad. "Hakika Mwenyezi Mungu amekutuma kwa haki. Hivyo ninataka nipate haki yangu japo kidogo!"

Mtume wa Mwenyezi Mungu, bila wasiwasi zaidi aliinua kanzu yake na kulifunua tumbo lake. "Ewe Sawad, lakini huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu," Maswahaba walikuwa wakijaribu kumtuliza na kumzuia. Lakini Aswad hakuwasikiliza.

"Hakuna mtu aliye bora juu ya mtu mwingine linapokuja suala la haki na uadilifu", alijibu. Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia alizawazishe suala hilo. Hapo Sawad akainama na kulibusu tumbo la Mtukufu Mtume ﷺ.

"Kwa nini umefanya hivyo ewe Sawad?" aliuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tunakaribia kwenda vitani. Hivyo nilitaka muda wangu wa mwisho niwe pamoja nawe!" Mtukufu Mtume ﷺ akamuombea kheri. (Ibn Hisham, II, 266-267; Ibn Sad, II, 15-16)

Majeshi hayo mawili yalijipanga safu tayari kwa makabiliano katika uwanja wa Badr mnamo tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhan. Ilikuwa siku yenye joto kali. Mpaka wakati huo, Waarabu walikuwa wakipigana vita kwa sababu za kikabili, wakihamasishwa na hoja za kuwalinda ndugu na jamaa zao. Sasa ujamaa na ukabila ulikuwa umebadilishwa na mahala pake ikaja dini; moyowa kidini ulikuwa umeachana kabisa na mshikamano imara wa ujamaa wa jana, kiasi kwamba baba walijikuta wakiziinua panga zao dhidi ya watoto wao wenyewe, wajomba dhidi ya wapwa wao na ndugu kwa ndugu wakipambana. Siku hiyo, Abu Bakr رضي الله عنه alipambana na mwanaye, Abu

Ubaydah ibn Jarrah ﷺ akapambana na baba yake na Hamza ﷺ akapambana na kaka yake. Yalikuwa mandhari yenye kustaajabisha sana.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِئَتَيْنِ الْتَقَتَا فِئَةٌ تُقَاتِلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَأُخْرَى كَافِرَةٌ يَرَوْنَهُم مِّثْلَيْهِمْ رَأْيَ الْعَيْنِ وَاللَّهُ يُؤَيِّدُ بِنَصْرِهِ مَن يَشَاءُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُوْلِي الأَبْصَارِ

"Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu katika yale majeshi mawili yalipo pambana. Jeshi moja likipigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine kafiri likiwaona zaidi kuliko wao mara mbili, kwa kuona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu humuunga mkono amtakaye kwa nusura yake. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye macho." (al-i Imran: 13)

Baada ya kuwasili katika uwanja wa mapambano wakiwa wamejawa na jeuri na takabari, washirikina walipotelea ndani ya majivuno yao wenyewe kwa kujiona kuwa watu wasioweza kushindwa hata kidogo. Hali yao hiyo imeelezwa ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

وَلاَ تَكُونُواْ كَالَّذِينَ خَرَجُواْ مِن دِيَارِهِم بَطَرًا وَرِئَاء النَّاسِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ وَإِذْ زَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَالَهُمْ وَقَالَ لاَ غَالِبَ لَكُمُ الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنِّي جَارٌ لَّكُمْ فَلَمَّا تَرَاءتِ الْفِئَتَانِ نَكَصَ عَلَى عَقِبَيْهِ وَقَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِّنكُمْ إِنِّي أَرَى مَا لاَتَرَوْنَ إِنِّيَ أَخَافُ اللَّهَ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ

"Wala msiwe kama wale walio toka majumbani mwao kwa fakhari na kujionyesha kwa watu, na wakawazuilia watu Njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ameyazunguka yote wanayo yafanya. Na pale Shet›ani alipo wapambia vitendo vyao, na akawaambia: Hapana watu wa kukushindeni hii leo, na hali mimi ni mlinzi wenu. Yalipo onana majeshi mawili, akarudi nyuma, na akasema: Mimi si pamoja nanyi. Mimi naona msiyo yaona. Mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." (al-Anfal: 47-48)

Lakini majivuno yao hayo yakabadilika baada ya kukutana na mwamba wa Jeuri ya Mwenyezi Mungu:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُواْ يُنفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ لِيَصُدُّواْ عَن سَبِيلِ اللَّهِ فَسَيُنفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ وَالَّذِينَ كَفَرُواْ إِلَى جَهَنَّمَ يُحْشَرُونَ



"Hakika wale walio kufuru hutoa mali yao ili kuzuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watayatoa, kisha yatakuwa juu yao majuto, na kisha watashindwa. Na wale walio kufuru watakusanywa kwenye Jahannam." (al-anfal: 36)

Msaaada wa Malaika

Mtukufu Mtume ﷺ aliwatazama makafiri; idadi yao ilikuwa karibu watu elfu moja. Maswahaba wake, kwa upande mwingine, walikuwa mia tatu na kumi na tatu.[102] Aligeukia upande wa Kaabah akainua mikono yake juu na kaunza kumuomba Mola Wake kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu…Itimilize ahadi uliyonipa! Nipe ushindi! Mola Wangu…Iwapo umma huu wa Waislamu utashindwa leo, kuanzia hapa na kuendelea hakuna atakayebaki Ardhi akikuabudu!"

Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea kuomba n asana huku mikono yake akiwa ameinyanyua kuelekea mawinginu kiasi kwamba *ridaa* yake ikadondoka kutoka mabegani mwake. Abu Bakr رضي الله عنه alipoona hivyo akaenda karibu naye na kuirudisha *ridaa* mabegani kwa Mtukufu Mtume ﷺ akisema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu…hakika umemuomba Mola wako sana. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ataitimiza ahadi Yake kwako!"

102. Bara رضي الله عنه baada ya tukio hilo alisema: "Tulikuwa tukielezana kuwa idadi ya Waislamu walioshiriki katika vita vya Badr ilikuwa sawa na ile ya jeshi la Talut wakati wakivuka mto; ambao ni mia tatu na kumi na tatu." (Bukhari, Maghazi, 6; Tirmidhi, Siyar, 38/1598)

Nyoyo za waumini pia zilikuwa katika hali ya kuomba; na haikuchukua muda mrefu wakajiwa na neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa rehma:

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُم بِأَلْفٍ مِّنَ الْمَلآئِكَةِ مُرْدِفِينَ وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلاَّ بُشْرَى وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ قُلُوبُكُمْ وَمَا النَّصْرُ إِلاَّ مِنْ عِندِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

"Mlipo kuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye akakujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanao fuatana mfululizo. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara na ili nyoyo zenu zituwe. Na haupatikani ushindi ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, na Mwenye hikima." (al-Anfal: 9-10)

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنتُمْ أَذِلَّةٌ فَاتَّقُواْ اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَإِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَن يَكْفِيَكُمْ أَن يُمِدَّكُمْ رَبُّكُم بِثَلاَثَةِ آلاَفٍ مِّنَ الْمَلآئِكَةِ مُنزَلِينَبَلَى إِن تَصْبِرُواْ وَتَتَّقُواْ وَيَأْتُوكُم مِّن فَوْرِهِمْ هَذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُم بِخَمْسَةِ آلافٍ مِّنَ الْمَلآئِكَةِ مُسَوِّمِينَ

"Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru. Ulipo waambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walio teremshwa? Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni

kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu." (al-i Imran: 123-125)

Siku hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapa Waslamu msaada wa Malaika;[103] na kadiri ikhlasi yao ilivyoongezeka ndivyo idadi yao ilivyoongezeka na kufikia elfu moja, elfu tatu na hatimaye elfu tano.

Japokuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekwishatabiri mahali ambapo kila muabudu sanamu atadondokea kwa kuchinjwa na kujua tokea mwanzo, kwa fadhila na neema ya Mwenyezi Mungu, kuwa atapewa ushindi, bado aliendelea kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu mpaka alfajiri, akimsihi sana kiasi cha kukaribia kuiangamiza nafsi yake. Hali hii ni mojawapo ya ishara muhimu za utumwa wa mja kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu hategemei chochote kutoka kwetu, mbali na utumwa wetu Kwake. Hakuna njia madhubuti ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, zaidi ya kumuomba kwa unyenyekevu na kumsihi.

Siku ya Badr, Mtukufu Mtume ﷺ alisikika akisema:

"Jibril amewasili! Amezikamata hatamu za farasi wake akiwa na zana za vita (na amekuja kuwasaidia)!" (Bukhari, Maghazi, 11)

Huwaytib ibn Abduluzza anakiriki akisema:

"Nilikuwa pamoja na Makafiri siku ya Badr na nilishuhudia matukio mengi yenye kushangaza, na matukio yaliyonishangaza zaidi ni Malaika. Walikuwa wakiwaua askari wa Kiqurayshi, baina ya mawingi na ardhi, na kuwachukua mateka. Niliposhuhudia hayo nikasema, 'Mtu huyo (yaani Muhammad) lazima atakuwa chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu.' Lakini kwa muda mrefu sikumwambia yeyote kuhusu yale niliyoyaona." (Hakim, III, 562/6084)

103. Bukhari, Maghazi, 4, 6; Muslim, Jihad, 58.

Abu Dawud al-Mazini anahadithia yafuatayo:

"Siku ya Badr nilimfuata kafiri mmoja ili kumshambulia na kumuua. Kabla upanga wangu haujampata, niliona kichwa chale kikigaagaa chini. Nikatambua kuwa mtu mwingine, yaani malaika, amemshambulia!" (Ahmad, V, 450)

Kwa mujibu wa ripoti ya Anas ﷺ, pindi makafiri walipoanza kukaribia, Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

"Jiandaeni kuingia katika Pepo ambayo upana wake ni mkubwa sawa na umbali uliopo baina ya mbingu na ardhi!" Umayr ibn Humam ﷺ, kutoka katika Ansar, akasema:

"…Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Pepo ambayo upana wake ni mkubwa sawa na umbali uliopo baina ya mbingu na ardhi?"

"Ndiyo", akajibu Mtume wa rehma ﷺ.

"Maajabu yaliyoje", alisema Umayr.

"Kitu gani kimekufanya useme hivyo?" akauliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu", alisema Umary, "Nilisema hivyo kwa tamaa yangu ya kuwa miongoni mwa wakazi wa Peponi; si vingine!"

"Dhahiri kabisa, wewe ni mmoja wao", hapo Mtukufu Mtume ﷺ alimhakikishia.

Muda mfupi baada ya maneno hayo ya Mtukufu Mtume ﷺ, Umayr alichukua vipande kadhaa vya tende kutoka kwenye mkoba wake na kuanza kula. Hata hivyop, wakati akiendelea kula akatamka maneno yafuatayo:

"Kama nitaishi muda mrefu mpaka kumaliza tende hizi, basi huo utakuwa muda mrefu". Baada ya kusema hivyo akazitupilia mbali tende zake na Kisha akaelekea kwenye uwanja wa mapambano. Alipigana kishujaa mpaka alipouawa kishahidi. (Muslim, Imara, 145; Ahmad, III, 137)

Vita vya Badr vilianza kwa *mubaraza*, yaani mapambano ya mtu mmoja kupambana na mtu mwingine kutoka upande wa pili. Mashujaa watatu walioteuliwa kutoka katika safu za Waislamu, yaani Hamza, Ali na Ubayda ﷺ hawakuwa na kazi ngumu dhidi ya maadui zao. Hata hivyo, Ubayda ﷺ alirudi akiwa amejeruhiwa vibaya mguuni, akafa shahidi muda mfupi baadaye, baada ya kuyasikia maneno matamu ya Mtukufu Mtume ﷺ:

"Umefanikiwa!" (Waqidi, I, 69-70)

Baada ya tukio hilo, majeshi ya pande zote mbili yakurubiana. Mtukufu Mtume ﷺ hakuwaruhusu Waislamu kuanzisha shambulizi la moja kwa moja, kwa sababu kulikuwa na watu wengi miongoni mwa Maqurayshi ambao walikuwa wakijaribu kupigana, baada ya kujua kwamba msafara wa biashara haukuwa tena katika hatari; na kwa kuwa Waislamu walikuwa wakichukua muda kushambulia, maquraysh nao walizidi kusita kupigana, na hivyo kudhoofisha uamuzi na hamasa ya Makurayshi. Mbali na hilo, tukio la wanajeshi wao watatu kuuawa mbele ya mashujaa wa Kiislamu kuliingiza hofu ndani ya nyoyo zao. Hata hivyo, ukimya wao wa kusita kupigana ulivunjwa na maneno ya uchochezi yaliyotolewa na Abu Jahl:

"Msipumbazwe na vifo vya watu wachache…Songeni mbele!" (Waqidi, I,71)

Kutokana na uchechezo huo, washirikina wakaanzisha mashambulizi ya jumla. Sauti zilizokuwa zikihanikiza kwa *Allahu Akbar* kutoka katika safu za Waislamu ziliendelea kuingiza hofu

ndani ya safu za Makafiri, huku zikijaza imani ndani ya nyoyo za Waislamu.

Hatimaye muda ulifika na Mtukufu Mtume ﷺ akawaamuru Waislamu kujibu mashambulizi. Pande zote mbili zikakutanisha panga. Vita vilianza kwa ukali; hapo ukatili wa vita ukaongezeka.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akipita ndani ya safu za Waislamu akiomba msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ili kuwahamasisha maswahaba, mara kwa mara alikuwa akisoma:

سَيُهْزَمُ الْجَمْعُ وَيُوَلُّونَ الدُّبُرَ

"Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma." (al-Qamar: 45), na wakati huo huo akitangaza:

"Kwa hakika, yule atakayestahmili dhidi ya adui na kufa shahidi, Mwenyezi Mungu Mtukufu atamuingiza Peponi. Pepo ya *Firdaws* inawasubiri wale watakaokufa kishahidi leo.Songa mbele na mshambulie!" (Ibn Hisham, II, 267-268)

Kisha alimgeukia Abu Bakr ؓ, ambaye alikuwa pembeni yake na kusema:

"Habari njema…! Jibril na Malaika wengine wamekuja kutusaidia!"

Wakati fulani, alichukua changarawe na kuzitupa upande wa waabudu - sanamu akisema "nyuso zao ziingie giza."[104] Wakati huo huo, upepo mkali ukaanza kuvuma sana kuelekea upande wa maadui, ukatimua vumbi kubwa kiasi kwamba walikuwa wakionana kwa taabu sana.

104. Ibn Hisham, II, 267.

Simba wa Badr

Ali ﷺ anaeleza kuwa:

"Siku ya Badr tulikuwa tukikimbilia kujikinga kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Ndiye aliyekuwa karibu zaidi na adui na ndiye aliyekuwa jasiri na mwenye ushujaa zaidi kuliko watu wote." (Ahmad, I, 86)

Kuhusu ujasiri wa Mtukufu Mtume ﷺ, Baraa ﷺ anatoa maelezo kama hayo akisema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, pindi vita vilipokuwa vikipamba moto, tulikuwa tukienda kujikinga kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Aliyekuwa akimfuatia kwa ushujaa miongoni mwetu ni Yule aliyekuwa na ujasiri wa kusimama kwenye msitari mmoja na Mtume ﷺ." (Muslim, Jihad, 79)

Wakati wote wa vita, Maswahaba walionyesha kiwango cha hali ya juu kabisa cha ushujaa na kujitoa mhanga. 'Simba wa Mwenyezi Mungu', shujaa asiyekuwa na hofu, Hamza ﷺ alioonyesha mfano wa hali ya juu wa ujasiri. Baadaye Umayya ibn Khalaf alimuuliza Swahaba Abdurrahman ibn Awf kuwa ni nani "mtu yule aliyekuwa amevaa ubawa wa mbuni kifuani mwake kama alama yake wakati wa vita."

"Alikuwa Hamza", alijibu Abdurrahman; "Hamza ibn Abdul-Muttalib."

"Lolote lililotupata siku ile", akasema Umayya, "ilikuwa ni kwa sababu yake." (Ibn Hisham, II, 272)

Katika kufuata nyayo za ami yake Hamza ؓ, Sayyidna Ali ؓ naye pia alionesha ujasiri mkubwa, akawaangusha washirikina mmoja baada ya mwingine.[105]

Akikariri tenzi za *rajaz*[106] akiwa juu ya farasi, Abu Jahl alikuwa akidai na kujifanya kaidi dhidi ya jaribio lolote la kulipiza kisasi dhidi yake, katika vita vyovyote, huku akijigamba kuwa "nilizaliwa kwa ajili ya siku kama hizi!" (Ibn Hisham, II, 275)

Abdurrahman ibn Awf ؓ anasimulia:

"Siku ya Vita vya Badr, nilitazama upande wangu wa kulia, Kisha upande wa kushoto, na kuona kuwa nilikuwa katikati ya vijana wadodgo wawili wa Kiansari hali ya kuwa nilipendelea niwe katikati ya watu wazima wenye nguvu na madhubuti. Mmojawapo akaniuliza taratibu, bila mwenzake kusikia, iwapo ninamjua Abu Jahl.

'Ndiyo, ninamjua' nilijibu. 'Kwani ana nini?'

'Nilivyomsikia ni kwamba alikuwa akisema mambo mabaya kabisa dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye roho yangu iko mikononi Mwake, nikimuona sitomuacha mpaka mmoja wetu awe amekufa!'

Nilistaajabishwa sana na maneno yake. Kijana mwingine akatamka maneno hayo hayo. Ghafla nikajisikia kuridhika sana

105. Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, IV, 97.

106. Rajaz ni jina la utenzi katia arudhi ya lugha ya Kiarabu. Kilugha neno hilo lina maana ya 'mtetemeko', na sauti yake inashabihiana na na rajaza, au ngamia jike, ambaye hutoa sauti maridadi anapoinuka. Vilevile neno rajaz lina maana ya 'ngurumo', na hivyo kuwa na uwezekano wa neno hilo kutokana na uimbaji unaofanana na ngurumo wakati wa kuimba nyimbo za vita. Maana hii inaonekana kuwa karibu zaidi na uhalisia. (Cehande, A.-Çetin, N. Milli Eğitim Bakanlığı, İslam Ansiklopedisi, "recez" entry, IX, 657)

kuwa bega kwa began a vijana hawa. Baada ya vita kuanza, nilimuona Abu Jahl akizungukazunguka kwenye medani ya vita akiwa juu ya farasi wake. Niliwageukia vijana wale na kuwaambia: 'Yule pale mtu mnayemtafuta!'

Waliposikia hivyo, walizichomoa panga zao na kukimbilia kule alikokuwa Abu Jahl. Baada ya purukushani ya muda mfupi, Abu Jahl aliishia kuchinjwa. Baadaye nilikuja kugundua kuwa vijana hao ni Muadh ibn Afra na Muadh ibn Amr." (Bukhari, Maghazi, 10; Muslim, Jihad, 42)

Muadh ibn Amr ﵁ anaelezea tena tukio hilo:

"Nilipomshambulia Abu Jahl kwa upanga wangu na kumjeruhi sana, mwanaye Iqrimah alinishambulia, lakini akaujeruhi vibaya mkono wangu ambao ulibaki ukiwa unaning'inia kwenye ngozi tu! Kwa kipindi chote cha siku nzima, niliendelea kupambana na huku mkono wangu ukiwa unaning'inia nyuma yangu lakini ikaniwea vigumu sana kupambana. Nilipoona kuwa unaninyima raha, nilikanyaga kwa mguu wangu na kuuondosha, ingawa niliumia sana!" (Ibn Hisham, II, 275-276)

Baada ya vita, Mtukufu Mtume ﷺ aliulizia mahali alipo Abu Jahl na kumtuma Abdullah ibn Masud ﵁ kwenda kumtafuta. Alimkuta Abu Jahl akiwa amelala ardhini. Majadiliano yaliyofuata yamehadithiwa na Abdullah ibn Masud mwenyewe:

'Ewe adui wa Mwenyezi Mungu…Hakika Mwenyezi Mungu amekufedhehesha na kukudhalilisha, je hajakufanyia yote hayo?' Nilimuuliza wakati wakiwa amelala mbele yangu.

'Amenifedhehesha na kunidhalilisha kwa kitu gani? Nionyeshe mtu mwingine aliye bora kuliko mimi katika watu wenu wote aliyeuliwa leo!' alijibu akiwa bado hajaacha kiburi chake. Kisha nikimuonesha kuwa nilikuwa nimeuweka mguu wangu juu ya kifua

chake, nilimwambia: 'Umefikia kilele kilichokushinda kupanda, ewe mchunga kondoo!' Baada ya kukaa kimya kidogo, aliniuliza: 'sawa, niambie…Nani kashinda leo?'

'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake…!' Nilimwambia. Kisha, bila mjadala zaidi, nilihitimisha utakabari wake kwa upanga wake mwenyewe. Baadaye nilirudi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia kuwa nilimuua Abu Jahl. Alishukuru na kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu na kusema:

'Alikuwa Fir'auni wa *ummah* huu!' (Bukhari, Maghazi, 12; Ahmad,I, 444; Ibn Hisham, II, 277; Waqidi, I, 89-90)

Mtoto wa kiume wa Ummu Haritha aliuawa kishahidi katika vita vya Badr kutokana na mishale iliyokuwa ikitupwa bila utaratibu kutoka katika safu za maadui. Mama huyo alikuja kwa Mtume wa Mwen yezi Mungu ﷺ na kusema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kama mwanangu Haritha yuko peponi nitaendelea kufanya subira na kutarajia malipo yake; lakini kama hayuko peponi, nitaendelea kumlilia!"

Lakini akafarijiwa na maneno maridhawa kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ:

"Ewe Ummu Haritha, Peponi kuna daraja mbalimbali, na mwanao amepata daraja ya juu kabisa, *Firdaws'ul-A'la*." (Bukhari, Jihad, 14; Ahmad, III, 272)

Wakati akirejea, tabasamu lilikuwa likichanua usoni mwa Ummu Haritha huku akijisemea:

"Uzuri ulioje wa malipo ya Haritha!" (Ibn Athir, Usd'ul-Ghaba, I, 426)

Kwa kuwa vilikuwa vita vikali vya kufa au kupona ambavyo vingeamua hatima ya Uislamu, Maswahaba waliopata bahati ya kushiriki katika vita hivi vikubwa vya kwanza, yaani vita vya Badr,

wamepata heshima kubwa ya kufadhilishwa juu ya Waislamu wengine wote. Vivyo hivyo, Malaika walioletwa na Mwenyezi Mungu kuja kuwasaidia Waislamu katika mawimbi hayo mazito ya imani iliyohamasishwa na shauku kubwa, wamepata heshima ya kuwa malaika bora zaidi juu yaw engine, kama inavyothibitishwa na mazungumzo baina ya Malaika Jibril ﷺ na Mtukufu Mtume ﷺ.

Alipoulizwa na Jibril ﷺ kuhusu namna anavyowachukulia wale walioshiriki katika vita vya Badr, Mtukufu Mtume ﷺ alijibu kwa kusema: "Tunawachukulia kuwa Waislamu wenye ubora juu ya Waislamu wengine wote!" Hapo Jibril ﷺ akajibu kwa namna hiyo hiyo:

"Nasi tunawachukulia Malaika walioshiriki katika vita vya Badr kuwa ndio Malaika bora kabisa zaidi ya Malaika wote!" (Bukhari, maghazi, 11)

Vita vilimalizika karibu majira ya mchana kwa Waislamu kupata ushindi mkubwa na wa wazi. Waislamu kumi na nne waliuawa kishahidi, huku kwa upande wa washirikina watu sabini wakiuawa, akiwemo Abu Jahl ambaye aliuawa katika uwanja wa mapambano. Licha ya washirikina kuonyesha nyuso za ujasiri kabla ya kuingia kwenye medani ya mapambano, hawakunywa pombe ya ushindi kama walivyokuwa wakitarajia, badala yake wakanywa sumu ya kifo kibaya. Badala ya kutoa burudani ya nyimbo, vijakazi wao wakazililia maiti zao. Badala ya kuyajaza matumbo yao kwa ngawira walizokuwa wakiziota kabla ya vita, wakaishia kuyajaza kwa uchafu wa Moto wa Jahannamu.

Akiwa amevaa ngao/deraya yake, Mtukufu Mtume ﷺ alitoka mahali alipokuwa amekaa kivulini huku akisoma aya ifuatayo:

سَيُهْزَمُ الْجَمْعُ وَيُوَلُّونَ الدُّبُرَ

"Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma." (al-Qamar: 45), aya ambayo Omar ﵁ anasema:

"Aya hiyo ilipoteremka – katika mji wa Makka -, nilijiuliza ni wingi gani huo utakaoshindwa na kusukumwa nyuma. Lakini siku ya badr nilipomsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiisoma, nikabaini kuwa Maqurayshi ndio kundi lililoelezewa kuwa litashindwa. Kwangu mimi, maana ya aya hiyo ilibainika siku hiyo." (Ibn Sad, II, 25; Ibn Kathir, al-Bidaya, III, 312)

Katika kutafsiri na kusherehesha aya isemayo:

"Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo?" (Ibrahim: 28), Ibn Abbas ﵁ anasema:

"Wallahi, watu waliokusudiwa katika aya hiyo ni Washirikina wa Kiqurayshi. Neema iliyobadilishwa kwa kufuru ni Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Nyumba ya maangamizo ambayo waliwapeleka watu wao ni moto waliowachimbia watu wao katika vita vya Badr." (Bukhari, Maghazi, 8; tafsir, 14/3)

Vita vya Badr, ambavyo vilifikia kilele kwa Uislamu na *iman* kupata ushindi, vimejaa matukio makubwa yanayotoa ushuhuda wa namna Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyowasaidia waja Wake wema na wenye *ikhlas* na usafi wa moyo.

Kufuatia ushindi huo mkubwa, ili kuwazuia Waislamu wasikumbwe na hali ya kujiona (*ujub*), Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ifuatayo:

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ رَمَى وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلاء حَسَناً إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

"Hamkuwauwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye wauwa. Na wewe hukutupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye tupa, ili awajaribu Waumini majaribio mema yatokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Msikizi na Mjuzi." (Al-Anfal: 17)

Nguvu na uwezo unaoonyeshwa na mwanadamu vimedhibiwa ndani ya nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu (*taqdir*), na hivyo ndiyo maana ikaelezwa kuwa 'hakuna mwenye uwezo tofauti na Mwenyezi Mungu Mtukufu'. Kile ambacho viumbe wanacho – viumbeambao hawakuwepo hapo tangu na tangu bali wamekuwepo kwa fadhila na rehma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu – kinatokana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo utashi mkuu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu unawazunguka viumbe na hata matukio yote. Hii ina maana kwamba asili ya utashi na uwezo iko kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini kwa kuwa wanadamu wameletwa hapa duniani kama sehemu ya mtihani, wamejaaliwa utashi na mtihani wa kumpima kwa mema na mabaya. Ufanikishaji wa mtihani huu kupitia matendo mbalimbali umeachwa kwenye utashi wao.

Safari ya kurudi kutoka Badr

Mtukufu Mtume ﷺ alibaki katika viunga vya jirani na medani ya vita kwa siku tatu zaidi baada ya kupata ushindi. Baada ya siku tatu kupita, Mtukufu Mtume ﷺ aliamuru aletewe ngamia wake. Ngamia akaamriwa kutembea na hapo Mtukufu Mtume ﷺ naye akaanza kutembea. Maswahaba wakafuata wakidhani kuwa 'Mtume wa Mwenyezi Mungu kuna kitu atakuwa amekikumbuka'. Hatimaye alisimama jirani na kisima kilichokauka ambacho ndani yake

maiti za washirikina zilikuwa zimetupwa na kisha akamuita kila mmoja kwa jina lake:

"Ewe Abu Jahl! Ewe Umayya ibn Khalaf! Ewe Utbah ibn Rabia! Ewe Shaybah ibn Rabia!" Kisha akaendelea kwa kusema:

"Je isingekuwa bora kwenu kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake? Hakika sisi tumepata yale tuliyoahidiwa na Mola wetu… je nanyi mmetimiziwa yale mliyoahidiwa na Mola wenu?"

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, unazungumza na maiti zisizokuwa na uhai?" aliuliza Omar رضي الله عنه. "Watawezaje kukusikia na kukujibu hali ya kuwa wamekuwa mizoga?"

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi ya Muhammad imo mikononi Mwake, wananisikia vizuri zaidi kuliko nyinyi… isipokuwa hawawezi kunijibu!" (Bukhari, Maghazi, 8; Muslim, Jannat, 77)

Baada ya vita kufikia kikomo, Jibril عليه السلام alikuja mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema: "Ewe Muhammad, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alinituma kwako na kuniamuru nisikuache mpaka uwe umeridhishwa na msaada wetu. Je umeridhika?"

"Ndiyo, nimeridhika", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ, na hapo Jibril عليه السلام akaondoka. (Waqidi, I, 113; Ibn Sad, II, 26-27)

Wakati upepo mwanana wa ushindi ukipuliza kwa mfululizo katika mji wa Madina, ushindi huo mkubwa ulipeleka vilio na huzuni kubwa katika mji wa Makka kiasi kwamba Abu Lahab alifariki kutokana na huzuni na uchungu mkubwa.[107] Hivyo ahadi ya Mwenyezi Mungu ikatimia.

107. Ibn Hisham, II, 289.

Hata hivyo, furaha ya Waislamu ilidumu kwa muda mfupi kutokana na kifo cha Ruqayya ﵂, binti wa Mtukufu Mtume ﷺ aliyefariki muda mfupi baada ya vita hivyo.

Muamala kwa Mateka wa vita

Aliporejea Madina baada ya kukaa kwa muda wa siku tatu katika eneo la Badr, Mtukufu Mtume ﷺ alijadiliana na maswahaba, hasa Abu Bakr, Omar na Ali ﵁, juu ya namna bora inayofaa kushughulikia suala la mateka wa vita. Abu Bakr ﵁ ndiye aliyekuwa wa kwanza kutoa maoni yake.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hawa ni ndugu na ni jamaa zetu. Hivyo ninapendekeza tuchukue fidia kutoka kwao na kisha tuwaachie huru. Fidia tutakayochukua kutoka kwao itasaidia kuongeza nguvu katika mapambano yetu dhidi ya makafiri. Na Mwenyezi Mungu akipenda, huwenda nao wakaongoka na kuungana nasi."

"Ni yepi maoni yako ewe ibn Khattab?" Mtukufu Mtume ﷺ alimuuliza Omar ﵁.

"Hakuna jinsi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu… maoni yangu sio kama ya Abu Bakr. Nakuomba uturuhusu tukate vichwa vyao. Niruhusu nifanye kazi hiyo na mimi mwenyewe nitavikata vichwa vya ndugu zangu. Mruhusu Ali akate kichwa cha kaka yake Aqil na Hamza ammalize kaka yake Abbas…mpaka pale Mwenyezi MunguMtukufu atakapoithihirisha nuru yake kiasi kwamba hakutokuwa na alama ya udhaifu na unyonge ndani ya nyoyo zetu kwa washirikina! Hawa mateka ni viongozi wa ushirikina na dhulma!"

Kwa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amebeba matumaini ya kwamba wataongoka na kutaraji kuwa ndani mwao vitatoka vizazi ambavyo vitamuabudu Mwenyezi Mungu pekee, aliegemea upande

wa maoni ya Abu Bakr ﷺ. (Muslim, Jihad, 58; Tirmidhi, Siyar, 18/1567; Ahmad, I, 30-31, 383-384; Waqidi, I, 107; Ibn Saad, II, 22)

Hivyo basi baada ya majadiliano hayo, mateka waliachiwa huru kwa kutoa kiasi fulani cha fidia au kikomboleo. Wale ambao hawakuweza kulipa waliachiwa huru waondoke bila kulipa chochote. Lakini katika watu hao, yule ambaye alikuwa na uwezo wa kuandika na kusoma, alitakiwa awafundishe maarifa hayo watoto kumi wa mjini Madina. Kwa kufanya hivyo walihesabiwa kuwa wametoa fidia. Zayd ibn Thabit, mwaandishi wa baadaye wa Qur'an Tukufu, ambaye baadaye alipewa kazi ya kukusanya Qur'an, alikuwa miongoni mwa watoto waliojifunza kusoma na kuandika kutoka kwa mateka hao. (Ahmad, I, 247; Waqidi, I, 129; Ibn Sad, II, 22)

Kuhusu mateka na fidia iliyochukuliwa kutoka kwao, Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema:

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَكُونَ لَهُ أَسْرَى حَتَّى يُثْخِنَ فِي الأَرْضِ تُرِيدُونَ عَرَضَ الدُّنْيَا وَاللَّهُ يُرِيدُ الآخِرَةَ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ لَّوْلاَ كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا أَخَذْتُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ فَكُلُواْ مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلاَلاً طَيِّبًا وَاتَّقُواْ اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Haimfalii Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda baraabara katika nchi. Mnataka vitu vya dunia, na Mwenyezi Mungu anataka Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hikima. Lau isingeli kuwa hukumu iliyo kwisha tangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingeli kupateni adhabu kubwa kwa vile mlivyo chukua. Basi kuleni katika mlivyo teka, ni halali na

vizuri, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu." (al-Anfal: 67-69)

Omar ﷺ anasimulia:

"Nilipokwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati wa asubuhi, nilimkuta akiwa amekaa na Abu Bakr ﷺ. Wote wawili walikuwa wakilia. 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, jambo gani linalokuliza wewe na sahibu yako?' nilimuuliza. 'Niambie ili niungane nanyi kama nikijua kitu gani kinachowaliza au kama sivyo angalau nijaribu kuungana nanyi!'

'Nitafanya nini kuhusu fidia iliyochukuliwa na hawa wenzako kutoka kwa hawa mateka? Nimeonyeshwa kuwa adhabu inayowangoja ipo karibu zaidi kuliko mti ule pale', alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. (Ahmad, I, 31; Muslim, Jihad, 58)

Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakufurahishwa na suala la kuwashikilia mateka na kisha kuwachia huru kwa malipo ya fidia, ikizingatiwa kuwa maadui walikuwa hawajashughulikiwa vilivyo, na Uislamu ulikuwa haujapata nguvu ulizotakiwa kuwa nazo na kabla *fitnah* (uovu) haujafutiliwa mbali. Hivyo akatoa onyo dhidi ya Waislamu. Kuchukua malipo ya fidia huongeza mzigo zaidi wa tamaa za kidunia, ilhali Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka Waislamu waizingatie zaidi Akhera. Kuchukua Mateka kutoka kwa maadui wa Haki kabla watu hao hawajazidiwa kungeiweka hatarini furaha ya Waislamu.

Kwa kuwa hakuna dhima katika makosa yatokanayo na maoni ya kisheria (ijtihad), kutokana na dhamana ya kwamba walioshiriki katika vita vya Badr wasingehusishwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu, kuliimarisha ukweli kwamba hakuna adhabu kwa tendo ambalo halijakatazwa wazi wazi kabla ya kulitenda, na hivyo Mwe-

nyezi Mungu Mtukufu aliwasamehe Waislamu na kutangaza kuwa malipo ya fidia waliyokuwa wameyachukua yalikuwa halali kwao.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamuru kuwa mateka na wafungwa waamiliwe kwa heshima na wema.[108] Vivyo hivyo Mtume wa Rehma ﷺ naye pia ana hadith nyingi kuhusu suala hilo. Kwa kweli, maneno yake ya mwisho aliyoyatamka kabla ya kufariki kwako ni pamoja na:

"Shikamaneni na swala na hasa swala...na mcheni Mwenyezi Mungu kwa wale walio chini ya uangalizi wenu." (Abu Dawud, Adab, 123-124/5156; Ibn Maja, Wasaya, 1)

Marur ibn Suwayd anafafanua:

"Siku moja nilimuona Abu Dharr ؓ akiwa amevaa mavazi ya thamani. Mtumwa wake pia alikuwa amevaa mavazi kama hayo. Nilimuuliza Abu Dharr sababu ya jambo hilo. Katika kunijibu alinambia kuwa siku moja katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ - yeye Abu Dhar – aliwahi kumtukana mama wa mtu na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamlaumu na kumwambia: 'Yaonekana bado umebeba athari za desturi za kijahiliya. Hakika wao ni watumishi wenu na wakati huo huo ni ndugu zenu. Mwenyezi Mungu amewaweka chini ya uangalizi wenu. Iwapo utakuwa na ndugu aliye chini ya uangalaizi wako, mlishe kile unachokula na mvishe kile unachovaa wewe mwenyewe. Usimpe kazi inayozidi uwezo wake; na iwapo utampa kazi, basi msaidie!" (Bukhari, Itq, 15; Muslim, Ayman, 40)

108. Tazama, an-Nisâ, 36.

Ushahidi wenye msisimko unatolewa na Abu Aziz, nduguye Musab ibn Umayr ﷺ:

"Mimi pia nilikuwa miongoni mwa waliochukuliwa mateka baada ya Vita vya Badr na nikakabidhiwa kwa kundi moja la *Ansar*. Amri ya Mtume ﷺ ya kutaka mateka watendewe wema ilitolewa kwa kila mtu lakini jukumu lililobebwa na *Ansar* ilikuwa kubwa zaidi kuliko kawaida. Usiku na mchana walikuwa wakitoa mgao wao wa mkate na kunipa mimi, huku wao wakila tende tu. Nilikuwa nikiwarudishia mkate huo kutokana na kutojisikia vizuri, lakini walikuwa wakinirejeshea bila mkate huo kuguswa na yeyote." (Haythami, VI, 86; Ibn Hisham, II, 288)

Ukarimu huo uliooneshwa na Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba wake katika zama ambazo dhulma na uonevu vilikuwa vimeshtadi, unaonesha ruwaza ya mfano kwa wanadamu wote mpaka Saa ya Mwisho. Katika kuamiliana na watu kwa uzuri na wema wa hali ya juu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiufanya mwenendo wake (*hal*) uzungumze katika kuwalingania kwenye njia ya Kweli; ni baada tu ya kuzipa uvuguvugu nyoyo zao, ndipo alipokuwa akianza kufafanua Uislamu kwa maneno. Kutokana na kuvutwa na muamala wake wa huruma na upole, mateka wengi wa Badr waliishia kuukubali Uislamu.

Sio tu kwamba Uislamu hauitetei taasisi ya utumwa[109], bali pia hauihamasishi. Uislamu uliliona suala la utumwa kuwa ni tatizo lililokita mizizi katika jamii; na kwa kuzingatia kuwa kuuliondosha kwa ghafla kungesababisha msukosuko katika mizania ya kijamii, hivyo haukufutwa kwa mara moja. Bali, ili kuzuia matumizi mabaya na unyonyaji unaoweza kutokea, Uislamu ulidhibiti utumwa kwa

109. Hapa uchukuaji mateka na utumwa vimetathiminiwa kwa pamoja, kwa sababu hakuna sababu nyingine ambayo ni chanzo cha utumwa zaidi ya ukamataji mateka; watumwa ni wale ambao wamekamatwa mateka katika vita.

kuweka sheria na kanuni kadhaa, ambapo sheria ya utumwa iliendelea kukamilishwa hatua kwa hatua kwa namna iliyokuwa bora.

Kwa kuwa vita ni jambo halisi lililopo miongoni mwa mataifa mbalimbali ambalo linaonekana kuwa halitoondoka mpaka siku ya mwisho, haja ya kuwepo sheria zinazowalinda wale wanaopoteza uhuru wao kutokana na tatizo hilo la vita itaendelea kuwepo.Kwa hiyo, badala ya kuukomesha, jambo ambalo lingekuwa limepuuza kabisa ukweli uliotajwa hapo juu, Uislamu uliona kuwa faida kubwa ipo katika kuweka kanuni za kinga na kusimamia sheria ya utumwa.

Kupitia kanuni na sheria mbalimbali inazozitekeleza, dini ya Uislamu huwaleta karibu mtumwa na bwana wake, na wakati huo huo kutafuta njia ya kumwacha huru wa kwanza. Kwa mfano, iwapo mtu atamuua kwa bahati mbaya mtu mwingine, basi Uislamu umeweka sheria ya fidia ambayo kwanza ni kumuacha huru mtumwa na kisha kutoa malipo ya pesa, ambayo itathaminishwa kwa fedha au ngamia, kwa kiwango kitakachoafikiwa baada ya majadiliano na familia ya muathirika. Adhabu ya kosa lililofanywa wakati wa Hijja, kwanza kabisa ni kumuacha huru mtumwa; na adhabu hiyo hiyo hutumika kwa mtu aliyeshindwa kutekeleza nadhiri, mwenye kufanya *zihar*[110] na hata kwa mwenye kula mchana wa mwezi wa Ramadhan. Katika kuusifu na kuuelezea ukubwa wa matendo fulani, ni kawaida kuona matendo hayo yakilinganishwa na 'kuucha huru kiwango kadhaa wa kadhaa cha watumwa', jambo linaloweka msisitizo juu ya ubora katika kufungua njia ya kuwaacha huru watu wengine. Kwa upande mwingine wa sarafu, jambo la haramu la kuwatia utumwani watu wengine linachukuliwa kuwa ni

110. *Zihar* ni desturi iliyokuwepo wakati huo miongoni mwa Waarabu ya kuwafafanisha wake zao na mama zao na hivyo kuhesabu kuwa sio sahihi tena kuendelea kuwa na uhusiano wa ndoa na wanawake hao. Uislamu uliharamisha desturi hii na kuweka adhabu (*kaffarah*) ya fidia kwa wale watakaofanya hivyo.

miongoni mwa madhambi makubwa kabisa. Uislamu unatoa amri ya wazi kabisa juu ya kutendea wema wa hali ya juu wale ambao hapo awali walikuwa wametiwa utumwani kwa namna moja ama nyingine.

Daima Uislamu unamuusia bwana kumlisha mtumwa chakula nachokula yeye mwenye, kumpa mavazi ambayo yeye mwenyewe anaweza kuyavaa, kutompa mzigo wa kazi za ziada hali ya kuwa akiwa katika swaumu na kuyatazama mahitaji yake. Daima kumuacha huru mtumwa inachukuliwa kuwa ni njia bora ya uokovu kwa Muumini. Uislamu umetambulisha sheria kadhaa kwa ajili ya watumwa ambapo ukali wa sheria hizo unapendekeza kuwa ni bora sana kuachana na suala la kuwanunua watumwa, kwa sababu sheria hizo zinamfanya mhusika wa baishara hiyo asionekene tofauti na mtumwa kwa kuzitekeleza.

Hivyo, Uislamu unafunga milango ya utumwa kwa kadiri mazingira yanavyoruhusu, na mahali pake ukafungua milango ya kuwakomboa watumwa na kuwaacha huru, kwa kuhamasisha kuwaacha huru watumwa katika kila fursa inayopatikana.

Mtukufu Mtume ﷺ alimpendekezea ami yake Abbas, miongoni mwa mateka wengine wa vita vya Badr kwa kumwambia:

"Ewe ami yangu, wewe ni mtu tajiri. Lipa fdia kwa ajili yako mwenyewe, mpwa wako Aqil, Nawfal ibn Harith na kwa ajili pia ya rafiki yako Utbah ibn Amr."

"Mimi ni Muislamu, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", alijibu Abbas. "Maquraysh wamenilazimisha kuja!"

"Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuaye undani wa hilo. Kama uliyosema ni ya kweli, basi ni hakika kwamba Mwenyezi Mungu atakulipa kwa hayo. Lakini kwa kadiri hali ilivyo, ulishika silaha kupambana nasi na hivyo unatakiwa kulipa fidia", alisema Mtukufu Mtume ﷺ na kisha akachukua dirhma 800 alizokuwa nazo Abbas, kama sehemu ya ngawira za vita.

"Angalau ifanye hiyo kuwa fidia, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", alisema Abbas katika hali ya kusihi.

"Hapana", alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. "Hizo ni ngawira ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia!"

"Inaonekana umeshikilia kulazimisha kuwa ombaomba katika siku zangu zilizobaki", alilalama Abbas kwa masikitiko.

"Vipi kuhusu dhahabu ulizomuachia mkeo Ummul-Fadhl?" alisema Mtume wa Rehma ﷺ.

"Dhabau gani unazozizungumzia?"

"Ninazungumzia dhahabu ulizomkabidhi mkeo Ummul-Fadhl wakati ukiondoka Makka, mkiwa sehemu ambayo hakuna aliyekuwa akiwaona isipokuwa Mwenyezi Mungu, ukamwambia: 'Sijui kitakachonitokea safari hii...nikitokewa na jambo lolote, basi chukua kiasi hiki cha dhahabu kwa ajili yako, na kiasi hiki umpe Ubaydullah, kiasi hiki umpe Fadhl, kiasi hiki umpe Qusam na kiasi hiki umpe Abdullah'".

Akiwa ameshtushwa na maneno hayo, Abbas hakuwa na lolote zaidi ya kusema:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu aliyekutuma kuwa Nabii, hakuna mtu mwingi aliyelijua jambo hilo isipokuwa mimi na Ummul-Fadh. Hakuna shaka yoyote kwambe wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu!" (Ahmad, I, 353; Ibn Sad, IV, 13-15)

Miongoni mwa mateka wa vita vya Badr alikuwemo pia Abul-As ibn Rabi, mume wa Zaynab ﵂ na mkwe wa Mtukufu Mtume ﷺ. Abul-As alikuwa mfanyabiashara mkubwa katika mji wa Makka. Mama yeke, Hala bint Khuwaylid alikuwa dada wa bibi Khadija ﵂, mke wa Mtume ﷺ, na hivyo Abul-As alionekana zaidi kuwa mtoto badala ya mpwa.

Wakiwa katika kilele cha juu kabisa cha uadui, washirikina wa Kiquraysh walikuwa wakiwachochea wakwe wa Mtukufu Mtume ﷺ kwa kuwaambia: "...wapeni talaka mabinti wa Muhammad muwarudishe kwake, ili aingiwe na wasiwasi!" Abul-As alilengwa na uchochezi kama huo huku washirikina hao wakimuahidi kuwa watamuozesha mwanamke yeyote anayemtaka iwapo atatekeleza jambo hilo la talaka. Lakini Abul-As alikataa vikali pendekezo lao, akisisitiza kuwa ataendelea kuwa upande wa mke wake bila kujali lolote litakalotokea.

Watu wa Makka walipoanza kutuma fidia iliyotakiwa kwa ajili ya kuwakomboa watu wao waliotekwa katika vita vya Badr, Zaynab ﵂ naye pia alituma mkufu wake aliokuwa amepewa kama zawadi na mama yake Khadija ﵂ wakati wa ndoa yake. Mtukufu Mtume ﷺ alipouona mkufu huo aliingiwa na mchomo wa moyo wenye hisia kubwa. Akawaambia maswahaba:

"Mnaweza mkazingatia kumuacha huru mateka wa Zaynab na kumrejeshea fidia yake, kama mkitaka".

Bila kusubiri, Maswahaba walikubali, wakamuacha huru Abul-As mara moja na kuuandaa mkufu huo kwa ajili ya kuurejesha mara moja kwa mwenye nao.

Kabla ya kumruhusu, Mtukufu Mtume ﷺ alimtaka Abul-As amuahidi kama atamtuma Zaynab kwenda Madina, likiwa kama sharti la kuchiliwa kwake ambalo lingebaki kuwa siri baina ya

wawili hao. (Ibn Hisham, II, 296-297; Abu Dawud, Jihad, 121/2692; Ahmad, VI, 276)

Wahb ibn Umayr naye pia alikuwa miongoni mwa mateka wa Vita vya Badr. Baba yake, Umayr, alikuwa miongoni mwa Maquraysh wakali sana na pia alikuwa miongoni mwa mashujaa wao. Katika zama hizo, yeye ndiye alikuwa nyuma ya hujuma nyingi zilizokuwa zikifanywa dhidi ya Waislamu. Wakizungumza na Safwan ibn Umayr, ambaye alikuwa amekaa naye jirani na Hijr, juu huzuni na machungu yake baada ya vita kuhusu hatima ya washirikina wenzao waliotupwa katika mashimo ya Badr, ambapo Safwan alikuwa amemwambia kwa huzuni na masikitiko:

"Hakuna haja ya kuishi baada ya kusikia yaliyowapata!"

"Uko sahihi kwa hilo", alisema Umayr. "Hakika kama nisingekuwa na deni na watoto ambao ninahofia ustawi wao, ningeenda na kumuua Muhammad. Ninayo sababu ya kwenda kwao wakaniruhusu kumkaribia. Nitawaambia tu kwamba nimekuja kwa ajili ya mwanangu aliyetekwa. Mbali na hivyo, kwa ninavyosikia, huwa anatembea mitaani bila hata hofu yoyote!"

Safwan alifurahi kusikia maneno hayo.

"Nitalipa deni lako. Ama kuhusu watoto wako, nitawatunza kama wanangu na kuwahudumia kila kitu katika kipindi chote cha uhai wangu", alimhakikishia Umayr.

Mwanaume anayeyafanyia kazi maneno yake, Umary, haraka sana akaunoa upanga wake na kuupaka sumu. Safwan akachangia safari hiyo kwa kumpatia ngamia na chakula kilichoandaliwa maalumu kwa ajili yake.

Haikuchukua muda mrefu Umayr akawa amewasili mjini Madina. Alisimama mbele ya mlango wa msikiti, akateremka kutoka juu ya ngamia na akaufunga kiunoni upanga wake. Kuonekana kwake mahali hapo kulimfanya Omar ﷺ, ambaye ndiye aliyeanza kumuona, apatwe na hasira, kwa sababu alijisemea moyoni "yule ni Umary, adui wa Mwenyezi Mungu... na wallah, lazima atakuwa amekuja akiwa na shari akilini mwake", kisha akaingia Msikitini na kumkuta Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Umayr amekuja akiwa an upanga mkononi mwake!" Omar alisema kumwambia Mtume ﷺ.

"Mleteni kwangu", Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijibu kwa upole. Hivyo Omar ﷺ akarudi kwa Umayr. Baada ya kumdhibiti kwa kumnyang'anya upanga wake, alimvuta Umayr na kumpeleka Msikitini huku akiwaambia Maswahaba wa *Kiansari* waliokuwa wamemzunguka kuwa "kaeni tayari kwa ajili ya kumlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu dhidi ya mtu huyo mshari, kwani si mtu wa kuaminika!"

"Muacheni aingie ewe Omar!" Mtukufu Mtume ﷺ alisema kwa sauti baada ya kushuhudia ugomvi uliokuwa ukitokea. "Nawe Umayr...sogea karibu!" Kisha akamuuliza sababu ya ujio wake.

"Nimekuja kwa ajili ya mwanangu aliyetekwa. Ninatarajia kuwa utakuwa mkarimu kwa kumuacha huru!" Umayr alieleza.

"Sasa kama ni hivyo upanga huo kiunoni mwako ni wanini?" aliuliza Mtukufu Mtume aliyebarikiwa ﷺ.

"Laana iwe juu ya upanga...! Zimetusaidia nini mpaka sasa?" alijibu Umary kwa namna ya ujanja.

Hata hivyo Mtume wa Rehma ﷺ aliendelea kumuuliza: "Kwa nini umekuja hapa?"

"Sina sababu nyingine zaidi ya mwanangu ambaye ameshikiliwa mateka mikononi mwenu!"

"Kama ni hivyo, ni jambo gani ulililomwambia Safwan mlipokuwa eneo la Hijr?"

"Ni jambo gani hilo ninaloweza kuwa nimemwambia?" Umayr alimumunya akiwa ameshikwa na mshangao.

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akamkumbusha Umayr, neno kwa neno, mazungumzo yake na Safwan, akaongezea kusema, "Hakika Mwenyezi Mungu ameingia baina yako na mipango yako na kukuzuia kufanya lilo ndani ya akili yako!"

Baada ya kusikia hivyo, Umayr akasema: "Ninashuhudia kuwa kwa hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Tulikuwa tukikupinga kuhusu ufunuo uliokujia kutoka mbinguni. Hakuna mtu mwingine aliyekuwa akijua habari hizi zaidi yangu mimi na Safwan. Ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye atakayekuwa amekueleza habari hizi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyenileta hapa na kunijaalia muongozo!" Kisha akatoa tamka la imani. Na hapo Mtukufu Mtume ﷺ akawaambia Maswahaba:

"Mfundisheni ndugu yenu kwa kina kuhusu Uislamu. Msomeeni na kumfundisha Qur'an na muacheni huru mateka wake!"

Amri ya Mtukufu Mtume ﷺ ikatekelezwa hapo hapo. Umayr kaongezea kusema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu...hakika nilikuwa mtu nisiyejali kabisa katika kujaribu kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu na sikuwa na hofu hata kidogo katika kutoa adhabu kali na mateso ya kinyama dhidi ya Waumini. Iwapo utapenda, ninaweza kwenda Makka na kuwalingania washirikina waje kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Mwenyezi Mungu akipenda, wanaweza wakaongoka!"

Mtukufu Mtume ﷺ akamruhusu.

Wakati huo huo, akiwa hana taarifa ya jinsi matukio yaliyobadilika, Safwan ibn Umayya alikuwa akiwaambia waabudu masanamu wa Makka kuwa: "...mtafurahi sana kwa habari mtakazozipata ndani ya siku chache tu; habari zitakazowafanya msahau maumivu ya Badr!"

Akiwa na shauku kubwa, alikuwa akiuliza kila msafara uliokuwa ukiwasilia mjini, kuhusu habari za mahali alipo Umayr. Hatimaye mtu mmoja akiwa juu ya farasi akamwambia kuwa Umayr ameingia katika Uislamu.

Baada ya kurejea mjini Makka, Umayr ibn Wahb رضي الله عنه hakupoteza muda kuanza kuwaita waabudu masanamu kuingia kwenye Uislamu. Majaribio kadhaa ya waabudu masanamu kutaka kumzuia hayakufaulu. Watu wengi waliongoka kupitia ulinganio wake. Siku moja Umayr رضي الله عنه alikutana na Safwan, karibu na Al-Kaabah, akamwambia: "Wewe ni miongoni mwa Maqurayshi maarufu sana. Bado huoni kuwa haya tunayoyaabudu na kuyatolea sadaka ni mawe? Hiyo yawezaje kuwa dini?" Safwan hakujibu lolote, akavamiwa na ukimya usiovunjika. (Ibn Hisham, II, 306-309; Waqidi, I, 125- 128; Ibn Sad, IV, 199-201)

Tokea wakati huo tukio hili limekuwa likitukuzwa kama kifupisho cha msemo usemao: "Mpe pumzi ya uhai yule anayekuja kukuua."

Habari za kuuawa kwa Maqurayshi wote maarufu na kuonekana kwa mateka wengine sabini walioletwa Madina mikono yao ikiwa imefungwa, ilipeleka hofu kwa waabudu Masanamu, wanafiki na Wayahudi wa Madina. Akisikitika kuwa 'mkondo wa ushindi sasa umegeukia kwa Mtume ﷺ', Abdullah ibn Ubayy na kundi lake

hawakuwa na chaguo lingine zaidi ya kula kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kutaka uhusiano na Uislamu.[111]

Hukumu ya Ngawira

Kwa kuwa sheria kuhusu ngawira ilikuwa bado kuteremshwa, mgogoro uliibuka kuhusu ugawaji wa ngawira zilizopatikana katika vita vya Badr. Katika mambo yanayoweza kutajwa hapa ni kuwa, Saad ibn Abi Waqqas ﷺ, ambaye kaka yake aliuliwa kishahidi katika vita vya Badr, alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ akiwa na upanga mkononi mwake aliouchukua kutoka kwa Said ibn As baada ya kumuua katika medani ya vita, akitaka kuwa upanga huo apewe yeye. Penginepo matukio na maombi mbalimbali ndiyo yaliyosababishwa kuteremshwa kwa aya ya kwanza ya suratul-Anfal, kabla ya Waislamu hawajaondoka Badr na kabla hawajazigawanya ngawira:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الأَنفَالِ قُلِ الأَنفَالُ لِلّهِ وَالرَّسُولِ فَاتَّقُواْ اللَّهَ وَأَصْلِحُواْ ذَاتَ بِيْنِكُمْ وَأَطِيعُواْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ

"Wanakuuliza juu ya Ngawira. Sema: Ngawira ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu, na mt›iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni Waumini (wa kweli). (al-Anfal: 1)

Kwa hali hiyo Mtukufu Mtume ﷺ akazikasimu ngawira hizo kwa uadilifu baina ya wapiganaji karibu na mji wa Madina.[112]

111. Bukhari, Tafsir, 3/15; Waqidi, I, 121.
112. Ahmad, I, 178; V, 323-324; Abu Dawud, Jihad, 144-145/2737-2744.

Baadaye iliteremshwa aya iliyokuwa na maelezo na ufafanuzi wa hukmu mbalimbali kuhusu ngawira. Aya ni ya 41 ndani ya sura hiyo hiyo:

وَاعْلَمُواْ أَنَّمَا غَنِمْتُم مِّن شَيْءٍ فَأَنَّ لِلّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَى
وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ إِن كُنتُمْ آمَنتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أَنزَلْنَا عَلَى
عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"NA JUENI ya kwamba ngawira mnayo ipata, basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri, ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyo yateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuo, siku yalipo kutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu." (al-Anfal: 41)

Kwa mujibu wa aya hiyo, sehemu moja katika tano ya ngawira za vita ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mtume, jamaa zake, mayatima, maskini na wasafiri.

Baada ya kudhamini mahitaji ya wanafamilia yake kwa sehemu ya ngawira za fungu lake, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akihifadhi kiasi kilichobaki katika Hazina ili kitumike kukidhi mahitaji ya Waislamu na matumizi ya jeshi.[113]

Amr ibn Abasa ﷺ anasimulia:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu alituongoza katika swala huku ngamia, aliyetokana na ngawira za vita, akiwa amewekwa upande wa *qiblah* kama *sutrah*.[114] Baada ya kumaliza swala, ali-

113. Bukhari, Faraid, 3, Khumus, 1, Nafaqat, 3; Muslim, Jihad 49.

114. *Sutrah* ni pazia au chochote kilichoweza kutumika kama kizuizi. Hasa hasa, kinachokusudiwa ni kile kinachowekwa mbele ya mtu anayeswali kwa lengo la kuzuia wengine wasipite mbele yake.

chukua unywele mmoja kutoka kwenye ngamia huyo, na akiwa ameushika mkononi mwake alisema: 'Siruhusiwi kuchukua hata kiasi cha unywele huu kutoka katika ngawira zetu, isipokuwa kutoka katika khums (sehemu ya tano) tu. Aidha, hata hiyo khums (sehemu ya tano) mwishowe hurudi kwenu (ikatumika kwa ajili ya mahitaji yenu).'" (Abu Dawud, Jihad, 149/2755)

Kila alichokuwa nacho Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akikitoa kuwapa masikini miongoni mwa Maswahaba, licha ya ukweli kwamba muda mwingi hapakuwepo na chochote cha kupika katika nyumba yake mwenyewe, huku jiko likiendelea kutowashwa kwa miezi kadhaa. Ni wazi, kutokana na simulizi mbalimbali kama hizo, kwamba mara nyingi yeye na familia yake walikuwa wakikaa bila chakula hata cha siku moja. Mwenendo wake huu unaoneshwa wazi kabisa katika tukio lifuatalo linalosimuliwa na Anas رضي الله عنه:

"Mizigo kadhaa ya mali kutoka Bahrain ililetwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, naye akaamuru zishushwe kwa muda ndani ya Msikiti. *Bayfar*, ndiyo iliyoletwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakati huo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alienda kuswali na akurudisha tena macho yake kwenye lundo hilo la mali. Baada ya swala alikuja na kusimama karibu na lundo hilo kisha akaanza kuzigawa kwa kila aliyemuona; hakuondoka mpaka alipoona kuwa hakubakisha dirham hata moja ambayo hajaitoa." (Bukhari, Salat, 42; Jizya, 4, Jihad, 172)

Surah al-Anfal iliteremshwa katika mwaka wa pili wa Hijra. Kwa kuwa sehemu yake kubwa inafafanua kuhusu Vita vya Badr,

pamoja na ukweli kwamba ilishuka siku chache kabla na baada ya vita, imeitwa pia *surah* ya Badr.

Kifo cha Kishahidi

Kifo cha kishahidi ndiyo daraja kubwa na ya juu kabisa duniani ambayo Muumini anaweza kuipata. Japokuwa daraja ya chini kabisa peponi ni bora kuliko dunia yote, mtu aliyekufa kishahidi, kutokana na ukuu wa daraja yake na ukubwa wa malipo yake Peponi, atatamani arudi duniani tena na tena ili auawe kila mara kishahidi. Mwenyezi Mungu Aliyetukuka anasema:

وَلَئِن قُتِلْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ لَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ
وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ

"Na pindi mkiuliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu, au mkifa, hakika maghfira na rehema zitokazo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko yote wanayo yakusanya." (Al'i Imran: 157)

Tukio lifuatalo linasimuliwa na Saad ibn Abi Waqqas ﵁:

"Siku moja kuna mtu alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ huku akituswalisha. Baada ya kuchukua nafasi yake katika safu, aliomba dua akisema: 'Ewe Allah...nijaalie kitu bora kabisa katika ulivyowajaalia waja Wako wema!'

Baada ya Mtume ﷺ kukamilisha swala yake akauliza: 'Ni nani aliyeomba dua hiyo awali?'

'Ni mimi', akasema mtu yule.

'Basi farasi wako ataangushwa' akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu, 'na wewe utauawa kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu.'" (Hakim, I, 325/748)

Sambamba na kutabiri kifo cha kishahidi ambacho kingewapata Maswahaba wake wengi, mwisho wa wale walioombewa maghfira na dua njema na Mtukfu Mtume ﷺ ilikuwa ni kuuawa kishahidi. Miongoni mwa mifano hiyo ni Amr ibn Aqwa ؓ, ambaye muda mfupi baada ya kupata neema ya kuombewa dua ya mwisho kutoka kwa Mtume ﷺ aliuawa kishahidi katika Vita vya Badr.[115]

Hatua ya dua ya maghfira ya Mtukufu Mtume ﷺ kujidhihirisha yenyewe katika vifo vya kishahidi vya wale walioombewa na Mtume ﷺ, ni uthibitisho mwingine wa ukubwa wa daraja ya kifo cha kishahidi. Hapo, wakiwa wamezoea kushuhudia matokeo hayo yakiwatokea wenzao kadhaa wa kadhaa, Maswahaba nao wakaja kutambua kuwa dua hizo ilikuwa bishara njema ya vifo vyao vya kishahidi.

Kwa mujibu wa riwaya iliyosimuliwa na Abu Qatadah ؓ, Mtukufu Mtume ﷺ siku moja alisimama katikati ya Maswahaba na kuwakumbusha kuwa "Kumuamini Mwenyezi Mungu na kupigana katika njia Yake ndio amali bora kabisa kuliko amali zote!"

Alipokwisha kusema hivyo mtu mmoja akasimama na kuuliza: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, iwapo nitakufa katika njia ya Mwenyezi Mungu, je hiyo itakuwa sababu ya kufutiwa madhambi yangu?"

"Ndiyo. Kama utathibiti kwenye safu, ukasimama imara dhidi ya adui, kwa subira na kwa kutarajia thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee, kisha ukauawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, itakuwa sababu ya kufutiwa madhambi yako. Isipokuwa madeni yako. Hivyo nilivyoambiwa na Jibril." (Muslim, Imarah, 117; Tirmidhi, Jihad, 33/1712)

Katika *hadith* nyingine imetangazwa:

115. Muslim, Jihad, 123, 132; Bukhari, Maghazi, 138.

"Dhambi zote za mtu aliyekufa kishahidi husamehewa na Mwenyezi Mungu, isipokuwa uvunjaji wa haki za wengine." (Muslim, Imarah, 119)

Wakati mwingine, Mtume wa Rehma ﷺ alieleza yafuatayao kuwaambia Maswahaba:

"Usiku wa jana niliwaona watu wawili ndotoni mwangu. Walinichukua mpaka kwenye mti huu na kisha wakanipeleka kwenye jengo moja ambalo sijawahi kushuhudia uzuri na ughali wake. Kisha watu hao wakaniambia, 'Jengo hili la kipekee ni kasri la mashahidi.'" (Bukhari, Jihad, 4; Janaiz, 93)

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akizifariji na kuzisaidia familia za mashahidi na wakati huo huo kuwa kuwatia moyo Maswahaba kupata daraja ya kifo cha kishahidi.

Jabir رضي الله عنه anaelezea:

"Mwili wa baba yangu, ukiwa umefanyiwa *muthlah*[116], ulileta na kuwekwa mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Nilisogea ili kwenda kufunua sehemu ya uso iliyokuwa imefunikwa nikazuiliwa na wale waliokuwa mahali hapo wakiwaza kuwa watu watakapouona mwili huo wataumia na kukarahika. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, 'malaika wanaendelea bila kuchoka kumfunika kwa kivuli cha mbawa zao.'" (Bukhari, Janaiz, 3, 35, Jihad, 20; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 129-130)

Kufa kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu sio kufa. Bali ni alama ya kupokea baraka za uhai wa milele tusiouona. Kwa hali

116. *Muthlah* ni kitendo cha kuukatakata mwili wa marehemu wakati wa vita kwa kukata sikio, pua na viungo vingine vya mwili, na kunyofoa macho. Mtukufu Mtume ﷺ alipiga marufuku kitendo hiki cha kinyama, alipiga marufuku pia hata kwa wanyama. (Bukhari, Mazalim, 30, Dhabaih, 25; Abu Dawud, Jihad, 110)

hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu amekataza kutumia neno 'wafu' kuwaelezea wale waliokufa kishahidi. Qur'an Tukufu inatangaza:

وَلاَ تَقُولُواْ لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتٌ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَكِن لاَّ تَشْعُرُونَ

"Wala msiseme kuwa wale walio uwawa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti; bali hao ni wahai, lakini nyinyi hamtambui." (al-Baqara: 154)

وَلاَ تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُواْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِندَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُواْ بِهِم مِّنْ خَلْفِهِمْ أَلاَّ خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلاَ هُمْ يَحْزَنُونَ يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ وَأَنَّ اللَّهَ لاَ يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ

"Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi. Wanafurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na wanawashangilia wale ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa Waumini." (Al'i Imran: 169-171)

Siku ya Kiyama, mashahidi watatambuliwa kwa damu itakayokuwa ikichuruzika kutoka katika majeraha yao, ikionekana kana kwamba yamefumuliwa wakati huo, na harufu nzuri kama ya miski ikitoka katika majeraha hayo. Watu wataamriwa kusimama kwa ajili ya kushuhudia heshima na ubora wa mashahidi hao. Ni kwa sababu hii kwamba, tofauti na watu wengine, miili ya masha-

hidi haifanyiwi taratibu za kuoshwa kabla ya kuzikwa na majeraha huachwa hivyo yalivyo.

Mtukufu Mtume ﷺ anaelezea huruma ambayo Mwenyezi Mungu huionesha kwa mashahidi wakati wanapovuta pumzi yao ya mwisho:

"Uchungu anaouhisi mtu anapong'atwa na sisimizi ndio uchungu mkubwa zaidi anaouhisi shahidi wakati wa mauti yake." (Tirmidhi, Fadail'ul-Jihad, 26/1668; Nasai, Jihad, 35; Ibn Majah, Jihad, 16)

Katika kuwahamasisha Waumini kuhusu kifo cha kishahidi, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَلْيُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيوةَ الدُّنْيَا بِالآخِرَةِ وَمَن يُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلْ أَو يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا

"Basi nawapigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu wale ambao wanao uza uhai wa dunia kwa Akhera. Na anaye pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauliwa au akashinda basi tutakuja mpa ujira mkubwa." (an-Nisa: 74)

Naye Mtukufu Mtume ﷺ akielezea tamaa yake ya kufa kishahidi, anasema:

"Lau isingekuwa mzigo juu ya *ummah* wangu, nisingebaki nyuma katika safari yoyote ya kijeshi (sariyya) na ningeshiriki katika safari zote. Ningetaka niuawe kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, nifufuliwe na niuawe kishahidi tena na tena." (Bukhari, Iman, 26; Muslim, Imarah, 103, 107)

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alimuona Omar رضي الله عنه akiwa amevaa kanzu fulani.

"Je kanzu hiyo ni mpya au imefuliwa tu?" Mtukufu Mtume ﷺ aliuliza.

"Sio mpya, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu; imefuliwa", akajibu Omar رضي الله عنه.

"Ujaaliwe kuivaa ikiwa mpya, uishi kwa kushukuru na ufe kishahidi!" (Ahmad, II, 89)

Kwa dua hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akimbashiria Omar رضي الله عنه kifo cha kishahidi.

Katika tukio lingine Mtume wa Rehma ﷺ alikuwa amesimama juu ya Mlima Uhud, akiwa pamoja na Abu Bakr, Omar na Uthman رضي الله عنهم, ambapo kwa ghafla mlima huo ulianza kutikisika. Mtukufu Mtume ﷺ akapiga kwa mguu wake ardhini akasema:

"Tulia ewe Uhud. Hakika waliosimama juu yako ni Mtume, *siddiq* na mashahidi wawili." (Bukhari, Ashab'un-Nabi, 6; Tirmidhi, Manaq-ib, 18/3703; Nasai, Ahbas, 4)

Omar رضي الله عنه pia alikuwa akiomba dua mara kwa mara akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu; nijaalie kifo cha kishahidi katika njia Yako na furaha ya kufia katika ardhi ya Mtume Wako!" (Bukhari, Fadhail'ul-Madina, 12) hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkubalia ombi lake. Binti yake, Hafsa رضي الله عنها anasema:

"Nilipoisikia dua ya baba yangu, nilishangazwa na kusema. 'Itawezekanaje; unataka kuuawa kishahidi na ukiwa Madina pia?' Lakini hakuwa na neno zaidi ya kusema, 'Mwenyezi Mungu akipenda atalifanya litokee.'"

Mshangao na wasiwasi watu kuhusu kutokea kwa jambo hilo uliendelea kuwepo mpaka Omar رضي الله عنه alipokuja kuuawa kishahidi. (Ibn'ul-Hajar, Fath'ul-Bari, IV, 101)

Katika kuashiria haja ya kila Muislamu kutamani kwa dhati kifo cha kishahidi, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Mwenye kutaka kifo cha kishahidi kwa moyo mmoja kutoka kwa Mwenyezi Mungu, atapewa daraja hiyo, hata kama atafia kitandani kwake." (Muslim, Imarah, 157; Nasai, Jihad, 36)

"Mwenye kutamani kifo cha kishahidi kwa moyo mmoja atapewa thawabu za kifo cha kishahidi, hata kama hatouawa kishahidi." (Muslim, Imarah, 156)

Aidha, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alizihesabu aina nyingine kadhaa za kifo kuwa ni katika vifo vya kishahidi. Siku moja aliwauliza Maswahaba: "Ni nani mnayemhesabu kuwa shahidi?"

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, shahidi ni yule anayekufa katika njia ya Mwenyezi Mungu", walijibu.

"Kama ni hivyo, mashahidi katika *ummah* wangu ni wachache sana", akasema Mtukufu Mtume ﷺ.

"Kwa hiyo ni nani shahidi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

"Mwenye kuuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, hufa katika njia ya Mwenyezi Mungu, mwenye kufa kutokana na maradhi ya kuambukiza,anayekufa kwa ugonjwa wa kuhara na anayekufa kwa kuzama majini, huyo ni shahidi", alieleza Mtukufu Mtume ﷺ. (Muslim, Imarah, 165; Ibn Majah, Jihad, 17)

Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ pia amewapa daraja ya mashahidi wale wanaokufa katika kujitetea au kuzitetea familia na mali zao.[117]

117. Tazama, Bukhari, Mazalim, 33; Muslim, Iman, 226; Abu Dawud, Sunnah, 28-29; Tirmidhı, Diyat, 21.

Zaynab ﵂ Awasili Madina

Baada ya kuachiwa huru, kitu cha kwanza alichofanya Abul-As, mkwe wa Mtume ﷺ aliyetekwa katika Vita vya Badr, baada ya kuwasili Makka ni kumruhusu Zaynab ﵂ kwenda Madina.Mwezi mmoja takriban baada ya Vita vya Badr, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Zayd ibn Haritha na Swahaba mwingine kutoka katika *Ansar*, waende Makka, akawaambia, "subirini katika Bonde la Yajij mpaka Zaynab atakapokuja hapo na kisha mumsindikize mpaka nyote mtakapofika Madina."

Hivyo, Abul-As akamwambia Zaynab ﵂ kuwa anaweza kwenda Madina, kwa baba yake. Zaynab hakupoteza muda katika kujiandaa. Kaka wa Abul-As, Kinanah, akaandaa ngamia pamoja na *hawdaj*, ambayo ingetumika kumsafirisha Zaynab. Baada ya kuning'iniza upinde na mkoba wake wa mishale begani mwake, Kinanah alichukua hatamu za ngamia na kuanza kutoka Makka wakati wa mchana.

Hata hivyo taarifa zilisambaa haraka miongoni mwa waabudu masanamu, na kundi la watu likatoka kwa ajili ya kwenda kumzuia, wakawakuta karibu na Zituwa. Akiwa amejificha, Habbar ibn Aswad aliishambulia *hawdaj* ambayo Zaynab ﵂ alikuwa amekaa ndani yake, jambo lililosababisha aangukie kwenye jiwe lililokuwa hapo. Kwa kuwa Zaynab ﵂ wakati huo alikuwa mjamzito,alipoteza ujauzito wake, damu zikamtoka na kuvilia. Alipata maumivu makali sana. Katika kujaribu kumlinda, Kinanah akauchomoa mshale na kuutega katika upinde, akauelekeza kwa waabudu masanamu huku akisema:

"Msisogee hata kidogo la sivyo nitawamiminia mishale!"

Baada ya kusitasita kwa muda, watu hao waliamua kuondoka. Lakini muda mfupi baadaye, Abu Sufyan alifika akisuhubiana na kundi lingine la waabudu masanamu, akamwambia Kinanah aweke

kando upinde na mshale wake, kwa kuwa wao walikuwa wamekuja tu kuzungumza. Baada ya Kinanah kuweka chini upinde na mshale wake, Abu Sufyan akasema:

"Ulifanya safari isiyokuwa sahihi kwa kumtoa Makka mchana kweupe, hali ya kuwa ukijua shida tunayoipitia na yale aliyotufanyia Muhammad! Kumpelekea binti yake wazi wazi huku watu wote wakiona, unawapa watu sababu ya kuamini kuwa umeweza kutoa nje ya mji kutokana na udhaifu na unyonge wetu na kwamba fedheha ya kushindwa kwetu ndiyo sababu ya wewe kufanya hivyo! Ninaapa kwa nafsi yangu mwenyewe kwamba hatukuona tabu Zaynab kwenda kwa baba yake au kubaki hapa. Wala suala hilo halitufanyi tufanye kisasi! Sasa nisikilize...Mrejeshe Makka. Watu wakishatulia na kuamini kuwa tumeweza kukushawishi umrejeshe, utamchukua kisirisiri na kumpeleka kwa baba yake!"

Kinanah alifanya hivyo. Baada ya kukaa masiku kadhaa mjini Makka, akisubiri mambo yatulie, akaanza kwa mara nyingine safari pamoja na Zaynab ﵂, mara hii akisafiri usiku. Alimkabidhi kwa Zayd ibn Haritha na rafiki yake ambao walikuwa wakisubiri katika Bonde la Yajij, nao wakampeleka Madina, ambapo hatimaye aliungana tena na baba yake.[118]

Katika mwaka wa sita wa Hijra, Abul-As alitekwa tena wakati akiongoza msafara mmoja wa Maqurayshi. Wakati wa alfajiri, alituma ujumbe kwenda kwa Zaynab ﵂ akimsihi aombe msamaha Mtukufu Mtume ﷺ kwa niaba yake. Mtukufu Mtume ﷺ alipomaliza kuswalisha swala ya alfajiri, Zaynab alitotokeza kichwa chake kutoka chumbani kwake na kusema:

"Enyi watu...Mimi ni Zaynab Binti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na nimemuweka Abul-As chini ya hifadhi yangu!"

118. Ibn Hisham, II, 297-299; Ibn Abdilbar, IV, 1854; Ibn Kathir, al-Bidayah, III, 362-363.

"Nasi tunamuweka chini ya hifadhi yetu yule ambaye umemuweka chini ya hifadhi yako!" Mtukufu Mtume ﷺ alijibu.

"Yeye ni jamaa, na pia, ni baba wa watoto wangu; hiyo ndiyo sababu ya mimi kumuweka chini ya hifadhi yangu", Zaynab alimfafanulia baba yake. Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akasema kuwaambia Maswahaba:

"Mkiona kuwa inafaa kumrejeshea (Abul-As) mali zake basi fanyeni, la kama haifa, kwa vyovyote, mna haki juu ya mali hiyo!"

Pasipo taabu yoyote, Maswahaba walikubali kumrejeshea Abul-As mali zake. Baada ya kurejeshewa mali hizo, Abul-As alirejea mjini Makka; na baada ya kumkabidhi kila mdau wa msafara huo hisa yake, akatangaza:

"Je kuna yeyote ambaye sijampatia fungu lake?"

"Hapana", wakajibu wale waliokuwa mahali hapo.

"Je nimetekeleza majukumu yangu kwenu?"

"Hakika umetekeleza", walisema. "Ulipwe kwa wingi kwa maana wewe ni mtu mwenye kuheshimiwa na muaminifu!"

Hapo Abul-As akaanza kutangaza akisema:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa, kitu pekee kilichonizuia kuukubali Uislamu nilipokuwa Madina ni hofu niliyokuwa nayo kuwa huwenda mngedhani kuwa nimeukubali Uislamu ili nipate kupora mali zenu. Lakini sasa kwa kuwa limemalizika, ninashuhudia kuwa hakuna Mungu apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni mja na mjumbe Wake!"

Kisha Abul-As akarejea Madina, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ kwa mara nyingine alimuozesha Zaynab kwake (Abul-As). (Waqidi, II, 553-554; Ibn Sad, VII, 32-33)

Mayahudi na Vita vya Banu Qaynuqa
(Shawwal, 2/ Aprili, 624)

Mayahudi ambao walikuwa akiunda jamii muhimu ndani na pembezoni mwa mji wa Madina, mara zote walikuwa wakiwaambia majirani zao Waarabu juu ya ujio wa mtume katika kipindi kifupi kijacho. Imani yao kwamba mtume huyo atatokana na jamii yao ilimaanisha kuwa hawakuona haya hata kidogo kueneza kwa nguvu habari hizo. Pindi mtume huyo alipokuja, akitokana na Waarabu badala ya Wayahudi, hisia zao za hamasa zilibadilika na kuwa husda na wivu. Haraka sana wakiwa wameubadilisha wimbo wao, waliukana utume wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatangaza kuhusu suala hilo:

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ لاَ تَعْبُدُونَ إِلاَّ اللَّهَ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَاناً وَذِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينِ وَقُولُواْ لِلنَّاسِ حُسْناً وَأَقِيمُواْ الصَّلوةَ وَآتُواْ الزَّكَوةَ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ إِلاَّ قَلِيلاً مِّنكُمْ وَأَنتُم مِّعْرِضُونَ

"Na tulipofunga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na shikeni Sala, na toeni Zaka. Kisha mkageuka isipo kuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuza." (al-Baqara: 83)

بِئْسَمَا اشْتَرَوْاْ بِهِ أَنفُسَهُمْ أَن يَكْفُرُواْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ بَغْياً أَن يُنَزِّلَ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ عَلَى مَن يَشَاء مِنْ عِبَادِهِ فَبَآؤُواْ بِغَضَبٍ عَلَى غَضَبٍ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُّهِينٌ

"Kiovu kweli walicho jiuzia nafsi zao, nacho ni kule kukataa kwao aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya kuona maya kwa kuwa Mwenyezi Mungu humteremshia fadhila yake amtakaye miongoni mwa waja wake. Basi wamejiletea wenyewe ghadhabu juu ya ghadhabu. Na makafiri watapata mateso ya kudhalilisha." (al-Baqara: 90)

Sababu nyingine ya uchungu wa Mayahudi ni mapenzi yao ya kuipenda dunia, ambayo yameelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاةٍ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُواْيَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحْزِحِهِ مِنَ الْعَذَابِ أَن يُعَمَّرَ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ

"Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi, na kuliko washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angelipewa umri wa miaka elfu..." (al-Baqara: 96)

Aidha, kuhodhi kwako maisha ya kibiashara kuliwapa Mayahudi anga la kuwa bora, ikizidishwa na kujiona kuwa wenye nguvu na uwezo, jambo lililowafanya waamini kuwa:

نَحْنُ أَبْنَاء اللَّهِ وَأَحِبَّاؤُهُ

"Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake..." (al-Maida: 18)

Walipokumbushwa kuhusu adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa uovu wao, walikuwa wakijibu kwa kujiamini:

لَن تَمَسَّنَا النَّارُ إِلاَّ أَيَّاماً مَّعْدُودَةً

"Hautatugusa Moto ila kwa siku chache tu..." (al-Baqara: 80)

Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu akatangaza vinginevyo:

بَلَى مَن كَسَبَ سَيِّئَةً وَأَحَاطَتْ بِهِ خَطِيئَتُهُ فَأُوْلَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

"Naam, anayechuma ubaya - na makosa yake yakamzunguka - hao ndio watu wa Motoni; humo watadumu." (al-Baqara: 81)

Licha ya mkataba waliokuwa wamewekeana na Mtukufu Mtume ﷺ, Mayahudi walikuwa wakiendeleza hisia za chuki za ndani dhidi yake, jambo lililowafanya waibue uhasama uliokuwepo mwanzo baina ya koo mbalimbali na kuwasha moto wa uovu na shari. Mwenyezi Mungu Mtukufualiwafichua kwa Mtume Wake na kwa Waumini:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَتَّخِذُواْ بِطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لاَ يَأْلُونَكُمْ خَبَالاً وَدُّواْ مَا عَنِتُّمْ قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الآيَاتِ إِن كُنتُمْ تَعْقِلُون هَاأَنتُمْ أُولاءِ تُحِبُّونَهُمْ وَلاَ يُحِبُّونَكُمْ وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ وَإِذَا لَقُوكُمْ قَالُواْ آمَنَّا وَإِذَا خَلَوْاْ عَضُّواْ عَلَيْكُمُ الأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ قُلْ مُوتُواْ بِغَيْظِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ إِن تَمْسَسْكُمْ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ وَإِن تُصِبْكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرَحُواْبِهَا وَإِن تَصْبِرُواْ وَتَتَّقُواْ لاَ يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ

"Enyi mlio amini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasio kuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayo kudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni Ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini. Hivyo basi nyinyi ndio mnawapenda watu hao, wala wao hawakupendeni. Nanyi mnaviamini Vitabu vyote. Na wanapo kutana nanyi husema: Tumeamini. Na wanapo kuwa peke yao wanakuumieni vidole kwa chuki. Sema: Kufeni kwa chuki yenu! Hakika Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo vifuani. Ikikupateni kheri huwaudhi. Na ikikupateni shari wanafurahia. Na nyinyi mkisubiri na mkajizuilia, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyazunguka yote wayatendayo." (Al-i Imran: 118-120)

Mayahudi walioanikwa na aya hiyo, walikuwa wameficha hila na kutengeneza kinyongo dhidi ya Waumini, walionekana kutokuwa na raha kufuatia ushindi wa Waislamu katika vita vya Badr. Mayahudi wa Banu Qaynuqa, kwa namna maalumu, waliamua kuzichukua hisia zao za kukosa raha kwenye hatua ya mbele zaidi na kuwalazimisha Waumini kuingia vitani. Huo ukawa mwanzo wa kuvunja mkataba waliokuwa wamewekeana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Mayahudi, wakisaidiwa na mshirika wao wa karibu Abdullah ibn Ubayy, kiongozi wa wanafiki, walikuwa wameigeuza Madina kuwa jungu la uchawi kwa kutengeneza njama mbalimbali dhidi ya Waumini. Njama hizi zilikuwa na matokeo yenye kutisha kwa Waislamu. Katika njama hizo walijumuisha hata mpango wa kumuua Mtume aliyebarikiwa ﷺ.

Mpaka hapo, Mayahudi hawakuitambua mipaka yoyote ya shari zao na ufidhuli wao ulifikiwa kiwango kilichopitiliza. Siku moja, Yahudi mmoja alimshambulia mwanamke wa Kiislamu aliyekuwa ameenda katika soko lao kwa ajili ya mahitaji yake, akim-

fanyia ufedhuli na uovu mbaya sana. Mayoe ya mwanake huyo akitaka msaada hayakwenda patupu, kwani Muislamu mwingine ambaye alikuwa wakipita mahali hapo na kushuhudia tukio hilo, aliingilia kati na kumkabili Yahudi huyo. Baada ya muda mfupi lakini wenye ugomvi, Yahudi yule alyejeruhiwa alifariki dunia, ambapo Mayahudi wengine walimshambulia Muislamu na kumuua. Lilikuwa tukio lenye vurumai. Hiyo ilimaanisha kwamba Mayahudi walikuwa wamevunja mkataba wao na Waumini. Hivyo Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya viongozi wao haraka sana na kuwahutubia akiwaambia:

"Enyi Mayahudi; muogopeni Mwenyezi Mungu! Muogopeni la sivyo mtapatwa na msiba kama uliowapata Maqurayshi! Zaidi ya yote, mnajua vyema kuwa mimi ni mtume wa kweli...imeandikwa katika vitabu vyenu na inajulikana kupitia ahadi ya Mwenyezi Mungu kwenu!"

Kwa hiyo Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza kuwa Mayahudi watalazimika kulipa fidia ya uonevu wao, lakini wakati huo huo, akautaka mkataba uliovunjwa. Akatoa pendekezo la kuufufua. Lakini jibu la Mayahudi likatiririka kwa kiburi na jeuri:

"Ewe Muhammad, unadhani sisi ni kama Maqurayshi wasiojua kupigana? Utakapopambana na sisi ndipo utakapojua maana ya vita!"

Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ifuatayo:

قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُواْ سَتُغْلَبُونَ وَتُحْشَرُونَ إِلَى جَهَنَّمَ وَبِئْسَ الْمِهَادُ قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِئَتَيْنِ الْتَقَتَا

"Waambie walio kufuru: Karibuni mtashindwa na mtakusanywa, mtiwe kwenye Jahannam; nako huko ni makao mabaya kabisa.

Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu katika yale majeshi mawili yalipo pambana." (Al'i Imran: 12-13)[119]

Mayahudi ndio ambao zamani walimpinga Nabii Musa عليه السلام na kumwambia:

فَاذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ

"Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa." (al-Maida: 24) Hapo zamani walikataa kupigana vita waliyoamriwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ambayo ingewapatia thawabu na malipo mengi mno, sasa walikuwa wameshika mtazamo mwingine kwa kujificha nyuma ya ushujaa wa bandia wa kuchukua silaha kuingia katika vita ambavyo ilikuwa wazi kuwa isingewapatia faida yoyote.

Kwa kutangaza vita dhidi ya Waislamu, Mayahudi walikuwa wamevunja mkataba. Sasa wakawa wazi kwa dhamira zao za kiovu. Akiwa amemfanya Ali رضي الله عنه kuwa mbeba bendera, Mtukufu Mtume ﷺ akaelekea na jeshi kwa Banu Qaynuqa, ambao walikimbilia katika ngome yao. Licha ya kuwa walikuwa wamefanya njama mbalimbali kwa kushirikina na wanafiki ili kuwaudhi Waislamu, Mayahudi hawakuweza hata kutupa mshale, achilia mbali kutoka nje ya ngome yao.Sambamba na kuweka mzingiro wa hali ya juu kwenye ngome yao, wakati huo huo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua hatua za kiusalama zinazowezekana kuzuia uwezekano wa wanafiki kuibuka nyuma yao.

Kiongozi wa wanafiki, Abdullah ibn Ubayy, ndiye aliyewashauri kukimbilia kwenye ngome yao, akiwahakikishia Mayahudi kuwa angekuja haraka kuwasaidia. Lakini hakufanya hivyo. Woga ulimzuia kutekeleza maneno yake.

119. Ibn Hisham, II, 422-423; Waqidi, I, 181-182; Ibn Saad, II, 30.

Mzingiro ulidumu kwa muda wa siku kumi na tano. Sasa woga uliokuwa umeingia katika nyoyo za Mayahudi usingeweza kuvumilika. Msaada waliokuwa wakiutarajia kutoka kwa wanafiki haukuja aslani, hiyo ikawa sawa na kuongeza chumvi kwenye majeraha yao. Sasa hawakuwa na chaguo tena zaidi ya kusalimu amri. Hivyo wakajisalimisha, wakiwa tayari kwa hukumu yoyote itakayotolewa na Mtukufu Mtume ﷺ juu yao.

Banu Qaynuqa walikuwa na mkataba pamoja na Khazraj kabla ya Hijra. Hivyo Abdullah ibn Ubayy, kiongozi wa Khazraj akageuka kuwa mnafiki, akawaombea msamaha; kwani kwa kaida walitakiwa kuuawa.

Kufuatia mlolongo wa mamombi yasiyokatika ya kuwaombea msamaha, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwaua bali aliwafukuza wakaelekea upande wa Syria. Njiani Mayahudi wa Banu Qaynuqa walisimama kwenye eneo la Wadil-Qura, ambapo walipata msaaada kutoka kwa Mayahudi wa eneo hilo. Japokuwa waliendelea mbele, maisha ya Mayahudi wa Banu Qaynuqa huko hayakudumu.[120]

Tukio la Sawiq (Dhil-hijjah, 2/ Mei, 624)

Abu Sufyan alichukua uongozi wa Maqurayshi kufuatia kifo cha Abu Jahl.Akiwa ameapa kulipiza kisasi, aliondoka Makka akiwa na jeshi la askari wa farasi mia mbili. Hatimaye alifika eneo la umbali wa saa moja kutoka mjini Madina; na kwa kutumia fursa ya giza, Abu Sufyan aliweza kufika katika makao ya Mayahudi wa Banu Nadir. Huko, alielekea kwenye nyumba ya Sallam ibn Mishkam, kiongozi na mhazini wao, ambaye alimkaribisha mgeni wake kwa namna iliyokuwa nzuri, ambapo kiongozi huyo alimpatia Abu Sufyan baadhi ya taarifa za ndani kuhusu Waislamu.

120. Tazama, Abu Dawud, Kharaj, 21-22/3001.

Baada ya kuondoka katika makao ya Banu Nadir, Abu Sufyan alirudi kwa wenzake, wakati huo huo akamuua Saada ibn Amr wa jamii ya *Ansar* na kuyachoma moto mashamba machache ya tende yaliyokuwa njiani. Kwa vitendo hivyo, Abu Sufyan sasa alijiona kama amelipiza kisasi dhidi ya Waislamu na bila kuchelewa akayarudisha haraka sana majeshi yake Makka kutokana na hofu ya kufuatwa. Mara tu baada ya kupata taarifa za tukio hilo, Mtukufu Mtume ﷺ alitoka kwenda kuwafuatilia waabudu masanamu. Waliona kwamba ili waweze kuwa na wepesi wa kuondoka, waabudu masanamu walidondosha mifuko ya unga uliokaushwa au *sawiq*, na hivyo mgogoro huo ukaitwa kwa jina hilo.[121]

Ndoa ya Ali na Bibi Fatimah ؓ

Mwaka wa pili wa Hijra ulishuhudia pia ndoa baina ya Fatma ؓ, binti wa Mtukufu Mtume ﷺ, na Ali ؓ.

Wanaume wengi wa Kiqurayshi wenye umaarufu na ushawishi, akiwemo Abu Bakr na Omar ؓ hapo awali walikuwa wameomba kumuoa lakini Mtukufu Mtume ﷺ hakutoa ridhaa, akawaambia kuwa 'anasubiri amri ya Mwenyezi Mungu kuhusu Fatimah'. Ni kwa sababu hiyo kwamba, licha ya ushawishi wa ndugu zake, hata Ali ؓ hakuweza kutoa wazo la kumuoa.Lakini muda mfupi baadaye, kwa msisitizo wa ndugu zake, Ali ؓ alifika mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ.[122]

Matukio mengine yaliyotokea yanasimuliwa na Ali ؓ:

"Baada ya muda mrefu, hatimaye nilienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kama kawaida alikuwa ameketi katika mkao

121. Ibn Hisham, II, 426-429; Waqidi, I, 176-180; Ibn Saad, II, 28-30.
122. Ibn Saad, VIII, 19.

wake mtukufu. Niliketi mbele yake na kukaa kimya. Sikuweza kutamka neno lolote.

'Kwa nini umekuja; unahitaji kitu?' aliuliza. 'Yaonekana umekuja hapa kwa ajili ya kumchumbia Fatimah!'

'Ndiyo', hilo ndilo neno pekee nililoweza kutamka". (Ibn Kathir, al-Bidayah, III, 379)

Kwa ruhusa ya Mtukufu Mtume ﷺ, Ali ؓ aliuza baadhi ya vitu vyake na kuandaa mahari ya dirhamu 480. Mtume aliyebarikiwa ﷺ alimshauri kuwa theluthi mbili aitumie kununua manukato na theluthi moja iliyobaki aitumie kununua mavazi.[123]

Kwa marembo na mavazi ya bibi harusi, Mtukufu Mtume ﷺ alimpatia Fatimah ؓ nguo ya kitani, kiriba cha maji na mto uliotengenezwa kwa *idhir* inayofanana na majani.[124] Kisha akamwambia Bilal:

"Ninataka iwe Sunnah kwa ummah wangu kuandaa chakula wakati wa harusi zao", akamtaka afanye maandalizi hayo. Kisha Ali ؓ akaweka rehani ngao yake kwa Myahudi mmoja na kununua nusu kipimo ya shayiri, ambayo ilitumika kutengeneza chakula kitamu cha harusi kiitwacho *hays*[125]. *Ansar* na *Muhajirun* walifika makundi kwa makundi kuja kushiriki katika chakula hicho. (Ibn Sad, VIII, 23; Abdurrazzaq, V, 487; Diyarbakri, I, 411)

Baadaye Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza jagi la maji akachukua wudhu. Kisha alimuita Ali ؓ aje mbele yake na kumnyunyuzia maji juu ya kifua na baina mabega yake. Vile vile alimuita Fatimah ؓ akamfanyia hivyo hivyo, akionyesha kuwa amemuozesha kwa

123. Ibn Saad, VIII, 19.

124. Nasai, Nikah, 81.

125. *Hays* ni chakula kilichotengenezwa kutokana na tende, mafuta safi na mtindi uliochunjwa. Wakati mwingine, *sawiq*, au ngano kavu, ilikuwa ikiongezewa.

ndugu yake aliye bora. Kisha aliwanyunyuzia maji nyusoni mwao na nyuma yao na kisha akauomba dua akisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu, ninawaweka wao na kizazi chao katika ulinzi wako dhidi ya shaytan!" (Ibn Sad, VIII, 24; Diyarbakri, I, 411)

Kisha Mtume aliyebarikiwa ﷺ alimuusia Fatimah ؓ kuangalia kazi za nyumbani na akamuusia Ali ؓ kufanya kazi kwa ajili ya kuihudumia familia yake.[126]

Zayd ibn Haritha ؓ anaelezea:

"Nilikuwa nimekaa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pindi Ali na Abbas ؓ walipokuja na kuomba ruhusa ya kuingia kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

'Unajua kwa nini wamekuja?' Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliuliza.

'Hapana, sijui', nilijibu.

'Lakini mimi ninajua', alisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, 'waruhusu waingie.' Hivyo nikawaruhusu.

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tumekuja kuuliza ni nani unayempenda zaidi katika jamaa zake', walisema.

'Fatimah bint Muhammad', alijibu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hatumaanishi familia yako mwenyewe!'

'Kama ni hivyo, jamaa yangu ninayempenda zaidi ni Zayd, ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha kwa uongofu nami nimemtunza.'

'Kisha nani?'

126. Kasani, IV, 24.

‘Ali!’ akajibu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Abbas ﷺ kalalamika akisema: ‘Umemshusha daraja ami yako na kumuweka mwisho’.

‘Lakini Ali lifanya Hijra kabla yako’, Mtume akafafanua.” (Tirmidhi, Manaqib, 40/3819)

Simulizi ifuatayo inasimuliwa na Ibn Abbas ﷺ:

“Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichora chini misitari minne na kutuuliza sababu ya yeye kufanya hivyo.

Tukasema: ‘Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ndio wanaojua zaidi’. Hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema kwa, ‘Wanawake bora wa peponi ni Khadijah bint Khuwaylid, Fatimah bint Muhammad, Maryam bint Imran na Asiyah bint Muzahim, mke wa Fir’aun.’” (Ahmad, I, 293)

Mtukufu Mtume ﷺ aliweka umuhimu wa hali ya juu kabisa katika kuwapatia malezi wanafamilia yake, akawalea kiroho na kuwaandaa kwa ajili ya maisha ya milele. Kwa mfano, kufuatia aya ifuatayo ya Surah al-Ahzab:

يَا نِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِّنَ النِّسَاءِ إِنِ اتَّقَيْتُنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا

"Enyi wake wa Nabii! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msiregeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema. Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishauwe kwa majishauwo ya kijahilia ya kizamani. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt›iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara..." (al-Ahzab: 32-33), kila siku asubuhi, kwa muda wa miezi sita,Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea kusimama kwenye mlango wa Fatimah na kuita, "Amke kwenye Swala enyi watu wa nyumba ya Mtume, kwani Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu na kukusafisheni baarabara" (Tirmidhi, Tafsir, 33/3206)

Kadhalika, katika kuwakumbusha kuhusu sala ya *tahajjud*, ambayo ni mojawapo ya ibada zinazompatia mja neema ya maisha ya milele, wakati fulani Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akigonga kwenye mlango wa Ali na Fatimah na kusema kwa upole, "Mtatekeleza swala?" (Bukhari, Tahajjud, 5)

Katika muktadha huu, Ali رضي الله عنه anasimulia tukio lifuatalo lenye kusisimua:

"Miongoni mwa wanafamilia wote, mtu aliyekuwa anapendwa zaidi na baba yake ni Fatimah. Mikono yake ilikuwa ikitoa kovu kutokana na kuzungusha jiwe la kusagia nafaka na bega lake likiota sugu kutokana na kubeba kiriba cha maji. Kufanya usafi maeneo yote ya nyumbani kulizidi kumuacha akiwa na vumbi mwilini. Wakati fulani baadhi ya watumishi walikuwa wameletwa kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

'Muombe baba yako akupatie mtumishi', nilimshauri.

Hivyo, Fatimah akaenda, lakini alipomuona baba ayke akiongea na watu, akarudi. Siku iliyofuata Mtume wa Mwenyezi Mungu alimtembelea.

'Ni kitu gani hicho ulichokuwa ukikihitaji?' aliuliza. Fatimah alikaa kimya na hakujibu chochote.

'Ngoja nifafanue ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', niliingilia kati na kuanza kumfafanulia.

'Ewe Fatimah, muogope Mwenyezi Mungu na utekeleze aliyoyaamrisha!', Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema. 'Ihudumie familia yako na kabla ya kulala, sema *Subhanallah* mara thelathini na tatu, *Alhamdulillah* mara thelathini na tatu na *Allah Akbar* mara thelathini na nne; yote idadi yake itakuwa mia moja.hiyo ni bora kwako kuliko kuwa na mfanyakazi.'

'Nimemridhia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake', alisema Fatimah. Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakumpatia mtumishi." (Abu Dawud, Kharaj, 19-20/2988)

Katika hadith nyingine pia Mtukufu Mtume ﷺ alisikika akisema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, siwezi kukupa mtumishi hali ya kuwa watu wa *suffa* wanafunga mawe kwenye matumbo yao kupunguza makali ya njaa na huku nikiwa sina uwezo wa kupata cha kuwapa. Ninakusudia kuchukua fidia ya kikomboleo kutoka kwa mateka wale na fidia hiyo itatumika kuwahudumia watu wa *Suffa*!" (Ahmad, I, 106)

Sawban ؓ, ambaye aliwahi kuwa mtumwa na kukombolewa na Mtukufu Mtume ﷺ, anaeleza:

"Fatimah ؓ ndiye aliyekuwa wa mwisho kuagwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pindi anaposafiri. Na ndiye aliyekuwa wa kwanza kutembelewa pindi anaporudi kutoka safarini. Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amerejea kutoka safa-

rini. Fatimah ؓ alikuwa ametundika pazia ghali kwenye mlango wake na kuwavika Hasan na Husayn bangili mbili za fedha. Ingawa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifika mpaka langoni, lakini hakuingia ndani. Haraka sana Fatimah ؓ alitambua kuwa vitu hivyo ambavyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliviona ndivyo vilivyomzuia kuingia. Hivyo akayachana mapazia yale na kuziondoa bangili za fedha kwenye mikono ya watoto wake. Hasan na Husayn wakaenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakiwa wanalia na huku wameshika bangili mikononi mwao. Mtume ﷺ alizishika bangili zile na kuseama:

'Ewe Sawban chukua bangili hizi uwapelekea familia fulani na fulani. Hasan na Husayn wanatokana na mimi (*Ahlul-Bayt wangu)*... sitaki watumie katika maisha haya vitu vizuri ambavyo Mwenyezi Mungu atawajaalia huko Akhera. Kisha mnunulie Fatimah mkufu uliotengenezwa kwa mfupa na bangili za aina hiyo kwa ajili ya Hasan na Husayn.'" (Abu Dawud, Tarajjul, 21/4213)

Ahl'ul-Bayt na kuwapenda

Ahl'ul-Bayt ina maana ya wanafamilia wanaoishi kwenye nyumba moja. Katika maana ya kitaalamu, neno hili linawajumuisha watu wote wa familia ya Mtukufu Mtume, vile vile familia yake ya nje ya nyumba yake. Kwa hivyo, familia ya kwanza kabisa ni ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na kisha familia za Ali, Jafar, Aqil na Abbas. Kama ambavyo ni wajibu kwa Waislamu wote kumtakia rehma na kumtolea salamu (salat'u salam) Mtukufu Mtume ﷺ, ndivyo ilivyo wajibu kuwaheshimu na kuwapenda *Ahl'ul-Bayt.*[127]

Ahl'ul-Bayt hawaruhusiwi kuchukua Zaka. Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alimuona Hasan ؓ akichukua kipande cha tende kutoka

127. Ahmad, VI, 323.

kwenye fungu lililowekwa maalamu kwa zaka katika Hazina na kukiweka mdomoni mwake, haraka sana akamwambia akiteme na kisha akasema:

"Hujui kwamba familia ya Muhammad haichukui Zaka?" (Bukhari, Zakat, 57; Ahmad, I, 200)

Tukio lifuatalo linasimuliwa na Zayd ibn Arqam ﵁:

"Siku moja, tukiwa katika bonde la Hum lililopo baina ya Makka na Madina, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisimama na kuzungumza nasi. Baada ya kutukuza na kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu, alitupa wosia kadhaa uliofuatiwa na maneno yafuatayo:

'Enyi watu! Hakika mimi pia ni mwanadamu. Hivi karibuni nitajiwa na mjumbe kutoka kwa Mola wangu, nitaitika wito wake na kuondoka. Ninakuachieni vitu viwili muhimu. Kimojawapo ni nuru na muongozo ambao humpeleka mtu kwenye ukweli, kitu hicho ni Qur'an. Shikamaneni nayo na msiiache!'

Aliendelea kutuusia kushikamana na Qur'an na kuifuata. Kisha akaendelea kusema:

'Na ninakuachieni *Ahlul-Bayt* wangu. Muogopeni Mwenyezi Mungu na waheshimuni! Muogopeni Mwenyezi Mungu na waheshimuni!'"

Zayd ibn Arqam ﵁ akaulizwa kuwa *Ahlul-Bayt* hasa ni wepi na iwapo wake wa Mtume ﷺ ni miongoni mwao au la.

"Wake zake ni miongoni mwao", alijibu Zayd. "Lakini *Ahlul-Bayt* halisi na wa kweli ni wale ambao wameharamishiwa kuchukua Zaka hata baada ya kufariki kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ."

"Ni wepi hao?"

"Ni familia za Ali, Aqil, Jafar na Abbas." (Muslim, Fadhail'us-Sahabah, 36)

Mtukufu Mtume aliyebarikiwa ﷺ amesema:

"Mpendeni Mwenyezi Mungu kwa baraka alizokujaalieni. Nipendeni mimi kwa ajili ya upendo wenu kwa Mwenyezi Mungu. Na wapendeni Ahlul-Bayt wangu kwa ajili ya upendo wenu kwangu!" (Tirmidhi, Manaqib, 31/3789)

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ, akiwa amewabeba wajukuu zake wapendwa Hasan na Husayn, alitangaza:

"Mwenye kunipenda mimi, akawapenda hawa na wazazi wao atakuwa pamoja nami Siku ya Kiyama." (Tirmidhi, Manaqib, 20/3733)

Maswahaba walikuwa na mapenzi na kuonesha heshima kubwa kwa familia na jamaa wa Mtukufu Mtume ﷺ. Kwa kawaida, mtu hawi na hisia za upendo kwa mpendwa wake tu, bali ukubwa wa upendo alionao humfanya awapende marafiki wa mpendwa wake na hufikia hatua akakipenda kila kitu kinachomfanya amkumbuke mpendwa wake, kama nguo zinazovaliwa, chakula kinacholiwa na kadhalika. Kadiri upendo unavyokuwa ndivyo unavyopenya katika kila kitu kinachomzunguka mpendwa.

Maswahaba walikuwa wakiuruhusu upendo wao kwa Mtukufu Mtume ﷺ utokeze nje kutoka kwenye vina vya nyoyo zao kwa kuonesha matendo mbalimbali, kama vile kushika hatamu za farasi au ngamia ambaye anatumiwa na jamaa wa Mtukufu Mtume ﷺ.[128] Kwa kutambua kwamba Siku ya Kiyama mafungamano yote ya damu yatavunjika isipokuwa mafungamano ya mtu kwa Mtukufu Mtume ﷺ, walikuwa wakifanya juhudi kuoa yeyote katika ndugu

128. Haythami, IX, 348.

wa Mtume ﷺ ili kuimarisha mafungamano yao ya upendo na ujamaa.[129]

Watu wanaotokana na kizazi cha Mtukufu Mtume ﷺ katika zama zetu hizi wanaishi katika maeneo mbalimbali ndani ya ulimwengu wa Kiislamu. Neno *Sayyid* linatumika kuwatambulisha wale wanaotokana na kizazi cha Husayn رضي الله عنه, na *Sharif* hutumika kwa ajili ya wale wanaotokana na kizazi cha Hasan رضي الله عنه. Wauthmaniyyah walimtambulisha *sayyid* kwa sifa ya *amir*, na kilemba anachovaa kichwani mwake kilijulikana kama kilemba cha *amir*. Wanawake wanaotokana na ukoo wa Mtukufu Mtume ﷺ nao pia walikuwa na alama ya kijani katika hijabu zao.

Wauthmaniyyah walilichukulia suala la kuwahudumia *Ahlul-Bayt* kuwa ni wajibu kiasi kwamba walianzisha taasisi rasmi kwa ajili ya lengo hilo. Maofisa walioteuliwa maalumu na kupewa jukumu la kutekeleza huduma hii walijulikana kama *naqibul-ashraf*, nao pia walikuwa wakiteuliwa kutoka katika *Ahlul-Bayt*. Miongoni mwa vipengele mbalimbali vya mahitaji ambayo *naqibul-ashraf* walishughulika nayo ni pamoja na kusajili ukoo wao, vizazi na vifo, kuzuia wasiingie katika imani za zamani (ukafiri), kuwagawia fungu lao la kodi na ngawira na kuhakikisha kuwa wanawake wao hawaolewi na wanaume wasioendana nao.[130]

Kutokana na kuwa warithi wa kizazi cha Mtukufu Mtume ﷺ na heshima ya jukumu walilopewa kulitekeleza, *naqibul-ashraf* walipewa mojawapo ya vyeo vya juu kabisa, wa pili baada ya Khalifa katika itifaki.*Naqibul-ashraf* ndio waliokuwa wa kwanza kula kiapo rasmi cha utii kwa sultani pindi anapoingia madarakani na kumuombea mema, kisha ndipo itifaki nyingine inafuata. Vilevile wa kwanza

129. Haythami, IX, 173.
130. Haythami, IX, 173.

kupewa salamu za pongezi wakati wa sikukuu za eid ni *naqibul-ashraf*, ambapo sultani alikuwa akitoka kwenda kumsalimia wakati wa sikukuu za eid.

Sayyid au *sharif* ambaye amekutwa na hatia ya kutenda kosa au mwenendo usiokubalika alikuwa akishughulikiwa na *naqibul-ashraf*, kama ni Istanbul, ambapo katika maeneo mengine alikuwa akishughulikiwa na gavana wa jimbo husika. Kabla ya kutekeleza adhabu, afisa huyo alikuwa akimvua kilemba cha kijani na kukibusa; kisha hutekeleza adhabu husika.

MWAKA WA TATU WA HIJRA

Uhud: Vita iliyobeba Hekma na Mazingatio

Kama ilivyokuwa kwa Badr, Vita vya Uhud[131] ni mapambano makali dhidi ya waabudu - sanamu wa Makka, yaliyotokea katika mwaka wa tatu wa Hijra, katika mwezi wa Shawwal.

Waabudu masanamu wa Makka walikuwa wametawaliwa na huzuni kubwa kutokana na watu waliowapoteza katika vita vya Badr. Katika vita hivyo kila mtu walikuwa amempoteza ndugu yake wa karibu, jambo ambalo lilitumika kuamsha tamaa yao kubwa ya kulipiza kisasi. Mtu ambaye alikuwa na wahaka kuliko watu wote wa kutaka kupoza uchungu huo alikuwa Hind, mke wa Abu Sufyan, ambaye wakati huo ndiye alishika hatamu ya uongozi wa Maqurayshi (kufuatia kifo cha Abu Jahl). Ndani ya muda mfupi, waliweza kuliandaa jeshi la washirikina elfu tatu, ambao wote walikuwa na joto la kutaka kulipiza kisasi. Bidhaa zilizotokana na msafara ambao Abu Sufyan aliweza kuuokoa wakati akielekea Badr zilitumika kufadhili jeshi hilo. Makabila ya kiarabu yaliyo jirani nayo pia yaliitwa kuja kusaidia.[132]

Wakati huo huo, Abbas, ami wa Mtukufu Mtume ﷺ aliitaarifu Madina juu ya yanayojiri.[133] Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu

131. Uhud ipo takriban maili moja kaskazini mwa mji wa Madina.
132. Waqidi, I, 199-203.
133. Ibn Saad, II, 37.

ﷺ akawakusanya Maswahaba ili kujadili iwapo wabaki Madina na kutumia mbinu ya kujilinda, au watoke nje ya mji kama sehemu ya kuunda safu ya mashambulizi. Mtukufu Mtume ﷺ yeye mwenyewe alitaka watumia mbinu ya kujilinda.[134]

Lakini hatimaye, kutokana na tamaa ya vijana ambao hawakupata bahati ya kushiriki katika vita vya Badr, ambao waliomba kwa hoja kwamba 'wamekuwa wakiisubiri fursa hii kwa muda mrefu', na kutokana na maoni ya wapiganaji mbalimbali wakiongozwa na Hamza رضي الله عنه, iliamuliwa kuwa mapambano dhidi ya washirikina yafanyike nje ya mji wa Madina kwa mbinu ya kushambulia.[135]

Kufuatia maamuzi hayo, Mtukufu Mtume ﷺ aliingia ndani na kuvaa ngao yake ya vita. Wakati huo huo wale waliotaka vita ipiganwe mjini Madina kwa namna ya kujihami, wakiongozwa na Saad ibn Muadh na Usayd ibn Khudayr, waliwashawishi wengine wakiwaambia kuwa "hawakuwa sahihi waliposisitiza kuwa wapigane nje ya mji wa Madina, hali ya kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na maoni tofauti. Kile anachoamrishwa hutoka mbinguni;

---

134. Hiyo ni kwa sababu ya ndoto aliyoiona Mtukufu Mtume ﷺ, ambayo baadaye alielezea:
"Katika ndoto yangu, nilikuwa nikipiga upanga; kichwa chake kikakatika. Hii inabainisha kuhusu matatizo ambayo Waislamu waliyapata katika vita vya Uhud. Kisha nikapiga tena kwa mara nyingine, kwa mara hii upanga ukawa katika hali nzuri zaidi kuliko awali. Hii inaonesha Baraka ya Mwenyezi Mungu katika namna ya ushindi na umoja wa Waislamu. Katika ndoto hiyo hiyo, niliona kundi la ng'ombe na baraka nyingine kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ng'ombe hao ni kundi la Waislamu siku ya Uhud (ambao waliuawa kishahidi). Baraka niliyoiona ilithibitika kupitia ushindi mbalimbali ambao Mwenyezi Mungu alitupatia baada ya Badr na thawabu ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia kama malipo ya subira yetu katika vita vya Badr". (Bukhari, Tabir, 39, 44; Manaqib, 25; Muslim, Ruya, 20)

135. Ibn Hisham, III, 6-7.

hivyo muachieni suala hilo na fanyeni kama anavyokuamrisheni!" (Waqidi, I, 213-214)

Bila kupoteza muda walikimbia haraka kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumwambia: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kamwe hatutaenda kinyume na maoni yako. Fanya lile unaloona kuwa ni sahihi!"

Lakini jibu lake lilikuwa wazi kabisa, akawaambia:

"Pindi mtume anapovaa ngao yake, hawezi kuiondoa ila baada ya vita! Sasa hivi shughulikieni yale ninayowaambia myafanye! Tutoke kwa jina la Mwenyezi Mungu! Iwapo mtaendelea kuwa na subira na kushikilia majukumu yenu, hapo Mwenyezi Mungu atawajaalieni ushindi!" (Waqidi, I, 214; Ibn Sad, II, 38)

Baada ya swala ya Ijumaa, Mtukufu Mtume ﷺ aliondoka Madina akiwa na jeshi la watu elfu moja, huku akiwa amemuacha Abdullah ibn Maqtum kama naibu wake. Lakini walipokuwa njiani, Abdullah ibn Ubayy, kiongozi wa wanafiki, alirudi nyuma akiwa na watu wake mia tatu, na hivyo idadi ya jeshi la Waislamu ikapungua mpaka kufikia mia saba, ambapo kufuatia tukio hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha ufunuo ufuatao:

وَمَا أَصَابَكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ وَلْيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُواْ وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْاْ قَاتِلُواْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوِ ادْفَعُواْ قَالُواْ لَوْ نَعْلَمُ قِتَالاً لاَّتَّبَعْنَاكُمْ هُمْ لِلْكُفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلإِيمَانِ يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِم مَّا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يَكْتُمُونَ

"Na yaliyo kusibuni siku yalipo pambana majeshi mawili yalikuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ili awajue Waumini. Na ili awapambanue walio kuwa wanaafiki, wakaambiwa: Njooni mpigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu au lindeni. Wakasema: Tungeli jua kuna kupigana bila ya shaka tungeli kufuateni. Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko Imani. Wanasema kwa midomo yao yasiyo kuwamo nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anajua kabisa wanayo yaficha." (al Imran: 166-167)

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّىءُ الْمُؤْمِنِينَ مَقَاعِدَ لِلْقِتَالِ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

إِذْ هَمَّت طَّآئِفَتَانِ مِنكُمْ أَن تَفْشَلاَ وَاللَّهُ وَلِيُّهُمَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

"Na pale ulipo toka asubuhi, ukaacha ahali zako uwapange Waumini kwenye vituo kwa ajili ya vita - na Mwenyezi Mungu anasikia na anajua. Makundi mawili miongoni mwenu yakaingiwa na woga kuwa watashindwa - na hali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wao; na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu." (al Imran: 121-122)

Hatua ya wanafiki kujiondoa katika jeshi la Waislamu ilithibitika kuwa bahati iliyojitokeza kwanza kwa sura ya balaa, badala ya kulidhoofisha jeshi ililiimarisha na kulikomaza kiroho kwa kulisafisha dhidi ya kushughulishwa na mambo mawili kwa wakati mooj, wanajeshi waoga. Khiyana ambayo ingeweza kutoka katikati ya mapambano ingeweza kuleta balaa zaidi na kuitikisa nguvu na kujiamini kwa Waislamu.

Shauku ya Maswahaba kufa kishahidi

Amri ibn Jamuh, kiongozi wa ukoo wa Salimah wa jamii ya *Ansar*. Alikuwa mlemavu ambaye watoto wake wanne walikuwa wakishiriki katika vita mbalimbali sambamba na Mtukufu Mtume ﷺ. Pindi Waislamu walipokuwa wakitaka kwenda katika vita vya Uhud, Amr alielezea tamaa yake ya kutaka kuungana nao.

"Sio wajibu kwako kwenda vitani", walisema watoto wake. "Mwenyezi Mungu anakuhesabu kama mtu mwenye udhuru halali. Sisi tutashiriki kwa niaba yako."

Akajibu: "Siku ya Badr mlinizuia nisiingie peponi, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa, hata kama leo nitaendelea kuishi, siku moja nitakufa kishahidi na kuingia Peponi!" Kisha akamgeukia mkewe:

"Unatarajia nitakaa hapa pamoja nawe hali ya kuwa kila mtu anapigania kuingia Peponi kwa kufa kishahidi?". Akaichukua ngao yake na kutoka ndani kuelekea kwa Mtume wa Rehma ﷺ huku aki-omba: "Ewe Mwenyezi Mungu! Unijaalie nisirudi kwenye familia yangu!"

Punde akafika mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ na kumwambia:

"Wanangu wanataka kuniacha Madina. Wananizuia nisitoke kwenda kupigana pamoja nawe, hali ya kuwa wallah ninataka sana kuingia peponi licha ya ulemavu wa mguu wangu!". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Mwenyezi Mungu amekusamehe. *Jihad* sio wajibu kwako."

Amr akajibu: "Lakini, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mung, nawe pia hupendi kuniona nikipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu mpaka mwisho na kisha nitembee kuingia peponi na mguu wangu huu wenye ulemavu?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Bila shaka ninapenda". Kisha akawageukia watoto wa Amr na kuwaambia: "Msimzuie tena baba yenu kushiriki katika vita. Huwenda Mwenyezi Mungu akamjaalia kifo cha kishahidi!"

Amr akaelekea upande wa *qibla* na kuomba dua akisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu, nijaalie shahada na usinifanye nirudi kwa familia yangu nikiwa mwenye huzuni na masikitiko!"

Amr alipambana kiume katika vita vya Uhud. Wakati akipambana alisikika mara kwa mara akiendelea kusema: "Wallah, Pepo ndiyo ninayoitamani." Hatimaye aliuawa kishahidi pamoja na mwanaye mmoja ambaye alikuwa akijaribu kumlinda. Baadaye, Mtukufu Mtume ﷺ alisema kumhusu:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu ipo Mikononi mwake, nilimuona Amr akitembea kwa mguu wake kuingia Peponi." (Waqidi, I, 264-265; Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, IV, 208)

Wakati akikagua jeshi kabla ya kuelekea Uhud, Mtukufu Mtume ﷺ alikataa kuwaruhusu wale waliokuwa wadogo sana kushiriki vitani. Miongoni mwa wale walioonekana kuwa wadogo sana ni Samurah ibn Jundab na Rafi ibn Hadij. Zuhayr ibn Rafi aliingilia kati kumtetea Rafi akisema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Rafi ni mahiri katika utupaji wa mishale!" Tukio kamili linasimuliwa na Rafi mwenyewe:

"Nilikuwa nimesimamia vidole vyangu ili nionekane mrefu. Hatimaye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniruhusu nibaki kundini. Samura aliposikia hivyo akamwambia Muray ibn Sinan,

baba yake mlezi, 'Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amemruhusu Rafi abaki na kuniambia nirudi nyumbani, lakini mimi mpiganaji mzuri sana kuliko Rafi!' Hivyo Muray ﷺ akamkhabarisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuhusu jambo hilo, naye akatutazama sote wawili, mimi na Samurah, akatuambia tupambane. Tulipambana na Muray akanishinda. Kwa matokeo hayo, naye aliruhusiwa kubaki kundini. (Tabari, Tarikh, II, 505-506; Waqidi, I, 216)

Walipofika Uhud, Mtukufu Mtume ﷺ alilipeleka jeshi lake mpaka mbele ya Mlima wa Uhud na kuwaweka watupa mishale hamsini kwenye Kilima cha Aynayn ili kuimarisha ulinzi pindi maadui watakapojaribu kupita kwenye bonde lililo katikati ya vilima hivyo. Alimteua Abdullah ibn Jubayr kuwa kamanda wao na kuwasisitizia akisema: "...wekeni ulinzi nyuma yetu na msitoke mahali hapa kwa hali yoyote ile, iwe tumeshinda au tumeshindwa!" (Ibn Hisham, III, 10; Ahmad, I, 288)

Kama kawaida, kwa mara nyingine Vita vilianza kwa mapambano ya mtu mmoja mmoja, *mubaraza*. Ilimchukua pigo moja tu kwa Ali ﷺ kumdhibiti mbeba bendera wa washirikia, Talha. Ndugu yake, Othman, ambaye alichukua bendera ya Maqurayshi baada ya Talha, hakumsumbua Hamza ﷺ. Hata mbebaji bendera wa tatu hakumtia wasiwasi Saad ibn Abi Waqqas ﷺ.

Vita vilianza kwa ukali. Kabla ukali haujafika kwenye kilele chake cha juu kabisa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua upanga na kuunyanyua juu huku akisema: "Fedheha na aibu ipo katika woga, na heshima na utu vipo katika ushujaa", akauliza:

"Nani anayetaka kuchukua upanga huu kutoka kwangu?"

Maswahaba wote wakanyanyua mikono yao juu wakishindana kuupata huo upanga.

"Ni nani atakayechukua upanga huu kutoka kwangu na kuulipia thamani?" aliuliza Mtukufu Mtume ﷺ ambapo walianza kuhisi uzito kidogo wa kuuchukua. Lakini Abu Dujanah ؓ, kutoka katika *Ansar*, akauliza:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni ipi thamani yake?"

"...ni wewe kupigana na adui mpaka upanga huu upinde na na kujikunja!" alisema Mtukufu Mtume ﷺ.

Nitauchukua na ninaahidi kuilipa gharama yake!" alisema Abu Dujanah.

Baada ya kuuchukua upanga na kilemba chake chekundu kichwani mwake, Abu Dujanah ؓ alianza kutembea kwa tambo katika katikati ya safu, akionekana kuwa mwenye majivuno. Mtukufu Mtume ﷺ alipouona mwendo wake wa kujivuna akasema: "Ile ni aina ya kutembea ambayo Mwenyezi Mungu anaichukia, isipokuwa katika mazingira kama haya!" (Ibn Hisham, III, 11-12; Waqidi, I, 259; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 128)

Muda mfupi baada ya Vita, Muhayriq, mwanazuoni wa Kiyahudi, alisilimu. Alikuwa akitambua vyema kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alisadifiana kikamilifu na sifa zilizoelezwa katika Taurati; lakini hakuweza kulidhihirisha hilo mpaka siku ya vita vya Uhud. Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akielekea Uhud, Maswahaba wakiwa nyuma yake, Muhayriq aliwakaripia Mayahudi wenzake:

"Nina hakika kuwa unatambua vyema kabisa kwamba Muhammad ni mtume na kwamba mnawajibika kumsaidia na kumnusuru!"

Mayahudi hao wakamkejeli wakimwambia:

"Leo ni Jumamosi...Hatuwezi kufanya chochote!"

"hakuna kitu hicho cha Jumamosi kwenu!" Muhayriq alijibu kwa hasira, akachukua upanga wake na chochote kingine alichokihitaji. Kabla ya kuondoka, aliacha ujumbe ufuatao kwa mmoja wa ndugu zake:

"Iwapo nitauawa leo, basi Muhammad ndiye atakayechukua urithi wangu wote. Atautumia katika njia nzuri kama ilivyoelekezwa na Mwenyezi Mungu." Ikawa kama alivyotaka, kwani aliuawa kishahidi katika Vita vya Uhud. Shamba la mitende alililoliacha likachukuliwa na Mtukufu Mtume ﷺ na kulifanya kuwa *waqf*. Mtukufu Mtume ﷺ alimuelezea kwa maneno yafuatayo:

"Muhayriq ni Myahudi bora kuliko Wayahudi wote!" (Ibn Hisham, III, 38; Waqidi, I, 263; Ibn Sad, I, 501-503)

Matukio ya kushangaza yalifuatana moja baada ya jingine katika vita vya Uhud.

Mkazi mmoja wa Madina aitwaye Quzman baada ya kuwaua washirikina saba katika medani ya mapambano alifariki baada ya kujeruhiwa vibaya. Pamoja na hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alitangaza akisema:

"Quzman ni mtu wa Motoni." Hii ni kwa sababu alipopongezwa na Qatadah ibn Numan, wakati akivuta pumzi yake ya mwisho, kwa kupata neema ya kuuawa kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Quzman alijibu:

"Nilipigana kwa ajili ya kabila langu, sio kwa ajili ya kupata shahada", baada ya kusema hivyo akajisukumiza kwenye upanga wake na kujiua. (Waqidi, I, 263)

Kwa upande mwingine, Usayram aliyehisi kujuta kutokana na upinzani wake mkubwa aliokuwa ameuonyesha mwanzo dhidi ya uamuzi wa watu wake kuingia katika Uislamu, alikuja kwa Mtu-

kufu Mtume ﷺ akiwa amejizatiti kwa silaha kutoka kichwani hadi miguuni na kuuliza:

"Je niungane nanyi katika Vita au nisilimu kwanza?"

"Silimu kwanza kisha uungane nasi", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ, ambapo Usayram alisilimu kabla ya vita ambavyo vilishuhudia akiuawa kiashahidi. Mtukufu Mtume ﷺ akasema kuhusu Usayram: "Amefanya kazi kidogo, akapata faida kubwa!" (Bukhari, Jihad, 13; Muslim, Imarah, 144)

Maneno yake ya mwisho kwa wale waliokuwa wakimtazama kwa huzuni akiwa amelala katikati ya majeruhi, ilikuwa ni "Nilikuja kwa ajili ya Uislamu tu, nikapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe Wake; na nijeruhiwa kwa ajili hiyo."

Baadaye Abu Hurayrah رضي الله عنه alimfanya kuwa fumbo ambapo alikuwa akiwauliza Maswahaba wenzake wamwambie jina la "mtu aliyeingia Peponi bila kuswali hata mara moja katika maisha yake." Bila shaka hakuna mwingine zaidi ya Amr ibn Thabit, akijulikana zaidi kama Usayram. (Ibn Hisham, III, 39-40; Waqidi, I, 262)

Wakati wa vita, upanga wa Abdullah ibn jahsh رضي الله عنه ulikatika. Badala yake Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akampa tawi la mtende, ambalo, baada ya kufika mikononi mwa Abdullah lilibadilika na kuwa upanga. Abdullah رضي الله عنه aliutumia upanga huo mpaka alipouawa kishahidi. Upanga huo uliojulikana kwa jina la *Urjun*, baadaye ulinunuliwa na chifu wa Kituruki kwa dinari mia mbili kutoka kwa warithi wa Abdullah رضي الله عنه.[136]

Shambulio la Waislamu lililotokana na hamasa kubwa ambayo haikuwahi kushuhudiwa hapo kabla lilileta ushindi ndani ya kipindi kifupi cha muda; waaabudu masanamu, licha ya wingi wa idadi na

136. Ibn Athir, Usd'ul-Ghaba, III, 195; Diyarbakri, I, 433.

ubora wa silaha walizokuwa nazo walianza kukimbia. Waislamu walianza kuwafukuza waabudu masanamu baada ya kuanza kuwa na uhakika kuwa sasa wameshinda vita, na mara wakaacha kuwafukuza na bdala yake wakageukia kwenye kukusanya mali za ngawira zilizoachwa na waabudu masanamu badala ya kushughuliaka na uhai wao. Hivyo tu, bali hata kundi la watupa mishale, licha ya kukumbushwa kuhusu maelekezo y Mtume ﷺ ya kutoondoka mlimani mpaka watakapoambiwa kufanya hivyo, waliyaacha maeneo yao na kuanza kukimbilia ngawira. Abdullah pekee, kamanda wa watupa mishale hao, na watu wengine saba ndio waliobaki wamesimama kwenye Mlima Aynayn.

Hatua hiyo ilibadilisha hali ya mambo. Khalid ibn Walid, kamanda wa maadui mwenye uerevu na ujanja, sasa alikuwa amepata fursa aliyokuwa akiisubiri kwa muda mrefu yeye na askari wake wa farasi. Kwa shambulio lao la ghafla wakitokea nyuma ya mlima, waliweza kuwaua watupa mishale wanane waliokuwa wamebaki na kuwafyeka kabisa baada ya kushindwa kuhimili uzito wa uvamizi huo. Sasa mashambulizi yalifika mpaka kwenye uwanja wa vita; Waislamu waliokuwa wameshughulishwa na ukusanyaji wa ngawira walishtushwa na shambulio kali kutoa nyuma yao, hali hiyo ikawapa wakati mgumu sana baada ya waabudu masanamu waliokuwa kugundua kuwa hali ya mambo imegeuka na kuwafanya warudi haraka kwenye medani ya vita ili kukamilisha kazi. Sasa jeshi la Waislamu lilikuwa limewekwa katikati. Wakajikuta katika mhemuko wa fujo na vurumai.

Hamza, Bwana wa Mashahidi Wote

Upepo wa bahati uliokuwa ukiwaelekea Maqurayshi ulishuhudia kuuawa kwa Hamza ﵁, shujaa mkubwa wa Uislamu aliyekuwa akizunguka huku na kule katikati ya safu za Waislamu. Hamza

aliuliwa kwa kuchomwa mkuki na Wahshi. Wahshi ambaye wakati huo alikuwa bado yu utumwani alitekeleza zoezi hilo ili tu apate uhuru aliokuwa ameahidiwa na Hindu. Akichemka kwa hisia kali ya kulipa kisasi, Hindu alibadilika na kuwa na hali ya unyama kiasi kwamba alilichomoa ini la Hamza ﷺ na kuling'ata kwa meno yake. Kutokana na tukio hilo akaitwa *akilatul-akbad,* yaani mla maini.

Kuanguka kwa Hamza ﷺ kuliwapeleka wanajeshi wa Kiislamu katika wimbi la majonzi na huzuni. Wakiwa tayari wameingia katika zahma na msukosuko, sasa Waislamu walisambaratika kabisa, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea hali hiyo katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ تَحُسُّونَهُم بِإِذْنِهِ حَتَّى إِذَافَشِلْتُمْ وَتَنَازَعْتُمْ فِي الأَمْرِ وَعَصَيْتُم مِّن بَعْدِ مَا أَرَاكُم مَّا تُحِبُّونَ مِنكُم مَّن يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنكُم مَّن يُرِيدُ الآخِرَةَثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ وَلَقَدْ عَفَا عَنكُمْ وَاللَّهُ ذُوفَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ

"Na Mwenyezi Mungu alikutimilizieni miadi yake, vile mlivyo kuwa mnawauwa kwa idhini yake, mpaka mlipolegea na mkazozana juu ya amri, na mkaasi baada ya Yeye kukuonesheni mliyoyapenda. Wapo miongoni mwenu wanaotaka dunia, na wapo miongoni mwenu wanaotaka Akhera. Kisha akakutengeni nao (maadui) ili akujaribuni. Naye sasa amekwishakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya Waumini." (al Imran: 152)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaonya watupa mishale walioyaacha maeneo yao kwa kuwaita kuwa 'wanaopenda dunia',

na wakati huo huo anawasifu wale walibaki katika maeneo yao na kustahmili kwa kuwaita kuwa 'wanaopenda Akhera.'

Siku hiyo, waabudu masanamu waliwaua Waislamu wengi. Kundi moja miongoni mwao lilijaribu hata kufanya shambulizi ambalo Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akilifikiria na punde mashambulizi yaliyomlenga Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ yakawa yanakuja kwa mfululizo. Talha ibn Ubaydullah ؓ anasema:

"Maswahaba waliposambaratika, waabudu masanamu walijiandaa kufanya shambilio wakaja na kumzunguka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutoka kila upande kiasi kwamba sikujua nimlinde kutokea upande wa mbele, nyuma, kushoto au kulia. Hivyo nilikuwa nikishambua kwa upanga wangu nyuma na mbele bila kuchoka mpaka waliposambaratika." (Waqidi, I, 254)

Malik ibn Zuhayr, mtupa mishale wa waabudu masanamu, alimtupia mshale Mtukufu Mtume ﷺ. Talha ibn Ubaydullah ؓ kwa kutambua kuwa mshale huo ungempata Mtukufu Mtume ﷺ, akafanya haraka sana kuuchomoa mkono wake. Pigo hilo lilimjeruhi Talha kwa kukipasua kidole chake na kukiacha kikiwa kimelemaa.[137]

Maswahaba kadhaa kutoka pande zote mbili za *Ansar* na *Muhajirun* walimzunguka Mtukufu Mtume ﷺ, wakaapa kumlinda mpaka mauti yawakute, wakayalinda maisha yake kwa kuifanya miili yao kuwa ngao yake na kutoondoka. (Ibn Sad, II, 45; Waqidi, I, 240)

Abu Talha ؓ alikuwa mtupa mishale mahiri ambaye alitumia nguvu kubwa sana katika kutupa mishale yake. Siku hiyo pinde mbili au tatu zilivunjika kutokana na nguvu kubwa ya mikono yake.

137. Ibn Saad, III, 217.

Kila aliyemuona akipita karibu yake akiwa na mkoba wa mishale, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akimwambia:

"Peleka mkoba huo kwa Abu Talha!" Kila mara Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akinyanyua kichwa chake kuwatazama waabudu masanamu ambao walikuwa wakishambulia kutoka upande wa nyuma, Abu Talha ؓ alikuwa akimsihi:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wazazi wangu wawe fidia kwa ajili yako! Tafadhali usiinue kichwa chako, kwa maana mishale inayotupwa na waabudu masanamu inaweza kukupata. Naomba uniruhusu niufanye mwili wangu kuwa ngao yako...acha shambulio ambalo litalengwa kwako linipate mimi badala yako!" (Bukhari, Maghazi, 18)

Katika kumlinda Mtukufu Mtume ﷺ, Qatadah ibn Numan ؓ alisimama mbele yake na kuwatupia mishale waabudu masanamu mpaka upinde wake ukaharibika. Mbali na hilo, katika harakati hizo alipigwa na mshale kwenye upande wa kulia wa jicho lake; mboni ya jicho lake ikaanza kuteremka chini kwenye shavu lake. Mtukufu Mtume ﷺ aliguswa na hali hiyo, akaishika mboni ya Qatadah na kuirudisha mahali pake. Jicho hilo lilikuwa na uoni mzuri na kuonekana kuwa bora kuliko jicho lake la pili.[138]

Swahaba wa kike Umm Umarah ؓ ni miongoni mwa wale waliopambana vikali na maadui kwa upinde na mishale yake. Vita vilipokwisha na kurejea Madina, Mtukufu Mtume ﷺ alisikika akisema:

"Kila nilipotazama kushoto na kulia wakati wa vita, nilimuona Umm Umarah akipambana sambamba nami." (Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 479)

138. Hakim, III, 334/5281; Haythami, VI, 113; Ibn Saad, III, 453.

Akiwa amehamasishwa na sifa na dua nyingi alizoombewa na Mtukufu Mtume ﷺ, Umm Umarah ﷺ alimwambia:

"...tuombee kwa Mwenyezi Mungu ili tuweze kuwa majirani zako Peponi!"

Hapo Mtume wa Rehma ﷺ akaomba, "Ewe Mwenyezi Mungu! Wafanye kuwa majirani na marafiki zangu Peponi!" Umm Umarah ﷺ alifurahi sana na kusema, "Kunzia sasa sitajali aina yoyote ya tabu itakayonisibu katika maisha haya!" (Waqidi, I, 273; Ibn Sad, VIII, 415)

Katikati ya joto la vita, katika moja ya mashambulizi makali yaliyolengwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ndugu wa Saad ibn Abi Waqqas ﷺ aitwaye Utbah ambaye alikuwa upande wa waabudu masanamu, alimtupia jiwe Mtukufu Mtume ﷺ. Shambulio hilo lilipelekea kamba mbili za helmeti ya Mtume ﷺ kuchomoka, likampiga shavuni na kuyavunja meno yake; tukio lililotikisa mbingu na ardhi.[139] Mbaya zaidi, Mtukufu Mtume ﷺ aliangukia katika shimo lililochimbwa na Abu Amir kwa lengo la kuwatega Waislamu. Ali ﷺ alimshika mkono mmoja na Talha ibn Ubaydullah ﷺ akamshika mkono wa pili na kumtoa Mtukufu Mtume ﷺ katika shimo hilo. Abu Ubaydallah ibn Jarrah ﷺ, kwa kutumia meno yake,alitoa kishwara kimoja katika vishwara vilivyotoboa shavu ya Mtukufu Mtume ﷺ, na wakati akifanya hivyo alivunja moja ya meno yake mwenyewe ya mbele. Wakati akitoa kishwara ya pili, alilivunja jino lake lingine. Tukio hilo lilitosha kuwahuzunisha na kuwasikitisha Maswahaba wote na hata malaika. Maswahaba waliumizwa sana kwa kushuhudia kitu kisichovumilika, wakamhimiza Mtukufu Mtume ﷺ kuwa:

139. Kwa tukio hili, watoto wa Utbah ibn Abi Waqqas walizaliwa meno yao ya mbele yakiwa yamekatika kama adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. (Ramazanoğlu Mahmûd Sâmî, Uhud Gazvesi, p. 26)

"...walaani maqurayshi!"

Lakini Mtukufu Mtume ﷺ alijibu kwa kusema:

"Sikutumwa kuwa mtu mwenye kulaani, bali nimetumwa kuwa rehma na mwenye kuwalingania watu kwenye njia ya haki. Ewe Mwenyezi Mungu! Waongoe watu wangu kwani hawajui walitendalo!" (Bukhari, Maghazi, 24; Haythami, VI, 117; Waqidi, I, 244-247; Qadi Iyad, I, 95)

Mtume wa Mwenyezi Mungu alipojeruhiwa alisema:

"Hakika Mwenyezi Mungu amewaghadhibikia wale walioujeruhi uso wa Mjumbe Wake!"

Saad ibn Abi Waqqas ؓ anasema:

"Wallah, nilipomsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akitamka maneno hayo, nilipatwa na hasira kubwa ya kutaka kumuua ndugu Utbah kwa kile alichofanya, hasira ambayo sikuwa kuipata hapo kabla na hata baadaye."

Kwa kweli Saad ؓ alipasua safu za maadui akimfuata ndugu yake ili amuue, lakini Mtukufu Mtume ﷺ akamzuia asitekeleze jambo hilo.[140]

Wakati huo Saad ibn Abi Waqqas ؓ alikuwa akiwamiminia mishale waabudu masanamu, huku Mtukufu Mtume ﷺ akimhamasisha kwa kusema , "Rusha mishale yake ewe Saad! Wazazi wangu wawe fidia yako!" Baadaye Ali ؓ ambaye alishuhudia tukio hili alisema:

"Hakika sikuwahi kumsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema kumwambia yeyote kuwa 'wazazi wangu wawe fida yako', isipokuwa kwa Saad." (Tirmidhi, Adab, 61, Manaqib, 26; Ahmad, I, 92)

140. Waqidi, I, 245.

Hata katikati ya kimbunga hiki cha fujo na vurumai, kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu na imani isiyotetereka, Mtukufu Mtume ﷺ, kwa upande mmoja, akipangusa damu usoni mwake, na kwa uapnde mwingine akijilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, alikuwa akiendelea kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika watu wangu hawajui walitendalo, wape muongozo wako!"

Sahl ibn Saad رضي الله عنه anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipojeruhiwa katika vita vya Uhud, Fatimah رضي الله عنها alianza kusafisha damu iliyokuwa usoni mwake huku Ali رضي الله عنه akimmiminia maji. Alipoona kuwa maji alikuwa yanazidisha damu kuendelea kuvuja, Fatimah رضي الله عنها alichukua kipande cha mwanzi akakichoma mpaka kikageuka kuwa majivu, na kisha akapaka kwenye jeraha. Hatimaye damu ilikoma kuvuja." (Bukhari, Jihad, 80; Maghazi, 24; Muslim, Jihad, 101)

Kwa hali hiyo Vita vya Uhud viligeuka kuwa jukwaa la matukio yenye kuhuzunisha. Nguvu ambayo Waislamu walikuwa nayo hapo awali sasa ilikuwa imekwenda upande wa waabudu masanamu. Hali hiyo ilitokea baada ya Waislamu kuyapuuza maelekezo waliyokuwa wamepewa. Ni watu kumi na nne pekee ndio walikuwa wamebaki pembezoni mwa Mtukufu Mtume ﷺ. Kwa upande wa watu wengine, ambao walijikuta katika hali nzito ya kuchanganyikiwa, Mtume wa rehma ﷺ aliwaita kwa sauti akisema:

"Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! Njooni kwangu, hakika mimi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu niko hapa!" (Waqidi, I, 237)

Qur'an Tukufu inatuletea picha ya tukio hilo katika maneno yafuatayo:

إِذْ تُصْعِدُونَ وَلاَ تَلْوُونَ عَلَى أَحَدٍ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِي أُخْرَاكُمْ فَأَثَابَكُمْ غُمَّاً بِغَمٍّ لِّكَيْلاَ تَحْزَنُواْ عَلَى مَا فَاتَكُمْ وَلاَ مَا أَصَابَكُمْ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

"Pale mlipo kuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote, na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu. Mwenyezi Mungu akakupeni dhiki juu ya dhiki, ili msisikitike kwa yaliyo kukoseeni wala kwa yaliyo kusibuni. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda." (al-i Imran: 153)

Kundi lingine la Waislamu ambao walikuwa wamesikia habari za uvumi zilizozagaa kwa kasi kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa ameuawa, waliingiwa na ubari kiasi kwamba baadhi yao, wakiwaza kuwa **'...hakuna sababu ya kubaki hasa baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kuuawa'**, walianza kuondoka kwenye medani ya vita. Huku wakiwa wanarudi, hifadhi pekee waliyokuwa nayo akilini mwao ni mji wa Madina, ingawa hata hivyo walishawishiwa na wanawake wa Madina wasifanye hivyo.

Kundi lingine likiwaza kuwa **'...hata kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekufa, Mwenyezi Mungu yu hai'**, hawakupoteza uvumilivu wao, waliendelea kupambana. Miongoni mwa Maswahaba wa kundi hili ni Anas ibn Nadr ؓ, ami wa swahaba maarufu Anas ibn Malik. Baada ya kupokea uvumi wenye kutisha,kutoka kwa baadhi ya Waislamu waliokuwa wamepoteza matumiani yote,kwamba Mtukufu Mtume ﷺ naye ameuawa, wasijue la kufanya mbele ya hali ya kukata tamaa, Anas ibn Nadr ؓ alisema kwa sauti

maneno yafuatayo, akionyesha imani thabiti na utegemezi wake kwa Mwenyezi Mungu aliokuwa nao ndani ya moyo wake:

"Kuna sababu gani ya kuishi baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Njooni tupambane na tuuawe kama yeye!" Kisha alianza kuwashambulia waabudu masanamu kwa upanga wake, ambapo baadaye alipatwa na majeraha nane, akauawa kishahidi. (Ahmad, III, 253; Ibn Hisham, III, 31)

Anas ﷺ anasimulia yafuatayo:

"Ami yangu Anas ibn Nadr hakuwa ameshiriki katika vita vya Badr, jambo ambalo alishindwa kulivumilia. Alimwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwamba '...hakika Mwenyezi Mungu ataona nitakayoyafanya iwapo nitajaaliwa fursa ya kushiriki katika vita dhidi ya waabudu masanamu!'

Hivyo alipata bahati ya kushiriki katika vita vya Uhud. Pindi Waislamu walipoanza kutawanyika, alisema kwa niaba ya Waislamu wenzake, 'Mola wangu! Ninakuomba msamaha kwa niaba yao'; kisha akasema huku akiwakusudia waabudu masanamu, '...na Ewe Mwenyezi Mungu, ninajiweka mbali na yale wanayoyafanya.' Kisha alisonga mbele ambapo alikutana na Saad ibn Muadh akamwambia, 'Ewe Muadh, Pepo ndiyo ninayoitafuta; na ninaapa kwa Mola wa Kaabah, ninahisi harufu ya pepo ikitokea pambizoni mwa Uhud!'

Baadaye, wakati akimsimulia tukio hilo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Saad alikiri akisema:

'Sikuweza kufanya yale aliyoyafanya!'

Hatimaye tulimkuta ami yetu akiwa ameuawa. Mwili wake ulikuwa ukining'inia juu panga nane, ukiwa na majeraha ya mkuki na mshale. Waabudu masanamu walikuwa wameukataka-

ta mwili wake. Sehemu nyingi za mwili wake zilikuwa hazionekani, sababu iliyofanya awali asitambuliwe na yeyote. Ni dada yake pekee ndiye aliyeweza kumtambua. Alimtambua kutokana na vidole vyake.

Aya hii iliteremka katika kumuelezea ami yangu na wengine mfanowe:

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا

'Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.' (al-Ahzab, 23)" (Bukhari, Jihad, 12; Muslim, Imarah, 148)

Idadi kubwa ya wale waliokuwa wameanza kutoka katika medani ya vita baada ya mambo kubadilika, walikuwa na nia ya kuendelea na vita nje ya medani hiyo. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambia katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ كُنتُمْ تَمَنَّوْنَ الْمَوْتَ مِن قَبْلِ أَن تَلْقَوْهُ فَقَدْ رَأَيْتُمُوهُ وَأَنتُمْ تَنظُرُونَ

"Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti kabla hamjakutana nayo. Basi sasa mmekwisha yaona na huku mnayatazama." (Al-i Imran: 143)

Wale ambao, licha ya kusisitiza kuwa walikuwa tayari kufa, wakakimbia baada ya kusikia uvumi wa uongo wa kifo vha Mtukufu Mtume ﷺ, walilaumiwa vikali na Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلاَّ رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىَ عَقِبَيْهِ فَلَن يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakaye geuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanao mshukuru." (Al-i Imran: 144)

Katika kuikabili mikasa yote hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ alisimama imara kama Nyota ya Kasikazini na kukabiliana na mashambulizi hayo kwa azma ya kiutume; ujasiri wa kishujaa ulioweka kilelezo cha mfano kwa Maswahaba wake, akitoa mwangwi adhimu wa maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلاَ تَهِنُوا وَلاَ تَحْزَنُوا وَأَنتُمُ الأَعْلَوْنَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِين إِن يَمْسَسْكُمْ قَرْحٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ قَرْحٌ مِّثْلُهُ وَتِلْكَ الأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ النَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُواْ وَيَتَّخِذَ مِنكُمْ شُهَدَاء وَاللَّهُ لاَ يُحِبُّ الظَّالِمِينَ

"Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini. Kama yamekupateni majaraha, basi na hao watu wengine yamewapata majaraha mfano wa haya. Na siku za namna hii tunaweletea watu kwa zamu, ili Mwenyezi Mungu awapambanue walio amini na awateuwe miongoni mwenu mashahidi. Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhaalimu." (Al-i Imran: 139-140)

Kwa fadhila na rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mtume Wake na kwa Waumini wake, licha ya vurumai zote zilizotokea siku ya vita vya Uhud, waabudu masanamu hawakuweza kufikia lengo lao. Wakati huo huo, Maswahaba walianza kujikusanya tena pembezoni mwa Mtukufu Mtume ﷺ wakajipanga kuzuia mashambulizi ya waabudu masanamu, wakamlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷻ kwa ulinzi wa hali ya juu, punde wakaanza kuwashambulia kwa nguvu waabudu masanamu kama awali. Kwa kutumia fursa ya kurejea kwa uthabiti, Mtukufu Mtume ﷺ alilelekeza jeshi lake juu ya mlima wa Uhud. Ingawa mara hii Abu Sufyan alijaribu kufanya mashambulizi kutokea juu ya mlima, lakini juhudu zake hazikuzaa matunda.

Katika muda huo wenye kuogofya sana, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwahurumia Waislamu kwa kuwapatia hali ya kuhisi usingizi na punde wakajikuta wakizama katika usingizi mwanana wenye amani. Walikuwa hawawezi hata kushika panga zao, na walikuwa wakianguka chini mara kwa mara kutokana na uchovu. Waislamu pekee ndio waliojaaliwa hali hiyo ya kuapata usingizi; wanafiki wachache wenye shaka miongoni mwao hawakuweza hata kupepesa jicho, wakitapatapa kutoka katika hali moja ya khofu kwenda hali nyingine, wakiwa na wasiwasi kuwa waabudu masanamu wangeweza kuja na kuwaua.[141]

Kulikuwa na vita fupi ya maneno, kwa upande mmoja, baina ya Abu Sufyan na Omar رضي الله عنه.[142] Akijiandaa kuondoka, Abu Sufyan akiwa amechukizwa na kutoapata matokeo ya wazi aliyoyatamani, alisema kwa sauti:

"Tukutane tena Badr mwaka ujao!"

141. Bukhari, Maghazi, 18, 20; Waqidi, I, 295-296.
142. Ibn Hisham, III, 45.

Omar ﷺ alisubiri kusikia ni jibu gani ambalo Mtukufu Mtume ﷺ angelitoa. Kisha akamwambia Omar ﷺ aseme kumwambia Abu Sufyan, "Allah akipenda, hayo ndiyo yatakayokuwa makutano yetu mwaka ujao!" (Ibn Hisham, III, 45; Ibn Sad, II, 59)

Waabudu masanamu walikuwa wakirudi nyuma kwa sababu mbegu za hofu zilikuwa zikiinyemelea migongo yao. Miongoni mwa miujiza ambayo Mtukufu Mtume ﷺ alijaaliwa ni uwezo wa kutia khofu katika safu za maadui, bila kujali wapo mbali naye kwa kiwango gani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

سَنُلْقِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُواْ الرُّعْبَ بِمَا أَشْرَكُواْ بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَأْوَاهُمُ النَّارُ وَبِئْسَ مَثْوَى الظَّالِمِينَ

"Tutazitia khofu nyoyo za walio kufuru kwa vile walivyo mshirikisha Mwenyezi Mungu na washirika ambao hakuwaterem-shia hoja yoyote. Na makaazi yao ni Motoni; na maovu yaliyoje maskani ya wenye kudhulumu!" (Al-i Imran: 151)

Hivyo, waabudu masanamu, kutokana na kuathiriwa na khofu iliyotiwa katika nyoyo zao, hawakuweza hata kuthubutu kuuvamia mji wa Madina ambao haukuwa na ulinzi, licha ya uwezo wa muda waliokuwa wameupata dhidi ya Waislamu. Aidha, hawakurudi hata na mateka mmoja Muislamu. Hakika hii ilikuwa fadhila ya Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya Mtume Wake na juu ya Waumini.

Wakati waabudu masanamu wakiondoka Uhud, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaamuru Waislamu kujipanga katika mistari ili apate '...kumhimidi na kumuomba Mwenyezi Mungu.'

Maswahaba walijipanga katika mistari nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ambaye alianza kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Shukrani na himidi ni zako! Hakuna awezaye kuzuia yale ambayo umeyanyoosha na kuyastawisha na hakuna awezaye kuyanyoosha na kuyastawisha yale ambayo umeyazuia! Hakuna awezaye kuyanyoosha yale ambayo umeyapindisha na kumpotosha yule ambaye umemuongoza! Hakuna awezaye kutoakile ambacho umekizuia, na kuzuia kile ambacho umekitoa! Hakuna awezaye kukikurubisha kile ambacho umekibaidisha na kukibaidisha kile ambacho umekikurubisha!

Mola wangu! Tunyunyizie rehma, neama, fadhila na baraka zako! Mola wangu! Ninakuomba baraka za milele ambazo hazitabadilika wala kunyauka! Mola wangu! Ninakuomba baraka wakati wa ufakiri na usalama wakati wa khofu! Mola wangu! Ninajilinda kwako kutokana na shari za kile unachokitoa na kile unachokizuia!

Mola wangu! Tujaalie iman; ipambe nyoyo zetu kwa imani! Tufanye tuichukie *kufr*, uonevu na uasi! Tujaalie kuwa miongoni mwa wale wanaojua yenye manufaa hapa duniani na Akhera, wale uliowaongoza kwenye njia ilinyooka!

Mola wangu! Tufishe tukiwa Waislamu na utuhuishe tukiwa Waislamu! Tujaalie kuwa katika kundi la watu wema, usitufanye tupoteze heshima na utu wetu na kustahikiwa adhabu!

Mola wangu! Waangamize makafiri na wale wanawapinga Mitume Wako na kuwapoteza watu dhidi ya njia yako iliyonyooka! Waingize katika naqma na adhabu yako! Mola wangu! Waangamize makafiri uliowapa Vitabu! Hakika Wewe ni Mola wa haki na Kweli...Amiin!" (Ahmad, III, 424; Hakim, I, 686-687/1868; III, 26/4308)



Saad ibn Rabi': Swahaba aliyefunga Mlango wa Udhuru

Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma swahaba wake mmoja kwenda katika medani ya vita kwa matumaini ya kumtafuta Saad ibn Rabi'. Alitafuta sana, lakini Swahaba huyo hakuweza kumpata Saad ibn Rabi'. Sauti zake za kuita hazikujibiwa. Akiwa amepoteza matumaini, aliita kwa mara ya mwisho:

"Ewe Saad! Nimetumwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ili kuona kama upo miongoni mwa walio hai au mashahidi!"

Papo hapo, akiwa anavuta pumzi zake za mwisho na akiwa hana nguvu za kuitika, aliposikia kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na wasiwasi kuhusu hali yake, Saad alikusanya nguvu zake zote zilizobaki, akaitika kwa sauti dhaifu yenye maumivu:

"Sasa hivi nipo miongoni mwa waliokufa!" Wakati huo alikuwa akivuta pumzi zake za mwisho na akiona kule anakokwenda.

Swahaba akamkimbilia Saad ﷺ. Mwili wake ulionekana kuwa na majeraha mengi ya upanga. Saad alikuwa na akiba moja tu ya nishati na hivyo akamnong'oneza yule swahaba maneno ya ajabu yafuatayo:

"Wallah, katika wakati ambapo macho yako yanatikisika, kama hutamlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ dhidi ya maadui zake mkaruhusu kitu kibaya kimkute, hamtakuwa na udhuru wowote utakaoupeleka mbele ya Mwenyezi Mungu!" (Muwatta, Jihad, 41; Hakim, III, 221/4906; Ibn Hisham, III, 47)

Saad ibn Rabi' ﷺ akauaga ulimwengu huu baada ya kutamka maneno haya ya kukumbukwa na *ummah* wote na kushikamana nayo.

Mashahidi wa Uhud

Pindi waabudu masanamu walipoondoka moja kwa moja katika medani ya Uhud, Mtukufu Mtume ﷺ na Waumini waliteremka kwenye medani hiyo ili kuwazika mashahidi wao. Waliokufa ni watu sabini, wakiwemo mashujaa Hamza na Musab ibn Umayr ﷺ.

Musab ibn Umayr ﷺ, mbeba bendera ya jeshi la Waislamu, aliuawa wakati akijaribu kumlinda Mtukufu Mtume ﷺ. Hapo malaika mmoja alitokea katika sura ya Musab na kuichukua bendera. Mtukufu Mtume ﷺ akiwa hajui kuwa Musab ameshauawa, alimuamuru kuwa:

"Songa mbele ewe Musab, songa mbele!"

Hapo mbeba bendera huyo akageuka na kumtazama Mtukufu Mtume ﷺ, naye akamtambua malaika huyo, hivyo akajua kuwa Musab ameshauawa. Ingawa baadaye mwili wake ulipatikana, lakini Waislamu hawakuweza kupata sanda ya kutosheleza mwili wake. (Ibn Sad, III, 121-122)

Wakiifunika sehemu ya juu ya mwili wake kwa ngu aliyokuwa nayo ingefanya sehemu ya chini kubaki wazi; na wangefunika sehemu ya chini, sehemu ya juu ingebaki kuwa wazi. Hivyo Maswahaba wakaenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ kutaka kujua jinsi watakavyoshughulikia mwili huo. Mtume wa Rehma ﷺ aliwashauri waifunike sehemu ya juu ya mwili wa Musab kwa kutumia nguo zake na watumie nyasi zinazonukiwa vizuri kufunika sehemu yake ya chini.

Angalia, Musab alizaliwa katika mojawapo ya familia bora na tajiri kabisa katika mji wa Makka. Takriban vijana wote wa Makka walikuwa wakimhusudu. Inasemekana kuwa hata wasichana walikuwa wakinyunyizia maua mazuri katika njia anayopita. Lakini, licha ya shinikizo lote kutoka kwa familia yake, alichagua kuwa pamoja na Mtukufu Mtume ﷺ, akaacha utajiri wote wa familia yake. Shauku kubwa aliyekuwa nayo ya kushikamana na Mtukufu Mtume ﷺ ndiyo iliyompatia heshima kubwa kiasi kwamba malaika alichukua sura yake huku yeye akiwa ameuawa na kulala katika medani ya Uhud.Huo ni utukufu na shukrani ambazo Mwenyezi Mungu alizitoa kwa mhanga wote uliotolewa na Musab.

Tukio hili lenye kugusa nyoyo liliacha athari kubwa na ya kudumu kwenye nyoyo za Waislamu. Miaka mingi baadaye, baada ya Waislamu kupata nguvu na mamlaka, mtoto wa Abdurrahman ibn Awf رضي الله عنه alimletea babake, ambaye alikuwa miongoni mwa Maswahaba matajiri, chakula cha aina mbalimbali ili aweze kufuturu. Kwa hisia kubwa akasema:

"Musab aliuawa katika Vita vya Uhud. Alikuwa bora kuliko mimi. Lakini alizikwa katika kipande kimoja tu cha nguo. Kipande hicho kilikuwa kidogo kiasi kwamba tungemfunika sehemu ya kichwa, miguu yake ingebaki wazi, na kama tukiifunika sehemu ya miguu yake basi kichwa nacho kingebaki wazi. Baadaye tulijaaliwa utajiri wote wa dunia...na ninahofia kuwa tayari tumelipwa kwa

matendo yetu yote hapa duniani." Kisha Abdurrahman ﷺ akaanza kulia sana na kukiacha chakula bila hata kukigusa. (Bukhari, Janaiz, 27)

Katika mashahidi wote wa Uhud, ni Hamza ﷺ, shujaa na kamanda wa jeshi la Kiislamu ambaye aliupeleka moyo wa Mtukufu Mtume ﷺ na nyoyo za Waislamu kwenye huzuni na majonzi makubwa.

Safiyya ﷺ alikimbia haraka kwenda kwa mashahidi ili kumtafuta baba yake, Hamza ﷺ. Akakutana na mwanaye, Zubayr ibn Awwam ﷺ ambaye alimwambia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekuamrisha urudi."

Safiyya aksema: "Kwa nini? Kwa hiyo sitamuona kaka yangu? Nimeshasikia kwamba ameuawa. Lakini amepatwa na haya kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata hivyo jicho letu halijapata kutua kwa kumuona. *Inshaallah* nitavumilia ana kutaraji malipo yake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Zubayr akaenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumpa ujumbe kutoka kwa mamaye.

Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia: "Basi mruhusu akamuone!" Safiyya akaenda kusimama na kuomba dua karibu na mwili wa Hamza. (Ibn Hisham, III, 48; Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 349)

Zubayr ibn Awwam ﷺ anasimulia kilichotokea hapo katika hali ya hisia ya hali ya juu kabisa inayoonesha udugu wa Kiislamu wenye kustahiki kuigwa.

"Mama yangu alitoa vitambaa viwili vya nguo alivyokuwa amekuja navyo na kusema, 'nimekuleteeni hivi vitambaa ili mvitumie kama sanda ya Hamza.' Tulivichukua vitambaa hivyo na kwenda mahali ulipokuwa mwili wa Hamza. Hata hivyo, jirani yake palikuwa na mtu mwingine aliyeuawa kishahidi kutoka katika jamii

ya *Ansar*, ambaye hakuwa na sanda. Tuliona haya kumvika Hamza vitambaa vyote huku tukimuacha yule shahidi mwingine bila sanda, hivyo tukaamua kumshonea kila mmoja kitambaa kimoja. Lakini kwa kuwa kitambaa kimoja kilikuwa kikubwa zaidi ya kingine, tulifanya kura ili kuchukua uamuzi." (Ahmad, I, 165)

Maelezo haya yenye kusisimua yanaonesha kwamba hisia za udugu kwa msingi wa imani zilikuwa zimeshika hatamu badala ya ujamaa na udugu wa damu.

Wakati huo, mashahidi nane waliletwa jirani na mwili wa Hamza ﷺ, na baada ya kuswaliwa wakazikwa, huku Hamza ﷺ akisubiri mashahidi wengine wanane waletwe na ndipo akazikwa pamoja nao. Kwa hali hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ alimsalia mara mbili ami yake mpendwa, bwana wa mashahidi.[143]

Kwa mujibu wa taarifa ya Jabir ﷺ, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaleta mashahidi wa Uhud wakiwa wawili wawili, akiwalekeza katika upande wa Qibla mashahidi hao kulingana na walivyoielewa na kuishi kwa mujibu wa maisha ya Qur'an. (Bukhari, Janaiz, 73, 75)

Ili kukusanya taarifa kutoka Uhud, bibi Aisha ﷺ alitoka nje ya mji wa Madina akiwa na kundi la wanawake. Alipofika jirani na Harra, alikutana na mwanamke mwema, Hind bint Amr ﷺ ambaye alikuwa akirejea Madina akiwa amebeba miili ya mumewe, Amr ibn Jamuh, mwanaye wa kiume, Khallad na kaka yake, Abdullah.

"Kuna habari gani kutoka Uhud?" bibi Aisha ﷺ aliuliza kwa shauku kubwa.

"Yote ni kheri kabisa", alijibu. "Mtume wa Mwenyezi Mungu ni mzima na hajambo. Hakuna mambo mengineyo!"

143. Ibn Majah, Janaiz, 28.

"Ni watu gani hao?" aliuliza Aisha ؓ akiashiria miili iliyokuwa imebebwa juu ya ngamia.

"Mume wangu Amr, kaka yangu Abdullah na mwanangu Khallad", alijibu mwanamke huyo mwema aitwaye Hind.

"Unawapeleka wapi?"

"Ninawapeleka Madina, ambapo nitawazika." Kisha Hind aliajaribu kumchochea ngamia ambaye alikuwa ameanza kupunguza mwendo, lakini ngamia yule akasimama kabisa na kupiga magoti.

"Je ni kwa sababu ana mzigo mkubwa sana?" aliuliza Aisha ؓ.

"Sijui. Siku zote ana uwezo wa kubeba mara mbili ya mzigo huu. Yaonekana kuna jambo limemtokea sasa hivi!"

Alipolazimishwa kusimama, ngamia huyo aliinuka lakini anapoelekezwa upande wa Madina anarudi tena kukaa chini. Lakini apoelekezwa upande wa Uhud alianza kutembea. Hind alimtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu hali hiyo akimtaka ushauri.

"Huyo ngamia ameamrishwa. Je Amr aliacha wosia wowote?"

"Muda mfupi kabla ya Amr kuanza safari ya Uhud alielekea upande wa qibla na kuomba akisema, 'Ewe Mwenyezi Mungu, nijaalie kifo cha kishahidi; usinirejeshe nyumbani nikiwa mwenye huzuni na maumivu.'" Alifafanua bibi Hind.

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Ndiyo maana ngamia hataki kuendelea na safari. Enyi Ansar, yeyote miongoni mwenu aliyeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu anatakiwa kushikamana na maneno yake. Ewe Hind, mumeo Amr ni miongoni mwa watu wema. Tangu alipouawa, malaika walimfunika kwa mbawa zao na kumtafuta mahali bora pa kumzika. Mumeo Amr, mwanao Khallad na kaka yako Abdullah watakutana Peponi kama jamaa."

Aliposikia maneno haya, Hind alitamani sana kuungana tena na mumewe mwema, Amr, katika maisha ya milele. Hivyo akamsihi Mtume ﷺ akisema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tafadhali niombee kwa Mwenyezi Mungu ili nami niungane nao." (Waqidi, I, 264-265; Ibn Hajar, Fath'ul-Bari, III, 216; Ibn Abdilbarr, III, 1168)

Kulikuwa na tukio lingine la kusisimua.

Siku ya Uhud, mji wa Madina ulitikiswa na habari kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa ameuawa. Hofu kubwa na vileo vilitanda angani kiasi kwamba mwanamke mmoja wa Kianswar, aitwaye Sumayra ؓ, licha ya kuambiwa kuwa mumewe, watoto wake wawili na kaka yake walikuwa wameuawa katika medani ya vita, hakushituka hata kidogo, bali wasiwasi wake haukutulia kabla ya kupata habari kama Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa salama. Hivyo muda wote alikuwa akiuliza:

"Yuko salama?"

Hatimaye alipata jawabu alilokuwa akilitarajia kutoka maswahaba waliokuwa wakirejea kutoka vitani:

"Ndiyo. *Alhamdulillah*, ni mzima na hajambo!"

Lakini Sumayra ؓ hakuridhika sana.

"Nionesheni alipo ili moyo wangu upate kutulia", alisema. Walipomuonesha, akamkimbilia Mtukufu Mtume ﷺ akashika upande wa kanzu yake na kusema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, wazazi wangu wawe fidia kwako... madamu upo hai basi sina jambo linalonipa wasiwasi tena!" (Waqidi, I, 292; Haythami, VI, 115)

Tukio lifuatalo linasimuliwa na Bashir ibn Aqrabah ؓ:

"Baada ya kugundua kuwa baba yangu Aqrabah alikuwa ameuawa katika vita vya Uhud (nikiwa bado mtoto), nilielekea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ nikilia. 'Kwa nini walia mwanangu? Je hutaki mimi niwe baba yako na Aisha awe mama yako?' aliniuliza.

Nikajibu: 'Wazazi wangu wawe fidia kwako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu; hakika ninapenda hivyo'. Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akakipapasa kwa upendo kichwa changu. Mpaka sasa, japokuwa nywele zangu zote zimebadilika rangi, mahali paliposhikwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu pamebaki kuwa na weusi." (Bukhari, at-Tarikh'ul-Kabir, II, 78; Ali al-Muttaqi, XIII, 298/36862)

Tukio lingine linaloonesha kiuu ya maswahaba kutamani kifo cha kishahidi linasimuliwa hapa chini na Jabir رضي الله عنه:

"Usiku ule kabla ya vita vya Uhud, baba yangu aliniita na kuniambia, 'Ninahisi kuwa kesho nitakuwa mtu wa kwanza kufa kishahidi miongoni mwa Maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mbali na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wewe ndiye mpendwa zaidi ninayemuacha katika maisha haya. Nina madeni; yalipe. Siku zote watendee wanao wema wa hali ya juu!'

Kweli kama alivyosema, baba yangu ndiye aliyekuwa wa kwanza kuuawa katika vita vya Uhud. Nilimuweka katika kaburi moja pamoja na shahidi mwingine. Baadaye nikataka kumzika katika eneo la peke yake. Hivyo, miezi sita baadaye, nilimfukua, nikamshika, alikuwa kama nilivyomuweka mwanzo kabisa, isipokuwa sehemu ya sikio lake. Niliendelea na kumuweka katika kaburi la peke yake." (Bukhari, Janaiz, 78)

Siku moja mashahidi wa Uhud walipotajwa, katika kubainisha daraja ya mashahidi hao waliokufa kishujaa, Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Wallah, furaha iliyoje lau ningekufa kishahidi na kila usiku nikiutumia chini ya mlima wa Uhud!" (Ahmad, III, 375)

Mara nyingine, Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alipowatembelea mashahidi wa Uhud, alisema:

"Hakika mimi ni shahidi wa imani na uthabiti wao!"

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, je sisi sio wenzao?" aliuliza Abu Bakr ؓ. "Tuliingia katika Uislamu kama walivyofanya wao, na kushiriki katika vita kama wao."

"Hilo ni kweli", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ, "lakini sijui mtakayozusha baada yangu."

Abu Bakr ؓ alijawa na huzuni na kulia sana, akauliza, "kwa hiyo tutaendelea kuwepo baada yako?" (Muwatta, Jihad, 32)

Wasiwasi wa Abu Bakr ؓ unaonesha mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuonesha kwa nini Qur'an ilimpa sifa ya kuwa 'wa pili katika wawili, wa tatu akiwa Mwenyezi Mungu.'

Maswahaba walimpenda sana Mtukufu Mtume ﷺ kuliko yeyote yule, na hata kuliko nafsi zao. Wanapokuwa nyumbani wakaanza kumfikiria Mtukufu Mtume ﷺ walikuwa hawawezi kukaa tena mahali hapo; walikuwa wakihisi kuwa mahali walipokaa palikuwa hapawatoshi kabisa. Wakishamfikiria Mtume walikuwa wakishindwa kukaa kabisa na badala yake hunyanyuka haraka na kwenda mbio kwa Mtukufu Mtume ﷺ ili wapate utuvu kwa kukaa mbele yake na kupata amani katika mazungumzo yake.[144]Kama wasipomuona, walikuwa wakishindwa kustahmili. Hofu ya kuwa mbali naye peponi ilitosha kuwafanya wasawijike na kuwachanganya

144. Kastallani, II, 104.

kabisa.[145] Rabia ﷺ alipoambiwa na Mtukufu Mtume ﷺ kumuomba kitu, aliomba kuwa pamoja naye Peponi.[146] Katika nyakati za mwisho za uhai wao, Maswahaba walikuwa wakijisikia furaha kwamba wanakwenda kuungana kwa mara nyingine na Mtukufu Mtume ﷺ.[147] Ndiyo sababu kwamba baada ya Uislamu, kitu walichokifurahia sana ni *hadith* isemayo, "Mtu atakuwa pamoja na yule anayempenda."[148]

Aya sitini za Surat al-i Imran zinazungumzia vita vya Uhud. Abdurrahman ibn Awf ﷺ alipoombwa na Miswar ibn Mahramah kuelezea kuhusu vita hivyo, alijibu:

"Soma surah Al-i Imran kuanzia aya ya120 na kuandelea utahisi kana kwamba ulikuwa pamoja nasi katika vita vya Uhud!" (Ibn Hisham, III, 58; Waqidi, I, 319)

Tunaipenda Uhud nayo yatupenda

Uhud ilikuwa na nafasi maalumu ndani ya moyo wa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ. Katika kipindi chote cha uhai wake –baada ya tukio la Uhud- alikuwa akifanya ziara eneo la Uhud pamoja na kuwazuru mashahidi waliozikwa huko, na mara zote akisema:

"Tunaipenda Uhud, nayo yatupenda!" (Bukhari, Jihad, 71; Muslim, Hajj, 504)

145. Qurtubi, V, 271.
146. Muslim, Salat, 226; Ahmad, III, 500.
147. Ahmad, I, 8; Ibn Majah, Janaiz, 4.
148. Bukhari, Adab, 96.

Kwa kutukuzwa na maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ na kwa kunyeshelezewa kwa upendo wa Mtume ﷺ, Uhud, mapumziko ya mashahidi, ilipata daraja kubwa na adhimu ya kuwa maonesho ya kukumbukumbu za Vita hivyo kwa *ummah* wote utakaokuja baadaye mpaka Saa ya Mwisho.

Wasiwasi wa kwamba Uhud ingekuja kuonekana kama eneo baya kwa Waislamu kutokana na matokeo ya Vita na labda hisia mbaya za uadui wa kuichukia Uhud ndiyo sababu iliyomfanya Mtukufu Mtume ﷺ aweke wazi upendo wake kwa eneo hili kwa kusema, 'tunaipenda Uhud na Uhud inatupenda.' Kutokana na upendo huu wa Mtume wa Rehma ﷺ, Uhud haikuangaliwa kama medani ya kushindwa, balieneo tukufu ambalo ndani yake kuna miili mitukufu ya mashujaa wa Uhud.

Kwa upande mwingine, jambo la kwamba Uhud inamtambua na kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ inatoa ushuhuda wa wazi katika kuunga mkono ukweli wa kwamba viumbe wote wanamjua na kushuhudia utume wake. Mtukufu Mtume ﷺ anaeleza:

"Kila kitu kilicho baina ya mbingu na ardhi kinatambua kuwa mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, isipokuwa wale walioasi miongoni mwa watu na majinni." (Ahmad, III, 310)

Mafunzo yanayopatikana katika Vita vya Uhud

Katika Vita vya Uhud waumini walipata kiwango kikubwa sana cha ukomavu, katika kukabiliana, kwa hekma, na uchungu mkubwa uliowalashurutisha kukabiliana nao baada ya upepo wa uimara na nguvu kuhamia upande wa Maqurayshi. Mwanzoni mwa mapambano walionesha kiwango cha juu cha kumtegemea Mwenyezi Mungu, kujituma na kuvumilia, lakini pindi mambo hayo yalipoondoka na mahali pake kuchukuliwa na mapenzi ya dunia,

Waislamu walilazimika kupitia hali ngumu na yenye uchungu na maumivu makubwa.

Hatua ya kupuuza kutekeleza kikamilifu amri ya Mtukufu Mtume ﷺ ilibadilisha mustakbali wa Vita hivyo mbele ya macho yao; ushindi ukasimamishwa, ishara za onyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu zikaonekana wazi. Waumini wote wakalipa gharama ya kosa lililofanywa na watu wachache, wakajikuta katikati ya hali ya kushindwa isiyoweza kurudi nyuma. Hiyo ndiyo *sunnatullah,* yaani Kanuni ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Mtume Wake kipenzi alikuwa miongoni mwa waumini aliweza kuibadilisha hali hiyo kidogo.

Hata hivyo, Maswahaba walikuwa katika hali ya utii usiokuwa wa kawaida kwa Mtukufu Mtume ﷺ kama inavyothibitishwa na maneno ya uaminifu wao kwake waliposema: "Tumekuamini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ...tuna imani ya kweli juu ya ukweli wa Qur'an uliyokuja nayo, na tunaapa kukutii na kukufuata. Fanya kama upendavyo; tupe amri nasi tutakuwa upande wako. Tunaapa kwa yule aliyekutuma, hata kama utaingia baharini, tutakufuata na hakuna hata mmoja wetu atakayebaki nyuma!" (Ibn Hisham, II, 253-254). Hiki ni kiwango cha juu kabisa cha utiifu na hamasa ya kweli waliyokuwa nayo.

Tabu waliyopata waumini katika vita vya Uhud ilikuwa imebeba onyo la Mwenyezi Mungu kwao kutokana na mghafala wa muda mfupi waliokuwa nao kuhusu utekelezaji wa majukumu kadhaa yenye umuhimu na yenye unyeti mkubwa.

Miongoni mwa hekma kubwa kabisa katika mapambano hayo ya Uhud ilikuwa kuwatakasa Waumini dhidi ya wanafiki waliokuwa wamejichanganya katika safu zao.

Vile vile, Vita vya Uhud viliwafanywa waabudu sana wa Kiqurayshi wawe na hisia potofu kuhusu ushindi ambao usingekuwa na athari yoyote ya nje, na hivyo kuwafanya wawe na hali ya kutulia na kutofanya chochote. Ushindi huo usiokuwa wa hakika ulishusha chini chuki na ghadhabu iliyokuwa imejikusanya katika nyoyo za makafiri tangu waliposhindwa katika vita vya Badr, hatimaye ubaridi wao kuhusu Uislamu ukaanza kupungua kidogokidogo kadiri muda ulivyozidi kusonga mbele.

Ni jambo la kusisimua kuona Maswahaba, kuanzia wale wadogo kabisa mpaka kwa wale wakongwe, wakishindana kwa wema katika kushiriki katika vita hivi na kufa kishahidi. Vijana wenye umri wa miaka kumi na nne walikuwa wakifanya kila liwezekanalo ili tu waweza kuwa sehemu ya jeshi la Mtukufu Mtume ﷺ. Siri ya wao kukikimbilia kifo inapatikana katika nyoyo zao zilizojaa imani na mapenzi yao makubwa na ya kina waliyokuwa nayo kwa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ, ambayo ndiyo sababu ya uwepo wa ulimwengu. Pindi imani inapoungana na upendo, patapatikana kila aina ya ushujaa na ujasiri wa hali ya juu, na pindi muungano huo unapokosekana, basi uvivu, khofu na wasiwasi hutawala. Jinsi ya kupandikiza upendo huu ni kuongeza *dhikr*, *salawat* au kumtakia rehma Mtukufu Mtume ﷺ, kuzitafakari na kuzitaamali neema na baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kujishughulisha kwa moyo mmoja katika kufuata nyayo za Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye ni nuru ya ulimwengu, alijeruhiwa katika vita vya Uhud, jambo lililopelekea kuzaa kwa uvumi kwamba ameuawa na kupeleka somo lenye mazingatio makubwa kabisa kwa Waislamu.Walipewa mtihani wa imani na msimamo wao. Tokea mwanzo, nyoyo zao zilikuwa zimeandaliwa kuutambua ukweli wa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, naye pia ni mwanadamu ambaye angerudi mbele ya Mola wake pindi muda

utakapofika, na kwamba walitakiwa kushikamana na njia aliyowaonesha na wasirudi nyuma baada ya kuondoka kwake.

Mbali na masomo hayo yenye mazingatio, Vita vya Uhud pia viliwafundisha njia inayoelekea kwenye ushindi na njia ya kuepukana hatari ya kupotea na kushindwa.

Hamra'ul-Asad (8 Shawwal, 3 / 24 Machi 625)

Waabudu masanamu walikuwa wameelekea moja kwa moja kwenye barabara iendayo Makka huku wakitetemeka kwa khofu iliyokuwa imewaingia nyoyoni mwao kiasi cha kutowaruhusu hata kufikiria mara mbili kuhusu hatua yao hiyo kurejea nyumbani. Walipokuja kushituka wakiwa njiani walianza kuwa na hisia ya kujuta kwa kutowamalizia mbali Waislamu. Hivyo wakaamua kurudi kushambulia kwa mara ya pili.

Mtukufu Mtume ﷺ ambaye wakati huo alikuwa ameshawasili katika mjia wa Madina, alihisi kuwa na haja kama hiyo ya kuwafuatilia Washirikina na hapo hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ifuatayo akiwausia waumini wasifanye ulegevu kuhusu suala hilo.

وَلاَ تَهِنُواْ فِي ابْتِغَاء الْقَوْمِ إِن تَكُونُواْ تَأْلَمُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمونَ
وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ مَا لاَ يَرْجُونَ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا

"Wala msifanye ulegevu kuwafukuzia kaumu ya maadui. Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyo umia nyinyi. Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasio yataraji wao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima." (an-Nisa: 104)

Mtukufu Mtume ﷺ alitaka watu wenye kujitolea miongoni mwa Maswahaba wake ambao wanataka kuchukua jukumu la kuwafuatilia maadui. Bila kuchelewa zaidi, kikosi kilichowajumuisha Abu Bakr na Zubayr ؓ kiliandaliwa. Maswahaba karibu wote waliokuwa katika kikosi hicho walikuwa bado wana majeraha mabichi kabisa ya vita vya Uhud. Bila kuchelewa, Maswahaba hao majeruhi waliungana na jeshi la Mtukufu Mtume ﷺ jirani na Kisima cha Abu Inabah.[149]

Hata Usayd ibn Khudayr ؓ, ambaye wakati huo alikuwa akiwatibu majeruhi, aliachana na kile alichokuwa akifanya, akachukua silaha zake na kwenda kuungana na Mtukufu Mtume ﷺ.

Mtu mwingine ambaye alijianda bila kuchelewa ni Saada ibn Ubadah ؓ, ambaye aliwaagiza watu wa ukoo wake kumfuata.[150]

Kikosi hicho kikiwa kinaongozwa na Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe kilianza safari ya kuwafuatilia maadui.

Abdullah ibn Sahl na kaka yake, Rafi ؓ, walikuwa wameshiriki pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vya Uhud na kurudi Madina wakiwa majeruhi. Waliposikia wito wa Mtukufu Mtume ﷺ wa kuwafuatilia maadui, wakasema:

"Wallah, hatuna kipandwa na tuna majeraha mazito. Lakini tutawezaje kutoshiriki safari ya kivita inayoongozwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Hivyo wakaanza safari huku wakisaidiana kutembea na wakati mwingine wakipeana zamu za kuwabeba wenzao migongoni mwao. Hatimaye walifanikiwa kufika kwa Mtukufu Mtume ﷺ, wakiwa hawawezi kustahmili kumuacha peke yake.[151]

149. Waqidi, I, 334-335.
150. Waqidi, I, 334-335.
151. Ibn Hisham, III, 53.

Waislamu hawa walioonesha kiwango cha hali ya juu cha kujitolea wamesifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika aya ifuatayo:

الَّذِينَ اسْتَجَابُواْ لِلّهِ وَالرَّسُولِ مِن بَعْدِ مَآ أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ
أَحْسَنُواْ مِنْهُمْ وَاتَّقَواْ أَجْرٌ عَظِيمٌ

"Walio mwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majaraha - kwa walio fanya wema miongoni mwao na wakamchamngu utakuwa ujira mkubwa." (Al-i Imran: 172)

Kikosi hicho kilisonga mbele mpaka kilipofika katika eneo liitwalo Hamraul-Asad, karibu kilomita nane kutoka mjini Madina. Bendera ya kikosi ilikuwa imeshikwa na Ali ﷺ. Usiku ulipoingia, Mtukufu Mtume ﷺ aliamuru moyo uwashwe katika maeneo mia tano tofauti tofauti. Mandhari hayo yalikuwa yenye kuvutia. Kwa mtazamaji ilionekana kana kwamba jeshi kubwa sana lilikuwa limeweka kambi mahali hapo. Mtu mmoja aitwaye Maabad, ambaye wakati huo hakuwa Muislamu, aliuona moto huo wa Waislamu akiwa njiani kuelekea Makka. Muda mfupi baadaye akakutana na makafiri, bila kuchelewa akawaambia kuwa walikuwa karibu kudirikiwa na Waislamu.

"Sijawahi kuona jeshi kubwa kama hilo", aliwaambia ili kuweka mkazo juu ya ukubwa wa jeshi hilo lilivyoonekana kwa mbali. Habari hiyo ilitosha mara moja kuingiza khofu ndani ya nyoyo zao.

"Waislamu hawakuwa na nguvu za kutosha hata kunyanyua vidole vyao; sasa jambo hilo linawezekanaje?" walianza kuulizana huku wakijikongoja. Kisha, kwa sababu zisizojulikana, wakaamua kwa pamoja "kuondoka kabla janga halijalipuka!"

Wakiwa wameshindwa na changamoto ya kupambana na Waislamu kwa mara ya pili, walianza kuvuta kasi ya kurudi nyumbani. Mtukufu Mtume ﷺ alipogundua kuwa wamerudi nyuma naye pia akawaongoza Maswahaba wake kurejea Madina.[152]

Suala la Mirathi

Katika kipindi hicho hicho aya kadhaa zilishuka kuhusu suala la mirathi, baada ya mkanganyiko kuibuka kufuatia vita vya Uhud. Kufuatia kifo cha Saad ibn Rabi ﷺ katika vita vya Uhud, kwa mujibu wa desturi za Enzi za Ujahiliyya, kaka yake alichukua mali zake zote zilizokuwa zimebaki bila kuwaachia chochote watoto wawili wa kike walioachwa na Saad. Kutokana na kuchukuliwa kuwa wenye thamani ndogo wakati wa enzi za Ujahiliyyah, wanawake hawakupewa haki za kurithi; dhulma ambayo ilikuja kukomeshwa na Uislamu:

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثَيَيْنِ فَإِن كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ وَإِن كَانَتْ وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ وَلِأَبَوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا السُّدُسُ مِمَّا تَرَكَ إِن كَانَ لَهُ وَلَدٌ فَإِن لَّمْ يَكُن لَّهُ وَلَدٌ وَوَرِثَهُ أَبَوَاهُ فَلِأُمِّهِ الثُّلُثُ فَإِن كَانَ لَهُ إِخْوَةٌ فَلِأُمِّهِ السُّدُسُ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دَيْنٍ آبَاؤُكُمْ وَأَبناؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفْعاً فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيما حَكِيمًا

152. Ibn Hisham, III, 52-56; Waqidi, I, 334-340.

"Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili. Na ikiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za alicho kiacha maiti. Lakini akiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi fungu lake ni nusu. Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sudusi ya alicho kiacha, ikiwa anaye mtoto. Akiwa hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake, basi mama yake atapata thuluthi moja. Na akiwa anao ndugu, basi mama yake atapata sudusi. Haya ni baada ya kutolewa alicho usia au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani baina yao aliye karibia zaidi kwenu kwa manufaa. Hiyo ni Sharia iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu. Bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima." (an-Nisa: 11)

Hivyo, mgawanyo wa kwanza kabisa wa mirathi katika Uislamu ulifanyika baina ya warithi wa Saad ibn Rabi رضي الله عنه.[153]

Sheria ya mirathi katika Uislamu imeweka uwiano wa kiuadilifu baina ya mafungu yaliyopangwa na majukumu ya mrithi. Wanaume, ambao wamepewa majukumu mazito sana ya kiuchumi, kuanzia kwenye kugharamia ndoa na malipo ya mahari mpaka kwenye kuzisaidia familia zao kiuchumi baada ya ndoa hiyo, wametengewa fungu kubwa kidogo kuliko wanawake. Kwa maneno mengine, tofauti baina ya wanaume na wanawake inayozingatiwa na sheria ya Kiislamu inatokana tu na tofauti za majukumu na wajibu. Kutokana na duru yao ya kuwaangalia watoto na haja ya moja kwa moja ya malezi ya watoto na familia, wanawake wameondolewa wajibu wa kuzitunza familia zao kifedha na kiuchumi. Kwa sababu hiyo, fungu lao la mirathi ni nusu ya lile la wanaume. Kilichozingatiwa ndani ya fungu hilo la wanawake ni yale mahitaji binafsi wanayoweza

153. Ahmad, III, 352, 375.

kuwa nayo kama vile kuwasaidia wanawake ambao hawajaolewa au walioachika katika kukidhi mahitaji yao.

Wanawake wamebarikiwa zaidi kwa kujaaliwa hisia za ndani, usikivu, huruma na kujitolea, mambo ambayo ni yenye kufaa kwa malezi ya watoto na kuziweka familia chini ya mbawa zao za huruma. Hali ya kuwa laini wa moyo kwa asili, pamoja na hisia nzuri za ulaini na zenye kuamsha kina kisichokuwa na mwisho cha huruma, kutokana na hali hiyo wanawake wana muelekea wa kuzidiwa na udhaifu wa kimwili na kiakili pindi wanapokabiliwa na mbinyo unaotokana na maisha. Ni kwa sababu hiyo tu kwamba mwanamke katika Uislamu anakuwana hadhi ya kuwa 'nusu ya shahidi mmoja'. Wale wanaolichukulia hili kama sababu ya kuushambulia Uislamu, ima kutoakana na pazia zao nene za uovu au ujinga wa hali ya juu, wanashindwa kuuona ukamilifu na uzuri wa kanuni hii ambayo ina motisha wake katika masuala kadhaa muhimu sana na yanayohusu mwelekeo wa binadamu.

Ukweli ni kwamba, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba kila kiumbe, ikiwa ni pamoja na kila chembeya kiumbe huyo, kwa madhumuni maalumu, sambamba na kumjaalia muundo unaofaa wa kimwili na kiakili. Kumpa mwanaume wajibu wa kuihudumia familia yake, ili waweze kuetekeleza wajibu wao huo katika namna iliyo bora kabisa, Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajaalia wanaume, kwa ujumla, nguvu kubwa ya kimwili na ujasiri mkubwa wa kimaanawi na kiroho. Wanawake, kwa upande mwingine, wamekabidhiwa jukumu la kuwalinda watoto, kuwalea, kuwaadilisha kuangalia mahitaji yao pale wanapokuwa katika hali yao ya udhaifu kabisa, mazingira magumu na wakiwa bado wadogo. Majukumu haya maalumu yanahitajia nyoyo zao zaidi, badala ya miili yao, hali ambayo huwafanya wawe hisia kubwa kabisa za utambuzi. Kwa hivyo, ili kuwakumbatia na kuwalea watoto kwa upendo na huruma ya hali ya juu katika nyakati za udhaifu wao, wanawake wamepewa

zawadi,kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ya hisia bora na nzuri za utambuzi. Matokeo hasi yatakuja tu iwapo mama huyo, ambaye ni chemchemu ghali ya huruma kutokana na muundo wake wenye thamani, atatwishwa mzigo wa kazi zilizo kinyume na nguvu zake na hekima ya kuumbwa kwake.

Kutokana na masuala hayo, tunaweza kusema pia kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa mwanamke kupotosha, kwa kuonesha huruma iliyozidi kwa mhalifu. Hii ndiyo hekma hasa inayopatikana ndani ya kanuni hii ya Mwenyezi Mungu ambayo inauchukulia ushahidi wa wanawake wawili sawa na ushahidi wa mtu mmoja.

Kwa upande mwingine, Uislamu unasimamia mchakato wa utoaji wa ushahidi mbele ya sheria kulingana na miundo ya kisaikolojia ya binadamu. Kwa mfano, ushuhuda wa wanawake pekee huchukuliwa kuwa wenye kutosha katika mazingira maalumu yanayohusisha matukio ambayo hayawaruhusu wanaume kutoa ushuhuda.[154]

Wale wanaotumia suala la ushahidi wa wanawake kama udhuru wa kuunanga Uislamu kwamba unawaweka wanawake katika nafasi ya chini, ima wanashindwa kuelewa au hawataki hata kuelewa kwamba Uislamu, kwa kuzingatia silika isiyobadilika ya binadamu na jamii nzima, katika kuimarisha uwiano wa uadilifu baina ya haki na majukumu, usingeweza kujiweka mbali na tuhuma hizo zisizokuwa na msingi.

Hali ya kuwa mwanamke hukamilika kwa kulinda na kukuza vipawa maridhawa vya wanawake walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwanamke akielekeza vipawa vyake vya asili kwenye uelekeo tofauti na alivyopangiliwa na Mwenyezi Mungu na kuutupa mkono uhalisia wake mwenyewe, ataishia kuiharibu

154. *Mecelle*, makala. 1685.

thamani yake yote, na matokeo yake atakosa amani yake ya ndani na kuangukia katika madhila na taabu. Mbaya zaidi kuliko hilo, na mahali patakatifu, yaani familia, patatelekezwa, na kamba ya jamii itakatika.

Zama zetu hizi zimeshuhudia kuanza kwa mashindano bandia na yasiyokuwa ya kiuadilifu kwa ajili ya usawa baina ya wanaume na wanawake. Katika kuzidhihaki na kuzipinga tabia za asili za wanawake, mbio hizo zinashambulia vikali moja kwa moja kwenye moyo wa sifa za kike za wanawake, ikiwemo sifa ya umama, na matokeo yake ni kuibomoa taasisi ya familia. Kitendo kiovu kilichozoeleka zama hizi cha kutoa mimba, ambacho ni sehemu ya mbio hizi, ni toleo jipya la kitendo cha kuwazika hai watoto wa kike kilichokuwa kimezoeleka sana katika Zama za Ujahiliyyah. Tofauti ya mavazi ndiyo kitu pekee kinachowatofautisha wanawake walioghafilika wa zama zetu hizi na wale wa Zama za Ujahiliyyah. Bila shaka, hili ni janga la kijamii lililosababishwa na malezi ya kimaada yasiyokuwa ya kiroho na kimaanawi.

MWAKA WA NNE WA HIJRAH

Tukio la Raji (Safar 4 / Julai, 625)

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na mazoea ya kutuma walimu kwenda kwenye vijiji vya makabila ya jirani kwa ajili ya kufikisha na kutoa mafundisho ya Uislamu. Hata hivyo, baadhi ya hawa walimu walikumbana na njama mbaya za khiyana. Miongoni mwa matukio haya mabaya kabisa ni tukio lijulikanalo kama Tukio la Raji.

Makabila ya jirani ya Adal na Qara yalikuwa yamemuomba Mtukufu Mtume ﷺ awapelekee baadhi ya Maswahaba wenye maarifa kwa ajili ya kuwafundisha Uislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikubali ombi lao na kuwatuma Maswahaba kumi wakiongozwa na Asim ibn Thabit رضي الله عنه.

Ujumbe huo ulifika eneo liitwalo Hudat, baina ya Usfan na Makka, ambapo walipumzika kidogo jirani na Kisima cha Raji, ambacho wakati huo kilikuwa chini ya udhibiti wa kabila la Huzayl. Wakati huo huo, baada ya kupata taarifa kwamba ujumbe wa Waislamu ulikuwa umefika katika eneo hilo, watu wa ukoo wa Lihyan wa kabila la Huzayl, waliandaa watupa mishale wapatao mia moja na kwenda kuwafuatilia Maswahaba. Walipotambua kuwa walikuwa wakifuatiliwa, Asim na Maswahaba hao walikimbilia kwenye kilima kilichokuwa jirani na eneo hilo, ambapo muda mfupi walizungukwa.

"Teremkeni huko. Wekeni chini silaha zenu na mjisalimishe. Tunawahakikishia kuwa hakuna yeyote miongoni mwenu atakayeumizwa!" waliita kwa sauti kutokea chini.

"Sitateremka chini kwa kuamini yasemwayo na mshirikina!" alisema Asim, kisha akaomba dua akisema: "Mola wangu! Mjulishe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu juu ya hali yetu hii!"

Watupa mishale hao wakamshambulia Asim na Maswahaba sita waliokuwa wamebaki pamoja naye, wakawaua wote. Asim ﷺ akiwa amejeruhiwa sana, aliomba dua akisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ulinde mwili wangu wakati wa jioni, kama nilivyoilinda dini yako wakati wa jua kali!"

Baada ya kupewa taarifa ya kuuawa kwa Asim, baadhi ya wakuu wa Maqurayshi waliwatuma askari wachache waende kuukatakata mwili wake na kurejea na baadhi ya viungo vya mwili wake vitakavyowathibitishia kuwa ndiye, ili kulipa kisasi kwa ajili ya kafiri mmoja aliyeuawa na Asim katika medani ya vita vya Badr. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu, alituma kundi la nyuki kwenda kuulinda mwili wa Asim, na washirikina wakashindwa hata kuchukua viungo vya mwili wake baada ya kufukuzwa na nyuki ambao walikuwa wakizunguka juu ya kiwiliwili chake bila kuchoka. (Bukhari, Jihad, 170; Maghazi, 10, 28; Waqidi, I, 354-363)

Washirikina walisubiri mpaka jioni ili nyuki waondoke, lakini wakakutana na kitu ambacho hawakukitarajia: mvua kubwa iliyonyeesha kwa wingi.Mafuriko yaliyotokana na mvua hiyo, ambayo yalifagia kila kitu katika bonde hilo, yaliuchukua mwili wa Asim mbali kabisa na macho yao. Hivyo, washirikina hao hawakuweza kupata hata nafasi ya kuchukua kipande cha mwili wa Asim. Kutokana na tukio hilo, baadaye Asim ﷺ alipewa sjina la 'Shahidi aliyelindwa na Nyuki.'(Ibn Hisham, III, 163)

Maswahaba watatu walioweka chini silaha zao na kuteremka mlimani kujisalimisha, punde wakatambua kuwa maadui zao hawakuwa na dhamira ya kutimiza waliyoyasema baada ya kuchukua hatua ya kuwadhibiti na kuwafunga kamba kwa nguvu. Mmoja wapo wa Maswahaba hao watatu alijaribu kupambana huku akisema, "Kamwe hatujawahi kufanyia khiyana kwa namna hiyo.... Wallah! sitajisalimisha. Mashahidi waliolala hapo ni mfano kamili kwangu!" Japokuwa maadui walijaribu kumkokota kwa nguvu, lakini alikataa kwa kujaribu kupambana na hatimaye akauawa kishahidi.

Na sasa, katika Maswahaba hao kumi ni Hubayb na Zayd ﷺ ndio pekee walikuwa wamebaki. Bani Lihyan waliwapeleka Makka na kuwauza kwa Maqurayshi. Hubayb ﷺ alinunuliwa na watoto wa Harith ibn Amr, ambaye aliuawa na Hubayb katika vita vya Badr. Hubayb ﷺ aliendelea kuwa mikononi mwao kama mfungwa mpaka walipoamua kumnyonga.

Mwanamke mmoja kutoka katika familia ya watoto wa Amr baadaye alieleza kuwa "...hapo kabla sikuwahi kumuona mateka mwema na mwenye maadili ya hali ya juu kama Hubayb. Ninaapa kuwa, nilimuona akila zabibu safi kabisa licha ya ukweli kwamba mikono yake ilikuwa imefungwa, na zaidi ya hapo, katika wakati ambao hakuna mtu ambaye angeweza kupata matunda ya aina yoyote katika mji wa Makka. Nilipoona tukio hilo, nilitambua kuwa hizo ni fadhila na neema za Mwenyezi Mungu. Hubayb alikuwa akisoma Qur'an na kuamka usiku wa manane kwa ajili ya swala ya *tahajjud*. Wale waliokuwa wakimsikia akisoma Qur'an walikuwa wakianza kulia kutokana na hisia kali ya hali ya juu. Siku moja nilimuuliza kama alihitaji kitu chochote. 'Sihitaji kitu', alisema, 'isipokuwa ninakuomba unipatie maji safi, uondoshe mbele yangu nyama uliyoichinja kwa jina la masanamu yenu na unitaarifu muda watakaoninyonga.'

Baada ya muda wa makubaliano ya usitishaji vita kufikia kikomo, nilikwenda kwa Hubayb kumtaarifu kuwa walikuwa wameamua kumnyonga. Lakini, ninaapa, sikuona hali yoyote ya woga au wasiwasi. Pindi watoto wa Harith walipomchukua kumpeleka kwenye eneo lililo nje ya viunga vya *Haram* kwa ajili ya kumnyonga, Hubayb aliwaomba wamruhusu aswali rakaa mbili. Wakakubali. Baada ya kuswali, Hubayb aligeuka na kusema, 'Wallah, ningekuwa najua kwamba hamtadhani kuwa ninaogopa kifo, ningeswali swala hii kwa urefu zaidi!' Hivyo, Hubayb ﷺ akawa mtu wa kwanza kuswali rakaa mbili kwa Waislamu pale wanaposubiri kunyongwa.

Kisha Hubayb aliomba dua akisema, 'ewe Mwenyezi Mungu! Waangamize wote! Yachukue maisha yao mmoja baada ya mwingine....usimuache hai yeyote miongoni mwao!'[155] Kisha alisoma kipande kifuatacho cha shairi:

'Madamu nitakufa nikiwa Muislamu, sitajali jinsi nitakavyokufa! Ninajua kuwa yote haya ni katika njia ya Mwenyezi Mungu, ambaye ni rahisi kunipa msamaha Wake, licha ya mwili wangu kutawanyika na kuharibika!'

Kisha aliongeza dua nyingine ya mwisho kwa kuomba, 'Mola wangu! Nyuso pekee ninazoziona hapa ni zile za maadui! Hakuna

155. Hubayb alipoomba dua hiyi, kila mtu aliyekuwepo mahali hapo alishikwa na khofu. Ili kujilinda na athari ya dua hiyo, walianza kukimbia huku na huku kutafuta mahali pa kujificha, wakidhani kuwa hawatoweza kupona kutokana na maangamizi ya dua hiyo. Hata baada ya mwezi mmoja kupita tangu tukio hilo lililpotokea, dua ya HUbayb iliendelea kuwa gumzo kubwa miongoni mwa Maqurayshi. Inasimuliwa kuwa Said ibn Amr alikuwa akipoteza fahamu mara kwa mara, kila alipokumbushwa dua hiyo. Wakati wa ukhalifa wake, Omar ﷺ alisikia kuhusu hali ya Said na kumuuliza iwapo alikuwa na maradhi yoyote."Sisumbuliwi na maradhi yoyote", alisema Said; "Isipokuwa nilikuwepo wakati Hubayb ananyongwa na nikasikia dua yake. Wallah, kila ninapoikumbuka, ghafla huwa naanza kupoteza fahamu!" (Waqidi, I, 359-360)

mtu hapa ambaye ninaweza kumuagiza kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ninakuomba ufikishe salamu zangu za amani Kwake!'

Wakati huo Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekaa pamoja na Maswahaba mjini Madina, mara akasikika akisema 'waalayhis-salaam', yaani amani iwe juu yake pia'.

'Ni salamu ya nani hiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?' waliuliza Maswahab hao ambao walishangazwa na jambo hilo.

'Ni ya ndugu yenu Hubayb', alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. 'Jibril ameniletea salamu zake!' Kisha Mtukufu Mtume ﷺ, muda huo huo, akawataarifu Maswahaba wake juu ya kuuawa kwa Hubayb ؓ." (Bukhari, Jihad, 170; Maghazi, 10, 28; Waqidi, I, 354-363)

Muda mfupi kabla ya kuuawa, Hubayb aliulizwa: "Je ungependa Mtume auawe badala yako?"

Bila kusita, Hubayb alijibu kwa sauti iliyotoa mwangwi wa ujasiri na heshima:

"Kamwe! Sikuwahi kuvumilia kumuona akichomwa na mwiba katika mji wa Madina, achilia mbali kuwaza kuwa aje kuadhibiwa badala yangu wakati huu!"

Akiwa ameshangazwa mno na jawabu hili, Abu Sufyan alishindwa kujizuia na kusema, "Ninaapa, sijawahi kumuona mtu anayependwa na wenzake kama Muhammad!" (Waqidi, I, 360; Ibn Sad, II, 56)

Walipokaribia kumnyonga, waliugeuza uso wake kuelekea upande wa Madina. Hubayb ؓ akamuomba Mwenyezi Mungu akisema: "Mola wangu! Iwapo ninayoyapitia yana thamani mbele Yako, basi ugeuze uso wangu kuelekea *qibla*!" Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyakubali maombi yake na kuugeza uso wake kuele-

kea upande naoutaka. Kadiri washirikina walivyojaribu kumgeuzia upande wa Madina, walishindwa. Aya ifuatayo iliteremka kuhusu Swahaba huyu mwenye nuru:

ارْجِعِي إِلَى رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً فَادْخُلِي فِي عِبَادِي وَادْخُلِي جَنَّتِي

"Ewe nafsi iliyo tua! Rejea kwa Mola wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha. Basi ingia miongoni mwa waja wangu, na ingia katika Pepo yangu." (al-Fajr, 27-30) (Qurtubi, XX, 58; Alusi, XXX, 133)

Zayd ﵁, ambaye aliuawa baada ya Hubayb ﵁, naye pia alikuwa katika hali hiyo hiyo ya msimamo uliotokana na imani. Katika kipindi chote alipokuwa mateka, alikuwa akihakikisha anaamka usiku kwa ajili ya swala ya *tahajjud* na kushinda mchana kutwa akiwa amefunga. Alikuwa hagusi chakula alicholetewa kikiwa na nyama, kwa sababu nyama hiyo ilikuwa ikichinjwa kwa jina la masanamu. Badala yake alipendelea maziwa. Alikuwa akifunga na kufuturu kwa maziwa. Alimuona Hubayb njiani wakati akipelekwa Tanim, mahali ambapo alitakiwa kuuawa, ambapo Maswahaba hao wawili waliusiana kufanya subira. Zayd ﵁ naye pia aliswali rakaa mbili kabla ya kunyongwa. Kama ilivyokuwa kwa Hubayb ﵁, naye pia alikutana na swali lililouliza iwapo angependa Mtukufu Mtume ﷺ aletwe na kuuawa badala yake, ambapo alitoa jawabu kama lililotolewa na Hubayb ﵁. (Waqidi, I, 361-362)

"Kufa nikiwa Muislamu ni bora kwangu kuliko kuishi mara elfu moja nikiwa muabudu sanamu", ndiyo maneno ya mwisho aliyoyatoa kuwaambia waaabudu masanamu hao waliokuwa wamemuahidi kumuacha huru iwapo angeikana dini yake. Na kwa

utu na heshima yenye thamani kwa Muumini, akanywa kikombe cha mauti ya shahida kwa furaha.

Tukio la Bi'r Maunah (Safar, 4 / Julai, 625)

Katika nyakati hizo hizo za tukio la Raji, Abu Bara, mtu maarufu kutoka eneo la Najd, alimuomba Mtukufu Mtume ﷺ ampe baadhi ya Maswahaba kwa ajili ya kuwafundisha Uislamu. Mtukufu Mtume ﷺ hakutaka kutekeleza ombi hilo, akisema, "Ninahofia Maswahaba wangu kukumbana na hujuma ya watu wa Najd!"

Abu Bara aliweka ahadi ya dhamana kwa niaba ya kabila lake kwamba kwa vyovyote vile Maswahaba hao wasingedhuriwa. Aidha, Mtukufu Mtume ﷺ alitaka ahadi hiyo iwekwe katika maandishi, kisha ikatumwa kwenda kwa mpwa wa Abu Bara, Amir, ambaye ndiye aliyekuwa akiongoza makabila ya Najd pindi ami yake huyo anapokuwa hayupo. Mtukufu Mtume ﷺ alikusanya kundi la Maswahaba sabini kutoka *Suffa* waliojulikana kama *Qurra* na kuwatuma pamoja na Abu Bara.

Lakini pindi ujumbe huo ulipofika kwenye Kisima cha Maunah (Bi'r Maunah), vituo vinne kutoka mjini Madina, walikumbana na hujuma nzito. Amir, mpwa wa Abu Bara, alifanya uvamizi akiwa na jeshi kubwa, bila kuwa amesoma hata barua ya Mtukufu Mtume ﷺ. Lakini pindi watu wa kabila lake walipoonekana kusita sana kuwashambulia Maswahaba baada ya kugundua kuwa Abu Bara alitangaza dhamana ya ulinzi wao, bila kujali Amir aliwahamasisha watu wa makabila ya Usayya, Ri'l, Zakwan na Banu Lihyan kuwashambulia na kuwaua Maswahaba. Amr ibn Umayya ndiye pekee aliyeweza kuokoka katuka mauaji hayo ya kutisha.[156]

156. Ibn Hisham, III, 184; Haythami, VI, 125-130.

Jabbar ibn Sulma, ambaye alikuwa miongoni mwa wavamizi hao katika tukio hili la kutisha, anaeleza kama ifuatavyo:

"Nilimchoma Amir ibn Afuhayrah kwa mkuki wangu. Ilikuwa muda mfupi tu baada ya yeye kuniita kuingia kwenye Uislamu. Niliweza kuona ncha ya mkuki wangu ikitokeza upande wa pili wa kifua chake. Lakini bado aliendelea kupiga kelele kwa furaha kubwa, 'Wallah nimeshinda!'

'Ameshinda kitu gani huyu?' nilijiuliza. Isitoshe, mimi ndo ndiye niliyekuwa nimemuuwa. Wakati huo huo, mwili wake ulipaa angani na kupotea machoni pangu. Nilichokiona ndicho kilichonifanya niingie katika Uislamu." (Ibn Hisham, III, 187; Waqidi, I, 349)

Jibril عليه السلام ndiye aliyekuwa wa kwanza kumtaarifu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba ujumbe huo wa Maswahaba ulikuwa umeungana na Mwenyezi Mungu kwa kuuawa kishahidi; kwamba Mola wao alikuwa amewaridhia nao pia wamemridhia.[157]

Mtume wa Rehma ﷺ alihuzunishwa sana baada ya kusikia tukio hili lenye kusikitisha. Kwa muda wa mwezi mmoja, kila baada ya swala ya alfajiri, alikuwa akiinua mikono yake kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na kuomba: "Mola wangu! Teremsha laana yako juu ya makabila ya Ri'l, Zakwan na Usayya ambao wametenda uasi dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!" (Bukhari, Jihad, 9, 19; Maghazi, 28; Muslim, Masajid, 297)

Machozi ya huzuni na maumivu kutoka kwa Waislamu yalikutana na furaha ya wanafiki na Wayahudi, ambao walionekana kufurahia sana yale yaliyokuwa yakitokea tangu wakati wa vita vya Uhud. Aidha, kusikitika kwao kwa kutotumia vizuri fursa ya matukio ya baada ya Uhud na kutaka kuwa juu ya Waislamu ilimaanisha kuwa sasa walikuwa wakidhihirisha uovu wao dhidi ya

157. Bukhari, Jihad, 9.

Waislamu. Wanafiki, kwa namna maalumu, walianza kuonesha khiyana yao dhdid ya Waislamu wakati wa safari ya kuelekea Uhud na baada ya vita wakaanza kuwalaumu na kuwakaripia Waislamu, ambao walikuwa wamejeruhiwa sana, wakawananga kwa kusema:

"Lau wale waliokufa wangetusikiliza tokea mwanzo, wasingekufa." Qur'an Tukufu ikawajibu kwa ukali ikisema:

الَّذِينَ قَالُواْ لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُواْ لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا قُلْ فَادْرَؤُوا عَنْ أَنفُسِكُمُ الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ

"Hao ndio walio waambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wengeli tut›ii wasingeli uliwa. Sema: Ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli." (Al-i Imran: 168)

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلاَّ بِإِذْنِ الله كِتَابًا

"Na haiwezi nafsi kuwa ife ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyo andikwa ajali yake..." (Al-i Imran: 145)

"Sikuwahi kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa na huzuni sana juu ya jambo lolote kuliko huzuni aliyokuwa nayo kwa mashahidi wa Bi'r Maunah", alisema Anas ﷺ (Muslim, Masajid, 302). Mashahidi wote waliouawa kwenye tukio hilo la Kisima cha Maunah ni Maswahaba wa *Suffa*, ambao ni walimu wema wa Qur'an na Sunnah waliopata malezi chini ya mafunzo maalumu ya kiroho kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

Matukio ya Maunah na Raji yanawaonesha Waislamu juu ya umuhimu wa wajibu wa kuufikisha Uislamu na kuwalingania watu kwenye uongofu. Mtukufu Mtume ﷺ alichagua kundi maalumu la Maswahaba kuwa walimu wa Uislamu, licha ya hatari ambazo

zingetokea. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewasifu Maswahaba hao adhimu waliouawa kwa ajili ya kazi hii, akatanga kuwaridhia, nao pia wakamridhia Mola wao.[158]

Njama chafu ya Usaliti wa Banu Nadhir

Baada ya kupona katika tukio la mauaji kwenye Kisima cha Maunah, Amir ibn Umayyah ﷺ aliwaua watu wa wawili, wakiwa wamelala, kutoka katika kabila lililowashambulia. Alikutana na watu hao akiwa njani kurejea Madina. Lakni hakuwa akijua kuwa kwa wakati huo watu hao wawili walikuwa chini ya dhamana ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na walikuwa wakirejea kutoka Madina. Kwa mujibu wa makubaliano yao ya awali, sehemu ya pesa ambayo ilitakiwa kulipwa kama fidia, ilitakiwa kutolewa na Banu Nadhir; na ili kupata kiasi hicho cha malipo, Mtukufu Mtume ﷺ, akiambatana na kundi dogo la Maswahaba, alielekea kwenye makao yao.

Banu Nadhir waliona kuwa kitendo cha kutembelewa na Mtukufu Mtume ﷺ akiambatana na kundi dogo tu la Maswahaba, kuwa ni fursa ya dhahabu; hivyo walipanga, kwa siri, njama ya kumuuwa. Walimwambia Mtukufu Mtume ﷺ kuwa walikuwa na furaha mno kulipa kiwango cha pesa walichotakiwa kukilipa, wakamkaribisha akae chini ya kivuli huku wao wakiandaa hiyo pesa na, wakati huo huo, wakiandaa karamu. Waliutumia muda huo kufanya mpango wa haraka lakini wa siri kuhakikisha njama yao hiyo inakamilika. Walikuwa wakifikiria kudondosha jiwe kubwa kutoka juu ya dari la nyumba ambayo chini yake ndipo alipokuwa amekaa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ na hivyo kummaliza kabisa. Isitoshe, walikuwa na uzoefu mkubwa sana wa kufanya uhalifu kama huo dhidi ya mitume wengi hapo kabla.

158. Bukhari, Maghazi 28, Jihad 9; Muslim, Masajid, 297.

Ni katika muda huo, Mtume Aliyebarikiwa ﷺ alisimama haraka sana kutoka mahali apokuwa amekaa na kuondoka kabisa eneo la makao yao. Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa amemhabarisha Mtume Wake juu ya njama hiyo na kumlinda. Mwenyezi Mungu anawakumbusha Waislamu juu ya neema hii aliyowajaalia katika aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اذْكُرُواْ نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هَمَّ قَوْمٌ أَن يَبْسُطُواْ إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنكُمْ وَاتَّقُواْ اللَّهَ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

"Enyi mlio amini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, walipo taka watu kukunyooshieni mikono, naye akaizuilia mikono yao kukufikieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu." (al-Maida: 11)

Aya hii inayozungumza na Waumini kwa ujumla, japokuwa njama ya mauaji ilimhusu Mtume Aliyebarikiwa ﷺ pekee, inaonesha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndio uhai na roho ya Waislamu na kwamba uhai wake unatakiwa kupewa thamani ya juu kuliko hata uhai wao wenyewe.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha aya zifuatazo kuhusu njama hiyo ya mauaji:

وَإِمَّا تَخَافَنَّ مِن قَوْمٍ خِيَانَةً فَانبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَى سَوَاء إِنَّ اللَّهَ لاَ يُحِبُّ الخَائِنِينَ

"Na ukichelea khiana kwa watu fulani basi watupilie ahadi yao kwa usawa. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi makhaini." (al-Anfal: 58)

وَإِن جَنَحُواْ لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ هُوَالسَّمِيعُ الْعَلِيمُ وَإِن يُرِيدُواْ أَن يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ هُوَ الَّذِي أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ

"Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua. Na wakitaka kukukhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutosheleza. Kwani Yeye ndiye aliye kuunga mkono kwa nusura yake na kwa Waumini." (al-Anfal: 61-62)

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma mjumbe kwenda kwa Banu Nadhir kuwaambia wachague moja kati ya mambo mawili: kufanya upya mkataba wao au kujiandaa kuondoka Madina ndani ya siku kumi. Wakati wakifanya maandalizi ya kuondoka Madina, ni katika kipindi hicho hicho ambapo wanafiki walituma ujumbe kwa Banu Nadhir wakiwaambia kuwa wasiondoke na kuwahakikishia Mayahudi hao kuwa watawasaidia kwa wingi iwapo Waislamu watatishia uwepo wao. Siri ya makubaliano baina ya Mayahudi na wanafiki ilifichuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur'an:

"Huwaoni wanao fanya unafiki wanawaambia ndugu zao walio kufuru katika Watu wa Kitabu: Mkitolewa na sisi lazima tutatoka pamoja nanyi, wala hatutamt'ii yeyote kabisa dhidi yenu. Na mkipigwa vita lazima tutakusaidieni. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa hao hakika bila ya shaka ni waongo." (al-Hashr: 11)

Licha ya mitego yote waliyokuwa wakiwategea Waislamu kila mahali, walikuwa wakiwaogopa mno Waislamu; jambo hilo linaashiriwa ndani ya Qur'an Tukufu:

"Hakika nyinyi ni kitisho zaidi katika vifua vyao kuliko Mwenyezi Mungu. Hayo ni kwa kuwa hao ni watu wasio fahamu kitu." (a-Hashr: 13)

Baada ya Banu Nadhir kubadilisha moyo wao na kuamua kutoondoka, Mtukufu Mtume ﷺ hakubaki na chaguo lingine zaidi ya kuyavamia makao yao. Banu Quraydhah, kabila lingine la Mayahudi wa Madina, walikuja kuwasaidia Banu Nadhir, wakakiuka mkataba wao na Waislamu.[159]

Mayahudi hao ambao Mtukufu Mtume ﷺ alikabiliana nao, walikuwa wakiyatumia kikamilifu makazi yao wakati wa mapambano; walikuwa wakipanda juu ya nyumba zao na kushambulia na kisha wanaporudi nyuma hukimbilia katika nyumba zao. Hivyo, kwa kuanza na nyumba iliyokuwa jirani kabisa, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ aliamuru kuvunjwa kila nyumba ya Myahudi na kukata baadhi ya mitende yao.

"Ewe Muhammad! Ulikuwa ukikataza uharibifu na kuwakemea waharibifu!" mayahudi walianza kupiga kelele kutoka nyuma ya nyumba zao. "Na sasa unaikata miti?" Jambo hili lilisababisha wasiwasi kwa baadhi ya Waislamu, kwani ghafla walianza kuhisi kunyemelewa na uzito. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu akaondoa shaka zote walizokuwa nazo:

"Mtende wowote mlio ukata au mlio uacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kuwahizi wapotovu." (al-Hashr: 5)[160] Aya hii pia inadokeza juu ya haja ya kuwa makini na michezo ya Wayahudi kuzichezea akili za watu.

Baada ya takriban siku ishirini wakiwa wamezingirwa, kufautia mkakati safi uliotekelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ na kutokana na msaada walioahidiwa na wanafiki kutofika kabisa, Banu Nadhir walijisalimisha na hatimaye Mtukufu Mtume ﷺ akawafukuza

159. Bukhari, Maghazi, 14.

160. Bukhari, Tafsir, 59/2; Ibn Hisham, III, 192.

kutoka mjini Madina. Banu Quraydha, kwa upande mwingine, kwa sababu ya kuridhia mkataba mpya, waliruhusiwa kubaki.[161]

Kabla ya kuondoka, Banu Nadhir walibomoa majengo yao yote yaliyokuwa yamebaki, ili kwamba yasije kumilikiwa na Waislamu. Hatimaye, baadhi yao waliweka makazi mapya katika eneo la Khaybar, huku wengine wakielekea upande wa Syria.[162]

Mwenyezi Mungu Mtukufu atangaza wazi usaidizi wake wa moja kwa moja kwa Waislamu katika mapambano yao dhidi ya Banu Nadhir, ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Yeye ndiye aliye watoa walio kufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu katika nyumba zao wakati wa uhamisho wa kwanza. Hamkudhani kuwa watatoka, nao walidhani kuwa ngome zao zitawalinda na Mwenyezi Mungu. Lakini Mwenyezi Mungu aliwafikia kwa mahali wasipo patazamia, na akatia woga katika nyoyo zao. Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini. Basi zingatieni enyi wenye macho!" (al-Hashr: 2)

Mali zilizoachwa na Banu Nadhir, kwa kuwa zilipatikana bila kutumia nguvu, ziliitwa *fay'*, na zikapewa hadhi tofauti na ngawira zilizopatikana kwa kutumia nguvu na mapambano:

"Mali aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu. Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu. Wapewe mafakiri Wahajiri walio tolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka

161. Bukhari, Maghazi, 14; Muslim, Jihad, 62.

162. Ibn Hisham, III, 191-194; Waqidi, I, 363-380.

kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio wa kweli." (al-Hashr: 7-8)

Fay' ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kama ilivyoelezwa na aya hiyo, ni maalumu kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya Kaabah na misikiti mingine. Wakati wote Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akitoa *fay'* iliyoangukia katika fungu lake kuwapa Maswahaba masikini. Hekma inayopatikana katika ugawaji wa namna hii, kama ilivyoashiriwa katika aya, ni kuzuia mali zisizunguke miongoni mwa matajiri pekee na hivyo kubaki zikiwa zimerundikana kwao tu. Maadili ya Uislamu katika masuala ya kifedha yanataka kuchungwa kwa hali ya kusaidiana miongoni mwa wanajamii, ili kuhakikisha kuwa tajiri na masikini, wote wanapata hadhi ya kumiliki na kunufaika. Iwapo hili litatekelezwa litazaa uwiano wa kijamii wenye uadilifu utakaoyaleta pamoja matabaka mbalimbali ya kijamii, ambapo hakutakuwepo tena makundi yanayowanyonya watu wengine.

kwa sababu hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu alizigawa ngawira za Banu Nadhir miongoni mwa *Muhajirun*, na akaacha kuwa *Ansar*, isipokuwa Maswahaba watatu waliokuwa masikini miongoni mwao. Kabla ya ugawaji, aliwahutubia *Ansar* akiwaambia:

"Mkipenda", akasema, "mali mlizokuwa mmewapa *Muhajirun* hapo mwanzo watabaki nazo na nyinyi muweze kupata sehemu ya ngawira hizi. Lakini mkitaka, mnaweza kuwaambia wawarudishie mali mlizowapa, ambapo wao watachukua ngawira zote hizi."

Hapo *Ansar* wakatoa jibu adhimu na lenye kuonesha moyo wa upendo, wakasema: "Hatutaomba waturejeshee mali na nyumba tulizowapa, wala hatutachukua chochote katika ngawira hizi!"

Hisia hii ya udugu usio na kifani iliyooneshwa na *Ansar* ni miongoni mwa sababu za kuteremka kwa aya ifuatayo:

"Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa." (al-Hashr, 9) (Razi, XXIX, 250; Qurtubi, XVIII, 25)

Kuharamishwa Pombe/Vileo na Kamari

Hukumu na sheria za Mwenyezi Mungu kuhusu vileo na kamari, kama tujuavyo, hazikutolewa katika miaka ya mwanzo ya Uislamu bali, kutokana na sababu maalumu, zilicheleweshwa. Marufuku ya ilifuata utaratibu na mpangilio ufuatao:

1. Katika mji wa Makka, iliteremshwa aya isemayo:

وَمِن ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا
وَرِزْقًا حَسَنًا إِنَّ فِي ذَلِكَ لآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

"Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi na riziki nzuri. Hakika katika hayo ipo Ishara kwa wanao tumia akili." (an-Nahl: 67). Aya hii inaeleza jinsi zabibu na tende, licha ya kuwa na virutubisho vizuri, zinazalisha vinywaji vyenye asili ya kulevya. Hii inaleta hisia kwamba vilevi havichukuliwi kuwa miongoni mwa vyanzo vizuri vya virutubisho na hivyo kuonesha kuwa baadaye vitapigwa marufuku. Hii ndiyo aya pekee iliyoteremshwa kuhusu pombe na vilevi wakati wa kipindi cha Makka.

2. Baada ya Hijra (kuhamia madina), Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akipokea maswali mengi sana kuhusiana na masuala hayo, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alitangaza kwa kusema:

"Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake..." (al-Baqara: 219)

Waumini wengi waliachana na unywaji wa vileo, huku wengine wakiendelea bila kujali.

3. Swahaba mmoja aliyekuwa amekunywa ulevi, alichanganya maneno ya aya, wakati akiswalisha swala ya Maghribi, kiasi cha kupotosha maana ya aya husika, jambo lililopelekea kuteremshwa kwa aya hii:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَقْرَبُواْ الصّلوةَ وَأَنتُمْ سُكَارَى حَتَّىَ تَعْلَمُواْ مَا تَقُولُونَ

"Enyi mlio amini! Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema..." (an-Nisa: 43)

Baada ya kuteremka ya hii, idadi kubwa ya Waislamu wenye kunywa ulevi ilipungua sana. Hata hivyo, kabla ya kila swala, alikuwepo Swahaba ambaye alikuwa akiita kwa sauti, 'Msikiaribi Swala hali mmelewa!' Sasa Waislamu walikuwa wameanza kutambua kikamilifu kuwa ni suala la muda tu ambapo matumizi ya ulevi yatapigwa marufuku kwa wema na walikuwa wakijiandaa kwa hatua hiyo.

4. Idadi kubwa mno ya Waislamu sasa ilikuwa imeacha ulevi. Kwa upande mwingine, baadhi yao walikuwa na huzuni sana juu ya mtukio mabaya yaliyochochewa na ulevi ambayo walikuwa waki-

kumbana nayo sana. Kwa mfano, Omar ﷺ alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu 'atoe tangazo la wazi na la moja kwa moja kuhusu ulevi!' Ugomvi uliotokea baian ya Maswahaba wachache baada ya karamu kutokana na kuchochewa na ulevi, jambo lililoondosha shaka yoyote juu ya faida za kupiga marufuku ulevi, yalitoa hoja sahihi ya marufuku hiyo kwa kuweka msingi wa sababu iliyopelekea marufuku hiyo kutangazwa bayana:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالأَنصَابُ وَالأَزْلاَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاء فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلاَةِ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ

"Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet›ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika Shet›ani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?" (al-Maida: 90-91)

Mtukufu Mtume ﷺ alimuitisha Omar ﷺ na kumsomea aya hiyo. Alipofika kwenye maneno yasemayo 'je mmeacha...?' Omar ﷺ akasema:

"Ndiyo ewe Mwenyezi Mungu, tumeacha; tumeacha!" Maneno hayo hayo yalisikika miongoni mwa Maswahaba wote.

Kufuatia kuteremka kwa aya hii, na kwa amri ya Mtukufu Mtume ﷺ, Swahaba mmoja alipita akiita kwa sauti katika mitaa ya mji wa Madina kuwa:

"Pombe na vileo vimeharamishwa kuanzia leo na kuendelea!"

Mito ya pombe ilitiririka katika mitaa ya Madina kutoka katika pombe iliyomwagika kutoka katika vyombo vya udongo na viriba vya ngozi ambavyo hapo awali vilikuwa vimejaa vinywaji hivyo vilivyoharamishwa.

Waislamu ambao hapoo awali walikuwa wakinywa ulevi, sasa walikuwa wakiharibu akiba yote ya pombe waliyokuwa nayo kufuatia tangazo hili la marufuku. Wasingekunywa tena pombe. Katika kusisitiza zaidi marufuku hii, Mtukufu Mtume ﷺ alieleza:

"Hakika Mwenyezi Mungu amevilaani vileo, mwenye kuvitengeza na mahali vinapotengenezwa; mwenye kuvitumia na mwenye kuhamasisha matumizi yake; mwenye kuvibeba, mwenye kuviuza, mwenye kuvinunua na mwenye kuishi kwa kutumia mapato yake (yaani mapato ya vileo)!" (Ahmad, I, 53; II, 351; Nasai, Ashribah, 1-2; Hakim, II, 305/3101)

Anas رضي الله عنه anaelezea:

"Vileo viliharamishwa wakati nikiwahudumia watu pombe katika nyumba ya Abu Talha. Amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ilipotoka, Swahaba mmoja alikuwa akipita na kutangaza juu ya habari hiyo. Tulisikia sauti yake tukiwa ndani. Abu Talha akaniambia, 'Nenda nje utazame kuna nini!'

Nilikwenda nje na kumsikia akitangaza kwamba kuanzia wakati huo vileo vilikuwa vimeharamishwa. Nilimwambia Abu Talha nilichokisikia. 'Kama ni hivyo', Abu Talha akasema, 'basi nenda kamwage pombe ile nje!' Punde si punde, pombe ilikuwa ikitiririka katika mitaa ya mji wa Madina." (Bukhari, Tafsir, 5/11)

Tukio hili linaashiria uharaka wa Maswahaba katika kutii amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Bila kuanza kutoa sababu yoyote au

kusubiri hata dakika moja, kwa haraka sana walimwaga vileo vyote walivyokuwa navyo, wakatafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa shauku kubwa, sio tu kwa kujisalimisha mbele ya amri ya Mwenyezi Mungu, bali pia kwa kuitii kikamilifu kutoka ndani ya vina vya nyoyo zao.

Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ anatangaza:

"Vileo vyote ni haramu. Hata kichache katika vileo, nacho ni haramu." (Ibn Majah, Ashriba, 10; Nasai, Ashribah, 24, 48)

"Vileo ni mama wa maovu yote." (Ahmad, V, 238)

"Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho asikae katika meza yenye vileo." (Tirmidhi, Adab, 43/2801)

"Watu katika umma wangu watakunywa vileo kwa kuvipa majina mbalimbali." (Ahmad, IV, 237)

Mchakato wa hatua kwa hatua unaotokana na kutilia umuhimu *maslahah*, yaani maslahi ya wote, ambao tunuona ukitumika katika kuharabisha na kupiga marufuku matumizi ya pombe na kamari, unatoa dalili ya wazi ya njia inayotumiwa na Uislamu katika ulinganiaji na mapambano yake dhidi ya uovu. Japokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua daima na kwa yakini wakati wa kupitisha uamuzi katika kuweka sheria za Uislamu, huzingatia vipawa na uwezo wa wanadamu, ambao ndio walengwa wa moja kwa moja wa sheria hizi, na uwezo wao wa ufanisi katika kuzifanya nafsi zao zipate mazoe ya sheria hizo.Labda dalili muhimu zaidi juu ya jambo hili inaweza kupatikana katika ukweli kwamba Ayah zote zinazohusu itikadi ya Uislamu (aqiida) ndizo zilioanza kutolewa na kuteremshwa katika kipindi cha Makka, kinyume na mazingira ya jumla ya utaratibu wa Qur'an ilivyopangwa leo hii. Kwa kuwa Qur'an Tukufu ilikuwepo katika *Lawhul-Mhafuudh* kabla ya kuteremshwa duniani, sio vigumu kukuta kwamba uzito maalumu uliowekwa

katika uteremshwaji wa baadhi ya aya za Qur'an ni wa *maslahah* ya moja kwa moja kabisa, yaani ilifanyika hivyo kwa faida ya moja kwa moja kwa Waislamu wote.

Uzito huu wa faida kwa wote unajumuisha kuangalia uwezo na kipawa cha wanadamu katika kuifuata Qur'an Tukufu na mafundisho yake; kama ambavyo mambo ya wajibu kwa mtoto huongezeka kadiri umri unavyosogea.

Kanuni ya kutenda jambo hatu kwa hatua, ambayo ilitekelezwa katika namna bora enzi za neema za Mtukufu Mtume ﷺ, ni sehemu ya *sunnatullah,* yaani utaratibu wa Mwenyezi Mungu uliojaa hekma kubwa sana na kuonesha Huruma na Rehma Yake. Utaratibu huu ambao unaweza kutekelezwa kipindi chochote kile cha kuutangaza Uislamu, ni utaratibu usiopitwa na wakati na wakati huo huo ni utaratibu unaokubaliana na maumbile ya mwanadamu. Kwa hakika, baada ya kuingia katika Uislamu kitu cha kwanza ambacho mtu anatakiwa kukifanya ni kuitakasa imani yake. Ni baada ya hatua hiyo ndipo mtu huyo husonga mbele na kuanza kufanya amali mbalimbali. Utaratibu wa hatua kwa hatua hurejea tena wakati wa kuyatekeleza matendo na amali hizo, lakini wakati huu ikiwa ni kuyawekea utaratibu kulingana na vipawa vya mwanadamu. Sio tu kwamba jambo hili linatekelezwa wakati wa kuwaita watu kwenye Uislamu, bali pia katika aina zote za mafundisho. Kwa hali hiyo, kutokana na wito wa Mwenyezi Mungu ulioanza kwa Adamu عليه السلام, kumekuwepo na maendeleo na mabadiliko mbalimbali katika Ujumbe huo – lakini misingi ya dini na imani ilibaki kuwa kama ilivyo-, mabadiliko ambayo alienda sanjari na maendeleo ya mwanadamu; mabadiliko hayo yalifikia kilele chake na kufikia kikomo ndani ya dini ya Kiislamu.

Dhatur-Riqah[163]

Koo za Muharib na Thalabah kutoka katika kabila la Ghatafan waliunganisha nguvu na majeshi yao kwenda kuanzisha mashambulizi dhidi ya Waislamu, ambapo katika kuwakabili, Mtukufu Mtume ﷺ alikwenda kukubaliana nao akiwa na jeshi la Maswahaba mia nne.

Maadui hao walipowaona Waislamu mbele yao walichanganyikiwa na kurudi nyuma. Muda mfupi baadaye, muda wa swala ya Adhuhuri uliingia na Waislamu wakaitekeleza swala hiyo kwa jamaah. Maadui waliokuwa wakitazama kwa mbali jinsi Waislamu wanavyokamilisha swala yao hiyo, walianza kujilaumu sana kwa kutotumia fursa hiyo kuwashambulia. Lakini askari mmoja akawafariji wenzake kwa kuwaambia:

"Msiwe na wasiwasi. Swala inayofuata ya alasiri ni swala wanayoipenda sana kuliko hata wanavyowapenda baba zao na watoto wao." Walimsikiliza na kuamua kusubiri mpaka wakati wa swala ya alasiri.

Ni wakati huo huo ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtuma Jibril عليه السلام kupelekea aya ifuatayo ambayo iliharibu mipango yao ya mashambulizi:

وَإِذَا كُنتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلوةَ فَلْتَقُمْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُم مَّعَكَ وَلْيَأْخُذُواْ أَسْلِحَتَهُمْ فَإِذَا سَجَدُواْ فَلْيَكُونُواْ مِن وَرَآئِكُمْ وَلْتَأْتِ طَآئِفَةٌ أُخْرَى لَمْ

163. Mapokezi mengine yanaeleza kuwa tukio hili lilitokea baada ya Vita vya Khadaq au Khaybar. Hata hivyo, tumependelea kufuata mlolongo huu kwa mujibu wa maoni ya wanazuoni na wasomi wengi wa historia ya maisha na zama za Mtume ﷺ.

يُصَلُّواْ فَلْيُصَلُّواْ مَعَكَ وَلْيَأْخُذُواْ حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ وَدَّ الَّذِينَ كَفَرُواْ لَوْ تَغْفُلُونَ عَنْ أَسْلِحَتِكُمْ وَأَمْتِعَتِكُمْ فَيَمِيلُونَ عَلَيْكُم مَّيْلَةً وَاحِدَةً وَلاَ جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِن كَانَ بِكُمْ أَذًى مِّن مَّطَرٍ أَوْ كُنتُم مَّرْضَى أَن تَضَعُواْ أَسْلِحَتَكُمْ وَخُذُواْ حِذْرَكُمْ إِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا

"Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Na watakapo maliza sijida zao, basi nawende nyuma yenu, na lije kundi jingine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe. Nao wachukue hadhari yao na silaha zao. Walio kufuru wanapenda mghafilike na silaha zenu na vifaa vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja. Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkawa wagonjwa, mkaziweka silaha zenu. Na chukueni hadhari yenu. Hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha." (an-Nisa, 102) (Tirmidhi, Tafsir, 4/3035)

Aina hii maalumu ya swala imekuja kujulikana kama *Salaatul-Khawf*, au Swala ya Hofu.[164] Jibril عليه السلام mwenyewe ndiye aliyem-

164. *Salaatul-khaw*f, yaani swala ya khofu, ni swala ambayo kundi moja hupeana zamu kuswali swala husika nyuma imamu mmoja, pindi panapokuwa na tishio la hatari kubwa kama vile shambulio la maadui linalotarajiwa kufanyika. Kundi la kwanza, linaloswali rakaa ya kwanza ya swala zenye rakaa mbili, au rakaa mbili za mwanzo kwa swala zenye rakaa nne, huondoka kwenye swala hiyo na kwenda kuweka ulinzi, baada ya sijda ya pili – katika swala ya rakaa mbili – au tahiyatu ya kwanza katika swala ya rakaa nne. Wakishanyanyuka hao, linafuata kundi la pili na kukamilisha rakaa zilizobaki za swala hiyo nyuma ya imamu huyo huyo, kisha hunyanyuka na kuchukua jukumu la kulinda. Imamu hutoa *salaam* kuhitimisha swala, yeye mwenyewe. Hapo litakuja kundi la kwanza kwa mara nyingine na kukamilisha swala yao bila kisomo cha Qur'an (*qiraa*), kwa sababu wanachukuliwa kama *lahiq*, yaani mtu anayeondoka kwenye swala kutokana na

fundisha Mtukufu Mtume ﷺ namna ya kuitekeleza. Siku hiyo, swala ya alasiri iliswaliwa kwa namna hii na maadui waliokuwa wakisubiri, huku matumaini yao pekee waliyaweka kwenye hizo dakika chache za hiyo swala, wakaangukia pua. Safari hii ya kivita, ambayo ilidumu kwa muda wa siku kumi na tano ilifikia kikomo kwa maadui kukimbia wakiwa na khofu.[165]

Maelezo yaliyotolewa na Abu Musa al-Ash'ari رضي الله عنه yanahusu safari hii ya kivita. "Tulikuwa safarini pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu رضي الله عنه. Watu sita miongoni mwetu walikuwa wakipeana zamu kupanda ngamia. Miguu yetu ilivimba sana kutokana na kutembea. Miguu yangu pia ilivimba; kucha zangu zikachomoka. Tulikuwa tukijifunga vipande vya nguo kwenye miguu yetu na hivyo mapambano haya yakaitwa *Dhaatur-Riqa*."

Abu Burdah, ambaye alisimulia maneno haya kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه akaongezea kusema: "Baada ya kueleza yote hayo, ghafla Abu Musa akahisi kujuta, akasema, 'sikufanya vizuri kukwambia haya', huku akionesha masikitiko yake. Huenda kilichompa wasiwasi ni kufichua hali ya ujasiri aliokuwa ameunesha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee." (Bukhari, Maghazi, 31)

Umasikini na ukosefu wa fursa havikuwazuia Maswahaba kutekeleza wajibu wao na kuendelea na *jihad* katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Licha ya hivyo, walikuwa makini sana kufichua hata shida ndogo sana inayowapata wakati wa kumtii

---

udhuru maalumu ingawa alikuwa nyuma ya imamu tokea mwanzo. Baada ya kundi hilo kukamilisha, kundi al pili hufuata na kukamilisha swala yao, lakini kwa kisomo, kwa kuwa wanahesabika kama *masbuuq*, yaani mtu anayejiunga katika swala nyuma ya imamu baada ya rakaa ya kwanza ya swala husika. Kwa kufanya hivyo, swala inakuwa haikuachwa na jukumu hilo linguine nalo pia linakuwa halikupuuzwa. (Komisyon, *Diyânet İlmihâli*, I, 334; Hamdi Döndüren, *Delilleriyle İslâm İlmihâli*, uk.377-378)

165. Ibn Hisham, III, 214-221; Ibn Saad, II, 61.

Mwenyezi Mungu, labda kama kukiwa na ulazima mkubwa katika kufanikisha madhumuni chanya, kama vile kutoa funzo kwa wengine au kuwafariji wanyonge.

Wakati wa safari hiyo ya kivita, Mtukufu Mtume ﷺ aliomba maji kwa ajili ya wudhuu. Lakini, hapakuwa na maji. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ aliingiza mikono yake ndani ya chombo kilichokuwa na maji kidogo sana ndani yake, na hapo ukatokea muujiza ambapo vidole vyake vyote viligeuka kuwa chemchem na kutoa maji mengi. Maswahaba wote waliweza kunywa na kukata kiu yao. Hata baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutoa mikono yake ndani ya chombo hicho, kiliendelea kujaa maji.[166]

Jeshi la Waislamu lilifika kwenye bonde moja lenye miti mingi, majira ya mchana, wakati wakirudi kutoka katika Vita vya Dhaatur-Riqa, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ aliamua kupumzika. Maswahaba nao pia wakashika njia kwenda kupumzika chini ya vivuli vya miti. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijilaza chini ya mti wa *samurah*, mti wenye majani mengi, akiwa ameuning'iniza upanga wake juu ya tawi la mti. Maswahaba walikuwa wamesinzia kidogo wakasikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwaita. Wakakimbia haraka sana kuelekea kwa Mtukufu Mtume ﷺ ambapo walimkuta Bedui mmoja akiwa amesimama mbele yake.

"Mtu huyu alichukua upanga wangu nikiwa nimelala", alielezea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. "Nilipoamka, upanga ulikuwa mkononi mwake, akauchomoa kwenye ala yake. 'Nani atakayekuokoa kutoka mikononi mwangu sasa?' aliuliza; 'Allah!' Nilimsjibu hivyo, mara tatu." (Bukhari, Jihad, 84, 87; Muslim, Fadhaail, 13)

Mtukufu Mtume ﷺ hakukimbilia kumuadhibu Bedui huyo aliyejaribu kumuua na badala yake akamlingania na kumuita kwenye

166. Bukhari, Wudhuu, 32; Manakib, 25; Muslim, Fadhaail, 5.

Uislamu. Bedui huyo akiwa amelainika kwa tabia na maadili haya adhimu ya Mtukufu Mtume ﷺ, aliporejea kwa watu wake hakuwa na la kufanya badala ya kusema: "Nimerudi kutoka kwa mbora wa watu!" (Hakim, III, 31/4322)

Akiwa njiani kurejea Madina wakati wa jioni, Mtukufu Mtume ﷺ aliamua kupumzika katika kituo kingine na kuwataka watu watakaojitolea miongoni mwa Maswahaba kwa ajili ya kuweka ulinzi wakati wengine wakiwa wamepumzika. Waliojitokeza kubeba jukumu hilo la kujitolea bila kusita ni Ammar ibn Yasir ؓ kutoka katika *Muhajirun*, na Abbad ibn Bishr ؓ kutoka katika Ansar. Abbad akamuuliza Ammar ni muda gani wa usiku ambao angependa kusimama na kulinda.

"Nusu ya pili ya usiku", Ammar ؓ alijibu. Kisha bila kuchelewa akalala na kuzama usingizini. Abbad ؓ akaanza kuswali, ambapo kafiri mmoja alisogea kwa siri na alipokiona kivuli cha Abbad aliyekuwa amesimama, alipiga mshale uliompata Abbad. Lakini Abbad alikusanya nguvu zake, akauchomoa na kuendelea na swala yake. Hilo halikumkatisha tamaa adui, alitupa mshale wa pili na wa tatu, ambayo yote ilimpata Abbad lakini akaichomoa na kuendelea kuswali. Hatimaye Abbad aliinama kwa ajili ya *rukuu*, akaenda kwenye *sajdah* na kuikamilisha swala yake kwa *salaam*. Hapo akamuamsha mwenzake:

"Amka ewe Ammar; nimejeruhiwa", alisema kwa sauti ya unyonge. Ammar akaamka mara moja. Adui alipoona kuwa amegundulika kwa Maswahaba, alikimbia. Lakini wakati huo Abbad alikuwa amejeruhiwa vibaya sana akiwa amelala chini.

"*Subhaanallah*", alihamaki Ammar. "Mbona hukuniamsha ulipopigwa mshale wa kwanza?"

Abbad alitulia kidogo, kisha akajibu kwa kuonesha mapenzi makubwa aliyokuwa nayo juu ya swala:

"Nilikuwa nikisoma sura ya Qur'an Tukufu na sikutaka kuikatisha swala yangu kabla ya kukamilisha kisomo. Lakini mishale ilipozidi kuniandama niliacha kusoma na kuelekea kwenye rukuu. Lakini, Wallah, lau kama si hofu ya kupoteza eneo hili ambalo Mtume wa Mwenyezi Mungu aliamrisha lilindwe, ningependelea kufa kuliko kukatisha kisomo cha sura hiyo." (Abu Dawud, Taharat, 78/198; Ahmad, III, 344; Ibn Hisham, III, 219; Waqidi, I, 397)

Wakati wa safari ya kurudi nyumbani, Jabir ؓ aliendelea kubaki nyuma ya wenzake. Mtukufu Mtume ﷺ alimfuata na kumuuliza kwa nini alikuwa anabaki nyuma sana. Jabir ؓ alipoeleza sababu, Mtume wa Rehma ﷺ alimchochea kidogo kwa ulaini ngamia wa Jabir kwa kutumia fimbo yake. Ngamia huyo akaanza kupiga hatua kubwa kiasi kwamba alikuwa sambamba na ngamia wa Mtukufu Mtume ﷺ.

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akaanza kuzungumza na Jabir ؓ, akagundua kuwa muda si mrefu alikuwa ameoa na hivyo alikuwa ameelemewa na mzigo wa baadhi ya madeni. Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuuliza Jabir kuwa alikuwa anamiliki nini kwa wakati huo.

"Ngamia mmoja tu", Jabir ؓ alijibu. Mtume wa Rehma ﷺ akamuomba Jabir amuuzie ngamia wake kama njia ya kumsaidia kulipa deni lake. Jabir ؓ akakubalia, kwa sharti kwamba aruhusiwe kumtumia ngamia huyo mpaka atakapofika Madina. Baada ya kukanyaga ardhi ya Madina, Jabir ؓ alishika hatamu ya ngamia na kufika mlangoni mwa Mtukufu Mtume ﷺ kwa ajili ya kumkabidhi ngamia. Lakini alikutana na tukio la kushangaza. Sio tu kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alilipa thamani ya ngamia, bali pia alimrudishia Jabir ngamia huyo kama zawadi. (Bukhari, Jihad, 49; Buyu', 34; Muslim, Musaqat, 109)

Jabir ﷺ mwenyewe anasimulia:

"Wakati nikirudi na ngamia huyo baada ya tukio hilo la ukarimu wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, nilikutana na Yahudi mmoja ninayefahamiana naye. Nikamueleza kilichotokea. Alishangazwa sana akawa anauliza mara kwa mara, 'kwa hiyo amelipia thamani ya ngamia kisha akakurejeshea?', kila mara nilimthibitishia juu ya kilichotokea." (Ahmad, III, 303)

Waumini walivutiwa mno na habari waliyoisikia juu ya kitendo cha ukarimu wa hali ya juu kilichofanywa na Mtukufu Mtume ﷺ, wakaukumbuka usiku huo kama*Laylatul-Bair,* yaani Usiku wa Ngamia.

Vita vya Badr Ndogo (Dhilqadah, 4/ Aprili, 626)

Kwa mujibu wa ahadi yao ya maneno kabla ya kuondoka katika uwanja wa Uhud, Waislamu na washirikina wangekutana tena katika eneo la Badr katika mwaka wowote ule kwa ajili ya mapambano. Lakini kwa sababu ya hisia za muda zilizomlazimisha kuitekeleza ahadi yake, Abu Sufyan aliliongoza jeshi la waabudu - sanamu mpaka kwenye eneo la Marr'uz-Zahran, ambapo, kutokana na kuzidiwa na wasiwasi na khofu, alihisi ulazima wa kurejea Makka. Hata hivyo, akiwa hataki kukimeza kiburi chake, alimtuma mjumbe kwenda Madina kuwataarifu kuwa alikuwa ameshatoka Makka na jeshi kubwa. Kwa kuwatisha, Abu Sufyan alitaka kuhakikisha kwamba Waislamu wanabaki Madina na hivyo kurudi na ushindi bandia.

Hata hivyo,kilichozidisha hali ya Abu Sufyani ya kukata tamaa, ni kuwa wakati mjumbe wake anawasili mjini Madina, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekwisha kamilisha mapema kabisa maandalizi yake kwa ajili ya vita, na alikuwa ameshawaamrisha Maswahaba

kuanza safari. Mjumbe huyo alijua kuwa Abu Sufyan ambaye alikuwa na hofu atakuwa anajiandaa kuwaongoza washirikina kurejea Makka; hivyo alifanya kila awezalo kuwatisha na kuwavunja moyo Waislamu wasiondoke Madina. Alikuja na urongo mkubwa, akidai kuwa iwapo Waislamu watakabiliana na washirikina katika huko Badr watapata hasara kubwa na kushindwa vibaya sana. Juhudi zake, zikisaidiwa na propaganda za wanafiki, hazikwenda patupu, baadhi ya Maswahaba walianza kuhisi shaka kidogo kutoka nyoyoni mwao kama kwenda kupigana vita lilikuwa jambo sahihi. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu Ambaye nafsi yangu ipo mikononi Mwake, hata kama asipotokea yeyote atakayefuatana nami, nitakwenda Badr peke yangu!" Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akawasaidia Waislamu kwa kuziongezea nguvu nyoyo zao. (Ibn Sad, II, 59; Waqidi, I, 386-387)

Hatimaye jeshi la Waislamu liliwasili Badr. Hapakuwepo hata athari ya adui. Kitu pekee kilichokuwepo ni maonesho madogo ya shughuli za kibiashara jirani na medani hiyo. Hivyo, hakuna kilichokuwa kimebaki kwa Waislamu zaidi ya kujiingiza katika kufanya baadhi ya biashara. Hata hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba waliendelea kubaki Badr kwa muda wa siku nane ili kuona kama adui anaweza kutokea; hata hivyo, hali iliendelea kuwa hivyo hivyo na Waislamu wakarejea Madina wakiwa na faida walioipata kutokana na biashara waliyoifanya katika maonesho hayo.[167]

Ujasiri na msimamo uliooneshwa na Waislamu katika tukio hili umesifiwa na Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

167. Ibn Hisham, III, 221; Ibn Saad, II, 59; Waqidi, I, 384-389.

الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُواْ لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَاناً وَقَالُواْ حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ فَانقَلَبُواْ بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ لَّمْ يَمْسَسْهُمْ سُوءٌ وَاتَّبَعُواْ رِضْوَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ

"Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu." (al-Imran, 3: 173-174)

Kwa mujibu wa Abdullah ibn Abbas ﵄, Nabii Ibrahim ﵇ ndiye aliyekuwa wa mwanzo kusema, 'Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa' muda mfupi tu kabla ya kutupwa katika moto. Mtukufu Mtume ﷺ aliyarudia maneno haya pindi alipoambiwa kuwa waabudu – sanamu wamejikusanya kwa wingi dhidi yake wakiwa na jeshi kubwa. Hivyo, *Iman* ya Maswahaba wote ikaongezeka kwa kuyarudiarudia maneno haya ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, wakaonesha mfano kamili wa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu.[168]

168. Tazama: Bukhari, Tafsir, 3/13.

MWAKA WA TANO WA HIJRA

Salman Farisi Aukubali Uislamu na Kuachiwa Huru

Salman Farisi, au Salman Muajemi ﷺ, ambaye awali alikuwa mtumwa wa Myahudi mmoja wa Madina, anamsimulia Ibn Abbas ﷺ safari yake yenye kusisimua ambayo ilifikia kikomo kwa yeye kuingia katika bustani iliyobarakiwa ya Uislamu:

"Nilikuwa nikiishi Jayy, kijiji kinachopatikana huko Isfahan. Baba yangu alikuwa miongoni mwa watu mashuhuri kijijini kwetu. Nilikuwa kipenzi chake mno katika maisha yake. Alinipenda kupita kiasi; hakuniruhusu kuondoka mbele yake. Daima alikuwa akinibakisha nyumbani, kama inavyokuwa kwa watoto wa kike, na ni mara chache sana alizoniruhusu kutoka nyumbani. Hali hiyo ilinifanya nizame sana katika imani ya dini ya Majusi, ambayo baba yangu alikuwa akiiamini na kuifuata, kiasi kwamba nilikuwa nimejipa jukumu la kuwasha na kuchochea moto mtakatifu hekaluni. Nisingekubali moto huo uzime hata kwa dakika moja.

Vilevile baba yangu alikuwa na shamba kubwa. Siku moja, kutokana na kuwa na shughuli nyingi za ujenzi, aliniambia: 'Kazi hii itanifanye nisipate nafasi kwa siku nzima, hivyo sitaweza kwenda shambani ... ni bora leo uende wewe huko.' Kisha akanieleza vitu vinavyotakiwa kuchukuliwa kutoka shamba, akaongezea kunambia: 'Lakini usikae huko zaidi ya muda unaotakiwa ukanifanya nijawe na wasiwasi na kuanza kukutafuta na hivyo kutoweza kumakinika kwenye kazi hii ninayotakiwa kuikamilisha!'

Alipokwishaniambia hivyo, nilielekea shamba. Njiani niliona kanisa moja la Kikristo. Nilijongea karibu zaidi na kusikia sauti kutoka ndani. Ilionekana kama wanasali. Lakini pia sikuwa na uhakika juu ya kile walichokuwa wakikifanya hasa, kwa maana baba yangu alikuwa amenifungia nyumbani kwa karibu kipindi chote cha maisha yangu. Hivyo sikuweza kuwa na uhakika juu ya kile hasa kinachofanywa na watu kanisani. Nikiwa ninataka kudadisi zaidi, niliingia kanisani ili nipate kujionea mwenyewe. Niliwatazama kwa muda. Mwishoni niliwaza: 'hakika dini yao yaonekana kuwa nzuri kuliko yetu.' Sikuondoka hapo kanisani mpaka jua lilipozama. Ama kuhusu shamba, sikwenda kabisa huko. Nikiwa ni mwenye kutaka kujua zaidi, niliwauliza wapi ninapoweza kuikuta dini yao kwa njia sahihi zaidi.

'Mjini Dameski', walinijibu. Jua lilikuwa limezama kabisa pindi niliporudi nyumbani kwa baba yangu, ambaye,niligundua kuwa alikuwa ameacha kazi yake na kuwatuma watu kwenda kunitafuta. Mara aliponiona akang'aka akisema: 'Ulikuwa wapi? Sijakwambia unachotakiwa kukifanya?'

'Ewe baba yangu! Niliwakuta watu wakiabudu ndani ya kanisa',nilianza kumfafanunulia. 'Nilivutika sana kwa kile walichokuwa wakifanya... kiasi kwamba sikugundua haraka kuwa jua lilikuwa limezama!'

'Katika dini yao hakuna kitu chenye manufaa kwako', aling'aka. 'Dini uliyonayo sasa, ambayo inatoka kwa babu zako, ndio njia bora!'

Kutokana na kuwa na wasiwasi kuwa naweza kukimbilia kwao, baba yangu alinifunga minyororo miguuni mwangu na kunifungia ndani. Hata hivyo, niliweza kutuma ujumbe kwa njia ya siri kwenda kwa watu wa kanisa, nikiwasisitiza 'wanitaarifu mara moja pindi msafara wa kibiashara utakapowasili kutoka Dameski'. Muda mfupi

baadaye nilipata habari kuwa msafara wa Wakristo unaoelekea Dameski ulikuwa umewasili. Kwa kiasi fulani niliweza kujikomboa kutoka kwenye minyororo ya chuma na kukimbia kanisani, ambapo niliungana na msafara huo uliokuwa ukielekea Dameski. Baada ya safari ndefu, tuliweza kuwasili Dameski.

Nilipofika huko, nilimtafuta mwanazuoni mkubwa wa mji huo. Wenyeji walinielekeza kwa askofu mmoja katika kanisa fulani. Nilipomuona nilimkimbilia. Wakati huo, alikuwa nje ya kanisa.

'Ninataka kujiunga na dini hii', nilimsihi. 'Nahitaji kubaki nawe, nilitumikie kanisa, nijifunze Ukristo kutoka kwako na nifanye ibada pembezoni mwako.'

'Njoo ndani!' alisema.

Niliingia naye kanisani. Siku zangu za kuishi hapo zikaanza. Baada ya muda mfupi nikagundua kuwa Askofu huyo wa Dameski hakuwa mtu mzuri kama wengi walivyofikiri. Alikuwa akiwaamuru watu wanaokuja Kanisani watoe sadaka kwa ajili ya watu maskini, kisha yeye huzikusanya na kuzihodhi. Siku moja nilimuona akichukua vyungu saba vilivyojaa sadaka za dhahabu na fedha, akazihodhi. Ghadhabu yangu ilikuwa ikiongezeka siku hadi siku. Lakini, haukupita muda mrefu askofu huyo akafariki dunia. Waumini wake walikuja kwa ajili ya kumfanyia ibada ya mazishi. Hapo ndipo nami nilipopata fursa ya kuepukana na makosa yaliyokuwa yakifanywa na askofu huyo.

'Alikuwa mtu muovu', niliwaambia waliohudhuria. 'Kweli alikuwa akiwahamasisha mtoe sadaka, lakini mara zote sadaka hizo alizitumia kwa anasa zake mwenyewe na hakuwapa maskini hata kidogo!'

'Umejuaje hilo?' waliuliza kwa udadisi.

'Ninaweza kuwaonesha mahali alipoficha hazina yake', niliwajibu.

Walivitoa vyungu saba vya dhahabu na fedha kwenye eneo nililowaonesha.

'Tunaapa kuwa hatutamzika!' walifoka kwa hasira. Walikuwa wakweli kwa ahadi yao hiyo, kwani badala ya kumzika, waliutundika mwili wake na kumpiga mawe. Walimleta askofu mwingine kuja kushika nafasi yake. Huyu alikuwa tofauti. Mpaka sasa, ukiacha wale wanaotekeleza swala tano kila siku, sikumbuki kuwa nimewahi kumuona mtu mwingine aliyekuwa ameipa kinyongo dunia. Aliitamani Akhera na kufanya ibada usiku na mchana.Baadaye, naye pia alikuwa katika kitanda cha mauti, akivuta pumzi zake za mwisho. Nilimwambia: 'Nimekuwa pamoja nawe muda wote huu na sijawahi kpenda mtu kama nilivyokupenda. Sasa waona wakati wako umewadia. Unaniusia kufanya nini baada yako? Niende kwa nani?'

'Ewe mwanangu! Simjui mtu anayefuata njia niifuatayo mimi', alisema kwa sauti ya chini. 'Watu wema wote wamekufa. Wale walio hai wameupotosha ukweli wa milele wa dini na kuyatelekeza mafundisho yake. Lakini nimekumbuka, kuna mtu mmoja katika mji wa Mosul, yuko katika njia kama yangu. Ni bora uende kwake.'

Baada ya mtu huyu mwema kufanriki dunia, nilielekea Mosul na kumkuta rafiki yake. Naye pia alifariki dunia, ambapo, kutokana na wosia wake nilielekea Nusaybin na kisha Ammuriya (eneo lililo jirani na Eskishehir). Huko, pamoja na mengine,niliweza kupata baadhi ya mali, ambazo ni ng'ombe na kondoo. Lakini, hatimaye, mauti yalibisha hodi kwa mtu huyo wa Ammuriya niliyekuwa kwake, naye pia akafariki dunia.

'Kwa kweli mwanangu! Simuoni mtu aliye katika njia yetu, ambaye naweza kukushauri uende kwake baada yangu... hakuna mwingine anayefuata njia yetu. Lakini, Mtume wa Zama za Mwisho yu karibu kuja; ni kama ninaona kivuli chake kikizunguka juu yetu. Mtume huyo atatumwa na kuhubiri dini ya Nabii Ibrahimu عليه السلام. Atadhihiri katika ardhi ya Arabia na kuhamia katika mji wenye mashamba ya mitende, uliozungukwa na maeneo mawili yenye mawe. Atapokea zawadi lakini hataigusa sadaka. Atabeba mhuri wa utume baina ya mabega yake. Kama una uwezo wa kwenda kwenye ardhi hiyo, nenda; usichelewe hata kidogo!'

Hatimaye alifariki dunia. Mwenyezi Mungu alipenda niendelee kubaki huko kwa muda mrefu kidogo. Kisha nilikutana na baadhi ya wafanyabiashara kutoka katika kabila la Kalb. Niliwapa kondoo na ng'ombe wangu kwa sharti kwamba wanipeleke Arabia. Walikubali na kuandamana nao. Lakini baada ya kufika katika Bonde la Qura, walinisakiti na kunifanyia khiyana, wakaniuza kama mtumwa kwa Myahudi mmoja. Nililazimika kubaki na Myahudi huyo kwa muda kidogo. Bonde la Qura ni eneo lenye miti mingi, hivyo, sikuweza kufanya lolote zaidi ya kuangalia iwapo nilikuwa nimefika mji ambao mwalimu wangu aliuelezea kuwa ndio mahali atakapohamia Mtume wa Zama za Mwisho. Lakini, japokuwa nilikuwa nimejenga matumaini makubwa, moyo wangu haukuwa umekinaika moja kwa moja.

Siku moja, nikiwa bado ninakaa katika Bonde hilo la Qura, binamu wa Myahudi huyo, kutoka katika ukoo wa Banu Quraydha, alininunua na kunichukua mpaka Madina. Wallah, nilipoiona tu Madina nikajua kuwa huo ndio mji aliouelezea mwalimu wangu kule Ammuriya. Sasa moyo wangu ulitua, nikaanza kumsubiri Mtume wa Zama za Mwisho. Sikuwa nikijua kuwa wakati huo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ alikuwa ameshadhihiri muda mrefu na kubaki miaka kadhaa katika mji wa Makka. Hata hivyo,

kutokana na kubanwa na majukumu yaliyotokana na kuwa mtumwa, sikuwa nimesikia chochote kumhusu. Kwa hakika sikuwa hata na wazo kuwa alikuwa ameshahamia Madina.

Siku moja, nilikuwa juu ya mtende, nikifanya kazi, na chini ya mtende huo alikuwa amekaa bwana wangu. Kisha akaja binamu yake akipiga kite: 'Washenzi hawa watu wa Aws na Khazraj! Wamekusanyika kwenye kijiji cha Quba wakimsikiliza mtu wanayedai kuwa ni mtume!'

Niliposikia maneno haya nilianza kutetemeka sana kiasi kwamba nilikaribia kudondoka.

'Umesemaje? Umesemaje?' niliuliza mara mbilimbili baada ya kushuka juu ya mti. Lakini, bwana wangu, ambaye alikuwa na hasira, alinipiga kofi kubwa lenye nguvu na kufoka: 'Inakuhusu nini hiyo? Wewe shughulika na mambo yako!'

'Hakuna tatizo', nilimwambia. 'Nilitaka tu kupata uhakika iwapo nilichokisikia kilikuwa ni kitu cha kweli.'

Ilipofika jioni, niliweza kuondoka Quba, nikaenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, nikachukua baadhi ya vitu vya kula ambavyo nilivitunza. Neno la kwanza nililomwambia ilikuwa: 'Ninasikia kuwa wewe ni mtu mwema na kwamba wafuasi wako ni wale walio maskini. Nimekuja na chakula ambacho nimekuwa nikikitunza kama sadaka. Niliposikia kuhusu hali yenu, niliona kuwa mtakuwa mnakihitajia zaidi kuliko mimi'. Kisha nikatoa nilichokuwa nacho kumpa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

'Chukueni chakula hiki mpate kujisaidia kwacho', alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwaambia Maswahaba wake na hakukigusa hata kidogo. 'Alama moja hiyo', nilisema nafsini mwangu. Kisha niliondoka na kurejea Madina. Kwa mara nyingine

nilikusanya vitu vingine zaidi. Wakati huo huo, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa amewasili Madina. Nilikwenda tena kwake.

'Niliona kuwa huchukui sadaka, lakini hii hapa ni zawadi niliyokuandalia', nilimwambia. Mara hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikula na kuwaambia Maswahaba nao wafanye kama alivyofanya. 'Alama ya pili', nilisema nafsini mwangu.

Baadaye, nilimtembea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ambaye wakati huo alikuwa katika Makaburi ya Baqi'ul-Gharqad, ambako alihudhuria mazishi ya Swahaba mmoja. Alikuwa amekaa katikati ya Maswahaba wake, akiwa amevaashuka mbili zilizomfunika kikamilifu.Nilimtolea salamu, kisha nikaenda nyuma yake, kwa matumaini ya kuangalia kama ninaweza kuuona mhuri wa Utume nilioelezwa na mwalimu wangu wa Ammuriya. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliibaini nia yangu; hivyo, taratibu alilishusha kidogo shuka lake katika sehemu ya mgongoni. Nilipouona tu niliutambua mhuri huo! Nilimuangukia, nikamkumbatia na kuanza kulia.

'Njoo upande huu', aliniambia Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hivyo, nilizunguka na kwenda kukaa mbele yake."

Salman رضي الله عنه alisita kidogo kumhadhithia Ibn Abbas رضي الله عنه, akamwambia:

"Ewe Ibn Abbas, nilimueleza Mtume wa Mwenyezi Mungu mambo yote niliyokumbana nayo, kama nilivyokueleza wewe. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na Maswahaba wake walifurahia sana kusikia kisa changu. Utumwa uliokuwa umemdhibiti Salman, haukumpa nafasi ya kuungana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika Vita vya Badr na Uhud." (Ahmad, V, 441- 444; Ibn Hisham; I, 233-242; Ibn Sad, IV, 75-80)

Sasa, Salman ﷺ alikuwa ameungana na Mtume aliyebarikiwa ﷺ, ambaye alikuwa akimtafuta kwa kipindi chote cha maisha yake. Hivyo, tamaa yake kubwa nilikuwa kuwa pembeni mwa Mtume huyu wa Mwisho ﷺ na kumhudumia. Kwa hakika, Mtukufu Mtume ﷺ alipoona jitihadi ya Salman ﷺ, siku moja alijaribu kumshauri kama aitawezekana kuwa: '...fanya makubaliano na bwana wako ili akuache huru.' Kweli, Myahudi yule alikubali kumuacha huru Salman ﷺ kwa sharti kwamba apande mitende mia tatu, ikiwa ni pamoja na kuchimba mashimo yake, vilevile amlipe *uqiyyah*[169] arobaini za dhahabu. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaamuru Maswahaba kumsaidia Salman ﷺ katika kutekeleza matakwa hayo. Wote walijitolea kwa kiwango chote cha uwezo wao na ndani ya kipindi cha muda mfupi, miche ya mitendemia tatu aliyohitaji Salman ﷺ ilikusanywa.

"Ewe Salman, chimba mashimo kwa ajili ya mitende hii, ukimaliza, niite nije kuipanda kwa mikono yangu mwenyewe", alisema Mtukufu Mtume ﷺ kumwambia Salman ﷺ.

Salman ﷺ anasimulia kilichotokea baadaye:

"Kwa msaada wa marafiki zangu, nilianza kuchimba mashimo kwa ajili ya kupanda miche hiyo ya mitende. Nilipomaliza kuchimba, nilienda na kumtaarifu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kurudi naye shambani na kuanza kupanda. Tulikuwa tukibeba miche na kumpa naye akipanda. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Ambaye nafsi yangu imo Mikononi mwake, kila mche uliopandwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ulistawi. Kwa hivyo, niliweza kutekeleza sehemu moja ya makubaliano. Mwaka mmoja tu baadaye mitende hiyo ilianza kuotesha tende kwenye matawi yake.

169. *Uqiyyah* moja ni sawa na gramu 128.

Haukupita muda mrefu, Mtume wa Mwenyezi Mungu alirejea kutoka vitani akiwa na ngawira. Katika ngawira hizo kulikuwa na kipande cha dhahabu chenye ukubwa wa yai. Aliagiza niitwe. Nilipofika mbele yake akasema: 'Ewe Salman, chukua kipande hiki ukalipe deni lako!'

'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kipande kidogo kama hiki kitawezaje kutosheleza kulipa deni kubwa linalonikabili?' nilimuuliza. Alikichukua kipande hicho na kukupangusa taratibu kwa ulimi wake na kuniambia: 'Chukua! Mwenyezi Mungu Mtukufu atalipa deni lako kwa kipande hiki!'

Nilikichukua hicho kipande cha dhahabu, kama nilivyoambiwa, na kukipeleka kwa Myahudi. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye nafsi ya Salman iko mikononi Mwake, kipande kile kiliweza kufikia uzito wa *uqiyyah* arobaini. Kipande hicho kilikuwa na baraka tele kiasi kwamba, hata mlima wa Uhud ungewekwa kwenye mizani moja na kipande hiki basi hiki kipande kingekuwa na uzito kushinda mlima huo.

Baaada ya kuachiwa huru na kuondokana na utumwa, Salman ﷺ alishiriki vilivyo katika Vita vya Khandaq, kama ambavyo hakubaki nyuma hata kidogo katika vita vyote vilivyotokea hapo baadaye na mara zote alikuwa bega kwa bega na Mtukufu Mtume ﷺ.[170]

Salman ﷺ alikuwa akipendwa mno na Maswahaba wenzake kiasi kwamba *Ansar* na *Muhajirun*, kila upande ulidai kuwa yu miongoni mwao. Lakini, bila shaka,sifa kubwa zaidi kuliko zote ilitolewa na Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe pale aliposema: "Salman ni katika sisi; *Ahlul-Bayt.*" (Ibn Hisham, III, 241)

170. Tazama, Ahmad, V, 443-444; Ibn Athir, *Usd'ul-Ghabah*, II, 419; Ibn Abdilbar, II, 634-638.

Katika kipindi chote cha maisha yake, mwenendo wa Salman ﷺ uliakisi uzuri wa maadili ya Kiislamu, ambapo aliacha athari ghali kwa wengine wapate kumfuata. Mfano mmoja wapo ni huu ufuatao:

Baada ya Dola ya Kiislamu kutawala eneo kubwa la mamlaka yake, Salman ﷺ, ambaye hapo awali alikuwa mtumwa wa Myahudi mmoja, sasa aliteuliwa kuwa Gavana katika eneo la Madain, ambalo hapo awali lilikuwa likitawaliwa na Wasassani. Mtu mmoja wa kabila la Taym, kutoka Dameski, alikuwa amewasili Madain akiwa na gunia la tini. Alimuona Salman ﷺ, ambaye hakuweza kumtambua kutokana na joho lake la sufi la hali ya chini alililokuwa amelivaa.

"Njoo, beba gunia hili", alimuita Salman ﷺ, ambaye, bila kutamka neno lolote, alinyanyua gunia na kuliweka begani mwake na kuanza kutembea. Lakini, tofauti na Mdameski huyo, wananchi walimtambua haraka gavana.

"Mtu huyo aliyebeba mzigo wako ni gavana!" walimfokea. Mtu yule alitaharuki na kuanza kuomba msamaha na kuomba asamehewe kwa kushindwa kumtambua kiongozi huyo.

"Hakuna tatizo", Salman ﷺ alimjibu kwa hali ya upole na ulaini. "Nitalibeba gunia hili mpaka nilifikishe mahali unapotaka lifike!" (Ibn Sad, IV, 88)

Kufutwa kwa Desturi ya Kuwaasili Watoto

Zayd ﷺ, ambaye, akiwa mtoto, aliletwa na bibi Khadija ﷺ kwa Mtukufu Mtume ﷺ kama zawadi kabla ya Utume, Mtukufu Mtume ﷺ alimuacha huru. Lakini Zayd ﷺ alipendelea kubaki kwa Mtukufu Mtume ﷺ kuliko kwenda nyumbani kwa baba yake. Hivyo Mtukufu Mtume ﷺ akamuasili na kumfanya kuwa mwanaye.

Kwa kuwa alimpenda mno Zayd ﷺ, Mtukufu Mtume ﷺ alimuozesha kwa Umm Ayman, ambaye naye aliwahi kuwa mtumwa kama Zayd na kuachwa huru na Mtukufu Mtume ﷺ, na baadaye akamuozesha kwa Zaynab bint Jahsh ﷺ, mtoto wa shangazi yake. Japokuwa mwanzoni, Zaynab alikuwa amesita kuolewa na Zayd, shauri hilo la Mtukufu Mtume ﷺ, likiungwa mkono na aya ifuatayo, lilimfanya akubali:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ

"Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi..." (al-Hujurat: 13)

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا

"Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi." (al-Ahzab: 36)

Hata hivyo, bado moyo wa Zaynab haukuwa umefurahishwa na Zayd, na matokeo yake, muda mfupi baada ya kuoana, walijikuta wakiwa kwenye ukingo wa kutengana na kuachana. Naye Zayd alikuwa na malalmiko yake dhidi ya Zaynab. Hatimaye aliyafunua matatizo yake ya ndoa mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ ambaye alimshauri kuwa:

"Shikamana na mkeo, na mche Mwenyezi Mungu!"

Ni wakati huo ambapo ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu ulimtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ kuwa Zaynab ataolewa naye; lakini alifanya kuwa siri kwa kuhofia ukosoaji ambao ungetoka kwa wanafiki, ambao wangevurumisha kimbunga cha upinzani wakidai kuwa 'Muhammad amemuoa mtalaka wa mwanaye'. Desturi na ada za wakati huo zilimpa mtoto wa kuasili hadhi ya mtoto wa kuzaa – walikuwa wakichukuliwa kuwa ni watoto wao, wakipewa ubini wao na kurithi.

Haukupita muda mrefu baada ya Zayd na Zaynab ﷺ kuachana, ukaja Ufunuo mwingine. Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa ameamuru kuwa Mtume Wake amuoe Zaynab. Hii ilimaanisha kuwa Mtukufu Mtume ﷺ atakuwa mtu wa kwanza kutekeleza amri itakayofuta desturi na mila ya kuasili watoto ambayo ilikuwa ikifanywa katika Zama za Ujahiliyya:

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللَّهَ وَتُخْفِي فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَن تَخْشَاهُ ۖ فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا ۚ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا

"Na ulipo mwambia yule Mwenyezi Mungu aliye mneemesha, nawe ukamneemesha: Shikamana na mkeo, na mche Mwenyezi Mungu. Na ukaficha nafsini mwako aliyo taka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye mwenye haki zaidi kumchelea. Basi Zaid alipo kwisha haja naye tulikuoza wewe, ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa

watoto wao wa kupanga watapo kuwa wamekwisha timiza nao shuruti za t›alaka. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa." (al-Ahzab: 37)

Zaynab ﵂, ambaye aliolewa na Mtukufu Mtume ﷺ kwa amri ya Mwenyezi Mungu, mara zote alikuwa akieleza furaha yake kwa kusema: "Mola wangu ndiye aliyeniozesha!" (Tirmidhi, Tafsir, 33/3213)

Lakini tukio hilo liliwasha cheche za moto wa uvumi mbaya miongoni mwa wanafiki, ambao walianzakudhihirisha chuki yao kwa kuonesha ukosoaji wenye maudhi kwa Mtukufu Mtume ﷺ juu ya kile walichokieleza kuwa ni kumuoa mtalaka wa mtoto wake. Lakini jibu likaja moja kwa moja kutoka ndani ya Qur'an Tukufu:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ
وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا

"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu." (al-Ahzab, 40)

Tukio hilo lilihitimisha ada na mila ya kuwaasili watoto iliyokuwa ikifanya katika kipindi cha Zama za Ujahiliyyah.

Tuhuma zinazotolewa leo hii na wanafiki wa zama hizi, ambao wanadai kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alivutiwa na uzuri wa Zaynab na hivyo ikawa sababu ya kumuoa, ni tuhuma zisizokuwa na mashiko ambazo ni alama ya ujinga. Kwa sababu, Zaynab ﵂ ni binamu wa Mtukufu Mtume ﷺ, binti wa shangazi yake. Hii ina maana kwamba alikuwa akimuona sana katika matukio mbalimbali kabla ya hapo. Kama Mtukufu Mtume ﷺ angekuwa na nia hiyo, angemuoa Zaynab

kwa urahisi kabisa kabla ya Zayd. Ndoa ambayo Zaynab asingekuwa na tabu nayo kabisa.

Watu wenye akili nyepesi wamezoea sana kutathmini ndoa kwa mtazamo wa kimatamanio tu na hawajui wala kuelewa uhalisia wa ndoa zilizofungwa na Mtukufu Mtume ﷺ.Hukumu za kijinga na za upendeleo zinazotolewa na wale waliozijaza akili na nyoyo zao mielekeo ya nafsi si jingine zaidi ya ishara za chuki na ulimwengu wenye giza. Mtukufu Mtume ﷺ alitumia miaka ishirini na nne ya maisha yake ya ndoa, umri wa ujana ambao kwa kawaida huwa na nguvu na nishati nyingi, aliutumia akiwa na bibi Khadija ؓ. Ndoa alizofunga baada ya bibi Khadija ؓ moja kwa moja zilikuwa na sababu maalumu, iwe za kisiasa au za kijamii, lakini daima zilikuwa kwa malengo ya kuimarisha Uislamu. Idadi kubwa ya wanawake hao walikuwa wajane na walikuwa na umri mkubwa kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Katika wanawake hao, ni bibi Aisha ؓ pekee ndiye aliyekuwa kijana na hakuwa ameolewa kabla ya hapo. Hata ndo hiyo pia ilifungwa ili kuimarisha safari ya kusafirisha mafundisho sahihi ya Uislamu, hususani mambo yanayohusu wanawake, kwenda kwa vizazi vya baadaye vya Waislamu. Kwa sababu hiyo, Aisha ؓ alijaaliwa uelewa na akili hali ya juu iliyomuwezesha kuyashika na kuyafahamu vyema mafundisho tatanishi ya masuala ya kisheria yanayohusu wanawake, na kwa miaka mingi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea kuwa nuru kwa wanawake wa Kiislamu kwa elimu na maarifa yake adhimu pamoja na kuwa nguzo kubwa ya kiungo muhimu sana cha sheria ya Kiislamu. Mmoja katika *mafukahaa* (wataalamu wa sheria za Kiislamu) saba ambao walikuwa na maarifa makubwa kuliko maswahaba wengine, alifikia daraja hiyo kupitia maarifa ya bibi Aisha kuhusu sheria ya Kiislamu na kuwa mnara miongoni mwa wanawake wa Kiislamu.

Kama ndoa hizi zingekuwa zimehamasishwa na matamanio, kama inavyodaiwa na wale wenye chuki, bila shaka Mtukufu Mtume

ﷺ asingepoteza muda wake mwingi wa ujana na wenye nishati katika maisha yake kwa kuishi miaka kumi na tano na mwanamke mwenye umri mkubwa ambaye alikuwa na watoto aliowazaa kabla ya kuolewa naye. Watu wenye hekima na utambuzi, wenye ujuzi wa mantiki ya kipekee ya imani, wanaweza kutambua hekma inayopatikana katika ndoa hizi na matokeo matukufu yaliyotokana nazo.

Amri ya Kujisitiri: Hijabu

Kabla ya Uislamu, Waarabu hawakuwa na wazo au dhana ya *hijab*, hali ambayo iliendelea mpaka miaka ya mwanzo ya Uislamu. Lakini, kama tulivyoeleza hapo awali kuhusu utaratibu wa kuharamisha jambo hatua kwa hatua kama ilivyokuwa katika suala la pombe na kamari, ilikuwa wazi kuwa suala hilo lisingeendelea kuwepo. Hatimaye, aya inayohusu *hijab* iliteremshwa, ikaenda sanjari na kuinua hadhi ya wanawake na kuongeza sifa yao kwa kulinda heshima na utu wao. Wanawake wanageuzwa kuwa alama ya staha na kujaaliwa utambulisho wenye utukufu na hadhi ya juu.

Kwa upande mweingine, sheria ya *hijab* haiwahusu wanawake pekee, bali pia inawahusu wanaume. Hii ina maana kwamba amri hii inashirikisha jinsia zote mbili za wanaume na wanawake, na kuwawajibisha wote. Hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

قُل لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ۚ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ وَقُل لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۖ وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

"Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za wanayo yafanya. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa unao dhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao..." (an-Nur: 30-31)

Kujisitiri hulinda hulka na silka ya kike. Kwa kuvaa *hijab*, mwanamke hutengeneza hali ya umaridadi na tabia njema. Na hivyo, mwanamke asiyejisitiri hugeuka kuwa zana ya matamanio na kujistareheshea ambayo huibua matamanio ya nafsi; na yote hayo hubomoa haiba, silika na utu wake, na kuishusha heshima na hadhi ya umama.

Kuna jambo moja ambalo lazima kuliashiria hapa,nalo ni kuwa, kuna tofauti ya kiasili baina ya nafsi za wanaume na wanawake, tofauti inayotokana na maumbile, na hivyo wajibu na dhima zinazotofautiana walizopewa na Mwenyezi Mungu ndizo zilizopelekea kuwepo kwa tofauti yao ya maumbile. Kwa maana hiyo, namna ya kujistiri kunatofautiana kati ya wanaume na wanawake. Tofauti na wanaume, wanawake wamejaaliwa uzuri na mvuto mkubwa. Mwanamke anayejiweka mbali na *hijab*, na kwa maana hiyo akajianika kwa watu, huuharibu na kuubomoa umaridadi na hadhi yake.Na kwa hiyo, sifa yake adhimu ya umama nayo hupata pigo la kiwango hicho hicho. Na ili kuchukua hatua dhidi ya yote hayo na kwa njia ya *hijab*, uzuri wa mwanamke umelindwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya mumewe tu. Baina ya mwanaume na mwanamke, mkondo wa kiasili na usiobadilika unaotokana na muongozo wa kisilika, ambao ni lazima uwepo ili kuendeleza kizazi cha binaadamu, muelekeo ambao bila kutii amri ya *hijab*, utapelekea kuchupa mipaka ya Mwenyezi Mungu na kuleta janga la uharibifu wa kimaadili. Bila shaka, miongoni mwa maana za amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo:

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنَىٰ

"Wala msikaribie uzinzi...!" (al-Isra: 32) ni 'msifungue milango ya uzinzi kwa kuidharau na kuikaidi *hijab*; msiweke msingi wa uzinzi!' Hii ni sheria ya moja kwa moja. Ni muhimu kuelewa kuwa Uislamu haukuweka amri hiyo ya kujisitiri kwa wanawake wenye mvuto pekee na kwa sababu tu hiyo hiyo moja. Yaani, mtu asiseme kuwa 'huna mvuto na hivyo usijifunike'; kwa sababu *hijab* kama *hijab* haikuwekwa kwa sababu ya mvuto bali inalenga kulinda utu na heshima ya mwanamke kwa ujumla.

Uislamu ambao umeweka sheria zake kulingana na silika ya maumbile ya mwanadamu, unazingatia pia kile kinachotakiwa kwa jinsia ya kiume na ya kike. Ni kwa sababu hiyo kwamba Mtukufu Mtume ﷺ aliwalaani wanaume wanaojaribu kuenenda na wanawake wanaojaribu kuenenda kama wanaume.[171] Ili kujilinda na hatari hii, wanawake wanapaswa kusuhubiana na wanawake wema; kwa maana, unaposuhubiana na mtu, baada ya kipindi kadhaa cha muda huchukua tabia zake. Hii ni kanuni ya saikolojia. Pindi wanawake wanapozoea kushiriki mazingira ya aina moja na wanaume, hupoteza hisia za uke na tabia zote za kike zisizokuwa na mbadala.

Imekatazwa pia kuvaa vazi la jinsia nyingine. Mtukufu Mtume ﷺ amesisitiza kuwa wanaume wanaovaa kama wanawake na wanawake wanaovaa kama wanaume,watawekwa mbali na Rehma za Mwenyezi Mungu.[172] Aidha, kuiga mavazi ya jinsia nyingine husababisha kasoro katika tabia. Wakati huohuo, ukengeukaji katika uchaguzi wa mavazi, huakisi jinsi mtu alivyo na kuidhibiti tabia yake na hilo linakuwa na maana kuwa silika yake ya kimaumbile imeangamizwa.

171. Tazama: Bukhari, Libas, 61.

172. Tazama: Abu Dawud, Libâs, 28/4098.

Vita vya Muraythi
(Shaban-Ramadhan, 5 / Januari-Februari, 627)

Vita hivi pia vinajulikana kama Vita vya Banu Mustaliq. Vimepewa jina hilo kwa sababu kabila hilo lilihamasishwa na Washirikina wa Makka kuishambulia Madina na hivyo wakaanza kufanya maandalizi makubwa ya kijeshi. Mtukufu Mtume ﷺ alipopata habari ya mpango wao, aliandaa jeshi kubwa la watu mia saba kwa ajili ya kukabiliana nao. Hivyo makundi hayo mawili yakakabiliana. Mtukufu Mtume ﷺ alimwambia Omar ؓ awaambie kuwa: 'Semeni *La ilaha illa-Allah* mtaziokoa nafsi zenu na mali zeno!' Sio tu kwamba Banu Mustaliq walikataa wazo hilo, bali pia wao ndio walioanza kutupa mshale wa kwanza ulioanzisha makabiliano.[173]

Vita vilifikia tamati kwa Waislamu kupata ushindi dhidi ya Banu Mustaliq. Vita hivi vilipiganwa katika eneo la Maji ya Muraythi. Askari kumi wa adui waliuawa katika medani ya vita, ilhali swahaba mmoja tu kwa upande wa Waislamu ndiye aliyeuawa kishahidi. Mali ya ngawira na mateka, akiwemo Juwayriya bint Harith, chifu wa kabila hilo, vilichukuliwa baada ya Vita.

Baadaye mateka waliachiwa huru, mmoja baada ya mwingine, baada ya kutoa fidia. Wakati huohuo Juwayriya alikuwa katika fungu la ngawira za Thabit ibn Qays. Akatoa ombi rasmi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ili aweze kumtolea fidia. Wakati huohuo, baba yake alikuwa amewasili. Baada ya kuona heshima yake ya kuwa binti wa chifu, baba yake alisisitiza kuwa binti yake asingeweza kufanywa kuwa mtumwa kwa njia yoyote ile na alikuwa akiomba heshima yake ilindwe. Alionesha kwa mkono wake ngamia

173. Tazama: Waqidi, I, 407.

aliowaleta na kusema: "Ngamia hawa ni fidia kwa ajili ya binti yangu, tafadhalini, muacheni huru!"

Alipokwisha kusema hivyo, bila kutegemea, Mtukufu Mtume ﷺ akamuuliza wapi alipokuwa ameficha 'ngamia wengine wawili aliokuwa amewaleta?'

Harith alishituka sana, kwa maana hakuna mtu mwingine aliyekuwa anajua kuwa alikuwa amewaficha ngamia wawili katika bonde la jirani. Hapo akasilimu, yeye pamoja na msafara wake wote.[174]

Baadaye Mtukufu Mtume ﷺ alitaka maoni yaJuwayriya. Alieleza wazi kuwa anapendelea kuendelea kuwa jirani naye, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe alilipa fidia yake na kumuacha huru (Ibn Sad, VIII, 118). Baada ya kuwa ameshakuwa huru, Juwayriya aliamua kusilimu kwa hiari yake mwenyewe.Kuna baraka nyingine ambayo ilikuwa njiani kutokea: alipata heshima ya kuolewa na Mtume wa Mwisho, Muhammad ﷺ, ikiwa ni kutimia kwa ndoto aliyowahi kuiota. Hii ndiyo hasa ya yeye kupendelea kubaki kwa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ, licha ya kwamba alikuwa ameshaachiwa huru, na angetaka kuondoka angeondoka, kupitia fidia iliyotolewa na baba yake.

Baada ya Maswahaba kupata taarifa kuwa Juwayriyya ataolewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, waliona kuwa isingekuwa sahihi kuendelea kuwashikilia mateka ndugu wa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ, hivyo wakawaacha huru. Baadaye bibi Aisha رضي الله عنها aliwahi kusikika akisema kuhusu kadhia hii: "Hatukuwahi kumuona mwanamke mwenye shakhsia na hadhi kubwa kabisa kuliko Juwayriyyah katika wanawake wa kabila lake. Familia mia moja za Banu Mustaliq ziliachwa huru kwa ajili yake." (Abu Dawud, Itq, 2/3931)

174. Tazama: Ibn Hisham, III, 340.

Vita vya
Bani Mustaliq
Aws na Khazraj
Juhayna
MADINA
Dhu'l-Khulayfah
Muzayna
Sulaym
Ghifar
Abwa
Badr
Juhfah
Rabigh
MURAYSI
Huzaa
Qudayd
BAHARI NYEKUNDU
Amaj
Adal and Qarah
Huzayma
Uzdan
Hudaybiyah
MAKKAH
Quraysh
Hawzin
Arafat
Taif
Thakif
Mazin
Azd

Kama tulivyoona, ndoa ya Mtume ﷺ ilifanyika kwa sababu za moja kwa moja wa kisiasa, na kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

"Wala hatamki kwa matamanio. Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa..." (an-Najm, 3-4), haikufanyika kutokana na matamanio, bali ilifanyika kwa malengo na madhumuni yaliyotakiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mateka wa Banu Mustaliq waliachwa huru, hawakutoa chochote, na zaidi ya hapo, wote waliungana na safu za Uislamu.

Tayammum

Bibi Aisha ؓ anasimulia:

"Tulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika Vita vya Muraythi. Tulikuwa tumefika katika eneo liitwalo Bayda au Dhatul-Jaysh, ambapo nilibaini kuwa bangili yangu ilikuwa imechomoka na kudondoka. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akabaki hapo kwa muda akiitafuta; hivyo watu wengine nao wakabaki naye. Katika eneo tulilokuwa hapakuwa na maji,na mbaya zaidi, sisi tulikuwa tumechoka. Baadhi walimlalamikia baba yangu Abu Bakr, wakisema: 'Unajua Aisha kafanya nini? Amemzuia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu pamoja na wengine katika eneo ambalo halina maji, nasi tukiwa tumechoka!' Mara alikuja Abu Bakr na kumkuta Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa amelala usingizi akiwa amekiweka kichwa chake juu ya paja langu.

'Umemuweka hapa Mtume wa Mwenyezi Mungu na watu wengine! Sio tu kwamba mahali hapa hakuna maji, bali pia maji yamekwisha!' alisema kwa kunilaumu. Kwa kushindwa kuizuia ghadhabu yake, alinipiga kidogo. Nilijaribu kutotikisika kwani

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amekiweka kichwa chake juu ya magoti yangu akiwa amelala.

Pindi Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoamka asubuhi bado maji yalikuwa hayajapatikana. Haukupita muda mrefu, Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ya *tayammum*:

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

"Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru." (al-Maida: 6)

Hapo Usayd ibn Khudayr ؓ akasema: 'hii ni miongoni tu mwa baraka zenu nyingi kwa *ummah* huu enyi familia ya Abu Bakr.'

Ngamia alipoamka na kusimama wima, tuliweza kuiona bangili ile ikiwa imelala chini yake." (Bukhari, Tayammum, 1; Ashab'un-Nabi, 5, 30)

Vilevile Usayd ؓ alimsifu Aisha ؓ akisema: "Mwenyezi Mungu akulipe kheri, kwa maana kila ulipokabiliana na jambo lislokuwa zuri, Mwenyezi Mungu alilibadilisha kuwa kheri, kwako na kwa Waislamu." (Bukhari, Tayammum, 1)

Tukio la *Ifk* au Kashfa na Uzushi

Kwa mara nyingine ilikuwa wakati wa kurejea kutoka katika vita vya Muraythi, ambapo bibi Aisha ﵂,[175] mke msafi na mtukufu wa Mtume ﷺ alikuwa amekwenda faragha kidogo kwa ajili ya haja maalumu. Lakini aliporejea jeshi lilikuwa limeshaondoka. Kwa kuwa wakati huo aya ya *hijab* ilikuwa imeshateremshwa, bibi Aisha ﵂, mama wa Waumini, alikuwa akisafiria ndani ya *hawdaj* iliyokuwa ikiwekwa juu ya kikalio cha ngamia. Hivyo, pindi jeshi lilipoondoka, Waislamu walidhani kuwa Aisha ﵂ bado alikuwa ndani ya *hawdaj*.

Aisha ﵂ alipoona ameachwa na jeshi na kwa hofu ya kupotea, badala ya kulifuata, aliamua kutotoka mahali alipokuwa. Wakati akiendelea kusubiri, alipitiwa na usingizi.

Safwan ibn Muattal ﵁, ambaye alikuwa amekabidhiwa jukumu la kuwakusanya wale wote waliokuwa wamebaki nyuma na ambao walikuwa wameachwa na jeshi, alimuona. Ili kumshtua Aisha ﵂, ambaye alikuwa amesinzia, alisema:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُون

"Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea..." (al-Baqara: 156).

Sauti hiyo ilimshtua Aisha ﵂ akaamka. Bila kutamka neno lolote, Safwan ﵁ alimuinamisha ngamia akapiga magoti na Aisha ﵂ akapanda. Waliwafikia Waislamu wengine wakati wa mchana. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Lakini wanafiki, kana kwamba sasa wali-

175. Kabla ya kwenda vitani, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa kipiga kura baina ya wake zake kuchagua mmoja atakayesuhubiana naye. Mara hii aliteuliwa Aisha ﵂

kuwa wamepata fursa nzuri ya kuonesha chuki yao, walikuwa na kitu kingine akilini mwao. Walishusha kashfa mbaya:

"Aisha hakubanduka kwa mwanaume huyo, wala mwanaume huyo hakubanduka kwa Aisha", walisema. Abdullah ibn Ubayy alikwenda mbali zaidi katika istihzai yake, akasema kuwaambia Waislamu: "Angalieni mke wa Mtume wenu...ametumia usiku mzima akiwa na mwanaume mwingine!"

Haraka sana, uvumi huu ulienea ndani ya jeshi lote. Pindi Abu Bakr ﷺ aliposikia taarifa hizo akaanza kutetemeka kwa uchungu usioelezeka. "Wallah, hata katika zama za Ujahiliyyah hatukuwahi kuwa na kashfa kama hiyo!" alilalama kwa masikitiko.

Safwan ﷺ, Sahaba ambaye aliwahi kuelezewa na Mtukufu Mtume ﷺ kuwa: "Hakika sioni ubaya wowote kwake zaidi ya kheri", sasa alikuwa katika huzuni ya hali ya juu.

Ama kwa upande wa Mtukufu Mtume ﷺ, bila shaka alikuwa ametamalakiwa na miale ya moto wa uhuzuni iliyokuwa ikiuchoma moyo wake. Kwa muda fulani, alilazimika kutotoka nje na kwa kiasi fulani akawa haonani na watu. Vilevile aliagiza kufanyika kwa uchunguzi mdogo juu ya suala hilo.

Hapakuwa hata na chembe ya ushahidi ilimuweka Aisha ﷺ hatiani. Lakini vinywa vya wanafiki havikukaa kimya.

Aisha ﷺ, ndiye aliyekuwa wa mwisho kusikia uvumi huo. Akiwa ameshikwa na huzuni nzito mno kama ilivyotarajiwa, alikusanya nguvu kwa kadiri alivyoweza, na baada ya kupata ruhusa kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ, alienda nyumbani kwa baba yake ili kuona kulikoni. Alipopewa maelezo ya kile alichokuwa akituhumiwa, aliishiwa nguvu, akanywea na kunyauka kama jani la majira ya kipupwe.

Mtukufu Mtume ﷺ alitaka kuzungumza na Aisha ؓ. Hivyo akaenda nyumbani kwa Abu Bakr ؓ:

"Nimekuwa nikisia mambo fulani. Kama huna hatia, Mwenyezi Mungu atalisafisha jina lako!"

Akiwa amehisi kitu kutoka katika maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ, Aisha ؓ, mwanamke mwema na mwenye hisia ya moyo na utambuzi, aliwatazama kwa huruma wazazi; lakini walikaa kimya. Kisha, macho yake yakitiririsha machozi, alisema maneno yafuatayo yenye hisia kali kumwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

"Wallah, kwa kiasi fulani nina hakika kuwa nawe pia unakaribia kuyaamini mambo hayo uliyoyasikia. Sasa, iwapo ningekwambia kuwa sina hatia – na kwa hakika Mwenyezi Mungu najua kuwa sina hatia – huwenda usingeniamini. Lakini, iwapo ningekwambia kinyume chake, ungeamini. Lakini Mwenyezi Mungu anajua kuwa sina hatia ... hivyo, nitasubiri msaada Wake dhidi ya yote yanayosemwa..."

Uvumi huo ukiwa umeenea kila kona, mahojiano yafuatayo yalitokea baina ya Abu Ayyub al-Ansari ؓ na mkewe Umm Ayyub ؓ:

"Umesikia yanayosemwa na watu kuhusu Aisha?" Umm Ayyub alimuuliza mumewe.

"Ndiyo, nimesikia, na maneno hayo yote ni uwongo mtupu unaozushwa", alijibu Abu Ayyub. "Je wewe waweza kufanya kitu kama hicho?"

"Hapana, siwezi kufanya uovu kama huo hata kidogo", alijibu Umm Ayyub, na hapo mumewe akasema: "Basi tambua kwamba Aisha ni mwema na mnyoofu zaidi kuliko wewe na kama wewe

huwezi kufanya hivyo basi yeye ni zaidi!" (Ibn Hisham, III, 347; Waqidi, II, 434)

Wahyi pekee ndio ulioweza kutuliza hali ya mambo; haukupita muda mrefu sana Mwenyezi Mungu Mtukufu akahitimisha uvumi huo. Ilidhihirika kuwa maneno hayo yaliyokuwa yakisemwa yalikuwa uzushi tu wa wanafiki. Sambamba na kumtakasa Aisha ﵂ dhidi ya hatia yoyote, pia tangazo hilo la Mwenyezi Mungu lilivurumisha urongo huu kwenye nyuso za wanafiki hao na kuwapa habari juu ya adhabu inayowasubiri na vilevile kuwaonya wajinga watakaoendelea na urongo huo usiokuwa na msingi wowote:

إِنَّ الَّذِينَ جَاؤُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنكُمْ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ لِكُلِّ امْرِئٍ مِّنْهُم مَّا اكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ

"Hakika wale walio leta uwongo ni kundi miongoni mwenu. Msifikiri ni shari kwenu, bali hiyo ni kheri kwenu. Kila mtu katika wao atapata aliyo yachuma katika madhambi. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa miongoni mwao, atapata adhabu kubwa.

لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بِأَنفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ لَوْلَا جَاؤُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاء فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشُّهَدَاء فَأُوْلَئِكَ عِندَ اللَّهِ هُمُ الْكَاذِبُونَ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِي مَا أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِأَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُولُونَ بِأَفْوَاهِكُم مَّا لَيْسَ لَكُم بِهِ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّنًا وَهُوَ عِندَ اللَّهِ عَظِيمٌ

Kwa nini mliposikia khabari hii, wanaume Waumini na wanawake Waumini hawakuwadhania wenzao mema, na kusema: Huu ni uzushi dhaahiri? Kwa nini hawakuleta mashahidi wane? Na ilivyo kuwa hawakuleta mashahidi wane basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake katika dunia na Akhera, bila ya shaka ingeli kupateni adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyo jiingiza. Mlipoyapokea kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyo yajua, na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa.

وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُم مَّا يَكُونُ لَنَا أَن نَّتَكَلَّمَ بِهَذَا سُبْحَانَكَ هَذَا بُهْتَانٌ عَظِيمٌ

Na kwa nini mlipo yasikia msiseme: Haitufalii kuzungumza haya. Subhanak Umetakasika! Huu ni uzushi mkubwa!

يَعِظُكُمُ اللَّهُ أَن تَعُودُوا لِمِثْلِهِ أَبَدًا إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ وَيُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

Mwenyezi Mungu anakuonyeni msirejee tena kufanya kama haya kabisa, ikiwa nyinyi ni Waumini! Na Mwenyezi Mungu anakubainisheni Aya. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَن تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ آمَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّه رَؤُوفٌ رَحِيمٌ

Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake, na kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye kurehemu....

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ وَمَن يَتَّبِعْ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنكُم مِّنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

Enyi mlio amini! Msizifuate nyayo za Shet›ani. Na atakaye fuata nyayo za Shet›ani basi yeye huamrisha machafu na maovu. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu, asingeli takasika miongoni mwenu kabisa hata mmoja. Lakini Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." (an-Nur: 11-21)

Aisha ﵂ alikuwa mtu wa kwanza kuambiwa na Mtukufu Mtume ﷺ juu ya habari hizi njema za Wahyi:

"Habari njema ewe Aisha", alisema kwa furaha, "Mwenyezi Mungu amekuondolea hatia!"

Baada ya kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, bibi Aisha ﵂ alijibu akisema: "Sikuwa nikifikiria kuwa Wahyi ungeshuka kuhusu mja dhaifu kama mimi. Nilitarajia tu kwamba Mtume angepewa ilhamu tu ndani ya moyo wake ambayo ingethibitisha kuwa sina hatia!"

Akimwambia baba yake, Abu Bakr ﵁, ambaye alimbusu kwenye paji lake la uso na kumshauri kurejea kwa mumuwe, alisema:

"Shukrani zinamsathiki Mwenyezi Mungu pekee; kwa maana amethibitisha kuwa sina hatia!"

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ alitabasamu. Dhiki na wasiwasi ambao ulidumu kwa muda wa mwezi mmoja sasa ulifikia kikomo kwa fadhila na rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu. (Bukhari, Shahadat, 15, 30; Jihad, 64; Maghazi, 11, 34; Muslim, Tawba, 56; Ahmad, VI, 60, 195)

Mwanamke ambaye alikuwa mhanga wa kashfa mbaya mno ni mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, mama wa Waumini, binti wa rafiki mkubwa wa Mtume ﷺ, ambaye ni miongoni mwa wanawake wasafi kabisa wa *ummah* huu. Majaribu haya yanatosha kuonesha uwezo wa subira na stahmala waliyonayo Mitume katika kukabiliana na misukosuko. Wakati huo huo, yanatoa liwazo kwa wahanga wote wa kashfa watakaoendelea kutokea mpaka Siku ya Mwisho.

Sasa, licha ya ukweli usiokanushika kuwa Qur'an Tukufu inamsafisha bibi Aisha رضي الله عنها dhidi ya tuhuma zote, kwa kulielezea tukio hilo kuwa ni 'uzushi wa dhahiri' na 'uzushi mkubwa', tuwaambie nini wajinga wanaoendelea kutoa tuhuma kuwa alishiriki katika Tukio la Jamal?

Wale waliokutwa na hatia ya kuzusha kashfa hiyo waliadhibiwa kwa kumsingizia mwanamke msafi kuwa alifanya uasherati. Wazushi hao walichapwa bakora themani kila mmoja.[176]

Kwa mujibu wa maelezo ya Ibn Abbas رضي الله عنه, katika historia kuna watu wanne tu ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaondoa katika hatia baada ya kutuhumiwa: Nabii Yusufu عليه السلام aliondolewa hatiani kupitia maneno ya shahidi kutoka miongoni mwa marafiki wa mwanamke aliyekuwa amemtuhumu.[177] Musa عليه السلام alitakaswa

176. Ahmad, VI, 35.

177. Tazama Surat Yusuf, 26-29.

dhidi ya uvumi uliozushwa na Mayahudi dhidi yake.[178] Mwenyezi Mungu alimuondoa Bibi Maryam tuhumani kwa kumfanya mwanaye mchanga azungumze.[179] Na Bibi Aisha ﵂ aliondolewa lawamani kupitia aya hizo tukufu za Qur'an Takatifu ambazo zitaendelea kusomwa mpaka Siku ya Mwisho. Kamwe hakuna ufasaha uliowahi kuonekana ambao unalingana na ufasaha unaopatikana katika ufunuo huo wa Mwenyezi Mungu kuhusu kumuondolea lawaama mke wa Mtume ﷺ na ambao unaonesha daraja kuu kabisa ya Mtume wake. (Zamakhshari, IV, 121)

Kuchelewa kuteremka kwa ufunuo katika kipindi kigumu kama hicho inatilia mkazo juu ya ukweli kwamba Mtume ﷺ, licha ya kuwa ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alikuwa mwanadamu ambaye hakuwa na mamlaka yoyote juu ya kuteremka kwa Ufunuo. Hilo lilitumika kama mtihani wa kupima ikhlasi na usafi wa moyo wa Waumini.

Kabla ya tukio hilo. Abu Bakr ﵁ mara kwa mara alikuwa akitoa msaada kwa maskini mmoja aitwaye Mistah. Baada ya kuona kuwa Mistah ni miongoni mwa waliotoa kashfa na uzushi wakati wa tukio hilo, aliapa kutomsaidia yeye au familia yake. Alipoacha kuwasaidia, Mistah na familia yake wakawa katika hali ngumu ya uhitaji, na hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha ufunuo akisema:

وَلَا يَأْتَلِ أُوْلُوا الْفَضْلِ مِنكُمْ وَالسَّعَةِ أَن يُؤْتُوا أُوْلِي الْقُرْبَى وَالْمَسَاكِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَن يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

178. Tazama Surat al-Ahzab, 69.

179. Tazama Surat Maryam, 29-33.

"Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na walio hama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." (an-Nur: 22)

"Wala msifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kuacha kufanya wema na kuchamngu na kupatanisha baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua." (al-Baqara: 224)

Aya hizo ni uthibitisho thabiti unaotoa ushahidi juu ya huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja Wake. Pia, zinaelezelea lengo la kuhamasisha kujipamba na mambo mema.

Abu Bakr رضي الله عنه aliposikia Ufunuo huo, hapohapo akasema: "Naam, ninapenda Mwenyezi Mungu anisamehe." Kisha alitoa fidia (*kaffarah*) ya kiapo chake, akaendelea kutoa sadaka na msaada wake kwa familia hiyo kama awali. (Bukhari, Maghazi, 34; Muslim, Tawba, 56; Tabari, Tafsir, II, 546)

Hivyo, Abu Bakr رضي الله عنه hakuacha kutoa sadaka hata kwa mtu ambaye alimsingizia binti yake, jambo linaloonesha jinsi alivyokuwa mtu mwema wa mfano kwa Maswahaba.

Hao ni maadui...Tahadhari nao!

Huo haukuwa mwisho wa msukosuko uliosababishwa na wanafiki wakati wa safari ya kurudi kutoka katika Vita vya Muraythi. Mabishano yaliibuka baina ya watu wawili, mmoja kutoka katika *Ansar* na mwingine kutoka katika *Muhajirun*, ambapo Abdullah ibn Ubayy, kiongozi wa wanafiki, alipata nafasi ya kuchomeka fitna zake. Aliwazungumza *Muhajirun*, alitoa maneno machafu akisema: "Tazama wanavyofanya sasa? Walianza kututawala katika mji wetu

wenyewe na sasa hawatutambui hata kidogo! Lakini wataona tutakaporudi Madina...watu watukufu watawafukuza watu dhalili!"

Zayd ibn Arqam ﷺ, Muumini mwema na mnyoofu, ambaye aliyasikia maneno haya ya ibn Ubayy, alijibu: "Wewe ndio mtu dhalili katika kabila lako! Mwenyezi Mungu Mtukufu amemfanya Muhammad ﷺ kuwa mtukufu!"

Baada ya wanafiki kugundua kuwa maneno yao ya majigambo yamemfikia Mtume ﷺ, haraka walibadilisha ukweli, wakaapa kuwa hawakusema kitu kama hicho; hivyo Zayd ibn Arqam ﷺ akaonekana kama mtu muongo, na kusababisha Swahaba huyo shupavu awe katika dhiki kubwa sana. Lakini, Omar ﷺ, alikuwa na jambo lingine akilini mwake: alimuomba ruhusa Mtukufu Mtume ﷺ awaue wanafiki, kwa kuanza na Abdullah ibn Ubayy. Lakini, akionesha uelewa mkubwa na mtazamo wa mbali kabisa, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: "Ewe Omar! Watu wasioelewa kile kinachoendelea watasema: 'Muhammad anaua watu wake!' Hapana, sitafanya kitu kama hicho! Waambie Waumini wajiandae kuendelea na safari!"

Waislamu waliendelea na safari yao kuelekea Madina. Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea na safari mpaka jioni, na kisha bila kupumzika, akaendelea mpaka asubuhi. Pindi jua lilipoanza kuonesha ukali wake wakati wa asubuhi, alitoa amri ya kupumzika. Waislamu wakiwa wamechoka kutokana na safari ndefu, hawakuchukua muda mrefu kuzama katika lindi la usingizi. Uamuzi huu wa Mtume ﷺ wa kufanya hivi ilikuwa tu kwa ajili ya kuzuia Waislamu wasishughulishwe na maneno ya Abdullah ibn Ubayy.[180] Mkakati huu mzuri uliotumiwa na Mtukufu Mtume ﷺ katika jambo hili

180. Tazama: Ibn Hisham, III, 335-336.

unaonisha uelewa wake mkubwa sana wa maumbile na silika ya mwanadamu.

Muda mfupi zikaja aya mfululizo zikionesha shari za wanafiki na sifa zao mbaya:

إِذَا جَاءكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ اتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّهُمْ سَاء مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ

"Wanapo kujia wanaafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanaafiki ni waongo. Wamevifanya viapo vyao ni kinga, na wao wakajizuia kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakiyafanya. Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote.

وَإِذَا رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ وَإِن يَقُولُوا تَسْمَعْ لِقَوْلِهِمْ كَأَنَّهُمْ خُشُبٌ مُّسَنَّدَةٌ يَحْسَبُونَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ قَاتَلَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْفَكُونَ

Na unapo waona, miili yao inakupendeza, na wakisema, unasikiliza usemi wao. Lakini wao ni kama magogo yaliyo ege-

mezwa. Wao hudhania kila ukelele unao pigwa ni kwa ajili yao. Hao ni maadui; tahadhari nao. Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوَّوْا رُؤُوسَهُمْ وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُم مُّسْتَكْبِرُونَ سَوَاء عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَن يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

Na wanapoambiwa: Njooni ili Mtume wa Mwenyezi Mungu akuombeeni maghfira, huvigeuza vichwa vyao, na unawaona wanageuka nao wamejaa kiburi. Sawa sawa kwao, ukiwatakia maghfira au hukuwatakia maghfira, Mwenyezi Mungu hatawaghufiria. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.

هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنفِقُوا عَلَى مَنْ عِندَ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّى يَنفَضُّوا وَلِلَّهِ خَزَائِنُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ يَقُولُونَ لَئِن رَّجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لَيُخْرِجَنَّ الْأَعَزُّ مِنْهَا الْأَذَلَّ وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ

Hao ndio wanaosema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanaafiki hawafahamu. Wanasema: Tukirejea Madina mwenye utukufu zaidi bila ya shaka atamfukuza aliye mnyonge. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye utukufu - Yeye, na Mtume wake, na Waumini. Lakini wanaafiki hawajui." (al-Munafiquun: 1-8)

Baada ya kuteremka kwa ufunuo huu, Mtukufu Mtume ﷺ alimuita Zayd ibn Arqam, na baada ya kumsomea aya hizo, akamwambia: "Ewe Zayd, Mwenyezi Mungu ameshuhdia ukweli wako!" (Bukhari, Tafsir, 63/1-2; Muslim, Sifat'ul-Munafiqin, 1)

Kisha alilishika taratibu sikio la Zayd na kusema: "Huyu ni kjana ambaye, kwa sikio lake, ametekeleza wajibu wake katika njia ya Mwenyezi Mungu." (Ibn Hisham, III, 336)

Ajabu ni kuwa, Abdullah ibn Ubayy, kiongozi wa gurudumu la wanafiki, alikuwa na mtoto wa kiume aitwaye Abudllah. Mtoto huyu alikuwa Muislamu wa kweli ambaye muda wote alikuwa akiambatana na Mtukufu Mtume ﷺ. Akiwa ni mwenye kusikitishwa sana na maovu ya baba yake kwa muda mrefu, matukio hayo mapya yaliifanya damu yake ichemke. Alihisi kuwa kuna haja ya kumuona Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ukitaka nitamuua baba yangu!" alisema. Kama ilivyotarajiwa, Mtukufu Mtume ﷺ hakumruhusu kutekeleza kile kilichokuwa akilini mwake, badala yake akamshauri kuwa: "Ishi naye kwa ulaini na uamiliane naye vizuri madamu bado yu miongoni mwetu."

Hata hivyo, Abdullah alimkimbilia baba yake, akapenya katika safu za Waislamu, na akıwa ameshikilia hatamu ya ngamia wa baba yake alisema kwa sauti: "Sitakuruhusu utikisike hata inchi moja mpaka useme 'heshima na utukufu ni vya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!"

Kiongozi wa wanafiki alibaki na mshangao mkubwa. Hakuyastahmilia yale aliyokuwa akitendewa na mwanaye mbele ya kundi la watazamaji.

"Kwa nini waniadhiri mbele ya watu hawa badala ya kuniacha niende Madina?"

"Leo sitakuacha mpaka nikufundishe mara moja na mara ya mwisho kuwa ni nani mtukufu na ni nani dhalili kabisa mbele ya watu hawa wote!" alijibu Abdullah kwa sauti ya ushupavu na ukakamavu. "Na kama hutakiri hapa", aliongeza, "Nitakikata kichwa chako!"

Mnafiki huyo hakuwa na pa kukimbilia; alihofu kuwa mwanaye alikuwa hafanyi maskhara na angefanya kile alichokisema. Hakuwa na chaguo linguine zaidi ya kuyafuta maneno yake ya mwanzo, japokuwa kwa lazima.

"Ninakubali", alisema kwa kigugumizi na kwa kusitasita, "kwamba heshima na utukufu ni vya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!"

Baada ya ibn Ubayy kusema hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ akamuombea dua mtoto wa ibn Ubayy: "Mwenyezi Mungu akulipe kheri kwa niaba ya Mtume Wake na Waumini", kisha akamwambia amruhusu baba yake aendelee na safari. (Ibn Hisham, III, 334-337; Ibn Sad, II, 65; Haythami, IX, 317-318; Zamakhshari, VI, 117)

Maswahaba walikuwa wakimpenda sana Mtukufu Mtume ﷺ kiasi kwamba wasingevumilia kuona akiumizwa hata kidogo. Kumvunjia heshima Mtukufu Mtume ﷺ kungewachukiza kiasi ambacho wangehisi kuwa mtu husika anatakiwa kuuawa mara moja, hata kama mtu huyo ni baba yao.

Majaribu Thakili na Mtihani Mzito:
Vita vya Khandaq (Shawwal-Dhilqadah, 5/ Machi, 627)

Yumkini Vita vya Khandaq ndiyo vita vikubwa na vya kutisha kabisa ambavyo Washirikina walivianzisha dhidi ya Waislamu

wakisukumwa na lengo moja tu, kuifuta dola ya Kiislamu ya Madina katika uso wa Historia.

Baadhi ya Mayahudi mashuhuri wa Banu Nadhir waliokuwa wamefukuzwa Madina na kukimbilia katika ngome za Khaybar, moto wa hisia za kisasi ulikuwa ukifukuta ndani ya nyoyo zao. Walitoa pendekezo la kuungana na Maqurayshi. Sio hivyo tu, bali pia waliwahakikishia Washirikina hao kuwa ibada yao ya masanamu ilikuwa bora kuliko Uislamu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alitangaza akisema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُواْ نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ كَفَرُواْ هَؤُلاء أَهْدَى مِنَ الَّذِينَ آمَنُواْ سَبِيلاً أُوْلَئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ وَمَن يَلْعَنِ اللَّهُ فَلَن تَجِدَ لَهُ نَصِيرًا

"Huwaoni wale walio pewa sehemu ya Kitabu? Wanaamini masanamu na Shet›ani! Na wanawasema walio kufuru, kuwa hao wameongoka zaidi katika njia kuliko Walio amini. Hao ndio Mwenyezi Mungu amewalaani. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani basi hutamwona kuwa na mwenye kumnusuru." (an-Nisa: 51-52)[181]

Wakisubiri muda mfupi upite, washirikina walikuwa wepesi kulifanyia kazi wazo lililotolewa na Mayahudi. Makabila mengi ya washirikina wa Kiarabu walikuwa wameshahamasika kutokana na kushindwa kwa Waislamu katika Vita vya Uhud, jambo lililowafurahisha sana Maqurayshi, ambao waliitumia hamasa hii kukusanya jeshi la watu elfu kumi.[182]

181. Tazama: Wahidi, p. 160.

182. Tazama: Waqidi, II, 444; Ibn Saad, II, 66.

Baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kutambua kuwa jeshi la washirika lilikuwa likijiandaa kuivamia Madina, alijadiliana na Maswahaba kuhusu suala hilo la dharura, akawahakikishia ushindi iwapo wataacha kwenda kinyume na amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na iwapo watajiandaa kustahmili matatizo na shida zitakazotokana na Vita hivyo. Aidha, Mtume ﷺ aliwaamuru kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake katika hali yoyote ile itakavyokuwa na katika mazingira ya aina yoyote.

Mtukufu Mtume ﷺ alipewa ilhamu na Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kuchimba mahandaki kuuzunguka mji wa Madina. Hivyo akawauliza Maswahaba iwapo itakuwa bora kumkabili adui nje ya mji wa Madina au wachimbe mahandaki kuuzunguka mji na kuulinda wakitokea ndani.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Katika ardhi ya Fursi tulikuwa tukichimba mahandaki kuuzunguka mji pindi tunapoteghemea kushambuliwa na adui!" alisema Salman رضي الله عنه.

Maneno ya Salman رضي الله عنه, yakithibitisha ushauri wa Mtukufu Mtume ﷺ, yalikubaliwa na Waislamu wote.[183] Aidha, walikumbuka kuwa wakati wa Vita vya Uhud Mtume ﷺ alitaka wabaki mjini na wapigane vita ya kujilinda. Hivyo, kwa moyo wote walikubali kuchimba mahandaki kuuzunguka mji wa Madina.

Upande mmoja wa mji ndio uliokuwa wazi na ambao ulitarajiwa kushambuliwa. Sehemu zilizobaki zilikuwa zimezungukwa na nyumba zilizokamatana kama Kasri.Sehemu za wazi zilikuwa chache, zilikuwa mbali na kwa kiasi kikubwa zilikuwa zimefunikwa na mitende na hivyo kufanya zoezi la kujaribu kupenya kuwa gumu sana. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliamua kwamba mahandaki yachimbwe sehemu iliyo wazi tu. Kwa kila eneo aliteua kundi

183. Ibn Hisham, III, 231; Waqidi, II, 445.

la Maswahaba kumi na kila kundi akalipangia sehemu maalumu katika eneo lililo baina ya majengo ya Shaykhayn mpaka Mazad, akawaambia kiwango hasa ambacho mahandaki hayo yanatakiwa kuchimbwa.[184]

Mtukufu Mtume ﷺ alishiriki moja kwa moja katika kufanya kazi ya uchimbaji wa handaki, huku akiwa amefunga jiwe tumboni mwake kwa ajili ya kuzuia ukali wa njaa iliyotokana na upungu wa chakula uliojitokeza katika kipindi hicho.[185] Licha ya hali hiyo, Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ aliendelea kumshukuru Mola wake kwa kila hali.

Baraa ibn Azib ؓ anasimulia:

"Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akibeba udongo pamoja nasi siku ya *Ahzab*,[186] huku akisoma shairi la Abdullah ibn Rawaha:

'Ewe Allah, kama isingekuwa kwa sababu ya uongofu Wako tusingeweza kutoa Zaka wala kuswali. Ewe Allah, tupe utulivu wakati wa kukabiliana adui; nyazo zetu zisiteleze. Wao ndio wametushambulia...wakitaka kutusukuma katika taabu tutasimama imara na hatutakimbia!'

Alipokuwa akifika kwenye neno *abayna* (tutasimama imara na hatutakimbia), alikuwa akinyanyua sauti yake." (Bukhari, Maghazi, 29)

Maswahaba walikuwa katika shida kubwa mno kiasi kwamba hawakuweza hata kujipatia chakula. Anas ؓ anatoa maelezo ya wazi kuhusu taabu na shida waliyokuwemo:

184. Tabari, *Târîkh*, II, 568; Diyarbakri, I, 482.

185. Bukhari, Maghazi, 29.

186. Vita vya Khandak vilijulikana pia kama vita vya *Ahzab*, yaani makundi au washirika, kwa sababu makabila mbalimbali yaliunganisha nguvu kwa ajili ya kuwashambulia Waislamu.

"Kibaba cha shayiri, baada ya kukandwa na siagi iliyopitwa na wakati, ilikuwa ikiwekwa mbele ya maswahaba ili waweze kula. Licha ya kuwa na njaa kali, ilikuwa haiwezekani kwa kila mtu kutokuonja ukali na ladha mbaya ya siagi hiyo. Chakula hicho kilikuwa kikibeba harufu nzito na isiyopendeza." (Bukhari, Maghazi, 29)

Waislamu wote, vijana na wazee, walikuwa wakishiriki katika uchimbaji wa handaki. Zayd ibn Thabit ﷺ, ambaye wakati huo alikuwa kijana mdogo mwenye umri wa miaka kumi na tano, wakati fulani alizidiwa na usingizi akiwa kazini. Maswahaba waliokuwa karibu naye walimuacha akiwa amelala kwenye ukingo wa handaki. Umarah ibn Hazm ﷺ alimfanyia istihzai kwa kuchukua silaha zake na kuzificha. Alipoamka na kuona kuwa silaha zake zimetoweka, Zayd alighadhibika. Mtukufu Mtume ﷺ alipopata taarifa alimuita Zayd mbele yake na kumwambia:

"Ulilala na silaha zako zikatoweka!" Baada ya kusema hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ akauliza: "Je kuna yeyote ajuaye mahali zilipo silaha za mtoto huyu?"

"Ninajua mahali zilipo Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ninazo mimi!" alisema Umarah ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ alimtaka Umarah amrudishie Zayd silaha zake na kisha akapiga marufuku kuwatisha Waislamu, hata kwa kuwatania, na kuficha mali zao zozote. (Waqidi, II, 448)

Habari Njema Wakati wa Kuchimba Khandaq

Maswahaba walimlalamikia Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu mwamba mkubwa waliokutana nao wakati wakichimba, ambao walishindwa kuuvunja. Hivyo Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua nyundo kubwa, akatamka jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu, kisha akaupiga mwamba huo mara tatu, akaupa-

sua kama kokoto dhaifu.[187] Kila pigo moja, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiwapa faraja Waislamu kwa habari njema. Alisema kuwa kwa pigo la kwanza alikuwa amepewa funguo za Damascus (Rumi), pigo la pili akapewa funguo za Uajemi (Fursi), na pigo la tatu alipewa funguo za Yemen. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba alikuwa akiyaona makasri ya sehemu hizo kutokea hapo alipokuwa. Aliwaeleza Waislamu kuwa maeneo yote hayo yatapata heshima ya kupata uongofu wa Uislamu na neno la Mwenyezi Mungu katika kipindi kifupi kijacho. Kwa kuwapa habari hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliingiza ndani ya nyoyo zao matumaini na matarajio ya ushindi mbalimbali utakaotokea.[188] Aliwahakikishia kuwa muda mfupi sana ujao Haki itaishinda batili, na sasa ushindi mbalimbali uliokuwa haujatokea ukaanza kutokea na kuonekana.

Mtukufu Mtume ﷺ alipoanza kulielezea kasri jeupe la Khosro lililokuwa katika ngome ya Wasasani ya Madain, Salman ؓ ambaye alikuwa akilijua vyema, alistaajabu sana na kusema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu aliyekutuma na dini na kitabu cha kweli, ulivyoelezea kasri hilo ndivyo lilivyo hasa! Ninashuhudia kwa mara nyingine kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu!"

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Ewe Salman, Mwenyezi Mungu atakupatieni ushindi huo baada yangu. Hakika Dameski itaanguka! Heraclius atakimbilia kwenye pembe ya mbali kabisa ya himaya yake! Mtalitawala eneo lote la Dameski! Hakuna atakayeweza kuwazuia! Hakika Yemen itaanguka! Baada ya hapo Khosro atauawa!"

Baada ya Mtume ﷺ kuondoka duniani, Salman ؓ alithibitisha kuona "...matukio yote hayo yakitokea na kuthibitika." (Waqidi, II, 450)

187. Bukhari, Maghazi, 29.

188. Tazama: Ahmad, IV, 303; Ibn Saad, IV, 83, 84.

Wakati maeneo yote haya yakianguka moja baada ya lingine, Abu Hurayra ﷺ alikuwa akisema: "Huu ni mwanzo tu! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi ya Abu Hurayra ipo Mikononi Mwake, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Muhammad ﷺ funguo za maeneo yote mliyoyachukua na mtayachukua mpaka Saa ya Mwisho!" (Ibn Hisham, III, 235)

Habari njema ambayo Mtukufu Mtume ﷺ aliwapa Waislamu iliwapatia faraja kubwa sana ya kuvumilia shida zitakazowakabili. Ukweli kwamba ushindi ungekwenda kwa Waislamu na fazaa ingekwenda kwa maadui zao iliwaimarisha zaidi katika subira na stahmala ya imani iliyojaa ndani ya nyoyo za Waislamu.

Kwa hakika, kiwango kikubwa sana cha subira na stahmala kilikuwa kikihitajika. Vita kali dhidi ya uchovu na njaa kwa upande mmoja, na baridi kali kwa upande mwingine. Yote hayo yalionesha kuwa Vita vha Khandak ni mtihani mzito sana.Lakini, dua iliyoombwa na Mtukufu Mtume ﷺ wakati wa kuchimba handaki uliwapa hisia na hamasa ya kwamba machungu na maumivu yote ambayo mwanadamu huyapitia katika ulimwengu huu si chochote mbele ya neema za milele zinazomsubiri, hata kama maumivu hayo yatakuwa makubwa kiasi gani. Mtukufu Mtume ﷺ aliomba dua ifuatayo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hakuna maisha isipokuwa maisha ya Akhera! Wanusuru *Ansar* na *Muhajirun*!" (Bukhari, Maghazi, 29)

Baraka Tele katika Chakula cha Jabir

Jabir ﷺ anasimulia tukio lifuatalo:

"Wakati tukiendelea kuchimba handaki kabla ya Vita vya Khandaq, tulikutana na jiwe kubwa lililotuzuia kuendelea. Baadhi ya Maswahaba wakaenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumwabia kuwa wamekutana na jiwe ambalo hawawezi kulivunja.

Mtume wa Mwenyezi Mungu akawaambia kuwa: 'Nitaterемka ndani ya handaki mimi mwenyewe'. Akanyanyuka mahali alipokuwa amekaa. Alikuwa amefunga jiwe tumboni mwake ili kujizuia ktokana na njaa. Siku tatu zilikuwa zimepita tangu tulipoonja chakula. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akachukua mpini wa nyundo na kupiga juu ya mwamba, ambao ulipasuka na kugeuka kuwa kama chungu ya mchanga.

Baadaye nilimuomba Mtume wa Mwenyezi Mungu nikisema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, niruhusu nifike nyumbani'. Aliniruhusu, nami nikaelekea moja kwa moja mpaka nyumbani na kumwambia mke wangu: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko katika hali ya mchoko na kulegea sana. Je tuna chakula chochote?'

'Tuna shayiri na kondoo mdogo', alijibu.

Nilimchinja kondoo na kuikanda shayiri. Tuliweka nyama katika chungu. Pindi mkate ulipokuwa tayari na chungu kikiwa kimeanza kuchemka, nilikimbia kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nina chakula kidogo. Tafadhali njoo na watu wawili ili tupate heshima ya kula pamoja nawe...'

'Kuna chakula kiasi gani?' aliuliza. Mikamwambia kiasi tulichokuwa nacho. Akasema: 'ni kizuri na ni kingi...mwambie mkeo asitoe chungu jikoni na auache mkate kwenye tanuu mpaka nitakapofika!'

Kisha aliwageukia Maswahaba na kuita kwa sauti: 'Enyi watu wa handaki; njooni ... Jabir ametuandalia karamu ya chakula!' Kila aliyekuwepo akaanza kusogea.

Nikiwa mwenye wasiwasi, nilikimbia nyumbani kwa mke wangu na kumwambia: 'angalia kilichotokea sasa...Mtume wa Mwenyezi Mungu anakuja na *Ansar*, *Muhajirun* na wengine wote!'

'Je, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuuliza kuna chakula kiasi gani?' mke wangu aliniuliza.

'Ndiyo', nilimjibu.

'Basi usiwe na wasiwasi', alijibu kwa utulivu, 'kwa maana anajua zaidi kuliko wewe!'

Baada ya muda mfupi waliwasili. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaambia waingie bila kusongamana. Maswahaba wakaingia katika makundi ya watu kumi kumi. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.aw) akaanza kuukata mkate, baadhi akauwekea nyama juu yake na kuwapa kila maswahaba waliokuwa wakisubiri; na kila anapomaliza kuwapa alikuwa akifunika kifuniko cha chungu na tanuu. Maswahaba wote wapatao elfu moja walipokula mpaka wakaridhika na kushiba, Mtume ﷺ alikuwa akirejea kufanya hivyo. Mpaka wanamaliza kula, chakua kilibaki. Kisha alimgeukia mke wangu na kusema: 'Chukua chakula hiki ule na jirani zako; kwani hakika njaa ilimkumba kila mmoja wetu!' (Bukhari, Maghazi, 29; Muslim, Ashribah, 141; Waqidi, II, 452)

Tukio hilo la muujiza wa Mtukufu Mtume ﷺ liliwafaidisha watu elfu moja, ikiwa ni pamoja na majirani wa eneo hilo, ambao walikula chakula kilichoonekana mwanzo kuwa kingewatosha watu wachache tu.

Kwa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akitumia vyote alivyonavyo katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakuwa akibaki na kingi mkononi. Anapohisi kuwa na haja kubwa ya kitu fulani, alikuwa akifanya siri na kutowaambia Maswahaba, kwa kuwa hakutaka kuwa mzigo kwa yeyote. Lakini Maswahaba walipogundua hali hiyo ya Mtukufu Mtume ﷺ walikuwa wakifanya kila liwezekanalo

kumsaidia pindi wanapohisi kuwa anahitaji jambo fulani. Wakati mwingine, sauti ya Mtume ﷺ ingeonesha kiwango fulani kutokana na njaa, ambapo Maswahaba wanapoona hivyo walikuwa wakifanya haraka kumpeleka majumbani mwao na kumpa chakula walicho nacho.[189] Kama wakimuona Mtukufu Mtume ﷺ akiwa mwenye uso uliosawajika, walikuwa wakifanya kila juhudi kumpatia kitu chochote cha kula, hata ikibidi kufanya kazi ndogondogo, kama vile kunywesha ngamia, ili tu wapate tende chache za kumpelekea.

Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikutana na swahaba mmoja wa Kiansari, ambaye alimuuliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wazazi wangu wawe fidia kwako, tafadhali niambie sababu ya uso wako kuwa wenye kusawajika sana, kwani hali hiyo yanitia wasiwasi!'

Baada ya kumtazama Swahaba huyo kwa sekunde kadhaa, Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia: "Njaa!"

Swahaba huyo hakupoteza muda akakimbilia nyumbani kwa ajili ya kuangalia chochote, lakini hakupata. Hima akaelekea kwenye makao ya Banu Quraydha na kufanya makaubaliano na mtu mmoja, ambapo kwa mujibu wa makubaliano hayo, angelipwa tende moja kwa kila kiriba cha maji ambacho angechota kutoka kisimani. Baada ya kupata kiasi kidogo cha tende, alizipeleka kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tafadhali chukua tende hizi", alisema.

Mtume wa Rehma ﷺ alimuuliza wapi alipozipata tende hizo. Akamuelezea kisa kamili. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Ninaamini unampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!"

189. Tazama: Bukhari, Atimah, 6; Muslim, Ashribah, 142.

"Ndiyo", alijibu swahaba huyo na kuongezea: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye alikutuma kwa Haki, hakika ninakupenda sana kuliko ninavyoipenda nafsi yangu, watoto wangu, mke wangu na mali zangu!"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Kama ni hivyo, basi dumisha subira dhidi ya ufakiri, jiandalie kinga dhidi ya matatizo na shida! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu aliyenituma kwa Haki, vitu hivi viwili (umasikini na shida) humfika kwa haraka yule anayenipenda mimi kuliko hata maji yanayotiririka kutoka mlimani!" (Haythami, X, 313; Dhahabi, Siyar, III, 54; Ibn Hajar, al-Isabah, III, 298)

Shida na tabu zilizowafika wakati wa Khandaq

Yalikuwa majira ya baridi. Sasa washirikina walikuwa wameizingira Madina kutoka kila upande. Lakini walikwamishwa na kushtushwa kutokana na handaki ambalo hawakuwa wakitarajia kukumbana nalo. Hawakuweza kuvuka.

Baada ya washirikina kuweka kambi pembezoni mwa mji, Mtukufu Mtume ﷺ alienda haraka kwenye handaki akiwa amesuhubiana na Maswahaba elfu tatu. Abdullah ibn Umm Maqtum ﷺ aliachwa Madina kama kaimu na naibu wake. Mtukufu Mtume ﷺ alisonga mbele na kuuacha mlima wa Sal nyuma yake, akaweka kambi kwenye viunga vya mlima huo, akawaamuru wanawake na watoto wabaki nyuma kwenye sehemu ya katikati ya mji wa Madina ambao ungelindwa na kuwekewa ngome.[190] Watoto ambao walikuwa hawajafikisha umri wa miaka kumi na tano walireje nyumbani kwenye familia zao ambapo watawekewa ulinzi, huku watu kama Ibn Omar, Zayd ibn Thabit na Baraa ibn Azib, ambao walikuwa na

190. Ibn Hisham, III, 235.

umri wa miaka kumi na tano wakati huo, waliruhusiwa kubaki na jeshi.[191]

Wakati huohuo, Mayahudi wa Banu Quraydha walitangaza rasmi kufanya uasi mjini, wakienda kinyume, kwa mara ya pili, dhidi mkataba wa makubaliano waliowekeana na Mtukufu Mtume ﷺ. Huu ulikuwa uhaini wa pili, wakiwaacha Waislamu katikati ya mzozo wa kutisha. Mayahudi hao walituma ujumbe kwenda kwa Abu Sufyan, wakimsisitizia kuwa "...subiri, tutawashambulia Waislamu kutokea upande wa nyuma na kuwamaliza!"[192]

Kwa hatua hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ametukanwa sana kwa uhaini huu wa Mayahudi. Hata hivyo, alikuwa na imani isiyotetereka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata kama wakati huo mgumu alisema: *"Hasbunallah wa ni'mal-wakil*: Mwenyezi Mungu anatutosha Naye ndiye Mbora wa kutegemewa!" (Waqidi, II, 457; Ibn Sad, II, 67)

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliomba mtu wa kujitolea kwenda kwa Banu Quraydha na kuona kama kuna ukweli wowote juu ya alichokisikia.

"Nitakwenda", alisema Zubayr ibn Awwam رضي الله عنه na kuanza kuondoka.

Hali ilipokuwa ya mashaka na wasiwasi zaidi, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtuma tena na tena Zubayr ibn Awwam kwenda kuangalia kama walikuwa wamesitisha azma yao au la.Baadaye alielezea kuridhishwa kwake na huduma za awali zenye thamani zilizotolewa na Zubayr رضي الله عنه, akasema: "Kila mtume ana mjumbe...na mjumbe wangu ni Zubayr!" (Ahmad, III, 314)

191. Waqidi, II, 453.
192. Abdurrazzaq, V, 368.

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliwatuma wajumbe kwenda kwa Banu quraydha, akawausia akisema: "Nendeni na muangalie iwapo tuliyoyasikia ni ya kweli. Iwapo ni ya kweli, basi nifahamisheni kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Msiniambie kwa namna ya moja kwa moja mkasababisha hofu ndani ya nyoyo za watu na kuwanya wakate tamaa! Lakini iwapo watakuwa bado wanatekeleza makubaliano yetu mnaweza kusema kwa namna ya wazi!"

Ujumbe huo ulihitimisha kazi yake kwa kugundua kuwa banu Quraydhawakiwa katika hali ya juu sana ya uasi kuliko ilivyosikika. (Ibn Hisham, III, 237)

Mtukufu Mtume ﷺ aliwatuma Maswahaba mia mbili chini ya uongozi wa Salamah ibn Aslam ؓ na wengine mia tatu chini ya uongozi wa Zayd ؓ katika mji wa Madina, kama hatua ya kinga dhidi ya uwezekano wa shambulio lolote linaloweza kufanywa na Mayahudi kwenye mji huo. Waliatakiwa kufanya ulinzi ndani ya mji na kuzunguka katika mitaa wakiita kwa sauti *Allahu Akbar*.[193]

Waislamu walipogundua kusudio la banu Quraydha, walikuwa wakishusha pumzi ya faraja kila asubuhi kwa kuona kuwa hawajashabuliwa na Banu Quraydha.

Abu Bakr ؓ baadaye alikiri akisema: "Hofu yetu kwa ajili ya wanawake na watoto wetu katika mji wa Madina dhidi ya kushambuliwa na Banu Quraydha ilikuwa kubwa sana kuliko hofu yetu kwa Maqurayshi na watu wa Ghatfan. Kila mara nilikuwa nikipanda kwenye kilele cha mlima Sal na kuzitazama nyumba za mji wa Madina; ninapoziona katika hali ya amani na utulivu nilikuwa nikimshukuru Mwenyezi Mungu." (Waqidi, II, 460)

Umm Salamah ؓ anatoa maelezo kama hayo akisema:

"Nilikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vingi vikali na vya kutisha kama Vita vya Muraythi, Khaybar,

193. Ibn saad, II, 67.

Ufunguzi wa Makka na Hunayn. Katika vita vyote hivyo hakuna vita iliyokuwa na tabu na ugumu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama Vita vya Khandaq. Hatukuwa na raha kwa hofu ya Banu Quraydha kuwashambulia wanawake na watoto wetu." (Waqidi, II, 467)

Wakati huo huo, washirikina waliokuwa upande wa pili wa handaki walikuwa wakifanya majaribio ya mara kwa mara ya kuvuka handaki, hali iliyopelekea kutokea kwa mashambulizi yaliyokuwa yakidumu mpaka usiku, huku hema la Mtukufu Mtume ﷺ likilengwa kwa mishale mingi.

Siku moja washirikina walianzisha mashambulizi makubwa kwenye eneo ambalo Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa ameweka kambi; na kwa sababu ya mashambulizi haya yasiyokoma, Mtume ﷺ na Maswahaba hawakupata fursa ya kuswali swala za Adhuhuri na Alasiri. Jua likiwa linakaribia kuzama, ambapo washirikina walirudi nyuma, Mtukufu Mtume ﷺ alimtaka Bilal ؓ atoe adhana. Iqama ilisomwa kwa kila swala na Mtukufu Mtume ﷺ akawaongoza wau-



mini katika swala zote ambazo hawakuziswali kwa wakati wake.[194] Mtukufu Mtume ﷺ, akiwa amehuzunishwa sana na tukio hilo, aliwaombea dua mbaya washirikina ambao hawakumpa hata fursa ya kuswali, amali ambayo aliita kama 'nuru ya macho yangu':

"Kwa kuwa walinishughulisha na kunizuilia kutotekeleza swala mpaka jua likazama, Mwenyezi Mungu azijaze moto nyumba zao, matumbo yao na makaburi yao!" (Bukhari Maghazi, 29; Ibn Sa'd, II, 68-69; Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 112)

Misimamo ya Ujasiri katika Vita vya Khandaq

Waislamu wote waliokuwepo, wadogo kwa wakubwa, walikuwa wakifanya kila wawezalo wakati wa Vita ili kuyalinda maeneo finyu ya handaki yaliyokuwa na upenyo.[195]

Umm Salamah رضي الله عنها anasimulia tukio lifuatalo:

"Nilikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu katika Vita vya Khandaq. Kamwe sikuondoka pembeni mwake au mahali pengine pale alipokuwa. Yeye mwenyewe alikuwa amesimama kwenye ukingo wa handaki. Huko tulikuwa katikati ya baridi kali. Nilikuwa nikimtazama; alikuwa ameanza kuswali. Kisha tuliendelea mbele. Baada ya kutazama upande wa handaki kwa muda, alisema: 'Yaonekana kama kwamba wale ni wapanda farasi wa jeshi la washirikina wanatafuta njia ili kuvuka handaki. Nani atakayewazuia?' Kisha alimuita Abbad ibn Bishr!

'Naam, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu', Abbad رضي الله عنه alijibu.

'Kuna yeyote pamoja nawe?' Mtume wa Mwenyezi Mungu aliuliza.

194. Tukio hili ni ushahidi wa swala ya qadhaa, ambayo ni lipa swala ambazo hukuziswali kwa wakati wake.

195. Waqidi, II, 463-464.

'Ndiyo...kuna baadhi ya maswahaba na muda wote nilikuwa nikisubiri jirani na hema yako.'

'Nenda na wenzako mtembee kwenye eneo lote la handaki! Wapanda farsa wanaoonekana kwa mbali wanaonekana kuwa ni maadui. Wanakuja kwa ajili yenu; wanataka kuwaondoa kwenye lindo, washambulie kwa ghafla na waue wengi uwezavyo!'

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akaomba akisema: "Mola wangu! Tunakuomba utuepushe na shari yao! Tunusuru dhidi yao na utuwezeshe kuwashinda! Hakuna awezaye kutupa ushindi ila Wewe!"

Abbad ibn Bishr ؓ alitoka na wenzake kwenda kufanya utafiti kwenye eneo la handaki, na wakati huo huo Abu Sufyan akiwa na kikosi cha wapanda farasi alikuwa akifanya juhudi hatarishi za kuvuka kupitia kwenye eneo lililokuwa na upenyo na lisilokuwa na upana mkubwa. Kundi hilo dogo la Maswahaba lilifika hapo katika wakati muafaka wakawatupia mishale na mawe ya kutosha ambayo yaliwalazimisha washirikina kurudi nyuma na kukimbia. (Waqidi, II, 464)

Safiyya ؓ, shangazi wa Mtukufu Mtume ﷺ, alikuwa katika nyumba kubwa ya Hassan ibn Thabit, iliyojulikana kama Fari, akiwa na wanawake wengine pamoja na watoto. Wakati mmoja, kundi la Mayahudi kumi lilikuja na kuishambulia nyumba hiyo kwa mishale, wakitaka kuingia kwa nguvu. Mmoja wao alikuwa akizunguka nyumba hiyo kwa siri akitumai kupata njia ya kuingia ndani. Wakati huohuo Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa katika makabiliano makali dhidi ya washirikina kwenye handaki.

Akiwa hana usaidizi na hivyo kutokuwa na njia nyingine zaidi ya kulichukua suala hilo mikononi mwake, Safiyya ؓ alifunga nguo kuzunguka kichwa chake na akiwa na ufito mkononi mwake, alishuka kwenye ngazi za nyumba hiyo kuelekea chini. Alifungua mlango

taratibu, akatembea kwa kunyata nyuma ya Myahudi na kwa haraka sana akampiga kwa ufito huo kichwani, akamuua papo hapo. Mayahudi wengine walipokuja kumkuta mwenzao akiwa amelala ardhini gizani, waliogopa na kushikwa na wasiwasi. "Tuliambiwa kuwa wanawake hapa wanalindwa na walinzi maalumu, je sio sisi?" walisema huku wakiwa na wasiwasi na kukimbia. (Haythami, VI, 133-134; Waqidi, II,462)

Bibi Aisha ﵂ anasimulia hamasa ya jihadi aliyoishuhudia kutoka kwa Maswahaba:

"Nilikuwa nikiwashuhudia wapiganaji wakati wa Vita vya Khandaq. Nilisikia sauti ikitokea upande wa nyuma. Niligeuka na kumuona Saad ibn Muadh na mpwa wake, Harithah ibn Aws. Nilikaa chini hapo hapo. Alikuwa amevaa ngao kuzunguka kifua chake huku mikono yake ikiwa haijawekewa ngao. Alikuwa akisoma shairi linalohamasisha jihad na kuzungumzia jinsi kifo kilivyo kizuri pindi kinapowasili. Mama yake alikuwa akimpigia kelele akisema: 'Kimbia mwanangu...nenda umuwahi Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwani wachelewa!'

'Nilitamani kuona ngao ya Saad ikiwa imeufunika mwili wake wote mpaka kwenye ncha za vidole', nilimwambia mama wa Saad. Nilikuwa na wasiwasi huwenda aKishambuliwa kwa mishale katika mikono yake iliyokuwa wazi.

'Mwenyezi Mungu atafanikisha anayoyataka', hilo ndilo lililokuwa jawabu lake. Siku hiyo Saad alijeruhiwa." (Ahmad, VI, 141; Ibn Hisham, III, 244)

Saad ﵁ alipoona kuwa jeraha lake ni kubwa sana, aliomba dua akisema:

"Mola wangu! Kama umetuandikia kupigana vita vingine na washirikina wa Kiqurayshi basi nipe nafasi ya kuishi mpaka wakati

huo! Kwa maana hakuna kabila lingine ninalotaka kupambana nalo zaidi kama Maqurayshi, ambao walimtesa na wakamtendea ubaya Mtume Wako, wakamkana na kumfukuza kutoka katika mji wake wa nyumbani! Lakini iwapo hii ndio vita yetu ya mwisho dhidi yao basi naomba jeraha langu liwe sababu ya mimi kufa shahidi! Nipokee mbele Zako Ewe Mola wangu! Na usiuchukue uhai wangu mpaka nishuhudie na kufurahia adhabu watakayoipata Banu Quraydha!" (Waqidi, II, 525; Ibn Sad, III, 423)

Mara Saad ؓ alipomaliza kuomba dua yake, damu ikakoma kuvuja.[196]

Mtukufu Mtume ﷺ aliweka hema maalumu kwa ajili ya Saad ؓ ndani ya Msikiti, ili aweze kumzuru mara kwa mara na kumhudumia kwa ukaribu zaidi.[197]

Washirikina wachache tu ndio walioweza kuvuka handaki wakipitia eneo pana. Miongoni mwao ni Amr ibn Abd, mpambanaji aliyekuwa akijulikana mno ndani ya Arabia yote.Changamoto yake yenye kiburi ilikutana na Ali ؓ ambaye alimshughulikia. Wengine waliuawa pia.

Vita ilikuwa ikipamba moto; ilionekana kana kwamba haitafikia kikomo. Waislamu walijikuta katika hali ngumu na tata ambayo sasa walitarajia sana msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hali yao imeelezwa ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

196. Tirmidhi, Siyar, 29/1582; Ahmad, III, 350.
197. Bukhari, Maghazi, 30.

إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُونَ وَزُلْزِلُوا زِلْزَالًا شَدِيدًا

"Walipo kujieni kutoka juu yenu, na kutoka chini yenu; na macho yalipo kodoka, na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali. Hapo ndipo Waumini walipo jaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali."

وَإِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ مَّا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا وَإِذْ قَالَت طَّائِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوا ۚ وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ ۖ إِن يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا وَلَوْ دُخِلَتْ عَلَيْهِم مِّنْ أَقْطَارِهَا ثُمَّ سُئِلُوا الْفِتْنَةَ لَآتَوْهَا وَمَا تَلَبَّثُوا بِهَا إِلَّا يَسِيرًا وَلَقَدْ كَانُوا عَاهَدُوا اللَّهَ مِن قَبْلُ لَا يُوَلُّونَ الْأَدْبَارَ ۚ وَكَانَ عَهْدُ اللَّهِ مَسْئُولًا قُل لَّن يَنفَعَكُمُ الْفِرَارُ إِن فَرَرْتُم مِّنَ الْمَوْتِ أَوِ الْقَتْلِ وَإِذًا لَّا تُمَتَّعُونَ إِلَّا قَلِيلًا

"Na walipo sema wanaafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu. Na kundi moja katika miongoni mwao lilipo sema: Enyi watu wa Yathrib! Hapana kukaa nyinyi! Rudini. Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: Hakika nyumba zetu ni tupu. Wala hazikuwa tupu; hawakutaka ila

kukimbia tu. Na lau kuwa wangeli ingiliwa kwa pande zote, kisha wakatakiwa kufanya khiana, wangeli fanya, na wasingeli sita ila kidogo tu. Na hakika walikwisha muahidi Mwenyezi Mungu kabla yake kwamba hawatageuza migongo yao. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa. Sema: Kukimbia hakukufaeni kitu ikiwa mnakimbia mauti au kuuwawa, na hata hivyo hamtastareheshwa ila kidogo tu." (al-Ahzab, 10-16)

وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَٰذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ ۚ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا

"Na Waumini walipo yaona makundi, walisema: Haya ndiyo aliyo tuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli. Na hayo hayakuwazidisha ila Imani na ut›iifu." (al-Ahzab, 22)

Vita ni Hadaa

Waislamu walikuwa imara na madhubuti sana. Sahaba maarufu kutoka katika kabila la Ghatafan, Nuaym رضي الله عنه, ambaye, akiungwa mkono na wosia wa Mtukufu Mtume ﷺ kuwa 'Vita ni Hadaa' (Bukhari, Jihad, 157; Muslim, Jihad, 17), akaufanya Uislamu wake kuwa siri dhidi ya Washirikina, aliweza kuwaweka washirikina na Banu Quraydha katika hali mbaya ya kutoelewana wao kwa wao. Upepo wa kusitasita uliyazuia majeshi ya washirika kwa kuendelea kuuzingira zaidi mji wa Madina. Ghafla kila kabila likaanza kuwatilia shaka washirika wake. Hatimaye Mayahudi walikubaliana na mbinu za ushawishi za Nuaym wakarudi katika ngome zao. Sasa Washirikina ndio pekee waliokuwa wamebaki kwenye medani, wakisubiri upande wa pili wa handaki. Bado Waislamu walikuwa katika hali

ngumu. Ni katika kipindi hicho ambacho Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba walikuwa wakipitia katika mtihani mzito uliosababishwa na mzingiro wa washirikina, ambapo tunaweza kusema nyoyo zilikuwa zimepanda kooni, ndipo aya ifuatayo ikashuka:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِكُم ۖ مَّسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّىٰ يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ مَتَىٰ نَصْرُ اللَّهِ ۗ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyo wajia wale walio pita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walio amini pamoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu." (al-Baqara, 2: 214)[198]

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ alinyanyua mikoni yake juu na kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu uliyeteremsha Qur'an Tukufu! Ewe Mwenyezi Mungu Mwenye wepesi wa kuwawajibisha maadui! Yatawanye makabila haya ya Waarabu waliokusanyika mbele ya Madina! Mola wangu! Uvunje umoja wao na uutikise uthabiti wao wasipate kustahmili!" (Bukhari, Maghazi, 29)

Punde tu Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amemaliza dua yake pindi msaada ulipowasili kutoka kwa Mwenyezi Mungu na weka tabasamu ka furaha kwenye uso wake mtukufu. Dhoruba kali yenye hasira ilianza kupiga katika safu za maadui; upepo mkali uling'oa kila kitu, ukawafunika washirikina kwa vumbi la jangwa

198. Tazama: Tabari, *Tafsir*, II, 464.

la Madina, ukayavurumisha mahema yao, ukavipindua vyombo vyao vya chakula na kuuzima moto wao. Wakiwa wamezingirwa na kushambuliwa na upepo huo mkali kutoka pande zote, ngamia wao walianza kugongana wao kwa wao.[199]

Washirikina, wakiwa wamezidiwa na nguvu ya dhoruba iliyotumwa na Mwenyezi Mungu, waliachwa wakihangaika katika hali ya kuharibikiwa. Hata Abu Sufyan, ambaye alikuwa mbishi zaidi miongoni mwa washirikina wote, hakuwa na chaguo zaidi ya kuwaambia askari wake:

"Ninarudi nyumbani na kwa hali hiyo nanyi pia yawapasa mrudi!" Akampanda ngamia wake na kuanza kurejea Makka bila hata kuangalia nyuma.[200]

Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa ametuma msaada wake kwa Waislamu. Hivyo, Qur'an Tukufu inasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا

"Enyi mlio amini! Zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilio juu yenu. Pale yalipo kufikilieni majeshi, nasi tukayapelekea upepo, na majeshi msiyo yaona. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda." (al-Ahzab, 33: 9)

وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ وَكَانَ اللَّهُ قَوِيًّا عَزِيزًا

199. Ibn Saad, II, 71.
200. Ibn Hisham, III, 251.

"Na Mwenyezi Mungu aliwarudisha nyuma makafiri juu ya ghadhabu yao; hawakupata kheri yoyote. Na Mwenyezi Mungu amewatosheleza Waumini katika vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na uweza." (al-Ahzab, 33: 25)

Wakiondoka katika hali ya unyonge na madhila, washirikina waliacha nyuma yao farasi wengi, ngamia, vifaa vya kijeshi, chakula na mali kadhaa wa kadhaa, ambavyo viligeuka kuwa neema kwa Waislamu katika kupambana na njaa na ukame mkali uliokuwepo wakati huo katika mji wa Madina. Kufuatia ushindi huu mkubwa, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba:

"Sasa ni zamu yenu! Kuanzi leo na kuandelea, Maqurayshi hawataweza tena kuwashambulia!" (Bukhari, Maghazi, 29)

Kuanzi siku hiyo, Waislamu hawakuwa tena katika nafasi ya kujilinda, kwa maana kiburi na nguvu za washirikina zilikuwa zimepata pigo kubwa lisiloweza kurejea katika hali ya kawaida. Sasa nyoyo za Waislamu zilikuwa zikitoa mwangwi wa ahadi ya Mtukufu Mtume ﷺ aliposema:

"Kuanzia leo, sisi ndio tutakaokuwa tukienda kwao!"

Kuelekea kwa Banu Quraydha
(23 Dhilqadah, 5/ 15 Aprili, 627)

Vita vya Khandaq vilikuwa vimefikia tamati na ushindi kupatikana. Washirikina ambao walilazimishwa kukimeza kiburi chao, walikuwa wamesharudi Makka wakiwa dhalili na wenye kushindwa. Mtukufu Mtume ﷺ, naye alikuwa amesharudi nyumbani, na kama alivyokuwa akifanya baada ya kila vita, alivua ngao yake na kuoga. Ni baada ya hapo ndipo Jibrail عليه السلام alipotokea.

"Mmeshaweka chini silaha zenu?" Jibrili alimuuliza Mtume ﷺ, naye akajibu "Bado!"

"Hiyo ina maana kwamba tuna vita vingine. Wapi?" Mtume ﷺ aliuliza.

Jibril عليه السلام akaonesha upande wa makao ya Banu Quraydha, ambao waliwafanyia khiyana Waislamu katika vita vya Khandaq.

"Sawa!" alijibu. (Bukhari, Maghazi, 30)

Kama ilivyokuwa kwa makabila mengine ya Mayahudi wenzao wa mji wa Madina hapo awali, Banu Quraydha walishindwa kutekeleza kiapo chao wenyewe walichokitoa katika makubaliano na wakawasaliti Waislamu katika kipindi kigumu sana. Kwa kweli, makubaliano ya mkataba yaliwataka kutoa msaada katika kuuhami na kuulinda mji wa Madina dhidi ya hujuma na uvamizi wa washirikina. Sio tu kwamba walijiweka pembeni na kuacha kuwasaidia Waislamu, bali hawakuacha kugeuza jiwe lolote katika kupanga njama za shari dhdid ya Waislamu kila walipopata fursa. Hawakujua kuwa walikuwa wakijiandikia mwisho wao wenyewe.

Baada ya kupokea amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu, haraka sana Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya Waislamu na kuwaashiria juu ya safari ya kuelekea kwa Banu Quraydha.

"Kila mwenye kusikia na kutii aswali alasiri kwenye makao ya Banu Quraydha!" (Bukhari, Maghazi, 30)

Hivyo, Waislamu waliondoka kabla ya kuwaruhusu Mayahudi hao kugundua hali inayowasubiri.

Kwanza, kikosi kidogo chini ya uongozi wa Ali رضي الله عنه, kilichokuwa kimetangulia, kilikutana na Mayahudi, ambao badala ya kujuta walizidi kuchafua hali na kumtukana Mtukufu Mtume ﷺ kwa maneno yenye kuudhi.[201] Lakini walipoona jeshi la Waislamu lenye askari shupavu elfu tatu wakitokea mbele ya ngome za Banu

201. Tazama: Waqidi, II, 499.

Quraydha chini ya uongozi wa Mtukufu Mtume ﷺ, walishtuka na kushdindwa kuongea. Haiba ya muonekano wa Mtukufu Mtume ﷺ iliwalazimisha kuyakana maneno yote waliyokuwa wameyasema hapo awali dhidi yake.

"Enyi maadui wa Mwenyezi Mungu! Hatutaondoa mzingiro kwenye ngome zenu mpaka mfe kwa njaa. Nyinyi ni mbweha walionasa katika matundu yao!" Alisema kwa sauti Usayd ibn Khudayr رضي الله عنه.

Wakiwa wameingiwa na hofu, Mayahudi walipiga kelele wakiomba kutoka kwenye ngome zao: "Ewe Ibn Khudayr, sisi ni washirika wenu...washirika wa Aws, sio Khazraj!"

"Hatuna makubaliano tena na nyinyi", alisema Ibn Khudayr رضي الله عنه kwa uwazi kabisa. (Waqidi, II, 499)

Hata hivyo, kabla ya kuashiria kuanza kwa vita, Mtukufu Mtume ﷺ alikaribia jirani na kuta za ngome zao na kuwaita kwenye Uislamu. Lakini walikataa katakata pendekezo lake.[202]

Kutokana na kuendelea kwa mzingiro uliowapeleka Mayahudi kwenye shinikizo zaidi, mmoja wa viongozi wao, Kaab Ibn Asad aliwashauri kuwa, "Fanyeni kiapo cha utii kwa mtu huyu na muukubali utume wake." Akaendelea: "Hakuna shaka kwamba yeye ndiye Mtume tuliyekuwa tukimsubiri ambaye sifa zake tunaziona katika vitabu vyetu. Tukitangaza kuwa tunamuamini, tutaweza kupata masamaha!"

"Hatutaiacha Taurati wala hatutachukua kitabu kingine mahali pake," Mayahudi hao walipinga wazo lake.

Baada ya pendekezo lake la kwanza kutosikilizwa, Kaab alipendekeza kuwaua wanawake na watoto wao wenyewe na kisha

202. Tazama: Abdurrazzaq, V, 216, 370.

waingie katika vita vya kufa na kupona dhidi ya Waislamu au wasubiri siku ya Jumamosi jioni, ambayo haitarajiwi sana kupigana, wawapige Waislamu kwa kuwashtukiza kwa matarajio ya kuwashinda. Wakiwa wameshindwa kuwa na uamuzi mmoja, hawakukubali pendekezo lolote[203], kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu, alikuwa ameifanya khofu ipenye ndani ya nyoyo zao.

Vijana watatu, Salabah, Usayd na Asad walimtambua Mtukufu Mtume ﷺ kuwa amebeba sifa zote zilizoelezwa na wanazuoni wa Kiyahudi kama sifa za Mtume wa mwisho. Wakishuka kutoka katika ngome zao wakati wa usiku wa giza, waliungana na Mtukufu Mtume ﷺ.[204]

Hatimaye Mayahudi walilazimika kusalimu amri bila masharti yoyote. Kwa kuwa Mayahudi wa Banu Quraydha walikuwa katika hifadhi ya Aws, ili kwenda sawa na ombi rasmi la Mayahudi hao, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Saad رضي الله عنه kama mpatanishi. Licha ya kuwa na majeraha mazito kutokana na vita vya Khandaq, Saad رضي الله عنه aliitikia kwa hamasa wito wa Mtukufu Mtume ﷺ. Kwa maana huko nyuma alimuomba Mwenyezi Mungu baada ya kujeruhiwa kwenye medani ya mapambano "...asivute pumzi yake ya mwisho mpaka mgogoro wa Banu Quraydha umalizike!"

Vilevile, kutokana na ombi la Mayahudi, Saad رضي الله عنه alifanya uamuzi kulingana na sheria ya Nabii Musa عليه السلام.[205] Mtukufu Mtume ﷺ naye alithibitisha hukmu ya Saad, akasema: "Ewe Saad, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika umehukumu kwa mujibu wa hukmu

203. Ibn Hisham, III, 254.

204. Ibn Hisham, III, 256.

205. Kwa mujibu wa Agano la Kale, adhabu ya kosa kama hilo lililofanywa na Banu Quraydha ni kuuawa kwa wanaume wote wakubwa, kuchukua mali zao zote kama ngawira na kuwachukua wanawake na watoto wote kama mateka. (Tazama: Agano la Kale, Kumbukumbu, 20/10-15)

ya Mwenyezi Mungu iliyo juu ya mbingu saba!" (Bukhari, Maghazi, 30; Ibn Sad, III, 426)

Dua ya dhati ya Saad ilikubaliwa na baada ya kutoa hukmu hiyo kuhusu Mayahudi waliofanya khiyana na njama za kiovu dhidi ya Waislamu wakati wa Vita, jeraha lake lilifumka tena. Haikuchukua muda mrefu, Swahaba huyo mtukufu aliyejitolea kwa dhati na kwa moyo wote kwa ajili ya Mtukufu Mtume ﷺ, akavuta pumzi yake ya mwisho akafa kishahidi na kupata rehma ya milele.[206]

Mtukufu Mtume ﷺ alimuelezea akisema: "Arshi ya *Rahman* ilitikisika kwa kifo cha Saad ibn Muadh." (Bukhari, Manaqib'ul-Ansar 12; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 125)

Japokuwa Saad alikuwa mtu mwenye misuli, wale waliobeba jeneza lake hawakuhisi uzito wowote mabegani mwao. Mtukufu Mtume ﷺ alifafanua akisema: "Watu wamembeba, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, malaika wanaifurahia roho ya Saad!" (Ibn Hisham, III, 271; Tirmidhi, Manaqib, 50/3848)

Baada ya kuongoza swala ya jeneza na kumzika Saad, Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea kusoma *tasbih* kwa muda kidogo. Maswahaba walimfuata Mtukufu Mtume ﷺ na kuungana naye. Kisha Mtume ﷺ akasoma *takbir*.

Maswahaba walilazimika kumuuliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa nini ulisoma *tasbih* na kisha *takbir*?"

"Kaburi lilimbana mja huyu mwema mpaka pale Mwenyezi Mungu alipolifanya kuwa pana," alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. (Ahmad, III, 360)

206. Tazama: Ibn Hisham, III, 271.

Mtume akaendelea kusema: "Lau kama angekuwepo mtu mwenye kinga ya kutopata mtihani wa kaburi, basi mtu huyo angekuwa Saad. Lakini kaburi lilimbana kwanza mpaka Mwenyezi Mungu alilifanya lipanuke." (Tabarani, Mujam'ul-Kaabir, X, 334)

Kwa mujibu wa maelezo ya Anas ﵁, siku moja Mtukufu Mtume ﷺ aliletewa zawad ya kaftan iliyopambwa, ambayo uzuri na ulaini wake uliwavutia wengi. Mtume wa rehma ﷺ akasema: "Ninaapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mikononi Mwake, vitambaa vya Saad peponi ni vizuri na vyenye thaman sana kuliko hiki." (Bukhari, Bad'ul-Khalq, 8; Muslim, Fadail, 126)

Qur'an Tukufu imeuelezea ushindi uliopatikana kufuatia Vita vya Khandaq kwa msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika aya ifuatayo:

وَأَنزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُم مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِن صَيَاصِيهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا وَأَوْرَثَكُمْ أَرْضَهُمْ وَدِيَارَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ وَأَرْضًا لَّمْ تَطَؤُوهَا وَكَانَ اللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا

"Na akawateremsha wale walio wasaidia (maadui) katika Watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao; na akatia khofu katika nyoyo zao. Baadhi yao mkawa mnawauwa, na wengine mnawateka. Na akakurithisheni ardhi zao na nyumba zao na mali zao, na ardhi msiyo pata kuikanyaga. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu." (Al-Ahzab, 33: 26-27)

MWAKA WA SITA WA HIJRA

Mkataba Wa Hudaybiyah: Msingi Wa Ushindi Wote Na Kichocheo Muhimu Cha Kurudi Makka

Kulinagana na ndoto aliyoiona, Mtukufu Mtume ﷺ aliwataka Waislamu kujiandaa na safari ya kwenda Al-Kaabah kwa ajili ya hijja.[207] Akisuhubiana na jumla ya Maswahaba elfu moja na mia nne[208] ambao waliitikia wito wake, Mtukufu Mtume ﷺ alianza safari ya kwenda Makka, katika Jumatatu ya mwanzo ya mwezi wa Dhilqadah, mwaka wa sita wa Hijrah. Kwa kuwa hawakuwa wameenda kwa ajili ya vita, hawakuchukua silaha zaidi ya panga kwa ajili ya kujilinda. Vilevile walikuwa na ngamia wapatao sabini kwa ajili ya ibada ya kuchinja.[209]

Omar رضي الله عنه alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ iwapo hakuwa na wasiwasi juu ya uwezekano wa kushambuliwa na Abu Sufyan na watu wake, na hivyo akashauri kuwa ingekuwa bora kwao kubeba silaha zaidi ya zile walizokusudia kuzibeba.

"Sina hakika", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. "Nisingependa kubeba silaha wakati nimekusudia kwenda kwa ajili ya *Umrah*." (Waqidi, II, 573)

---

207. Waqidi, II, 572.
208. Ibn Saad, II, 95. Kwa mujibu wa vyanzo vingine, walipofika njiani, Mabedui wa Kiarabu waliungana na msafara wake na hivyo idadi yao ikaongezeka na kufikia watu elfu moja na mia tano mpaka elfu moja na mia saba.
209. Ibn Saad, II, 95.

Walipofika kwenye mpaka wa *miqat* wa Dhuhulayfah, Mtukufu Mtume ﷺ alivaa *ihram* na kuweka nia ya kutekeleza ibada ya *Umrah*.

Maswahaba nao walifanya hivyo hivyo. Wakaanza kutoa *talbiyah* kwa sauti ya juu, wakiakisi na kuonesha hamu na shauku yao kubwa ya kuungana na Kaabah haraka iwezekanavyo.Kila hatua waliyopiga, hamasa na shauku ya kimaanawi iliwasogeza Waislamu karibu na kusudio la safari yao.

Lakini wasiwasi usioelezeka uliwakumba washirikina wa Kiqurayshi mara baada ya kupata taarifa za ujio wa Waislamu. Katika kikao cha dharura walichoketi, waliamua kutowaruhusu Waislamu kuingia Makka kwa gharama yoyote ile. Kikosi kidogo chenye askari mia mbili kilichokusanywa chini ya uongozi wa Khalid ibn Walid na Iqrimah kiliondoka Makka kwenda kuwakabili Waislamu.

Wakati huo Mtukufu Mtume ﷺ na Waislamu walikuwa wamefika Sariyyah, eneo ambalo ilikuwa ni rahisi kwao kuteremkia Makka. Lakini Qaswa, ngamia aliyekuwa amepandwa na Mtukufu Mtume ﷺ alipiga magoti na kugoma kuendelea na safari. Juhudi zote zilizofanywa na Maswahaba kumfanya aendelee na safari hazikuzaa matunda.Wakaanza kusema kuwa ngamia alikuwa hataki kusonga mbele.

"Hajagoma kwenda na hana tabia ya aina hiyo. Bali amesimamishwa na Yule aliyemzuia kuingia Makka!" alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Kisha akaongeza kusema: "Ninaapa kwa Yeye ambaye nafsi yangu ipo mikononi Mwake, masharti yoyote watakayoyaweka Maqurayshi katika kuheshimu kile ambacho Mwenyezi Mungu amepiga marufuku kisifanyike katika Nyumba Yake tukufu, nitayakubali!"

Kisha akamuamrisha ngamia kuondoka; naye akasimama. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akabadilisha njia kuwakwepa Maqurayshi na kuteremka jirani na kisima kisichokuwa na maji. Hili lilikuwa eneo lililo mbali zaidi na Makka kutokea Hudaybiya. Kisima hicho hakikuwa na maji; kiasi kidogo cha maji kilichokuwepo kilikuwa kimekauka kabisa. Maswahaba wakamlalamikia Mtukufu Mtume ﷺ juu ya ukosefu wa maji. Mtume ﷺ akachukua mshale kutoka katika mkoba wake na kuwaambia wauisimike katikati ya kisima. Haukupita muda mrefu, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, kisima hicho kikaanza kububujisha maji, kikaendelea kumwaga maji kwa wingi mpaka Maswahaba walipoamua kuondoka.

Wakati huo huo, Budayl, kiongozi wa kabila la Khuzaa, aliwasili akiwa na askari wachache. Alizungumza kuhusu wasiwasi wa watu wa Makka na maandalizi waliyokuwa wameyafanya kwa ajili ya vita. Licha ya wasiwasi huo wa Maqurayshi, Mtukufu Mtume ﷺ alimuelezea Budayl sababu ya ujio wao kama ifuatavyo:

"Hatukuja kupigana na yeyote. Lengo letu ni kuitembelea Nyumba ya Mwenyezi Mungu; kutekeleza ibada ya *umrah*. Vita vimewaua Maqurayshi wengi...vimewadhoofisha na kusababisha hasara kubwa. Ikiwa watapenda, tunaweza kufanya makubaliano ya mkataba kwa kipindi fulani cha muda. Kwa kufanya hivyo hawataziba njia baina yangu na watu wengine. Nitakapowavuta wengine, basi Maqurayshi wakipenda nao wanaweza kuingia katika Uislamu kama watakavyoingia watu hao. Nikishindwa, basi Maqurayshi watapumua zaidi. Wakilikataa pendekezo hili, basi naapa kwa Allah kwamba nitapambana kwa ajili ya Dini hii mpaka kichwa changu kitenganishwe na mwili wangu. Hakika Mwenyezi Mungu atatimiza ahadi Yake."

Budayl alirejea Makkah na kuyafikisha maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa Maqurayshi, ambapo baada ya kuyasikia, Urwa ibn Masud alisimama na kusema: "Hakika mtu huyu anaku-

onesheni njia ya wema. Kubalini pendekezo lake na mnitume kwake ili kufanya mkataba!"

Wakubwa wa Kiqurayshi walikubali na kumtuma. Mtukufu Mtume ﷺ alirejea kumueleza Urwa maneno yale yale aliyomwambia Budayl. Wakati wote wa mazungumzo, Urwa alikuwa akiwachunguza maswahaba. Aliporejea Makka aliwahadithia washirikina kile alichokiona bila kumung'unya maneno:

"Ndugu zangu! Nisikilizeni kwa makini. Ninawaapia kwamba kama balozi wenu nimewahi kufika mbele ya wafalme wengi. Nimewahi kusimama mbele ya Khosrou, Kaisari na Najjashi. Lakini kote huko sijawahi kuona utii na heshima ambayo Waislamu wanampa Muhammad! Anapotaka kitu, wote hukimbia kumchukulia. Anapochukua wudhu, hushindana kugombania maji yake. Anapozungumza, wote humsikiliza. Mbali na heshima yao kwake, huyashusha macho yao na hawamtazami moja kwa moja usoni mwake hata kidogo. Nywele moja inapodondoka kutoka kichwani mwake hufanya haraka kuichukua na kuitunza kama kitu cha thamani mno. Mtu huyu ametoa pendekezo lenye maana. Tulikubali!"[210]

Baada ya Urwa kuzungumza aliyotakiwa kuyazungumza, mtu mwingine kutoka kabila la Kinanah aliomba ruhusa ya kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Hivyo alitumwa. Mtukufu Mtume ﷺ alipomuona, alisema:

210. Thomas Carlyle anahisi kuwa ni lazima akiri ukweli huu pale anaposema: "Hakuna mfalme mwenye taji kichwani mwake ambaye amewahi kupata heshima kama aliyopata Muhammad, alivaa mavazi ambayo aliyanunua kutokana na kipato cha kazi ya mikono yake mwenyewe."

"Amekuja mtu kutoka katika kabila linalothamini ngamia waliowekwa maalumu kwa ajili ya hijja na *umrah*. Waachieni ngamia wenu wa sadaka ili aweze kuona!"

Mtu huyo hakuweza kufanya lolote zaidi ya kuwaambia wenzake: "Haionekani kuwa jambo sahihi kuwazuia kuitembelea Kaabah!" (Bukhari, Shurut, 15; Ahmad, IV, 323-324)

Bila kujali mambo waliyoambiwa na wajumbe wao, Maquraysh walitumia kikosi cha askari wa farasi kuanzisha mashambulizi dhidi ya Waislamu. Japokuwa washambuliaji hao walishikiliwa kama mateka na Waislamu, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaachia huru ili kuweka wazi kuwa nia yake ni kufanya Umrah, sio kumwaga damu.[211]

211. Muslim, Jihad, 132, 133.

Hapo Hudaybiya, hema la Mtume ﷺ lilikuwa limewekwa nje ya mipaka ya Haram. Pamoja na hivyo, katika kipindi chote alichokaa hapo, bado Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akienda ndani ya mipaka ya Haram kwa ajili ya kuswali.[212] Zaidi ya hivyo, swala inayoswaliwa katika viunga vya Kaabah ina daraja kubwa kuliko swala laki moja zinazoswaliwa katika maeneo mengine.[213]

Kiapo cha Utii cha Ridh-waan: Tukio lililoridhiwa na kumfurahisha Mwenyezi Mungu

Mabalozi wengine kadhaa kutoka upande wa Maqurayshi walitembelea Waislamu katika kipndi hicho kifupi. Lakini kwa sababu makubaliano ya mwisho ya amani yalikuwa hayajafikiwa, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Othman رضي الله عنه kwenda Makka kuongea na washirikiana na kulimaliza suala hilo. Alimwambia:

"Nenda kwa Maqurayshi! Waambie kwamba hatukuja hapa kupigana na yeyote, bali tumekuja kuzuru Nyumba ya Mwenyezi Mungu, tukiwa ni wenye kuheshimu na kuchunga utukufu wake, na kwamba tutachinja wanyama wa sadaka tuliokuja nao na kisha tutarejea! Kisha waite kwenye Uislamu!" Wakati huo huo, Mtukufu Mtume ﷺ alimuamuru kuongea na kila Muislamu mjini Makka, wanaume kwa wanawake, na awape bishara njema ya ufunguzi wa Makka unaokuja hivi karibuni, awahakikishie kwamba Mwenyezi Mungu anainusuri dini Yake na kwamba inakuja siku ambayo watatangaza waziwazi imani yao mjini Makka. (Ibn Sad, II, 97; Ibn, Qayyim, III, 290)

Kutokana na amri hiyo ya Mtukufu Mtume ﷺ, haraka sana Othman رضي الله عنه akaelekea Makka na kuwafikishia washirikina ujumbe

212. Waqidi, II, 614; Ahmad, IV, 326.
213. Ibn Majah, Iqamah, 195.

huo. Washirikina waliendelea kuwa wagumu na kutowaruhusu Waislamu kuingia. Walimuweka Othman ﷺ chini ya uchunguzi wa karibu, wakamwambia anaweza kuizunguka Nyumba Tukufu iwapo atataka kufanya hivyo. Lakini, aliona kuwa hilo halimfai yeye kama mtu anayetakiwa kumtii Mtukufu Mtume ﷺ na heshima kuu aliyonayo kwake, hivyo akajibu:

"Sitafanya mpaka pale Mtume wa Mwenyezi Mungu atakapofanya hivyo. Sitaizuru Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu kabla yake!" (Ahmad, IV, 324)

Othman ﷺ alizuiliwa na Maqurayshi kwa muda mrefu zaidi ya ilivyotarajiwa; kiasi kwamba minong'ono kwamba 'Othman ameuawa' ikavuma ndani ya safu za Waislamu na kuibua hali tete bain ya pande mbili. Baada ya kupima uwezekano kwamba yumkini mjumbe wake akawa ameuawa, Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya Maswahaba wote, akawaambia: "Yaonekana hatutaweza kuondoka bila kupigana na waabudu masanamu!" (Ibn Hisham, III, 364)

Kisha alitaka kiapo cha utii kutoja kwa Maswahaba wote. Kiapo cha kufa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu iwapo itahitajika. Kila mmoja alitoa kiapo chake cha utii kwa moyo wote. (Waqidi, II, 603)

Waislamu waliahidi kupambana mpaka mauti yawakute katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Walifanya hivyo kwa kuiweka mikono yao juu ya mkono wa Mtukufu Mtume ﷺ. Mwisho wa kiapo hicho, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliushika mkono wake mmoja akauambatanisha na mwingine,akasema: "...na hiki ni kiapo cha Othman!" (Bukhari, Ashab'un-Nabi, 7)

Kiapo hicho kilifanyika chini ya mti na hivyo ikaitwa kuwa ni Kiapo cha utii cha Ridh-wan au Hudaybiya. Pakiwa hakuna mnafiki hata mmoja, siku hiyo kila Swahaba alitoa kiapo chake cha utii; kiapo ambacho kilifanya Mwenyezi Mungu Mtukufu awe radhi nao:

لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walipo fungamana nawe chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa Ushindi wa karibu." (Surat al-Fath, 48: 18)

Hapo baadaye, akiwa mbele ya bibi Hafsa ﵂, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Inshaallah, katika wale waliotoa kiapo cha utii na mafungamano chini ya mti hakuna yeyote miongoni mwao atakayeingia Motoni."

Bibi Hafsa ﵂ akiwa mwenye kutaka kudadisi zaidi akalazimika kuuliza: "Lakini, Ewe Mjumbe wa Allah, itakuwaje hivyo hali ya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَإِن مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَى رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا

"Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe." (Surat Maryam, 19: 71)

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu kwa kusema: "Mwenyezi Mungu pia anaeleza:

ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوا وَّنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثِيًّا

"Kisha tutawaokoa wale waliomcha Mungu; na tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti." (Surat Maryam, 19: 72)

Kwa hiyo, imedhihirika kuwa aya hiyo haihusu kuingia hasa Motoni, bali wakati wa kupita kwenye *sirat*. (Muslim, Fadail'us-Sahabah, 163)

Jabir ﷺ anasimulia:

"Siku ya Hudaybiya watu walikuwa wamechoka mno kutokana na kiu, kiasi kwamba walikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ambaye wakati huo, alikuwa na kiriba cha maji kilichotengenezwa kwa ngozi. Alikuwa amemaliza kuchukuwa wudhu pindi watu walipokwenda karibu naye.

'Kitu gani kimewasibu?' aliuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

'Hatuna maji ya kunywa na ya kuchuka wudhu isipokuwa kiasi kidogo kilicho mbele yetu,' walieleza.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliweka mikono yake ndani ya kiriba. Mara moja maji yakaanza kububujika katikati ya vidole vyake; yalibubujika kwa nguvu kama chemichemi inayofoka. Sote tulikunywa na kuchukua wudhu kutokana na maji hayo."

"Mlikuwa wangapi siku hiyo?" aliulizwa Jabir ﷺ.

"Kama tungekuwa laki moja, bado maji hayo yangetosha; lakini wakati huo tulikuwa watu elfu moja na mia tano." (Bukhari, Manaqib, 25)

Mkataba wa Hudaybiyah: Awamu Mpya
Kabisa katika Kazi ya ulinganiaji

Washirikina wa Makkah walipatwa na wasiwasi mkubwa walipopata habari kuwa Waislamu wameahidi kupambana nao mpaka

mauti yawakute itakapohitajika kufanya hivyo. Wakiwa wameingiwa na khofu kwa kutambua kuwa sasa mambo yalikuwa yamefikia katika hali tete, haraka sana waliamua kufikia makubaliano ya amani na kumtuma Suhayl ibn Amr kwenda kufanya mazungumzo kwa niaba yao.

Mtukufu Mtume ﷺ alipoona kuwa Suhayl ndiye anayekuja kwa mazungumzo ya amani, aliwaambia Waislamu: "Sasa mambo yatakuwa mepesi kwenu; aliyekuja ni Suhayl!" Alisema hayo kutokana na ukweli kwamba jina Suhayl katika lugha ya Kiarabu lina maana ya *mwepesi*. Hapo Mtume wa Rehma ﷺ akaweka mkakati wa amani kulingana na amri ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَإِن جَنَحُواْ لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا

"Na wakielekea amani nawe pia elekea..." (Surat al-Anfal, 8: 61)

Lengo la awali na la kwanza kabisa la washirikina wa Makka ilikuwa ni kuwazuia Waislamu wasifanye *umrah*, angalu kwa mwaka ule. Aidha, waliweka masharti ambayo, kwa nje, yalionekana kuwa mazito sana. Baada ya muda mrefu wa mazungumzo na majadiliano makali, masharti yao yalikubaliwa.

Mtukufu Mtume ﷺ alimpa Ali رضي الله عنه jukumu la kuviweka katika maandishi vipengele walivyokubaliana. Ali رضي الله عنه alianza kuandika waraka huo kwa *Bismillahir-rahmanir-rahiim*, lakini Suhayl akaweka pingamizi. Hivyo badala yake akaandika *Bismikallahumma*. Huo haukuwa mwisho wa vipingamizi vya Suhayl; pia alipinga kuandika jina la Mtume kwa kutumia neno la 'Mtume wa Mwenyezi Mungu.'

"Je, kama tungekuwa tumekukubali kwamba wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu tungekupiga vita na kukuzuia kuizuru Kaabah?" alieleza Suhayl.

Wakiwa wenye kuhisi taabu kutokana na kuwekewa masharti mazito ya mkataba, Maswahaba waliokuwa wamehamanika sasa walikuwa wamefikia hatua ya kuchemka. Ali ﷺ aliiweka pembeni kalamu yake na kusema: "Wallah, kamwe siwezi kufuta neno 'Mtume wa Mwenyezi Mungu'!"

"Kwa vyovyote mtakavyojitahidi kunikana, lakini mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu", Mtume ﷺ alimwambia wazi Suhayl. Kisha aliomba aoneshwe sehemu hiyo iliykuwa imeandikwa neno 'Mtume wa Mwenyezi Mungu', ambapo baada ya kuoneshwa alilifuta kwa mkono wake na badala yake akataka iandikwe: Muhammad ibn Abdillah.

Kutokana na hekma nyingi zilizokuwemo ndani ya mkataba huo, Mtukufu Mtume ﷺ alikubali masharti yaliyokuwa yamewekwa na Maqurayshi. Miongoni mwa masharti ya mkataba huo ni haya yafuatayo:

1. Mkataba huu utadumu kwa muda wa miaka kumi.

2. Waislamu hawataizuru Kaabah kwa sasa bali ziara yao itaahirishwa mpaka mwaka ujao. Mahujaji watakaofika Makka mwaka ujao hawatakaa zaidi ya siku tatu, ambapo wenyeji, ambao hawataruhusiwa kuwasiliana na Waislamu, watakuwa wameondoka Makka.

3. Mtu wa Makka atakayekimbilia Madina atarejeshwa, hata kama akiwa Muislamu. Lakini mtu wa Madina atakayekimbilia Makka hatarejeshwa.

4. Makabila mengine ya Kiarabu yatakuwa na uhuru wa kuwa pamoja na Waislamu au Maqurayshi.

Mud mfupi tu baada ya Abu Jundal kumaliza kuandika masharti hayo, mtoto wa mjumbe wa Maqurayshi, Suhayl ibn

Amr, alifika mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ akiburuza miguu yake iliyokuwa imefungwa minyororo. Baada ya kupata upenyo, aliweza kuwatoroka washirikina na kwenda kwa Waislamu. Lakini, Suhayl, huku akimpiga mwanaye usoni kwa fimbo yake, aliingilia kati na kuwaambia Waislamu kuwa Abu Jandal anatakiwa kuwa mtu wa kwanza kurejeshwa kwa washirikina, kwa mujibu wa mkataba huo, la sivyo wangekuwa tayari kuvunja masharti ya mkataba. Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alipoona tukio hilo, alijawa na huzuni isiyo kifani, akasisitiza Abu Jandal asihusishwe na masharti ya mkataba na aachwe abaki kwa Waislamu. Lakini, Suhayl, kwa moyo wa jiwe, alipinga vikali. Wakati akikabidhiwa ili kurejeshwa kwa washirikina, Abu Jundal ؓ aliwaeleza Waislamu kwa hisia kali akiwaomba msaada:

"Je mnanirejesha kwenye moto uleule?" aliuliza kwa hisia kali, na hilo lilitosha kuamsha hisia za Waislamu ambao walikuwa na huzuni nzito, na kuwafanya wengi wao watokwe na machozi. Ni wakati huo ambapo Mtukufu Mtume ﷺ alimfariji Abu Jundal akisema:

"Fanya subira zaidi ewe Abu Jandal; fanya vumilia! Hakika malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu! Hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu atatoa kimbilio na faraja kwa Waislamu wanyonge na wasiokuwa na msaada kama wewe! Imetokea kwamba tumefanya mkataba na hawa watu na tumetoa ahadi yetu kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba tutaulinda na kuuheshimu. Nao pia, wametoa ahadi yao kwa jina la Mwenyezi Mungu. Hatuwezi kukiuka ahadi yetu, kwa maana haitakuwa na faida!" (Ahmad, IV, 325; Ibn Hisham, III, 367)

Mbali na maneno hayo, Mtume ﷺ, ambaye alikuwa na huruma isiyokuwa na mipaka, alijaribu tena kuwashawishi washirikina wamuache:

"Tafadhalini! Muacheni abaki nami", alimuomba Suhayl kwa mara nyingine. Suhayl hakubadili msimamo wake.

"Basi angalau muwekeni chini ya hifadhi yenu," Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliomba tena. Suhayl hakulikubali hata hilo. Wawakilishi wengine wawili wa Kiqurayshi, Huwaytib na Miqraz, walimkwepa Suhayl na kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakamhakikishia kuwa watamuweka Abu Jandal chini ya hifadhi yao na watamlinda dhidi ya mateso yoyote yanayoweza kutokea. (Waqidi, II, 608; Balazuri, I, 220)

Kwa kiasi fulani Mtukufu Mtume ﷺ aliaondoka akiwa na uhakika.

Kutokana na kujaa na kufurika kwa mto wa imani ndani ya moyo wake, Omar ؓ, ambaye hakuweza tena kuvumilia na kustahmili msimamo wa ukaidi na kiburi wa washirikina, alishindwa kujizuia. Kwa hakika, Maswahaba wengine, isipokuwa Abu Bakr ؓ, nao walikuwa na hali hiyo hiyo. Omar ؓ alienda mbali zaidi kiasi cha kuzungumza dhidi ya namna ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alililishughulikia suala hilo, kwa matumaini ya kuukwepa mkataba ambao kwa juu juu ulionekana kuwa pigo la dhahiri kwa Waislamu. Hata hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alimkumbusha kuwa alichokuwa anakifanya ni kutekeleza amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

"Mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", alisema na kuongeza: "Siwezi kwenda kinyume au kuasi amri Yake. Yeye ndiye Msaidizi wangu!" (Bukhari, Maghazi, 35; Muslim, Jihad, 90-97)

Wakati Suhayl akirejea Makka kwa majigambo baada ya kusaini mkataba huku ukiwa na mwanaye pembeni, Mtukufu Mtume ﷺ ali-

waashiria Maswahaba kuwa: "Chinjeni wanyama wenu wa sadaka na mkate nywele zenu!"

Lakini, hakuna Swahaba yeyote aliyetikisika hata kidogo kwenda kutekeleza amri hiyo. Walikuwa wamehujawa na huzuni na kuishiwa hamu kufuatia matukio ambayo fumbo lake hawakuweza kulifumbua. Hata hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alirudia amri yake mara tatu. Kwa mara nyingine, hakuna aliyetikisika. Huu haukuwa uasi hata kidogo. Bali ilikuwa ni hali ya kuduwaa kwa muda, kwa matarjio yenye matumaini kwamba huwenda mkataba huo, ambao wino wake ulikuwa haujakauka, ungebatilishwa. Kusubiri huko kulichochewa na shauku kubwa ya kuitembelea Kaabah ambayo ilikuwa ikizichoma nyoyo zao. Aidha, hawa ndo Maswahaba wale wale ambao, siku moja kabla, walikuwa wamekula kiapo cha utii na kula yamini ya kufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mbele ya Mpendwa wao, Mtume ﷺ.

Hali ya kutojali iliyooneshwa na Maswahaba ilimhuzunisha sana Mtukufu Mtume ﷺ ambaye, kutokana na kuwa katika hali ya kuvunjika moyo, aliingia ndani ya hema la mkewe mpendwa, Umm Salamah. Baada ya kumwambia kuhusu hali hiyo, bibi huyo mwenye busara, Umm Salamah alimfariji Mtukufu Mtume ﷺ na kumwambia: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mchinje mnyama wako wa sadaka, bila kuwaambia chochote Maswahaba wako, na ukate nywele zako. Baada ya wewe kufanya hivyo, nao watakufuata hata kama wana mzigo mkubwa wa huzuni na uchungu...tafadhali wasamehe!"

Baada ya mazungumzo hayo mafupi, Mtukufu Mtume ﷺ alitoka na kwenda kufanya kama ilivyoshauriwa. Hapo Maswahaba wakajua kuwa isingwezekana tena kuachana na mkataba huo na wote wakafanya kama alivyofanya Mtume ﷺ. Wote waliwachinja wanyama wao wa sadaka na kukata nywele zao. Umm Salamah

ﷺ, ambaye alishuhudia hali, anasema: "Waislamu waliruka kwa hamasa kwenda kuwachinja ngamia wao wa sadaka kiasi kwamba nilihofu kuwa watakanyagana." (Bukhari, Shurut, 15; Ahmad, IV, 326, 331; Waqidi, II, 613)

Waislamu walipomaliza kuwachinja wanyama wao wa sadaka na kukatwa nywele zao, Mwenyezi Mungu Mtukufu alituma upepo mkali uliozipeperusha nywele zao kuelekea upande wa Haram. Maswahaba wakachukulia hiyo kama alama ya kukubaliwa kwa *umrah* yao.[214] Kisha wakaanza safari ya kurudi Madina.

Baadaye, Surat al-Fath iliteremshwa kutokana na Maswahaba kuanza kuingiwa na hofu ya kughadhibikiwa na Mwenyezi Mungu kutokana na kwamba mwanzo hawakufurahia na wakaonesha tofauti juu ya mkataba huo uliokuwa na hekima ambazo wao hawakuzifahamu:

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا وَيَنصُرَكَ اللَّهُ نَصْرًا عَزِيزًا

"Hakika tumekufungulia Ushindi wa dhaahiri. Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyo tangulia na yajayo, na akutimizie neema zake, na akuongoe katika Njia Iliyo Nyooka. Na Mwenyezi Mungu akunusuru nusura yenye nguvu." (al-Fath, 1-3)

Mujammi ibn Jariyah ﷺ anasimulia juu ya hofu waliyokuwa nayo Maswahaba baada ya kuteremshwa kwa Surat al-Fath:

"Wote walikuwa wametawanyika kuelekea kwenye ngamia wao, kwa hofu. Walikuwa wakiulizana nini hasa kitakachoendelea. 'Mtume wa Mwenyezi Mungu amepokea Wahyi', baadhi walisema.

214. Ibn Saad, II, 104; Halabi, II, 713.

Kisha tulirudi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu tukiwa na hofu. Pindi watu wote walipokusanyika, Mtume wa Mwenyezi Mungu akasoma Surat al-Fath." (Ibn Sad, II, 105)

Omar ﵁ anaeleza hivyo hivyo: "Kutokana na kuhofia matokeo ya kile nilichomwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu siku hiyo, na ili kuwa na mwisho mwema, nilifunga swaumu mfululizo, nikatoa sadaka nyingi, nikaswali swala za sunna na kuwalisha maskini wengi." (Ibn Sayyidinnas, II, 167)

Surah al-Fath ilikuwa ufunguo wa awali wa milango ya ushindi ambayo ilikuwa ikianza kuwafungukia Waislamu. Haukupita muda mrefu, matunda yaliyodokezwa na sura hiyo yakaanza kuchumwa. Makabila ya jirani yalikuwa yameikebehi safari hiyo ya Waislamu kwa kuipa jina la 'safari isiyokuwa na kurejea'. Walipomuona Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba wakirudi bila majeraha yoyote, walimkimbilia kwenda kumuomba msamaha. Hali yao hiyo imeelezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ifuatavyo:

بَلْ ظَنَنتُمْ أَن لَّن يَنقَلِبَ الرَّسُولُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَى أَهْلِيهِمْ أَبَدًا وَزُيِّنَ ذَلِكَ فِي قُلُوبِكُمْ وَظَنَنتُمْ ظَنَّ السَّوْءِ وَكُنتُمْ قَوْمًا بُورًا وَمَن لَّمْ يُؤْمِن بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ فَإِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَعِيرًا

"Lakini mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu, na mkadhania dhana mbaya, na mkawa watu wanao angamia. Na asiyemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi kwa hakika Sisi tumewaandalia makafiri Moto mkali." (al-Fath: 12-13)

Kwa juu juu, vipengele vya mkataba wa Hudaybiyya vilionekana kutokuwa na faida kwa Waislamu. Ni baada tu ya kuteremshwa kwa Surat al-Fath ndipo ilipodhihirika kwamba kile ambacho awali kilionekana kuwa pigo na kuanguka, kwa ndani kilionekana kuwa kushindi wa dhahiri na wenye kudumu. Qur'an Tukufu inasema kuwa:

"...huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." (al-Baqara: 216)

Hekma mbalimbali zilizokuwa nyuma ya tukio hili lenye ukungu, ambalo mwanzo ilimuwea vigumu Mtume ﷺ kulifafanua, zilizijidhihirisha waziwazi kabisa baada tu ya miaka miwili. Mazingira ya amani yaliyotengenezwa na mkataba huo yalikuwa sababu ya kwa watu mbalimbali kuingia katika Uislamu; walikuwa watu wengi mno kiasi kwamba ndani ya miaka hiyo miwili, idadi yao ilivuka idadi ya Waislamu wote waliokuwepo kabla ya mkataba wa Hudaybiyyah.

Ni kweli kuwa Waislamu walizuia kufanya ibada ya *umarah* kwa mwaka huo na wakalazimika kuvumilia kwa muda fulani kile kilichoonekana kuwa masharti magumu. Lakini faida zilizopatikana katika kipindi hicho zilikuwa kubwa na nyingi sana kushinda maumivu hayo. Kwa kufanya mkataba huo ilimaanisha kwamba sasa Uislamu unatambulika rasmi. Sasa walitakiwa kusubiri tu mwaka mwingine ili kufanya ziara ya uhakika kwenye Kaabah. Yeyote ailiyetaka kuungana na Waislamu kutoka katika makabila jirani ya Kiarabu, sasa alikuwa na uwezo huo. Hii ilishiria kupungua kwa ushawishi wa Makurayshi wa Makkah na kutoa nafasi kwa wito wa Uislamu kusambaa.

Sababu nyingine iliyomfanya Mtukufu Mtume ﷺ kupendelea amani ni idadi kubwa na muhimu ya watu wa Makkah ambao, kwa

sababu za wazi kabisa, walikuwa wakiutekeleza Uislamu wao kwa siri. Lau kama vita ingetokea baina ya Waislamu na Washirikina, basi Waislamu hao wa Makka wangefichuliwa na kuuawa.

Kwa kufanya mkataba huo, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Nabii wa rehma, alikuwa akituma ishara zisizokuwa za wazi kwa Waislamu watarajiwa kutoka Makka na wale wa makabila jirani ya Kiarabu na kuwakaribisha kwenye Uislamu. Haikuchukua muda mrefu matunda ya sera hii yakapatikana.

Ushindi wa Wazi: Uwongofu Wenye Kuendelea Milele

Waabudu masanamu wa Makka, ambao walifurahi mno kwa kukubaliwa kwa vipengele vya masharti ya mkataba wa Hudaybiyyah, kwa kweli walikuwa wameondoa vizuizi vilivyokuwa vikiwazuia kupanua ujumbe wao na walikuwa wamewaweka katika nafasi bora kwa mikono yao wenyewe. Maqurayshi walipoona kwamba takriban Maswahaba wote hawakuwa tayari kuyatambua masharti ya mkataba, kwa kudhani kuwa ingekuwa na hasara kubwa kwao, hali hiyo ilitia kifuniko mbele ya macho ya maqurayshi, wakasaini mkataba huo kwa hamasa kubwa, kwa mategemea kwamba watapata ushindi mkubwa. Lakini, uhalisia halisi wa mkataba huo, ambao hata waumini walifichwa hekma yake mwanzo, ilianza kudhihiri pindi vipengele hivyo vilipoanza kutekelezwa.

Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye tokea mwanzo alijua vyema baraka na neema zilizokuwa ndani ya mkataba huo, alikuwa na hima sana ya kutekeleza mkataba wa Hudaybiyya na kujitahidi kuitumia kila fursa inayojitokeza. Kwa mfano, kundi moja la wanawake kutoka Makkah lilipokuja Madina kutaka hifadhi, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyakataa matakwa ya Maqurayshi waliotaka awakabidhi kwao. Aliwakatalia Maqurayshi hao kwa misingi kwamba kipengele husika cha mkataba kinawahusu wanaume tu. Kwa kweli Mwenyezi

Mungu alikuwa ametoa amri kwamba wanawake hao wasirudishwe kwa Makafiri:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا جَاءَكُمُ الْمُؤْمِنَاتُ مُهَاجِرَاتٍ فَامْتَحِنُوهُنَّ اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ وَآتُوهُم مَّا أَنفَقُوا وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَن تَنكِحُوهُنَّ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ وَلَا تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ وَاسْأَلُوا مَا أَنفَقْتُمْ وَلْيَسْأَلُوا مَا أَنفَقُوا ذَلِكُمْ حُكْمُ اللَّهِ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

"Enyi mlio amini! Wakikujilieni wanawake Waumini walio hama, basi wafanyieni mtihani - Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua zaidi Imani yao. Mkiwa mnawajua kuwa ni Waumini basi msiwarudishe kwa makafiri. Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalikii wanawake Waumini. Na wapeni hao wanaume mahari walio toa. Wala hapana makosa kwenu kuwaoa mkiwapa mahari yao. Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu. Na takeni mlicho kitoa, na wao watake walicho kitoa. Hiyo ndiyo hukumu ya Mwenyezi Mungu anayo kuhukumuni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima." (Surat al-Mumtahinah: 10)[215]

Wakati huohuo, Abu Basir, mkazi wa Makka ambaye alikuwa amesilimu, alikuja Madina akitaka hifadhi. Kutokana na kulazimishwa na masharti ya mkataba, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa na chaguo jingine zaidi ya kumkabidhi kwa Makafiri. Kama ilivyokuwa kwa Maswahaba wengine, mwanzo Abu Basir aliona ugumu kuon-

215. Tazama: Bukhari, Shurut, 15; Waqidi, II, 631-632.

doka. Akiwa ametahayari, alimuuliza Mtukufu Mtume ﷺ iwapo alitaka arejee kwenye ibada ya kuabudu masanamu. Lakini kwa upole kabisa, Mtukufu Mtume ﷺ alimhakikishia Abu Basir kwamba hawataweza kuvunja ahadi yao na akamfariji kwa kumwambia "... kuwa na subira, hakika hivi karibuni Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuonesha wewe na wenzako njia."

Abu Basir alikubaliana na matakwa ya Mtume ﷺ. Akiyaweka maslahi ya Waislamu mbele yake, alijisalimisha kwa waabudu masanamu wa Makka. Sasa akawa mfu anayetembea, kwa maana alijua kwamba washirikina hawakuwa wakimpeleka Makka bali walikuwa wakimpeleka kwenye kifo. Kwa kulijua hili, alifanya upinzani mkali pindi fursa ya kwanza ilipotokea. Katika watu wawili waliokuwa wakimpeleka, alimuua mmoja, Hunays na mwingine akakimbia. Abu Basir alichukua mavazi, upanga na vitu vya kafiri aliyekuwa amemuua akarudi Madina kwa Mtume wa Mwenyei Mungu ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, chukua khumsi (moja ya tano) katika mali hii", alisema kumwambia Mtukufu Mtume ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Nikifanya hivyo nitakuwa nimekwenda kinyume na masharti ya mkataba. Kitendo ulichofanya na mali za mtu uliyemuua zinakuhusu wewe." (Waqidi, II, 626-627)

Yule mshirikina mwingine aliyekimbia, alirudi Madina kumtafuta Abu Basir.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ulitekeleza ahadi yako uliponikabidhi kwao... lakini nililazimika kuyaokoa maisha yangu;, alisema Abu Basir kumwambia Mtukufu Mtume ﷺ.

Sasa akiwa ameanza kutambua hekima ya ushauri aliopewa na Mtukufu Mtume ﷺ, Abu Basir aliondoka Madina na kwenda kuishi katika eneo liitwalo Is, eneo la pwani lililoko baina ya Makka na

Damascus. Ndani ya muda mfupi, eneo hili la Is lilibadilika kuwa ukanda usiokuwa chini ya upande wowote na kutumika kama kituo cha hifadhi kwa Waislamu wote waliokimbia mateso ya watu wa Makka. Katika kipindi kifupi mno, idadi ya Waislamu, ikiwa ni pamoja na Abu Jandal aliyefanikiwa kutoroka, ilifikia watu mia tatu, na hivyo kuhatarisha njia ya muhimu ya misafara ya kibiashara ya Maqurayshi wa Makka kwenda Syria, na kusababisha hasara kubwa kwa biashara ya Maqurayshi. Washirikina wa Makka hawakuwa na njia nyingine zaidi ya kumsisitizia Mtukufu Mtume ﷺ atengue sharti husika la mkataba. Na sasa walimtaka Mtume ﷺ akubali Waislamu wakimbilie Madina. Hivyo, kipengele ambacho hapo mwanzo kilionekana kuwa tatizo kwa Waislamu sasa kikaonekana kuwa tofauti kabisa na mawazo hayo ya mwanzo.[216]

Kufuatia maombi hayo, Mtukufu Mtume ﷺ alituma barua kwenda kwa jamii ya watu wa Is iliyokuwa ikiongozwa na Abu Basir. Wakati huo, Abu Basir alikuwa kwenye kitanda cha mauti na alipomaliza kusoma barua hiyo akavuta pumzi yake ya mwisho na kufariki dunia. Abu Jandal alimzika mahali alipofia na kujenga msikiti jirani na kaburi lake, kisha akawaongoza Waislamu wenzake kuelekea Madina, kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ.[217]

Mazingira ya amani yaliyotengenezwa kupitia mkataba wa amani wa Hudaybiyyah, mkataba ambao Mwenyezi Mungu ameuelezea kama 'ushindi wa wazi' *(fathan mubinan)* ulithibitika kuwa nguzo muhimu sana ya kusambaa kwa ujumbe wa Uislamu.[218]

216. Tazama: Bukhari, Shurut, 15; Ibn Hisham, III, 372.
217. Tazama: Waqidi, II, 629.
218. al-Fath, 1.

Pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipotangaza kuwa Hudaybiyyah ni ushindi mkubwa, Swahaba mmoja alisema: "Tulizuiwa kuitembelea Kaabah, tukazuiwa kutoa kuchinja wanyama wetu wa sadaka ndani ya Haram, na zaidi tukawakabidhi watu wawili waliokuwa wakihitaji hifadhi... huu waweza kuwa ushindi wa aina gani?"

Mtukufu Mtume ﷺ aliyasikia vizuri maneno haya, ndipo alipoelezea asili ya ushindi uliopatikana Hudaybiyyah:

"Kwa hakika, mkataba huu ni ushindi mkubwa. Waabudu masanamu wamekubali kuja, kuingia katika ardhi zao, kutekeleza ibada zenu na nyinyi kuwa salama mnapokuja na kurudi. Sasa watajionea na kujifunza kwenu Uislamu ambao wamekuwa wakiupinga na kuupiga vita. Mwenyezi Mungu Mtukufu atawapa ushindi na mtarudi nyumbani mkiwa mmefaidika, mkiwa safi na salama... na huo ndio mshindi mkubwa kabisa!" (Halabi, II, 715)

Abu Bakr ؓ alizua gumzo kutokana na maoni yake juu ya mkataba huo wa amani pindi aliposema kuwa: "Uislamu haujawahi kupata ushindi mkubwa kuliko ule wa Hudaybiyah. Lakini wengi ambao hawakufahamu kwa kina maneno yake hayo na wenye akili finyu, walimpinga. Watu ni wenye haraka katika mambo ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Lakini, Mwenyezi Mungu Mtukufu hana haraka na hafanyi kitu mpaka wakati wake sahihi ufike." (Waqidi, II, 610; Halabi, II, 721)

Matokeo ya kwanza chanya yaliyotokana na mkataba huo ni kuenea Uislamu kwa kasi.Maeneo mengi ambayo hapo mwanzo yalikuwa yamezuiwa, sasa yakawa wazi kwa ajili ya Ujumbe huo. Sasa Waislamu waliweza kukutana na waabudu masanamu na kuzungumza nao waziwazi na kuwaalika kuingia kwenye Uislamu.

Hata wale walokuwa wakiificha imani yao ya Uislamu kwa hofu sasa waliweza kuidhihirisha bila hofu yoyote.[219]

Lakini, kabla ya mkataba huo, makundi haya mawili hayakuweza kuingiliana kwa uhuru, achilia mbali kusafiri kwa uhuru kutoka Makka au Madina kama walivyofanya baada ya mkataba huo wa amani. Sasa, pande zote mbili, Waislamu na Washirikina walikuwa na uhuru wa kutembelea familia na marafiki kutoka pande zote mbili. *Akhalaq* za Mtukufu Mtume ﷺ, mwenendo na maadili yake yake, pamoja na miujiza yake sasa vilikuwa vikionekana wazi mbele ya Maquraysh; na kutokana na mawaidha mazito yaliyokuwa yakitolewa na Waislamu, sasa waabudu masanamu wakajikuta wakiegemea upande wa Uislamu. Mbali na hayo, Waarabu wa jangwani walikuwa wakiwasubiri watu wa Makka waingie katika Uislamu nao wapate kufuata.Ni katika kipindi hiki ambapo watu mashuhuri wa Makka kaama vile Amr ibn As, Khalid ibn Walid na Othman ibn Talha waliingia katika Uislamu.[220]

Wajumbe wa Kiislamu walikuwa na uhuru wa kutembelea eneo lolote walitakalo na kuuzungumzia Uislamu kwa kila fusra iliyopatikana. Idadi ya Waislamu ikaongezeka sana katika kipindi hiki cha mkataba wa amani.

Katika kuzidurusu ahadith husika za Mtukufu Mtume ﷺ, Imam Zuhr anatoa tathmini athari mbalimbali ziliotokana na Mkataba wa amani wa Hudaybiyyah:

"Hapo mwanzo, Waislamu na Makafiri walikuwa wakipambana kila wanapokutana. Baada ya Mkataba wa Hudaybiyya, mapigano yalifikia kikomo. Pingu za uaminifu zikaasisiwa baina ya pande mbili. Waliweza kukutana na kuchanganyikana, na hata kusaidiana

219. Tazama, Ibn Qayyim, III, 309-310.

220. See, Waqidi, II, 624.

katika mambo mbalimbali. Wakati huo huo, mtu alipokuwa akitangaziwa Uislamu, baada ya kutafakari, alikuwa akiukubali ukweli na kusilimu. Miaka miwili ya kati ya Hudayibiyya na Ufunguzi wa Makka ilishuhudia idadi kubwa ya watu wakiingia katika Uislamu kwa wingi kuliko kipindi chote cha miaka kumi na tisa cha Da'wah mpaka wakati wa Mkataba huo."

Ibn Hisham anaongezea akisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikwenda Hudaybiyyah akiwa na Waislamu elfu moja na mia nne. Miaka miwili baadaye, alienda Makka akiwa na Waislamu elfu kumi, na kwa mujibu wa maelezo mengine, watu wengine elfu mbili waliungana naye njiani, na hivyo idadi yao kufikia watu elfu kumi na mbili. Takwimu hizi zinaonesha kiwango kikubwa cha usahihi wa maelezo ya Imam Zuhri." (Haythami, VI, 170; Ibn Hisham, III, 372)

MWAKA WA SABA WA HIJRA

Kuwalingania Wafalme Mbalimbali Kwenye Uislamu

Kufuatia Mkataba wa Amani wa Hudaybiyyah, Mtukufu Mtume ﷺ mtume aliyetumwa kwa watu wote, alianza kuyalingania mataifa ya karibu na yale ya mbali kuingia katika Uislamu. Hiyo ndiyo iliyokuwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي
لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ

"Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi." (al-Araf: 158)

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ وَإِن لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ
رِسَالَتَهُ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ

"Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu." (al-Maida: 67)

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

"Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui." (Surat Sabaa: 28)

Mtume ﷺ aliwalingania watu hawa kuingia kwenye Uislamu kwa kuwaandikia barua mbalimbali, ambazo zilizo maarufu zaidi ni barua sita au nane. Kila barua ilikabidhiwa kwa Swahaba maarufu. Pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipotaka ziandikwe barua kwenda kwa mataifa mbalimbali, Maswahaba wakasema:

"Ewe Mtume wa Allah! Hawatazisoma mpaka ziwe na mhuri." Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na pete ya fedha iliyokuwa imechorwa juu yake maneno ya *'Muhammad Rasuulullah'* kwa mistari mitatu ya wima. Hivyo akaitumia pete hiyo kama mhuri rasmi.[221] Pete hiyo ilikuwa imechorwa neno *'Muhammadun Rasulullah'*, lakini kwa sababu ya hadhi na heshima ya jina la Mwenyezi Mungu, jina hilo likawekwa juu kwenye msitari wa kwanza, likifuatiwa na neno *Rasul* na kisha chini kabisala likaja neno *Muhammad*.

Dihyat'ul-Kalbi رضي الله عنه alichukua barua ya Mtume ﷺ kwenda kwa Heraclius, Mtemi wa Rumi. Wakati barua hiyo ilipomfikia, Heraclius alikuwa Syria akiwa amerejea kutoka katika vita vilivyompatia ushindi dhidi ya Waajemi. Alipoipokea, Mtemi huyo hakukuudhika wala kukereka kama ilivyokuwa kwa wafalme wengine wenye kujivuna. Kinyume chake, barua hiyo ilimpa hamu kubwa na kutaka kujua zaidi kuhusu asili na msingi wa ujumbe huo. Akaamuru atafutwe mtu anayeishi katika mji wa Mtume ﷺ na aletwe mbele yake ili aweze kumuuliza yeye mwenyewe.

Bahati nzuri Abu Sufyan, ambaye wakati huo alikuwa adui mkubwa wa Mtukufu Mtume ﷺ, alikuwa mjini Damascus akwa kama kiongozi wa kundi la wafanyabiashara wa Makka. Wakati huo,

221. Tazama: Bukhari, Ilm, 7; Muslim, Libâs, 57, 58; Ibn Saad, I, 258.

Mkataba wa amani wa Hudaybiyya ulikuwa ukiendelea kutekelezwa. Walisindikizwa na askari wa Mtemi huyo kwenda mbele yake. Pindi watu hao walipopelekwa kwake, Heraclius, akiambatana na wasaidizi wake, alikuwa katika eneo la Ilia, katika viunga vya mji wa al-Aqsa. Akiwa amezungukwa Wakubwa wa Kigiriki, Mtemi huyo aliwapokea watu hao na kuagiza aletwe mkalimani ambaye atatafsiri maneno yake na yale ya Maqurayshi.

"Kati yenu ni nani ambaye ni jamaa wa karbu wa mtu huyu anayesema kuwa yeye ni mtume?" alisema Mtemi huyo kupitia kwa mkalimani.

"Mimi", alisema Abu Sufyan.

"Mleteni yeye na jamaa zake karibu zaidi nami; lakini ninapozungumza naye, wenzake hawa wawe nyuma yake kwa hatua moja", aliamuru Heraclius. Kisha alimgeukia mkalimani wake na kusema: "Waambie wenzake kuwa nitawauliza masuali kadhaa kuhusu mtu huyu. Kama akianza kuzungumza uongo, waambie wanipe ishara."

Kwa kweli, Abu Sufyan alikiri baadaye kuwa: "Kwa kweli, lau isingekuwa kujisikia vibaya juu ya namna wenzangu wangesema hapa na pale kuhusu uongo ambao ningeusema, ningezungumza uongo kumhusu!" Yaliyotokea katika makutano hayo yanasimuliwa na Abu Sufyan mwenyewe:

"Swali la kwanza nililoulizwa na Mtemi huyo ni: 'Nasaba yake iko vipi?'

'Ana nasaba tukufu miongoni mwetu!' Nilijibu.

'Je kuna mtu kabla yake aliyedai utume?'

'Hapana', nilijibu.

'Je kuna mfalme yeyote katika wahenga wake?'

'Hapana.'

'Wale wanaomfuata...je wanatokana na tabaka la juu au watu wa chini?'

'Wanatokana na mataba ya chini', nilijibu.

'Je idadi yao inaongezeka au kushuka?' aliuliza Heraclius.

'Wanaongezeka...' nilijibu.

'Je katika wale walioikubali dini yake, kuna aliyeritadi kwa hiari yake?'

'Hapana!'

'Je mmeshawahi kumtuhumu kwa uongo kabla ya kudai kuwa mtume?'

'Hapana!'

'Je kuna siku ambayo hakutekeleza ahadi yake?'

'Hapana, kila analoahidi hulitekeleza. Lakini kwa sasa tumefanya naye makubaliano ya amani. Hatujui atakavyofanya katika kipindi hiki', nilisema. Sikuwa na maneno mengine ya kumhakiri zaidi ya haya!

Heraclius akauliza tena: 'Je mmeshawahi kupigana naye vita?'

Nikajibu: 'Ndiyo.'

'Matokeo yalikuwaje?'

'Wakati fulani hutushinda, na wakati mwengine tunamshinda!'

'Sawa, anakuamrisheni kufanya nini?'

'Anatuamrisha kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee na tusimshirikishe na yeyote na tuyaache masanamu ya wahenga wetu.

Anatuamrisha kuswali, kuwa waaminifu, kuamiliana vyema na jamaa zetu na kuwajali.'

Kisha Mtemi huyo akamwambia mkalimani wake vitu fulani, ambapo alitutafsiria:

"Mwambie...Nilikuuliza kuhusu nasaba yake ukanambia kuwa ana nasaba tukufu kabisa miongoni mwenu. Hao ni mitume. Wanatokana na nasaba tukufu kabisa katika kaumu zao.

Nilikuuliza kama kuna yeyote kabla yake aliyewahi kuwa na madai kama yake. Umenambia kuwa hakuna. Kama angekuwepo, ningesema kuwa anamuiga.

Nilikuuliza iwapo kulikuwa na mfalme katika wahenga wake na ukanambia kuwa hapakuwahi kuwa mfalme kati yao. Kama angekuwepo, ningesema kuwa anajaribu kutaka kurejesha na kudai mamlaka ya mfalme huyo kutoka katika familia yake.

Nilikuuliza iwapo mmeshawahi kumuona akisema uongo kabla ya kuja na dai hii na ukajibu kuwa hakuwahi kufanya hivyo. Mimi mwenyewe ninajua kuwa mtu ambaye hawaongopei watu kamwe hawezi kumsingizia Mungu!

Niliuliza iwapo wafuasi wake wengi wanatokana na tabaka la juu au la chini. Ukasema kuwa wanatokana na tabaka la chini. Watu hao ndio ambao huanza kuwafuata mitume.

Nilikuuliza iwapo wanaongezeka au wanapungua. Ulisema kuwa wanaongezeka. Hizo ni sifa za dini ya kweli kwa maana wafuasi wake huendelea kuongezeka.

Niliuliza iwapo kuna aliyeikimbia dini yake baada ya kuikubali nawe ukasema hakuna. Hilo ndilo linalotokea pindi imani inapotandaza mizizi yake moyoni na kuisimika.

Niliuliza iwapo kuna wakati alishindwa kutekeleza ahadi yake; ukasema hapana. Hao ni mitume. Kamwe hawakhalifu ahadi zao.

Nilikuuliza iwapo mmewahi kupigana vita. Ukasema mmeshawahi kupigana naye na wakati fulani mlishindwa na wakati mwingine mlishinda. Katika hali yoyote ile, mitume wako hivyo. Hupitia katika majaribu na mitihani mbalimbali lakini hatimaye wao ndio hushinda.

Nilikuuliza anakulinganieni kufanya nini. Ukasema kuwa anawalingania kumuabudu Mungu bila kumfanyia washirika, kuacha kuabudu masanamu; na anakuamrisheni kuswali, kuwa waaminifu na muamala mwema.

Kama uliyoyasema ni ya kweli, basi muda si mrefu mtu huyu atatawala hata kwenye ardhi hii niliyosimama. Aidha, nilikuwa na taarifa juu ya ujio wa Mtume huyu, lakini sikujua kama atatokana nanyi. Lau ningejua ningefika mbele yake, ningesafiri, nikavumilia shida na tabu za safari ili tu kumuona. Kama ningekuwa mbele yake, ningeiosha miguu yake."

Kisha Heraclius alitaka barua aliyotumiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Barua hiyo iliwasilishwa na Dihya ﷺ kwa gavana wa Busra, ambaye naye aliituma kwa Mtemi huyo. Ilisema:

"Kutoka kwa Mja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Muhammad, kwenda kwa Heraclius, kiongozi wa Warumi,

Amani iwe juu ya wale wenye kufuata uongofu! Ninakulingania kuingia katika Uislamu. Ingia katika Uislamu ili upate kuokolewa; na Mwenyezi Mungu atakulipa mara dufu! Iwapo utageuka, basi dhambi zote za wakulima wako (ambao ni raia wako).

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْاْ إِلَى كَلَمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَاوَبَيْنَكُمْ أَلاَّ نَعْبُدَ إِلاَّ اللَّهَ وَلاَ نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلاَ يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضاً أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْاْفَقُولُواْ اشْهَدُواْ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ

'Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.' (Al-i Imran: 64)

Abu Sufyan anasimulia kilichoendelea:

"Baada ya Heraclius kumaliza kuzungumza na barua kusomwa, palizuka ghasia kubwa; sauti zilipazwa kutoka kila kona. Hapo wakatupeleka nje. Tulipofika nje nikawaambia wenzangu: 'Umaarufu wa mwana wa Kabsha[222] umevuka kiwango...hata Mfalme wa Banu Asfar[223] (Heraclius) anamuogopa!' Ni katika kipindi hicho ambapo niliimarisha imani thabiti juu ya ushindi wake usioepukika...na hatimaye Mwenyezi Mungu Mtukufu akaniongoza."

Kisha Heraclius aliwaita viongozi wa serikali yake. Wote walikusanyika katika kasri la Mtemi.

"Enyi Wabyzantine...mnaonaje iwapo mtapata wokovu wa milele na mamlaka?" Mtemi huyo aliwaambia, huku akiwaita waziwazi kuingia kwenye Uislamu. Lakini, wakiwa kama punda mwitu aliyefurushwa, wote walikimbia kuelekea kwenye milango

222. Jina Abu Kaabshah lilikuwa likitumika kwa ajili ya Mtukufu Mtume ﷺ. Rejea Juzuu 1, Uk. 164.

223. Banu Asfar, kilugha ina maana ya watu wenye rangi ya Manjano. Ndilo jina lililotumiwana Waarabu kwa Warumi.

ya kutokea, lakini ikawa imefungwa. Alipoona kuwa viongozi hao wa serikali yake hawako tayari kukubali wito wa Uislamu, Heraclius aliwaita kwa upole na kufuta kauli yake ya mwanzo, akasema:

"Nilikuwa tu najaribu msimamo na utii wenu juu ya Ukristo... nami ninapenda kile ninachokiona!" Baada ya kuhakikishiwa, viongozi hao wakainama mbele yake kuonesha shukrani zao kwake. (Bukhari, Bad'ul-Wahy 1, 5-6, Iman, 37, Shahadat, 28, Jihad, 102; Muslim, Jihad, 74; Ahmad, I, 262)

Mtemi huyo aliruhusu nadhari za kidunia zimshawishi, na hivyo akaikana neema ya Uislamu, licha ya kupima na kuuelewa ukweli. Baada ya kuwa amefika kwenye mlango wa neema za milele, akageuka na kurudi nyuma.

Barua nyingine kama hiyo ilipelekwa na Abdullah ibn Huzafah ﷺ kwa mfalme wa Fursi, Khosro, ambaye radiamali yake ilikuwa kali sana kuliko ile ya Heraclius. Akiwa amekasirishwa mno na kitendo cha jina lake kuandikwa chini ya jina la Mtukufu Mtume ﷺ, haraka sana akaichanachana barua hiyo na kumtupia mjumbe maneno mazito na kashfa za matusi.

Abdullah ﷺ aliendelea kuwa mtulivu, akatamka maneno yafuatayo kumwambia Khosro na viongozi wenzake:

"Enyi Wafursi, mnaishi siku zenye kuhesabaika bila Mtume, Kitabu na mkiwa mnatawala sehemu ndogo sana ya aradhi...Mnaishi katika ndoto ya mpito! Sehemu ya ardhi mnayoitawala haina tena ushawishi wowote tena.

Ewe Khosro, wafalme wengi walikuja kabla yako, na kutawala kwa kutaka dunia au Akhera. Wale waliotaka Akhera, pamoja na

kuipata, lakini pia wamepata fungu lao la dunia. Ama wale waliotaka dunia, walipoteza fungu lao la Akhera.Vyovyote utavyokipuuza kile tunachokushauri, lakini naapa kwa Mwenyezi Mungu, popote utakapokuwa, pindi hiki unachokipuuza kitakapokujia, utafungwa ndani ya khofu na hutaweza hata kujilinda na kujitetea!"

Khosro hakubadili mawazo yake na kwa kiburi akajigamba kuonesha kuwa ufalme ni sehemu yake na ni maisha yake, na kwamba kushindwa au kuibuka kwa mpinzani kusingeweza kuingiza hofu ndani ya moyo wake. (Suhayli, VI, 589-590) Kisha aliwaamuru walinzi wake wampeleke Abdullah ﷺ nje ya kasri lake.

Abdullah ibn Huzafah ﷺ hakupoteza muda akampanda farasi wake na kurudi Madina huku akiwaza: "Wallah, sitahofu chochote ambacho kitakachonipata (kurudi Madina au kifo), kwa maana nimetekeleza jukumu langu la kufikisha barua ya Mtume ﷺ." (Ahmad, I, 305; Ibn Sad, I, 260, IV, 189; Ibn Kathir, al-Bidaya, IV, 263-6; Hamidullah, al-Wasaiq, p. 140)

Kuna tukio jingine linalomhusu Abdulillah ibn Huzafah ﷺ linaloonesha ubora na ujasiri wake:

Katika zama za ukhalifa wa Omar ﷺ, Abdullah ibn Huzafah ﷺ alikuwa sehemu ya jeshi la Kiislamu lililokwenda Syria, kwenye mkoa wa Kaysariyya, kukabiliana na Wabyzantine (Warumi), ambapo alikamatwa kama mateka. Maafisa wa Kirumi, kwa kumuona kuwa ni mateka maalumu, walimpeleka mbele ya Mfalme wao, wakasema kuwa ni "...Swahaba wa Mtume!"

Mfalme huyo alitoa amri ya Abdullah ﷺ kufungiwa katika nyumba maalumu ambapo alinyimwa chakula na maji. Baadaye Swahaba huyo alitumiwa mvinyo na nyama ya nguruwe. Walimchunguza Abdulah ﷺ kwa siku tatu mpaka mwisho; lakini hakuweka mkono wake kwenye mvinyo huo wala nyama ya nguruwe.

"Sasa ameanza kuhangaika", askari walimwambia mfalme. "Usipomtoa atafariki dunia!"

Mfalme aliamuru Abdullah ؓ aletwe mbele yake.

"Kitu gani kinakuzuia kula na kunywa kile nilichokutumia?" aliuliza.

Swahaba huyo akajibu: "Ingawa dharura inaniruhusu kula na kunywa kile ulichonitumia, lakini sikutaka kugeuka mimi au Uislamu kuwa kichekesho kwako!"

Mfalme alivutiwa sana na msimamo wa Abdullah ؓ, akamwambia atamuozesha binti yake, na zaidi ya hapo, atampa ugavana, kwa sharti abadili dini na kuwa Mkristo.

Abdullah ؓ akajibu: "Hata kama ungenipa utawala wako na ardhi zote za Arabia ili niiache dini ya Muhammad ﷺ kwa muda wa kupepesa jicho, sitaweza kufanya hivyo!"

"Basi nitakuua!" Mfalme alimtisha.

"Hilo ni uamuzi wako!" alisema Abdullah ؓ.

Kufuatia msimamo wake, Swahaba huyo mtukufu akawekwa juu ya mti kwa ajili ya kunyongwa. Kwa makusudi, watupa mshale walilenga kwa mishale, lakini wakamkosa, kwa sababu walikuwa wamepewa amri ya kumtisha kidogo. Kisha akapewa fursa ya mwisho aukane Uislamu lakini Swahaba huyo mtukufu alikataa.

"Ima uingie katika Ukristo au nitakutupa katika sufuria inayochemka!" Mfalme alisema kwa sauti ya juu kutokea mbali. Abdullah ؓ alipokataa, sufuria ya shaba ililetwa ikiwa imejaa mafuta ya mzaituni na maji, kisha yakachemshwa. Mtemi huyo aliagizwa aletwe mateka mwingine wa Kiislamu, ambaye alimpa fursa ya mwisho kama alivyofanya kwa Abdullah ؓ. Naye akakataa, akatupwa moja kwa moja katika chungu hicho cha shaba, mbele ya macho ya

Abdullah ﷺ. Mwili wake ulisambaratika mara moja ndani ya mafuta makali yenye kuchemka, akafa kifo kitukufu zaidi kuliko vifo vyote.

Mtemi alirudia maneno yake kwa Abdullah ﷺ. Lakini, kwa mara nyingine, alikataa. Hivyo, akatoa amri ya kutupwa ndani ya chungu cha mafuta. Kabla hajatupwa, Abdullah ﷺ alianza kudondosha machozi. Mfalme akadhani kuwa Swahaba huyo amebadili moyo wake, akaagiza aletwe mbele yake. Aliporudia tena kumtaka abadilike, alikataliwa kwa hasira.

"Sasa kwa nini ulilia?" aliuliza Mtemi kwa mshangao, ambapo Abdullah ibn Huzafah alitoa jibu la kihistoria:

"Usidhani kuwa nimelia kwa sababu ya kuogopa kile unachotaka kunifanyia. Nimelia kwa sababu nina roho moja tu ya kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Niliwaza mwenyewe, 'Kwa sasa una roho moja, ambayo inakaribia kutupwa ndani ya chungu cha mafuta, na utakufa mara moja katika njia ya Mwenyezi Mungu. Lakini ninatamani lau kama ningekuwa na roho nyingi kama nywele kwenye mwili wangu ili nizitoa katika njai ya Mwenyezi Mungu, niteswe tena na tena katika njia Yake.'"

Msimamo wa ajabu uliooneshwa na Abdullah ﷺ pamoja na taadhima na heshima ya imani, vilimuathiri sana Mtemi na kutaka kumuacha huru:

"Basi libusu paji la uso wangu nitakuacha uende", alisema.

Swahaba akauliza: "Nikifanya hivyo utawaachia huru mateka wengine wote wa Kiislamu waondoke pamoja nami?"

"Ndiyo", alisema Mtemi. "Nitawaacha huru!"

Abdullah ﷺ anahadithia kuwa: "Wakati huo niliwaza kama kulikuwa na madhara gani kwa kulibusu paji la uso wa adui wa

Mwenyezi Mungu kwa malipo ya kujiokoa mimi mwenyewe na hata mateka wengine Waislamu?"

Siku hiyo, mateka themanini wa Kiislamu waliachiwa huru. Waliporejea Madina walimhadithia Khalifa Omar ؓ juu ya tabu na shida walizokumbana nazo.

"Kulibusu paji la uso wa Abdullah ni wajibu kwa Waislamu wote nami nitakuwa wa kwanza kutekeleza wajibu huo", alisema Omar ؓ na kusimama kwenda kulibusu paji la uso wa Abdullah ؓ. (Ibn Athir, Usd'ul- Ghabah, III, 212-213; Dhahabi, Siyar, II, 14-15)

Hivyo, Swahaba mwenye ujasiri kama Abdullah ibn Huzafah ؓ ndiye aliyetakiwa kufikisha barua ya Mtukufu Mtume ﷺ kwa Khosro wa Fursi; kuwa na ujasiri wa kumhutubia ndani ya kasri la kifalme, akiwa amezungukwa na walinzi wenye miraba minne wanaosubiri ishara ndogo tu kutoka kwa Mtemi wao wapate kummaliza.

Mtukufu Mtume ﷺ aliposikia kuwa Khosro aliichana barua yake na kutoa maneno makali, alisema: "Allah auchanechane utawala wake!" (Bukhari, Ilim, 7; Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, III, 212)

Haukupita muda mrefu, muujiza wa dua hiyo ya Mtume ﷺ ukatokea. Katika kipindi cha *Khulafaur-Raashidun,* yaani Makhalifa Walioongoka, himaya yote ya Fursi ikawa chini ya Wasialmu.

Khosro alienda mbali zaidi, alituma barua kwenda kwa Bazan, Gavana wa Yemen, akimtaka amlete Mtume ﷺ mbele yake. Kwa sababu hiyo, ujumbe wa Bazan uliwasili kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumkabidhi barua ya Khosro. Baada ya kusomewa barua hiyo, Mtume wa Allah ﷺ alitabasamu. Kisha akawalingania wajumbe hao kuingia katika Uislamu. Wajumbe walimuomba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama hakutaka kuandamana nao angalau basi aandike jibu la barua ya Khosro. Kutokana na wahyi aliokuwa ameupokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu, akawaambia:

"Mwenyezi Mungu amemsalitisha Khosro kwa mwanaye Shirawahy. Shirawayh amemuua katika mwezi fulani, siku fulani na siku hiyo ni usiku wa jana!"

Wajumbe hao walishtuka sana. Wakauliza: "Tuandike ulichotuambia na tumtaarifu Gavana?"

Mtume wa Mwenyezi Mungu akawajibu: "Ndiyo! Mpeni taarifa Gavana juu ya mlichokisikia na vilevile mwambieni kuwa dini na himaya yangu vitavuka mipaka ya himaya na ufalme wa Khosro na kufika maeneo ya mbali kabisa kufikiwa na nyayo za farasi na ngamia. Mwambieni pia kwamba: Akiingia katika Uislamu, atapewa ardhi zilizo chini ya ugavana wake na kufanya kuwa mfalme wa kabila lake (Wafursi wanaoishi Yemen)!"

Maneno ya Mtukufu Mtume ﷺ yalipowasilishwa kwa Bazan, alisema: "Ninaapa, hakika maneno haya si maneno ya wafalme. Ninaamini mtu huyu ni Mtume kama anavyosema! Vyovyote itakavyokuwa, ngoja tusubiri matokeo ya kile alichosema kuhusu Khosro. Kama ni kweli, basi ni mtume aliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa watu. Kama hayatakuwa kweli basi tutaamua hatua za kuchukua!"

"Mlimuonaje?" Bazan aliwauliza wajumbe wake.

"Hatujawahi kumuona mtawala mwenye ukuu lakini mnyenyekevu asiyekhofu chochote, licha ya kutokuwa na walinzi wanaomlinda; ambaye hutembea kwa miguu kama watu wa kawaida! Wafuasi wake hawanyanyui sauti zao mbele yake na huzungumza kwa sauti laini..." walimwambia Bazana na kuendelea kumpa taarifa juu ya walichokiona.

Hawakulazimika kusubiri muda mrefu kuwasili kwa barua ya kifalme kuelezea kuwa Shirawahy alikuwa amemuua baba yake. Zaidi ya hivyo, muda wa kifo cha Khosro uliendana kabisa na

muda ulioelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Gavana Bazan akasema: "Kwa hakika, mtu huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu!" Kabila la Abna, watu wa asili ya Fursi waishio Yemen, walimfuata gavana wao, wakaingia katika Uislamu. (Ibn Sad, I, 260; Abu Nuaym, Dalail, II, 349-350; Diyarbakri, II, 35-37)

Mfalme Najjashi wa Abyssinia alionesha ukarimu wa hali ya juu kabisa kwa kuipokea barua ya Mtukufu Mtume ﷺ na kwa mjumbe aliyeiwasilisha, Amr ibn Umayyah رضي الله عنه. Pamoja na wito na ujumbe wa wazi wa kumlingania kwenye Uislamu, barua iliyotumwa kwa Najjashi pia ilikuwa na taarifa na maelezo mafupi kuhusu Bibi Maryamu na Nabii Isa عليه السلام. Akiwa ameshajifunza Uislamu kwa kiasi fulani kutoka kwa Waislamu ambao awali walihamia Abyssinia na akiwa amechukua hatua ya ujasiri ya kuupokea tokea mwanzo, Najjashi aliishikilia ndege ielekeayo kwenye anga ya *iman* baada ya kupokea barua rasmi ya kumuita kwenye Uislamu. Alitangaza imani yake mbele ya Ja'far رضي الله عنه, mtoto mkubwa wa Abu Talib, ambaye wakati huo alikuwa pamoja naye. Kisha katika kutekeleza maelekezo ya Mtukufu Mtume ﷺ, aliwapakia kwenye majahazi mawili wahamiaji wa Kiislamu na kuwavusha upande wa pili wa Bahari Nyekundu. Vilevile alimtumia Mtukufu Mtume ﷺ barua yake mwenyewe, akieleza wazi kuwa ameshaingia katika Uislamu. Ilisema:

"Kwa Muhammad ﷺ, Mtume wa Mwenyezi Mungu, kutoka kwa Najjashi,

Amani, rehma na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu, ambaye hakuna mungu ila Yeye, ameniongoza kwenye Uislamu.

Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu...! Nimepokea barua yako ambayo ndani yake umeelezea hali ya Isa عليه السلام. Naapa kwa Mola wa Mbingu na Ardhi, hakika ulichosema kumhusu ndicho hicho hicho alichokisema yeye. Ujumbe wake ulikuwa kama usemavyo. Tumejifunza misingi ya Uislamu ambao umepewa kazi ya kuutangaza. Tumempa hifadhi binamu yako (Jafar) pamoja na wenzake waliohamia katika ardhi yetu. Ninashuhudia kwamba wewe ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Maneno yako ni ya kweli. Wewe ni mkweli na mwenye kusadikishwa.

Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nimekula kiapo cha utii kwako kupitia kwa binamu yako, mwakilishi wako. Nimejisalimisha kwa Mola wa Ulimwengu mbele yake. Ninamtuma kwako mwanangu Arha. Sina mamlaka juu ya chochote zaidi ya nafsi yangu; na iwapo utataka nije kwako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nitafanya hivyo mara moja. Ninashuhudia kwamba unachosema ni kweli. Amani iwe juu yako, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu..."
(Ibn Sad, I, 259; Ibn Qayyim, III, 689; Hamidullah, al-Wasaiq, p. 100, 104-105)

Katika siku hizo hizo, Mtukufu Mtume ﷺ alitaka mtu atakayejitolea "kupeleka barua kwa Muqawqis[224] wa Alexandria, kwa kutarajia malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu", ambapo Khatib ibn Abi Baltaah رضي الله عنه alijitokeza mara moja na kujitolea kupeleka barua hiyo.

224. Watawala mbalimbali walikuwa wakijulikana kwa majina ya jumla kutokana na maeneo yao. Jina lililokuwa likitumika kwa Mfalme wa Wabyzantine (Warumi) ni Kaysar, mtawala wa Fursi (Uajemi) Khosrau, mfalme wa Abyssinia Najjashi na Yule wa Misri akijulikana kama Fir'auni; vivyo hivyo gavana wa Alexandria alijulikana kama Muqawqis, mfalme wa India akijulikana kama Batlimus and Yule wa Yemen akijulikana kama Tubba. Haya ni majina ya jumla, sio majina yao makhsusi. (Ibn Kathir, al-Bidayah, XI, 228)

"Mwenyezi Mungu aifanye safari hii kuwa tukufu kwako", Mtume ﷺ alimuombea.

Khatib ﷺ aliichukua barua hiyo kwenda kwa Muqawqis wa Alexandria. Barua ilisema hivi:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu,

Kutoka kwa mja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Muhammad, kwenda kwa Muqawqis, Kiongozi wa Waqibti,

Amani iwe juu ya wale wenye kuufuata uongofu na kushikamana na njia ya haki.

Ninakualika kuingia kwenye Uislamu. Silimu nawe utapata amani ili Allah akulipe mara dufu. Iwapo hutaukubali wito huu, basi utabeba dhambi za Waqibti.

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْاْ إِلَى كَلَمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَاوَبَيْنَكُمْ أَلاَّ نَعْبُدَ إِلاَّ اللَّهَ وَلاَ نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلاَ يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضاً أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْاْفَقُولُواْ اشْهَدُواْ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ

'Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu. (al-i Imran: 64)"

Barua ya Mtume ﷺ iliposomwa, Muqawqis alimtaka Khatib ﷺ asogee karibu naye, na katika makutano hayo walikuwe viongozi wake wakubwa wa kidini. Khatib ﷺ anasimulia kilichotokea baadaye:

"Muqawqis alinambia kuwa anataka kuongea na mimi na anataka kuniuliza vitu kadhaa ambavyo alitaka kuvijua. 'Sawa...uliza', nilimwambia.

'Je bwana wako huyu si mtume?' aliuliza.

'Bila shaka...ni Mtume wa Mwenyezi Mungu', nilimjibu.

'Kama kweli ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa nini basi hakuwalaani watu wake waliomlazimisha kuhama kutoka katika mji wake wa nyumbani na kukimbilia kwengine?' aliuliza. Nilimjibu kwa kumuuliza:

'Je, waamini kuwa Isa mwana wa Maryamu alikuwa mtume wa Mwenyezi Mungu? Sasa basi, kwa nini hakumuomba Mola wake kuwaangamiza watu wake pindi walipotaka kumsulubisha, badala yake akaomba apaishwe?'

Muqawqis alikaa kimya. Baada ya ukimya mfupi, aliniambia nirudie maneno yangu. Nikafanya. Akawa kimya tena.

Kisha akasema: 'Umesema vyema. Wewe ni mtu mwenye busara ambaye hupima kile unachosema; na unatoka kwa mtu mwenye busara!' Nikiwa nimehamasika, nilizungumza yafuatayo:

'Katika nchi hii aliishi mtu mmoja kabla yenu, ambaye alidai kuwa ndiye mola mkuu. Lakini Mwenyezi Mungu alimkamata na kumuadhibu kwa adhabu nzito hapa duniani na kesho Akhera. Chukua fundisho kwa wale waliokuwa kabla yako, ili usiwe funzo kwa wengine!'[225]

Akasema: 'Tayari tuna dini na hatutaiacha mpaka tupewe kitu bora zaidi!'

225. Kuna methali nzuri isemayo: Anayeshindwa kuchukua mazingatio katika historia siku moja atakuja kuwa mazingatio kwa watakaokuja baadaye.

'Kwa hakika Uislamu ndio dini bora ambayo sasa waifuata! Tunakuita kwenye Uislamu, dini ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameichagua iwe ndio dini ya wanadamu wote. Muhammad Mustafa ﷺ hakulinganii wewe peke yako, bali pia anawalingania wanadamu wote.Watu waliomtendea ufidhuli na ukatili ni Waqurayshi wenzake. Waliomtendea fitna na shari ni Wayahudi. Na walio karibu naye zaidi, kwa upande mwingine, ni Wakristo. Kama ambavyo Musa عليه السلام alibashiri ujio wa Isa عليه السلام, naye Isa عليه السلام akabashiri na kutoa habari juu ya ujio wa Muhammad عليه السلام. Ulinganio wetu kwako kuifuata Qur'an ni kama ulinganio wenu kwa wafuasi wa Taurati kuifuata Injili. Kila mmoja ana wajibu wa kumfuata mtume wa zama zake... na nyinyi mmpo katika zama za mtume Muhammad Mustafa ﷺ. Hivyo tunapokuiteni kwenye Uislamu hatukuwekeni mbali na dini ya Isa عليه السلام. Bali tunakulinganieni na kukuiteni kuishi kulingana na mafundisho ya utume wake.'

Hapo, Muqawqis akajibu:

'Kwa kadiri nionavyo, dini ya mtume huyu haiamrishi kuipiga teke dunia wala haikatazi kuwa na vitu vizuri na halali. Haonekani kuwa mchawi wala muongo anayedai kupokea taarifa kutoka kusikojulikana. Bali amebeba alama za utume kana kwamba kuna mtu asiyejulikana ambaye alimfunulia na kumtaarifu mambo mbalimbali kabla hayajatokea. Lakini, bado ninahitaji muda zaidi ili nifikirie.'

Baadaye, aliandika majibu ya barua niliyomletea:

'Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu,

Kwenda kwa Muhammad ibn Abdillah, kutoka kwa Muqawqis,

Amani iwe juu yako! Nimesoma barua yako na nimekielewa ulichokieleza na kunilingania. Nilijua atakuja mtume lakini nilitarajia

kuwa atatokea maeneo ya Damascus. Nimemkaribisha mjumbe wako. Na sasa ninakutumia zawadi ya vijakazi wawili wanaoheshimika mno miongoni mwa Wakopti na baadhi ya mavazi; na pia ninakutumia baghala (nyumbu) utakayemtumia kwa safari. Amani iwe juu yako!'

Muqawqis hakufanya zaidi ya hapo; hakuukubali Uislamu. Wakati nikitoka, aliniambia: 'Yote yaliyotokea, usifanye Wakoptiki wasikie hata neno moja kutoka kwako!'" (Ibn Kathir, al-Bidaya, IV, 266-267; Ibn Sad, I, 260-261; Ibn Hajar, al-Isaba, III, 530-531)

Kwa kweli, Muqawqis aliupokea ujumbe wa Mtume ﷺ kwa namna ya urafiki. Alikuwa akitarajia ujio wa mtume wa mwisho, lakini matarajio yake ni kuwa mtume huyo angetokea katika viunga vya Damascus. Dhana hii iliishia kumziba akashindwa kuukubali ukweli na hatimaye Muqawqis akafa bila kusilimu. Lakini alimkabidhi Khatib ؓ zawadi ya nyumbu na vijakazi wawili, bibi Mariyah na dada yake, Sirin.

Wakati wa safari yake ya kurejea Madina, Khatib ؓ alihakikisha anawaelezea akina dada hao kuhusu Uislamu, akiwalainisha kuwa Waislamu; matokeo yake wakasilimu.[226] Waliuelewa ukweli wa milele hata kabla ya kukanyaga ardhi ya Madina.

Pindi Khatib ؓ alipofikisha maneno ya Muqawqis, Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Mkaidi huyo hakutaka kupoteza utawala wake...lakini hicho ambacho hakutaka kukipoteza hatabaki nacho." (Ibn Sad, I, 260-261; Diyarbakri, II, 38)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuozesha Sirin kwa Hasan ibn Thabit ؓ, naye akamuoa Mariyah, ambaye alimzalia mtoto wa kiume, Ibrahimu. Ndoa hii, iliyofanyika kwa Amri ya Mwenyezi Mungu, ilileta faidi nyingi za kisiasa. Hili liliacha athari ya kudumu

226. Ibn Saad, VIII, 212.

kwa Wamisri na kuchangia sana katika kuwatupa mkono Wabyzantine (Warumi) katika vita vyao dhidi ya Waislamu ambavyo vingetokea baadaye, na hivyo kuwawizesha Waislamu kupata ushindi kwa urahisi zaidi.

Mtukufu Mtume ﷺ aliwapa Maswaba wosia ufuatao, akielezea muamala bora na unaofaa kuwafanyia jamaa na ndugu:

"Mtaifungua Misri, ardhi ambayo wanatumia kipimo kiitwacho *qirat*. Ninawausia kuwatendea wema watu wake. Tekelezeni wosia wangu, kwani sisi ni ndugu zao, kwa nasaba na ndoa." (Muslim, Fadail'us-Sahabah, 226-227)

Kama tujuavyo, nasaba ya Mtume ﷺ inafika kwa Ismail عليه السلام; na kwa kuwa Hajar, mama wa Ismail عليه السلام, alitoka Misri, Mtukufu Mtume ﷺ anawachukulia Wamisri kama ndugu zake. Ama kuhusu udugu wa ndoa, unatokana na yeye kumuoa bibi Mariyah.[227]

Harith, chifu wa kabila la Kiarabu la Ghassani la Syria, alifanya ujeuri mkubwa dhidi ya barua ya Mtume ﷺ iliyowasilishwa kwake na Shuja ibn Wahb رضي الله عنه. Alienda mbali zaidi na kutaka kibali rasmi kutoka kwa Mfalme wa Rumi aende kupigana vita na Waislamu. Lakini ombi lake lilikataliwa.[228]

Hawza, kiongozi wa eneo la Yamamah, naye pia aliukataa wito wa Mtukufu Mtume ﷺ uliowasilishwa kwake na Salit ibn Umayr رضي الله عنه. Muda mfupi baadaye alikufa katikati ya ujinga wake.[229]

227. Ibn Hisham, I, 4.
228. Ibn Saad, I, 261.
229. Ibn Saad, I, 262.



		Heraclius, Mtawala wa Warumi	Ilia, Quds	Hakusilimu kwa hofu ya kupoteza ufalme wake
1	Dihya ibn Khalifah	Heraclius, Mtawala wa Warumi	Ilia, Quds	Hakusilimu kwa hofu ya kupoteza ufalme wake
2	Abdullah ibn Huzafah	Khosrau	Madain	alirarua vipande barua ya Mtume na Allah akaurarua ufalme wake
3	Amr ibn Umayyah	Najjashi	Abyssinia	Alisilimu
4	Khatib ibn Baltaa	Muqawqis	Misri	Hakusilimu, lakini alimpokea vizuri mjume wa Mtume
5	Ala ibn Hadrami	al-Munzir ibn Sawa, Mfalme wa Bahrain	Bahrain	Alisilimu
6	Salit ibn Amir	Kiongozi wa Yamamah	Yamamah	Alitaka aachiwe utume
7	Shujaa ibn Wahb	Haris al-Ghassani, Mtawala wa Waghassani	Hawran	Alitishia kuishambulia Madina
8	Muhajir ibn Umayya	al-Haris al-Khimyeri	Yemen	Alisilimu
9	Amr ibn al-As	Julandi, Mfalme wa Oman	Oman	Alisilimu

Mtukufu Mtume ﷺ alimpa wosia muhimu kila mjumbe kabla ya kumpa ujumbe wake. Kwa mfano, kabla ya kutaka barua ipelekwa kwa kabila la Khimyar, alimuusia yafuatayo mjumbe wake, Iyash ؓ:

"Ukifika huko wakati wa usiku, subiri mpaka asubuhi ndo uingie. Chukua wudhu kwa namna iliyo bora kabisa na uswali rakaa mbili. Muombe Mwenyezi Mungu akuwezeshe, kukupa mafanikio na ili upokelewe kwa furaha. Kisha jiandae, chukua barua yangu kwa mkono wako wa kuume na uiwasilishe kwa mkono wako wa kuume kwa kuwakabidhi katika mkono wao wa kuume. Iwapo utafanya hivyo, watakukubali..."

Iyash ؓ anaeleza: "Nilifanya kama nilivyousiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu. Matokeo yake ni watu hao kusilimu. Yaliyotokea baadaye pia yalitokea kama alivyoyabashiri." (Ibn Sad, I, 282-283)

Barua hizi ilikuwa hatua za mwanzo zilizoutoa Uislamu Madina na kuupeleka ulimwenguni kote. Baada ya kupata nguvu na uhai katika Peninsula ya Arabia, Uislamu uliendelea kukustawi siku hadi siku. Uzuri wa mambo ni kuwa, misingi ya muendelezo wa ushindi huo iliasisiwa na Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe.

Kutupiwa Sihiri na Mayahudi

Ni katika kipindi hicho ambapo viongozi wa Kiyahudi walimpa pendekezo mtengeneza sihri, Asam ibn Labid, ambaye kwa juu juu alionekana kuwa Muislamu, lakini kwa ndani akiwa amebeba imani ya kiyahudi kwa siri:

"Wewe ni mtengeneza sihiri wetu mahiri", walisema. "Muhammad amewafanyia sihiri wanaume na wanawake wetu na hatuwezi kufanya lolote kuhusu jambo hilo. Umeona mambo ambayo ametufanyia; namna ambavyo ameihakiri dini yetu, kuwaua na

kuwapeleka uhamishoni wengi wetu. Kwa hasara yote ambayo ametusababishia, tunakukabidhi jukumu la kumuadhibu kwa kumtupia sihiri!" Walimpa Asam ibn Labid ujira wa dinari tatu za dhahabu kwa ajili ya kazi hiyo.

Ibn Labid, haraka sana, alijiandaa kwa kazi hiyo na kuanza kutafuta njia ya kupata za Mtukufu Mtume ﷺ. Kwa kiasi fulani alifanikiwa kupata kile alichokuwa akikitafuta. Alifunga vitu kama mafundo kwenye nywele hizo na kupuliza ndani yake, akaziweka katika gamba kavu la maua ya tende. Kisha aliyaweka chini yjiwe ndani ya Kisima cha Zarwan. Baada tu ya kumaliza kutengeneza sihiri hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliumwa. Nuru ya macho yake ilififia. Maradhi hayo yaliyoendelea kwa siku kadhaa hatimaye yalimpunguzia hamu ya kula na akawa hawezi kula na kunywa chochote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfahamisha Mtume Wake mtu hasa aliyemfanyia sihiri na mahali nywele hizo zilizofungwa zilipokuwa. Hivyo Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Ali na Ammar ﷺ kwenda kwenye Kisima hicho cha Zarwan. Walitoa maji yaliyokuwa humo, ambayo yalikuwa yamebadilika rangi kama hina, na kukikausha kabisa kisma hicho. Walipotoa jiwe hilo walikuwa sihiri iliyofungwa mafundo chini yake.

Wakati huohuo, Malaika Jibril عليه السلام alileta sura mbili za al-Falaq na an-Naas. Mtume ﷺ aliposoma kila aya, fundo moja lilifunguka; na aliposoma aya ya mwisho, alihisi kupona, kana kwamba alikuwa amefunguliwa kamba. Hamu yake ya kula ilirejea. Kufuatia tukio hilo, aliamuru kisima cha Zarwan kifungwe. Ama kuhusu Ibn Labid, Mtukufu Mtume ﷺ hakumuita wala hakuutaja uhalifu wake na kumuwajibisha. Sio tu kwamba hakumuadhibu Ibn Labid, kwa kosa la kujaribu kumuua, bali pia hakufanya kisasi binafsi dhidi ya watu wa jamii ya Ibn Labid, Mayahudi wa Banu Zurayq.[230]

230. Tazama: Ibn Saad, II, 197; Bukhari, Tıbb, 47, 49; Muslim, Salâm, 43; Nasai, Tahrîm, 20; Ahmad, IV, 367, VI, 57; Aynî, XXI, 282.

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Jiepusheni na mambo saba yenye kuangamiza!"

"Ni mambo gani hayo, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" waliuliza Maswahaba.

"Kumfanyia Mwenyezi Mungu washirika, kufanya sihiri, kuua nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha kuuliwa, kujiingiza katika riba, kula mali ya yatima kwa dhulma, kukimbia medani ya vita na kumtuhumu mwanamke msafi na asiyekuwa na hatia kuwa ni mzinifu..." (Bukhari, Wasaya, 23; Muslim, Iman, 145)

Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Mwenye kufunga mafundo na kuyapulizia, atakuwa amefanya sihiri. Mwenye kufanya sihiri atakuwa ameangukia katika *shirk*." (Nasai, Tahrim, 19)

"Swala ya *arraf*[231] (mpiga ramli), anayetoa habari za mahali ilipo mali iliyoibiwa na kupotea, na anayemuuliza kitu na kukisadikisha, haitakubaliwa kwa siku arobaini." (Muslim, Salam, 125)

Pigo la Mwisho Dhidi ya Uadui wa Mayahudi: Ufunguzi wa Khaybar (Safar-Rabiulawwal, 7 / Juni-Julai, 628)

Mayahudi wa Khaybar waliungana na washirikina katika kuuhakiri Mkataba wa amani wa Hudaybiyyah na kudhani kuwa unaakisi udhaifu wa ndani wa Waislamu. Wakichochewa na Mayahudi waliofukuzwa Madina ambao walikimbilia katika ngome zao,

231. *Kahin* au kuhani, ni mtu anayedai kuwa anajua yatakayotokea. Ingawa kwa mtazamo mmoja *arraf* naye ni *kahin*, neon hilo hutumika kwa mtu anayeelezea juu ya kitu kilichoibiwa au kupotea. Kuna *munajjim* au mnajimu, ambaye naye ni *kahin*, tofauti ikiwa kwamba anadai kuwa anajua matukio ya baadaye kwa kutazama nyota.

haukupita muda, moto wa uadui ukaichukua Khaybar. Mayahudi waliwaahidi watu wa kabila la Ghatafan kuwa wangewapa nusu ya mazao yao, iwapo wataungana nao katika kuwapiga Waislamu. Ghatafan wakiwa tayari na kutoa ushirikiano wote, walifikiria namna ya kuyaingiza majeshi yao kazini. Waliandaa na kuupitisha mpango wa kutuma jeshi Madina.[232]

Katika kukabiliana na uadui huu wa Mayahudi, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma Abdullah ibn Rawaha ؓ kwenda Khaybar kufanya mazungumzo ya amani. Baada ya muda mfupi, Swahaba huyo alirudi akiwa na jibu la kukataliwa kwa wazo hilo. Vita ikawa ni jambo lisiloepukika na safari ya kwenda Khayba ikawa dhahiri. Mtukufu Mtume ﷺ akatangaza:

"Wale tu wanaotaka *jihad* ndio wataungana nasi!" (Ibn Sad, II, 92, 106)

Madina, kwa upande mwingine, ilikuwa katikati ya Makka na Madina; na hivyo, kila palipotokea vita dhidi ya upande wa Makka, Khaybar ilikuwa ikiweka tishio kubwa sana kutokea upande wa nyuma.

Kwa hamasa kubwa, Maswahaba waliitikia wito wa Mtukufu Mtume ﷺ. Hata hivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuruhusu kujiunga kwa wale ambao hawakuwepo katika tukio la Mkataba wa Hudaybiyyah. Katika matukio ya huko nyuma, jeshi la Kiislamu lilipata tabu sana, katika nyakati ngumu sana, kutokana na khiyana ya wanafiki, ambao kwa kiasi fulani walifanikiwa kupenya katika safu za jeshi wakati wa harakati za kijeshi kwa lengo pekee la kutaka ngawira. Watu hao hao sasa walitaka kuungana na jeshi kwa wingi mno, kwa matumaini ya kujipatika utajiri mkubwa wa Mayahudi

232. Tazama: Waqidi, II, 530-531, 566, 640; Ibn Saad, II, 92.

wa Khaybar. Hivyo walikataliwa. Aidha, hilo lilifanyika kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

قُل لَّن تَتَّبِعُونَا

"...Sema: Hamtatufuata kabisa!" (al-Fath: 15)

Maandalizi ya Waislamu kwa ajili ya kwenda Khaybar yalitia hofu juu ya Wayahudi waliokuwa wamebaki Madina, ambao bado walikuwa wakitekeleza mkataba waliowekeana na Mtukufu Mtume ﷺ. Walikuwa na hisia kuwa Wayahudi wenzao wa Khaybar walikuwa wakisubiri hasara kama iliyowapata wenzao wa Qaynuqa, Nadhir na Quraydha. Katika matarajio ya kuwadhoofisha Waislamu, kila Myahudi wa Madina aliyekuwa akimdai Muislamu pesa alitaka amlipe haraka. Tukio lifuatalo, pamoja na kuonyesha mabadiliko haya ya mazingira na hali, pia linaonesha umakini wa Mtukufu Mtume ﷺ katika kuchunga haki za watu wengine:

Abu Shahm, Myahudi, alikuwa akimdai Abdullah ibn Hadrad ﷺ kiasi cha dirham tano kutokana na shayiri aliyomuuzia. Pindi Abu Shahm alipomtaka amlipe deni lake, Ibn Hadrad ﷺ alimwambia: "...nipe muda kidogo. Inshaallah, nitalipa deni langu, kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuahidi Mtume Wake ngawira za Khaybar. Tunaenda kwenye mji wenye utajiri zaidi kuliko miji yote ya Hijaz!"

Maneno hayo yalichochea ghadhabu na wivu wa Myahudi huyo. Akasema: "Mnadhani kuwa Mayahudi wa Khaybar ni kama Waarabu mliopigana nao mpaka sasa? Ninaapa kwa Taurati kwamba kule kuna wapambanaji wakali elfu kumi!"

Ibn Hadrad akajibu: "Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Umesahau kuwa unaishi chini ya hifadhi yetu. Naapa kwa Mwenyezi

Mungu, nitakupeleka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu!" Akamshika kwa mkono wake na kumpeleka kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Sikia asemacho Yahudi huyu", kisha akamsimulia maneno yaliyotamkwa na Abu Sham. Mtukufu Mtume ﷺ akakaa kimya, hakusema neno lolte. Walichoweza kuona ni mtikisiko mdogo wa midomo yake lakini hawakuweza kujua alichosema.

"Ewe Abul Qasim (Mtume)! Amenifanyia dhulma, hajalipa deni langu!" alilalama Yahudi huyo.

"Mpe haki yake", alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumwambia Ibn Hadrad.

Ibn Hadrad alizuzngumzia umaskini wake na kutoa uhakika kuwa angemlipa Abu Shahm kutokana na ngawira za Khaybar. Bado Mtukufu Mtume ﷺ alirrudia amri yake kwa mara nyingine. Hapo Ibn Hadrad ؓ akaenda faragha. Aliporudi alikuwa amebeba nguo zake huku akiwa amejifunga *imamah* yake.

"Nitakuuzia nguo zangu", alisema kumwambia Yahudi, ambaye alikubali kuzinunua kwa dirham nne na kufanikiwa kulipa deni lake. (Ahmad, III, 423; Waqidi, II, 634-635)

Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiongoza jeshi la Maswahaba kuelekea Khaybar, alikuwa akijilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama afanyavyo siku zote, kupitia dua ifuatayo:

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu saba na vilivyomo, ardhi saba na vilivyomo, maibilisi na wanaowapotosha, mola wa upepo na unaovipeperusha! Tunakuomba kheri ya mji huu, wakazi wake na vile vilivyo ndani yake! Na tunajilinda kwako na shari za

mji huu, wakazi wake na vilivyomo ndani yake!"[233] (Ibn Hisham, III, 379; Waqidi, II, 642)

Njiani, Maswahaba walianza kupaza sauti za *takbir*, kwa kusema *'Allah-u Akbar Allah-u Akbar; La ilaha ill-Allah-u w-Allahu Akbar!'* Mtukufu Mtume ﷺ akawaambia: "Jihurumieni, kwa maana mnayemwambia siyo kiziwi, wala mnayemuita hayuko mbali! Mnamuita Yeye Ambaye anawaona na kuwasikia, na yupo popote mtakapokuwa. Hakika Yeye mnayemuomba, yu karibu na kila mmoja wenu kuliko hata mishipa yenu ya shingo!" (Bukhari, Daawat, 50, 67; Muslim, Dhikr, 44)

Mtukufu Mtume ﷺ aliwasili Khaybar wakati wa usiku na kusubiri mpaka kuche. Haikuwa desturi yake kufanya shambulizi lolote wakati wa usiku na mara zote alikuwa akisubiri mpaka asubuhi, ndipo anaposhambulia. Ilipofika asubuhi, Mayahudi walitoka nje ya ngome zao wakiwa na majembe na sululu zao kwa ajili ya kwenda mashambani kwao kama kawaida. Lakini walipoliona jeshi la Waislamu limeweka kambi mbele ya ngome zao, walirudi haraka wakipiga kelele: "Ni Muhammad...Muhammad na jeshi lake!"

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "*Allah Akbar*... Khaybar ni yenye kuangamia! Tutakaposhuka katika ardhi yao, asubuhi mbaya itakuwa ya wale walioonywa!" (Bukhari, Maghazi, 38; Ibn Hisham, III, 380)

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ aliweka kambi yake katika eneo la Raj, katikati ya Ghatafan na Khaybar, na hivyo kukata mawasiliano ya washirika wawili na kuzuia mipango yao ya kuasaidiana. Ghatafan walipojaribu kuwasaidia Mayahudi pindi walipowaomba usaidizi, hawakuwa na chaguo lingine ila kurudi, wakiwa na khofu, baada ya Waislamu wameziba njia yao. Maya-

233. Hii ni dua iliyokuwa ikiombwa na Mtukufu Mtume ﷺ kila anapoingia katika mji fulani, pindi anapoyaona makazi kwa mbali. (Hakim, I, 614/1634)

hudi wa Khaybar walipolazimika kupambana na Waislamu wakiwa peke yao (bila msaada wa washirika wao wa Ghatafan), walikimbilia katika ngome zao.

Wakati mazingiro (uliofanywa na jeshi la Waislamu kwenye ngome za Khaybar), mtu mmoja alieneza uvumi kati ya Mayahudi ili kuwahamasisha kupambana na Waislamu, kama ilivyoashiriwa na Mtukufu Mtume ﷺ:

"Ibilisi aliwaendea Mayahudi na kusema, 'Muhammad anakupigeni kwa lengo tu la kutwaa mali zenu!' Waambie, 'Semeni *La ilaha ill-Allah* na hivyo mtakuwa mmeilinda mali na damu yenu... na kuhusu hali yenu Akhera hilo ni juu ya Mwenyezi Mungu!'"

Wayahudi hao wa Khaybar walitolewa wito katika namna hiyo lakini jibu lao likawa: "Tunaapa kwa Taurati ya Musa ambayo tunayo, hatutafanya mnayotaka tufanye, wala hatutaiacha dini yetu!" (Waqidi, II, 653)

Mzingiro huo ulidumu kwa siku kadhaa. Waislamu walielekea kuishiwa mahitaji yote. Sasa vita vilielekea kuwa na taathira kubwa kwao. Waislamu walikuwa wakitoa mashambulizi mengi, huku wengi wao wakiwa na majeraha mazito. Pamoja na hayo yote, jambo pekee lililokuwa akilini mwa Mtukufu Mtume ﷺ ni kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kuna tukio moja wakati wa mzingiro wa Khaybar, linaloonesha kuwa Mtukufu Mtume ﷺ hakumpuuza yeyote linapokuja suala la kuwaita watu kwenye Uislamu. Tukio hili lilishuhudia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akimfafanulia Uislamu kwa undani kabisa mtumwa mmoja aliyekuwa akichunga kondoo wa Mayahudi, jirani na ngome zao, hatimaye akafanikiwa kumuongoza kwenye mwanga na nuru ya ukweli.[234] Hivi ndivyo ilivyotokea:

Yasar, ambaye alikuwa akipata riziki yake kwa kazi ya kuchunga kondoo wa Yahudi mmoja, asubuhi moja alikutana na Mtu-

234. Ibn Hisham, III, 398.



kufu Mtume ﷺ wakati akichunga kondoo nje ya kuta za ngome za Khaybar. Baada ya mazungumzo kwa muda kadhaa, Yasar aliamua kusilimu, akabadili jina lake na kuitwa Aslam baada ya kushauriwa na Mtume ﷺ. Kisha alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ afanye nini kuhusu kondoo aliokabidhiwa kuwachunga.

"Waonyeshe njia wapate kurejea!" alishauri Mtukufu Mtume ﷺ na kuongeza: "Bila shaka watarejea kwa mmiliki wao."

Aslam akachukua changarawe na kuzitupa upande wa kondoo, huku akisema kwa sauti: "Nendeni; rudini kwa mmiliki wenu...Naapa kwa Allah, tunaachana milele!"

Kondoo hao, kwa pamoja, walirudi kwa unyenyekevu na kuingia ngomeni, kana kwamba kuna mtu aliyekuwa akiwaongoza. Kisha Aslam aliungana na Waislamu wengine katika mapambano yao pembezoni kabisa mwa kuta za ngome.[235] Akiwa ndo kwanza

235. Ibn Hisham, III, 397-398; Ibn Hajar, al-Isabah, I, 38-39.

amesilimu, Aslam ﷺ aliunesha ushupavu mkubwa sana katika vita hivyo, na muda mfupi baadaye akauawa kishahidi. Mwili wake uliletwa mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye alikuwa amezungukwa na kundi la Maswahaba. Alipouona tu akageuza macho uso wake kuangalia sehemu nyingine. Alipoulizwa sababu, akasema:

"Sasa hivi yupo pamoja na wake zake wawili wenye macho mazuri wa Kihurul-ayn!" (Ibn Hisham, III, 398; Ibn Hajar, al-Isaba, I, 38-39)

Vita ilifikia kiwango ambacho sasa kilikuwa kiujaribu ustahmilivu wa Waislamu. Walikuwa wakizidiwa na mchoko kutokana na mashambulizi yao yote kuzuiwa. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akatangaza:

"Kesho, nitampa bendera yangu mtu ambaye, kupitia kwake, Mwenyezi Mungu ataidondosha Khaybar. Anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na napendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake..."

Usiku huo, Maswahaba walioshiriki katika vita hawakupata usingizi, wakitafakari nani atakayepewa bendera ya Mtume ﷺ. Asubuhi kila mtu alikimbilia kwa Mtukufu Mtume ﷺ kwa matumaini ya kuwa mtu atakayepata upendo wa wa kupendwa na Mwenyezi Mtukufu na Mtume Wake. Walikuwa na shauku kubwa sana kiasi kwamba siku moja Omar ﷺ alikiri kuwa: "Sikuwahi kutamani kuwa kamanda (kiongozi) kama nilivyofanya siku hiyo. Niliendelea kujaribu kuwa wazi nikitarajia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ataniita!"

Hatimaye, Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza Ali ﷺ aletwe, ambaye wakati alikuwa akiumwa macho na hivyo akaongozwa mpaka mbele ya Mtukufu Mtume. Kutokana na maradhi, hakuweza kuona kili-

cho mbele yake. Mtukufu Mtume ﷺ alipomuona Ali ؓ akipata tabu ya kuona, alipuliza katika macho yake na kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, 'simba huyo wa Allah' akapona. Kisha Mtukufu Mtume ﷺ alimvika mavazi ya vita, akampa bendera na kusema:

"Ewe Ali, sasa songa mbele...usitazame kushoto au kulia mpaka Mwenyezi Mungu atakapokupa ushindi!"

Ali ؓ alisonga mbele kisha akasimama. Bila kutazama nyuma, akauliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nipambane nao juu ya jambo gani?"

"Pambana nao mpaka watakaposhuhudia kuwa hakuna mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kwamba Muhammad ni Mtume Wake. Wakikubali, mali na damu yao vitakuwa salama dhidi yako, isipokuwa kama wakifanya mambo ambayo dini imeyakataza, na hesabu yao itakuwa kwa Mwenyezi Mungu. Wakurubie kwa utaratibu na upole. Kwanza, waite kwenye Uislamu. Mtu mmoja atakayeongoka kwa wito wako huo ni bora kwako kuliko kupewa ngamia wekundu!" (Bukhari, Ashab'un-Nabi, 9; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 32-34; Haythami, VI, 151)

Siku hiyo, majemadari maarufu wa Kiyahudi wote waliuawa. Khaybar ikaanguka, pamoja na ngome zake nane, ambapo mbili kati yake zilisalimu amri bila mapambano. Yale yaliyokuwa yametabiriwa na Mtukufu Mtume ﷺ yakathibitika. Mayahudi walikuwa hasara ya watu tisini na tatu kwa ujumla, ikilinganishwa na Waislamu kumi na tano waliouawa kishahidi.[236]

Abu Hurayrah ؓ anasema:

236. Sayyid Sayfullah anatamathali na kusawiri tukio hilo kwa kusema, "Usiusifie vibaya mkate, huo ni ujinga. Ivunje nafsi yako inayofanana na Khaybar, huo ndio ujasiri na ushujaa wa hali ya juu…"

"Tulikuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika Vita vya Khaybar. Kuna mtu mmoja ambaye siku zote alikuwa akisema kuwa yeye ni Muislamu, na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, 'Huyo ni mtu wa Motoni.' Vita vilipoanza, mtu huyo akapambana kwa ushupavu mkubwa na kujeruhiwa vibaya sana. Baadhi ya Maswahaba wakamtaarifu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuwa, 'mtu uliyesema kuwa ni wa Motoni amepigana kwa ushupavu na kufariki dunia!' Kwa mara nyingine, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aksema kuwa, 'Ameenda Motoni!'

Baadhi ya Waislamu walikuwa katika ncha ya kuangukia katika shaka kufuatia jibu hilo. Muda mfupi baadaye, wakamwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuwa mtu yule alikuwa hajafariki dunia bali amejeruhiwa vibaya na amelala chini. Ilipofika usiku, mtu yule hakuweza kuvumilia maumivu, akausogeza mwili wake kwenye ncha kali ya upanga, akajiua. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akataarifiwa juu ya hali hiyo.

'*Allah-u Akbar*…! Ninashuhudia kuwa mimi ni mja na mjumbe wa Mwenyezi Mungu', alisema. Kisha alimuamuru Bilal ﷺ atangaze kuwa, 'Waislamu pekee ndio watakaoingia Peponi. Hii inaonesha kwa uthabiti kuwa vilvile Mwenyezi Mungu huimarisha dini hii kupitia kwa mtu mkosaji pia.'" (Bukhari, Jihad, 182, Maghazi, 38; Qadar, 5; Muslim, Iman, 178)

Kufuatia ushindi wa Khaybar, Mayahudi waliomba wabaki wakifanya kazi katika ardhi zao kwa malipo ya kutoa nusu ya mazao. Hivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuwapeleka uhamishoni Mayahudi wote. Mtukufu Mtume ﷺ alikubali ombi lao la kubaki katika ardhi hizi zenye rutuba na kupokea nusu ya mazao yote, kwa sharti kwamba ataweza kuwafukuza muda atakaoona

unafaa. Mayahudi hawa walibaki katika eneo hilo mpaka zama za ukhalifa wa Omar ﷺ.[237]

Abdullah ibn Rawaha ﷺ alipewa kazi ya kwenda Khaybar kila mwaka kwa ajili ya kufanya tathmini na kukusanya nusu ya mazao kutoka kwa Mayahudi kama ilivyokubaliwa. Haukupita muda mrefu, Mayahudi hao wakaanza kumsumbua na kumkera Ibn Rawaha ﷺ katika kutathmini mazao. Walienda mbali zaidi kiasi cha kutaka kumpa hongo ili awafanyie ulaini kidogo.

"Naapa kwa Allah kwamba, kwa yote hayo mliyoyafanya, mmekuwa watu hakiri zaidi kwangu kuliko viumbe wote wa Mwenyezi Mungu. Pamoja na hivyo, hilo halinizuii kuwa mwadilifu kwenu. Mnachotaka kunipa ni hongo; na kujihusisha na rushwa ni haramu. Hatuigusi kabisa hiyo!" Alitangaza Ibn Rawaha ﷺ.

Mayahudi walishangazwa sana, wakajibu: "Ni kwa sababu ya uadilifu kwamba mbingu na ardhi zimesimama imara!" (Muwatta, Musaqat, 2)

Umakini Katika Kuchunga Haki za Wengine

Ngawira za Khaybar ziligawiwa miongoni mwa wale waliokuwepo katika tukio la Hudaybiya, bila kujali iwapo walishiriki katika vita vya Khaybar au la, kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyokuwa amewaahidi Waislamu walioshiriki tukio la Hudaybiyah kupitia aya ya 20 ya *surah Fath* kuwa watapata utajiri wa Khaybar.[238]

Maelezo yafuatayo yanatolewa na Omar ibn Khattab ﷺ:

237. Muslim, Musaqat, 5; Abu Dawud, Kharaj, 23-24/3007.
238. Waqidi, II, 684.

"Ilikuwa siku ya Vita vya Khaybar. Kundi moja la Maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu lilikuja na kuanza kutangaza majina ya wale waliokuwa wameuawa kishahidi. Kisha alipita majeruhi mwingine akitembea, wakasema, 'fulani na fulani wameuawa kishahidi'.

'Hapana!' Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliingilia kati. 'Nilimuona katika Moto wa Jahannamu akiwa amevaa joho alililolichukua pasipo haki kutoka katika ngawira!'" (Muslim, Iman, 182)

Licha ya kuwa kifo cha kishahidi kuwa miongoni mwa daraja za juu kabisa ambazo hufuta dhambi nyingi za mtu, daraja hiyo haiwezi kufuta dhambi ya kupokonya haki za watu wengine kwa kuhodhi mali ya umma. Kwa kueleza kuwa Swahaba aliyetangazwa kufa kishahidi ataadhibiwa ndani ya moto wa Jahannamu kwa joho alililochukua bila haki, Mtukufu Mtume ﷺ aliufundisha umma wake kuwa kuiba mali ya umma na kukiuka haki za watu wengine ni kosa lisilosameheka.

Palikuwa na mtumwa mmoja mweusi aitwaye Midam. Aliletwa na Rifaa ibn Zayd kama zawadi, na alikuwa akimhudumia Mtukufu Mtume ﷺ. Alipatwa na mshale uliokosea njia wakati akipakuwa mizigo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, akafariki dunia. Kama ilivyokawaida, Maswahaba walibashiri kheri kuhusu kifo cha Midam, kwa kuona kuwa alikuwa ameuawa kishahidi. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ akawaambia kinyume kabisa:

"Hapana, sivyo mnavyodhani. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, ambaye uhai wangu uko Mikononi Mwake, hakika hivi tunavyozungumza, blanketi alililolichukua siku ya Khaybar kabla ngawira hazijagawiwa linapanda kumfuataka kama moto!"

Waumini waliingiwa na woga. Mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumpa gidamu moja au mbili, akasema huku akiwa mwenye aibu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nilichukua gidamu hizi kwa ajili ya viatu vyangu, kabla ngawira hazijagawiwa..."

"Basi gidamu hizi ni Moto wa Jahannamu kwako..." alijibu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. (Bukhari, Ayman, 33; Muslim, Iman, 183)

Siku ya kuanguka kwa Khaybar, mtu mmoja alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akadai kuwa ametengeneza "... faida kuliko wakazi wa jangwa hili walivyofikiria."

"Ni kweli hayo? Ulifanya nini?" aliuliza Mtukufu Mtume ﷺ.

'Nilikuwa nanunua na kuuza bila kupumzika, mpaka nikaweza kutengeneza faida ya *uqiyya* mia tatu!"

"Je nikwambie faida bora kabisa kuliko zote?" Mtukufu Mtume ﷺ alimuuliza.

"Ndiyo, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu..."

"Swala yenye rakaa mbili utakayoiswali baada ya swala ya faradhi...!" (Abu Dawud, Jihad, 168/2785)

Baada ya kupokea fungu lao la bidhaa na mashamba ya tende ya Khaybar, Muhajirun waliweza kuboresha hali zao za kiuchumi, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ aliwarejeshea *Ansar* mashamba yao ya tende na miti ambayo hapo awali walikuwa wamewapa au kuwaazima *Muhajirun*.[239]

Daws awasili Mjini Madina

Katika kipindi hicho hicho, kundi moja kutoka kabila la Daws lilikuja mjini Madina. Kiongozi wao, Tufayl ibn Amr, aliwahi kuja Makka katika zama za mwanzo kabisa za kudhihiri kwa Uislamu

239. Ibn Qayyim, III, 359.

na kuukubali Uislamu baada ya kuzungumza na Mtukufu Mtume ﷺ. Baada ya kupata idhini ya Mtume ﷺ alirudi kwa watu wake, akawalingania kwenye Uislamu. Abu Hurayrah ؓ ni mtu wa kwanza kuutikia wito wake.[240] Baadaye idadi ya Waislamu iliongezeka hatua kwa hatua na kufikia kaya sabini mpaka themanini, ambao wote walihamia Madina wakati wa Vita vya Khaybar. Walipofika tu Madina, waliungana moja kwa moja na Mtukufu Mtume ﷺ katika vita hivyo.

Wakati wote wa safari, Abu Hurayrah ؓ alikuwa na hamu na shauku kubwa mno ya kukutana na Mtukufu Mtume ﷺ. Njiani alikuwa akisoma utenzi ufuatao wa shairi:

"Ewe usiku wa safari! Nimechoshwa na urefu wako... lakini umeniokoa kutoka kwenye ardhi ya ukafiri!" (Bukhari, Maghazi, 75; Waqidi, II, 636)

Wakati Abu Hurayrah ؓ na wenzake wakiwasili Khaybar katika safari hiyo ndefu, Khaybar ilikuwa imeshaanguka.[241]Mtukufu Mtume ﷺ alipomuona, alimuuliza mahali anapotoka.

"Daws", alijibu Abu Hurayrah ؓ, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Kheri pekee ndiyo niliyoiona kwa kila niliyekutana naye kutoka Daws!" (Tirmidhi, Manaqib, 46/3838)

Mtukufu Mtume ﷺ alitenga fungu maalumu la ngawira za Khaybar kwa ajili ya watu hao wa Daws.[242]

Kurejea kwa Wahamiaji wa Abyssinia

Wakati Khaybar ikianguka, kundi la Maswahaba kumi na sita wakiongozwa na Jafar ؓ lilikuwa likirejea kutoka Abyssinia kue-

240. Ibn Hajar, al-Isabah, II, 226.
241. Ibn Saad, IV, 328.
242. Ibn Saad, I, 353.

lekea Madina. Wahamiaji hao walipopata taarifa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ yuko Khaybar, haraka sana wakanyoosha kuelekea huko, na muda mfupi baadaye wakaungana naye.

"Unafanana nami sana katika muonekanano na tabia", Mtukufu Mtume ﷺ alianza kusema baada ya kumuona Jafar. Kisha akaongeza: "Sijui nifurahie zaidi jambo lipi: kuanguka kwa Khaybar au kurejea kwa Jafar!" (Ibn Hisham, III, 414)

Jafar ؓ alikuwa katika furaha isiyo kifani kwa kupokea sifa hizo za Mtukufu Mtume ﷺ, na kama mtoto mdogo, akaanza kuzunguka, juu ya mguu mmoja, kumzunguka Mtume ﷺ, mpaka akasindwa kujizuia.[243]

Mtukufu Mtume ﷺ hakumkataza Jafar ؓ kufanya hivyo. Baadaye, baadhi ya wanatariqah au Masufi, walilichukulia hilo kama ithibati (*sunnat'ut-taqri*) ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kama utangulizi wa *wajd* au hali ya utakaso wa kiroho.[244]

Wengine waliowasili sanjari na wahamiaji hao ni Kabila la Ash-ari la Yemen. Miongoni mwao ni Abu Musa al-Ash-ari ؓ ambaye anasema:

"Tukiwa Yemen, sisi (watu wa kabila la Ash-ari), tulipata taarifa ya kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amedhihiri,ambapo nikiwa pamoja na watu wengine hamsini na mbili au na tatu katika kabila letu, tulifunga safari ya kufanya hijra mahali alipo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya sana, jahazi letu lilitupeleka kwenye nchi ya mfalme Najjashi wa Abyssinia. Huko, tulikutana na Jafar ؓ na wenzake, akatwambia, 'Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alituagiza tuje katika nchi hii na

243. Ahmad, I, 108; Ibn Saad, IV, 35.

244. Sama, au kuzunguka kwa kasi, inayoanza baada ya kufikia hatua fulani ya kiroho katika mafunzo ya twariqah ya Mawlawi ilitokana na tukio hili.

kutuamuru tubaki hapa kwa muda. Ninakushaurini pia mbaki hapa pamoja nasi!'

Baada ya kukaa huko kwa muda, hatimaye tulipanda jahazi na kurudi pamoja Madina. Tuliungana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wakati Khaybar ilipoanguka. Hivyo, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akatupatia pia sehemu ya ngawira za Khaybar." (Bukhari, Maghazi, 38; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 169)

Njama ya Mayahudi Kumpa Sumu Mtukufu Mtume ﷺ

Mayahudi hawakuacha kabisa khiyana zao licha ya muamala mzuri na wa kibinaadamu waliokuwa wakiupata kutoka kwa Waislamu. Walipanga njama, kwa siri, ya kumuua Mtukufu Mtume ﷺ. Wakati athari zilizofuatia uhalifu wao wa mwanzo zikiwa bado kufutika, sasa walikuwa wakijaribu tena kumsaliti Mtume ambaye, bdala ya kuwafukuza kama alivyofanya kwa makabila mengine ya Kiyahudi, alikuwa amewasamehe hapo awali kwa kujaribu kufanya njama ya kumua inayofanana na hiyo. Ajabu ni kwamba, kwa mara nyingine walikuwa wakikiuka makubaliano yao.

Ili kutekeleza njama hii ya kiovu, Zainab, binti wa Yahudi mmoja maarufu aitwaje Harith, alimualika Mtukufu Mtume ﷺ, pamoja na baadahi ya Maswahaba zake, kwenye karamu ya nyama ya mwanakondoo ailiyechomwa, ambayo aliitia sumu. Kwa kujua kuwa Mtukufu Mtume ﷺ ni mpenzi wa nyama ya bega la mwanakondoo, hata huko aliongeza sumu pia. Mtume alipochukua kipande cha nyama, alikitema na kuwaonya Maswahaba: "Nyama hii yaniambia kuwa imewekwa sumu...msile!" Hata hivyo, Bishr ibn Bara رضي الله عنه alikuwa ameashapeleka mdomo kipande cha nyama baada ya kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameanza kula na wakati onyo hilo linatolewa alikuwa ameshameza kipande hicho. Wengine walikuwa hawajaigusa.

Muda mfupi baadaye, mwanamke huyo muovu alikamatwa na kuletwa mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ni wewe uliyetia sumu kwenye nyama hii?" alimuuliza.

"Uligunduaje kuwa ilikuwa na sumu?" aliuliza mama wa Kiyahudi.

"Nyama ya mwanakondoo iliyo mbele yangu imenitaarifu kuwa imewekwa sumu", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ.

"Ndiyo, mimi ndiye niliyemuwekea sumu", alisema na kukiri kosa lake.

Alipoulizwa na Mtukufu Mtume ﷺ kilichomsukuma kufanya hivyo, akasema: "Ulimuua baba, ami na mume wangu. Hakuna kilichobaki ambacho hujawawafanyia watu wangu. Niliwaza mwenyewe kuwa 'iwapo mtu huyu ni mtume kweli, basi Mwenyezi Mungu atamhabarisha kuhusu njama yangu na sumu hii haitamdhuru; lakini kama ni muongo na mtawala wa kawaida tu, basi atakufa kwa sumu hii na tutakuwa tumelipa kisasi kwa vivyo vya ndugu zetu na kuondokana naye kabisa!'"

Mtume aliyebarikiwa akasema: "Mwenyezi Mungu hajakupa uwezo wa kufanya hivyo."

Baada ya kuona kuwa mpango wake umegundulika, mwanamke huyo aliathiriwa sana na kile alichokishududia, akaamua kusilimu, akatamka shahada na kuomba msamaha. Mtukufu Mtume ﷺ ambaye, alitumwa kama rehma kwa walimwengu, alimsamehe kosa lake la kujaribu kumuua. Lakini kwa kuwa Bishr ibn Bara ؓ alikuwa amefariki dunia muda mfupi baada ya kula sumu hiyo, ndugu zake walidai *qisas* (kisasi). Hivyo, ili kulipa kisasi, binti huyo wa Harith akalazimika kula sumu hiyo hiyo iliyomuua Bishr.

Ili kuondoa athari ya sumumwili mwake, Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza kutolewa damu baina ya mabega yake. (Bukhari, Jizya, 7; Muslim, Salam, 45; Ibn Hisham, III, 390; Waqidi, II, 678-679; Haythami, VI, 153)

Miaka mitatu baadaye, kabla ya kuvuta pumzi yake ya mwisho, inaelezwa alibaini athari ya sumu hii kuwa ndiyo chanzo cha kifo chake. (Hakim, III, 242/4966)

Kadhia ya Ndoa ya Mutah

Vilevile, suala liloharamishwa na kupigwa marufuku katika kipindi hicho cha Vita vya Khaybar ni suala la ndoa ya muda ijulikanayo kama *mutah*, ambayo kabla ya hapo hakuna ufunuo uliokuwa umeteremka kuiharamisha.

Ali ؓ anasimulia kuwa: "Wakati wa Vita vya Khaybar, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikataza kuoa wanawake kwa *mutah* na kula nyama ya punda wanaotumikishwa." (Bukhari, Maghazi, 38; Nikah, 31; Dhabaih, 28; Hiyal, 3; Muslim, Nikah, 29-32; Muwatta, Nikah, 41; Nasai, Nikah, 71)

Ndoa hii ya *mutah*, ambayo mizizi yake inaanzia Zama za Ujahiliya, ni aina ya ndoa ambayo mwanamke hukodiwa kwa kipindi fulani cha muda kwa kiasi fulani cha mahari. Ndoa ya mutah hufikia tamati baada ya muda uliokubaliwa kufikia kikomo. Katika ndoa ya mutah, hakuna haki ya mirathi, marupurupu na kipindi cha kusubiri baada ya talaka, kama ilivyo katika ndoa za kawaida. Hivyo ilipigwa marufuku baada ya vita vya Khaybar kupitia ahadith mbalimbali kuhusu suala hilo. Miongoni mwa hizo ni: "Sasa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiharamisha mpaka Siku ya Kiyama. Yeyote aliyemuoa mwanamke kwa *mutah* anatakiwa kumuacha huru na asichukue chochote kutoka kwake kama malipo!" (Muslim, Nikah, 21; Ibn Majah, Nikah, 44; Darimi, Nikah, 16; Ahmad, III, 406)

Wakati akirejea kutoka katika Vita Vya Tabuk, Mtukufu Mtume ﷺ aliamua kupumzika jirani na eneo la Saniyyat'ul-Wada. Hapo, aliwaona wanawake wakilia na alipowauliza kinachowaliza, mmoja wao akasema kwa niaba ya wenzake kuwa wao ni "...wanawake walioolewa kwa *mutah*." Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ akasema: "Mutah ilifutwa na sheria za Uislamu za ndoa, talaka, eda na mirathi!" (Ibn Balban, VI, 178; Darakutni, III, 259)

Hivyo, mwanamke aliyeolewa kwa ndoa ya mutah sio mke, na kwa mujibu wa makubaliano (ijmaa) ya wanazuoni wa Kiislamu, *mutah* ni sawa na zinaa.

Maelezo yafuatayo yanatolewa na Ibn Abbas رضي الله عنه:

"Kabla ya Uislamu kulikuwa na *mutah*. Mtu anapofika kwenye ardhi ya ugenini, alikuwa akimuoa mwanamke wa eneo hilo kwa *mutah* kwa kipindi maalimu cha muda aliodhani kuwa atakaa huko. Mwanamke alikuwa akitunza mali za mwanaume huyo na kumfanyia kazi mbalimbali. Hilo liliendelea mpaka ulipoteremka ufunuo wa '...Na ambao wanazilinda tupu zao. Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa.' (al-Muminun, 5-6). Hivyo, uhusiaono mweingino wote usiokuwa huo ulioelezwa, ni haramu." (Tirmidhi, Nikah, 29/1122)

Athari mbaya za kijamii zitokanazo na *mutah* ni pamoja na:

a) Hasara inayowasibu watoto waliozaliwa katika ndoa hizo za muda, ambao, kama watoto waliozaliwa nje ya mahusiano ya ndoa, huwafanya wakue bila baba, na hivyo kukosa malezi mema na matunzo stahili.

b) Kwa kuwa mipaka ya nasaba inakuwa imeparaganyika na watoto kutojulikana, kunakuwa na uwezekano wa mwanamke husika kuingia katika mahusiano na mtoto wake mwenyewe, ambaye alimzaa kutoka kwa mwanaume aliyefunga naye *mutah* hapo

mwanzo. Vivyo hivyo kwa mwanaume; kuna uwezekano wa kuingia katika uhusiano na binti yake, mjukuu au hata mpwa wake; au tuseme anaweza kujikuta amefunga ndoa na mtu ambaye ni haramu kwake kuoana naye. Bila shaka hili ni miongoni mwa hatari kubwa kabisa za *mutah*, kama zilivyoshuhudiwa na wengi katika historia.

c) Katika mazingira mengi, inashindikana kugawa mirathi ya mtu aliyefunga ndoa ya mutah, kwa sababu idadi ya na utambulisho wa warithi wanaendelea kutojulikana.

Kwa kweli hatari zitokanazo na ndoa ya *mutah* ni zenye kuogofya. Ni sawa na kupoteza kizazi na dhuria. Kwa upande mwingine, mwanamke aliyefunga ndoa ya *mutah*, huingia katika anguko la kiroho na la kimaanawi kwa sababu kuhisi kuwa anakodishwa kwa muda ni jambolenye kuvunja moyo sana. Hivyo, *mutah* ni pigo kali dhidi ya roho ya usafi wa mwanamke. Je mtu aweza kuridhia kumuona binti au mamaye akifunga ndoa ya *mutah* licha ya ubaya wake wote wenye kuchukiza? Hilo pekee linatosha kufichua chukizo la *mutah*.[245]

Kurejea Kutoka Khaybar

Kufuatia Ushindi wa Khaybar, Mtukufu Mtume ﷺ alituma mjumbe kwenda eneo la Fadak, ambalo lipo umbali wa siku mbili kutoka Madina, na kulifanya eneo hilo kujumuishwa chini ya utawala wa Waislamu bila kumwaga damu.

Mwisho, Wadi'il-Qura, kijiji kidogo cha Wayahudi kilicho katika njia ielekeayo Madina, nacho pia kilichukuliwa baada ya mzingiro uliodumu kwa muda wa siku moja. Kama ilivyokuwa kwa

245. Kwa maelezo zaidi kuhusu suala la mutah, tazama: *İbrâhim Cânan, Nâmus Fitnesi Mut'a*, İstanbul, 1993.

wakazi wa Khaybar, nao pia waliachwa wafanye kazi katika ardhi yao kwa makubaliano ya kutoa nusu ya mazao yao.

Ama kuhusu Mayahudi wa Tayma, walikubali kutoa jizyah, kama malipo ya kuendelea kubaki katika kijiji chao. Hapo mwanzo, makabila yote mawili ya Kiyahudi yalikuwa yamefanya mkataba na Khaybar wa kwenda kuivamia Madina na kuishambulia.[246]

Ushindi wa Khaybar na eneo jirani uliwaandalia Waislamu njia kwa ajili ya ushindi mkubwa wa kuifungua Makka. Kushindwa kwa Banu Qaynuqa, Banu Nadhir, Banu Quryadha na hatimaye Mayahudi wa Khaybar kuliyatisha makabila mbalimbali ya peninsula hiyo, na kuondoa wingu lolote la shaka katika akili zao juu ya ushindi adhimu wa Mtukufu Mtume ﷺ.Ilikuwa ni hali yenye kutoa tahadhari, kwa maana makabila yaliyotajwa yaliyokuwa ndiyo makabila tajiri na yenye nguvu sana kuliko makabila yote ya Kiyahudi katika eneo la Arabia na ustadi wao katika vita ulikuwa wenye kujulikana na kuogopwa. Walikuwa na ngome madhubuti zisizopenyeka, kiwango kikubwa cha mashamba ya mitende na walikuwa na uwezo wa kuwalinda Waarabu wote iwapo wangekimbilia kwao. Lakini sasa ilikuwa wazi jinsi ujasiri na nguvu waliyodhaniwa kuwa nayo vilivyonyauka pindi walipozingirwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ na jinsi walivyofalazimishwa kukubali kwa unyenyekevu mizigo mizito. Sasa upepo mwanana ulikuwa ukivuma kuelekea kwa Waislamu.[247]

Baada ya Vita vya Khaybar, Mtukufu Mtume ﷺ alimuoa bibi Safiyya, ambaye aliachwa akiwa mjane baada ya mumewe kuuawa katika vita.[248] Alilikuwa ameolewa na mumewe, ambaye alikuwa mtu maarufu katika Wayahudi wa Khaybar, siku chache kabla ya

246. Tazama: Ibn Hisham, III, 391; Waqidi, II, 707, 711.

247. Tazama: Waqidi, II, 729-731; Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 234.

248. Ibn Saad, VIII, 121-126.

mzingiro wa Khaybar. Usiku wa harusi, aliona ndoto iliyoonesha mwezi ukichomoza kutoka Madina na kuja kuangukia juu ya paja lake. Alipomuhadithia mumewe juu ya ndoto hiyo, alijawa na hasira mno na kufoka: "Unataka kuwa mke wa Muhammad, Mfalme wa Hijaz, sio?" kisha akampiga kofi lililomuachia alama nyeusi jichoni, mchubuko ambao bado alikuwa nao pindi alipokuwa na Mtukufu Mtume ﷺ siku chache baadaye. Alimwelezea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ masaibu yake pindi alipomuuliza juu ya mchubuko aliokuwa nao. Mtukufu Mtume ﷺ alimuelezea kuhusu Uislamu na kumwambia: "Hatutakulazimisha iwapo utaamua kubaki katika dini yako! Iwapo utamkubali Mwenyezi Mungu na Mtume Wake basi nitakukubali kama mke wangu. Lakini ukichagua kubaki kama Myahudi, nitakuacha huru a unaweza kurudi kwa kabila lako!"

Safiyya ؓ alichagua kuwa Muislamu na kuwa 'mama wa Waumini.' (Waqidi, II, 674, 707; Ibn Sad, VIII, 123; Ahmad, III, 138)

Ndoa ya Mtukufu Mtume ﷺ kwa bibi Safiyya Bint Huyay, ilileta ukaribu na Wayahudi wa Khaybar, na kwa kupunguza uadui, iliimarisha maendeleo ya uhusiano wa kirafiki. Kwa hali hii, Safiyya ؓ aliendelea kuwa karibu na Wayahudi, kiasi cha hata kuleta malalamiko, akionekana kuwa mwakilishi wao katika nyumba ya Mtume ﷺ.

Siku moja, mtumishi wa kike wa Safiyya ؓ alikwenda kwa Omar ؓ, zama za Ukhalifa wake na kulalamika jinsi "...Safiyya alivyoendelea kuipenda mno siku ya Jumamosi na kuendeleza mawasiliano yake na Wayahudi."

Hivyo, Khalifa Omar ؓ akamuagiza mtu kufanya uchunguzi juu ya hali hiyo. Safiyyah ؓ alitoa maelezo yafuatayo:

"Kuhusu Jumamosi, siipendi siku hiyo kwa sababu Mwenyezi Mungu ameshanipa mbadala wake, ambayo ni Ijumaa. Ama kuhusu

swali lako juu ya Mayahudi, nina ndugu na jamaa miongoni mwao, ambao huenda kwao kuwatembelea." (Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 347)

Baadaye Safiyya ؓ alimuuliza mtumishi wake kwa nini alitoa tuhuma hizo. "Nilivutwa na Shetani", alikiri. Jibu la Safiyya ؓ kwa mtumishi huyo ilionesha wazi ni kwa kiwango gani alikuwa ameathirika na maadili ya Uislamu:

"Unaweza kwenda; nimekuacha huru", alisema, na kumuacha huru mtumishi wake aliyejaribu kumtengenezea tuhuma za uongo. (Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 347)

Umrat'ul-Qada (Dhilqada, 7 / Machi, 629)

Umra hii yajulikana kama Umratul-Qada (Umra ya kulipa) kwa sababu ilifanyika kufidia umrah ya mwaka mmoja uliopita, ilioyozuiliwa na washirikina wa Makka.

Sasa mwaka mmoja ulikuwa umepita baada ya Mkataba wa Hudaybiyah na muda ulikuwa umefika wa kutekeleza ibada ya umrah kama ilivyokubaliwa katika Mkataba wa Hudaybiya. Ulipowadia mwezi wa Dhilqada katika mwaka wa saba wa Hijra, Mtukufu Mtume ﷺ alitoa amri kwa kila mtu aliyeshiriki tukio la Hudaybiya kuanza kujiandaa kwa ajili ya *umrah*. Aliipanua amri yake kwa Waislamu wengine pia. Waarabu wa maeneo ya jirani waliokuwa Madina wakati huo wakasema kuwa "...hawana chakula kwa ajili ya safari wala hawana wa kuwalisha!"

Hivyo, Mtume wa Rehma ﷺ akawataka Waislamu wa Madina kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuwapa wale wenye kuhitaji na kukidhi mahitaji yao, na kuonya kuwa kuzuia mikono yao isiwasaidie kutawapaleka kwenye maangamizi.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kipi tunachoweza kutoa ilhali hatuna chochote?" walisema.

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Chochote mlichonacho, hata kama ni kipande cha tende..." (Waqidi, II, 731-732)

Hatimaye Mtukufu Mtume ﷺ alianza safari akiwa na Maswahaba elfu mbili, farasi mia moja, na baadhi ya zana za kijeshi kama vile helmeti, mavazi ya vita na mikuki. Alichukua zana hizo kwa ajili ya tahadhari tu. Baadhi ya Maswahaba walimkumbusha Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu sharti lililowekwa na Maqurayshi linawalozuia kubeba silaha isipokuwa kiwango kidogo tu kinachokubalika kwa msafiri yeyote.

"Hatutaingia na silaha hizo eneo la Haram; lakini, ni bora tuwe nazo karibu kwa tahadhari ya kutokea shambulizi lolote", Mtukufu Mtume ﷺ alifafanua. Kisha aliwaagiza Maswahaba mia mbili kuzipeleka silaha hizo katika eneo la Batn-i Yajaj, umbali wa maili tatu kutoka Makka. (Waqidi, II, 733-734)

Njiani, mahujaji walisimama katika eneo la Abwa. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amepewa idhini na Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kulizuru kaburi la mama yake. Wakati wa ziara hiyo, alilirekebisha kaburi hilo kwa mikono yake na kutoa machozi ya uchungu. Waumini wakashindwa kuyazuia machozi yao, wakalia. Baadaye Mtukufu Mtume ﷺ alipoulizwa sababu ya kulia kwake, akasema: "...kwa sababu nimeikumbuka huruma na upendo wa mama yangu aliokuwa nao kwangu." (Ibn Sad, I, 116-117)

Ili kuenda sambamba na masharti ya mkataba wa Hudaybiyah, waabudu masanamu waliondoka Makka kwa muda wa siku tatu na kuelekea kwenye milima ya jirani na kuuacha mji ukiwa wazi kwa ajili ya Waislamu. Kwa furaha ya kuiona Kaabah kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka saba, Waislamu waliokuwa na shauku kubwa wakaanza kutoa *talbiyah* kwa pamoja.

Kwa mujibu wa ripoti ya Ibn Abbas رضي الله عنه, Mtukufu Mtume ﷺ alipokuwa akiingia Makka alikutana na kusalimiana na watoto kutoa katika ukoo wa Muttalib. Alimchukua mtoto mmoja na kumuweka mbele ya tandiko la ngamia wake na mwingine kwa upande wa nyuma na kisha akaongoza kuelekea katikati ya mji.[249]

Ili kuwaonesha waabudu masanamu wa Makka kuwa hapakuwa na ukweli wowote kuhusu uvumi kwamba Waislamu walikuwa wamedhoofika kutokana na homa kali ya Madina, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaamuru kutembea kwa haraka na kwa ukakamavu.[250]

"Mwenyezi Mungu amrehemu yule atakayeonekana mkakamavu kwa makafiri!" aliomba dua. (Ibn Hisham, III, 424-425)

Waislamu hao ambao waliwasili Makka baada ya kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa mia nne kutoka Madina, walikuwa wakihisi uchovu wa safari; lakini walitekeleza kikamilifu agizo la Mtume ﷺ na kutekeleza ibada ya *umrah* kwa ukakamavu, heshima na ushupavu. Waliweza hata kukimbia kwa ushupavu wakati wa *ashwat* tatu za mwanzo za kuizunguka Kaabah, hasa wanapofika katika eneo la baina ya nguzo mbili za kijani zilipo leo.

Wakati huohuo, Makafiri walikuwa wakiwapeleleza Waislamu kwa udadisi. Kama wangeona uchovu na ulegevu wowote kwa Waislamu, wangekuwa na mawazo mengine. Walipoona kwa macho yao ushupavu na ukakamavu wa Waislamu, walishindwa kuuficha mshangao wao:

"Hawa ndio watu mliosema kuwa wamedhoofika kwa homa kali? Wana nguvu na afya kuliko hata sisi!" walisema. (Muslim, Hajj, 240)

---

249. Bukhari, Umrah, 13; Libâs, 99.
250. Bukhari, Hajj, 55; Muslim, Hajj, 240; Ahmad, I, 305-306.

Sauti yenye mvuto kutoka kwenye adhan iliyotolewa na Bilal Habashi akiwa juu ya paa la Kaabah siku hiyo, pamoja na kuzipa furaha nyoyo za Waislamu, iliongeza mshangao kutoka kwa makafiri waliokuwa wakishuhudia.

Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiizunguka Kaabah pamoja na Maswahaba, Abdullah ibn Rawaha رضي الله عنه alianza kusoma shairi fulani.

"Mpaka lini utaendelea kusoma shairi hilo mbele ya Mtume na katika Haram ya Mwenyezi Mungu?" Omar رضي الله عنه alilalama. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ mwenye akaingilia kati.

"Usimzuie! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, maneno yake ni yenye kuwachoma Maqurayshi kuliko mishale! Endelea ewe Ibn Rawaha!" alisema, kisha akawambaia Abdullah aseme:

"Sema, hakuna mungu wa kuabudiwa ila Allah. Yeye ni Mmoja. Yeye Ndiye pekee asiyekhalifu ahadi Yake. Yeye ndiye Mwenye kulipa nguvu jeshi Lake. Yeye pekee ndiye Mwenye kuyatawanya majeshi ya makabila yaliyoungana!"

Maswahaba wengine walikariri maneno hayo ya Abdullah ibn Rawaha رضي الله عنه. (Waqidi, II, 736; Ibn Sad, II, 122-123)

Muonekano maridhawa wa upole ulijionesha katika nyuso za Waislamu mara tu baada ya kurejea Madina kutoka katika ziara ya siku tatu waliyoifanya kwenye Kaabah Tukufu. Ziara ya kwanza kwenye Kaabah Tukufu ilikuwa imefanyika na ndoto ya Mtukufu Mtume ﷺ aliyoiona mwaka mmoja uliopita ilikuwa imetimia kwa haki; ukweli ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu ameutaja ndani ya Qur'an Tukufu, kwa kugusia juu ya ushindi waliokuwa wameupata katika Vita vya Khaybar na kubashiri juu ya ushindi mkubwa wa Makka watakaoupata muda mfupi ujao:

لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِن شَاءَ اللَّهُ آمِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُؤُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِن دُونِ ذَلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَى وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا

"Hakika Mwenyezi Mungu amemtimizia Mtume wake ndoto ya haki. Bila ya shaka nyinyi mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza nywele. Hamtakuwa na khofu. Yeye anajua msiyo yajua. Basi atakupeni kabla ya haya Ushindi karibuni. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki, ili aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi." (al-Fath, 27-28)

Ibada ya *umrat'ul-qada* iliacha athari kubwa kwa watu wa Makka na muda mfupi watu kama Khalid ibn Walid aliyeifungua Syria, Amr ibn As, aliyeifungua Misri na Othman ibn Talha wakashuhudiwa wakiungana na safu za Uislamu.

Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiondoka Makka, Umamah ؓ binti wa Hamza ؓ, alimkimbilia, akimuomba aende naye Madina. Ali ؓ alimchukua kwa mkono wake na kumleta kwa mkewe bibi Fatimah ؓ, akamuomba amtunze. Lakini waliporejea Madina, ulizuka mgogoro mdogo baina ya Ali, Zayd na Jafar ؓ, kila mmoja akitaka amtunze.

"Ni mtoto wa ami yangu!" alisema Ali ؓ.

"Nami pia ni mtoto wa ami yangu, na zaidi ya hayo nimemuoa shangazi yake (dada wa mama yake)!" alisema Jafar ؓ.

"Sawa, ni mtoto wa kaka yangu!" alisema Zayd, akiwakumbusha namna Mtukufu Mtume ﷺ alivyomuunganisha yeye na Hamza ؓ kuwa ndugu.

Mtukufu Mtume ﷺ aliamua kuwa itakuwa bora kwa Umamah kukaa na mama yake mdogo, akisema kuwa: "Mama mdogo ni kama mama mzazi!" Kisha akamgeukia Ali ؓ na kumwambia:

"Wewe watokana na mimi, nami natokana nawe!"

Akamwambia Jafar ؓ: "Wewe washabihiana nami katika muonekano na tabisa."

Kisha akamwambia Zayd ؓ: "Mimi na wewe ni ndugu na ni marafiki!" (Bukhari, Maghazi, 43, Umrah, 3; Muslim, Jihad, 90)

Ali ؓ anasema: "Zayd alifurahi mno aliposikia sifa kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba alianza kumzunguka Mtume, akiwa amesimama kwenye mguu mmoja. Kisha Jaafar alimfuata Zayd nyuma akifanya hivyo hivyo; nami pia, kutokana na furaha, nikaanza kuzunguka kwa mguu mmoja nyuma ya Jafar." (Ahmad, I, 108; Waqidi, II, 739)

MWAKA WA NANE WA HIJRA

Kifo cha Zaynab, binti wa Mtukufu Mtume ﷺ

Kamwe Zaynab ؓ hakupona majeraha aliyoyapata baada ya kusukumwa kutoka juu ya ngamia wakati wa safari yake ya kuelekea Madina. Hatimaye alivuta pumzi yake ya mwisho katika mwaka wa nane wa Hijra. Mwili wake ulioshwa na Umm Ayman, mwanamke wa *Kiansari* Umm Atiyya na wake watukufu wa Mtume ﷺ, Sawda na Umm Salama. Kabla hawajaanza, Mtukufu Mtume ﷺ aliwajia na kuwaambia waanze kumuosha, "...kuanzia upande wa mkono wa kulia na viungo vyake vya wudhu! Muosheni kwa witiri kwa maji ya *sidr*;[251] mara moja, mara mbili, mara saba na zaidi, ikibidi. Wekeni kiasi cha kafuri katika maji kabla ya muosho wa mwisho. Nipeni taarifa mtakapomaliza!"

Walizichana nywele za Zaynab ؓ, wakazigawanya katika sehemu tatu na kuzifunga katika mafungu matatu; moja kwa kila upande na nyingine kwa ajili ya nywele zake zilizo juu kabisa ya kichwa chake. Walipomaliza kumuosha, Mtukufu Mtume ﷺ aliwapatia sanda aliyokuwa ameishika mkononi mwake na kuwaambia: "Itumieni kama sanda ya ndani ya Zaynab!"[252] (Bukhari, Janaiz, 9, 13, 17; Muslim, Janaiz, 36; Ibn Sad, VIII, 34-36)

---

251. *Sidr* ni aina ya mcheri unaopatikana Arabia. Ni mti maarufu kwa harufu nzuri na kivuli. Majani yake hutumika kuoshea maiti. (Âsım Efendi, *Kâmus*, II, 385)

252. Ni Sunnah kwa sanda ya mwanaume kuwa na pande tatu: *izar* inayofunika mwili

Baada ya kuongoza swala ya jeneza, Mtukufu Mtume ﷺ aliteremka kaburini, akiwa mwenye huzuni na majonzi. Alikaa huko kwa muda, kisha akatoka na tabasamu likionekana usoni mwake, akasema: "Nilipofikiria udhaifu wa Zaynab, nilimuomba Mwenyezi Mungu amuondoshee misukosuko na joto la kaburini...na Mwenyezi Mungu akayakubali maombi yangu." (Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, VII, 131)

Vita vya Mu'ta: Tukio la Kihistoria Lililoandikwa na Maswahaba Wachache (Jamadiyalawwal, 8 / Agosti-Septemba, 629)

Wajumbe waliotumwa na Mtukufu Mtume ﷺ kwenda kwa wafalme na magavana mbalimbali, bila kuangalia mapokezi mabaya yaliyowakumba baadhi yao kwa nyakati fulani, walikuwa wakirejea Madina wakiwa salama, kutokana na ada na desturi ya muda mrefu iliyokataza 'kumuua mjumbe.' Hata hiivyo, Harith ibn Umayr رضي الله عنه aliyetumwa kwa Chifu wa Busra, hakurejea. Alipofika katika eneo la Mu'ta, alizuiwa na Shurahbil ibn Amr, Chifu wa Ghassani, ambaye alimuuliza Swahaba huyo alikokuwa akielekea. Baada ya kugundua kuwa ni mjumbe wa Mtukufu Mtume ﷺ, Shurahbil aliamua kufanya jambo lisilofikirika kabisa na kumuua kikatili Swahaba huyo.[253]

Mtukufu Mtume ﷺ alisikitishwa mno na jinsi Harith رضي الله عنه alivyouawa. Aidha, mauaji hayo yalikuwa uadui wa wazi kabisa dhidi ya Uislamu na dharau kubwa kwa Waislamu. Ilikuwa ni lazima ichukuliwe hatua ya kukabiliana na tukio hilo ili kuokoa heshima ya Dola ya Kiislamu na kuzuia tukio hilo kusababisha athari mbaya na

wake wote, kanzu na setiri. Kwa mwanamke, inakuwa na pande tano: *izar*, *hijab* kichwani mwake, setiri, kitambaa kinachofungwa kuzunguka matiti na tumbo lake na kanzu.

253. Waqidi, II, 755; Ibn Qayyim, III, 381.

za kutisha. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ akaandaa jeshi la Waislamu elfu tatu.

Kutokana na sera kuu ya Uislamu iliyoondosha tofauti za matabaka zilizokuwepo zama za Ujahiliya, Mtukufu Mtume ﷺ alimteua Zayd ؓ, aliyewahi kuwa mtumwa, kama kamanda wa jeshi la Waislamu. kisha akampa kamanda huyo maelekezo yafuatayo:

"Iwapo utauawa, basi Jafar ndiye atakayeongoza jeshi! Na Jafar akiuawa, Abdullah ibn Rawaha atachukua uongozi! Naye pia akiuawa, basi Waislamu watamchagua kamanda miongoni mwao atakayeliongoza jeshi!"

Yahudi mmoja aliyeyasikia maelekezo haya aliyachukulia kuwa ni tangazo la kifo kwa wale waliotajwa. Alimkaribia Zayd ؓ, na akiwa na nia ya kutia hofu ndani ya moyo wake, akamwambia "Andaa wosia wako! Kwa maana kama Muhammad ni Mtume kweli basi hutarudi kwake.Wale waliokuwa wakitajwa na Mitume wa Israel kabla ya vita walikuwa hawarudi!"

Maneno hayo yalimfanya Zayd ؓ azidi kuwa na furaha. (Ibn Kathir, al-Bidaya, IV, 238) Yahudi huyo hakuwa akijua kuwa, kama ilivyokuwa kwa Maswahaba wengine, Zayd alikuwa na shauku kubwa ya kufa kishahidi.

Abdullah ibn Rawaha ؓ ambaye alikamilisha maandalizi yake kwa ajili ya vita hivyo, alikuja kumuaga Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ambaye alikuwa akimpenda mno, akamwambia: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, niusie jambo nitakaloshikamana nalo moyoni mwangu!"

"Punde utafika ardhi ambayo *sajdah* ya kumsujudia Mwenyezi Mungu hufanywa kwa uchache. Kithirisha swala na sajdah utakapofika huko!" aliusia Mtukufu Mtume ﷺ.

"Niusie zaidi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", alisisitiza tena Ibn Rawaha.

"Daima mkumbuke Mwenyezi Mungu, kwa maana kumkumbuka Mwenyezi Mungu kutakusaidia kupata unachokitaka!" (Waqidi, II, 758)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilisindikiza jeshi la Kiislamu mpaka eneo la Saniyyat'ul-Wada na kuwaaga kwa ajili ya safari yao hiyo baada ya kuwaombea dua nyingi. Aliwaamuru kwenda mpaka mahali alipouawa Harith ؓ, wawalinganie maaduia kwenye Uislamu na, wakikataa, wapambane nao, kwa kutarajia msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee.[254]

Kwa kugundua ujio wa jeshi la Kiislamu, Shurahbil aliyekuwa akiungwa mkono na Warumi, aliandaa jeshi lililosemekana kuwa na watu laki moja, akazidi kulipa nguvu jeshi lake kwa kuajiri wanajeshi wengine laki moja kutoka kwa Waarabu wa Kikristo.[255]

Jeshi la Kiislamu lilikuja kugundua ukubwa wa jeshi la maadui baada ya kufika Syria. Baada ya kukabiliwa na hali hiyo ambayo hawakuwa wameitarajia hata kidogo, walifanya majadiliano. Kwa kuwa uwiano wa kijeshi ulikuwa tofauti sana, tofauti ambayo hawakuwahi kuishuhudia hapo kabla, wengi wakapendekeza kumtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu hali hiyo na wasubiri maelekezo yake. Walikaribia kufikia uamuzi wa kutuma taarifa kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ, ndipo Abdullah ibn Rawaha ؓ akazungumza:

"Hilo tunalosita kulifanya sasa ndilo lililotuleta hapa. Je tunapambana na adui kwa ubora wa idadi au nguvu? Hapana! Tunpambana kwa nguvu ya dini ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia.

254. Ibn Saad, II, 128.

255. Ibn Hisham, III, 429.

Sasa tunasubiri nini? Kinachotusubiri ni moja kati ya mambo mawili: kufa kishahidi au kupata ushindi!"

Hivyo Maswahaba walikubaliana kuingia vitani.

Zayd ibn Arqam ﷺ anaelezea:

"Nilikuwa yatima niliyokuwa nikitunzwa na Abdullah ibn Rawaha. Wakati wa kwenda katika Vita vya Mu'ta, alinikalisha upande wa mbele wa kiti cha ngamia wake. Baada ya kusafiri kwa muda fulani wakati usiku, nilimsikia akijinong'oneza kwa shairi lililokuwa na misitari isemayo: 'Ewe ngamia wangu! Nipeleke na unitue kwenye vituo vinne, mbele ya kisima kilicho jirani na mchanga, na kamwe sitakupanda tena kwenda kwenye vita vingine. Baada ya hapo utakuwa huru, na hakuna atakayekumiliki! Yaonekana kuwa sitarudi kwenye familia yangu! Kuuawa kishahidi ndio tumaini langu! Waislamu wamekuja na kuniacha katika ardhi ya Damascus, ambapo nina shauku ya kukaa milele! Sijali tena kuhusu mitende mibivu, iliyonyeshelezewa kwa mvua na zilizo jirani!'

Baada ya kumsikia, nilianza kulia. Abdullah ibn Rawaha ﷺ akanishtua kwa utaratibu na kusema: 'Mwanangu! Kuna ubaya gani kwa Mwenyezi Mungu kunipa kifo cha kishahidi nawe ukarudi na ngamia pamoja na mizigo yako? Nitakuwa nimepumzishwa na matatizo na shida za dunia!'

Usiku wa manane aliteremka kutoka juu ya ngamia wake na kuswali rakaa mbili. Baadaye aliomba dua ndefu, na baada ya dua hiyo akasema: 'In Shaa Allah, mara hii Mwenyezi Mungu atanijaalia kifo cha kishahidi!'" (Ibn Hisham, III, 431-432; Waqidi, II, 759)

Walipofika katika viunga vya kijiji cha Mu'ta, mahali ambapo maadui walikuwa wameweka kituo, Waislamu hao wachache wakiongozwa na Zayd ﷺ,bila kupoteza muda, walifanya shambulizi la kijasiri dhidi ya safu za maadui. Waislamu hao ambao walizitoa

nyoyo zao kuipa *tawhid*, sasa walikuwa kwenye ukingo wa kuyatoa maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu. Katikati ya mapambano makali yaliyoshtadi, Zayd ﵁, kipenzi cha Mtukufu Mtume ﷺ na ambaye alikuwa miongoni mwa Waislamu nane wa mwanzo waliosilimu mjini Makka, alipata jeraha kali sana lililotokana na kupigwa mkuki na adui na hivyo kufa kishahidi.

Kulingana na maelekezo ya Mtukufu Mtume ﷺ, hapo hapo Jafar ﵁ aliichukua bendere ya Waislamu na kushika uongozi wa jeshi. Alipambana kwa nguvu na kwa ushujaa mkubwa katikati ya safu za maaduina katika makabiliano makali yatakayoendelea kubaki katika kumbukumbu za historia alikumbwa na majeraha mengi ya panga, mikono yake miwili ilikatwa na kufa kishahidi muda mfupi baadaye.

Sasa ilikuwa zamu ya Abdullah ibn Rawaha ﵁ kushika uongozi wa jeshi. Akiwa na hamasa kubwa, aliinyakua bendera ya Waislamu na kupasua katikati ya wimbi la safu za maadui.

Aliwaambia wale waliokuwa karibu naye: "Shuhudieni ya kwamba vyote nilivyonavyo Madina ninaviacha katika Hazina (ya Waislamu)!"

Kisha alipambana kishujaa mpaka mwili wake ulipozidiwa na majeraha ya mikuki. Kufuatia kifo cha Abdullah ibn Rawaha ﵁, ilikuwa zamu ya Khalid ibn Walid ﵁ kuchukua bendera ya Waislamu na kuendelea kuongoza mapambano hayo ya kishujaa. Kundi dogo la Maswahaba lilikuwa likitoa upinzani mkali dhidi ya maadui waliokuwa wengi mno kama kundi la panzi.

Wakati vita vikiendelea, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekaa kwenye mimbari ya Msikiti wa Madina akiwataarifu Maswahaba kilichokuwa kikiendelea muda huo huo katika medani ya vita. Ilikuwa kana kwamba medani hiyo ya vita iko mbele ya macho yao.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwaakiwaeleza kwa sauati ya huzuni juu ya vifo vya kishahidi vilivyokuwa vikitokea katika uwanja wa Mutah, kimoja baada ya kingine:

"Zayd ibn Harithah amechukua bendera. Shetani amekuja haraka mbele yake ili kumfanya aipende dunia, ayachukie na kuyabeza mauti. Lakini Zayd anasema: 'Unajaribu kunifanya niipende dunia wakati ambapo ninatakiwa kuingiza imani ndani ya nyoyo za Waislamu!' Amesonga mbele na ameuawa. Muombeeni kwa Mwenyezi Mungu amsamehe na kumrehemu!"

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea:

"Sasa hivi anakimbiakimbia Peponi. Na sasa Jafar amechukua bendera.Shetani anakuja haraka mbele yake, anataka aione dunia ni tamu na kumfanya akichukie kifo na kukibeza. Lakini Jafar anamjibu: 'Sasa hivi ni zamu yangu kuingiza imani na uthabiti ndani ya nyoyo za Waislamu!' anasonga mbele, anapambana mpaka ameuawa kishahidi. Ninashuhudia kuwa ameuawa."[256]

"Muombeeni ndugu yenu rehma na maghfira", alisema na kuongeza: "Sasa hivi ameingia peponi kama shahidi, akiruka kwenda popote atakapo kwa mbawa mbili za rubi."

"Abdullah ibn Rawaha amechukua bendera kutoka kwa Jafar", alieleza Mtukufu Mtume ﷺ kisha akaingia katika kimya cha ghafla. Uso wa *Ansari*mmoja ulibadilika rangi, akidhani kuwa Ibn Rawaha amefanya jambo ambalo Mtukufu Mtume ﷺ hakulifurahia. Wakati

256. Ibn Omar ﷺ anasema: "Tulimtafuta Jafar na kumkuta katika waliouawa kishahidi. Tulihesabu takriban majeraha tisini na panga na mishale katika eneo la mbele la mwili wake. Hakuna hata jeraha moja lililokuwa upande wa nyuma." (Bukhari, Maghazi, 44) Wakati anauawa, alikuwa na umri wa miaka thelathini na tatu. (Ibn Hisham, III, 434) Hii ina maana kwamba alikuwa na umri wa miaka kumi na saba tu wakati anahamia Abyssinia na kumweleza mfalme Najashi maneno mazito yaliyokuwa yamejaa elimu, hekma na ujasiri.

huo, Abdullah ibn Rawaha ﷺ, katika medani ya Mu'ta, wakati akimuongoza farasi wake kuelekea upande wa maadui,alikuwa akipambana kuitiisha nafsi yake:

"Nimeapa kupambana nawe mpaka usalimu amri", alikuwa akiiambia nafsi yake. "Ima ukubali kwa hiari yako au nikulazimishe kutii! Ninaona kwamba hupendi Pepo! Hakika wewe sio chochote zaidi tone la maji katika chupa ambalo ni mwili! Ewe nafsi! Je utaweza kukikwepa kifo iwapo utaishi leo? Iwapo utachagua kufuata mambo mawili yaliyo mbele yako na kupata kifo cha kishahidi, utakuwa umechukua hatua sahihi! Lakini ukichelewa, utaishi katika sikitiko!"

Baada ya kujeruhiwa vibaya kwenye kidole chake, ambacho kilikuwa kikining'inia, Ibn Rawaha aliteremka kutoka juu ya farasi wake, akakiweka kidole hicho chini ya mguu wake na kusema:

"Hakika wewe si chochote bali ni kidole tu kinachovuja damu katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu", alisema kwa sauti ya kishairi, kisha akauvuta mkono kutoka kwenye mguu wake, akakiondoa kidole chake kilichokuwa kikining'inia. Kisha aliendelea kupigana. Wakati akishughulika na *jihad* ndogo dhidi ya maadui, wakati huohuo alikuwa amenasa katika *jihad* kubwa dhidi ya nafsi yake mwenyewe:

"Kama wasiwasi wako unatokana na kutengena na mkeo, basi tambua kuwa nimemuacha! Kama kukosa msaada wa watumishi wake ndicho kinachokuzuia, tabmbua kuwa nimewaacha huru! Au kama mashamba yako huwezi kuyaacha basi tambua kuwa nimeyaacha chini ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!"

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliendelea kuwapa Maswahaba taarifa mpya za kilichokuwa kikitokea katika medani ya mapambano:

"Abdullah ibn Rawaha amekusanya nguvu zake, amepambana na maadui akiwa na bendera mkononi na sasa ameuawa. Ameingia peponi akiwa na wasiwasi. Naye pia muombeeni maghfira na rehma ya Mwenyezi Mungu!"

"Ni wasiwasi gani huo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" aliuliza Ansari huyo ambaye alitaka kujua namna Abdullah alivyoingia Peponi.

"Alisita kupambana na adui baada ya kujeruhiwa. Kisha aliilaumu nafsi yake, akakusanya nguvu zake, akapambana na kuuawa kishahidi! Ameingia peponi. Nimeoneshwa wakiwa Peponi, wakiwa wamekaa kwenye viti vya dhahabu. Kiti cha Abdullah kilikuwa chini ya kila cha wenzake na kikiwa na matege. Nilipouliza sababu, niliambiwa , 'Abdullah alikuwa na shaka kabla ya mapambano!'"

Kwamba Abdullah alikuwa amekufa kishahidi na kuwa ameingia peponi vilimpa *Ansari* huyo sababu ya kufurahi.

Wakati akiendelea kutoa taarifa na habari za medani ya mapambano, Mtukufu Mtume ﷺ aliingiwa na huzuni na matone ya machozi yakaanza kudondoka kutoka machoni mwake. Kisha alisema: "Sasa benderea imechukuliwa na panga miongoni mwa panga za Mwenyezi Mungu...na matokeo yake Mwenyezi Mungu amewapa ushindi *mujahidun*." (Bukhari, Maghazi, 44; Ahmad, V, 299; III, 113; Ibn Hisham, III, 433-436; Waqidi, II, 762; Ibn Saad, III, 46, 530; Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, III, 237)

Kisha akiwa mwenye kujawa na machozi, Mtukufu Mtume ﷺ aliinyanyua mikono yake na kuielekeza kwenye milango ya Rehma za Mwenyezi Mungu na kuomba: "Ewe Mwenyezi Mungu...Khalid ni panga miongoni mwa panga zako. Mpe Msaada Wako!" (Ahmad, V, 299)



Umahiri, na Ujasiri wa Khalid ibn Walid kama Kamanda

Khalid ibn Walid ﷺ aliimudu vita kwa mbinu za kipekee mpaka jua lilipozama na majeshi pande zote mbili kuelekea katika kambi zao baada ya giza kuingia.Katikati ya giza nene la usiku, alibadilisha kabisa mpangilio wa jeshi la Kiislamu. Askari waliokuwa upande wa kulia aliwapeleka upande wa kushoto, wale wa kushoto akawapeleka kulia, wale waliokuwa mbele akawarudisha nyuma na wale waliokuwa nyuma akawapeleka kwenye msitari wa mbele kabisa. Ilipofika asubuhi, maadui walishikwa na bumbuwazi; walipoona nyuso mpya kabisa mbele yao, walishtuka, wakidhani kuwa jeshi la Waislamu liliongezewa nguvu wakati wa usiku. Khalid ibn Walid ﷺ, panga la Mungu, alikuwa na uhakika wa kutumia fursa hii ya kuwa na maadui waliockanganyikiwa mbele yake. Alianzisha shambulizi kali dhidi ya maaudui, ambao hawakuwa wametarajia kukabiliwa na shambulizi la nguvu kama hilo, wakashindwa kustahmili mawimbi ya *iman* yaliyoonesha ishara zote za kuwatu-

pilia mbali.Walianza kuonesha dalili za kushindwa na, ili kuchukua hatua za kiusalama, wakalazimika kurudi nyuma.

Khalid ibn Walid ؓ ambaye, siku hiyo panga tisa zilikatikia mikononi mwake,[257] naye alitumia fursa hiyo, akaliamuru jeshi la Kiislamu lirudi nyuma bila maadui kujua.Huu ni ushuhuda wa pili wa umahiri wake wa vita. Mbinu hiyo ilimaanisha kuwa majesho ya pande zote yaliondoka bila kupata ushindi. Khalid ؓ alimuda kulirejesha Madina jeshi la Kiislamu bila maafa mengi. Idadi ya waliokufa katika vita hivyo vilivyodumu kwa muda wa siku saba ni kumi na nne pekee. Kwa upande mwingine, maadui waliokufa walikuwa zaidi ya hao. Aidha, jeshi la Kiislamu liliweza kuleta ngawira. (Waqidi, II, 764, 768; Ibn Saad, III, 407)

Mtukufu Mtume ﷺ aliwaagiza Waislamu waliokuwa Madina '..kukusanyika na kwenda kuwapokea ndugu zao wanarejea nyumbani', ambapo Waislamu wote waliokuwa Madina waliungana na Mtukufu Mtume ﷺ wakimkokota ngamia wake, walivumilia joto kali na kukusanyika kwenda kuwapokea *mujahidun* hao. Kulikuwa na kundi la watoto wakimfuata Mtume ﷺ mwenye baraka. Alipowaona, aliwaagiza Waislamu wawachukue watoto wao na kuwaweka juu ya vikalio vya ngamia wao, naye akamchukua Abdullah, mtoto wa Jaafar ؓ na kumuweka juu ya ngamia wake. Abdulah alikaa juu ya ngamia wa Mtukufu Mtume ﷺ, kwa upande wa mbele wa kikalie. (Ahmad, V, 299; Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 244)

Mtukufu Mtume ﷺ aliyasifu mafanikio ya Khalid. Wale waliobaki Madina, ambao hawakuwa na utambuzi juu ya suala husika, walikuwa wakiwashutumu askari waliorudi kuwa wamekimbia vita. Mtukufu Mtume ﷺ aliwajibu:

257. Khalid ibn Walid ؓ anaapa: "Wallah, panga tisa zilikatikia mkononi mwangu Siku ya Vita vya Mu'tah. Upanga mkali uliotengnezwa Yemen ndiyo ulioweza kuhimili." (Bukhari, Maghazi, 44)

"Hakika wao si katika wale wanaokimbia kupigana vita katika njia ya Mwenyezi Mungu...bali ni wale wanaorudi nyuma na kujipanga kwa kushambulia tena na tena!' (Ibn Hisham, III, 438; Waqidi, II, 765).

Hakika, Vita vya Mu'tah vilishuhudia kikosi kidogo kikiliadhiri jeshi kubwa lenye idadi kubwa ya askari, kana kwamba ilitamathali ukweli unaoelezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu anaposema:

"Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kusubiri. (al-Baqara, 249)

Vita vya Mu'tah, ambapo Waislamu elfu tatu liliweza kulikabili jeshi madhubuti la askari laki mbili, ndio mwanzo wa mzozo mkali na Wakristo, Watu wa Kitabu.

Asma bint Umays, mke wa Jafar ﷺ, anaelezea:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alitujia pindi Jaafar na wenzake walipouawa. Siku hiyo, nilikuwa nimevipaka rangi vipande arobaini vya ngozi. Baada ya kuandaa vipande vyangu vya mkate, niliwaogesha wanangu, nikawachana nywele na kuzipaka mafuta.

'Wako wapi wanao, ewe Asma?' aliniuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nipowaita, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwakumbatia wote kwa hali ya huruma. Hapo hapo akaanza kumwaga machozi.

'Wazazi wangu wawe fidia kwako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mung; kwa nini unalia? Kwa nini waamiliana na wanangu kama ufanyavyo kwa yatima? Au umepokea habari mbaya kutoka kwa Jafar na wenzake?' nilimuuliza.

'Ndiyo' alijibu. 'Wameuawa leo...'

'Oh Jafar wangu', nililia na kuanza kuomboleza.

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimwambie binti yake, Fatmah, kuandaa chakula '...kwa ajili ya familia ya Jafar, kwani wameshughulishwa na yaliyowasibu leo!'

Chakula kililetwa nyumbani kwa muda wa siku tatu. Katika siku zote hizo tatu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakututembelea. Alifanya hivyo ili kutupa muda wa kupumua na kupumzika. Kisha alikuja na kutuambia, 'Msilie tena kwa ajili ya ndugu yangu! Kuanzia leo na kuendelea, nitawatunza na kuwaangalia watoto wake!'"

Abdullah, mtoto wa Jafar ﷺ, anasema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alituchukua kwa namna ya heshima na upendo, atakupelekea nyumbani kwake, kama makinda, na kisha akaagiza aletwe kinyozi. Kinyozi alikuja na kutukata nywele. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akanyanyua mikono yake na kuomba dua akisema; 'Mola wangu! Ninakuomba ipe kheri familia ya Jaafar na uwe mrithi wao! Ijaalie mikono ya Abdullah neema katika biashara!' aliomba dua hiyo mara tatu.

Mama yangu alipokuja, nilimuelezea jambo hilo. Alifurahi mno. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia, 'Usiwe na wasiwasi kuhusu maisha ya watoto hawa! Mimi ndiyemlezi wao hapa duniani na Akhera!' (Ahmad, I, 204-205; Abu Dawud, Tarajjul, 13/4192; Ibn Hisham, III, 436; Waqidi, II, 766; Ibn Saad, IV, 37)

Abdullah ibn Jafar ﷺ anaelezea kwa furaha jinsi Mtukufu Mtume ﷺ alivyokuwa akiwahurumia na kuwapenda:

"Ninakumba vyema. Siku moja, mimi na Qusam na Abdullah, watoto wa Abbas ﷺ, tulikuwa tukicheza mtaani, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitokea mbele yetu akiwa amepanda ngamia.

'Mpandisheni, mleteni kwangu', alisema kuwaambia wale waliokuwa mahali hapo akiniashiria mimi.

'Na yule pia', alisema kwa sauati ileile akimuashiria Qusam.

Japokuwa Abbas ﷺ, ami wa Mtume ﷺ, alikuwa na mapenzi makubwa kwa Abdullah kuliko Qusam, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakuhisi ubaya wowote kumpandisha Qusam. Kisha alikipapasa kichwa cha Qusam mara tatu, huku akimuombea:

'Mola wangu! Waangalie watoto wa Jafar!'"[258] (Ahmad, I, 205; Hakim, III, 655/6411)

Ushindi wa Ufunguzi wa Makka:
Haki Imekuja na Batili Imeondoka

Kwa mujibu wa Mkataba wa amani wa Hudaybiyah, uliosainiwa baina ya Waislamu wa Madina na Makafiri wa Makka, kipindi cha amani kingedumu miaka kumi. Hata hivyo, kila siku, hisia za ugumu zilikuwa zikipenya ndani ya nyoyo za makafiri, kwa kuona Uislamu ukiiweka Arabia yote chini ya udhibiti wake. Hivyo wakaanza kuhisi kuwa kuna haja ya kuvuruga vipengele vya masharti Mkataba huo, na kadiri muda ulivyosonga mbele, wakaanza kuonesha wasiwasi na kutoa ishara kuwa hawataweza kuendelea kushikamana na masharti hayo.Ilikuwa imepita miezi kumi na saba au kumi na nane pekee tangu Mkataba huo usainiwe, ndipo Makafiri wa Makka waliwashawishi washirika wao, kabila la Banu Bakr, kulishambulia kabila la Khuzaa, ambao ni Waislamu na ambao kwa mujibu wa Mkataba huo hawakutakiwa kuguswa kabisa. Baadhi

258. Mpokezi mmoja wa *hadith* anasema: "Nilimuuza Abdullah ibn Jafar 'Baadaye kitu gani kilimtokea Qusam?' Akasema: 'Alikufa kishahidi'. Nikasema, 'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanajua zaidi'. Akasema: 'Bila shaka'" (Hakim, III, 655/6411)

ya Maqurayshi walishiriki kikamilifu katika mashambulizi haya ya kinyama.[259]

Wakati wanashambuliwa, Khuzaa, ambao walikuwa wamekula kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume ﷺ, walikuwa wakitekeleza ibada ya swala. Baadhi walikuwa katika *sajdah*, baadahi katika rukuu, na wengine wakiwa katika *qiyam*, mauaji hayo ya kinyama yakayachukua maisha yao. Baadhi walifanikiwa kufika katika eneo la Haram, eneo takatifu ambalo hairuhusiwi kuuawa kiumbe hai chochote kwa matumaini ya kuyaokoa maisha yao. Lakini, Banu Bakr ambao walikuwa na ghadhabu, wakiwa pamoja na askari kadhaa wa Kiqurayshi waliwafuata na kuwaua bila huruma. Muda mfupi baadaye Mtukufu Mtume ﷺ alipata habari ya tukio hilo.[260]

Machozi yalikuwa yakitiririka bila kukoma kutoka katika macho ya Mtukufu Mtume ﷺ wakati akimsikiliza Amr ibn Salim رضي الله عنه akimfikisha taarifa ya janga hilo lenye kuumiza.Alihuzunika mno. Katika kumfariji Amr ibn Salim, alimwambia: "Utasaidiwa, ewe Amr!" (Ibn Hisham, IV, 12; Waqidi, II, 784-785)

Licha ya yote yaliyokuwa yametokea, kwa kutambua kuwa bado alikuwa na Mkataba na Makafiri wa Makka, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma mjumbe kwenda Makka kuhusu shambulizi lililofanywa dhidi ya Khuzaa. Vivyo hivyo, Maqurayshi walitakiwa kulipa fidia kwa watu wa Khuzaa waliouawa au kuwaondosha Banu Bakr katika ulinzi na hifadhi yao. Walikuwa wakijua vyema kuwa, kushindwa kutekeleza lolote katika mambo hayo kungepelekea kuvunjika kwa Mkataba wa Hudaybiyah.

259. Ibn Hisham, IV, 4; Bayhaqi, *Dalâil*, V, 6.

260. Ibn Hisham, IV, 11; Waqidi, II, 783.

Waabudu masanamu, wakiwa wamepumbazwa na chuki na tamaa ya kumwaga damu, walikuamua kuchagua jambo la mwisho: kuuvunja Mkataba.[261]

Hawakuwa wakijua kwamba kwa kufanya kwao hivyo walikuwa wakiwavutia Waislamu kuja kuifungua Makka.

Japokuwa Waabudu masanamu walikuja kushtuka muda mfupi baadaye, walikuwa wamechelewa sana, kwa sababu pande mbili zilikuwa zimeshaupatilisha rasmi Mkataba. Katika kutaka kurekebisha hali ya mambo, Abu Sufyan alifunga safari kwenda Madina akiwa mwenye kukata tamaa na kujawa na wasiwasi. Baada ya kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hapo hapo Mtukufu Mtume ﷺ akawataarifu Maswahaba kwamba Abu Sufyan ameondoka Makka kwenda kuurejesha Mkataba.[262] Waislamu mjini Madina, wakiwa bado na maumivu kutokana na mauaji ya kinyama yaliyofanywa dhidi ya Khuzaa, waliamua kutojishughulisha na Abu Sfuyan pindi atakapowasili; hata binti yake, Umm Habiba, mmojawapo wa wake watukufu wa Mtukufu Mtume ﷺ, aliuondosha mkeka pindi Abu Sfyan alipotaka kuukalia, jambo lililomshangaza sana.

"Mimi ndiye nisyestahiki mkeka au wenye ndio usiostahiki?" alimuuliza binti yake.

Bibi Umm Habibah, ambaye alikuwa amezama ndani ya upendo wa Mtukufu Mtume ﷺ alijibu: "Mkeka huu ni wa Mtume wa Mwenyezi Mungu; na wewe, kwa kuwa ni muabudu sanamu, hustahiki kukaa juu yake!"

Abu Sufyan alitishika mno na kusema: "Umebadilika mno tangu ulipoondoka kwetu."

261. Waqidi, II, 787.

262. Ibn Hisham, IV, 12.

Umm Habiba akajibu: "Hapana, bali Mwenyezi Mungu amenipa heshima na neema ya Uislamu!" (Ibn Hisham, IV, 12-13)

Msimamo uliooneshwa na Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba ulimaanisha kwamba Abu Sufyan hakuwa na njia nyingine zaidi ya kurudi Makka mikono mitupu. Alipofika Makka alizungukwa na waabudu masanamu waliokuwa na hamu kubwa ya kutaka kujua matokeo ya ziara yake. Wakati akijaribu kuwaelezea ukweli kwamba mkataba wa amani halikuwa jambo linalowezekana tena, Abu Sufyan alishindwa kuuzuia mshangao wake. Akasema:

"Nimetoka kwa watu ambao nyoyo zao ziko pamoja. Niamini ninapowaambia kuwa nilizungumza na wanaume, wanawake, vijana, wazee na kila niliyedhani kuwa angenisaidia... lakini yote ilikuwa kazi bure!" (Abdurrazzaq, V, 375)

Wakati huo huo, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaagiza Waislamu kujiandaa kwa ajili ya safari ya Makka. Aliyaita makabila ya jirani kuja Madina huku akiyataka yale yaliyokuwa mbali kubaki katika sehemu zao na kuungana na jeshi la Kiislamu wakati wa safari. Maandalizi makubwa yalifanywa kwa siri kubwa sana. Ili kuwazuia Makafiri wa Makka kuwa na shaka, Mtukufu Mtume ﷺ alituma kikosi kidogo kwenda Syria. Maeneo yote yalikuwa chini ya udhibiti mkali. Kwa msaadawa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mtume Mtukufu ﷺ aliendelea na mipango yake ya kuinyakua Makka bila kumwaga hata tone moja la damu. Ili kufanikisha hilo halichukua hatua kadhaa za kimkakati:

Kwanza, japokuwa Mtukufu Mtume ﷺ aliwaagiza Maswahab kujiandaa kwa ajili ya vita, hakuainisha sehemu husika, na hivyo nia yake kubaki kuwa siri.[263] Hata rafiki yake na mtunza siri wake mkubwa, Abu Bakr ؓ, hakujua kama vita hiyo itakuwa Makka na kumuuliza binti yake Aisha ؓ, mke wa Mtume ﷺ, juu ya eneo

263. Ibn Saad, II, 134.

husika. Lakini, naye, kama ilivyokuwa kwa baba yake, alikuwa hajui kabisa:

"Sijui", alisema. "Labda anataka kwenda kwa Banu Sulaym au Thaqif au hata ikiwezekana Hawazin!" (Ibn Hisham, IV, 14)

Katika kuhakikisha kwamba ufunguzi wa Makka unafanyika kwa amani, Mtukufu Mtume ﷺ alihakikisha njia zote za kuingia Madina zinakuwa chini ya upelelezi na uchunguzi, ili waabudu Masanamu wasigundue kuhusu maandalizi ya Waislamu, na wakiingiwa na shaka wataanza kujiandaa. Vivyo hivyo, alichukua hatua dhidi ya wapelelezi wenye kupeleka Makka habari za maandalizi hayo. Aliomba dua akisema:

"Mola wangu! Wadhibiti wapelelezi wa Maqurayshi, wafanye kuwa viziwi na vipofu, mpaka tutakapoivamia ardhi yao kwa ghafla! Ondoa nuru ya macho yao ili ghafla wanione nikiwa mbele yao!" (Ibn Hisham, IV, 14)

Hatimaye jeshi la Kiislamu lilipoondoka Madina, ili kuwazubaisha tena Makafiri, Mtukufu Mtume ﷺ aliliongoza kuelekea upande mwingine, ambapo walisimamishwa na washirika wao. Hatua ya kupitia njia ya mzunguko ilizidi kuwachanganya watu juu ya eneo hasa linalokusudiwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Walipofika eneo ambalo mtu huweza kuiona Makka kwa macho, Mtukfu Mtume ﷺ aliagiza kila askari kuwasha moto katika eneo lake peke yake ili kuonesha kuwa walikuwa wengi kuliko ilivyofikiriwa na Maqurayshi.[264] Vivyo hivyo, wakati wa kuingia Makka, jeshi la Waislamu halikupitia Dhulhulayfa, eneo la *miqat* lililo katika njia ya kuelekea Makka, na hivyo Mtume ﷺ kuendelea kuufanya mwisho wa safari kuwa siri.[265]

264. Hamîdullâh, I, 264-265.

265. Nebî Bozkurt, *DİA*, "Mekke" ingizo XXVIII, 557.

Mtukufu Mtume ﷺ alipopata ushindi hakuutumia vibaya kwa kuua watu na kutwaa ardhi zao kwa nguvu. Badala yake aliutumia kuzifungua nyoyo zao kumuelekea Mwenyezi Mungu na kuwaonesha furaha na uongofu wa kweli. Kwa sababu yeye ni Mtume mwenye Huruma aliyetumwa kuwa rehma na muongozo kwa walimwengu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu, anaielezea tafsiri ya Uislamu ya vita na amani katika aya ifuatayo:

الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنكَرِ وَلِلَّهِ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ

"Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Sala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote." (al-Hajj, 41)

Wakati Maswahaba wote wakiendelea kufanya siri ya eneo wanalokwenda, Khatib ibn Baltaa, aliyewahi kushiriki vita vya Badr, alipogundua aliandika barua kwenda Makka, kwa kumtumia mwanamke fulani, akiwataarifu kuhusu hali hiyo. Mtukufu Mtume ﷺ akapata taarifa ya tukio hilo kwa njia ya ufunuo, akawaagiza Ali, Zubayr, na Miqdad ﷺ kwenda kumkamata na kumleta mwanamke huyo mbele yake, akawaambia mahali alipokuwa. Walikamatwa akiwa sehemu ileile iliyoelezwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Barua hiyo ilisema:

"Enyi Maqurayshi! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakuja na jeshi kubwa, lenye kutisha kama usiku wa giza, ambalo litamiminika kama damu. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, hata kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu angekuja pekee yake, Mwenyezi

Mungu angempa ushindi na kutimiza ahadi Yake. Kuweni makini na kuchukua tahadhari kuanzia sasa!" (Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 278)

Kwa kweli, maneno haya hayakuwa kinyume na ukweli na wala hayakuwa na pendekezo la uhaini na usaliti. Lakini ilimaanisha kuwa maadui wametaarifiwa juu ya safari ambayo ilitakiwa iendelee kuwa siri. Hivyo Mtukufu Mtume ﷺ alimuita Khatib na kumuuliza:

"Kwa nini umefanya hivi Kahtib?"

Khatib akaeleza huku akiwa amejawa na wasiwasi: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, *Muhajirun* wote wana watu wanaoziangalia familia na mali zao mjini Makka. Lakini mimi sina mtu yeyote. Kwa kuwaandikia barua, nilidhani kuwa ningeweza kutambulika kwao na hivyo wakamlinda mke na watoto wangu walioko huko. Kinyume na hivyo Wallah mimi sio mpelelezi ninayewafanyia kazi. Siwezi kuukubali ukafiri baada ya kuwa nimeshaukubali Uislamu. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, *iman* yangu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake haina mipaka. Sijabadilisha dini...siwezi kamwe kufanya hivyo!"

Mtukufu Mtume ﷺ, bahari ya huruma, alimsamehe na kusema: "Utetezi wa Khatib ni wa haki." Kisha alimkumbusha Omar رضي الله عنه, ambaye alitaka Khatib auawe kwa usaliti, juu ya msamaha wa jumla uliotolewa na Mwenyezi Mungu kwa wale wote walioshiriki katika Vita vya Badr. Alimwambia: "Alikuwepo katika Vita vya Badr. Yumkini usijue; huwenda ndo maana Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kujua hali yao, akasema, 'Fanya utakavyo; nimekusamehe!'" (Bukhari, Maghazi, 9; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 161)

Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kusema hayo, aliwafikishia Maswahaba wote madhara ya kuwa na urafiki na maadui wa Mwenyezi Mungu, akianza hasa na Khatib, kupitia aya ifuatayo iliyokuwa imeteremka wakati huo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمْ أَوْلِيَاء تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا بِمَا جَاءكُم مِّنَ الْحَقِّ يُخْرِجُونَ الرَّسُولَ وَإِيَّاكُمْ أَن تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ رَبِّكُمْ إِن كُنتُمْ خَرَجْتُمْ جِهَادًا فِي سَبِيلِي وَابْتِغَاء مَرْضَاتِي تُسِرُّونَ إِلَيْهِم بِالْمَوَدَّةِ وَأَنَا أَعْلَمُ بِمَا أَخْفَيْتُمْ وَمَا أَعْلَنتُمْ وَمَن يَفْعَلْهُ مِنكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاء السَّبِيلِ إِن يَثْقَفُوكُمْ يَكُونُوا لَكُمْ أَعْدَاء وَيَبْسُطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ وَأَلْسِنَتَهُم بِالسُّوءِ وَوَدُّوا لَوْ تَكْفُرُونَ لَن تَنفَعَكُمْ أَرْحَامُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

"Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni, wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu. Mnapotoka kwa ajili ya Jihadi katika Njia yangu na kutafuta radhi yangu, mnafanya urafiki nao kwa siri, na Mimi nayajua mnayo yaficha na mnayo dhihirisha. Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa. Wakikuwezeni wanakuwa maadui zenu, na wanakukunjulieni mikono yao na ndimi zao kwa uovu. Na wanapenda muwe makafiri. Hawatakufaeni jamaa zenu, wala watoto wenu Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu atapambanua baina yenu, na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda." (al-Mumtahinah, 1-3)[266]

Aya hizo zilikataza kufanya urafiki na makafirikutoka katika mambo yanayohusiana na familia au mali. Mtoto wa Nabi Nuh عليه السلام, Kan'an, aliangamia kwa sababu ya kuendelea kuwa miongoni mwa

266. Bukhari, Tafsir, 60.

makafiri. Mke wa Lut ﷺ alijisababishia maangamizi kwa sababu kuwa pamoja na wale waliolaaniwa na hivyo akakumbwa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Hatimaye, ukaribu wao wa kimaada na Mitume hao haukuwasaidia hata kidogo.

Katika mwaka wa nane wa Hijra, tarehe kumi ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Mtukufu Mtume ﷺ aliliongoza jeshi lake kubwa la Waumini madhubuti elfu kumi kutoka Madina. Alipokuwa safarini katika mapambano kwa ajili ya Mwenyezi Mungu alifungua swaumu yake na kuwaamuru Waislamu kufanya hivyo.[267]

Walipofika jirani na Juhfah, walikutana na Abbas رضي الله عنه, ambaye mpaka wakati huo alikuwa akiwaficha Maqurayshi juu ya Uislamu wake na kubaki Makka, alikuwa akimtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ aliyekuwa mjini Madina juu ya hali iliyokuwa ikiendelea mjini Makka. Sababu nyingine ya kubaki kwake Makka ni kazi ya kutoa huduma ya maji kwa mahujaji, kazi aliyokuwa amekabidhiwa kuifanya. Alipoona kuwa sasa muda umewadia, aliondoka Makka pamoja na familia yake kwa ajili ya kukamilisha Hijra yake aliyokuwa akiisubiri kwa muda mrefu.[268] Mtume ﷺ alikuwa na furaha mno kwa kumuona:

"Kama ambavyo mimi ni mtume wa mwisho, nawe ni *muhajir* wa mwisho", alisema. (Ali al-Muttaqi, XI, 699/33387)

Safari hii yenye kuvutia ya kwenda kuifungua Makka pia ilishuhudia tukuo tukufu la huruma, na athari ya mfano inayotakiwa kufuatwa na wanadamu wote. Ilikuwa ni kielelezo kamilia cha kumtazama kiumbe kupitia jicho la Muumba. Jeshi la Mtukufu Mtume ﷺ lilikuwa likitembelea kama mafuriko makubwa. Makabila yaliyomiminika kutoka kona zote nne za Arabia yalikuwa yakiungana na jeshi la Kiislamu makundi wa makundi na kuongea ukubwa

267. Bukhari, Maghazi, 47.
268. Ibn Hisham, IV, 18.

wa kundi umati huo ambao haukuwahi kushuhudiwa hapo kabla. Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiongoza jeshi lake kubwa kutoka Arj kwenda Talub, alimuona mbwa ambaye alikuwa amejilaza akiwanyonyosha watoto wake. Haraka sana akamuita Juayl ibn Suraqa na kumuagiza asimame kumlinda mbwa yule na vitoto vyake, akamuamuru ahakikishe kuwa hakuna mtu atakayefanya hata jambo dogo la kuwashitua na kuwaogofya.[269]

Ajabu iliyoje! Nani aliyewahi kuona huruma ya namna hii katika historia ya mwanadamu?[270]

Hata wakati wa tukio kubwa kihistoria kama ufunguzi wa Makka, Mtukufu Mtume ﷺ alijishughulisha na kile ambacho wengi wangekichukulia kuwa kisichokuwa na maana na kujihesabu kuwa mwenye kuwajibika kwa usalama na ustawi wa mbwa na vitoto vyake. Funzo na somo linalopatikana hapa linawahusu wale wenye nafasi za kiutendaji; wanatakiwa kuwa na hisia ya uwajibikaji katika kutekeleza kila jambo katika majukumu yao na kuwa tayari kwa lolote linaloweza kuwatokea kuhusiana na hilo.[271]

---

269. Waqidi, II, 804.

270. Hata hivyo, wapinzani bado wanauhusisha Uislamu na ugaidi, ambalo ni janga la mwanadamu wa zama hizi. Ugaidi na machafuko ni mambo yaliyojengwa kwenye ugumu wa moyo, bila hata chembe ya maadili. Tangu kudhihiri kwake, Uislamu, kwa upande mwingine, umekuwa na msimamo imara dhidi ya ugaidi na vurugu na umeufanya msimamo huo kuwa kipaumbele cha kulinda haki za viumbe wote, Waislamu na wasiokuwa Waislamu, na hata viumbe visivyokuwa na uhai. Kimsingi, miaka ishirini na tatu ya utume wa Mtukufu Mtume ﷺ imekuwa ni ya kupambana na ugaidi.

271. Malenga Mehmet Akif Ersoy anapaza sauti tamu kuhusu hisia adhimu ya Omar رضي الله عنه kuhusu uwajibikaji wa kiutawala:
Kama mbwa mwitu angemkamata kondoo kando yam to Tigris,
Omar ndiye angehesabiwa na kuwajibishwa na mahakama ya Mwenyezi Mungu,
Kikongwe wa kike aliyeachwa na upweke…Omar ndiye angelaumiwa!

Wakati huo huo, Makafiri wa Makka hawakuwa na habari yoyote juu ya kilichokuwa kikiendelea. Hivyo walishikwa na bumbuwazi baada ya kusikia kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekuja na jeshi kubwa na alikuwa ameweka kambi katika Bonde la Marr'uz-Zahran jirani na Makka, wakazidi kutishika zaidi waliposhuhudia moto uliokuwa umewashwa na vikosi vya Waislamu kwa amri ya Mtukufu Mtume ﷺ. Akili zao zilistaajabu.

Abu Sufyan, akiandamana na Hakim ibn Hizan na Budayl, alitoka Makka kwenda kushuhudia kile kilichokuwa kikiendelea. Muda mfupi walikutana na moto mkubwa uliokuwa umewashwa na wanajeshi wa Kiislamu. Mwanzo walijaribu kukisia ni askari gani hao walioweka kambi, huku wakiwa hawana hisia hata kidogo kuwa waliokuwa wakiwashudia mbele yao ni Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba zake. Baada ya Makka kuzungukwa pande zote, Abu Sufyan na wenzake hao wawili, walitiwa nguvuni na muda mfupi baadaye wakaletwa mblele ya Mtukufu Mtume ﷺ.[272]

Wakati Omar ؓ akimuomba ruhusa Mtukufu Mtume ﷺ amkate shingo Abu Sufyan, Abbas ؓ, ami wa Mtme ﷺ, alikuwa akisisitiza kuwa asamehe. Lakini badala yake, Mtukufu Mtume ﷺ, kwa kutumia umahiri wake wa kisiasa kwa mbinu za kisaikolojia,

---

Yatima waliotokomezwa na maafa…Omar ndiye wa kulaumiwa!
Kiota cha umaskini kilichopuuzwa kubomoka,
Ni Omar tena, si mwinginewe, atakayeachwa chini ya kifusi chake
Pindi mtu anapomwaga tone la damu kwa kufanya khiyana,
Tone hilo moja huibuka kumzamisha Omar katika mafuriko yake,
Omar husikika katika kila vunjiko la moyo,
Omar hutoonekana katika kila majonzi,
Omar anapokuwa Khalifa, nani mwingine wa kulaumiwa?
Ewe Mola, Omar anaweza kufanya nini pindi mtu anapokuwa dhalimu na mlemavu,
Kitakachotakiwa kwa Omar ni kile kilichotarajiwa kufanywa na Muhammad,
Omar, ewe Omar…mzigo huu uliwezaje kutulia mabegani mwako?

272. Bukhari, Maghazi, 48.

alimwambia ami yake, Abbas, kuwa, "Mpeleke Abu Sufyan mahali anapoweza kuliona jeshi la Uislamu likipita na muache astaajabia ukubwa wake!"

Hatua hii ilikuwa ni kuhakikisha kuwa kiongozi huyo wa Maqurayshi anaigiwa na hali itakayomshawishi kwamba maandalizi yoyote yatakayofanywa dhidi ya Waislamu, baada ya hatua hiyo, yatakuwa si chochote. Hivyo, iwapo Makafiri hawataonesha upinzani wowote, kutakuwa na uhakika wa kuzuia umwagikaji wa damu.

Katika kufanyia kazi ushauri wa Mtume ﷺ, Abbas رضي الله عنه alimchukua Abu Sufyan na kumpeleka mahali ambapo anaweza kulishuhudia jeshi la Kiislamu kwa macho yake na kwa uwazi kabisa. Jeshi lilikuwa limeanza kutembea na kusonga mbele katika vikosi mbalimbali. Sauti za *Allah Akbar* kutoka ndani ya vifua vya *iman* zililitetemesha anga.

Abu Sufyan alishtuka mno. Pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipokuwa akitembea mbele ya kikosi chake, Abu Sufyan alishindwa kujizuia na kuutoa mshangao wake, "Ewe Abbas, ukubwa ulioje wa ufalme ambao mtoto wa nduguyo amejijengea!"

"Huu sio ufalme", alijibu Abbas, "huu ni utume!"

"Kweli, kweli..."ndiyo maneno aliyoweza kuyatamka Abu Sufyan. (Bukhari, Maghazi, 48;

Haythami, VI, 164; Ibn Saad, II, 135; Ibn Athir, al-Kamil, II, 242)

Wote wawili walirudi kwa Mtukufu Mtume (s.a.wa), ambaye baada ya kumtazama Abu Sufyan alimuuliza: "Haujafika muda wa kusema *La ilaha illa Allah*?"

Baada ya kutafakari kidogo, Abu Sufyan alirudia kutamka maneno hayo ya tawhid, bila kuongezea kipande kinachothibitisha

kuwa ameukubali utume wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Hivyo, akamuuliza tena:

"Je muda haujafika kwako kukubali kuwa mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"[273]

Ingawa Abu Sufyan aliomba muda wa kufikiria, kutokana na shinikizo la Abbas ؓ, aliyatamka kikamilifu maneno ya *shahaadah*. Ili kuzidi kuuvuta moyo wake kikamilifu na kuukumbatia Uislamu, Mtukufu Mtume ﷺ aliielezea nyumba ya Abu Sufyan kuwa miongoni mwa maeneo salama kwa wakazi wa Makka, pindi jeshi la Kiislamu lilipoingia mjini:

"Mwenye kuingia *Masjid'ul-Haram* anatakuwa salama. Atakayebaki ndani ya nyumba yake atakuwa salama. Na mwenye kukimbilia katika nyumba ya Abu Sufyan atakuwa salama!" (Abu Dawud, Kharaj, 24-25/3021-3022; Haythami, VI, 164-166; Ibn Hisham, IV, 22)

---

273. Kupitia tangazo lifuatalo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur'an Tukufu:

قُلْ أَطِيعُواْ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنَّ اللَّهَ لاَ يُحِبُّ الْكَافِرِينَ

"Sema: Mt›iini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri" (Al-I Imran: 32) tunapata kuelewa kuwa *iman* ya kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumtii peke yake havitoshi. Wale wanaomuamini na kumtii Mwenyezi Mungu peke yake na kumuacha Mtume Wake, au kinyume chake, wanaelezewa na aya hiyo kuwa hawamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jambo la muhimu ni mtu kuifanya imani yake iafikiane na Matakwa na Amri ya Mwenyezi Mungu, badala ya uelewa wake wa kimakosa.

Kwa muktadha huu, Mwenyezi Mungu Mtukufu alipompa Mjumbe Wake daraja hii na kueleza wazi kuwa kumtambua na kumtii Mtume Wake ni nguzo ya imani, utawaona watu wajinga wakidai kuwa Qur'an pekee yatosha na kwa kisingizio kitokanacho na uelewa wao finyu, huzikanusha Sunnah za Mtukufu Mtume ﷺ.

Wakati Abu Sufyan akirejea Makka baada ya kuachiwa huru, Mtume wa Allah alimpa amri yake ya mwisho:

"Usitoe upanga wako mpaka utakaposhambuliwa!" (Ibn Hisham, IV, 28)

Muda mfupi baadaye, Mtukufu Mtume ﷺ aliliamuru jeshi la Kiislamu, ambalo alikuwa ameshaligawa katika makundi manne, kusonga mbele. Makka ikaanza kuzizima kwa sauti za *Allah Akbar* zikihanikiza kutoka pande zote.

Miaka nane baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kulazimishwa kuondoka Makka, akiwa dhalili na akiwa amesindikizwa na watu wawili tu na ngamia wawili, sasa kwa neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa amerudi kwenye ardhi hiyo tukufu akiwa amesindikizwa na jeshi kubwa la Waislamu elfu kumi. Mtu aliyeteswa na kubughudhiwa vibaya sasa alikuwa ameibuka mshindi katika ardhi yake ya nyumbani. Lakini bila kuyaruhusu majivuno kumteka, alingia Makka akiwa juu ya ngamia, akizama katika hali ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyemjaalia neema hii kubwa. Alikiinamisha kichwa chake kwa unyenyekevu kiasi kwamba ndevu zake zilikuwa zikigusa kikalio cha ngamia wake. Wakati huo huo, alikuwa akirudiarudia kusema, "Ewe Mwenyezi Mungu...Maisha ya kweli ni maisha ya Akhera!"[274] (Waqidi, II, 824; Bukhari, Riqaq,1) Hali hiyo hiyo ndiyo waliyokuwa nayo Maswahaba, ambao walipata mafunzo chini ya maadili ya Mtume ﷺ.

---

274. Katika zama za uhai wake, Mtukufu Mtume ﷺ alionekana akiirudiarudia sana dua hii, jambo linaloonesha uzito wa maisha ya Akhera yakilinganishwa na maisha ya dunia. Miongoni mwa matukio ambayo aliomba dua hii ni wakati wa ujenzi wa *Masjid'un-Nabawi*, wakati wa kuchimba mahandaki kabla ya Vita vya Khandaq, wakati akiingia Makka siku ya Ufunguzi na wakati wa hijja ya mwisho pindi alipoona idadi kubwa ya Waumini mbele yake. (Tazama: Bukhari, Jihad 33, 110, Manaqib'ul-Ansar 9, Maghazi 29; Muslim, Jihad, 126, 129; Tirmidhi, Manaqib, 55; Ibn Majah, Masajid, 3)

Jeshi la Kiislamu takriban halikukutana na upinzani. Mbinu zilizotumika kwa Abu Sufyan zilizaa matunda; aliporejea Makka, aliwashawishi Maqurayshi kuwa hapakuwa na msingi wa kufanya upinzani na matokeo yake hakuna mtu aliyethubutu kuanzisha mapambano. Kulikuwa na mzozo kidogo tu katika njia aliyopita Khalid ibn Walid ﵁ wakati akiingia mjini lakini hali hiyo ilidhibitiwa haraka sana.

Akisoma *surah al-Fath*, Mtukufu Mtume ﷺ aliikaribia Kaabah akiwa pamoja na Maswahaba zake. Bila kuteremka juu ya ngamia wake, aliizunguka Nyumba hiyo Tukufu na kusoma aya ifuatayo:

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ

"Na sema: Kweli imefika, na uwongo umetoweka..." (al-Isra, 81). Yeye mwenye alianza kuyapindua na kuyaharibu kabisa masanamu yaliyokuwa yamewekwa ndani ya Kaabah, kwa kutumia fimbo iliyokuwa mkononi mwake. (Bukhari, Maghazi, 48; Muslim, Jihad, 87; Waqidi, II, 831-832)



Alipoona picha ndani ya kuta za Kaabah, mwanzo Mtukufu Mtume ﷺ hakuingia, bali alitoa amri ya kufutwa kwa picha hizo. Maswahaba wakatekeleza amri hiyo mara moja. Ndani, kulikuwa

na picha za Ibrahim na Ismail عليه السلام wakiwa ameshika vishale mikononi mwao. Alipoziona, Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Mwenyezi Mungu awaangamize waabudu masanamu walioyachora haya...Wallah Mitume hawa kamwe hawakutafuta bahati na ushindi wao kwa vishale!" (Bukhari, Anbiya, 8; Hajj, 54, Maghazi, 48)

Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu amrehemu – anaelezea kuwango cha shukrani tunayopaswa kuwa nayo kwa Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye kwa kipindi chote cha uhai wake alivumilia tabu na shida kubwa ili kuyavunja masanamu na kuondosha dhulma:

"Ewe ambaye leo hii unafurahia kuwa Muislamu; tambua kuwa kama si juhudi kubwa za kipenzi chetu Ahmad, na azma yake katika kuyavunja masanamu, nawe pia ungekuwa muabudu sanamu kama wahenga wako."

Siku hiyo ambayo Waislamu waliifungua Makka na kuiweka chini ya udhibiti wao, waliendelea kuizunguka Kaabah mpaka Asubuhi huku wakihanikiza kwa sauti za *Allah Akbar*. Akiwatazama kutokea mbali, Abu Sufyan alimnong'oneza mkewe, Hind, "Unaamini kuwa hili linatoka kwa Mwenyezi Mungu?"

"Ndiyo", Hind alijibu. "Haya hayawezi kutoka kokote isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu!"

Asubuhi mapema ya siku iliyofuata, Abu Sufyan alimtembelea Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye alimsimulia Abu Sufyan mazungumzo yaliyotokea baina yake na Hind. Abu Sufyan aliposikia hivyo akasema:

"Ninashuhudia kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, hakuna aliyesikia nilichosema isipokuwa Mwenyezi Mungu na Hind!" (Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 296)

Wakti huo huo, watu wa Makka walikuwa wakiwapeleka watoto wao kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ambaye alikuwa akiwapapasa vichwa vyao na kuwaombea kheri na ustawi. (Ahmad, IV, 32)

Siku ya Usamehevu

Wenyeji wa Makka walikuwa wamesongamana ndani ya *Masjid'ul-Haram*, wakisubiri kwa hamu kujua hukmu na hatma yao. Mtukufu Mtume ﷺ alitoa hotuba fupi, ambayo sio tu kwamba iliwahusu Maqurayshi bali pia iliwahusu wanadamu wote:

"Hakuna Mungu apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Mmoja na wa pekee. Hana mfano wala mshirika. Mwenyezi Mungu ametimiza ahadi Yake, amemnusuru mja Wake na amewashinda maadui wetu. Mila na matendo yote ya zamani, ukabaila na unyonyaji, yote yapo chini ya miguu yangu (yaani vimefutwa), isipokuwa kuihudumia Kaaba na kuwahudumia mahujaji kwa maji.

Enyi Maqurayshi...!

Allah amekuondosheni katika majivuno ya Kijahiliya, ya kujifakaharisha kwa nasaba na koo. Watu wote wameumbwa kutokana na Adam, naye Adam ametokana na udongo."

Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisoma aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ
لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

"Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwe-

nyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari." (al-Hujurat, 13)" (Ibn Majah, Diyat, 5; Ahmad, II, 11; Tirmidhi, Tafsir, 49/3270)

Kwa kupata fath (ufunguzi wa) ya kiroho ikiambatana na usamehevu, amani, usalama na muongozo, kama ilivyoahidiwa katika Mkataba wa Hudaybiyyah, sasa Makka ilikuwa imefungua moyo wake kwa ajili ya wakazi wake halisi, jamii yake kipenzi. Maumivu na kulalama kulikotokana na kutengenishwa na Makka sasa vilikuwa vimefikia kikomo. Miaka ya machungu sasa ilikuwa imefungua njia ya furaha. Katika kuonesha furaha kwa safari hii ya kurejea, muda mfupi kabla ya kutangaza msamaha mkubwa kabisa katika historia, Mtukufu Mtume ﷺ aliwauliza Maqurayshi:

"Enyi Maqurayshi, mnadhani nitawafanya nini?"

"Tunataraji kheri na wema kutoka kwako... hivyo tunasema kuwa hutatufanyia ila kheri. Wewe ni ndugu mkarimu na mwana wa ndugu nkarimu!"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu, "Kama Yusufu alivyosema kuwa-ambia ndugu zake, nami pia ninasema:

لاَ تَثْرَيبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

'Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu.' Nendeni, nyote mko huru!"

Mahali pengine alisema: "Leo ni siku ya huruma. Leo ni siku ambayo Mwenyezi Mungu atawapa nguvu na kuwainua Maqurayshi kwa Uislamu."

Matokeo ya hatua hiyo, hata wale waliokuwa na damu ya Waislamu wengi mikononi mwao kabla ya ufunguzi wa Makka waliingia

katika Uislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliwaweka Maquraysh katika huruma ya Mtume Wake na kuwafanya warejee kwake. Hapo, Mtukufu Mtume ﷺ akawasamehe na kuruhusu waachiwe huru. Tokea siku hiyo, wenyeji hao wa Makka wakajulikana pia kama *tulaqaa*, yaani watu walioachiwa huru.[275]

Raghba kubwa kabisa ya Mtume ﷺ ilikuwa ni kuona wanadamu wote, kwa ujumla wao, wanaukubali Uislamu bila kubaki mtu hata mmoja. Wakati alipokuwa katika kilele cha madaraka, licha ya kuwa na haki ya kufanya kisasi kwa wale waliomtesa vikali yeye na Maswahaba zake, Mtukufu Mtume ﷺ alitangaza msamaha rasmi, ikiwa ni kielelezo na dhihirisho la ajabu kabisa la namna alivyowatazama viumbe kwa jicho la huruma la Muumba.

Mji wa Makka ambao hapo awali ulishuhudia uonevu, istihzai na uadui kwa miaka mingi, sasa ulikuwa ukifurahia upepo mwanana wa upendo na huruma uliotokana na msamaha uliotolewa na Mtukufu Mtume ﷺ. Lakini mkazi mmoja wa Makka aitwaye Fadala, akiwa na nia ya kutia wingu jeusi juu ya siku hii ya furaha, alimkaribia Mtukufu Mtume ﷺ kwa lengo la kumuua. Lakini, Mtukufu Mtume ﷺ aliielewa hiyo nia chafu mapema kabisa, bila kuonesha ishara yoyote ya kuhamaki au hasira, akatandaza mbawa zake za huruma kwa Fudala na kumwambia huku akiwa ameuweka mkono wake mtukufu juu ya kifua cha Fadala:

"Tubu ewe Fadala kutokana na njama iliyo akilini mwako!" Tokea hapo, nia hiyo chafu ikatoweka kabisa katika akili ya Fadala; moyo wake ukasafika na kujaa nuru ya *iman*. Ghafla, Mtukufu Mtume ﷺ akawa ndiye mtu kipenzi zaidi kwake kuliko kiumbe mwingine yeyote. (Ibn Hisham, IV, 37; Ibn Kathir, as-Sirah, III, 583)

Abu Sufyan alikuwa amekaa pembezoni mwa Kaabah, akitafakari na kupima mawazo yake. Wazo la kukusanya upya jeshi dhidi

275. Tazama: Ibn Hisham, IV, 32; Waqidi, II, 835; Ibn Saad, II, 142-143.

ya Mtukufu Mtume ﷺ na kupambana naye lilimjia akilini mwake, hasa baada ya kuwaona Waislamu wakitembea kwa ukakamavu na kwa wingi nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alilifutilia mbali wazo hilo pale Mtukufu Mtume ﷺ, bila kujua, alipokuja na kukaa nyuma yake; akampigapiga kwa nyuma, baina ya mabega yake, akamwambia, "...Hapo ndipo Mwenyezi Mungu atakapokutweza na kukudhalilisha!"

Abu Sufyan alipoinua kichwa chake akamuona Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amesimama jirani naye, akasema: "Mpaka wakati huu nilikuwa sijatambua kuwa wewe ni Mtume; na sasa, ninatubia kwa Mwenyezi Mungu kwa mawazo yaliyonipitia akilini mwangu na ninaomba msamaha Wake!" (Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 296)

Bibi Hind, ambaye aliwahi kuyatumbukiza meno yake katika ini la Hamza ؓ baada ya Vita ya Uhud, naye pia alisilimu siku hiyo ya Ufunguzi wa Makka, na hivyo kufurahia fungu lake katika msamaha wa jumla uliotolewa na Mtukufu Mtume ﷺ. Alisamehewa na Mtukufu Mtume ﷺ kwa sababu ya heshima la tamko la *tawhid*.[276]

Ikrimah, mtoto wa Abu Jahl, ambaye alikuwa miongoni mwa maadui wakubwa kabisa wa Uislamu, alikimbilia Yemen baada ya jeshi la Waislamu kuingia Makka. Hatimaye, mkewe alimleta mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ akiwa ameshasilimu. Mtume wa Rehma ﷺ alimpokea kwa amani na kwa namna ya urafiki. "Karibu ewe mzururaji mwenye kupanda farasi" alisema kwa furaha pasipo kumshutumu kwa makosa na uhalifu aliowahi kuufanya dhidi ya Waislamu. (Hakim, III, 271/5059; Waqidi, II, 851-852)

276. Waqidi, II, 850.

Kama ilivyokuwa kwa Ikrimah, Habbar ibn Aswad naye alikuwa miongoni mwa maadui wakubwa kabisa wa Uislamu. Kwa kutumia mkuki wake, alimshambulia ngamia aliyependwa na Zaynab ﵂ wakati akisafiri kwenda Madina, akasababisha binti huyo wa Mtukufu Mtume ﷺ kudondoka, akaumia na kujeruhiwa vibaya, na zaidi ya hapo, alikuwa mjamzito wakati huo na hivyo ujauzito wake ukaharibika. Jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa majeraha hayo makali ndiyo yaliyosababisha kifo chake hapo baadaye. Habbar alikuwa mhusika wa maovu na uhalifu mwingi. Siku ya Ufunguzi wa Makka, alikimbia na kukwepa majaribio yote ya kukamatwa. Muda mfupi baadaye alitokea Madina kwa majaribio mbele ya Mtume wa Rehma ﷺ, akiwa amekaa na Maswahaba zake. Hakuwa na budi zaidi ya kutangaza kuwa alisilimu. Sio tu kwamba Mtume ﷺ alimsamehe, bali pia aliwakataza watu wote kumshutumua na kumtupia Habbar matusi.[277] Aidha, Qur'an Tukufu ilitangaza wazi kuwa:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ

"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili." (al-Araf, 199)

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa Qur'an iliyo hai. Alikuwa mfano unaotembea kwa kuonesha ubora wa maadili ya Qur'an. Alikuwa akisamehe makosa yote yaliyotendwa dhidi yake bila kusita hata kidogo. Ama kuhusu makosa yaliyotendwa dhidi ya watu wengine, hakuna mtu ambaye angeweza kumtuliza mpaka asimamishe uadilifu kwa kuuweka mahali unapostahiki na kumrejeshea haki muathirika husika. Pamoja na kutangaza msamaha wa jumla ambao haukuwahi kushuhudiwa hapo kabla, kwa faida na maslahi ya *ummah*, vilevile Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ aliagiza adhabu

277. Waqidi, II, 857-858.

ya hapo hapo kwa idadi ndogo sana ya makafiri ambao hali zao zisingesafika.[278]

Hakuna ngawira zilizochukuliwa kutoka Makka.[279] Badala yake, Mtukufu Mtume ﷺ alichukua mkopo kutoka kwa matajiri wa Makka ili kugharamia huduma za dharura za jeshi la Kiislamu, ambapo baadaye alililipa deni hilo kwa ngawira za Hawazin, akaeleza, "Mkopo unastahili kushukuriwa na kulipwa." (Waqidi, II, 863; Abu Dawud, Buyu', 88/3562; Nikah, 44)

Wakati watu wa Makka wakiendelea kufurahia mandhari ya huruma waliyopewa na msamaha wa Mtukufu Mtume ﷺ, sasa ilikuwa ni wakati wa adhuhuri. Kama kawaida, Mtukufu Mtume ﷺ alimuashiria Bilal Habashi ؓ kutoa adhana kwa ajili ya swala ya adhuhuri. Bilal ؓ alikumbuka zama alipokuwa mtumwa, alipolalama kwa maumivu akisema '*Ahad*, *Ahad*' huku akiadhibiwa vikali. Sasa uonevu ulikuwa umefikia kikomo chake. Na sasa alikuja Makka akiwa mtu huru, na akiwa sehemu ya jeshi la ushindi wa *iman*. Akiwa ni mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, alipanda juu ya paa la Kaabah na kuanza kutoa adhana katika sauti maridhawa na yenye msisimko. Adhana ya Bilal ilikuwa na msisimko sana kiasi kwamba milima na anga lote la jirani vilizizima kwa sauti yake. Mbingu ziling'ara na ardhi ikafurahi. Adhana iliyotolewa na Bila ؓ siku hiyo iliacha kumbukumbu ya kudumu kwa Waislamu wote. Baadhi ya waabudu masanamu walioshuhudia mandhari hayo walisikika wakisema, "Aibu iwe juu yetu...tumeshindwa hata kuwa kama watumwa! Angalia namna walivyo juu na jinsi tulivyo-

278. Abu Dawud, Jihad, 117/2683; Nasai, Tahrîmud-Dam, 14.

279. Abu Dawud, Kharaj, 24-25/3023.

baki kuwa chini!" Walikuwa tu wakijilaumu kwa matendo yao ya zamani, ukweli ambao mpaka wakati huo walikuwa wameukana.

Kiapo cha Utii cha Watu wa Makka

Baada ya swala ya adhuhuri, Mtukufu Mtume ﷺ alipanda juu ya Mlima wa Safa kwa ajili ya kupokea kiapo cha utii kutoka kwa watu wa Makka. Wanaume wa Kiqurayshi ndio walioanza kutoa kiapo chao cha utii cha 'kuupokea Uislamu na *jihad*'. Wanawake wakafuatia.[280] Kuhusu kiapo cha utii cha wanawake, Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa ameshatangaza kuwa:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعْنَكَ عَلَى أَن لَّا يُشْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ وَلَا يَعْصِينَكَ فِي مَعْرُوفٍ فَبَايِعْهُنَّ وَاسْتَغْفِرْ لَهُنَّ اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Ewe Nabii! Watakapo kujia wanawake Waumini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawauwa watoto wao, wala hawataleta uzushi wanao uzua tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi peana nao ahadi, na uwatakie maghfira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi maghfira, Mwenye kurehemu." (al-Mumtahinah, 12)

280. Ahmad, III, 415; Bukhari, Maghazi, 53.

Wanawake walitoa kiapo chao cha utii kwa kutumbukiza mikono yao ndani ya chombo kidogo cha maji ambacho Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa ametumbukiza mikono yake. Hakuna tukio lolote ambapo Mtume ﷺ alikubali kiapo cha utii cha wanawake kwa kushika mikono yao.

Umaymah bint Ruqayqah anasimulia:

"Pindi wanawake wa Kiansari walipokwenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kusema, tunakuahidi ya kwamba hatutamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hatutaiba, wala hatutazini, wala hatutawauwa watoto wetu, wala hatutaleta uzushi, wala hatutakuasi katika mambo mema', alijibu: 'Katika mambo tu yaliyo ndani ya uwezo wenu na mnayoweza kuyastahmili...'

Tulipsikia maneno haya yenye uwastani, tukasema, 'Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni wenye huruma kwetu kuliko tunavyojihurumiwa sisi wenyewe...hivyo tumpe kiapo chetu cha utii!'

Wanawake hao walitaka kushika mkono wake lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, 'Sishikani mikono na wanawake. Ni neno ninalosema kwa wanawake mia moja kwa pamoja kana kwamba nimelisema kwa mwanamke mmoja mmoja.'" (Muwatta', Bayat, 2; Tirmidhi, Siyar, 37/1597)

Zirejesheni Amana kwa Watu Wake

Mtukufu Mtume ﷺalikuja jirani na Kaabah, akakaa kwenye kona la mkabala na Nyumba Tukufu, huku Maswahaba zake wakichukua nafasi zao kumzunguka. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtuma Bilal ؓ kwenda kuchukua ufunguo kwa Othman ibn Talha ؓ.

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakutaka umpelekee ufunguo wa Kaabah", Bilal ؓ alimwambia Othman, ambaye alikubali na

kwenda kwa mama yake, Sulfah ambaye wakati huo ndiye alikuwa akiutunza.

"Nimekuja kuomba ufunguo wa Kaabah", Othman alimwambia mama yake, "kwa maana Mtume wa Mwenyezi Mungu ameniamuru nimpelekee."

"Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu dhidi yako kukichukua kwa mikono yako kitu ambacho kabila lako linajifhakharisha nacho! Atakapouchukua ufunguo huu kutoka kwako, kamwe hataurejesha!" alijibu Sulafah. Baada ya muda mfupi Othman aliweza kumshawishi mama yake na kuupata ufunguo. Alipouleta kwa Mtukufu Mtume ﷺ, alisema:

"Ninakupa kwa muda ufunguo huu kama amana ya Mwenyezi Mungu!" Alikuwa na wasiwasi kwamba huwenda hatarudishiwa funguo hizo. (Waqidi, II, 833; Haythami, VI, 177)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliufungua mlango wa Kaabah. Alipoingia ndani akaomba mlango ufungwe kwa nyuma. Alibaki humo kwa muda, ambapo aliswali rakaa mbili. (Waqidi, II, 835; Ibn Saad, II, 137)

Mtukufu Mtume ﷺ alitoka ndani ya Kaabah; na baada ya kutoa hotuba fupi kuhusu tukio la ufunguzi wa Makka, aliuliza mahali alipo Othman. Othman, ambaye muda wote alikuwepo, akasimama. Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akasoma aya ifuatayo:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تُؤدُّواْ الأَمَانَاتِ إِلَى أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ النَّاسِ أَن تَحْكُمُواْ بِالْعَدْلِ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا

"Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa

uadilifu. Hakika haya anayo kuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (an-Nisa, 58)

Kisha akasema: "Enyi wana wa Abu Talha! Ichukueni amana hii ya Mwenyezi Mungu na mkae nayo daima, shikamaneni nayo kwa uthabiti! Hakuna mtu atakayeichukua kutoka kwenu ispokuwa mtakapoanza kufanya dhulma! Leo ni siku ya wema na utii!" (Ibn Hisham, IV, 31-32; Waqidi, II, 837-838; Ibn Saad, II, 137)

Tukio hili linaelezea umuhimu wa kurejesha amana kwa wenye haki nazo. Kuwapa watu haki yao wanayostahiki huimarisha amani na uthabiti kwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla. Sio ajabu kuona hata madola makubwa yakianguka pindi watu wanaponyimwa kile wanachostahiki. Historia ni shahidi wa mifano mbalimbali ya silika hii.

Mtukufu Mtume ﷺ anaakisi kwa uzuri kabisa juu ya umuhimu wa suala hili katika *hadith* moja akisema:

"Amana zinapoachwa kurejeshwa kwa wenye nazo, basi subiri-ni Kiyama!" (Bukhari, Ilim, 2; Ahmad, II, 361)

Kwa mukhtasari, kuacha kuwapa amana wale wanaostahiki ni moja ya alama za Kiyama.

Abbas رضي الله عنه, ambaye tokea zamani alikuwa amepewa jukumu la kuwapatia maji mahujaji pia aliomba kazi ya *hijabah*[281] kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akamwambia ami yake huyo:

"Sitakukabidhi kazi ambayo utapata maslahi kutokana na vitu ambavyo watu watakutumia kama pazia la Kaabah bali nitakupa kazi ngumu ambayo utaitekeleza kwa kutoa kilicho mfukoni mwako ili kuwahudumia mahujaji kwa kuwa pa maji na hivyo kupata tha-

281. Tazama juzuu ya kwanza ya kitabu hiki ili kujua maana na makusudio ya *hijabah*.

wabu." Kisha alimshauri ami yake huyo kuendelea na huduma ya kuwahudumia mahujaji kwa kuwapa maji.

Abbas ﷺ alikuwa na shamba la mizabibu katika eneo la Taif. Kabla na baada ya Uislamu, alikuwa akibeba zabibu, akiongezea na maji ya zamzam na kuwapatia mahujaji. Watoto wake waliendelea na kazi hii baada yake. (Ibn Hisham, IV, 32; Ibn Saad, II, 137; Waqidi, II, 838)

Katika siku ya pili baada ya swala ya adhuhuri, Mtukufu Mtume ﷺ alisimama katikati ya umati wa watu na baada ya kumhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, alisema:

"Enyi watu...! Hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu ameitangaza Makka kuwa eneo tukufu na takatifu siku aliyoumba mbingu na ardhi, jua na mwezi! Litaendelea kuwa tukufu na takatifu mpaka Siku ya Mwisho! Bila shaka, Mwenyezi Mungu hakuliruhusu Jeshi la Watu wa Tembo kuingia Makka lakini sasa amempa ushindi Mtume Wake na Waislamu. Makka haitahalalishwa kwa yeyote baada yangu. Wanyama wa Makka hawatatishwa, miiba yake haitakatwa, mali iliyopotea katika eneo hilo haitaokotwa isipokuwa kama anatafutwa mmiliki wake. Iwapo ndugu wa mtu ameuawa, atakuwa na hiari ya kuchagua mambo mawili: Fidia au kisasi."

Kisha Abbas ﷺ akasisitiza kuwa*idhir*, aina ya mti wenye majani, uondolewe katika mti na majani ambayo hayatakiwi kuguswa. "Kwa maana tunautumia katika makaburi na nyumba zetu", alisema.

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akatangaza: "Isipokuwa mti wa *idhir*!"[282] (Bukhari, Luqata, 7; Maghazi, 53; Ahmad, IV, 31-32; II, 238)

Tukio jingine lililotokea siku hiyo hiyo linaloonesha vina vikubwa vya utambuzi na hisia kubwa ndani ya nyoyo za Maswahaba. Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amekaa jirani na Kaabah, Abu Bakr ؓ aliwasili akiwa ameandamana na baba yake, Abu Quhafah.

"Hukutakiwa kumsumbua baba yako kumleta mpaka hapa", alisema Mtukufu Mtume ﷺ baada ya kuwaona. "Badala yake ningekuja."

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni bora kwake kuja kuliko wewe kwenda kwake", alisema Abu Bakr ؓ.

Mtukufu Mtume ﷺ alimkalisha Abu Quhafah mbele yake na kuuweka mkono wake juu ya kifua chake, akasema, "Silimu ewe Abu Quhafah utapata amani!" Abu Quhafah akafanya hivyo, akayatamka maneno ya *shahaadah* kwa ikhlasi na kusilimu. (Ibn Saad, V, 451)

---

282. Idhir, ni mmea mkubwa wenyewe asili ya Makka, ambao una majani mapana na harufu nzuri. Mbali na kuwa chakula cha wanyama, mti huu pia hutumika ndani ya nyumba na kabaruni. Mimea ambayo imeharamishwa kukatwa ndani ya viunga vya *Haram*, imeainishwa kuwa ni 'ile iliyoota yenyewe.' Pamoja na tofauti ya maoni kuhusu kukata miti iliyopandwa na watu, idadi kubwa ya wanazuoni wamekubaliana na uhalali wake. Kwa mfano, kukata mti wa *miswaq*, kuchuma jani au tunda nayo pia inahesabiwa kuwa ni halali, ikiwa tu kwa kufanya hivyo hakutakuwa na madhara kwa mti wenyewe. (Tazama: İbrâhim Cânan, *Hadîs Ansiklopedisi*, XII, 525-526)
Ni halali kukata majani na miti mibichi katika eneo la *Haram* ya Madina, pindi inapohitajika. Kwa kuwa Madina ni eneo linalostawi kilimo, Mtukufu Mtume ﷺ aliombwa ruhusa kuhusu suala hilo, na hivyo, mji huo ulipewa tahfifu zaidi kuliko Makka kuhusu matumizi ya mimea. Vilevile iliwekwa tahfifu kuhusu kuwinda nje ya mji wa Madina. (Tazama: Hamdi Döndüren, Şâmil İslâm Ansiklopedisi, "Harem" entry)

Uaminifu wa Kipekee

Mtukufu Mtume ﷺ alibaki Makka kwa siku kumi na tano baada ya Ufunguzi. Muda huo ulioongezeka wa kuendelea kubaki Makka, uliwafdhaisha *Ansar*, ikawatia wasiwasi kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ hatarejea tena Madina. Walizidi kuwa na wasiwasi kutokana na ukweli kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu, alikuwa amempa ushindi katika mji mtukufu ambao alizaliwa na kutumia kiwango kikubwa cha umri wake ndani ya mji huo. Wakati akiswali juu ya Mlima wa Safa, Mtukufu Mtume ﷺ aligundua wasiwasi huo wa *Ansar*. Baada ya kumaliza kuswali, alikuja mbele yao na kuuliza: "Kitu gani hicho mnachokizungumia?"

Ansar wakatoa sauti kamili juu ya wasiwasi walionao, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ, akionesha picha ya mfano ya uaminifu, alisema:

"Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya kufanya kitu kama hicho. Nilihamia katika ardhi yenu. Uhai wangu ni uhai wenu; na hivyo nitakufa pembezoni mwenu!"

Ansar wakavuta pumzi ndefu ya faraja. (Muslim, Jihad, 84, 86; Ahmad, II, 538)

Mtukufu Mtume ﷺ alizidisha himidi na shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kufuatia Ufunguzi wa Makka. Alikuwa akisoma *dhikr* ifuatayo, hasa wakati wa rukuu na *sajdah* katika swala zake:

"Ninamhimidi na kumtakasa Mwenyezi Mungu dhidi ya kasoro zote zisizoendana na dhati, sifa, majina na Matendo Yake; ninamshukuru kwa sifa Zote njema anazostahiki. Ninamuomba Mwenyezi Mungu msamaha na kutubia kwake kwa makosa yangu yote."

Bibi Aisha ؓ alipomuuliza sababu ya kuomba dua hii, Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Mola wangu alinifunulia ya kuwa nitaona ishara katika ummah wangu, na nilipoomba dua hii sana niliiona ishara hiyo." (Muslim, Salat, 220)

Kupitia *surah* Nasr, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ameamriwa kuzidisha istighfaar na kumtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu mara tu baada ya kupata msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ushindi, na akawaona watu wakiingia katika Uislamu makundi kwa makundi. Neno *nasr*, ambalo ni jina maalumu la *surah*, limetafsiriwa kama ushindi juu ya Waarabu wote, na *fath* ya ushindi wa kuifungua Makka.Kutokana na maana ya neno *fath*, yaani 'kufungua', Ibn Abbas ؓ aliuita ushindi wa Makka kuwa ni *fath* ya *fath* zote, kwa maana kilichokusudiwa ni 'ufunguzi' wa mji wenye Nyumba Tukufu, Kaabah, kuingia kwenye Uislamu.*Fath*, sio tu ufunguzi wa eneo ambalo hapo mwanzo lilikuwa chini ya udhibiti wa maadui. Bali ni 'ufunguzi' wa nyoyo za watu waishio humo kuingia kwenye dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na pia 'kuwafungulia' milango ya Uislamu, na hatimaye, kuwafungulia wanadamu wote milango hiyo. Siku hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ hakuufungua sana mji kama alivyozifungua nyoyo za wakazi hao kuingia kwenye Uislamu. Hivyo, ufunguzi wa Makka unachukuliwa kama mwanzo wa Uislamu kusonga mbele katika kuufungua ulimwengu kwa ajili ya Uislamu. Njia ya 'ufunguzi' wa Arabia yote na kisha kuufungua Ulimwengu mzima, ilianza na 'ufunguzi' wa mlango wa Kaabah. Kwa hakika, lilikuwa ni tukio ambalo makabila mengine yote ya Arabia yalikuwa yakilisubiri, tukio ambalo ndilo lililosababisha kuingia kwao katika Uislamu. Walikuwa wakisema: "Muacheni kwanza ashughulike na kabila lake mwenyewe. Akiweza kuwashinda hiyo itakuwa na maana kwamba ni mtume wa kweli!" (Bukhari, Maghazi, 53)

Kwa mujibu wa simulizi kutoka kwa Hasan Basri, pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipoitwaa Makka, Waarabu walisema: "Kama Muhammad ﷺ ameweza kuwashinda watu wa Makka, ilihali Mwenyezi Mungu aliwalinda dhidi ya jeshi la Tembo, basi hatutaweza kumfanya lolote!" Hapo ndipo walipoanza kuingia katika dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, makundi wa makundi. (Elmalılı, IX, 6236-6238)

Vita ya Hunayn (11 Shawwal, 8 / 1 Februari, 630)

Mtukufu Mtume ﷺ sio tu kwamba aliyavunja masanamu ndani na pembezoni mwa kaabah, bali pia alituma vikosi kwenda kwenye miji ya jirani kuondosha mawe haya yasiyokuwa na uhai ambayo yalikuwa yakiabudiwa. Utakaso wa *tawhid* ulikuwa umeanza.[283]Lakini, kabila la Hawazin la Hunayn na Banu Thaqif la Taif hawakulipendelea hilo, wakaamua kuanzisha mapambano

283. Waqidi, III, 873. Pindi Khalid ibn Walid رضي الله عنه aliporejea Makka baada ya kulivunja sanamu la Uzza akiwa na kikosi cha Waislamu mia tatu na thelathini, Mtukufu Mtume ﷺ alimtuma kwenda kwenye kabila la Banu Jazimah kuwalingania kwenye *iman* ya kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutokana na sintofahamu iliyotokea, Khalid رضي الله عنه aliwaua watu wapatao thelathini kutoka katika kabila hilo. Pindi taarifa hizo zilipomfikia Mtukufu Mtume ﷺ aliinua mikono juu na kuomba dua mara mbili, 'Ewe Mwenyei Mungu…Ninajisalimisha Kwako kwamba niko mbali na yaliyofanywa na Khalid!' na akajilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kasha alimtuma Ali رضي الله عنه na kiwango cha pesa kwenda kwa Banu Jazimah na kumwambia atoe fidia kwa tukio hilo kwa kutoa pesa hiyo kwa familia za waathirika.
Ali رضي الله عنه alitoa fidia ya mali zote zilizochukuliwa kama ngawira, hata vihori vya maji ya mbwa. Kasha pesa zilizobaki aliziacha kwa Banu JAzimah, ili waweze kugharamia hasara za ziada ambazo wangezigundua baadaye. Ali رضي الله عنه aliporejea kwa Mtume wa Rehma ﷺ na kumwelezea hatua aliyoichukua, Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Umefanya vyema; umefanya jambo sahihi!" (Bukhari, Maghazi, 58, Ahkâm 35; Nasai, Âdâbul-Kudât, 16; Ibn Hisham, IV, 53-57; Waqidi, III, 875-884)

dhidi ya Waislamu. waliandaa jeshi kubwa, wakafunga safari wakiwa na vitu vyao vyote, kana kwamba wanaenda katika vita ya kufa na kupona.[284]

Mtukufu Mtume ﷺ alipopata taarifa ya maandalizi yao, alijibu kwa kuandaa jeshi la Waislamu, huku akiwaorodhesha askari wengine mia mbili kutoka Makka ambao walikuwa wamesilimu. Kitu cha kufurahisha katika maajabu ya Mwenyezi Mungu ni kumuona Abu Sufyan, ambaye kwa miaka mingi alikuwa akipambana dhidi ya Waislamu kwa ajili ya masanamu ya mawe na kuwasababishia machungu na mateso, sasa alikuwa akishiriki kama Muumini katika jeshi la Kiislamu, mara hii akiwa tayari kuupigania Uislamu. Jeshi hili lilijumuisha pia Makafiri wapatao themanini kutoka Makka.[285]

Jeshi la Kiislamu lilionekana kuwa jeshi kubwa lisiloshindwa katika hali zote, wakati likielekea Hunayn kwa madaha yenye kustaajabisha. Arabia haikuwahi kuona jeshi kama hilo lenye maandalizi na nidhamu ya hali ya juu. Na kwa muda mfupi, muonekano huo wenye taadhima uliruhusu vumbi la ufakhari kupenya katika nyoyo za Maswahaba. Kwa kudhani na kuwa na fikra kuwa 'jeshi kubwa kama hili haliwezi kushindwa', walianza kuwabeza na kuwatweza maadui, wakidhani kuwa ushindi ni wa kwao tu, kutokana na muonekano wao wa nje. Ni katika kipindi hicho cha ujivuni na ufakhari ndipo Waislamu walipokumbana na mtihani mkali kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Katika kiza cha usiku, muda mfupi kabla ya alfajiri, kikosi cha mbele cha jeshi la Waislamu kilipokuwa kikitembea kwa kuji-

---

Tukio hili linaonesha huruma kubwa aliyekuwa nayo Mtukufu Mtume ﷺ na jinsi alivyowatazama viumbe kwa jicho la Muumba. Kufidia hata vihori vya maji ya mbwa kunatoa kiwango cha mfano cha kuchunga haki za wanyama.

284. Ibn Hisham, IV, 65; Ibn Saad, II, 150.

285. Ibn Hisham, IV, 68; Waqidi, III, 890.

amini katikati ya njia nyembamba iliyo baina ya vilima viwili kuelekea Hunayn, ghafla walishambuliwa na maadui ambao walikuwa wameweka mtego kuwasubiri. Wakashikwa na hali ya kuhamanika na kuvurugika. Waislamu walizuiwa na ukuta wa mishale waliyotupiwa kutoka kusikojulikana na kujikuta wakiwa katika hali ya wasiwasi na kusita, ikawapelekea kuwa katika hali ya kuchanganyikiwa na kuparaganyika bila kikomo, ambapo muda mfupi tu vikosi vya nyuma navyo vikakumbwa na hali hiyo. Waislamu walilazimishwa kurudi nyuma, lakini Hawazin na Thaqif waliendelea kuwafutilia kwa bidii, pasipokuwa na nia ya kuacha kuwafukuza.

Mtukufu Mtume ﷺ ndiye pekee aliyesimama kishujaa katikati ya mvurugiko huyo mkubwa, akizidi kumpeleka mbele farasi wake katikati ya safu za maadui. Siku hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ alionesha kiwango kisichomithilika cha ushujaa na ujasiri, licha ya juhudi kubwa za ami yake, Abbas na Abu Sufyan ﷺ kukamata hatamu za farasi wake kumzuia asisonge mbele, asije akapatwa na jambo.[286]

Wakati huo huo, mkanganyiko wa jeshi la Kiislamu ulikuwa ukiendelea, bila kuonesha dalili za kupoa. “Leo apizo limevunjwa”, baadhi walisikika wakisema, huku wengine wakilia kwa kukata tamaa “tukikimbilia baharini tutaweza kukomesha ufukuzwaji huu!” Wale waliotoka Makka walisikika wakieneza uvumi kuwa “Mtume ameuawa na kwamba Waarabu watarejea katika dini yao ya masanamu!”

Lakini, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa hai na salama, akiwa amesimama kwa ujasiria kabisa kuwakabilia maadui. Kama kawaida, imani yake aliiweka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, akawaita Maswahaba wake:

286. Muslim, Jihad, 76.

"Enyi *Ansar*...Enyi *Muhajirun*! Enyi waja wa Allah! Njooni! Mimi ni mja na mjumbe wa Mwenyezi Mungu!"

Kisha alimuashiria Abbas ﵁, ambaye alijulikana kwa sauti yake imara, kuwaita askari wa Kiislamu. Kwa sauti yake yote, Abbas ﵁ aliita: "Wale waliokula kiapo cha utii siku ya Aqabah...Wale waliokula kiapo cha utii chini ya mti wa Ridhwan! Njooni haraka! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yuko hapa!"

Baada ya kuusikia mwangwi wa sauti hii, Maswahaba walimkimbilia Mtukufu Mtume ﷺ. Wakiwa kama vipepeo waliosukumwa kwa kasi na upepo mkali, walikusanyika kuuzunguka mwanga wenye kuvutia. Nyoyo za Waumini, walioungana tena pembezoni mwa Mtumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, zilisafishwa dhidi ya wasiwasi wa awali na kuzipa amani. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu, safu zaote za jeshi la Kiislamu zilirejea katika hali yake ya kawaida. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akainua mikono yake juu na kuomba: "Mola wangu! Nijaalie ushindi ulioniahidi!"

Kama alivyofanya katika Vita vya Badr, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua mchanga na kuurusha upande wa maadui, kisha akawaambia Maswahaba wake:

"Sasa songeni mbele, kwa uaminifu na utii!" (Muslim, Jihad, 76-31; Ahmad, III, 157, V, 286; Ibn Hisham, IV, 72; Waqidi, III, 897-899)

Sasa jeshi la Kiislamu likafanya shambulizi kali dhidi ya maadui, kana kwamba vita ndo ilikuwa inaanza. Hawazin na Banu Thaqif wakiwa wamekumbwa na wimbi la mashambulizi makali, hawakuweza kuhimili na ndani ya muda mfupi wakawa wameshindwa. Ni Waislamu wanne pekee ndio waliofariki, huku majeshi ya ushirika yakipoteza watu sabini. Walishindwa vibaya sana kiasi kwamba

walilazimika kuviacha vitu vyote walivyokuja navyo kwenye medani ya vita. Ngawira walizoziacha hazikuwa na idadi maalumu.[287]

Bila shaka, hii ni baraka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyowajaaliwa Waumini. Licha ya mwanzo wa Vita kuwa nyuma, lakini kwa sababu ya ujasiri na uthabiti wa Mtukufu Mtume ﷺ na dua zake za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hatimaye waliweza kupata ushindi. Mwenyezi Mungu Mtukufu analieleza hili ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ثُمَّ أَنزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنزَلَ جُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا وَعذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُواْ وَذَلِكَ جَزَاء الْكَافِرِينَ

"Hakika Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu. Na ardhi ikawa dhiki kwenu juu ya upana wake. Kisha mkageuka mkarudi nyuma. Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya Waumini. Na akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale walio kufuru. Na hayo ndiyo malipo ya makafiri." (at-Tawba, 25-26)

Maadui waliosilimu baada ya kushiriki katika vita vya Hunayn, baadaye walithibitisha kuwaona askari, ambao 'hawakuwahi kuwaona hapo kabla', wakiwashambulia, jambo linalodhihirisha kuwa

287. Ibn Hisham, IV, 79.

siku hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwatumia msaada Waislamu ili kuwapa nguvu.[288]

Sehemu ya jeshi la Hawazin lililoshindwa walikimbilia Taif, baadhi wakaelekea Nakhlah, huku wengine wakiweka kambi katika eneo la Awtas.[289]

Akiwa amepata ushindi katika vita vya Hunayn, Mtukufu Mtume ﷺ alitoa agizo la kuwafuatilia maadui waliokimbia na kutaka mateka na ngawira zihamishiwe katika eneo la Jiranah. Baadaye, ili kukamilisha vita hivyo, alituma kikosi chini ya uongozi wa Abu Amir, ami wa Abu Musa al-Ash-ari, kwenda Awtas, huku yeye akiliongoza jeshi la Kiislamu kuelekea Taif.



288. Ahmad, V, 286; Haythami, VI, 182-183; Ibn Hisham, IV, 79.
289. Ibn Hisham, IV, 84.

Vita vya Awtas (Shawwal, 8 / Februari, 630)

Katika Vita vya Awtas, ambavyo Mtukufu Mtume ﷺ hakushiriki kutokana na yeye kuelekea Taif, kamanda wa jeshi la Kiislamu, Abu Amir, aliuawa. Mkabala wake, kamanda wa jeshi la maadui, naye akauawa.

Akiwa amepatwa na jeraha kubwa na kukosa matumaini yote ya kupona, Abu Amir ؓ alimgeukia mtoto wa nduguye, Abu Musa ؓ na kumwambia: "Peleka salamu zangu kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na muombe aniombee maghfira!"

Baada ya kumpoteza ami yake, Abu Musa ؓ alishika uongozi wa jeshi na kuwazuia Waislamu wasitawanyike. Safu kamili ya mashambulizi ilimuwezesha kuwafurusha maadui na kuipeperusha bendera ya ushindi wa Waislamu huko Awtas. Aporejea kwa Mtukufu Mtume ﷺ alimtaarifu kuhusu ombi la ami yake. Mtukufu Mtume ﷺ akaagiza maji na kuchukua wudhuu, kisha akainua mikono yake na kuomba: "Mola wangu! Mghufurie mja Wako Abu Amir! Siku ya Kiyama mnyanyue katika daraja ya juu kuliko wengi wa wale uliowaumba!" (Bukhari, Maghazi, 55)

Kuizingira Taif (Shawwal, 8 / Februari, 630)

Taif, mji maarufu katika eneo la Hijaz unaostahiki kuitwa pepo ya dunia, ulikuwa na kasri lenye ngome imara lililojengwa juu ya mlima. Mzingiro uliowekwa na jeshi la Kiislamu ulionekana kuwa ni kazi ngumu na yenye kuhitajika.

Mzingiro wa Taif haukufanywa kwa lengo la kulipiza kisasi dhidi ya muamala mbaya aliotendewa Mtukufu Mtume ﷺ miaka kadhaa ya nyuma kutoka kwa wenyeji wa mji huo, bali ilikuwa ni muendelezo na pazia la mwisho la Vita vya Hunayn. Kiwango kikubwa cha askari wa maadui, ikiwa ni pamoja na kiongozi

wao, Malik ibn Awf, ambao walikimbia kutoka Hunayn, walikuwa wamekuja Taif na kujificha katika kasri hilo. Huko waliungana na Banu Thaqif kwa mara nyingine, wakajiandaa kwa vita mpya kabisa ya kujilinda.

Mikakati kadhaa ilifanywa na zana mbalimbali zilitumiwa na Waislamu. lakini, kuta za kasri hilo zilionekana kuwa imara sana dhidi ya majaribio ya Waislamu ya kutaka kuingia. Hawakuweza kuwatoa maadui ndani ya kasri hilo. Pindi Khalid ibn Walid ﷺ alipowataka wamtume nje mpambanaji kwa ajili ya makabiliano ya mmmoja mmoja, walisema: "Hatuna mtu anayeweza kusimama kukabiliana nanyi!"

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Adui amekimbilia mafichoni kama mbweha. Hata tukiwaacha, hataweza kuleta madhara tena!" Sasa walikuwa wamedhoofishwa, na kwa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ ni mtume wa rehma, hakuona sababu ya kuendelea kuwazingira, kwa maana alitaka kuwangoa watu wa Taif, sio kuwaangamiza. Haukupita muda, akaamuru mzingiro uondolewe.

Wakati mzingiro ukihitimishwa, Maswahaba walimuomba Mtukufu Mtume ﷺ awalaani Banu Thaqif, ambao waliwasababishia hasara kubwa Waislamu. Lakini Mtume wa Rehma ﷺ,badala yake, aliwaombea uongofu. "Mola wangu! Wajaalie uongofu Banu Thaqif! Walete kwetu!" alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, kabla ya kuondoka Taif. Haukupita muda mrefu, Banu Thaqif walikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ kwa hiari yao na kusilimu. (Ibn Hisham, IV, 134; Tirmidhi, Manaqib, 73/3942)

Mtukufu Mtume ﷺ hakuepuka tu kulilaani kabila ambalo miaka kadhaa iliyopita lilimpiga kwa mawe, wakamjeruhi na kumfanya avuje damu, bali pia alionesha tamaa kubwa ya wao kupata uongofu. Kwa kweli, mwaka mmoja baadaye, walipomwendea na kueleza raghba yao ya kusilimu, hatua hiyo ilimfurahisha mno

Mtukufu Mtume ﷺ kiasi kwamba alitenga muda wa siku kadhaa kwenda kuwaona.

Faida kubwa iliyopatikana katika mzingiro wa taif, kwa wakati huo, ni kundi kubwa la watumwa kutoka upande mwingine kuukubali Uislamu, ambao kufuatia ahadi ya Mtukufu Mtume ﷺ kuwa watakuwa huru wakisilimu, walilitoroka jeshi la maadui na kuungana na Waislamu.[290]

Abu Zuraa رضي الله عنه anasimulia:

"Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipotaka mnyama wake wakati akiondoka Qarnul Manazil wakati wa Vita vya Taif, nilimuandaa ngamia wake, Qaswa. Nilikamata hatamu ake mpaka alipopanda; kisha nikamkabidhi hatamu nami nikakaa juu ya tandiko la ngamia, nyuma yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akimchochea taratibu ngamia huyo, kwa upande wa nyuma, kwa kutumia mjeledi wake ili apate kufanya haraka, nami nikiwa nyuma yake nilikuwa nikihisi pigo la mjeledi huo kila lilipopigwa. Kisha alitazama nyuma na kuuliza, 'Mjeledi unakupiga?' 'Ndiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', nilijibu, 'wazazi wangu wawe fidia kwa ajili yako!'

Baadaye tuliwasili Jiranah, ambapo baadhi ya kondoo walikuwa wamefungwa. Mtume wa Mwenyezi Mungu akamuuliza kitu mtu anayehusika na ngawira kuhusu kondoo hao na kumpa taarifa alizozihitaji. Mara tu baada ya mazungumzo yao, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akaniita. 'Niko hapa ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', niliitika.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, 'Chukua hawa kondoo kwa niaba ya mijeledi iliyokupata jioni!' Niliwahesabu kondoo

290. Bukhari, Maghazi, 56.

hao; walikuwa mia moja na ishirini. Hiyo ndio milki niliyofaidika nayo sana." (Waqidi, III, 939)

Umakini uliooneshwa hapa na Mtukufu Mtume ﷺ kwenye haki za watu wengine unatosha kuwa muongozo katika zama na mahali popote.

Ugawaji wa Ngawira

Baada ya kuondoa mzingiro kwenye mji wa Taif, Mtukufu Mtume ﷺ aliliongoza jeshi la Kiislamu kuelekea eneo la Jiranah, mahali walipokuwa mateka na ngawira za vita. Muda huo huo aliwasili Abu Musa al-Ash-ari ؓ, akiwa na kikosi take, akirudi na ushindi kutoka katika Vita vya Awtas. Waislamu walikuwa wameshawatawanya maadui zao wote na sasa ulikuwa umefika muda wa kugawa ngawira. Kiasi cha ngawira kilichopatikana katika vita vyote vilivyopigana katika muda wa karibuni zilifikia idadi ya ngamia elfu ishirini na nne, kondoo elfu arobaini na uqiyyah elfu nne za fedha, bila kutaja mateka elfu sita.[291]

Kabla ya kuanza kugawa ngawira, Mtukufu Mtume ﷺ alitangaza: "Wale ambao walichukua kitu chochote katika ngawira, hata kama ni sindano au uzi, basi warejeshe! Tambueni kwamba vitendo vya udanganyifu kuhusu ngawira humsababishia mhusika fedheha na moto siku ya Kiyama!" (Muwatta, Jihad, 22' Ahmad, V, 316)

Wakati huo huo, Mtukufu Mtume ﷺ alitaarifiwa kuwa Shayma, dada yakewa kulea, alikuwa miongoni mwa mateka. Hapo hapo, Mtukufu Mtume ﷺ akaagiza aletwe mbele yake. Alivua *rida* yake na kumtandikia sakafuni ili apate kukaa, akamkaribisha kwa wema na huruma. Mtukufu Mtume ﷺ alipomuona Shayma ؓ alikumbuka zama walipokuwa wadogo. Macho yake yalijawa na

291. Ibn Saad, II, 152.

simanzi. Akamuuliza mahali walipo wazazi wake, ambao, iligundulika kuwa walifariki dunia miaka kadhaa iliyopita. Kisha, baada ya kumuuliza mahli walipo ndugu zake, Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Ukitaka, unaweza kubaki pamoja nami ambapo utaamiliwa kwa upendo na heshima kubwa. Lakini ukitaka, ninaweza pia kukupa baadhi ya mali na kukupeleka kwa kabila lako. Naweza kufanya hivyo pia!"

Shayma ؓ alichagua kurudi kwa kabila lake na baadaye akasilimu. Mtukufu Mtume ﷺ alimpa yeye na wanafamilia yake idadi kadhaa ya ngamia na kondoo. Vile vile alimpa watumishi wawili kamazawadi, mmoja wa kiume na mwingine wa kike, ambao baadaye waliozeshwa na Shayma ؓ. (Ibn Hisham, IV, 91-92; Waqidi, III, 913)

Mtukufu Mtume ﷺ alichelewa kidogo kugawa ngawira. Wale wenye udhaifu ndani ya nyoyo zao, ambao hawakuona hekma ya ucheleweshaji huu, hawakuridhika. Hasa hasa Waarabu wa Kibedui wakataka ugawaji ufanywe mara moja. Walienda mbali zaidi kiasi cha kumzingira na kumzonga Mtukufu Mtume ﷺ aliyekuwa amepanda ngamia wake karibu na mti wa *samurah*, kiasi kwamba joho lake lilikamatwa na moja ya matawi ya mti huo. Alimsimamisha ngamia wake na kusema: "Nipeni joho langu! Lau kama ningekuwa na ngawira nyingi kama miti hii, bado ningezigawa zote baina yenu, kisha mngeona kwamba mimi sio bakhili au muongo au mwoga!" (Bukhari, Jihad, 24)

Hata baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kuanza kugawa ngawira, umati uliomzonga kwa kumzunguka ulikuwa ukimnyima raha kiasi kwamba ikalazimu awaambie jambo kwa kutolea mfano wa nabii mmoja wa zamani: "Mwenyezi Mungu alimtuma mja wake kwenda kwenye kabila fulani, wakampiga na kukipasua kichwa chake. Lakini mja huyo, wakati akifuta damu iliyokuwa ikitiririka

kutoka kichwani kwake kwa kutumia mkono wake, alikuwa akiomba: 'Mola wangu, wasamehe watu wangu, kwa maana hawajui walitendalo!'" (Ahmad, I, 456; Muslim, Jihad, 105)

Sababu ya uchelewaji huo ilikuja kubainika siku ya kumi tu baada ya kuwasili Jiranah. Siku hiyo, mjumbe kutoka kwenye kabila lililoshindwa la Hawazin alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ akitangaza kuwa watu hao wameukubali Uislamu na hivyo wanaomba kurejeshewa kwa mateka na mali zao zilizochukuliwa. Akizungumza kwa niaba yao, mtu mmoja kutoka ukoo wa Saad alichomoza na kusema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wale wanaosubiri chini ya kivuli ni shangazi, mama na baba zako wa kulea, na wanawake ambao walikunyonyesha na kukulea ulipokuwa mtoto! Kwa mfano, kama mtu ambaye tulimnyonyesha na kumlea angekuwa Mfalme wa Syria au Iraq, halafu tukaangukia katika hali kama hii na kuwaomba huruma na kutendewa wema, wasingetukatalia! Lakini wewe ni mtu bora ambaye mtu yeyote anatamani kumlea na kumtunza!"

Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Nilichelewa kugawa ngawira mpaka leo, lakini mmefika mkiwa mmechelewa sana. Sasa chagueni kati ya mateka wenu au mali zenu!"

Mjumbe huyo akapendekeza wakabidhiwe mateka wao. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: "Ninawarejeshea mateka waliokuwa katika fungu langu na fungu la Bani Abdulmuttalib. Njooni kesho baada ya swala ya adhuhuri kwa ajili ya mateka wengine!"

Siku iliyofuata, Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya Maswahaba na kuwafafanulia kuhusu hali hiyo. Aliwaeleza kuwa yeye mwenyewe ameshawarudishia mateka waliokuwa katika fungu lake. Kisha akasema: "Wenye kutaka kuwaacha huru mateka wao kwa hiari na hivyo kuwafanya ndugu zao wafurahi, basi wafanye hivyo. Na mwenye kutaka kutomtoa bure mateka aliyeangukia katika

fungu lake basi tutamfidia kwa ngawira za kwanza tutakazojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Wale wanaotaka hilo wanaweza kufanya hivyo!"

Mtukufu Mtume ﷺ aliwashaurisha Maswahaba zake kuhusu suala hili kwa sababu ya ukweli kwamba walikuwa na haki juu ya mateka hao.

Maswahaba walipomuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwaacha huru mateka wake mwenyewe, bila kusita, nao pia wakawaacha huru mateka wao, wakiwa na hamasa kubwa ya kupata fungu lao la dhawabu zinazowasubiri. Wakasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nasi pia tunawarudisha mateka wetu!" (Bukhari, Maghazi, 54; Ibn Hisham, IV, 134-135)

Hivyo, maelfu ya mateka walikabidhiwa kwa kabila la Hawazin siku hiyo, bila malipo ya fidia yoyote. Tukio hilo halikuwahi kushuhudiwa kabla katika historia. Lakini sasa, historia ilifanywa kusherehekea maelfu ya mateka wakiachiwa huru bila malipo yoyote ya kidunia, yote hayo kwa juhudi za Mtukufu Mtume ﷺ ambaye aliulea umma wake kwa maadili ya Kiislamu.

Ulikuwa ni uaminifu wa hali ya juu kabisa ambao Mtukufu Mtume ﷺ aliuonesha kwa watu, kwa sababu ya mwanamke aliyemnyonyesha wakati wa utoto wake, ambaye alikuwa ametokana nao. Ni somo la aina yake kwa wale waliozibwa macho na kuwa vipofu wakubwa; hususan wale wanaodhani kuwa wanadamu, kwa ujumla wao, wana silika na mwelekeo wa kufuta kumbukumbu za wema waliotendewa na wengine, badala ya kuzidhihirisha. Hivyo kwao, uaminifu hugeuzwa kuwa msamiati tu unaopatikana katika kamusi.

Wakiwa wamevutiwa mno na tendo hili kubwa la uaminifu, kabila lote la Hawazin lilisilimu. Hata kiongozi wao, Malik ibn Awf, ambaye wakati huo alikuwa Taif, alifurahi mno na kushangaa baada

ya kusikia habari hizo, kiasi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumtolea wito kidogo tu wa kuingia katika Uislamu. Mtukufu Mtume ﷺ alimpatia ngamia mia moja na kumsimika kuwa kiongozi wa kabila lake.[292]

Somo kubwa zaidi linalopatikana hapa ni kuwa njia bora ya kufanya *tabligh* ni kupitia maadili na tabia njema. Vilevile inaonesha ukweli kwamba wakati njia ya busara na ya kidiplomasia huleta faida kubwa, njia isiyokuwa na busara huleta hasara ya kiwango kikubwa.

Mtukufu Mtume ﷺ alizigawa ngawira kwa uadilifu, kwa njia bora kabisa. Katika mafungu matano ya ngawira yaliyogawanywa katika sehemu mbili, manne yaligawiwa miongoni mwa askari, huku fungu moja likipelekwa katika *Bayt'ul-Mal*, yaani Hazina. Ingawa hazina ilikuwa chini ya mamlaka ya Mtukufu Mtume ﷺ, hakuitumia kwa matumizi binafsi, kama alivyowaeleza Maswahaba zake kabla ya kuanza ugawaji, kwa kunyonyoa unywele kutoka kwa ngamia aliyekuwa mbele yake na kusema:

"Sina cha kuzifanyia ngawira zenu hata kidogo; hata nywele zake, achilia mbali ngamia...Kwa nini hamna subira? Hata kama ngawira zitakuwa nyingi kama mawe na miti ya bonde hili, nitazikabidhi kwenu. Iwapo nitabakisha moja ya tano ya hizi ngawira, itatumika tu kwa ajili ya maskini walio miongoni mwenu!" (Muwatta', Jihad, 22; Ahmad, V, 316)

Kutokana na amri aliyopewa na Mwenyezi Mungu, Mtukufu Mtume ﷺ alichukua fungu lililozidi kutoka katika hiyo moja ya tano na kuwapa *muallafat'ulqulub*, yaani wale ambao nyoyo zao zinatakiwa kuvutwa kwenye Uislamu. Miongoni mwao ni Hakim ibn Hizam, ambaye anasema:

292. Ibn Hisham, IV, 137-138.

"Nilitaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anipe kiasi cha ngawira. Akanipa ngamia mia moja. Nikaomba zaidi, akanipa nyingine mia moja. Nikaomba tena, akanipa nyingine mia moja. Kisha akasema, 'Ewe Hakim, hakika mali ni tamu na zenye kudanganya. Atakayezichukua bila ulafi atapata baraka kubwa katika mali hizo. Yule atakayezikodolea macho na kuzichukua kwa ulafi hatapata baraka ndani yake. Huo ni mfano wa wale wanaokula sana na wasishibe. Mkono unaotoa ni bora kuliko mkono unaopokea.'

Nikasema, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu aliyekutuma na dini ya haki, kwa muda wote nitakaoishi, sitapokea chochote kutoka kwa yeyote ila wewe.'"

Hakim ﷺ alichukua ngamia mia moja tu za mwanzo alizopewa na alizopewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, akawaacha waliobaki. Miaka mingi baadaye, zama Abu Bakr ﷺ alipokuwa Khalifa alimuita ili ampe fungu lake la ngawira, lakini alikataa. Baadaye, zama Omar ﷺ alipokuwa Khalifa alimuita Hakim kuja kuchukua ngawira, lakini akakataa kwa mara nyingine. Kwa kutambua kuwa hakuna mtu anayeweza kumshawishi Hakim ﷺ kuchukua kile alichokuwa akipewa, Omar ﷺ alihisi kuwa ni lazima awaambie wale waliohudhuria mahali hapo:

"Ndugu Waislamu, shuhudieni kwamba ninampa fungu lake la ngawira alilotengewa na Mwenyezi Mungu lakini amekataa kulichukua!" Hakim ﷺ aliendelea kutekeleza ahadi yake ya kutochukua chochote kutoka kwa mtu yeyote kwa muda wote aliokuwa hai. (Bukhari, Wasaya, 9; Waqidi, III, 945)

Safwan ibn Umayya, alikuwa mtu maarufu miongoni mwa Maqurayshi. Licha ya kutokuwa Muislamu, hakuondoka pembezoni mwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vya Hunayn na Taif. Vilevile Safwan alikuwa pamoja na Mtume ﷺ wakati akitembea katikati ya ngawira katika eneo la Jiranah pindi alipokuwa

akizikagua. Safwan ambaye alishikwa na mshangao, alikuwa akilikodolea macho bonde lililokuwa limejaa ngamia, kondoo na wachungaji kadhaa wanaowachunga. Mtukufu Mtume ﷺ alimtazama Safwan kwa pembe ya jicho lake. Akamuuliza:

"Unapenda unachokiona bondeni?"

"Ndiyo", alijibu Safwan.

"Unaweza kupata vyote...bonde na kilichomo!"

Safwan alishindwa kujizuia, akasema: "Moyo wa mtume ndio pekee unaoweza kuwa na ukarimu wa kiasi hicho!" papo hapo akatamka *shahadah* na kuwa Muislamu. (Waqidi, II, 854-855)

Baadaye, Safwan ؓ alirudi kwa Maquraysh na kuwaambia: "Enyi watu wangu, ingieni katika Uislamu. Naapa kwa Allah, hakika Muhammad anatoa kwa moyo bila hofu ya umaskini hata kidogo!" (Muslim, Fadail, 57-58)

Muallafa'tul-qulub wapatao arobaini, wakiwemo Abu Sufyan, Aqra ibn Habis, Uyaynah ibn Hisn, Abbas ibn Mirdas na Malik ibn Awf, walipewa kiwango cha kushangaza cha mali.[293]

Mshairi mmoja aitwaye Abbas ibn Mirdas, hakuridhika na kiwango alichopewa, akasoma shairi kali na lenye maneno machungu kuhusu Mtukufu Mtume ﷺ. Mtukufu Mtume ﷺ alipogundua, alimuita na kumwambia:

"Nitaukata ulimi wako!" Kabla ya kumwambia hivyo, alikuwa ameshamwambia Bilal Habashi ؓ kuwa: "Nitakapokuamuru kumkata ulimi mpe jozi ya nguo!"

Muda ulipofika, Mtume ﷺ alimuashiria Bilal kuwa "nenda kaukate ulimi wake!" Bilal alipommkamata, Abbas alianza kupiga

293. Waqidi, III, 944-947.

kelele na mayowe, "Hivi Mjumbe wa Mwenyezi anakwenda kunikata ulimi? Enyi Muhajirun! Anaukata ulimi wangu! Ee Ansar! Anaukata ulimi wangu!" Bilal ﷺ aliendelea kumsindikiza, huku mikono yake ikiwa imemkamata barabara. Lakini Abbas aliinyanyua zaidi sauti yake ya mayowe na makelele, Bilal ﷺ akamwabia: "Nyamaza! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amenimuru nikunyamazishe kwa jozi ya nguo!" Kisha Bilal ﷺ akampa Abbas jozi ya ziada, hapo akatulia na kunyamaza. Vilevile, Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alimpa ngamia mia moja. (Ibn Saad, IV, 273; Muslim, Zakat, 137)

Wakati wa kugawa ngawira, Saad ibn Abi Waqqas ﷺ alisema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, umemuacha mtu masikini kama Juayl ibn Suraqa na kuwapa watu maarufu kama Uyaynah na Aqra ngamia mia moja kwa kila mmoja!" Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Naapa kwa Allah, ambaye uhai wangu uko mikononi mwake, hatakama ardhi ingejaa watu kama Uyaynah na Aqra, bado Juayl angeendelea kuwa bora kuliko wote kwa pamoja! Lakini ninawaaangalia watu hawa kwa ajili ya kuwavuta kwenye Uislamu na kumpeleka Juayl kwenye Uislamu, ambao ameshikamana nao kikamilifu, na kumpeleka pia kwenye thawabu bora alizoandaliwa Siku ya Kiyama!" (Ibn Hisham, IV, 143; Ibn Saad, IV, 246)

Hatua ya *muallafat'ul-qulub* kupewa ngawira nyingi halikueleweka na wengi na lilisababisha ukosefu wa raha miongoni mwa Maswahaba. Mtu mmoja aitwaye Dhul-Huwaysirah, kutoka katika Ukoo wa Tamim, alivuka mpaka na kuonesha utovu wa heshima kiasi cha kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Fanya uadilifu!" Radiamali hii ilimhuzunisha mno Mtukufu Mtume ﷺ, akasema: "Ni hivyo? Ni nani atakayekuwa muadilifu kama sio mimi?" (Muslim, Zakat, 148)

Haukupita muda mrefu ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu ukateremka:

وَمِنْهُم مَّن يَلْمِزُكَ فِي الصَّدَقَاتِ فَإِنْ أُعْطُواْ مِنْهَا رَضُواْ وَإِن لَّمْ يُعْطَوْاْ مِنهَا إِذَا هُمْ يَسْخَطُونَ وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوْاْ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَقَالُواْ حَسْبُنَا اللَّهُ سَيُؤْتِينَا اللَّهُ مِن فَضْلِهِ وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ

"Na miongoni mwao wapo wanao kusengenya katika kugawa sadaka. Wanapo pewa wao huridhika. Na wasipopewa hukasirika. Na laiti wao wangeli ridhia kile alicho wapa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosheleza, Mwenyezi Mungu atatupa katika fadhila yake - na pia Mtume wake; hakika sisi ni wenye kumtaka Mwenyezi Mungu!" (at-Tawbah, 58-59)

Aya hizo zinaeleza kuwa licha ya suala la ugawaji wa ngawira kushughulikiwa na Mtume ﷺ, kiukweli ilitokana na maagizo ya Mwenyezi Mungu. Vilevile zinasisitiza uwepo wa tofauti baina ya mtu mjingi na Yule aliyetosheka moyoni.

Radiamali kubwa ilitoka upande wa Ansar. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa ametumia fungu kuu, yaani nne ya tano ya ngawira, kuwapa watu hao waliolalamikiwa. Bali alitumia fungu linaloitwa *fay*, moja ya tano ya ngawira hizo, ambayo alikuwa na udhibiti wa kipekee juu yake. Hata hilo pia lilionekana kuamsha radiamali ya vijana wa *Kiansari*.[294] Ili kutuliza pingamizi lililokuwa likitolewa kutokana na hatua yake hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya *Ansar* kabla hali hiyo haijavuka mpaka. Katika mkusanyiko huo ambao ulikuwa maalumu kwa Ansar pekee, ili kuwafanya waelewe kiini cha suala hilo, Mtukufu Mtume ﷺ alizungumza nao kwa namna ifuatayo, akiwakumbusha neema walizokuwa wamepewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu:

294. Kâmil Mîras, Tecrîd Tercemesi, X, 341.

'Enyi Ansar…! Ninasikia malalamiko kuhusu mimi ambayo yanatembea ndani ya nyoyo zenu. Lakini niambieni…je Mwenyezi Mungu hakuwaonesha njia ya haki kupitia mimi mlipokuwa mmepote? Je hamkutajirika baadaya mimi kuja kwenu, ambapo hapo kabla mlikuwa masikini? Je nyoyo zenu hazikuunganishwa na Mwenyezi Mungu kwa ujio wangu, pindi chuki na uadui vilipokuwa vikiwatafuna?"

Walimjibu maswali yote hayo wakisema: "Baraka zote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu na shukran kwa Mtume Wake!"

Mtukufu Mtume ﷺ aliendelea na hotuba yake yenye mguso. Akasema: "Kama mkinambia kuwa ulikuja kwetu baada ya watu wako kukukataa nasi tukakusadiki! Tulikusaidia pindi watu wako walipokataa kukusaidia! Watu wako walikufukuza nasi tukakupoke! Ulikuwa maskini nasi tukakufanya kuwa mashirika katika mali yetu', nitakubali na kusema, 'mlichosema ni kweli!'

Enyi Ansar…! Je ni kweli kuwa mmesema mambo Fulani kwa sababu ya mimi kuwapa mali za kidunia baadhi ya watu? Je mlikasirishwa na mimi kuwapa mali hafifu za kidunia baadhi ya watu ili kuwavuta kwenye Uislamu na kuwanyima nyinyi, kwa sababu ya kuiamini nguvu na ukomavu wa imani yenu…je hilo ndilo linalowahuzunisha? Enyi Ansar…je hamtaki kurejea nyumbani mkiwa na mtume wenu huku watu wengine wakirudi na mali zao?"

Machozi ambayo yalikuwa yameshaanza kujikusanya katika macho ya Ansar, sasa yalianza kutiririka kwa wingi kutokana na kuguswa na maneno ya Mtukufu Mtume ﷺ. Walikuwa wakilia huku wakisema: "Tunataka kurudi nyumbani pamoja nawe, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Upendo mkubwa waliokuwa nao kwake ukapata nguvu upya. Mtukufu Mtume ﷺ, naye pia, alikuwa akilia pamoja nao. Ili kuwafariji na kutambua moyo waliouonesha, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Enyi Ansar…Lau kusingekuwepo na

heshima na ubora wa Hijrah, bila shaka ningependa niwe mwenye kutokana na Ansar. Enyi Ansar…lau kila mtu angetakiwa kufuata njia, basi ningefuata njia ya Ansar!"

Kufuatia mkutano huu mkubwa, malalamiko ya yaliyotokea yalitengeneza njia ya hisia za kutosheka na kuridhia kuwa pamoja na "Mwenyezi Mungu na Mtume Wake", ambayo baadaye uligeuka kuwa shauku inayorindima kutoka katika safu za Ansar. Jeraha lililosababishwa na sintofahamu likawa limepatiwa tiba ya kudumu na Mtukufu Mtume ﷺ. (Bukhari, Maghazi, 56; Muslim, Zakat, 135; Haythami, X, 31)

Kuna mazingatio na mafunzo mengi kutokana na mwenendo huo wa mfano ulioneshwa na Mtukufu Mtume ﷺ hapo juu. Kwa asili, binaadamu ni wenye kupenda kutendewa wema na kukirimiwa. Adui anapotendewa wema na kukirimiwa hawezi kuendeleza uadui wake tena; na kama anayefanyiwa wema huyo ni rafiki, urafiki huo utaimarika zaidi na zaidi.

Mtukufu Mtume ﷺ alivaa *ihram* kwa ajili ya umrah na kuondoka Jiranah baada ya kukaa huko kwa muda wa siku kumi na tatu.[295] Na kwa hivyo inahesabiwa kuwa kuna fadhila na ubora mkubwa kwa wale wanaokaa Makka na viunga vyake kuvaa *ihram* katika eneo la Jiranah.

Adhabu ya Kosa la Kumuua Muislamu

Kabla ya kuondoka Madina, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amekwishatuma kikosi kidogo chini ya uongozi wa Abu Qatadah

295. Bukhari, Umrah, 3; Tirmidhi, Hajj, 92/935.

kwenda Najd, kama mbinu ya kuficha eneo hasa ambalo jeshi la Kiislamu lilikusudia kuelekea. Kikosi hicho kilipofika katika eneo la Izam, walikutana na mtu aitwaye Amir ibn Adbat, ambaye baada ya kutoa salamu na kutamka shahaadah, aliwaambia kuwa yeye ni Muislamu. Lakini kutokana na mzozo uliokuwepo huko nyuma baina yake na Muhallim ibn Jassamah, ambaye alikuwepo katika kikosi hicho, alidai kuwa Amir hakuwa Muislamu bali alikuwa akijionesha hivyo, akamuua na kuchukua mali zake kama ngawira.

Wakati kikosi cha Abu Qatadah kikirejea kutoka Najd, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amemaliza kuswali swala ya adhuhuri katika Bonde la Hunayn na alikuwa amekaa chini ya mti huku akiwa amezungukwa na Maswahaba.Mtume ﷺ alijulishwa juu ya tukio hilo na kufuatiwa na aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُواْ وَلاَ تَقُولُواْ لِمَنْ أَلْقَى إِلَيْكُمُ السَّلاَمَ لَسْتَ مُؤْمِنًا تَبْتَغُونَ عَرَضَ الْحَيوةِ الدُّنْيَا فَعِندَ اللَّهِ مَغَانِمُ كَثِيرَةٌ كَذَلِكَ كُنتُم مِّن قَبْلُ فَمَنَّ اللَّهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُواْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا

"Enyi mlio amini! Mnapo safiri katika Njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni, wala msimwambie anaye kutoleeni salamu: Wewe si Muumini; kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii, hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi. Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu akakuneemesheni. Basi chunguzeni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda." (an-Nisa, 94)

Muda mfupi baadaye, familia ya Amir iliwasili kwa ajili ya kumshtaki Muhallim kwa kosa la mauaji. Baada ya mashtaka marefu, kwa uthibitisho wa familia ya Amir, Mtukufu Mtume ﷺ alimpa adhabu Muhallim ya kulipa fidia kwa familia ya marehemu.

"Kwa hiyo ulimuua Amir licha ya kukwambia kuwa yeye ni Muislamu…" alithibitisha Mtukufu Mtume ﷺ.

Muhallim hakuwa na la kufanya zaidi ya kusema: "Ewe Mjume wa Mwenyezi Mungu, niombee msamaha!" jambo lililoonesha kukubali kuwa alitenda kosa kwa kujua. Kwa kuwa alikuwa amemuua mtu asiyekuwa na hatia licha ya kuwa Muislamu, kosa la Muhallim halikuwa kosa la kusamehewa kiurahisi. Kuonesha uvumilivu hata kidogo kuhusu jambo hilo kungesababisha ugumu wa kukabiliana na makosa kama hayo katika siku za baadaye. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ alilikataa ombi la Muhallim la kuombewa msamaha na badala yake akasema: "Mwenyezi Mungu asikusamehe!"[296]

Kutokana na kuathiriwa na ghadhabu ya Mtukufu Mtume ﷺ, Muhalli, alienda nyumbani na kubaki mafichoni. Hatimaye alifariki wiki moja baadaye kutokana na huzuni na majuto yaliyokithiri. Familia yake ilipojaribu kumzika, ardhi iliutoa nje mwili wake. Kila walivyojaribu, ilitokea hali hiyo hiyo. Wakiwa wanyonge na wenye kushtushwa, walikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuelezea kuhusu tukio hilo. Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Ardhi imezipokea maiti nyingi zenye uovu zaidi, lakini Mwenyezi Mungu anataka kukufundisheni somo na thamani ya *La ilaha illa Allah*!" Kisha akawaelekeza wamzike Muhallim kwa mara nyin-

296. Swahaba aliyesimulia hadith hii anasema: "Miongoni mwetu tulikuwa tukisema 'Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuombea msamaha lakini alifanya vile ili kuonesha ukubwa wa kosa la Muhallim na kuwazuia watu wasiuane wao kwa wao.'" (Ahmad, V, 112; Ibn Hisham, IV, 304)

gie na waweke mawe juu ya kaburi lake. (Ahmad, V, 112; Ibn Majah, Fitan, 1; Ibn Hisham, IV, 302; Waqidi, III, 919)

Mtukufu Mtume ﷺ alifanya hivyo ili kuweka mkazo wa ubaya wa kuvunja haki na heshima ya *La ilaha illa Allah* na ya Muislamu mwenzetu, ili kuonesha kuwa ni dhambi kubwa kumuua Muslamu mwenzako kwa sababu tu ya mali za kidunia na hivyo kuwazuia wengine wasifanye makosa na uhalifu kama huo.

Tukio hili linaonesha kwamba watu wote wanatoa shahada ya *tawhid* wanahesabiwa kuwa ni Waislamu. Ni haramu kuitilia shaka imani ya mtu, mpaka pale atakapoonesha ukafiri wake waziwazi.

Vilevile, tukio hili linaonesha umuhimu kwa Waislamu kutazama ukweli wa dhahiri (nje) wa jambo husika wakati wa kulihukumu. Kwa kuzingatia kuwa siku zote kuna chembe ya udanganyifu hata wakati wa kupitisha hukumu kwa kutegemea mambo ya nje, kama wanadamu wangepewa nafasi ya kupitisha hukumu zao kwa kuangalia mambo ya ndani, wasingeweza kuepuka kufanya dhulma nyingi kutokana na tafsiri zao za kujipendelea.

Sababu nyingine ya ulazima wa kuhukumu kwa kuangalia mambo ya nje ni ili kuwazuia baadhi ya watu wasitumie visingizio kama vile 'tazama moyo wangu, usitazame matendo yangu' kuhalalisha uhalifu na makosa yao. Mbinu hii ambayo hutumika siku hizi inabatilishwa na kanuni ya hapo juu iliyowekwa na Uislamu na pia matendo ya Mtukufu Mtume ﷺ. Kuhukumu kwa kuangalia mambo ya nje kunaweza kuonekana kutoa mwanya wa muda mfupi kwa wanafiki kwa kuwapa fursa ya kuficha unafiki wao wa ndani kwa kuonesha matendo yao ya nje; lakini bado inaendelea kuwa kizuizi dhidi ya dhulma kwa kutoa ushahidi wa kukisia badala ya kukiri.

Kumteua Gavana na Mwalimu wa Makka

Kabla ya kuondoka Makka, Mtukufu Mtume ﷺ alimteua Attab ibn Asid ؓ kama gavana, kuongoza mji huo na kuendesha mambo yanayohusiana na hijja. Kabla ya hapo, wakati Mtukufu Mtume ﷺ akielekea katika Vita vya Hunayn alikuwa amemuacha Attab ؓ kama kaimu wake mjini Makka. (Ibn Hisham, IV, 69, 148) Wakati huo, Attab ؓ alikuwa na umri wa miaka ishirini.[297] Licha ya kuwepo kwa Maswahaba wenye uzoefu na umaarufu mkubwa, Attab ؓ ndiye aliyekabidhiwa jukumu la ugavana. Hii inaonesha kuwa nyadhifa na majukumu vinatakiwa kutolewa kwa watu wenye uwezo, wenye kutumia elimu na maadili, na wanaojulikana kwa usafi na wema wao.

Kwa kweli, Maswahaba waliotoa mchango mkubwa sana katika kuupeleka Uislamu kwa vizazi vijavyo, wengi wao walikuwa vijana kama Attab ibn Asid ؓ. Kwa mfano, Abdullah ibn Omar na Ibn Abbas ؓ, ambao ni miongoni mwa Maswahaba waliopokea idadi kubwa zaidi ya ahadith, walikuwa na umri wa miaka kumi na tatu wakati wa kifo cha Mtukufu Mtume ﷺ, huku Anas, Ibn Masoud na Aisha ؓ wakiwa na umri wa miaka kumi na nane. Vilevile Maswahaba wengi waliokuwepo katika Makubaliano ya Aqabah walikuwa vijana; na vivyo hivyo walimu wengi wa Qur'an waliouawa katika tukio la Bi'r Maunah walikuwa vijana. Hii inaonesha umuhimu wa kuwalea na kuwaandaa vijana watakaobeba majukumu ya kutengeneza mustakbali wa Uislamu.

Daima Mtukufu Mtume ﷺ aliwataka Waislamu wapya wajifunze Qur'an na Sunnah bila kupoteza muda. Hivyo, alikuwa akiwapa mafunzo ya ndani kabisa wale walikuja kusilimu kwake sanjari na Maswahaba zake, hata kama mafunzo hayo yatakuwa kwa siku

297. Hâkim, III, 303/5181.

chache tu. Kila baada ya kuswali swala ya alfajiri, alikuwa wakiwatembelea na kuangalia walichojifunza na anapoona kuwa maarifa yao hayajabadilika, alikuwa akiwatuma kwenda kwa maswahaba wengine na kuhakikisha wanajifunza kikamilifu.

Kutokana na umakini huu wa kuyapa umuhimu mafunzo ya Uislamu, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaacha Muadh ibn Jabal[298] na Abu Musa al-Ash'ari[299] رضي الله عنه mjini Makka kwa kazi ya kuwafundisha wenyeji Qur'an na *fiqh*, yaani sheria za Uislamu. Hii inathibitisha umuhimu tunaotakiwa kuutoa kwenye mafunzo ya Uislamu.

298. Waqidi, III, 959.

299. Ibn Saad, II, 160.

MWAKA WA TISA WA HIJRAH

Upanga wa Fasihi

Mtukufu Mtume ﷺ alituma kikosi kidogo cha askari wa farasi chini ya uongozi wa Uyaynah ﷺ kwenda kwa kabila la Banu Tamim, ambao walikuwa wamegoma kulipa Zaka. Kwa shambulio la ghafla, Waislamu waliweza kuwashinda waasi hao na kurejea Madina wakiwa na kiasi kikubwa cha ngawira na mateka.[300]

Idadi kubwa ya watu mashuhuri wa Banu Tamim, wakiandamana na washairi wao wakubwa, walikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ kwa ajili ya kuwakomboa mateka wao. Wakati wakimsubiri Mtukufu Mtume ﷺ atokee ndani ya msikiti, walishindwa kuwa wavumilivu na badala yake wakaanza kupiga kelele bila heshima "Njoo sasa hivi! Njoo twakusubiri!"

Mtukufu Mtume ﷺ alihisi kuhuzunishwa na makelele yao. Baadaye aya ifuatayo ikateremka:

إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ

"Hakika hao wanao kuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili." (al-Hujurat, 4) (IbnHisham, IV, 223, 233)

300. Bukhari, Maghazi, 68.

Baada ya swala ya Adhuhuri, Mtukufu Mtume ﷺ alikaa katika uwanja wa Msikiti.

"Tumekuja na washairi na malenga wetu ili tusomeane mashairi", alisema msemaji wa kabila hilo.

"Sikutumwa kusoma mashairi", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. "Lakini mnaweza kuendelea." (Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, I, 128)

Mtu mmoja kutoka katika kabila hilo alisimama kwa miguu yake na kutoa hotuba yenye ufasaha. Mtukufu Mtume ﷺ akamuashiria Thabit ibn Qays ؓ, ambaye alisimama na kutoa hotuba ya kipekee juu ya ukuu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na utume wa Mtukufu Mtume ﷺ, hotuba ambayo ilikuwa bora kuliko ile iliyotolewa na msemaji wa Tamim.

Shairi lililosomwa na Zibriqan ibn Badr kutoka Banu Tamim lilijibiwa na shairi zuri sana lilotolewa na mshairi mahiri, Hassan ibn Thabit ؓ, na kuipa heshima kuu dini ya Uislamu.

Ushindi wa Maswahaba ulitokana na umahiri na kuzama kwao ndani ya Qur'an Tukufu, ambayo ni kilele cha ajabu cha fasihi, na kutokana na mafunzo waliyopata wakiwa mbele ya Mtume ﷺ, ambaye ndiye mzungumzaji fasaha na mzuri zaidi kuwahi kutokea, mwenye maneno yanayojulikana kama *jawami'ul-kalim* kutokana na uwezo wake wa ajabu wa kuelezea maana kamili ndani ya maneo machache na rahisi. Msukumo huu kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ umepewa sauti tamu katika utenzi usemao:

Kumuona mara moja, hugeuka kuwa waridi,
Hugeuka kuwa kurumbizi, wale wanaoyasikia maneno yake…

Kwa kutambua matokeo, mashairi Aqra ibn Habis kutoka kabila la Tamim akasema, "Malenga wake ni wazuri kuliko wetu na washairi wake ni bora sana kuliko wetu. Maneno yao yapo juu ya

maneno yetu!" Baada ya kusema hivyo, alitangaza kuingia katika Uislamu, hatua iliyofuatiwa na wenzake kusilimu bila kusita. Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akawapa wajumbe hao kiwango kikubwa cha zawadi. (Ibn Hisham, IV, 232)

Ni wakati huo huo ambapo yalizuka mabishano baina ya Abu Bakr na Omar ؓ mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ, tukio lililopelekea kuteremka kwa aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

"Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui." (al-Hujurat, 1-2)

Baada ya hapo, Omar ؓ alianza kushusha sauti yake kiasi kwamba anapokuwa mbele ya Mtume ﷺ wakati mwingine hata Mtume ﷺ alikuwa akipata shida kusikia kile anachokisema, na kulazimika kumtaka arudie maneno yake mara mbilimbili.[301]

Maswahaba wengine pia waliingiwa na hisia ya kumheshimu Mtukufu Mtume ﷺ. Walikuwa wakifanya kila linalowezekana

301. Bukhari, Tafsir, 49/1.

kuhakikisha kuwa Mtukufu Mtume ﷺ hahisi kukosa raha. Baada ya kuteremka kwa aya hizo, Swahaba mmoja aliyekuwa maarufu kwa sauti yake ya juu, alilazimika kubaki nyumbani kwake kwa siku kadhaa, akihofia kuwa sauti yake yaweza kumkera Mtukufu Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alimtembelea na kumtuliza ndipo akamudu kutoka nje.[302]

Mtukufu Mtume ﷺ anapokuwa amekaa kwenye meza ya chakula, Maswahaba wasingenyoosha mikono yao kuchukua chakula kabla yake.[303] Wanapogonga mlango wa nyumba yake walikuwa wakigonga kwa ncha za vidole vyao na kuepuka kila aina ya tabia inayoweza kusabbaisha kero kwa Mtukufu Mtume ﷺ.[304] wanapomuelezea walikuwa wakimsifia kwa kumfananisha na jua au mwezi kutokana na upendo na heshima waliyokuwa nayo kwake.[305] Umakini wao ulienda mbali zaidi hata wakati wa kusimulia *ahadith* za Mtume ﷺ. Wakati wa kusimulia hadith, mazungumzo yao yalikuwa yakibadilika, jasho likitiririka kwa wingi nyusoni mwao, machozi yakijikusanya machoni mwao na mishipa katika shingo zao ikituna kutokana na msisimko.[306] Wanaposikia sauti yenye makelele, kama vile sauti ya nyundo wakati wa kupigilia msumari au nguzo kutoka kwenye nyumba za jirani na Msikiti, mara moja walikuwa wakituma ujumbe kumwambia mtu husika kuacha kumsumbua Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ. Baadhi walikuwa wakitengenezea milango yao nje ya mji wa Madina, kuepuka kusababisha hali ya maudhi.

302. Abu Dawud, Atimah, 15/3766.
303. Bukhari, *Adabu'l-Mufrad*, uk.316; Haythami, VIII, 40.
304. Muslim, Fadail, 109.
305. Ibn Saad, III, 156; Ibn Majah, Muqaddimah, 38; Dârimî, Muqaddimah, 28.
306. Kastallânî, II, 386.

Mwanzoni Kaab ibn Zuhayr alikuwa miongoni mwa washairi waliokuwa wametangaza vita dhidi ya Uislamu.Kutokana na shairi la dhihaka alilolisoma, adhabu ya kifo ilitolewa dhidi yake. Ili kumuweka sawa, ndugu yake, Bujayr, ambaye alikuwa Muislamu, alimtumia shairi, akimshauri kuwa alikuwa akikabiliwa na mwisho mchungu mpaka atakapojisafisha kutokana na mwenendo wake. Alipatwa na wasiwasi sana, na kwa kusaidiwa na Swahaba mmoja, Kaab akaenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kula kiapo cha utii, lakini bila kujitambulisha. Alipiga magoti na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kaab ibn Zuhayr naye anataka kuja mbele yako na kuomba msamaha kwa kuukubali Uislamu. Je unamkubalia?"

Mtukufu Mtume ﷺ alipokubali, Kaab akasema kwa furaha ya hali ya juu: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mimi ni Kaab!" (Ibn Hisham, IV, 152; Hakim, III, 675/6480; Haythami, IX, 393)

Katika kuonesha shukrani kwa wema wa kusamehewa na Mtume ﷺ, Kaab akaanza kusoma *qasidah* ya *Banat Suade* aliyokuwa ameiandaa. Mtukufu Mtume ﷺ, katika kutambua kilichofanywa na Kaab, alivua joho lake kutoka mgongoni mwake na kuliweka yeye mwenye mgongoni kwa Kaab. Kwa hiyo, *qasidah* hiyo imekuja kujulikana kama *Qasidatul-Burdah*. *Burdah* ni joho katika lugha ya Kiarabu.

Baada ya kifo cha Kaab, joho hilo alililopewa zawadi lilinunuliwa na Muawiyah رضي الله عنه. Joho hili ndiyo *Hirka* iliyohifadhiwa katika Kasri ya Topkapi katika chumba cha Hirka –Saadatnchini Uturuki. Hirka ina maana ya joho katika lugha ya Kituruki. Joho hili limetunzwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine mpaka sasa.

Kuna *qasidah* nyingine ijulikanayo kama Qasidatul-Burdah, ya Imam Busiri.[307] Hata hivyo, jina sahihi la qasidah hii ya pili ni *Qasida-i Bur'a.Bur'a* ni neon la Kiarabu lenye maana ya kupona kutokana na maradhi. Imam Busiri aliita qaswida yake kwa jina hili katika kukumbuka tukio la kupona maradhi yake ya kupooza. Kisa hiki kilitokea kama ifuatavyo:

Imam Busiri alikuwa amepooza nusu ya mwili wake. Hivyo, akaandika *Qasidal-i Bur'a* na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amponye. Usiku aliomaliza kuandika *qasidah* hiyo, aliona ndoto. Katika ndoto hiyo alimsomea Mtukufu Mtume ﷺ kile alichoandika. Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amefurahi kulisikia shairi, aliupiga upande wake uliokuwa umepooza. Imam Busiri alipoamka na kuona kuwa hakuwa na maumivu tena, alimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu. Alipokuwa akielekea msikitini kwa ajili ya swala ya alfajiri, alikutana na mwanazuoni mkubwa, Abu'r-Raja, ambaye alimtaka asome *qasidah* hiyo ambayo ndani yake alimsifu Mbora wa Viumbe ﷺ.

"Nina mashairi mengi kama hayo. Lipi unalotaka?" aliuliza Imam Busiri.

"Ile uliyomsomea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu usiku", alisema Sheikh Abur-Raja. "Nilimuona akiwa na furaha kubwa wakati ukilisoma."

Imam Busiri alishtuka, akauliza kwa mshangao: "Ulijuaje kuhusu ndoto hiyo wakati sijamwambia mtu yeyote?"

"Nilikuwepo pia", alijibu Sheikh Abur-Raja, kisha akasoma ubeti wa kwanza:

307. Muhammad ibn Saîd al-Bûsirî anatoka Misri, aliishi katika karne ya 13 katika zama za utawala wa Mamluk. (608/1211-694/1296) (H. İbrâhim Şener, *Kasîde-i Bürde Kasîde-i Bür'e ve Su Kasîdesi*, uk. 32, 60)

Ewe moyo wangu, ni watu wa Salam[308] *unaowakumbuka,*

Kiasi kwamba umechanganya damu kwenye machozi yanayotiririka kutoka machoni mwako?

Imesimuliwa kuwa, wakati qasidah hii ikisomwa mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ, alikuwa akitabasamu na kuutikisa mwili wake taratibu kwa furaha, kama mtetemeko wa madaha wa majani.

Kwa njia Fulani, tangu wakati huo, *qasidah* hii imeendelea kusomwa kwa wagonjwa, kwa matumaini ya kudhihirisha hali ya kiroho ya Mtume ﷺ, na pia imekuwa ikitumiwa kama njia ya kuomba ponyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.[309]

Chunguzeni Ukweli wa Habari !

Walid ibn Uqbah, alitumwa na Mtukufu Mtume ﷺ kwenda kwa Banu Mustaliq kukusanya Zaka. Alirudi baada ya kuona kundi la watu wa kabila hilo wakija kumpokea, akidhani kuwa walikuwa wamekuja kumuua, kutokana na kwamba huko nyuma, katika zama za Ujahiliya, alikuwa na mgogoro na watu hao. Aliporudi Madina, alimpa Mtukufu Mtume ﷺ taarifa ya uongo juu ya kile kilichokuwa kimetokea, akaenda mbali zaidi kiasi cha kuwakashifu Banu Mustaliq kwa lengo la kujisafisha.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, wametoka katika Uislamu!" alisema. "Sio tu kwamba walikataa kutoa Zaka, walikaribia hata kuniua!"

Haraka sana, Mtume ﷺ aliandaa kikosi cha jeshi kwenda kukabiliana na kile kilichoonekana kama kabila lililoasi. Hata hivyo,

308. *Salam* ni jina la kijisitu ambacho Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akikaa na kuzungumza na Maswahaba wake mara kwa mara.

309. İlhan Armutçuoğlu, *Kasîde-i Bürde*, Konya 1983, uk.8-11.

Banu Mustaliq walipogundua hali hiyo, haraka sana, wakatuma ujumbe uleule uliokuwa umeenda kumpokea Walid, kwenda Madina. Huko walikutana na kikosi cha farasa cha jeshi la Kiislamu kilichokuwa kimeandaliwa kwenda kuwakabili. Ukweli uliosababisha mkanganyiko huo ukapatikana. Hapo, Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha ufunuo kuwaonya Waislamu wasipitishe uamuzi mpaka wajue undani wa suala husika:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَى مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ وَاعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ اللَّهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ أُوْلَئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ

"Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda. Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angeli kut›iini katika mambo mengi, bila ya shaka mngeli taabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka." (al-Hujurat, 6-7)

Mtukufu Mtume ﷺ akamuagiza Abbad ibn Bishr ﷺ kuwa: "…rudi pamoja nao na ukusanye Zaka; lakini usichague Zaka bora katika bidhaa zao!" Abbad ﷺ alikaa kwa Banu Mustaliq kwa muda wa siku kumi, kipindi ambacho alikitumia kuwafundisha Qur'an na Uislamu. (Ahmad, IV, 279; Ibn Hisham, III, 340-341; Ibn Saad, II, 161)

Habari na taarifa nyingi kutoka kwa watu waovu husafiri kutoka kinywa kimoja kwenda kingine na hatimaye kumfikia mtu mwema lakini mjinga, ambaye japokuwa hajishughulishi na matendo maovu, anausambaza uvumi huo kwenda kwa wengine kwa nia njema. Yapaswa kueleweka wazi kuwa kuchukua taarifa zisizithibitishwa na kuzisambaza ni kinyume na uwajibikaji, bila kujali kama mtu anayezisambaza ni muovu au la. Yumkini yasiwepo madhara yoyote iwapo ikigundulika kuwa habari hizo ni za kweli lakini kwa upande mwingine, iwapo itabainika kuwa ni habari za uzushi, basi usambazaji wake utamfanya mhusika kuingia katika dhambi kubwa kama kukashifu na kusengenya. Hivyo, daima mtu anatakiwa kuwa mdadisi juu ya habari, hususan habari mbaya kutoka kwenye vyanzo vyenye kutia shaka.

Safari ya Kivita ya Tabuk: Mtihani Mkubwa wa Iman (Rajab, 9 / Septemba-Oktoba, 630)

Safari ya Tabuk, ambao ni mji ulio katikati ya Madina na Damascus, ndiyo safari ya mwisho ya kivita iliyofanywa na Mtukufu Mtume ﷺ. Safari hii inahesabiwa kuwa muendelezo wa Vita Vya Muta. Mtemi wa Warumi, akiwa bado hajapumzika kutoka katika Vita vya Muta, alikuwa na nia ya kuivamia Arabia yote kabla nguvu za Waislamu hazijafikia kilele cha kutisha. Akiwa na lengo la kuzima kile alichokiona kama shambulio na uvamizi wa Waislamu, alitaka kuwatumia Wakristo wa Kiarabu. Waghasani, ambao aliwaona kama wastahiki sahihi na halisi wa jambo hili, walikuwa tayari kabisa kwa kazi hiyo. Habari za kuwepo kwa shambulizi kubwa zililetwa Madina na misafara ya wafanyabiashara, wakionya kuwa miji yao ilikuwa ikikabiliwa na shambulizi kubwa muda mfupi ujao.

Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya Maswahaba wote, vijana kwa wazee. Mpaka wakati huo, maandalizi kwa ajili ya safari yoyote ya

kivita yalikuwa yakifanyika kwa siri, ili kwamba maadui wasijue eneo husika linalokusudiwa kushambuliwa. Lakini sasa hali ilikuwa tofauti. Ilikuwa ni siku zenye joto kali mno la kiangazi. Walikuwa wakikabiliwa na adui imara na umbali mkubwa. Aidha, Waislamu walikuwa katika hali ngumu kiuchumi, wakiwa wamekumbwa na njaa na ukame ulioishambulia Madina mwaka huo.[310]

Kama kawaida, katika kusababisha tabu kubwa, wanafiki waliwasha upya moto wao wa shari na kujaribu kuwakatisha tamaa Waislamu. Kiongozi wao, Abdullah ibn Ubay, akiwa na kiburi kama kawaida yake, alianza kutoa dhihaka akisema: "Hivi Muhammad anadhani kuwa Warumi ni watoto wa kuchezea? Kuanzia sasa ninamuona akikamatwa mateka yeye na Maswahaba wake!"

Wanafiki wengine walifuata mfano huo wa ibn Ubay na kusema: "Mnawezaje kwenda vitani katika joto kali kama hilo?" Wahyi ukateremka kujibu dhihaka hizo:

فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلاَفَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُواْ أَن يُجَاهِدُواْ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُواْ لاَ تَنفِرُواْ فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَّوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ

"Walifurahi walio achwa nyuma kwa kule kubakia kwao nyuma na kumuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walichukia kupigana Jihadi kwa mali zao na nafsi zao, na wakasema: Msitoke nje katika joto! Sema: Moto wa Jahannamu una joto zaidi, laiti wangeli fahamu!" (at-Tawba, 81)

310. Ibn Saad, II, 165; Bukhari, Tafsir, 66/2.

Baadhi ya Mabedui, kwa upande mwingine, walikuja kwa Mtume ﷺ na kutoa nyudhuru za kutengenezwa, wakiomba wasishiriki katika Vita hivyo, kama inavyoelezwa na aya ifuatayo:

وَجَاء الْمُعَذِّرُونَ مِنَ الأَعْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُواْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ سَيُصِيبُ الَّذِينَ كَفَرُواْ مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

"Na walikuja wenye kutoa udhuru katika Mabedui ili wapewe ruhusa, na wakakaa wale walio mwambia Mwenyezi Mungu na Mtume wake uwongo. Itawafika walio kufuru katika wao adhabu chungu." (at-Tawbah, 90)[311]

Kufuatia hali hiyo, Qur'an Tukufu ikaweka vigezo vya wazi vinavyowatengenisha Waumini na wanafiki:

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لاَّتَّبَعُوكَ وَلَكِن بَعُدَتْ عَلَيْهِمُ الشُّقَّةُ وَسَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَوِ اسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ يُهْلِكُونَ أَنفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

"Na lau ingeli kuwa ipo faida ya papo kwa papo, na safari yenyewe ni fupi, wangeli kufuata. Lakini wameona ni mbali na kuna mashaka. Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu: Tungeli weza bila ya shaka tungeli toka pamoja nanyi. Wanaziangamiza nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa hakika hao ni waongo." (at-Tawbah, 42)

311. Waqidi, III, 993-996; Ibn Saad, II, 165.

لاَ يَسْتَأْذِنُكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ أَن يُجَاهِدُواْ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ إِنَّمَا يَسْتَأْذِنُكَ الَّذِينَ لاَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ وَارْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ

"Hawatakuomba ruhusa wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, wasende kupigana Jihadi kwa mali yao na nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua wachamngu. Wasio muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na nyoyo zao zikatia shaka, hao tu ndio wanao kutaka ruhusa. Basi hao wanataradadi katika shaka zao." (at-Tawbah, 44-45)

Mpaka wakati huo, wanafiki hawakuwa wamefanya maandalizi yoyote. Hii ilionesha wazi kuwa hawakuwa na nia kabisa ya kuungana na Waislamu katika safari ya kuelekea Tabuk. Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu akatangaza:

وَلَوْ أَرَادُواْ الْخُرُوجَ لأَعَدُّواْ لَهُ عُدَّةً

"Na ingelikuwa kweli walitaka kutoka bila ya shaka wangeli jiandalia maandalio…" (at-Tawbah, 46)

Lakini kwa baraka ya Mwenyezi Mungu, wanafiki hao walikuwa wakijivuta na kuonesha uzito wa kuungana na jeshi la Kiislamu. Hata kama wangeshiriki, bado Abdullah ibn Ubayy angerudia kuonesha tabia yake aliyoionesha wakati wa Vita vya Uhud na kujitenga na Waislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَلَكِن كَرِهَ اللَّهُ انبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ وَقِيلَ اقْعُدُواْ مَعَ الْقَاعِدِينَ لَوْ خَرَجُواْ فِيكُم مَّا زَادُوكُمْ إِلاَّ خَبَالاً ولأَوْضَعُواْ خِلاَلَكُمْ يَبْغُونَكُمُ الْفِتْنَةَ وَفِيكُمْ سَمَّاعُونَ لَهُمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ

"…lakini Mwenyezi Mungu alichukia kutoka kwao, na kwa hivyo akawazuia na ikasemwa: Kaeni pamoja na wanao kaa! Lau wangelitoka nanyi wasingeli kuzidishieni ila mchafuko, na wange tanga tanga kati yenu kukutilieni fitna. Na miongoni mwenu wapo wanao wasikiliza. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhaalimu." (at-Tawbah, 46-47)

Ingawa wanafiki tayari walikuwa washari na wenye kuasi, hiyo haikuwa chochote ikilinganishwa na madhara waliyosababisha wakati wa vita ambavyo walishiriki kwa kiasi fulani, wakilivuruga jeshi zima la Kiislamu kwa kueneza uvumi, urongo na sumu yao ya hofu na wasiwasi usiokwisha. Kila mnafiki alikuwa tatizo linalosubiri kufyatuka. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu akaingilia kati na kuwazuia wanafiki kujiunga na Safari ya kivita Vita ya Tabuk; safari ambayo shida na tabu zake zilionekana kuwa kikwazo kwao. Hivyo, Maswahaba wakapata sahali dhidi ya tabu zilizokuwa zikitengenezwa na wanafiki.

Wanafiki walitoa udhuru, wakitaka waruhusiwe kutoshiriki katika Vita hivyo. Wengine walienda mbali zaidi kiasi cha kudai kuwa walikuwa hawataki kushiriki kwa hofu kwamba wanaweza kutamanishwa na wanawake wa Kigiriki. Walikuwa wakijaribu kuficha unafiki wao kwa kujionesha kuwa wanaguswa na jambo fulani. Lakini, kwa mara nyingine, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaumbua:

وَمِنْهُم مَّن يَقُولُ ائْذَن لِّي وَلاَ تَفْتِنِّي أَلاَ فِي الْفِتْنَةِ
سَقَطُواْ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ

"Na miongoni mwao wapo wanao sema: Niruhusu wala usinitie katika fitina. Kwa yakini wao hivyo wamekwisha tumbukia katika fitina. Na hakika Jahannamu imewazunguka." (at-Tawbah, 49)

Wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwaonya wanafiki juu ya adhabu kali inayowasubiri, wakati huo huo alikuwa akiwaonya baadhi ya Waislamu, ambao walikuwa wakionesha dalili za ulegevu kutokana na athari za propaganda za wanafiki:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انفِرُواْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الأَرْضِ أَرَضِيتُم بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الآخِرَةِ إِلاَّ قَلِيلٌ إِلاَّ تَنفِرُواْ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلاَ تَضُرُّوهُ شَيْئًا وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache. Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu." (at-Tawbah, 38-39)

انْفِرُواْ خِفَافًا وَثِقَالاً وَجَاهِدُواْ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ

"Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kheri kwenu mkiwa mnajua." (at-Tawbah, 41)

Maonyo haya yalikuwa na athari ya moja kwa moja kwa Waislamu, yakawapa nguvu mara moja. Ulegevu ualiokuwa umezifunika nyoyo zao ukaondoka, na mahali pake ikaja nguvu na hamasa. Maandalizi ya *iman*, yaliyochanganywa na hamasa, sasa yalikuwa yamekamilika. Aidha, ilikuwa ni *fard'ul-ayn*, kwa maana ya faradhi ya lazima kwa Waislamu wote kuitikia wito wa *jihad* kuelekea sehemu ambayo adui alikuwa akijiandaa kuishambulia ardhi ya Waislamu.Pamoja na hayo, wale ambao kisheria walikuwa na ruhusa ya kutoitikia wito wa *jihad* waliainishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَّيْسَ عَلَى الضُّعَفَاء وَلاَ عَلَى الْمَرْضَى وَلاَ عَلَى الَّذِينَ لاَ يَجِدُونَ مَا يُنفِقُونَ حَرَجٌ إِذَا نَصَحُواْ لِلّهِ وَرَسُولِهِ مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِن سَبِيلٍ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Hapana lawama kwa wanyonge, wagonjwa, na wasio pata cha kutumia, maadamu wanamsafia niya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hapana njia ya kuwalaumu wanao fanya wema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." (at-Tawbah, 91)

Kwa mujibu wa tangazo la aya hiyo, wale ambao wameruhusiwa kutoshiriki vita, wanapobaki nyuma, hawatakiwi kusababisha maovu katika mji wao au kusambaza uongo, kueneza uvumi na wanatakiwa kufanya haraka kuzisaidia familia za wale wanaoshiriki katika vita; na iwapo watakuwa 'wenye kutenda kheri', hawatakuwa na lawama yoyote juu yao wala dhambi. Wakati huo huo, kwa kuwa

hakuna tangazo la wazi linalowakataza kushiriki katika vita, kama wakitaka na wakawa na uwezo wa kufanya hivyo, wana uhuru wa kuungana na jeshi kwa sharti kwamba wasiwe mzigo kwa wengine.

Sasa Maswahaba walijikuta katikati ya kimbunga cha furaha na msisimko, wakitarajia kuyatoa maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata hivyo, Maswahaba saba ambao walikuwa masikini, hawakuweza kupata vipandwa kwa ajili ya kushiriki katika safari hiyo. Kwa hali yoyote, Maswahaba wote kwa ujumla walilazimika kushirikiana ngamia mmoja na wakati mwingine Maswahaba watatu walikuwa wakipanda ngamia mmoja. Lakini hawa saba hawakuweza kupata hata ngamia mmoja ambaye wanaweza kushirikiana angalau wawili au watatu, licha ya hamu yao ya kutaka kushiriki katika vita hivi. Hivyo, waliamua kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ kumtaarifu juu ya tatizo lao. Lakini, Mtukufu Mtume ﷺ alipowaambia kuwa hakuwa na ngamia wa kuwapa, waliangua kilio na kurudi nyumbani wakiwa na majonzi. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyatambua machozi yaliyomwagika katika njia tukufu kabisa na machozi yao hayo yamezungumziwa ndani ya Qur'an Tukufu:

وَلاَ عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لاَ أَجِدُ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّواْ
وَّأَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلاَّ يَجِدُواْ مَا يُنفِقُونَ

"…Wala wale walio kujia ili uwachukue ukasema: Sina kipando cha kukuchukueni. Tena wakarudi na macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kukosa cha kutoa." (at-Tawbah, 92)

Wakati Abdurrahman ibn Kaab, Abdullah ibn Mughaffal ﵁ na wengine waliotajwa katika aya hiyo, walipokuwa wakirejea kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ huku wakilia, Ibn Yamin aliwasogelea na kuwauliza sababu ya kilio chao.

"Tulienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kama hatua yetu ya mwisho ili aweze kutupatia kipandwa", walisema. "Lakini hakuweza kupata…na sisi hatuna kipandwa ili tuweze kuungana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika harakati yake."

Ibn Yamin ؓ aliwapa ngamia washirikiane wote wawili pamoja na baadhi ya tende kama chakula. Vivyo hivyo, Abbas ؓ aliwapa vipandwa wengine wawili na Othman ؓ akawapa watatu waliobaki.[312] Baadaye Mtukufu Mtume ﷺ aliweza kupata vipandwa kwa ajili ya Maswahaba wengine masikini.[313] Maswahaba hawa ambao, licha ya kuwa wanaruhusiwa kutoshiriki Vita walishindwa kuvumilia kuwa mbali na Mtukufu Mtume ﷺ hata kwa muda mfupi na ambao nyoyo zao zilikuwa zimejaa upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu, walijaaliwa heshima ya kushiriki katika safari ya Tabuk, kwa sababu ya hamasa na raghba yao ya hali ya juu ya kutaka kushiriki.

Huu ni mfano mmoja tu katika mifano kadhaa inayoonesha jinsi Maswahaba walivyojitolea kimwili na kiroho katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuonesha ubora na ukuu wa roho zao.

Tukio jingine lenye kusisimua kutoka katika safari ya Tabuk linasimuliwa na Wasilah ibn Aqsa ؓ:

"Siku kadhaa kabla ya safari ya kwenda Tabuk, nilitangaza katika mji wa Madina, nikitafuta mtu atakayeweza kunibeba juu ya kipandwa chake kwa malipo ya fungu langu la ngawira. Mzee mmoja wa Kiansari akaniambia kuwa ataweza kunibeba kwa kufanya zamu ya kupanda ngamia wake. 'Nimekubali' nilisema haraka

312. Ibn Hisham, IV, 172; Waqidi, III, 994.
313. Bukhari, Maghazi, 78.

haraka, naye akajibu kwa kusema, 'Basi tutaenda kwa Baraka za Mwenyezi Mungu!'

Niliondoka Madina nikiwa na rafiki mzuri katika safari. Mwishoni, Mwenyezi Mungu alinijaalia kupata fungu la ngawira za ngamia. Nilizipeleka kwa rafiki yangu huyo wa Kiansari na kumwambia.

'Chukua ngamia wako na uondoke!' alisema.

'Lakini ngamia hawa ni wako kwa mujibu wa makubaliano yetu ya mwanzo', nilimsisitizia.

Lakini akaniambia: 'Ndugu yangu, chukua ngawira zako, kwa sababu mwanzo sikutaka fungu lako la mali za kimaada. Nilitaka nipate sehemu ya thawabu zako utakazopata Akhera.'" (Abu Dawud, Jihad, 113/2676)

Msisimko wa kuyabadilisha maisha na mali kuwa rasilimali ya Akhera na hivyo kuinunua Pepo ulishuhudiwa kwa kiwango cha juu sana wakati wa maandalizi ya safari hiyo ya kivita, na kutoa mazingira yanayoweka viwango vya juu kwa ummah utakaokuja mpaka siku ya mwisho. Katika kushindana kumhudumia Mtukufu Mtume ﷺ, Maswahaba walikuwa kama vipepeo wanaozunguka juu ya moto, na kila kazi waliyoifanya walikuwa wakirudia rudia kusema 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wazazi wangu wawe fidia kwa ajili yako'. Hii inaonesha kuwa uhai wa wazazi wao haukuwa lolote mbele ya upendo wao kwa Mtukufu Mtume ﷺ.

Msisimko huu ulitunzwa na Maswahaba kwa ajili ya vizazi vijavyo. Katika kuitanguliza *taqwa* mbele ya ruhusa ya kutoshirikia vitani waliyopewa wale waliotajwa katika aya iliyotajwa hapo juu, Swahaba kipofu Ibn Umm Maqtum alishiriki katika Vita vya Qadisiyyah, akiwa kama mbeba bendera wa jeshi la Kiislamu, licha ya upofu wake.

Maonyo yaliyotolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu yalikuwa na athari katika kuandaa jeshi kubwa la Kiislamu leny askari zaidi ya elfu thelathini ndani ya muda mfupi.[314] Mwanzo, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amempa Umarah ibn Hazm ؓ bendera ya Najjar; lakini alipomuona Zayd ibn Thabit ؓ, akaamua kuichukua bendera hiyo na kumpa Zayd.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, umenighadhibikia?" akauliza Umarah ؓ.

"Hapana. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, sijakughadhibikia hata kidogo!" alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. "Bali unatakiwa kuitanguliza Qur'an pia. Ameiweka Qur'an akilini mwake zaidi yako. Yule ambaye amehifadhi Qur'an zaidi daima anatakiwa kutangulizwa, hata kama atakuwa mtumwa mweusi mwenye pua fupi!"

Kisha Mtume wa Mwenyezi ﷺ aliwashauri Aws na Khazraj kuwapa bendera zao watu ambao wamehifadhi Qur'an kushinda wengine. Hivyo, Abu Zayd ؓ akapewa bendera ya Awf, huku Muadh ؓ akipewa bendera ya Banu Salimah. (Waqidi, III, 1003)

Kushindana Katika Kujitolea

Kabla ya kuanza safari hiyo ya kivita, Mtukufu Mtume ﷺ aliwakusanya ili kujitolea kwa ajili ya kugharamia mahitaji mengi ya jeshi. Wakati huo, Madina ilikuwa katika maumivu ya ukame na njaa kali. Hata hivyo, Maswahaba waliweka pembeni mawazo na sababu binafsi na kuzitanguliza juhudi za *iman*. Wakapanda katika safina ya mashindano ya uungwana na *ithaar*. Abu Bakr ؓ alileta mali zake zote. Pindi Mtukufu Mtume ﷺ aliposema: "Sijafaidika na mali ya mtu kama nilivyofaidika na mali za Abu Bakr", Abu Bakr ؓ akabubujikwa na machozi, akasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi

314. Waqidi, III, 1002; Ibn Saad, II, 166.

Mungu, je mimi na mali zangu hatupo kwa ajili yako pekee?" (Ibn Majah, Muqaddimah, 11). Huu ulikuwa uthibitisho kwamba alikuwa ameyatoa maisha yake yote kama sadaka kwa Mtukufu Mtume ﷺ na amezama ndani yake.

"Ewe Abu Bakr, umeacha nini kwa ajili ya mke na watoto wako?" aliuliza Mtukufu Mtume ﷺ ambapo Swahaba huyo, kwa mara nyingine, alijibu kwa imani thabiti: "Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!" (Tirmidhi, Manaqib, 16/3675)

Omar ؓ alileta nusu ya mali yake, akidhani kuwa mara hii ataweza kumshinda Abu Bakr ؓ katika kujitolea. Lakini kwa mara nyingine akazidiwa.

Othman ؓ aliandaa ngamia mia tatu, wakiwa na kila kitu, na kuwatoa sadaka kwa ajili ya jeshi, pia akatoa dinari elfu moja. Mtukufu Mtume ﷺ akatamka maneno yafuatayo kumhusu: "Kila atakachofanya Othman hakitakuwa na madhara kwake!" (Tirmidhi, Manaqib, 18/3700; Ahmad, V, 63)

Vile vile, Othman ؓ na familia yake walitoa vito vyote vya thamani walivyokuwa navyo katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vivyo hivyo, Maswahaba wote wa kike walileta vito vya thamani na mapambo walivyokuwa navyo na kuviweka mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ.[315] Binti mmoja wa miaka kumi na moja alishindwa kuvua hereni zake, akazivuta kutokana na hamasa kubwa aliyokuwa nayo na kuziweka hereni hizo mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ zikiwa na damu.

Hata maswahaba masikini, ambao hawakuwa na chochote cha kutoa, walikuwa na hamasa na msisimko mkubwa wa kutoa chochote. Miongoni mwao ni Abu Aqil ؓ, ambaye alifanya kazi usiku mzima na kupata vibaba viwili vya tende. Kibaba kimoja ali-

315. Waqidi, III, 992.

kipeleka nyumbani na kingine akakitoa kama mchango wake kwa jeshi la Kiislamu. Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Mwenyezi Mungu akistawishe kile ulicholeta na kile ulichokibakisha", kisha akaamuru tende hizo zijumuishwe kwenye sadaka nyingine. (Tabari, Tafsir, X, 251)

Wanafiki, kwa upande mwingine, walianza kukidhihaki kile walichodhani kuwa ni sadaka na michango midogo, wakimtuhumu Abu Aqil kwa kutokuwa na ikhlasi. Uqbah ibn Amir رضي الله عنه anasema:

"Aya ya kutoa sadaka[316] ilipoteremshwa, tulianza kubeba kuni migongoni mwetu na kutoa sadaka kile tulichokipata. Kisha alikuja mtu mmoja ambaye alitoa kiwango kikubwa, wanafiki wakasema, 'Anajionesha'. Alikuja mwingine na kutoa kipimo cha tende, wanafiki wakasema tena, 'Mwenyezi Mungu hana haja ya kipimo chake kimoja cha tende.' Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ifuatayo:

الَّذِينَ يَلْمِزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فِي الصَّدَقَاتِ وَالَّذِينَ لاَ يَجِدُونَ إِلاَّ جُهْدَهُمْ فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ سَخِرَ اللَّهُ مِنْهُمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

'Wale wanao wabeuwa Waumini wanao toa sadaka nyingi na wasio nacho cha kutoa ila kadri ya juhudi yao, basi huwakejeli. Mwenyezi Mungu atawakejeli wao! Nao watapata adhabu chungu!' (at-Tawbah, 79)" (Bukhari, Zakat, 10; Muslim, Zakat, 72)

---

316. Aya ya 103 ya Surah at-Tawbah, ambayo sehemu kubwa iliteremka kuhusu Vita vya tabuk:

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ إِنَّ صَلاَتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

"Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua."

Katika Riwaya hiyo, mtu aliyetoa kiwango kikubwa alikuwa Abdur-Rahman ibn Awf ﷺ, na aliyeleta kipimo kimoja cha tende ni Abu Aqil ﷺ.

Swahaba mwingine katika orodha ya Maswahaba waliokuwa masikini ni Ulbah ibn Zayd ﷺ. Usiku wa manane aliamka na kuswali kisha akaomba akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu…umeamrisha na kuhamasisha *jihad*. Lakini hukunijaalia kuwa na mnyama mmoja ambaye ninaweza kumtumia kutoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hata Mtume Wako hujamjaalia mnyama ambaye ninaweza kumtumia! Daima nimekuwa nikitoa sadaka inayoniwajibikia kutoa, kutokana na mali na nafsi yangu. Ewe Mwenyezi Mungu… na sasa nina sahani moja tu ambayo umenijaalia, na hiyo ndiyo nitakayoitoa!"

Ilipofika asubuhi alienda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kusema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sina cha kutoa kama sadaka isipokuwa hii sahani moja! Kuanzia leo sina kinyongo na wale wanaoweza kunisema vibaya au kunidhihaki kwa sadaka hii!"

Mtukufu Mtume ﷺ katika kujibu maneno haya yaliyojazwa upendo na huruma, alisema: "Mwenyezi Mungu aikubali sadaka yako!" hakusema zaidi ya hayo. Siku iliyofuata alimwambia Ulbah, "Nilichukua sadaka yako na nina habari njema kwako! Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake, umeandikwa katika kitabu cha wale waliokubaliwa sadaka zao!" (Ibn Hajar, al-Isabah, II, 500; Ibn Kathir, as-Sirah, IV, 9; Waqidi, III, 994)

Baadhi ya wanafiki walikuwa wakiendelea kufanya jitihada za kuwashawishi Waislamu wenye imani dhaifu wasishiriki katika Vita hivyo. Walikuwa wamefanya kambi na makao katika nyumba ya Yahudi mmoja aitwaye Suhaylim. Mtukufu Mtume ﷺ alivyopata taarifa, alimtuma Talha ﷺ na baadhi ya Maswahaba na kuwaagiza waichome moto nyumba hiyo. Na kwa hiyo, wanafiki wakalazimika

kutawanyika, ujasiri wao wa kujiingiza katika shari kama hiyo tena ukatoweka.[317]

Kwa upande mwingine, Waislamu ambao nyoyo zao zilikuwa zimezungukwa na na hofu ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kutokana na Maonyo yake dhidi ya ulegevu wao waliouonesha mwanzo, sasa walishiriki katika Safari hiyo wote, kiasi cha mji wa Madina kuonekana kama umehamwa kwa kuondoka kwao. Bado kulikuwa na uwezekano kuwa Safari hiyo ingechukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa na mgogoro wowote ambao ungeibuka katika mji huo ungesababisha Dola kupata shida sana kujijenga upya. Vivyo hivyo, hasara kubwa ambayo ingetokea katika medani ya vita ingeudhoofisha Uislamu ndani ya muda mfupi. Pamoja na athari nyingine mbaya ambazo zingewakumba Waislamu, kufa kwa watu wenye elimu na maarifa, ambao wanahitajika kutengeneza nguvu kazi ya Waislamu, ingesababisha Dola kuanguka. Ili kulizuia tokea mwanzo kabisa, Mwenyezi Mungu Mtukufu alitangaza kiwango maalumu cha ushiriki katika vita:

وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُواْ كَآفَّةً فَلَوْلاَ نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ
لِّيَتَفَقَّهُواْ فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُواْ قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُواْ إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ

"Wala haiwafalii Waumini kutoka wote. Lakini kwa nini hawatoki baadhi katika kila kundi miongoni mwao, wakajifunze vyema Dini, na kisha waje kuwaonya wenzao watakapo warejea, ili wapate kujihadharisha?" (at-Tawbah, 122)

Katika kutekeleza amri hii, Mtukufu Mtume ﷺ alimuacha Ali na Maslamah رضي الله عنه mjini Madina, ili kuhakikisha usalama katika kipindi chote hicho.

317. Ibn Hisham, IV, 171.

***as-Saat'ul-Usrah*: Nyakati za Shida Ngumu**

Hatimaye, licha ya hali ngumu na shida mbalimbali, jeshi la Kiislamu liliwea kuanza safari, katika hali ya taadhima kubwa. Lakini, bado Waislamu walitakiwa waendelee kuvumilia shida zinazotokea na kudumisha subira na stahmala. Bado ugumu wa hali haukuwa umepungua. Miongoni mwa hali hizo ngumu ni pamoja na:

1) Ukame wa hali ya juu.

2) Umbali wa masafa wanayotakiwa kusafiri, njia ndefu inayopita katika jangwa ambalo sio rafiki kwa kutembea.

3) Msimu wa mavuno uliosadifiana na Safari hiyo ya kivita; matunda yakisubiri kuchumwa.

4) Joto kali.

5) Makabiliano ya muda mrefu dhidi ya nguvu za Warumi kutokana na idadi yao ambayo ingejitokeza siku hiyo.

Kutokana na shida mbalimbali zilizohusika, Vita hivyo vikaitwa *Ghazwat'ul-Usrah*, yaani Vita vya Shida, na nyakati za Vita hivyo zikaitwa kama *Saat'ul-Usrah*, yaani Nyakati za Shida.

Muda mfupi baada ya jeshi la Kiislamu kuondoka, Ali ﵁ alikuja akikimbia na kuwadiriki kwa lengo la kumuomba ruhusu ya kujiunga na safari hiyo. Akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wanafiki wanaeneza uvumi kwamba uliniacha kwa sababu hunipendi! Tafadhali niruhusu niungane nawe!"

"Ewe Ali! Wanasema uongo!" alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. 'Nimekupa jukumu la kuwa kaimu wangu kwa watu niliowaacha. Rudi haraka, uwe jicho na sikio kwa ajili ya familia yako na yangu; uwe naibu wangu kwao! Je huridhiki kuwa kama Harun kwa Musa (pindi alipoenda katika Mlima Sina)? Ispokuwa,

hakuna nabii baada yangu!" (Ibn Hisham, IV, 174; Bukhari, Maghazi, 78; Muslim, Fadail'us-Sahabah, 31) Baada ya kupokea sifa hizi maridhawa, Ali ؓ alirejea akiwa ameridhika na kuanza tena jukumu lake kama kaimu wake.

Jeshi lilikuwa limesafiri umbali mkubwa. Baada ya muda Abu Dharr ؓ alilidiriki jeshi. Ngamia wake dhaifu alishindwa kuvumilia shida za safari, sababu iliyomfanya abaki nyuma ya jeshi. Mwishowe alilazimika kumuacha mnyama wake, na licha ya tabu kubwa, alitembea kwa miguu na kuweza kulidiriki jeshi. Mtukufu Mtume ﷺ alipomuona, alitabasamu na kusema: "Mwenyezi Mungu amrehemu Abu Dharr! Anaishi peke yake, atakufa peke yake na atafufuliwa akiwa peke yake!"

Maneno haya ya ajabu ya Mtukufu Mtume ﷺ yalithibitika katika uhai wa Abu Dharr ؓ, kwani aliishi na kuvuta pumzi yake ya mwisho akiwa peke yake. (Waqidi, III, 1000)

Safari ilikuwa ngumu na nzito sana. Joto lilikuwa likiongezeka. Ugumu na shida nyingine ilikuwa katika ukweli kwamba Maswahaba watatu walilazimika kufanya zamu ya kumpanda ngamia mmoja. Watu wawili walikuwa wakigawa tende mara mbili ili kushirikiana. Kupata maji lilikuwa jambo gumu sana. Wakati wa kuchukua wudhu, mtu alilazimika kuosha kiungo mara moja tu. Walio safarini waliagizwa kufanya *mas'h* kwa viganjwa vyao kwa muda wa siku tatu, tofauti na wasiowajibikiwa na hukmu ya msafiri (*muqim*).[318] Wakati fulani, Mtukufu Mtume ﷺ aliomba dua na mvua ikanyesha pale tu jeshi la Kiislamu lilipoweka kambi.[319]

Wakati Jeshi likipita katika mji wa kale wa Hijr, mahali ambapo watu wa Thamud walikumbwa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu

318. Ibn Majah, Taharat, 45; Ahmad, VI, 27.
319. Ibn Hisham, IV, 177.

Mtukufu na kuangamizwa, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba: "Hili ni bonde ambalo mtu anatakiwa kulikimbia!" (Waqidi, III, 1008) Kisha akaongeza kwa kusema: "Ingieni katika ardhi ya wale waliozidhulumu nafsi zao mkilia, ili msikumbwe na balaa lililowakumba!" Akakifunika kichwa chake na kupita haraka katika eneo hilo. Aliagiza kumwagwa maji yote yaliyokuwa yamechukuliwa kutoka eneo hilo; licha ya kuwa makini kutopoteza kitu chochote, hata chakula kilichoandaliwa kwa maji hayo kilitupwa. (Bukhari, Anbiya, 17; Tafsir, 15/2; Muslim, Zuhd, 39)

Maeneo yaliyokumbwa na maangamizi na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yanaendelea kuwa na maangamizi milele. Ili kuepuka kukumbwa na athari mbaya za kimaanawi zinazotokana na maeneo hayo yaliyokumbwa na maangamizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, maeneo ambayo yalikuwa yamezama katika uasi na dhambi, ni bora kupita katika maeneo hayo kwa mwendo wa haraka, kama ilivyoelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ.

Usiku mmoja wakiwa katika kiunga cha Hijr, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Usiku wa leo kutakuwa na kimbunga kikali! Wafungeni ngamia wenu haraka, endeleeni kukaa mahali mlipo na msinyanyuke!" Kweli, upepo mkali ulivuma usiku huo. Mtu mmoja aliyekuwa amesimama kwenda kuchukua wudhu aliangushwa chini, huku mwingine ambaye alitoka kwa ajili ya kumtafuta ngamia wake akisukumwa mpaka jirani na Mlima Tay. (Bukhari, Zakat, 54; Muslim, Fadail, 11)

Wakiwa umbali wa siku kadhaa kutoka Tabuk, wanajeshi wa Kiislamu walikumbwa tena na kiu kali. Muadh ibn Jabal رضي الله عنه anasimulia kama ifuatavyo:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu alituambia, 'Allah akipenda, kesho mtafika kwenye chemchem ya Tabuk!' Siku moja baadaye, tuliwasili kwenye chemchem hiyo. Tulichota kidogo tuliyoyakuta

hapo kwa vitanga vya mikono yetu na kuyaweka katika kiriba cha ngozi. Mtukufu Mtume ﷺ akatumia maji hayo kuosha uso na mikono yake, kisha yaliyobaki akayanyunyizia ndani ya chemichemi hiyo. Kisha alirusha katika chemichemi hiyo vijiti vitatu, na kila kimoja kikiwa na ncha ya chuma. Hapo hapo chemichemi tatu za maji zikaanza kububujika. Wanajeshi wote walikunywa na kukata kiu yao. Kisha Mtukufu Mtume ﷺ akaniambia, 'Ewe Muadhi, iwapo utaishi muda mrefu, utaliona eneo hili likiwa limejaa mabustani na mizabibu!" (Muslim, Fadail, 10; Ahmad, V, 238)

Kutokana na kukumbwa na njaa kali wakati wa Safari hiyo, Maswahaba walimuomba Mtukufu Mtume ﷺ awape ruhusa ya kuwachinja ngamia wao, ili wabaki na shahamu zao. Wakapewa ruhusa. Omar ؓ akashauri: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ukiwapa ruhusa ya kuwachinja ngamia wao,basi kutakuwa na upungufu wa vipandwa. Badala yake unaweza kuwaambia walete vyakula walivyo navyo na kisha umuombe Mwenyezi Mungu avibariki. Bila shaka tunataraji kuwa Mwenyezi Mungu atavibariki."

"Vizuri sana, tutafanya hivyo", alisema Mtukufu Mtume ﷺ. Muda mfupi baadaye, aliagiza nguo iletwe iliyotengenezwa kwa ngozi na ilipoletwa akaitandika sakafuni. Kisha aliwaamuru askari kuleta vyakula walivyokuwa navyo. Baadhi walileta kiasi kidogo cha nafaka, wengine wakaleta kiwango cha tende kama hicho hicho huku wengine wakileta vipande vya mkate. Ni chakula kidogo sana kilichomwagwa kwenye nguo hiyo. Mtukufu Mtume ﷺ alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akipe Baraka kipate kuongezeka, na kisha akawaambia Maswahaba kuwa "leteni vyombo vyenu na mchukue chakula chenu!" Askari walileta makasha yao na kuyajaza. Hakuna kasha lililobaki bila kujaa. Kisha wakala wakaridhika mpaka chakula kingi kikabaki. Mtukufu Mtume ﷺ akasema, 'Ninashuhudia na kukiri kuwa hakuna Mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na Mimi ni Mjumbe Wake. Yule ambaye hatakuwa pamoja na

Mwenyezi Mungu kwa kuuamini Umoja Wake kwa imani thabiti na kuuamini utume wa Muhammad hataingia Peponi!" (Muslim, Iman, 45)

Jeshi la Kiislamu sasa lilikuwa limeweka kambi Tabuk; lakini hapakuwa na dalili yoyote ya kuwepo kwa maadui. Mara hii, hali ya kujiamini waliyokuwa nayo Wakristo wa Kiarabu iliondoka baada ya kuliona jeshi kubwa la Waislamu; na walipokumbuka ushujaa wa ajabu wa wapiganaji elfu tatu wa Kiislamu katika vita vya Mutah, waliamua kuachana na mapigano moja kwa moja. Aidha, muda mrefu Warumi walikuwa wameshabadilisha mpango wao wa kuivamia Arabia na Mfalme wao alikuwa ameshughulishwa mno na kazi ya kuzima mgogoro wa ndani uliokuwa umeibuka katika eneo la Humus. Muda mfupi baadaye mambo mengi yaliibuka. Ilibainika kuwa habari za Warumi kuivamia Arabia ni uvumi uliotengenezwa na Waghasani wa Kiarabu.

Waislamu na bila shaka Uislamu ulipata faida kubwa kwa kuelekea Tabuk. Mipaka ya kasikazini mwa Arabia ililindwa. Mfalme wa Ayla, watu wa Jarba na Azruh na Wayahudi wa Makna waliingia katika hifadhi ya Waislamu kwa kukubali kumlipa *jizyah* Mtukufu Mtume ﷺ. Khalid ibn Walid رضي الله عنه akiwa na askari wa farasi mia nne na ishirini alifanya shambulizi katika eneo la Dumat'ul-Jandal, akamchukua Mateka Mfalme wa Kikristo Uqaydir ibn Abdulmalik na kumleta kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Naye pia aliachwa huru kwa sharti la kulipa *jizyah*. (Ibn Hisham, IV, 180-182; Ibn Saad, I, 276-277; Ahmad, V, 425)

Jeshi la Kiislamu lilibaki tabuk kwa muda wa siku ishirini. Mtukufu Mtume ﷺ hakutaka kusonga mbele zaidi, kwa maana hakutaka kuupeleka Uislamu kwa watu kwa nguvu ya upanga. Aidha, Warumi walikuwa wamedhoofika sana na pia hapakuwa na adui aliyethubutu kukabiliana nao. Wakati huo huo, ugonjwa hatari

wa tauni ulikuwa umeikumba Syria, ambapo Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Unaposikia kuhusu ugonjwa wa tauni mahali fulani, usiende! Kama uko eneo hilo, usiondoke!" (Bukhari, Tibb, 30)

Baada ya kushauriana na Maswahaba, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliamua kuliongoza jeshi kurudi Madina.

Swahaba mwingine, Abu Haythamah ؓ, ambaye alishiriki katika jeshi lwa Waislamu katika safari ya Tabuk. Ugumu na tabu za safari hii zilimfanya mwanzo alazimike kubaki Madina. Siku moja, mkewe alimuita kwenye chakula kizuri alichokuwa amekiandaa chini ya mtambalio wa mimea katika bustani yake. Abu Haythamah alipokiona chakula hicho cha fakhari, aliingiwa na ubaridi. Alipovuta picha ya tabu ambazo Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba walikuwa wakizikabili wakati huo, alijisemeza: "Nawezaje kufanya hivyo hali ya kuwa wanakabiliana na matatizo haya katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Alijuta sana, akashindwa kuunyosha mkono kula chakula alichokuwa ameandaliwa, na hapo hapo akaondoka Madina na hatimaye akalidiriki jeshi la Kiislamu katika eneo la Tabuk. Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amefurahi kumuona, alisema: "Ewe Abu Haythamah! Ulikaribia kuangamia!" Kisha alimuombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu. (Ibn Hisham, IV, 174; Waqidi, III, 998)

Matukio hayo ni kama wosia hai kwetu, ambao ni nyenzo na kipimo cha kuona jinsi tunavyoweza kuviweka vipawa vyetu vya kiroho na kimwili katika kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuayatafakari majukumu yanayomuwajibikia mtu anapoingia katika Uislamu.

Asubuhi moja, Mtukufu Mtume ﷺ akiwa ameegemea kwenye mtende huko Tabuk, alisema:

"Mtu bora ni Yule ambaye husafiri juu ya farasi, ngamia au akitembea kwa miguu kwenda katika *jihad* kwa ajili ya Mwenyezi

Mungu mpaka akafikwa na mauti. Ni mtu mbaya kabisa ni muovu na safihi ambaye anasoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu lakini akawa hafaidiki nacho.

Tambueni kuwa maneno ya kweli kabisa ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na kamba imara kabisa ni *taqwa*. Dini bora kabisa ni ile ya Ibrahimu عليه السلام (Uislamu). Sheria bora ni Sunnah ya Muhammad. Maneno matukufu kabisa ni maneno ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu. Visa vizuri zaidi ni visa vya Qur'an.[320] Matendo bora ni yale yaliyofaradhishwa na Mwenyezi Mungu. Matendo mabaya kabisa ni yale ya uzushi. Njia bora ni njia ya Mtume. Kifo cha heshima kuliko vyote ni kifo cha kishahidi.

Upofu mbaya kabisa ni mtu kupotea kwenye njia ya haki baada ya kuipata. Kidogo kinachokutosha ni bora kuliko kingi kinachokushughulisha na kukuzuia kumuabudu Mwenyezi Mungu. Msamaha mbaya ni ule unaoombwa baada ya mauti kufika. Majuto mabaya kabisa ni mtu kujuta huko Akhera. Mtu mbaya kabisa ni yule anayefika mwisho Wakati wa Swala ya Ijumaa na kumzung-

---

320. Zaidi ya theluthi moja ya Qur'an inazungumzia visa. Katika kusisitiza umuhimu wake, Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa amri ya kutafakari ukweli unaoelezwa na visa hivyo, kuzingatia na kutathmini mafunzo hayo katika hali yoyote ile. Qur'an Tukufu inasema:

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ هَذَا الْقُرْآنَ وَإِن كُنتَ مِن قَبْلِهِ لَمِنَ الْغَافِلِينَ

"Sisi tunasimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qur›ani hii." (Yusuf, 3)

فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

"Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari." (al-Araf, 176)

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِن كُلِّ مَثَلٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ

"Na bila ya shaka tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qur›ani ili wapate kukumbuka." (az-Zumar, 27)

umza Mwenyezi Mungu kwa namna mbaya. Mtu mwenye makosa zaidi ni Yule ambaye ulimi wake hutawanya mambo ya urongo.

Utajiri bora ni utajiri wa moyo. Maandalizi bora ni mtu kujiandaa kwa *taqwa*. Kumuogopa Mwenyei Mungu ndiyo mwanzo wa hekma. Mashairi bila hekma hugeuka kuwa kazi ya *Iblis*. Ulevi ndiyo mama wa madhambi yote. Wanawake waovu ni mitego ya shetani. Ujana ni sehemu ya uwendawazimu. Mapato mabaya kabisa ni riba. Kitu kibaya kabisa kula ni mali ya yatima. Mtu mwenye furaha ni Yule anayejifunza kutokana na hali za wengine.

Kila mmoja wenu ataenda *arshin* nne (futi tisa) chini; na matendo yenu yatahesabiwa siku ya Qiyama. Kitu muhimu katika matendo ni yale matokeo yake. Fikra mbaya kabisa ni fikra za ulaghai. Kumuapia Muumini ni dhambi, kumuua ni ukafiri.Kumsengenya Muumini ni kuasi amri za Mwenyezi Mungu.

Mwenye kusema uongo baada ya kuahidi kusema ukweli hatakubaliwa. Mwenye kuomba msamaha, Mwenyezi Mungu atamsamehe. Atakayeishinda hasira yake, Mwenyezi Mungu atamlipa. Mwenye kustahmili kwa hasara anayoipata, Mwenyezi Mungu atamfidia. Mwenyezi Mungu atamlipa mara dufu Yule mwenye kustahmili mateso. Mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu atakabiliwa na adhabu kali.

Mola Wamgu! Nisamehe mimi na *ummah* wangu!

Mola wangu! Nisamehe mimi na *ummah* wangu!

Mola wangu! Nisamehe mimi na *ummah* wangu!

Ninamuomba maghfira Mwenyezi Mungu kwa niaba yenu na mimi pia!" (Waqidi, III, 1016-1017; Ahmad, III, 37; Ibn Kathir, al-Bidayah, V, 13-14)


MEDITERANIA
Quds
Bahari ya Chumvi
Muta
Azruh
Maan
Ayla
Sina
TABUK
Dumat'ul-Jandal
Ardhi ya Thamud
Mji wa Nabii Salih
Khaybar
BAHARI NYEKUNDU
Misri
MADINA
Hijaz

Shahidi Wa Tabuk

Swahaba mmoja tu ndiye aliyeuawa kishahidi katika safari ya Tabuk: Abdullah al-Muzani ؓ, ambaye alipata heshima ya kuwa Muislamu licha ya kuwa katika kabila la waabudu masanamu. Baba yake hakumuachia mali wakati anakufa, hivyo Abdullah alilelewa na ami yake mwenye utajiri, ambaye alimtunza na kumfanya kuwa mtu tajiri kama yeye. Licha ya kuwa na hamu na raghba kubwa ya kuwa Muislamu wakati Mtukfu Mtume ﷺ alipofanya Hijra ya kwenda Madina, Abdullah hakuweza kufanikisha azma yake hiyo kutokana na ami yake, aliyekuwa muumini wa ibada ya masanamu. Pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipojejea Madina baada ya ufunguzi wa Makka, Abdullah alimwambia ami yake: "Nimekusubiri muda wote huu uwe Muislamu. Lakini sikuoni kama una raghba yoyote kwa Muhammad. Lakini angalau niruhusu niwe Muislamu!"

Ami yake akajibu: "Ukianza kumfuata Muhammad kwa hali yoyote ile, nitachukua kila kitu nilichokupa, hata mavazi yaliyo juu ya mgongo wako!"

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa, nimeanza kumfuata Muhammad. Nimeshaacha kuabudu mawe na miti! Hivyo unaweza kuendelea kuchukua chochote unachotaka kutoka mikononi mwangu", alijibu.

Ami yake alichukua kila kitu mpaka mavazi yaliyokuwa mgongoni kwake, kama alivyotishia kufanya. Abdullah ؓ alirejea kwa mama yake, akiwa hana kitu. Mama yake alikata blanketi nene na kuligawa katika vipande viwili. Abdullah ؓ akatumia nusu kufunika sehemu ya juu ya mwili wake, na nusu nyingine upande wa chini. Alikuwa ameazimia; alitaka kwenda Madina mapema iwezekanavyo akaungane na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Vikwazo vilivyokuwa vimewekwa mbele yake sasa havikuwa kitu. Hakutaka kuendelea kusubiri zaidi. Alitoka usiku kwa siri, akiwatoroka watu

wa kabla lake waliokuwa wakimfuatilia kwa karibu na kumuweka chini ya uangalizi maalumu. Baada ya safari ndefu na ya kuchosha, hatimaye alifika katika eneo ambalo aliweza kuuona mji wa Madina. Mikono na miguu yake vilikuwa vimeloa damu. Alichoshwa na mwendo mrefu wa safari na alikuwa amepoteza nguvu zake kutokana na kiu na njaa. Lakini hamasa na msisimko wake bado uliendelea kumsukuma; alitaka kufuka kule anakokwenda. Ghafla alisimama na kuwaza kwamba asingeweza kutokea mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa na blanketi hafifu alilokuwa amelivirингisha mwilini mwake kama nguo. Lakini hakuwa na chaguo jingine, aliendelea kutembea, na kijana huyu, Swahaba mtarajiwa, aliweza kufika kwenye Msikiti wa Mtume ﷺ katikati ya macho ya wale waliokuwa wakimtazama mgeni aliyejifunga blanketi. Alilala huko mpaka asubuhi. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaswalisha Maswahaba swala ya alfajiri. Kisha, wakati akiwakagua wale waliohudhuria swala kabla ya kuelekea nyumbani kwake, alimuona Abdullah na kumtambua. Mtume wa Rehma ﷺ, kimbilio la wapweke na wanyonge, akamkumbatia Abdullah kwa upendo mkubwa. Alipogundua kuwa alikuwa akiitwa Abduluzza, Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

"Utaitwa Abdullah *Dhul-Bijadayn* (mwenye mapande mawili ya blanketi)! Endelea kuwa pamoja nami na nitembelee mara kwa mara!" Kisha Abdullah ﷺ aliungana na watu wa *suffa*, ambapo alianza kujifunza kusoma Qur'an. Muda mfupi baadaye, aliweza kusoma na kuhifadhi sura nyingi.

Swahaba huyu mkubwa, ambaye aliambatana na Mtukufu Mtume ﷺ kwa upendo, akawa anatembea pamoja naye katika vita mbalimbali, akiwa na hamu kubwa ya kufa kishahidi na kuyatoa maisha yake katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kabla ya kuanza safari ya kuelekea tabuk, alimsisitiza Mtukufu Mtume ﷺ amuombee dua awe miongoni mwa watakaokufa kishahidi. Mtuku-

fu Mtume ﷺ akaomba: "Mola wangu! Ifanye damu yake isidhuriwe na makafiri!"

Abdullah ؓ akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hilo sio nililolitaka." Mtume ﷺ akamjibu: "Unapokwenda kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu ukakumbwa na homa na kufariki, utakuwa umekufa kishahidi! Ukiangushwa na ngamia wako, ukavunja shingo yako, utakuwa umekufa kishahidi! Usiwe na wasiwasi! Lolote litakalotokea katika haya, itatosha kwako kuwa shahidi!"

Kwa maajabu kabisa, Abdullah ؓ alikufa kwa njia ileile iliyoelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Usiku mmoja, wakati jeshi likijiandaa kurejea, watu watatu walikuwa wameubeba mwili wa swahaba mmoja aliyekuwa amefarikia dunia huku wakiwa na taa yenye mwanga hafifu; watu hao ni Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba zake wawili wa karibu, Abu Bakr na Omar ؓ. Ulikuwa ni mwili wa Abdullah *Dhul-Bijadayn* ؓ.

Abdullah ibn Masud ؓ anasimulia kwa mshangao kile alichokishuhudia:

"Katika giza la usiku, niliona mwanga hafifu ukipita kwenye kona ya uwanja ambao wanajeshi walikuwa wamesimika mahema yao. Nilisimama na kufuatilia. Tahamaki, alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Abu Bakr na Omar ؓ wakiwa wameubeba mwili wa Abdullah *Dhul-Bijadayn* ؓ. Walifika sehemu, wakasimama na kuchimba kaburi. Kisha Mtume ﷺ akaingia kaburini, huku Abu Bakr na Omar ؓ wakijiandaa kumkabidhi mwili huo.

'Msogezeni ndugu yenu karibu nami', alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Wakafanya hivyo. Mtume ﷺ aliuchukua mwili huo kwa mikono yake na kuuweka kaburini, na kisha akasimama na kuomba: 'Mola wangu! Nilikuwa radhi naye; daima nilimridhia…Ninakuomba nawe uwe radhi naye!'

Nilivutiwa sana na kile nilichokiona. Nilimhusudu *Dhul-Bijadayn*. Niliwaza na kusema: 'Lau ingekuwa ni mimi niliyewekwa kaburini na kuombewa na Mtume!'" (Ibn Hisham, IV, 183; Waqidi, III, 1013-1014; Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, III, 227)

Khiyana ya Wanafiki na Masjid'ud-Dirar

Kundi moja la wanafiki lilipanga njama ya kumuua Mtukufu Mtume ﷺ wakati jeshi likipita usiku kwenye njia nyembamba, wakati akirejea kutoka Tabuk. Mtukufu Mtume ﷺ alitaarifiwa juu ya mpango huu wa shari, akamtuma Hudhayfatul-Yaman na wanafiki wakakimbia baada ya kumsikia Swahaba huyo akiwapigia kelele. (Ahmad, V, 453)

Kulikuwa na mtego mwingine uliotegwa na wanafiki dhidi ya Mtukufu Mtume ﷺ. Abu Amir Fasiq, Mkristo kutoka kabila la Khazraj, ambaye aliondoka Madina baada ya kuwasili kwa Uislamu na kuungana na Warumi, alikuwa akiwahamasisha wanafiki kuchukua hatua.Katika kilele cha uchemkaji wa jungu hili la shari, walijenga msikiti katika eneo la jirani kidogo na Masjid Quba. Msikiti huo uliojengwa ndiyo msikiti unaojulikana kama Masjid Dhirar (Msikiri wa Madhara).

Ili kutekeleza mpango mwingine wa mauaji, walimualika Mtukufu Mtume ﷺ kwenye msikiti wao kabla hajaanza safari ya kwenda Tabuk. "Nitakaporejea, *inshaallah*", alijibu Mtukufu Mtume ﷺ. Sasa walikuwa wakisubiri kurejea kwa jeshi la Kiislamu.

Waislamu walikuwa umbali mdogo kutoka mji wa Madina, Jibril عليه السلام akaja kumtaarifu Mtukufu Mtume ﷺ juu ya kitovu hiki cha uovu na kumtaka asiingie katika msikiti huo. Hivyo, mtego uliowekwa na wanafiki katika mfumo wa msikiti hasimu ili kumtega Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ na Waislamu, ulibatilika kabla

haujatekelezwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliifichua njama yao kwa namna maalumu:

وَالَّذِينَ اتَّخَذُواْ مَسْجِدًا ضِرَارًا وَكُفْرًا وَتَفْرِيقًا بَيْنَ الْمُؤْمِنِينَ وَإِرْصَادًا لِّمَنْ حَارَبَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ مِن قَبْلُ وَلَيَحْلِفَنَّ إِنْ أَرَدْنَا إِلاَّ الْحُسْنَى وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ لاَ تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا لَّمَسْجِدٌ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَن تَقُومَ فِيهِ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُواْ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَّهِّرِينَ

"Na wapo walio jenga msikiti kwa ajili ya madhara na ukafiri na kuwafarikisha Waumini, na pa kuvizia kwa walio mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake hapo kabla. Na bila ya shaka wataapa kwamba: Hatukukusudia ila wema tu. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa wao ni waongo. Usisimame kwenye msikiti huo kabisa. Msikiti ulio jengwa juu ya msingi wa uchamngu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo wamo watu wanao penda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wanao jitakasa." (at-Tawbah, 107-108)

Mara hii, kadhia hii ilikuwa ni zaidi ya kadhia ya undumilakuwili wa wanafiki; walikuwa wamepanga njama kabambe dhidi ya Mtume ﷺ na Waislamu. Hivyo walitakiwa kufichuliwa na masikiti wao kubomolewa.

Mtukufu Mtume ﷺ aliporejea Madina alifanyia kazi amri hiyo ya Mwenyezi Mungu na kuagiza Masjid Dhirar ichomwe moto. (Ibn Hisham, IV, 185)

Tumetoka kwenye *Jihad* Ndogo kwenda Kwenye *Jihad* Kubwa

Tabuk, ni safari ya mwisho ya kijeshi iliyoongozwa na Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe. Ni safari iliyojaa tabu na shida. Jeshi la Kiislamu lilitembea kilometa elfu moja kufika Tabuk na kutembea umbali huo huo wakati wa kurudi. Vumbi lilienea katika nywele na ndevu zao. Kwa hakika tabu na shida za safari hiyo ziliwakondesha. Pamoja na shida hizo zote, bado Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia: "Tumetoka kwenye *jihad* ndogo kwenda kwenye *jihad* kubwa!"

Maswahaba walishtuka: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, angalia namna tulivyo. Kuna *jihad* kubwa zaidi ya hii?" waliuliza kwa mshangao.

Mtukufu Mtume ﷺ akarudia maneno yake: "Tumetoka kwenye*jihad* ndogo, na sasa tunaelekea kwenye *jihad* kubwa, *jihad* ya nafsi." (Suyuti, II, 73)

Jihad dhidi ya nafsi ni kuufunda moyo kiroho na kimaanawi, kuendeleza lengo la kujitakasa kiroho kwa kuunyanyua mwenendo wa kimaadili na kumbadilisha mtu kuwa mwanadamu kamili (insan-i kamil). Njia ya kuelekea huko inapatikana ndani ya tafakuri iliyozama katika ukweli, moyo uliopambwa kwa imani na maadili mazuri, hali ya jumla iliyopambwa kwa hali ya kiroho ya Qur'an na Sunnah, na ukamilifu unaopatikana kwa kukwea kilele cha *tawhid* na kuwa na mwenendo ulionyooka.

Waislamu wote mjini Madina, watoto kwa wakubwa, walimiminika *Saniyyat'ul-Wada* kwenda kumlaki Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba wakati wakirudi kutoka katika safari yao hiyo ya ushindi.[321]

321. Bukhari, Jihad, 196.

Watatu Waliotubu

Kulikuwa na makundi matatu ya wanaume ambao hawakushiriki katika Vita ya Tabuk. Makundi hayo ni:

1) Wale wenye sababu halali na za kisheria, kama ilivyotangwa na aya ya Qur'an, hawakuweza kushiriki kwa sababu ya kukosa nyenzo, licha ya kuwa na shauku na hamu ya kutaka kushiriki. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba kuhusu watu hawa: "Kuna watu mjini Madina ambao hakuna bonde hata moja tulilopita bila kuwa pamoja nao! Dharura (halali) ziliwafanya wabaki." (Bukhari, Maghazi, 81; Muslim, Imarah, 159)

Katika hadith nyingine, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: "Matendo ya mtu hutokana na nia…" (Bukhari, Bad'ul-Wahy, 1)

2) Wanafiki: Pamoja na sababu nyingine nyingi, sababu yao kubwa ya kutoshiriki ni kuamini kwao kuwa, kwa vyovyote vile, Mtukufu Mtume ﷺ hataweza kurudi kutoka Tabuk. Lakini walipomuona Mtume ﷺ amerudi salama, akiwa amepata mafanikio mengi wakati wa safari hii ya kivita, moja kwa moja walimkimbilia, na baada ya kutengeneza dharura za urongo, wakaomba msamaha. Wanafiki hawa, wapatao themanini, walizungumziwa na Qur'an Tukufu:

وَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنَّهُمْ لَمِنكُمْ وَمَا هُم مِّنكُمْ وَلَكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرَقُونَ لَوْ
يَجِدُونَ مَلْجَأً أَوْ مَغَارَاتٍ أَوْ مُدَّخَلاً لَّوَلَّوْاْ إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُونَ

"Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi, wala wao si katika nyinyi. Lakini ni watu wanao ogopa. Lau kama wangelipata pa kukimbilia au mapango au pahala pa kuingia basi wangeli fyatuka mbio kuelekea huko." (at-Tawbah, 56-57)

يَعْتَذِرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ قُل لاَّ تَعْتَذِرُواْ لَن نُّؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَّأَنَا اللَّهُ مِنْ أَخْبَارِكُمْ وَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ سَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا انقَلَبْتُمْ إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُواْ عَنْهُمْ فَأَعْرِضُواْ عَنْهُمْ إِنَّهُمْ رِجْسٌ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاء بِمَا كَانُواْ يَكْسِبُونَ

"WATAKUTOLEENI UDHURU mtapo warudia. Sema: Msitoe udhuru; hatukuaminini. Mwenyezi Mungu amekwisha tueleza khabari zenu. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wataviona vitendo vyenu. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa ya siri na ya dhaahiri; naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda. Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu mtakapo rudi kwao ili muwaachilie mbali. Basi waachilieni mbali. Hakika hao ni najsi, na makaazi yao ni Jahannamu, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyachuma." (at-Tawbah, 94-95)

kwa kuteremshwa aya hizi, wanafiki wakaondolewa katika jamii ya Waislamu. Kwa kuitwa 'wachafu', hawakuhesabiwa tena kuwa ni Waislamu. Vilevile walipigwa marufuku kushiriki katika vita vyovyote kwa jina la Uislamu.

1) Wale ambao hawakuwa na udhuru wowote wa kutoshiriki. Walikuwa katika makundi mawili:

a) Wale ambao hawakushiriki vitani, licha ya kutokuwa wanafiki wala kuwa na udhuru wowote halali. Lakini, kabla Mtume ﷺ hajarejea kutoka Vitani, walitambua makosa yao na kujutia sana. Waliziadhibu nafsi zao, wakajifunga kwenye nguzo za Msikiti na kuapa kubaki katika hali hiyo mpaka Mtume ﷺ alipokuja na kuwa-

fungua yeye mwenyewe. Mtukufu Mtume ﷺ aliporeja aliambiwa kuhusu watu hawa, naye akasema: "Ninaahidi kuwa sitawafungua mpaka nipokee amri kuwahusu." Ndipo aya ifuatayo ikateremshwa:

وَآخَرُونَ اعْتَرَفُواْ بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُواْ عَمَلاً صَالِحًا وَآخَرَ سَيِّئًا عَسَى اللَّهُ أَن يَتُوبَ عَلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Na wengine walikiri dhambi zao, wakachanganya vitendo vyema na vingine viovu. Asaa Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akaenda kuwafungua Maswahaba hao waliokuwa wamejifunga kwenye nguzo kwa kujutia makosa yao.

b) Wale ambao hawakushiriki Vitani licha ya kutokuwa wanafiki wala kuwa na udhuru halali unaowazuia kushiriki, lakini wakaendelea kujitenga na wenzao waliojifunga kwenye nguzo za msikiti. Walikuwa watatu: mshairi Kaab ibn Malik, Murarah ibn Rabi na Hilal ibn Umayya. Tofauti na wanafiki, watu hawa hawakuongopa badala yake walikiri mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ kuwa hawakuwa na udhuru wa kutoshiriki vitani. Kwa majuto makubwa waliyokuwa nayo kwa kutoshiriki, walimuomba Mtume ﷺ awasamehe.

Lakini, ili kuendelea kushikamana na amri ya Mwenyezi Mungu, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwasamehe mara moja. Aidha, wakati akisubiri Ufunuo utakaoelezea hatma yao, hakudiriki hata kuzungumza nao. Maswahaba ambao walishikamana na mwenendo wa Mtume ﷺ muda wote, nao pia walifanya hivyo hivyo.

Maswahaba hao watatu walishiriki katika vita zote zilizotangulia; isipokuwa Kaab ؓ, ambaye hakuwepo katika Vita vya Badr. Dunia ikawa finyu mbele ya macho yao, nyoyo zao zikabana kwa

kupuuzwa na jamii yote ya Kiislamu kwa sababu ya uamuzi wao wa kutoshiriki katika safari ya Tabuk. Baya zaidi ni ule ukweli kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amejitenga nao kiasi cha kutoitikia salamu zao. Ardhi yote wakaiona dhiki; hata wake zao wakawa kama wageni. Hakuna waliloweza kufanya zaidi ya kulia, usiku na mchana. Walikuwa kama mishumaa inayoyeyuka kutokana na vilio vyao vya kudumu. Walikuwa wamefanya kosa, lakini hilo halikuwaweka mbali na ikhlasi na unyoofu; wala halikuitikisa imani yao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na haikuwafanya wasijutie na kutubu. Hali iliendelea hivyo kwa muda wa siku hamsini, ndipo toba yao ya kweli ikakubaliwa na aya zifuatazo zikateremshwa:

وَعَلَى الثَّلاَثَةِ الَّذِينَ خُلِّفُواْ حَتَّى إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنفُسُهُمْ وَظَنُّواْ أَن لاَّ مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلاَّ إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُواْ إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ وَكُونُواْ مَعَ الصَّادِقِينَ

"Na pia wale watatu walio achwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake, na nafsi zao zikabanika, na wakayakinika kuwa hapana pa kumkimbia Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwake Yeye. Kisha akawaelekea kwa rehema yake ili nao waendelee kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli." (at-Tawbah, 118-119)

Mtukufu Mtume ﷺ alimpa habari njema Kaab ibn Malik kwa kumwambia: "Ninakupa habari njema ya siku ya furaha zaidi kwako tangu siku uliyozaliwa!"[322]

322. Wakati Kaab ؓ akielekea kwa Mtukufu Mtume ﷺ baada ya kupata habari njema, alikutana na Talha ibn Ubaydullah ؓ, ambaye alimkumbatia Kaab na kumpongeza; hali ambayo Kaab ؓ aliendelea kuikumbuka kwa kipindi chote cha maisha yake.

Katika kuonesha shukrani, Kaab ibn Malik ﷺ alisema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ninataka kuitoa mali yangu yote kama sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!"

"Itakuwa bora iwapo utatoa sehemu ndogo tu ya mali yako", alishauri Mtukufu Mtume ﷺ.

Kaab ﷺ akasema: "Hivyo basi nitabakisha fungu langu la Khaybar. Mwenyezi Mungu ameniokoa katika janga hili kwa sababu ya uaminifu wangu. Hivyo, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nitazungumza ukweli tu katika kipindi chote cha maisha yangu!"

Kaab ﷺ anasema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, zawadi kubwa kabisa niliyopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya kupata heshima ya kuwa Muislamu ni kunijaalia kusema ukweli mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na hivyo kuiokoa nafsi yangu kutokuwa miongoni mwa wale walioangamia. Kwa maana Mwenyezi Mungu alitoa maneno makali mno kuhusu wale waliojitengenezea dharura na kutoshiriki katika vita vya Tabuk, akasema:

فَأَعْرِضُواْ عَنْهُمْ إِنَّهُمْ رِجْسٌ

'…Basi waachilieni mbali. Hakika hao ni najsi!'" (at-Tawbah, 95) (Bukhari, Maghazi, 79, Wasaya, 16, Jihad, 103; Muslim, Tawbah, 53; Musafirin, 74)

Maswahaba hao watatu walizongwa na adhabu kwa kutoshiriki vita moja tu, licha ya kuwa wamewahi kuwa bega kwa began a Mtukufu Mtume ﷺ katika vita nyingine zote za awali. Tukio hili linatoa onyo na tahadhari kwa wale ambao, bila dharura ya halali, hawashiriki katika kuipigania tawhid katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Angalia somo kubwa na la ajabu linalopatikana katika kisa hiki! Mtu amebeba hadhi ya 'Swahaba' na kukabiliana na ana kwa ana na kifo katika vita mbalimbali, kwanza katika vita ya Badr, kisha anakumbana na karipio zito kwa kutoshiriki vita yenye sulubu lakini isiyokuwa na mapambano na umwagaji damu kama Tabuk! Sio tu kwamba kuna funzo la ajabu kwa wale wenye kutafakari, bali pia tukio hili limebeba indhari na matokeo yake. Tukizingatia kuwa kuupigania Uislamu ni jambo la lazima katika zama hizi, kama ambavyo imekuwa lazima siku zote, ni jambo la kusikitisha mno kuwaona watu wengi wakilipuuza, wakiwa wazito na hata kuliacha kabisa. Fikiria Swahaba aliyeshiriki vita vya Badr analazimika kulipa gharama kubwa na nzito kwa kupuuza. Yatupasa kuacha kupuuza na tutafakari juu ya athari za kupuuza zilizowakumba wenzetu; na hivyo tujitahidi kwa hali yoyote kusuhubiana na kuwa pamoja na watu wakweli, kama tunavyoamrishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ili Waislamu waweze kupata matokeo mazuri na kuepuka athari mbaya, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameawaamuru kuwa pamoja na wakweli; kusuhubiana nao, kutafuta ukaribu nao, kuwaunga mkono na kutokuwa mbali nao katika vipengele vyote vya maisha. Hilo linatakiwa kufanyika ili kuzuia hali ya 'ardhi kuwa nyembamba', kuutibu moyo wenye maumivu na hivyo kujiokoa kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuondosha vizuizi vyote vinavyomzuia mtu kupata radhi Zake. Utenzi ufuatao unaelezea, kwa uzuri kabisa, umuhimu wa kuwa na urafiki na watu wakweli na wema:

Mwiba huangamia unapokuwa peke yake,
Lakini humwagiliwa unapokuwa na maua waridi…

Ni jambo la maana sana kuwa amri hii iliteremshwa wakati wa Safari ya Tabuk, 'Vita Ngumu na Nzito.' Ni jambo la umuhimu

mkubwa kusuhubiana na watu wema, sio tu wakati wa furaha, bali pia pindi wanapokabiliwa na matatizo na shida, pindi wanapotoka kwenda kupigana *jihad* katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kustahmili shida na tabu zinazowakabili watu wema na kushiriki katika juhudi zao bila kubaki nyuma ni jambo la msingi kabisa.

Surah Tawbah, ambayo sehemu yake kubwa inahusu Vita vya Tabuk, imeweka msisitizo mkubwa juu ya umuhimu wa *jihad* ya kimwili na kiroho kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. *Jihad* ya kimwili na kiroho huwa ndio ushuhuda wa wazi wa kuwa Muislamu anaifuta na ni mtiifu kwa dini yake na wakati huo huo huonesha tofauti baina ya Muumini na mnafiki. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُم بِأَنَّ لَهُمُ الجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَاةِ وَالإِنجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُواْ بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُم بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa." (at-Tawbah, 111)

Aidha, katika zama zote, wanafiki wamekuwa ndio tishio kubwa wa Waislamu. Jambo hili limewekwa wazi na Surah Tawbah na matukio halisi katika Safari ya Tabuk.

Hazina za Mbingu na Ardhi ni za Mwenyezi Mungu

Licha ya majaribio na jitihada zote za makafiri, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliinua juu dini Yake na kuwajaaliwa Waislamu ushindi. Hiyo ilikuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyokuwa amempa Mtume ﷺ na wale waliomfuata kwa ikhlasi na moyo mmoja. Kwa hivyo, ahadi hiyo iliendelea kutimizwa licha ya chuki za maadui. Qur'an Tukufu inasema:

هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنفِقُوا عَلَى مَنْ عِندَ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّى يَنفَضُّوا وَلِلَّهِ خَزَائِنُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ

"Hao ndio wanao sema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanaafiki hawafahamu." (al-Munafiqun, 7)

Kwa hakika, karne nyingi za juhudi zisizokoma zinazofanywa na makafiri kuidhoofisha nguvu ya kiuchumi ya Uislamu zimekuwa zikizuiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye alizikabili kwa kuwajaalia Waislamu Baraka nyingi, kwa sababu ni zake hazina za mbingu na ardhi. Kwa kutumia majeshi Yake yanayoonekana na yasiyooneka, daima Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaaliwa Waislamu ushindi mwepesi kwa gharama ya makafiri wenyewe, ambao wamekuwa wakishindwa vibaya.

Historia ina mifano mingi ya Waislamu kupata ushindi mwingi wakiwa na idadi ndogo kwa msaada wa Mwenyezi Mungu Mtuku-

fu. Vita vya Badr, Muta, Andalus na Malazgirt ni mifano michache tu katika mifano mingi. Ni askari mia nne tu wa farasi ndio wali-oasisi Dola ya Othmaniya, ambayo iliacha athari kubwa ya *i'la-yi kalimatullah*, yaani kupigana ili kulinyanyua neno la Mwenyezi Mungu na kulifanya litawale dunia nzima.

Hiyo inaonesha kwamba mafanikio ya Waislamu yanafanan na yanategemea *ikhlas* yao, yaani kumsafia nia Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kupoteza *ikhlas* ni kupoteza nguvu; kushikamana na *ikhlas* huleta nguvu na taadhima.Iwapo Waislamu watakuwa na *ikhlas*, daima maadui wa Uislamu watashindwa kila watakapoja-ribu kuwadhuru Waislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea kuhusu ulinzi huu ndani ya Qur'an Tukufu:

وَإِن تَصْبِرُواْ وَتَتَّقُواْ لاَ يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ

"…Na nyinyi mkisubiri na mkajizuilia, hila zao hazitakud-huruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyazunguka yote wayatendayo." (Al-i Imran, 120)

Historia ya Kiislamu ni shahidi wa matokeo ya aya hii.

Hakuna Faida kuwa Muislamu bila Ibada

Mtukufu Mtume ﷺ aliporejea Madina baada ya kufanikisha malengo yaliyokusudiwa, Urwah ibn Masud, kiongozi wa Taif aliwasili haraka sana mjini Madina kwa lengo la kutangaza kuwa ameukubali Uislamu. Bila kupoteza muda, alirejea Taif na kuanza kuwalingania wenyeji wa mji huo kuingia katika Uislamu. Lakini watu hawa ambao miaka iliyopita waliwahi kumpiga mawe Mtume ﷺ bila kosa lolote zaidi ya kuwalingania kwenye ukweli, na sasa

radiamali yao kwa Urwah ilikuwa mbaya zaidi. Walimpiga mishale na kumuua.[323]

Mtukufu Mtume ﷺ alimuamuru Malik ؓ, chifu wa Hawazin ambaye baada ya kusilimu alimteua kuwa kiongozi, aidhibiti Taif. Mashambulizi ya mfululizo yaliyofanywa na Maliki yaliichakaza Thaqif, akawafanya wakwame ndani ya ngome zao. Wakiwa wameshikwa na wasiwasi mkubwa, waliamua kuwatuma watu wao maarufu kwenda Madina.[324]

Ili kuzivuta nyoyo zao kwenye Uislamu, Mtukufu Mtume ﷺ aliukaribisha ujumbe wa Thaqif ndani ya Msikiti.[325] Kwa namna hiyo, walipata kusikia Qur'an iliyokuwa ikisomwa na Maswahaba wakati wa usiku na wakati wa swala za *tahajjud*, na kuwaona Waislamu wakijipanga, bega kwa bega, wakati wa swala tano za kila siku.[326]

Hatimaye, ujumbe wa Thaqif ulisema kuwa ulikuwa tayari kusilimu kwa sharti kwamba waruhusiwe kutoswali.

"Hakuna faida katika dini bila rukuu (swala)", hilo ndilo lililokuwa jawabu la Mtukufu Mtume ﷺ. (Abu Dawud, Kharaj, 25-26/3026)

Thaqif hawakuishia hapo. Walifanya upumbavu mwingine. Walitaka Mtume ﷺ aruhusu sanamu laola Lat linaloheshimika sana, liendelee kubaki mahali pake kwa miaka 3 mingine. Ombi lao lilipokataliwa, wakaomba sanamu hilo libaki kwa mwezi mmoja zaidi. Hilo nalo lilikataliwa. Baada ya kuona hawana jinsi, wakasilimu. Kisha waliomba angalau wasihusike katika kuliangusha sanamu la Lat. Mtukufu Mtume ﷺ hakuwakatalia, na badala yake alimtuma Abu Sufyan pamoja na Mughirah ؓ kwenda kufanya kazi

323. Ibn Hisham, IV, 194; Hâkim, III, 713/6579.
324. Ibn Hisham, IV, 138, 195.
325. Ahmad, IV, 218.
326. Waqidi, III, 965.

hiyo.[327] Jambo la kushangaza zaidi, sanamu hilo lilipoanguka chini, wanawake wa Thaqif walimiminika katika mitaa ya Taif na kuanza kuomboleza. Lakini haukupita muda mrefu wakasahau kabisa hata jina la masanamu yao ya zamani na kuwa Waislamu wa kweli, wakiutambua ubora wa Uislamu.

Sasa dua iliyojaa huruma ambayo Mtukufu Mtume ﷺ aliwaombea watu wa Taif mwaka wa tisa wa kipindi cha Makka ili wapate kuongoka, licha ya mabaya waliyomfanyia, ilikuwa imejibiwa.

Wajumbe hao wa Thaqif walifundishwa mambo ya wajibu katika Uislamu na kanuni ambazo walihitaji kuzijua kwa ajili ya matendo ya ibada za kila siku. Vile vile, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia kufunga siku zilizobaki za mwezi wa Ramadhani walizozidiriki wakati huo. Kwa kipindi chote walichokaa Madina, Bilal Habashi ؓ alikuwa akiwapelekea *sahur* (daku) na futari.[328]

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akikutana na wajumbe mbalimbali waliokuja kumuona pindi anapokuwepo, mchana au usiku, na kuwapa ushauri wa kina kuhusu mambo yao.[329] Vivyo hivyo, ilikuwa ni kawaida yake kukutana na wajumbe wa Thaqif baada ya swala ya isha. Siku moja, walisimama wakizungumza kwa muda mrefu kupita kawaida mpaka Mtukufu Mtume ﷺ akahisi dharura ya kuweka uzito wa mwili wake kwenye mguu mmoja ili kuupumzisha mwingine.[330]

---

327. Ibn Hisham, IV, 197; Waqidi, III, 967-968.
328. Waqidi, III, 968.
329. Omar ؓ anasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na Abu Bakr walikuwa wakijadili jambo husika kuhusu Waislamu mpaka usiku mwingi; nami nilikuwa nikikaa pamoja nao." (Tirmidhî, Salât, 12/169)
330. Abu Dawud, Shahr-u Ramadan, 9/1393.

Aws ibn Hudhayfah ﵁, mmoja wa wajumbe hao wa Thaqif anasimulia:

"Siku moja, baada ya swala ya isha, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichelewa, tofauti na ilivyokuwa kawaida yake. 'Kitu gani kilichokuchelewesha ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?' tulimuuliza alipotokea.

'Nimejiwekea utaratibu wa lazima kusoma *hizb* moja ya Qur'an kwa siku.Sikutaka kuja kabla sijaimaliza', alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Asubuhi tuliwauliza Maswahaba jinsi walivyosoma Qur'an kwa *hizb*. Wakasema, 'Tunazifanya sura tatu za kwanza kuwa *hizb* ya kwanza, kisha sura tano zinazofuatia kama *hizb* ya pili, kisha kwa utaratibu, tunachanganya sura saba zinazofuta, kisha tisa, kisha kumi na moja na kisha sura kumi tatu zinazofuatia na kuzifanyia *hizb*. Na kisha tunaanza kusoma surah Qaf na kufanya *hizb* ya mwisho mpaka mwisho. Hivyo tunaisoma Qur'an katika *hizb* saba. (Ahmad, IV, 9; Ibn Majah, Salat, 178)

Kutokana na kuamrishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na amana waliyoachiwa na Mtume ﷺ, Maswahaba waliipa Qur'an Tukufu umuhimu mkubwa. Sio tu kwamba walikuwa wakiisoma kwa urefu wakati wa swala, bali pia walihakikisha wanaisoma sana wanapokuwa safarini, vitani na nyakati za usiku. Kamwe kiu yao ya kuisoma Qur'an ilikuwa haikatiki; hakuna siku ambayo ingepita bila kuisoma Qur'an Tukufu.[331] Walikuwa wakianza siku kwa kusoma Qur'an na kumshauri kila mwenye maradhi ya macho kuzikodolea macho kurasa za Qur'an Tukufu. Inasemekana kuwa

331. Ibn Saad, III, 75-76.

Othman ﷺ alimaliza nakala mbili za Qur'an, kwa kuchanika, kutokana na kusoma sana.[332]

Mtu aliyekuwa na hamasa zaidi ya Qur'an katika wajumbe wa Thaqif ni Othman ibn Abil-As. Yeye alikula kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kusilimu kabla na bila wajumbe wengine kujua. Kwa kuwa alikuwa mdogo kuliko wote, alikuwa akiachwa nyuma kwa ajili ya kuwaangalia ngamia. Wenzake wanaporudi wakati wa mchana kuja kupumzika, Othman ﷺ huenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumuuliza maswali kuhusu mambo mbalimbali, kusikiliza na kujifunza Qur'an. Kwa namna hiyo aliweza kusikia na kuhifadhi baadhi ya sura moja kwa moja kutoka kwa Mtume ﷺ. Akikuta Mtume ﷺ ana shughuli nyingi, alikuwa akienda kwa Abu Bakr au kwa Ubay ibn Kaab ﷺ na kuwauliza au kuwasomea kile alichokihifadhi. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiipenda mno bidii ya Othman ﷺ na kuwa na upendo maalumu kwake. Pindi wajumbe wa Thaqif walipoelezea raghba yao ya kutaka kurudi Taif, walimuomba Mtukufu Mtume ﷺ kumteua kiongozi miongoni mwao. Mtume ﷺ akamtea Othman ﷺ licha ya kwamba alikuwa mdogo kuliko wote. (Ibn Hisham, IV, 185; Ibn Saad, V, 508; Ahmad, IV, 218)

Matukio Mengine Baada ya Tabuk

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na mtoto aitwaye Ibrahim aliyezaliwa kutoka kwa mwanamke wa Kimsri, Mariyah ﷺ. Baada ya Mtume ﷺ kurejea kutoka katika safari ya Tabuk, Ibrahim alishikwa na maradhi na muda mfupi baadaye akafariki dunia. Mtukufu Mtume ﷺ alihuzunika mno kwa kifo cha mwanaye huyo. Kwa ukimya lakini kwa huruma, machozi yalitiririka kutoka machoni mwake. Kisha akasema: "Macho yanalia, moyo unahuzunika, lakini hatusemi lolote zaidi ya yale yanayomridhisha Mola wetu! Ewe

332. Kattânî, II, 197.

Ibrahim, ninaapa kwa Allah, hakika tumehuzunika kwa kututoka!" (Bukhari, Janaiz, 44; Ibn Saad, I, 138)

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ aliagiza aletewe jiwe, akaliweka upande wa kichwa wa kaburi. Sasa kaburi la Ibrahim likawa na alama. Ndiyo kaburi la kwanza kunyunyiziwa maji.[333]

Siku hiyo hiyo, jua lilipatwa. Kutokana na desturi za enzi za Ujahiliya, baadhi ya Maswahaba wakadai kuwa kifo cha Ibrahim ndio sababu ya tukio hilo. Kwa upande mwingine, wakati jua linapatwa, Mtukufu Mtume ﷺ aliswali rakaa mbili, na ili kuonesha kuwa anapinga fikra na dhana walizokuwa nazo maswahaba kuhusu tukio hilo, akasema: "Kupatwa kwa jua na mwezi ni ishara katika ishara za Mwenyezi Mungu. Haitokei kwa sababu ya kifo au uhai wa mtu. Unapoona vimepatwa, jishughulisheni na dhikri ya kumtaja Mwenyezi Mungu na kuswali!"[334] (Nasai, Kusuf, 14)

Katika mwezi wa Rajab, mfalme Najjashi wa Abyssinia (Ethiopia) alifariki dunia. Siku hiyo hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ akawapa taarifa Maswahaba juu ya kifo chake licha ya uwepo wa bahari na umbali mrefu baina ya nchi hizo mbili.

"Mswalieni swala ya jeneza ndugu yenu ambaye amefariki dunia katika ardhi ya mbali", alisema Mtume ﷺ.

"Ni nani huyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Maswahaba waliuliza, naye akawajibu: "Najjashi Ashama…. Leo, Ashama, mja mwema wa Allah, amefariki dunia. Muombeni maghfira Mwe-

333. Ibn Saad, I, 144; Ibn Abdilbarr, I, 59.

334. Sherehe zinazoshuhudiwa katika baadhi ya maeneo wakati wa kupatwa kwa jua na mwezi ni imani potofu ambazo hazihusiani na hazitambuliwi na Uislamu. Badala yake Uislamu unaamrisha kuswali na kuomba dua wakati wa matukio hayo. Kusema kuwa sauti ya bundi ni ishara mbaya na kuanza kulia, yote hayo ni imani potofu.

nyezi Mungu kwa niaba ya ndugu yenu!" Kisha akawaongoza Maswahaba katika swala ya jeneza kwa ajili ya Najjashi. (Muslim, Janaiz, 62-68; Ahmad, III, 319; IV, 7)

Haukupita muda mrefu, habari zikafika Madina, zikithibitisha kuwa Najjashi alifariki dunia siku ileile iliyoelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ,

Mwezi uliofuata, mwezi wa Shaaban, Umm Kulthum ؓ, binti wa Mtukufu Mtume ﷺ na ambaye alikuwa mke wa Othman ؓ, alifariki dunia.[335]

Miezi miwili baada ya Vita vya Tabuk, mwezi wa Dhilqadah, palishuhudiwa maisha ya shari na ya uovu ya Abdullah ibn Ubay, kiongozi wa wanafiki, yakifikia kikomo. Kifo chake kiliitikisa misingi ya vuguvugu la wanafiki mjini Madina. Baada ya kifo chake, wanafiki wengi walitubu na kuwa Waislamu wazuri.

Mtoto wa ibn Ubayy, aliyekuwa akiitwa Abdullah, alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ baada tu ya kifo cha baba yake na kumpelekea ombi lake, akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sasa Abdullah ibn Ubayy amekufa. Ninakuomba kanzu yako iwe sanda yake, na pia wewe uongoze swala ya jeneza lake na kumuombea maghfira!"

Mtukufu Mtume ﷺ alitoa kanzu yake na kumpa Abdullah ؓ mara baada ya mwili kuandaliwa, alimswalia swala ya jenenza.

335. Ibn Saad, VIII, 38.

Lakini, kitendo chake hicho kilipelekea kuteremshwa kwa Ufunuo ufuatao:

وَلاَ تُصَلِّ عَلَى أَحَدٍ مِّنْهُم مَّاتَ أَبَدًا وَلاَ تَقُمْ عَلَىَ قَبْرِهِ إِنَّهُمْ كَفَرُواْ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَاتُواْ وَهُمْ فَاسِقُونَ

"Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa, wala usisimame kaburini kwake. Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakafa na hali ni wapotofu." (at-Tawbah, 84) (Bukhari,Janaiz, 23; Ibn Majah, Janaiz, 31)

Alipoulizwa kwa nini alikubali kutoa kanzu yake kuwa kama sanda ya mwili wa mnafiki mkubwa na kumswalia swala ya jeneza, Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, "Kanzu na swala yangu niliyomswalia havitamlinda dhidi ya adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Bali kwa kufanya hivyo, ninatarajia kuwa maelfu ya watu wake wataongoka!"

Hakika, maelfu ya wanafiki kutoka kabila la Khazraj, waliposhuhudia muamala huo wa Mtume ﷺ waliachana na desturi yao ya unafiki na kuwa Waislamu wazuri.[336]

Mwaka wa Wajumbe Mbalimbali

Makka ilikuwa imechukuliwa, ushindi wa Vita vya Hunayn ulikuwa umepatikana, watu wa Taif waliingia katika Uislamu mwaka mmoja baada ya mzingiro na safari ya kivita ya Tabuk ilikuwa imekamilika kwa ushindi. Na sasa hapakuwepo na kizuizi chochote katika Peninsula ya Arabia ambacho kingeweza kuuzuia Uislamu. Makabila mbalimbali katika Arabia, ambayo wakati huo

336. Aynî, VIII, 54; Diyarbakrî, II, 140-141.

yalifurahia fursa ya kupata maarifa mengi ya Uislamu, yalianza kutuma wajumbe kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ kula kiapo cha kumkubali na kumtii. Wajumbe hawa waliowasili kutoka Yemen, Hadramawt, Bahrain, Amman, mipaka ya Syria na Fursi, walikuja kwa lengo la kusilimu mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ au kumtaarifu kuwa wameshasilimu, na kumuomba Mtume ﷺ awatumie walimu wa kuwafundisha Uislamu.

Kabila la Banu Tujib ni mfano mzuri wa kabila ambalo baada ya kurudi kwa watu wao na kuwafundisha kile ambacho walijifunza kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Ujumbe wa watu kumi na tatu wa kabila hilo waliwasili mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ, wakiwa na Zaka zao. Mtukufu Mtume ﷺ alipendezwa sana na tabia yao na baada ya kuwakaribisha akamwambia Bilal Habashi ؓ kuwakaribisha na kuwakirimu kwa njia nzuri kabisa.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tumekuletea haki ya Mwenyezi Mungu katika mali zetu!"

"Rejeeni nazo na mzigawe kwa maskini miongoni mwenu", alisema Mtukufu Mtume ﷺ.

"Lakini tumeleta kile tu kilichobaki kutoka kwa maskini wetu", walieleza.

Abu Bakr ؓ aliwasifu na kusema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakuna ujumbe mwingine katika Waarabu kama watu hawa wa Tujib!"

"Uongofu upo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Huzifungulia milango ya iman nyoyo za wale anaowatakia kheri", alisema Mtukufu Mtume ﷺ.

Wajumbe wa Banu Tujib walimuuliza Mtume ﷺ maswali kadhaa kuhusu Qur'an na Sunnah. Maswali yao yaliandikwa na kukabidhiwa kwao. Bidii yao iliongeza upendo wa Mtume ﷺ kwao. Baada ya kukaa siku kadhaa, ujumbe huo ulielezea raghba yao ya

kutaka kurudi. Walipoulizwa kwa nini walikuwa na haraka ya kurudi, wakajibu: "Tunataka kurejea kwa watu wetu mapema ili tuweze kuwafundisha yale tuliyoyaona na kujifunza kuhusu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" Walikutana na Mtume ﷺ kwa mara ya mwisho na kumuaga. Mtume ﷺ alimtuma Bilal ؓ kwenda pamoja nao na akawapa zawadi nyingi kuliko ujumbe mwingine wowote. (Ibn Saad, I, 323; Ibn Qayyim, III, 650-651)

Kutokana na wingi wa wajumbe waliokuja Madina na kukaa kwa kipindi fulani cha muda, Mtukufu Mtume ﷺ alihakikisha wanajifunza Qur;an na misingi ya Uislamu. Aliwafundisha dini kwa vitendo kwa kuwafanya waone jinsi yeye mwenye alivyokuwa akiitekeleza na kuifanyia kazi misingi hiyo. Kwa mfano, pindi ulipowasili ujumbe kutoka kabila la Abdul-Qays, aliwataka Ansar wawakaribishe na kusimamia mahitaji yao katika kipindi chote watakachokaa Madina, na wakati huo huo akawaambia wawafundishe wageni wao hao misingi ya Uislamu na wahakikishe wanahifadhi sura za kutosha za Qur'an ili waweze kutekeleza ibada zao za swala. Siku iliyofuata, wakati wa swala ya alfajiri, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaliza hali zao na kama walifurahia huduma za wenyeji wao. Alipoona kuwa walikuwa na furaha sana, aliwagawa kwa jozi baina ya maswahaba ili wapate fursa ya kujifunza Uislamu kwa undani na kwa utulivu zaidi. Akiwa ameridhishwa na juhudi za Maswahaba wake na bidii ya ujumbe wa Abdul-Qays, aliwatembelea wageni hao, mmoja mmoja, na kuwasikiliza yeye mwenyewe jinsi wanavyosoma yale waliyoyahifadhi na kuwasahihisha pale wanapokosea kusoma.[337]

Kwa namna hii, Uislamu ulienea Arabia yote na kukua. Watu walikuwa wakija makundi kwa makundi kwa ajili ya kusilimu na kila Madina ilijaa wageni wapya. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ

337. Ahmad, III, 402.

alikuwa akiwakaribisha kwa upendo, akiamiliana nao kwa heshima na wema, kuzungumza nao kulingana na hali na uelewa wao, akiulizia kuhusu maeneo yao, kusikiliza mahitaji yao na kutatua matatizo na shida zao, na kwa ufupi, akiingiza nuru ya furaha na amani ya Uislamu ndani ya nyoyo zao.[338]

Shida na tabu za zamani sasa zilikuwa zimetengeneza njia ya Baraka na neema. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtaka Mtume Wake na Waumini wote, waliovumilia shida na tabu za miaka ya mateso, kuonesha shukrani zao kwa Baraka na neema alizowajaalia:

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا
فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا

"Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi, na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi. Zitakase sifa za Mola wako Mlezi, na umwombe msamaha; hakika Yeye ndiye anaye pokea toba." (an-Nasr, 1-3)

Kutokana Uislamu kusambaa kwa kasi katika eneo la Arabia na kuwasili kwa wajumbe wa makabila mbalimbali mjini Madina, makundi kwa makundi, kwa ajili ya kujifunza dini ya Haki, mwaka wa tisa wa Hijra unajulikana kama Mwaka wa Wajumbe.

Hajj: Hijja ya Wajibu

Hajj ilikuwa ni ibada ambayo tayari ilikuwa ikitekelezwa kila mwaka kwa mujibu wa Dini ya tawhid ya Nabii Ibrahim ﷺ. Hata hivyo, ibada hiyo ilikuja kuchanganywa na taratibu nyingi za ibada ya masanamu. Katika mwaka wa tisa wa Hijra, Mtukufu Mtume ﷺ

338. Tazama, Nasaî, Umrah, 5.

alimteua Abu Bakr ﷺ kama *amir*, au kiongozi wa Mahujaji, akatuma kundi la Maswahaba mia tatu kwenda Makka kuwafundisha Waislamu jinsi ya kutekeleza ibada yao ya hija, akatangaza wazi kuwa mwaka unaofuata atahudhuria ibada hiyo yeye mwenyewe. Vile vile aliagiza kundi hilo lichukue ngamia ishirini, wote wakiwa wamewekwa alama, kwa ajili ya kuchinjwa kama sehemu ya ibada ya hija.

Wakati Abu Bakr ﷺ akiongoza kundi hilo kutoka Madina, aya za mwanzo wa surah at-Tawbah ziliteremshwa, zikiamuru kuwa waabudu masanamu watoke katika viunga vya Nyumba Tukufu (Al-Kaabah), kama ambavyo muda mfupi uliopita masanamu yalikuwa yameondolewa kabisa. Mpaka wakati huo, waabudu masanamu walikuwa wameachwa huru kutekeleza ibada yao katika Kaabah. Lakini sasa, Kaabah iliporejeshwa katika hali yake ya asili, matendo ya ibada za waabudu masanamu, ikiwa ni pamoja na kuizunguka Kaabah utupu wa mnyama huku wakipiga makofu, haikuhitajika katika Uislamu, na zaidi ya hayo, ilikuwa ikisababisha usumbufu kwa watu. Hivyo, aya hizo za surah at-Tawbah zilikomesha matendo yasiyokuwa na heshima yaliyokuwa yakitendwa mbele ya Nyumba hii Tukufu:

بَرَاءةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدتُّم مِّنَ الْمُشْرِكِينَ فَسِيحُواْ فِي
الأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَاعْلَمُواْ أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَأَنَّ اللَّهَ مُخْزِي
الْكَافِرِينَ وَأَذَانٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الأَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ
بَرِيءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ فَإِن تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُواْ
أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُواْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ إِلاَّ الَّذِينَ عَاهَدتُّم

مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنقُصُوكُمْ شَيْئًا وَلَمْ يُظَاهِرُواْ عَلَيْكُمْ أَحَدًا فَأَتِمُّواْ إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَى مُدَّتِهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ

"Huku ni kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenye jukumu la maagano na mlioahidiana nao katika washirikina. Basi tembeeni katika nchi miezi mine, na jueni kwamba nyinyi hamwezi kumshinda Mwenyezi Mung, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anaye wahizi makafiri. Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wote siku ya Hija Kubwa kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawana jukumu lolote kwa washirikina. Basi mkitubu itakuwa kheri kwenu, na mkigeuka basi jueni kuwa nyinyi hamumshindi Mwenyezi Mungu. Na wabashirie makafiri kuwa watapata adhabu chungu. Isipo kuwa washirikina ambao mliahidiana nao kisha wasikupunguzieni chochote, wala hawakumsaidia yeyote dhidi yenu, basi hao watimizieni ahadi yao mpaka muda wao. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wacha-Mungu." (at-Tawbah, 1-4)

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلاَ يَقْرَبُواْ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ إِن شَاء إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

"Enyi mlio amini! Hakika washirikina ni najsi, kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu. Na ikiwa mnakhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu atakutajirisheni kwa fadhila yake akipenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima." (at-Tawbah, 28)

Mtukufu Mtume ﷺ alimuagiza Ali ؓ, nyuma ya Abu Bakr ؓ, kwenda kutoa tangazo la aya hizo mjini Makka. Katika siku ya kwanza ya *eid*, Ali ؓ alisimama jirani na Aqabah na kutoa hotuba kutekeleza jukumu aliloagizwa. Baada ya kusoma aya hizo, alitangaza masharti manne yaliyowekwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ ili kila mmoja ayasikie:

1) Waumini ndiyo pekee watakaoingia Peponi.

2) Uzushi wa Washirikina wa kuizunguka kaabah wakiwa uchi umefikia kikomo na hautavumiliwa tena.

3) Kuanzia mwaka huo na kuendelea, hakuna *mushrik* ambaye angeruhusiwa katika viunga vya Kaabah.

4) Ama kwa wale washirikina waliokuwa na mkataba maalumu na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na ambao waliendelea kuutekeleza, mikataba hiyo ingeendelea mpaka mwisho wa muda waliokubaliana.

Baada ya mwaka huo, hakuna mshirikina angeweza kwenda kuhiji, na ndio mwisho wa watu kuizunguka Kaabah kwa kutumia desturi za zamani. Aidha, kundi dogo la waabudu masanamu lililokuwa limebaki lilikubali kuwa imani zao zilikuwa potofu na hatimaye wakaingia katika Uislamu. Kama ambavyo hapo kabla ilisafishwa dhidi ya masanamu, sasa Kaabah ilikuwa imesafishwa dhidi ya waabudu masanamu na kuwa tayari kwa ajili ya Hijja Kuu ambayo ingehudhuriwa na Mtukufu Mtume ﷺ mwaka uliofuata.[339]

339. Ibn Hisham, IV, 201; Tirmidhi, Hajj, 44/871; Waqidi, III, 1077.

MWAKA WA KUMI WA HIJRA

Adiy ibn Hatim aukubali Uislamu

Baba wa Adiy ni mtu maarufu aitwaye Hatim Tai. Hatim anatoka katika kabila la Tayy na alikuwa maarufu sana kwa ukarimu wake. Kama ilivyokuwa kwa baba yake, Adiy alikuwa mtu mkarimu na maadili mema aliyeheshimika ndani ya kabila lake. Alikimbilia Damascus katika mwaka wa kumi wa Hijra pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipomtuma Ali ؓ kwenda kwa kabila la Tayy kuvunja sanamu lao, Fuls. Dada yake, Saffanah, kwa upande mwingine, aliletwa Madina akiwa miongoni mwa mateka wengine.

Mtukufu Mtume wa Rehma ﷺ alimuacha huru Saffanah, akampa zawadi za mavazi, ngamia mmoja na vitu atakavyotumia safarini, na akamtuma mpaka Damascus akisindikizwa na watu waaminifu.

Adiy ibn Hatim anasimulia:

"Safannah alikuwa mwanamke mwerevu sana. 'Unasemaje kuhusu mtu huyu?' nilimuuliza. Akajibu, 'Ninaapa, ni bora uungane naye haraka. Kama kweli ni mtume, ukishindana na wengine katika kuungana naye utapata heshima na neema. Kama ni mfalme, basi hutapoteza nafasi yako huko Yemen na kuwekwa katika nafasi ya chini. Sasa chaguo ni lako!'

'Hilo ni kweli kabisa', nilisema. 'Nitaenda kwa mtu huyu. Kama ni muongo, uongo wake hautanidhuru chochote. Kama anayoyasema ni ya kweli basi nitayasikiliza na kushikamana naye!' Haukupita muda mrefu nikawasili Madina.Nilipomuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katikati ya ndugu zake, wanawake na watoto, nikabaini kuwa hakuwa Kaisari wala Khosro! Mtume wa Mwenyezi Mungu alinishika mkono na kunipeleka nyumbani kwake. Tukiwa njiani, mwanamke mmoja kikongwe alimsimamisha na kuzungumza naye kuhusu shida fulani. Alimsikiliza kwa umakini akiwa amesimama na kumtatulia shida yake. Tulipofika nyumbani kwake, alinipatia mto uliojazwa majani ya mitende na kuniambia; 'Chukua ukae!'

Nikamwambia, 'tafadhali, wewe ungekaa juu ya mto!'

'Hapana… Wewe kalia!' alijibi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Hatimaye nilikaa juu ya mto huku Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akikaa chini. 'Haya hayawezi kufanywa na mfalme', niliwaza.

'Ewe Adiy, ingia katika Uislamu utapata amani', alisema.

'Tayari nina dini', nilimjibu.

'Ninaijua dini yako vizuri zaidi kuliko unavyoijua', aliniambia.

'Unaijua dini yangu kuliko mimi?'

'Ndiyo…Wewe si *Raqusi*? [340]Huchukui robo ya ngawira zinazochukuliwa na kabila lako?' aliuliza.

'Bila shaka', nilimjibu.

340. Imani ya *Raqus* ni mchanganyiko wa imani zilizochukuliwa kutoka kwenye dini za Ukristo na Sabai.

'Lakini kwa mujibu wa dini yako, hilo haliruhusiwi' alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Hakuongeza kitu. Nilitahayari aliposema hivyo. 'Ni kweli', hilo ndilo nililoweza kusema. Lakini kwa kuwa alikuwa makini kutoendelea na suala hilo lililonitahayarisha, niliwaza kuwa atakuwa ni Mtume aliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

'Ninajua kinachokuzuia kuingia kwenye Uislamu', aliendelea kusema. 'Unawaza kuwa 'watu wanyonge na wale walio duni machoni mwa Waarabu ndio wanaoungana naye'. Unaijua Hirah?'

'Sijawahi kufika huko lakini nimeisikia'.

'Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, Mwenyezi Mungu ataikamilisha dini hii, kiasi kwamba mwanamke ataweza kusafiri kutoka Hirah na kuja kuizunguka nyumba ya Mwenyezi Mungu. Kisha hazina za Khosro Hurmuz zitachukuliwa!'

'Khosro Hurmuz?' niliuliza kwa mshangao.

'Muda si mrefu, mali zitarundikana kiasi kwamba hakuna mtu atakayetaka kuzichukua na hapatukuwa na mtu hata mmoja mwenye sifa ya kupokea zake!'

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifurahi mno kuniona nikiukubali Uislamu. Wajihi wake ulichanua kutokana na kufurahi na kuridhika. Nilipatiwa makazi katika nyumba ya Ansar kama mgeni. Baada ya hapo, nilikuwa nikimtembelea mchana na usiku. Hakuna muda wa swala ambao ungepita bila kuonana naye!"

Baada ya miaka mingi kupita, Adiy رضي الله عنه alisimulia kumbukumbu hiyo akisema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, nilimuona mwanamke akitoka Hirah juu ya ngamia bila wasiwasi wowote kwenda kwenye

Kaabah na kutekeleza ibada yake ya hija! Name pia nilikuwa miongoni mwa wale waliotwaa hazina za Khosro. Naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu iko mikoni mwake, bila shaka tukio la tatu litatokea kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alivyotabiri!" (Bukhari, Manaqib, 25; Ahmad, IV, 257, 377-379; Ibn Hisham, IV, 246; Ibn Kathir, al-Bidayah, V, 62)

Kwa hakika, habari ya tatu iliyotabiriwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ilitokea. Khalifa Omar ibn Abdulaziz alimtuma mgawaji rasmi wa zaka kwenda Afrika, baada ya kuona kuwa katika maeneo mengine ya dola ya Kiislamu hapakuwa na watu wenye sifa. Lakini mtu huyo naye alirejea bila kupata mtu mwenye sifa za kupokea zaka. Pesa hiyo ikatumika kuwanunua na kuwaacha huru watumwa wengi.[341]

Hijja ya Kwanza na ya Mwisho ya Mtukufu Mtume ﷺ: Hijja ya Kuaga

Hija ya kwanza na ya mwisho iliyohudhuriwa na Mtukufu Mtume ﷺ baada ya kufaradhishwa, ni *Hajjul-Wada'*, yaani Hija ya Kuaga. Katika hija hii, ambayo Mtukufu Mtume ﷺ aliwaaga Waislamu, Maswahaba waliichukulia kuwa ni alama ya kuondoka kwake duniani, na hiyo ndiyo sababu ya kuitwa jina hilo.[342] Kwa upande mwingine, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiita hija hii kama *Hajjatul-Islam*.[343]

Waislamu wote waliitwa kuhudhuria hijja hii iliyosadifiana na mwaka wa kumi wa Hijra, katika zama ambazo Arabia yote ikiwa

341. Tazama, Bûtî, uk.434.
342. Bukhari, Hajj, 132.
343. Haythami, III, 237.

imeikubali nuru ya uongofu na kufurahia kilele cha mamlaka na ukuu.

Nyoyo zilizojaa upendo tele wa kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake, ziliitikia wito huu. Pindi taarifa hizo zilipofikishwa nje ya Madina, watu walimiminika kutoka kila kona. Wale walioungana na halaiki njiani hawakuwa na idadi maalumu. Halaiki ya watu ilikuwa imelifunika kila eneo linaloonekana kwa macho. Idadi ya waumini waliowahi ili wapate fursa ya kutekeleza ibada ya hijja pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ilifikia watu laki moja na elfu ishirini. Nyoyo zao zote zilikuwa zikipiga kwa mdundo mmoja, na kutengeneza mandhari ya ajabu.

Mtukufu Mtume ﷺ alianza safari baada ya kutoa maelezo mbalimbali kuhusu hijja na *ihram*. Alichukua ngamia wapatao mia moja kwa ajili ya kuchinja wakati wa ibada hiyo. Njiani, alizungumza na Waislamu kuhusu vipengele mbalimbali vya hijja, akielezea hasa ya wajibu na ya faradhi kuhusu ibada hiyo. Baada ya kufika Dhul-Hulayfah, katika Bonde la Aqiq, aliwaambia Maswahaba maneno yafuatayo:

"Jibril alinijia usiku kutoka kwa Mola wanguna kuniambia, 'Swali katika bonde hili tukufu na weka nia ya hijja na *umrah*.'" (Bukhari, Hajj, 16)

Hapo, Mtukufu Mtume ﷺ aliswali rakaa mbili kabla ya kuvaa *ihram*. Baada ya kumtukuza na kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu na kusoma *takbir*, akaomba akisema: "Mola wangu! Ifanye hijja hii kuwa hijja yenye kukubaliwa na iliyotakasika dhidi ya unafiki na udanganyifu." (Ibn Majah, Manasiq, 4)

Baada ya kuomba dua hiyo alivaa vazi la *ihram* na kuanza kusoma *talbiyah*. (Bukhari, Hajj, 23) Kisha alisema: "Mwenye kutaka kunuia ibada ya hijja na *umrah*, afanye hivyo!" Mtme ﷺ alipoanza kusoma *talbiyah*, aliwaambia Maswahaba kuwa Jibril عليه السلام alimjia

na kumwambia: "Waamuru Maswahaba wako wanyanyue sauti zao wakati wa kusoma *talbiyah*, kwa kuwa ni miongoni mwa ishara za hijja!" (Ibn Majah, Manasiq, 16)

Mbingu na ardhi zilijaa mvumo wa sauti za *talbiyah*. Hali ya kiroho ilikuwa ikitawanya amani yake, kama utando, kila kona. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaswalisha Waislamu kila alipokwenda. Miaka mingi baadaye, misikiti ilijengwa katika kila eneo alilowaswalisha waislamu, kama ishara ya utiifu na upendo.[344]

Mtukufu Mtume ﷺ alipoiona Nyumba Tukufu, alinyanyua juu mikono yake na kuomba, "Mola wangu! Iongezee Nyumba Yako heshima, utukufu, ukuu na adhama! Pia wale wataiheshimu wakati wa hijja na *umrah*, waongezee heshima, ukuu, utukufu, adhama na wema!" (Ibn Saad, II, 173)

Akiwa na *rida* yake aliyoining'iniza kuzungua geba lake la kushoto kutokea chini ya ubavu wake wa kulia, na kuliacha wazi bega la kulia, Mtukufu Mtume ﷺ aliingia *Masjid'ul-Haram*. Kisha aliisogelea *Hajar'ul-Aswad* na kuigusa. Macho yake yalijaa machozi. Akalibusu Jiwe Jeusi, na baada ya kulishika kwa mkono wake, aliipangusa mikono yake usoni mwake.

"Mola wangu! Ninaanza kwa *iman* juu Yako, kusadikisha Kitabu Chako na kushikamana na sheria za Mitume wake", akamba dua na kisha akaanza kuizunguka Kaaba kutokea kwenye kona ya Jiwe Jeusi. (Haythami, III, 240)

Wakati wa mizunguko mitatu ya kwanza, Mtukufu Mtume ﷺ alifupisha hatua zake na kutembea ka hatua ya haraka, huku akiyabembeleza mabega yake. Kila alipofika usawa wa *Rukn'ul-Yamani* na *Hajar'ul-Aswad* alikuwa akisoma aya hii:

344. Ibn Saad, II, 173.

وِمِنْهُم مَّن يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

"Na katika wao wapo wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto!" (al-Baqara, 201)

Baada ya kukamilisha hatua hiyo ya kuizunguka Kaabah, kwa mara nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ aliibusu *Hajar'ul-Aswad*, akaiweka mikono yake juu ya Jiwe hilo na kisha akaufuta uso wake kwa mikono yake. Baada ya hapo, aliweza kupita katikati ya umati mkubwa wa Waislamu na kufanikiwa kufika kwenye *Maqam-u Ibrahim* kwa tabu na shida. Alipoiweka *Maqam* baina yake na Kaabah, aliswali rakaa mbili. Kisha, kwa mara nyingine, aligeuka na kuligusa Jiwe Jeusi na kumpa wosia Omar ؓ ambaye alikuwa amesimama jirani naye. "Ewe Omar! Hakika wewe ni mtu mwenye nguvu. Usisababishe matatizo kwa wanyonge kwa kuwasukuma na kuwapiga vikumbo watu ili ufike kwenye *Hajar'ul-Aswad*! Usipate tabu na usisababishe tabu! Utakapoona kuwa kuna nafasi, basi iguse *Hajar'ul-Aswad* na uibusu. La sivyo, itazame kwa mbali na upite huku ukisema *La ilaha ill-Allah* na *Allah'u Akbar*!"[345] (Haythami, III, 241; Ahmad, I, 28)

---

345. Hata Omar ؓ alikuwa akilitazama Jiwe Jeusi kutokea mbali, akihofu kuwa anaweza kuwaumiza mahujaji wengine kama akilisogelea. Hiki ni kitu ambacho Waislamu wanaoenda hijja wanatakiwa kukiwekea maanani sana. Wanatakiwa wasipoteze thawabu wanazozipata kwenye hijja kwa kuwaumiza Waislamu wenzao. Katika kushikamana na wosia uliotolewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, muumini anatakiwa kuacha kabisa kuwasukuma na kuwapiga vikumbo Waislamu wenzake kwa ajili ya kuikaribia Kaabah au Jiwe Jeusi. Imesimuliwa kuwa siku moja Omar ؓ alilibusu Jiwe Jeusi na kusema: "Ninajua kuwa wewe ni jiwe tu; huwezi kudhuru wala kunufaisha. Lau si kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akikubusu, nisingekubusu!" (Bukhari, Hajj, 50; Muslim,

Kisha alitoka *Masjid'ul-Haram* kupitia mlango wa Banu Mahzum, akaelekea kwenye Mlima wa Safa. Alipoukaribia, akasoma:

إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ اللَّهِ

"Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu…" (al-Baqara, 158) Kisha akasema: "Ninaanzia sehemu iliyoanza kutajwa na Mwenyezi Mungu katika aya" na kusogea upande wa Safa ili kuanza *sa'y*. alipoiona Kaabah, aliitazama na kusema *La ilaha ill-Allah, Allah'u Akbar*. Alifanya hivyo mara tatu au mara saba, kisha akasema: "Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah, Mmoja, hana mwenza wala mshirika. Ufalme ni Wake, na Yeye pekee ndiye anayeshukuriwa. Anahuisha na kufisha… Naye ni Muweza juu ya kila kitu. Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah. Allah ametimiza ahadi Yake. Amemnusuru mja Wake na Yeye Mwenyewe akayashinda majeshi yaliyojikusanya kwa ajili ya uadui." (Ibn Majah, Manasiq, 84)

Kutoka Safa, Mtume ﷺ akaelekea kwenye Mlima wa Marwa kwa miguu. Akiwa katikati ya njia aliongeza kasi ya kutembea, na kisha akatembea kwa mwendo wa wastani na huku akiomba: "Mola wangu! Nighufurie na unirehemu! Hakika Wewe ni Mwenye Kusamehe na Mwenye kurehemu!" (Haythami, III, 248)

Mtukufu Mtume ﷺ alipofika Mlima wa Marwa, alirudia kusema kile alichosema kwenye Mlima wa Safa.Alikwenda na kurudi mara saba baina ya vilimi vya Safa na Marwa, akakamilisha *sa'y*.

Hajj, 251) Huu ni uthibitisho wa ulazima wa kumfuata Mtukufu Mtume ﷺ katika mambo yote, hata kama mtu hafiki kwenye kina cha kulielewa tendo husika.

Mtukufu Mtume ﷺ alikaa Makka kwa muda wa siku nne. Siku ya tano, siku ya *tawriyah*, baada ya kumaliza kuizunguka tena Kaabah, alipanda ngamia wake na kuelekea Mina, ambapo alibaki huko mpaka siku iliyofuata, huko akaswli Adhuhuri, alasairi, maghribi isha na alfajiri. Asubuhi ya siku ya tisa ya Dhulhijjah, alielekea Arafat, huko akafanya *talbiyah*.

Baada ya kuonesha kwa vitendo jinsi hijja itakavyotekelezwa na umma wake na baada ya kukamilisha wajibu zote zinazohusu hija, Mtukufu Mtume ﷺ alitoa Hotuba yake ya Kuaga, katika mlima Arafat, mahali ambapo leo kuna Masjid Namirah:

"Enyi watu!

Yasikilizeni maneno yangu kwa umakini! Hakuna ajuaye… huwenda mwaka huu ukawa wa mwisho kwangu kuwa hapa pamoja nanyi!

Enyi watu!

Kama ambavyo siku hizi, miezi hii na mji huu ni vitukufu, vivyo hivyo, uhai wenu, mali zenu na staha zenu ni vitukufu. Ni haramu kuvikiuka.

Enyi Waislamu!

Kesho, mtakunana na Mola weny na kuhesabiwa kwa yale mnayoyatenda leo! Msirejee kinyumenyume kwenye mila zenu za zamani na kuchinjana nyinyi kwa nyinyi baada yangu! Jueni kwamba nitawatangulieni na kuwasubiri kwenye Birika (la Kawthar)! Nitajifakhiri kwa idadi yenu juu ya umma nyingine! Angalieni msinishushe chini (kwa kuangukia katika dhambi)!

Enyi Waislamu!

Kila mwenye amana ya mtu airejeshe kwa mwenye nayo! Kila aina ya riba imefutwa; iko chini ya migu yangu. Bali mtu anatakiwa

kurejesha mkopo. Usidhulumu wala usidhulumiwe! Sasa kujihusisha na riba kumeharamishwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Mambo yote yenye kuchukiza, yaliyokuwa yakifanywa katika zama za Ujahiliya, sasa yako chini ya miguu yangu. Riba ya kwanza ninayoifuta ni ile ya (ami yangu) Abbas ibn Abdulmuttalib.

Enyi Maswahaba!

Uhasama wa enzi za Ujahiliya, nao umefutwa moja kwa moja. Taasubi ya kwanza ninayoifuta ni ile ya Rabia, mjukuu wa Abdul-Muttalib.

Enyi watu!

Leo shetani amepoteza nguvu yake ya kurejesha ushawishi na mamlaka yake katika hii ardhi yenu. Lakini, bado ataendelea kufurahi iwapo mtamfuata katika mambo ya upuuzi, mbali na yale ambayo nimeyafuta. Jiepusheni nayo pia ili kuilinda dini yenu!

Enyi watu!

Chungeni haki za wanawake! Amilianeni nao kwa upendo na huruma! Ninawausieni kumcha Mwenyezi Mungu kuwahusu wanawake! Mmewachukuwa wanawake kama amana ya Mwenyezi Mungu; staha na heshima yao kwa jina la Mwenyezi Mungu! Mna haki juu ya wanawake, nao wana haki juu yenu! Haki mliyonayo juu ya wanawake ni kwamba wasiruhusu yeyote kuikanyaga heshima ya familia yenu! Haki ya wanawake juu yenu ni kuwa mnatakiwa kuwapa, kihalali, matumizi na mavazi. Hairuhusiwi kwa mwanamke kutoa kitu katika mali ya mumewe na kumpa mtu bila ruhusa yake.

Ama kuhusu watumishi wenu, walisheni katika vile mnavyokula nyinyi wenyewe na muwavike katika vile mnavyofaa nyinyi wenyewe. Wakifanya kitu ambacho hamuwezi kuwasamehe, basi

waacheni waondoke! Lakini msiwaadhibu; kwa maana, nao ni waja wa Mwenyezi Mungu.

Enyi waumini!

Sikilizeni maneno yangu na myazingatie vizuri! Muislamu ni ndugu wa Muislamu; hivyo Waislamu wote ni ndugu. Hairhusiwi kudhulumu haki ya ndugu yako katika dini, labda kama ataitoa kwa ridhaa yake mwenyewe.

Enyi Maswahaba!

Msizidhulumu nafsi zenu! Nafsi zenu zina haki juu yenu pia!

Enyi watu!

Mhalifu ni mwenye kuwajibika kwa kosa lake yeye mwenyewe. Mtoto hatabeba adhabu ya kosa la baba! Wala baba hatawajibika kwa uhalifu wa mwanaye!

Enyi watu!

Mwenyezi Mungu amempa kila mwenye kustahiki, haki yake (katika Qur'an)! Mwenye kurithi hahitaji wosia![346] Kitanda atakachozaliwa mtoto, hapo ndipo kwake. Mzinifu atanyimwa. Ghadhabu na laana ya Mwenyezi Mungu, Malaika na Waislamu wote itamkuta yule mwenye kudai kuwa katika nasaba tofauti na ile ya baba yake au mtumwa asiye na fadhila anayedai kuwa anatoka kwa mtu mwingine tofauti na bwana wake![347] Mwenyezi Mungu haikubali toba na ushuhuda wa watu hao.

Enyi watu!

346. Kabla ya kuteremka kwa aya ya mirathi iliyoweka haki za warithi kwa kuanisha wale wenye kurithi mali za marehemu, ilikuwa wajibu kwa Muslamu kuacha wosia. Hata hivyo, bado Muislamu anaruhusiwa kuacha wosia kuhusu theluthi moja ya mali yake, ambayo hukmu ya kisheria inaweza kuzingatiwa.

347. Kwa maelezo kuhusu utumwa, tazama uk. 157-160

Mola wenu ni Mmoja! Vivyo hivyo baba yenu ni mmoja; nyote ni watoto wa Adam, na Adam anatokana na udongo. Mwenye thamani zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mwenye *taqwa* zaidi. Mwarabu hana ubora juu ya asiyekuwa mwarabu, isipokuwa kama atakuwa na *taqwa*.

Enyi watu!

Hakika zama ambazo zimeendelea kuzunguka, zimerejea katika awamu ambapo Mwenyezi Mungu aliumba mbingu na ardhi. Mwaka una miezi kumi na mbili. Katika yake kuna minne mitukufu (*haram*). Mitatu kati yake ni yenye kufuatana, ambayo ni Dhil-qadah, Dhil-hijjah na Muharram, na wa nne ni Rajab ((baina ya Jamadi'al-Akhir na Shaban). Mwaka huu, miezi mitukufu imerejea katika zama zake za kale. Msimu wa hijja umesadifiana na siku ya kumi ya Dhil-hijjah.

Enyi Waumini!

Ninakuachieni amana, ambayo mkishikamana nayo hamtapotea kamwe. Amana hiyo ni Qur'an, Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Enyi watu!

Muabuduni Mwenyezi Mungu! Tekelezeni swala tano za kila siku! Fungeni swaumu wakati wa mwezi wa Ramadhan na mtii maamrisho yangu! Hivyo mtaingia Peponi.

Enyi watu!

Tahadharini na kupindukia hali ya kiasi! Kupindukia katika dini ndiyo sababu iliyowafanya waliokuwa kabla yenu kuangamia! Jifunzeni taratibu za hijja kutoka kwangu! sijui, huwenda nisiweze kukutana nanyi tena hapa, baada ya mwaka huu! Wale waliopo wafikishe maneno yangu kwa wale ambao hawapo! Huwenda yule

aliyefikishiwa akayaelewa vizuri zaidi na kuyalinda maneno yangu kuliko mfikishaji."

Baada ya kusema maneno hayo, aliwauliza maswahaba zaidi ya laki moja na elfu ishirini waliokuwepo hapo: "Enyi watu…kesho mtaulizwa kuhusu mimi; mtasema nini?"

"Tunashuhudia kuwa ulitekeleza wajibu wako kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ukatuonya na kutuusia", umati wa waumini ulisema kwa pamoja.

Kufuatia ushuhuda huo wa Waumini, Mtukufu Mtume ﷺ akauliza mara tatu: "Je nimefikisha?" Maswahaba wote wakatoa kauli za ushuhuda, ndipo alipoinua mikono yake juu na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awe shahidi:

"Shuhudia ewe Mola wangu! Shuhudia ewe Mola Wangu! Shuhudia ewe Mola wangu!" (Muslim, Hajj, 147; Abu Dawud, Manasiq, 56; Ibn Majah, Manasiq, 76, 84; Ahmad, V, 30; Ibn Hisham, IV, 275; Hamidullah, al-Wasaiq, uk. 360)

Hotuba hii ya Kuaga ni sheria zinazoratibu mahusiano ya kijamii, mukhtasari wa mafunzo ya Uislamu na, wakati huo huo, ni mizani ya mwenendo na haki za binaadamu. Kabla ya uundwaji wa Azimio maarufu la Haki za Binaadamu, La Fayette, mwanafalsafa maarufu wa Kifaransa anayetambulika kuwa miongoni mwa waasisi na nguzo muhimu ya Mapinduzi ya Ufaransa ya mwaka 1789, baada ya kufanya utafiti wa kina kuhusu mifumo mbalimbali ya kisheria duniani, hatimaye alikutana na Hotuba ya Mwisho ya Mtukufu Mtume ﷺ; na alipoiona kuwa inawakilisha misingi ya haki na uadilifu kwa wanadamu wote, akalazimika kukiria: "Ewe Muham-

mad Mwenye ukuu…! Umefikia kilele cha juu kabisa cha uadilifu kiasi kwamba hakuna mtu aliyekifikia na hakuna atakayekifikia!”[348]

Katika Hotuba hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaainisha kanuni ambazo wanadamu wanatakiwa kuzijua ili pasiwepo na udhuru kwa kutozijua. Umati mkubwa uliokuwepo uliwezesha yaliyomo katika Hotuba hiyo kuwafikia wanadamu wote.

Baada ya Hotuba hiyo, Bilal Habashi رضي الله عنه alitoa adhana. Mtukufu Mtume ﷺ akawaswalisha Waislamu swala za Adhuhuri na Alasiri kwa kuzikusanya (jam’), kwa *iqamah* moja kabla ya kila swala. Kisha alimpanda ngamia wake Qaswa, akaenda sehemu ya waqfah jirani na Jabal’u-Rahmah. Alimuelekeza Qaswa upande wa miamba, kwenye uelekeo wa Kaabah. Alisimama katika *waqfah* mpaka jua lililipozama na kupoteza mwanga wake kabisa.

Wakati wa *waqfah*, akiwa amezishikilia hatamu za ngamia wake kwa mkono mmoja huku akiwa ameuinua juu mkono mwingine, Mtume ﷺ aliomba dua ndefu, kuonesha hisia zake za kiroho na unyenyekevu wake; sehemu ya dua hiyo ni kama ifuatavyo:

“Mola wangu! Himidi ni Zako kama ulivyozitangaza na kwa namna iliyo bora zake ya tunavyozielezea! Ewe Mwenyezi Mungu…! Hakika swala, ibada, uhai na mauti yangu ni kwa ajili Yako pekee! Kwako nitarejea!

Mola wangu! Ninajilinda Kwako dhidi ya adhabu ya kaburini, wasiwasi na shari ya nafsi! Ewe Mwenyezi Mungu… ninajilinda kwako kutokana na majanga yaletwayo na upepo!

348. Tazama, Kâmil Mîras, *Tecrîd-i Sarîh Tercemesi*, IX, 289.

Ewe Mola wangu! Nijaalie nuru machoni mwangu, nuru masikioni mwangu na nuru moyoni mwangu! Ewe Mwenyezi Mungu…Kikunjue kifua change! Yafanyie wepesi mambo yangu! Ewe Mwenyezi Mungu…Ninajilinda kwako dhidi ya mabadiliko ya siha kuwa maradhi, dhidi ya adhabu Yako inayokuja bila hadhari na kutokana na ghadhabu Yako! Ewe Mwenyezi Mungu…Niongoze kwenye njia Yako ya haki! Nisamehe makosa yangu yaliyotangulia na yajayo!

Ewe Mwenyezi Mungu, Mwenye kunyanyua daraja, Mwenye kuteremsha neema na Baraka… Ewe Mwenyezi Mungu uliyeumba mbingu na ardhi! Sauti za huruma kutoka lugha mbalimbali hupanda kuja Kwako, zikikuomba na kukusihi! Nami ninakuomba unikumbuke katika uwanja wa majaribu nitakaposimama nikiwa nimetengwa na watu wa ulimwengu!

Mola wangu! Unayasikia maneno yangu, unaona mahali nilipo na unajua kila jambo langu, liwe na siri au la dhahiri! Hakuna jambo langu lolote linalofichika Kwako! Hakika mimi ni mnyonge na maskini; ninakuomba msaada na huruma Yako! Ninakiri upungufu wangu; hakika mimi ni mwenye khofu! Ninakuomba kwa namna akuombavyo mtu asiye na msaada! Ninakuomba kwa namna ambayo mja Wako, dhalili mbele yako, anavyokuomba kwa machozi yanayomiminika kutoka machoni mwake, akiupangusa uso wake katika vumbi, ambaye hujisalimisha moja kwa moja kwa ajili Yako! Mola wangu usinikatalie dua yangu! Nikirimu na unirehemu… Ewe mbora wa wenye huruma na mbora wa wenye ukarimu!" (Ibn Kathir, al-Bidayah, V, 166-168; Haythami, III, 252; Ibn Qayyim, II, 237)

Ifuatayo ni sehemu ya dua iliyokuwa ikiombwa na wema waliotanguliza (*salaf 'us-salihin*) katika mlima Arafat:

"Ewe Mwenyezi Mungu…Nani mwenye kuweza kujisifu mbele yako? Mola wangu! Ulimi wangu umefungwa na madhambi yangu…sina amali ambayo ninaweza kuitumia kama njia ya kuelekea Kwako wala sina muombezi tofauti na raghba yangu! Mola wangu…Ninajua kwamba sina nafasi mbele Yako kutokana na dhambi zangu na wala sinauso ambao naweza nikasimama mbele yako na kukuomba msamaha! Mola wangu…japokuwa sisitahili msamaha Wako, bado huruma Yako inaweza kunifikia, kwa maana huruma Yako imekienea kila kitu! Mola wangu…Hata kama dhambi zangu zitakuwa na ukubwa kiasi gani, msamaha Wako ni mkubwa zaidi! Hivyo, Ewe Mola wangu Mkarimu, nisamehe makosa yangu!

Mola wangu! Kama utawasamehe waja Wako wasafi tu, basi wakosaji wamkimbilie nani? Ewe Mwenyezi Mungu! Kama utawahurumia waja Wako wema tu, wenye dhambi waombe msaada kutoka wapi?

Ninakuhitaji nyakati zote; lakini Wewe hunihitajii hata kidogo! Unaweza kunisamehe tu kama Muumba wangu! Nirejeshe kutoka sehemu niliyosimama nikiwa nimetimiziwa mahitaji yangu na maombi yangu yakiwa yamejibiwa!

Ewe Mola wangu mwenye kuweza kutimiza mahitaji ya wale wote wanaoomba! Ewe Mola wangu mwenye kujua kinachopita katika akili za wale waliokaa kimya! Ewe Mola wangu ambaye hana aliyemuumba wa kumhofia! Ewe Mola wangu usiyekuwa na waziri tunayepaswa kumtembelea, wala mlinzi tunayepaswa kumpa hongo! Ewe Mola wangu ambaye ukarimu wake haupungui kwa maombi mengi; ambaye hutoa kwa mahitaji yote yaliyopo! Mola wangu! Hakika Wewe huwakirimu wageni wote! Nasi pia ni wageni Wako! Tukirimu kwa Pepo Yako!

Ewe Mola wangu! Wageni wote wamekirimiwa zawadi; wale wote wenye kuendelea kuomba wamepewa zawadi zao, huku wage-

ni wote wakiamiliwa vyema! Kila mtu anayetarajia malipo amepewa! Sote kwa pamoja tumekuja kwenye Nyumba Yako Tukufu! Sote tumesima katika eneo hili tukufu! Sote tumekuwa katika ardhi hii takatifu! Tumaini letu ni kupata thawabu zinazotusubiri mbele ya hadhira Yako Kuu! Ewe Mwenyezi Mungu, usiyatupilie mbali matumaini yetu!" (Ghazzali, Ihya, I, 337-338; Bayhaki, Shuab'ul-Iman, II, 25-26)

Wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiwa bado yuko Arafat, baadhi ya watu kutoka Najd walimkaribia na kumuuliza: "Ewe Mjumbe wa Allah, hijja ni nini na inakamilishwaje?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Hijja ni Arafat. Atakayefika Arafat kabla ya swala ya alfajiri usiku wa Muzdalifah atakuwa ameikamilisha hijja. Siku za kukaa Mina ni tatu. Hakuna lawama kwa atakayewahi na kukaa huko kwa muda wa siku mbili tu; wala hakuna lawama kwa yule atakayechelewa kufika." (Ibn Majah, Manasiq, 57)

Leo Nimekukamilishieni Dini Yenu

Aya iliyoteremshwa muda wa maghribi wakati Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amesimama kwenye *waqfah*, ilitangaza kuwa sasa Uislamu ulikuwa umetimilizwa na kukamilishwa:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الإِسْلاَمَ دِينًا

"…Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini." (al-Maida, 3) (Tirmidhi, Tafsir, 5/3043)

Kwa maono yake ya mbali, Abu Bakr ﷺ alipoisikia aya hiyo, alibaini kitu. Alitambua wazi 'neema iliyotimizwa' ilimaanisha nini na tukio ambalo lingefuata baada ya 'kukamilishwa kwa dini.'

Kwa wale wenye maono ya mbali, aya hiyo ilitoa habari kwamba si muda mrefu Mtukufu Mtume ﷺ angefariki dunia. Ndani ya muda mfupi, Mwenyezi Mungu Mtukufu angemchukua Kipenzi chake na Mtume Wake ﷺ kwenda kwenye ulimwengu wa milele. Macho ya Abu Bakr ﷺ yakajawa na machozi akilia kwa maumivu ya kutengena naye, ilhali hakuna mtu mwingine aliyeweza kuelewa kilichokuwa kikiashiriwa na aya hiyo.[349]

Na sasa amana tukufu, ambayo iliteremshwa kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu, ilikuwa katika kilele cha kukabidhiwa kwa kila mwana umma huu mpaka Siku ya Kiyama.

Baada ya jua kuzama kabisa, Mtukufu Mtume ﷺ, akiwa pamoja na Usamah ibn Zayd ﷺ, alitoka Arafat kwenda Muzdalifah. Alipofika huko, aliswali swala za maghribi na isha kwa kuzikusanya (jam'), kwa adhana moja na *iqamah* kabla ya kila swala. Alikaa Muzdalifa mpaka mapambazuko na kubaki katika *waqfah* mpaka jua lilipochomoza kikamilifu, akifanya *talbiyah* na kuomba dua mbalimbali.

Akiwa hapo Muzdalifah, Mtukufu Mtume ﷺ alikusanya mawe ambayo angeyatumia Mina, na kuwaamuru Maswahaba nao kukusanya mawe watakayoyarusha kwenye jamrah.[350] Akitumia mikono

349. Elmalılı, III, 1569.

350. *Jamrah* ina maana ya kaa la moto, kijinga cha moto au mawe madogo madogo. Hapa inaashiria mahali ambapo *jamrah* hutupwa wakati wa ibada ya hijja; kiwango cha kokoto kinachorushwa eneo maalumu, yaani *jamrah* kubwa, za kati na ndogo.

yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alionesha njia sahihi ya kurusha mawe hayo, akiwaambia waumini kuchukua kokoto ndogo ndogo na kuzitupa kwa kutumia vidole vyao viwili.

Mahali Iliposhuka Adhabu

Wakati wa Hijja yake ya mwisho, Mtukufu Mtume ﷺ alipofika katika eneo la Batn-I Muahssir, lililopo kati ya Mina na Muzdalifah, aliharakisha mwendo wake.

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa nini uliongeza mwendo wako?" waliuliza Maswahaba kwa shauku.

"Pale ndipo mahali ambapo Mwenyezi Mungu aliliangamiza jeshi la tembo la Abrahah kwa kuwatuma kundi la ndege. Niliongeza kasi ya mwendo wangu kuhakikisha kuwa hakuna mtu atakayepata sehemu ya nakma hiyo." (Nawawi, Sharh-u Muslim, XVIII, 111; Ibn Qayyim, II, 255-256)

Kwa kweli wakati wa hi jja hakuna *waqfah* katika eneo hilo.

Athari za rehma au nakma huweza kuonekana hata kwenye vitu vinavyopatikana katika eneo husika. Kwa hiyo, mtu anatakiwa kutembelea sana maeneo yenye athari za rehma ya Mwenyezi Mungu kama vile Kaabah, misikiti au makumbusho ya watu wema, na pia ajiepushe kuwa katika maeneo yaliyojaa dhambi na uasi, ambayo nakma ya Mwenyezi Mungu hujidhihirisha.

Vilvile, vitu vinakumbwa na kanuni ya mvutano na taathira. Kwa mfano, gogo la mtende ambalo Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akikaa juu yake wakati wa kuzungumza na Waislamu lilijaa msisimko wa hali ya kiroho. Mtukufu Mtume ﷺ alipoanza kutoa hotuba akiwa amekaa sehemu nyingine, gogo hilo lilianza kulia.[351]

351. Bukhari, Manaqib, 25; Buyû, 32.

Ahadith zinazoelezea tukio hili ni *ahadithmutawaatir*, kwa maana kwamba usahihi wake hauna shaka.

Kuhusu hilo, Mawlana Rumi anasema: "Hewa, ardhi, maji na moto ni viumbe vya Mwenyezi Mungu na vinamtii. Havina uzima mbele yako lakini mimi nina uzima mbele ya Mwenyezi Mungu."

Baada ya kupita kwa haraka katika Bonde la Muhassir, Mtukufu Mtume ﷺ alifika kwenye *jamrah* kuu, ile ya Aqabah. Huko alitupa mawe baada ya mapambazuko siku ya kuchinja. Alipoanza kutupa mawe madogo madogo yenye ukubwa wa kuanzia kwenye kidole gumba mpaka kwenye kidole chake cha shahada, umati wa Waislamu nao ukafanya hivyo. Hata hivyo walianza kusongamana hali iliyosababisha wakanyagane. Mtukufu Mtume ﷺ aliwaita na kuwaambia: "Enyi watu…Msiuane! Mnapotupa mawe kwenye *jamrah*, tupeni mawe madogomadogo yaliyo baina ya vidole vyenu!" [352] (Ahmad, VI, 379)

Qudamah ibn Abdullah ؓ anakumbua hali ya Mtukufu Mtume ﷺ wakati wa kutupa mawe:

"Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akitupa mawe akiwa juu ya ngamia. Hakuwa akiwasukuma, kuwapiga vikumbo au kuwaambia watu wampishe!" (Ibn Majah, Manasiq, 66)

Baada ya kuchinja jumla ya ngamia sitini na tatu, kwa mikono yake mwenyewe, kila mmoja akiwa ni kwa ajili ya mwaka mmoja wa uhai wake, Mtukufu Mtume ﷺ alimkabidhi kisu Ali ؓ, akachinja waliobaki. Kisha Mtume ﷺ aliagiza kipande cha nyama kichukuliwe

352. Kwa bahati mbaya, leo hii tendo la 'kumpiga mawe shetani' halifanywi kwa hisia kutoka moyoni, kwa kutambua kuwa ni tendo la ibada, wakati lilitakiwa kufanywa katika namna ileile iliyofanywa na Nabii Ibrahimu ؑ wakati yeye mwenye alipompiga mawe shetani.

kutoka katika kila ngamia aliyechinjwa. Vipande vyote viliwekwa katika chungu kimoja vikapikwa, na kisha yeye na Ali ؓ wakala. Baadaye, Mtukufu Mtume ﷺ alimuagiza Ali ؓ kuwagawa kwa maskini zote nyama zilizobaki, pamoja na ngozi za ngamia waliochinjwa.

Baada ya hapo, Mtukufu Mtume ﷺ alimuita kinyozi na kuzikata nywele zake. Akasema: "Msizikate nywele za wanawake; bali zipunguzwe," akakataza kunyoa nywele zao. (Darimi, Manasiq, 63)

Anas ibn Malik ؓ anasimulia:

"Baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kumaliza kumpiga mawe shetani, alichinja na kuzikata nywele zake. Kisha akasema: "Msizikate nywele a wanaweke; bali zipunguzwe," akakataza wanawake kukata nywele zao au kunyoa vichwa vyao. (Darimi, Manasiq, 63)

Maelezo mengine yanatolewa na Anas Ibn Malik ؓ kwa upana zaidi:

"Baada ya kumpiga mawe shetani, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichinja wanyama wa sadaka na kukata nywele zake. Kinyozi alilishika shungi la nywele zake za upande wa kulia na kulikata. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuita Abu Talha na kumpa shungi hilo. Kisha kinyozi akalishika shungi la upande wa kushoto. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia, 'kata'; akalikata. Shungi hilo nalo akampa Abu Talha na kumwambia, 'zigawanye miongoni mwa watu!'" (Muslim, Hajj, 323-326; Bukhari, Wudu, 33)

Wakati nywele za pembezoni za Mtume ﷺ zilipokatwa, Khalid ibn Walid ؓ alisisitiza kuwa apewe nywele hizo. "Usimpendekeze mwingine zaidi yangu katika hili…wazazi wangu wawe fidia kwako!"[353] Baada ya kupewa nywele hizo alizotamani kuzipata, alizipanguza usoni mwake na kuziweka kuziweka upande wa mbele

353. Wakati huo huo, Abu Bakr ؓ alikuwa akitazama kwa mshangao, akilinganisha hali ya Khalid ؓ katika Vita vya Uhud, Khandak na Hudaybiya na haya aliyokuwa akiyafanya sasa. (Ibn Saad, II, 174)

chini kilemba chake. Alipofanya hivyo, kila adui aliyekabiliana naye alimshinda.

"Kila nilipozielekeza kwenye eneo husika nilikuwa nikilitwaa!" alisema Khalid ﷺ.[354] (Waqidi, III, 1108; Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, II, 111)

Kabla ya swala ya adhuhuri siku ya kwanza ya *eid'ul-adha*, Mtukufu Mtume ﷺ alimpanda ngamia wake na kuelekea kwenye Kaabah kufanya twawaafu ya *ifada*. Baada ya kumaliza, akaswali swala ya adhuhuri. Kisha aliekea kwenye kisima cha maji ya zamzam. Usiku ulikuwa unakaribia kuingia ndipo akaanza safarai ya kurudi Mina, ambapo alitakuwa kukaa siku na mikesha ya

354. Hikmet Atan anaelezea tukio kama hilo la Baraka zilizopatikana kupitia nywele na ndevu za Mtukufu Mtume ﷺ:
"Mwaka 1983 nilimsikia Ali Yücel Efendi akielezea tukio lifuatalo. 'Nilipokuwa imam katika Msikiti Mkuu wa Suluova, imam mwingine kutoka katika kijiji cha jirani alikuja na kuniambia, 'Kuna kitu ambacho kimetokea ambacho sikukielewa vizuri', alisema wakati akianza kunisimulia.
"Hivi karibuni, watu fulani walikuja kutoka kwenye kijiji cha jirani walinijia kwenye kijiji nilichokuwa nikiongoza kama imam wakiwa na idadi kadhaa ya vitabu. 'Baba yetu amefariki dunia na ametuachia vitu hivi,' walisema. Lakini hatuwezi kuvisoma. Wewe ni mwanazuoni, unaweza kufaidika na vitabu hivi. Hivyo tumefikiria tukupatie vitabu hivi kama zawadi.' Nilivichukua na kwenda navyo nyumbani. Kisha nilikaa mbele ya stovu, ambalo lilikuwa likiwaka sana, na kuanza kuchunguza vitabu hivyo. Ndani ya vitabu hivyo kulikuwa na barua na bahasha kadhaa za imam huyo aliyefariki. Niliona kuwa zilikuwa ni barua binafsi na kuamua kuzikusanya na kuzitupa ndani ya stovu lililokuwa likiwaka sana mbele yangu. Lakini nilivyofanya hivyo, ghafla likalipuka na kuzima. Nilikimbilia nje nikiwa mwenye woga. Nilikaa huko mpaka nilipopata nguvu na ujasiri wa kurudi ndani."
Akaendelea Ali Efendi, "Hivyo nikamwambia *hodja* kuwa ndani ya bahasha moja kulikuwa na ncha ya ndevu za Mtukufu Mtume ﷺ."
Baada ya muda, nilimuangalia *hodja* tena, naye akaniuliza moja kwa moja, "Ulijuaje kuwa katika moja ya bahasha zile kulikuwa na ncha ya ndevu za Mtukufu Mtume ﷺ? Watu walionipa vitabu hivyo walirejea tena na kuniambia 'Wakati ule hatukujua kuwa kuna ncha ya ndevu za Mtukufu Mtume ﷺ katika bahasha hizo. Unaweza kuturejeshea?'"

tashriq. Hata hivyo, nyakati za jioni aliendelea na ziara zake za kawaida za kuitembelea Kaabah.

Baada ya siku ya kuchinja,wakati wa mchana wa siku ya kwanza na ya pili ya *tashriq*, Mtukufu Mtume ﷺ alitembea kwa mguu kwenda kwenye *jamrah* ya kwanza jirani na Msikiti wa Mina. Katika siku ya mwisho ya *tashriq*, alitupa *jamrah* yake ya tatu na ya mwisho, kisha akaondoka Mina na kuelekea Muhassab[355] wakati wa alasiri. Mtukufu Mtume ﷺ alipogundua kuwa Waumini walikuwa wakitaka kutawanyika na kuondoka Muhassab kwa kupita njia zao wenyewe, akatangaza, "Msiondoke mpaka mfike kwenye Kaabah!" (Darimi, Manasiq, 85)

Baada ya hapo Mtukufu Mtume ﷺ alitangaza kuwa kutakuwa na suala la kuizunguka Kaaba kwa mara ya mwisho kabla ya swala ya alfajiri katika siku ya kumi na nne ya Dhil-hijjah. Ni katika kipindi hicho ambapo mtu mmoja alikua na kuuliza swali kuhusu kubaki Makka. Mtume ﷺ alijibu kuwa: "Hatutabaki Makka. Wale waliokuja kutoka nje ya Makka kufanya ibada ya Hijja, muda wao wa kubaki hapa ni siku tatu." (Ahmad, IV, 339)

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiamiliana na Nyumba hii Tukufu kwa heshima ya hali ya juu. Kama akitaka kula au kukidhi haja fulani, alikuwa akitoka katika eneo hilo na kwenda sehemu ya mbali. Akihofia kuwa panaweza kutokea uchovu au ulegevu katika kuonesha heshima yake kwa Kaabah, alikuwa hakai hapo kwa muda zaidi. Aidha, kuwa katika eneo linguine huku moyo wako ukiwa umeshikamana na Kaabah ni bora kuliko kukaa katika viunga vya Kaabah huku ukipatazama kama sehemu nyingine tu, huku ukien-

355. Eneo la Muhassab liko baina ya Mina na Makka, jirani zaidi na Mina. Eneo hilo ndio mahali ambapo viongozi wa Maqurayshi walifanya maamuzi ya kuwawekea vikwazo Waislamu hapo zamani. Mtukufu Mtume ﷺ alipofika Muhassab alilikumbuka eneo hilo. (Bukhari, Hajj, 45)

delea kutoiheshimu na kushughulishwa na raghba na tamaa ya kurudi nyumbani au kwenda sehemu nyingine.

Baada ya kutekeleza ibada ya kuizunguka Kaaba kwa mara ya mwisho, Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba walianza safari ya kurejea Madina. (Bukhari, Hajj, 21, 70, 128; Muslim, Haj, 147; Ibn Majah, Manasiq, 84)

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa ameitimiza neema Yake na kuikamilisha dini Yake, sasa ulikuwa umewadia wakati wa mtengano na muungano mkubwa kuliko yote.

MWAKA WA KUMI NA MOJA WA HIJRA

Muungano na Mtengano Mkubwa: Safari Kuu ya Kuelekea kwa 'Rafiki wa Juu kabisa'

Kiunganishi cha kwanza na cha mwisho katika nyororo ya mitume, Nabii Muhammad Mustafa ﷺ, Nuru ya viumbe, rehma kwa walimwengu wote, alishambuliwa na homa mara tu baada ya kurejea kutoka kwenye Hija ya Mwisho. Homa hiyo ilionesha kuwa ni maradhi ambayo yangemteganisha na *ummah* wake na kumuunganisha na *Rafiq'ul-A'la*, Rafiki wa Juu kabisa; muungano ambao alikuwa akiusubiri kwa kipindi chote cha uhai wake. Akiwa ametambua kuwa muda wake ulikuwa umekaribia, hususan baada ya kuteremshwa *Surah* an-Nasr, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akijiandaa kwa safari ya mwisho, kuwaaga watu wote, walio hai na waliokufa, kwa namna ya ishara. Siku moja kabla ya kushikwa na maradhi, alienda kwenye makaburi ya Jannat'ul-Baqi, akayatamazama makaburi na kuomba: "Mola wangu Mtukufu! Usiwanyime rehma zako wale waliolala hapa!" (Ahmad, III, 489)

Baada ya kurejea kutoka makaburini, alipanda juu ya *minbar* ya msikiti na kuwahutubia Maswahaba katika namna iliyoonekama kama kuwaaga:

"Nitawatangulia kufika kwenye Chemchem ya Kawthar na nitakutana nanyi huko! Makutano yetu ni kwenye chemichemi hiyo. Sasa hivi ninaiona! Nitatoa ushuhuda kwa niaba yenu! Sasa

hivi nimepewa hazina za ardhi na funguo zake. Sina hofu ya kuwa mtarejea kwenye ukafiri baada yangu! Bali ninachohofia ni kuzama katika tamaa ya dunia na kuhusudiana ninyi kwa nyinyi, mkauana na kuangamia kama walivyoangamia wale waliokuwa kabla yenu!" (Bukhari, Janaiz, 73; Muslim, Fadail, 31)

Baada ya kushuka kwenye *minbar*, Mtukufu Mtume ﷺ alielekea nyumbani kwake, akiwa amechoka. Ugonjwa ulizidi siku hadi siku. Maradhi yalipomzidia sana, Mtukufu Mtume ﷺ aliwaomba ruhusa wake zake amalizie siku zake zilizobaki katika nyumba ya bibi Aisha ؓ. (Bukhari, Tibb, 22; Ahmad, VI, 34, 38; Balazuri, I, 545)

Hapo zamani Mtukufu Mtume ﷺ hakuwahi kupatwa na maradhi mazito kama hayo. Maisha matakatifu na safi aliyokuwa akiishi ni maisha ambayo yalimuweka mbali na maradhi yote. Lakini majukumu makubwa ya utume[356] ambayo ni mazito sana kupita uwezo wa kawaida wa mwanadamu, ambayo alikuwa ameyabeba kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu na vitendo viovu na vya shari alivyokumbana navyo kutoka kwa maadui zake, yote hayo yaliuchosaha mwili wake. Yote hayo yaliweza kusababisha mwili wake upatwe na maradhi.

Kwa upande mwingine, maradhi hayo yangemuinua kwenye daraja ya juu na nafasi kubwa. Athari ya sumu aliyoionja katika nyama aliyopewa wakati wa vita ya Khaybar nayo ilikuwa na nafasi

356. Wakati wa kupokea Wahyi (Ufunuo), mwili wa Mtukufu Mtume ﷺ huwa mzito sana. Kwa mfano, akiwa juu ya ngamia, basi miguu ya ngamia huyo ingepinda kiasi kwamba watazamaji wangeanza kuhofia kuwa miguu hiyo itavunjika, na hivyo humlazimu ngamia kupiga papo hapo. (Ahmad, II, 176; VI, 445; Ibn Saad, I, 197) Zayd ibn Thabit ؓ anasema, "Siku moja nilikuwa nimekaa jirani na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (.a.w). Kwa sababu ya umati wa watu, magoti yake yaliegemea juu ya magoti yangu kidogo. Ghafla, alianza kupokea Wahyi. Wallah, sikuwahi kuona kitu kizito kama magoti yake. Kabla goti langu halijakandamizwa, nilidhani ni suala la muda mfupi tu." (Ahmad, V, 190-191)

kubwa katika maradhi haya. Wakati maradhi hayo yalipokuwa yakishtadi, Mtukufu Mtume ﷺ alimwambia Aisha رضي الله عنها: "Ewe Aisha, nimekuwa nikihisi maumivu ya sumu iliyowekwa katika nyama niliyoionja wakati wa vita ya Khaybar; na sasa ninahisi maumivu makali ya vena katika moyo wangu." (Bukhari, Maghazi, 83)

Vivyo hivyo, Anas ibn Malik رضي الله عنه ameripotiwa akisema: "Nilikuwa nikiona aalama na athari ya sumu hii kwenye kidakatonge chake." (Muslim, Salam, 45)

Kwa sababu ya sumu, Mtukufu Mtume ﷺ, Nuru ya Ulimwengu, alikufa akiwa shahidi; na sasa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye alikuwa ameshampa heshima ya utume, alikuwa akimpa Baraka ya kifo cha kishahidi. (Ibn Hisham, III, 390; Waqidi, II, 678-679; Haythami, VI, 153)

Joto la homa lilikuwa kali mno kiasi kwamba lilikuwa likimfanya atoke jasho mfululizo; ilikuwa kama maji yanayomiminika kutoka kwenye chupa ya maji iliyotundikwa. Abu Said al-Khudri رضي الله عنه, ambaye alimtembelea, alishikwa na fazaa na kusema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Joto lililoje mwilini mwako." Akaendelea kusimulia:

"Niliuweka mkono wangu juu ya mwili wake. Nılıweza kuhisi joto la homa yake mpaka juu ya blanketi lake. Una homa kali sana ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', nilisema, naye akajibu, 'Sisi (Mitume) tuko kama hivyo. Masaibu hutukuta kwa wingi lakini thawabu zake pia ni nyingi.'

Nikamuuliza, 'Ni watu gani wanaokumbwa zaidi ya masaibu, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?'

'Mitume', alisema.

'Kisha?'

'Watu wema', alijibu na kuongeza, 'miongoni mwao kuna wanakutana na masaibu kiasi kwamba hawawezi kupata chochote cha kujistiri isipokuwa vazi la sufu. Hufurahia masaibu kama wanavyofurahia neema.'" (Ibn Majah, Fitan, 23)

Katika nyakati za mwisho, uzito wa maradhi haukumruhusu kuungana na swala ya *jamaah*. Alimteua Abu Bakr ﷺ kuwaongoza Maswahaba katika swala. Siku moja alipopata nafuu alitoa Masjid, mbele ya Maswahaba, akaawambia:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa mja Wake hiari ya kuchagua dunia na mapambo yake au Neema na Baraka za kwenda mbele Yake…na mja huyo amechagua neema za kwenda mbele Yake!"

Papo hapo Abu Bakr ﷺ akabaini kuwa maneno yaliyotamkwa na Mtukufu Mtume ﷺ yalikuwa maneno ya kuwaaga.Huzunı ilimtamalaki. Alihisi kuvunjika moyo na kulia, akasema huku akigugumia, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wazazi wetu wawe fidia kwa ajili yako! Tuko tayarı kuzitoa nafsi zetu, wazazi wetu, watoto wetu na chochote kile kwa ajili yako!" (Ahmad, III, 91)

Katika maswahaba waliokuwepo mahali hapo hakuna aliyeweza kuielewa maana ya ndani ya maneno ya Mtume ﷺ, isipokuwa Abu Bakr ﷺ, swahaba aliyepewa sifa na Qur'an Tukufu kama 'wa pili katika wawili' ndani ya pango la Thawr.

İmeripotiwa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ aliwahi kusema, "Nimeingiza moyoni mwa Abu Bakr chochote kilichomo ndani ya moyo wangu."

Maswahaba walipomuona sahibu wa Mtukufu Mtume ﷺ akilia, walishtuka na kuanza kuulizana, "Mtume wa Mwenyezi Mungu amemzungumzia mtu fulani mwema anayetaka kurudi kwa Mola wake, kwa nini Abu Bakr analia?" (Bukhari, Salat, 80)

Kwa hakika, moyo laini wa Abu Bakr رضي الله عنه ulikuwa umehisi mtengano mkubwa uliokuwa ukionekana na akaanza kulia kama filimbi ya mwanzi inayolalama kutokana na kutengana na shina lake. Hali ya Mtukufu Mtume ﷺ ilipozidi kuwa mbaya, Maswahaba wengine nao pia wakaanza kûhisi ishara ya utengano mkubwa kabisa kuliko utengano wote, ambao sasa muda wowote ungetokea. Huzuni nzito iliwatamalaki *Ansar* na *Muhajirun*.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa nini usiombe dua ili hali ya afya yako irejee?" baadhi ya Maswahaba walitoa wazo. Lakini, Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye mpaka wakati huo, alikuwa na mazoe ya kuomba dua ya ustawi wa afya yake, mara hii alikataa kufanya hivyo.

Aisha رضي الله عنها anasema:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa akiumwa, alikuwa akisoma surah al-Falaq na An-Nas, akapuliza mikononi mwake na kisha kujipangusa mwili mzima. Maradhi yake yliposhtadi, nilianza kumfanyia hivyo; nikamsomea sura hizo, nikapulizia mikononi mwangu na kisha kumpangusa mwili wake wote. Pia nilisoma dua iliyowahi kusomwa na Jibril عليه السلام pindi Mtume ﷺ alipoumwa, ambayo ni, 'Ewe Mola wa watu! Uponye ugonjwa huu! Hakika ponyo iko mikononi Mwako! Hakuna awezaye kutoa ponyo isipokuwa Wewe! Nipe ponyo ambayo haitaacha mabaki yoyote ya maradhi!' Lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alinigeukia na kusema, 'Bora uondoe mikono yako, kwa maana dua yako haitafaa kitu…ninasubiri wakati wangu!" (Ahmad, VI, 260-261; Ibn Saad, II, 210)

Aisha ﵂ anaendelea kusema:

"Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuita binti yake, Fatimah. 'Karibu binti yangu', alisema pindi Fatmah alipowasili. Alimkalisha pembezoni mwake, kisha akamwambia kitu kwa sauti ya chini. Fatmah akaanza kulia. Kisha akamnong'oneza kitu kingine, ambacho kilimfanya mara hii afurahi na kutabasamu.

Sikuwahi kuona tabasamu likiandamana na machozi na machozi yakiandamana na furaha isipokuwa siku hiyo. Nilimuuliza Fatimah sababu ya hilo naye akasema, 'Alitaarifu kuwa atafariki kwa ugonjwa wake. Nikalia kusikia vile. Kisha akaniambia kuwa nitakuwa wa kwanza kuungana naye. Hilo ndilo lililonifanya nifurahi.'" (Bukhari, Maghazi, 83)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliweza kuwaswalisha Maswaba pale maradhi yalipokuwa yakipungua. Siku moja aliwahutubia Maswahaba, ambao walikuwa wamechanganywa na simanzi ya kusubiri muda wa kutengana na Mtukufu Mtume ﷺ. Aliwahutubia akisema:

"Enyi watu…

Ninasikia kuwa mnahofia kifo cha Mtume wenu! Lakini je kuna mtume yeyote kabla yangu aliyewahi kuishi na watu wake milele ili nami nizidi kuishi nanyi milele? Tambueni kuwa ninakwenda kukutana na Mola wangu; nanyi pia mtakutana naye! Bila shaka kila kitu hutokea kwa idhini na amri ya Mwenyezi Mungu.

Tambueni kuwa nitawatangulieni na kuwasubiri! Tambueni, makutano yetu kesho Akhera ni Bwawa la Kawthar. Mwenye kutaka kukutana nami kesho, aiondoshe mikono na ulimi wake katika dhambi. Enyi watu…dhambi husababisha mambo mazuri kubadilika na kuwa mabaya. Watu wanapokuwa wazuri, viongozi wao pia huwa wazuri…watu wanapokuwa wabaya, viongozi wao

pia huwa wabaya. Ninaapa kwa Allah Ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, wakati huu, nimesimama juu ya Bwawa hilo na ninaitazama kutoka mahali nilipo…"

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ alimgeukia Abu Bakr ؓ ambaye wakati huo alikuwa akilia:

"Usilie ewe Abu Bakr," alimsihi na kuendelea kuzungumza."Enyi watu…Hakuna ambaye amekuwa karimu kwa mali na urafiki kuliko Abu Bakr. Kama ningetakiwa kuchagua rafiki miongoni mwa wanadamu tofauti na Mola wangu, bila shaka ningemchagua Abu Bakr…Fungeni milango yote inayotazama Msikiti isipokuwa mlango wa Abu Bakr…ninaiona nuru ikitandaa juu ya mlango wake." (Bukhari, Salat, 80; Ibn Saad, II, 227)

"Enyi Maswahaba,

Hakika mimi ni mwanadamu. Hivyo huwenda nilivunja haki ya baadhi ya watu miongoni mwenu. Yeyote ambaye niliiumiza ngozi yake, basi hii hapa ngozi yangu! Aje kuchukua haki yake! Yeyote ambaye niliupiga mgongo wake, basi huu hapa mgongo wangu! Yule ambaye nilichukua mali zake bila kujua, basi mali zangu hizi hapa, aje kuchukua!

Ewe Mola wangu! Hakika mimi ni mwanadamu. Kama kuna Muislamu niliyemkaripia, niliyempiga au kumlaani, yafanye kuwa sababu ya wao kutakaswa, kupata thawabu na rehma Yako! (Ahmad, III, 400)

Mola wangu! Kama kuna Muislamu ambaye nilimkaripia, basi ifanye hiyo kuwa nyenzo ya kuwa karibu Nawe Siku ya Kiyama!" (Bukhari, Daawat, 34; Darimi, Muqaddimah, 14; Ibn Saad, II, 255; Tabari, Tarih, III, 191; Halabi, 463-464)

Kwa maneno haya Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiwaaga Maswahaba. Baada ya maneno haya, alielekea chumbani kwake akiwa

amechoka. Hiyo ndiyo iliyokuwa mara ya mwisho kwake kuwaswalisha Waumini. Baadaye, siku moja tu, aliweza kukusanya nguvu zake nakuswali nyuma ya Abu Bakr ﷺ.

Siku ya Jumatatu, tarehe 12 ya Rabiul-Awwal, Mtukufu Mtume ﷺ alihisi nafuu kidogo kwa mara ya mwisho, lakini hakuwa na nguvu kabisa za kutosha kujumuika na Maswahaba katika swala. Alinyanyua tu pazia iliyokuwa ikining'inia juu ya mlango wake, akawatazama kwa mara ya mwisho, Maswahaba waliokuwa wamesimama bega kwa bega, wakiswali swala ya Alfajiri nyuma ya Abu Bakr ﷺ. Akiwa amefurahishwa na hali aliyoiona, alitabasamau akionesha kuridhika. Ilikuwa kana kwamba uzito wa maradhi yake thakili uliondoka kwa muda, na kumpa nafasi ya kufurahia kuwaacha Waumini wema, huku akifurahi zaidi kwa kutekeleza kikamilifu jukumu alilokabidhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. (Bukhari, Maghazi, 83; Adhan, 46, 94; Muslim, Salat, 98; Nasai, Janaiz, 7)

Bibi Aisha ﷺ ambaye alishuhudia tukio hilo, anasema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akitabasamu alipowaona Maswahaba zake wakiswali. Sikuwahi kumuona akiwa mwenye furaha kubwa kama siku hiyo." (Ibn Hisham, IV, 331)

Mwenyezi Mungu alikuwa amempa Mtukufu Mtume ﷺ neema kubwa kuliko mtume yeyote aliyemtangulia. Aliushuhudia ushindi wa Ujumbe na Wito wake. Peninsula ya Arabia sasa ilikuwa imetakaswa dhidi ya masanamu, yaliyovunjwa na kubomolewa na watu wale wale ambao hapo kabla walikuwa wakisimama na kuyaabudu. Watu ambao, muda mfupi kabla, walikuwa wakiwazika mabinti zao wenyewe wakiwa hai, sasa walikuwa wamegeuka na kuwa nguzo za huruma, wakalelewa na mikono ya Mtukufu Mtume ﷺ, mlezi bora kabisa, ambaye aliwabadilisha kiasi cha kustaajabiwa na viumbe wote.

Asubuhi ya siku hiyo hiyo, aliliamuru jeshi la Maswahaba alililokuwa ameliandaa kabla, lianze safari yake. Jeshi hilo lilikuwa limechelewa kuondoka kutokana na maradhi yake. Alimteua kijana, Usama bin Zayd ؓ kuwa kamanda wa jeshi hilo, akamwambia: "Anza safari katikati ya asubuhi, kwa baraka za Allah!" (Waqidi, III, 1120)

Siku hiyo hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ alimwambia Bibi Aisha ؓ awape maskini dinar sita au saba alizokuwa amemkabidhi azitunze. Muda mfupi baadaye alimuuliza kama alikuwa amefanya alivyo-muagiza. Alipoana kuwa jambo hilo liliisumbua akili yake kutokana na kuwa na wasiwasi juu ya maradhi yake, aliomba aletewe hizo dinar. Baada ya kuzishika alisema:

"Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu, haifai kwake kwenda kukutana na Mola wake akiwa na dinari hizi mkononi mwake bila kuzitoa kuwapa masikini." Alizitoa dinar hizo kwa familia tano za Kiansari na kisha akasema, "Sasa najisikia faraja", kisha akapumzika kidogo. (Ahmad, VI, 104; Ibn Saad, II, 237-238)

Huku ni kujitolea kusikokuwa na kikomo!

Kwa upande wa *Ahl'ul- Bayt* aliwaambia maneno yafuatayo:

"Enyi watu, tahadharini na miale ya moto. Tabu zinaandamana na kufuatana kama mapande ya viza vya usiku! Nimehalalisha yale tu yaliyohalalishwa na Qur'an, Kitabu cha Allah, na kuharamisha yale tu yaliyoharamishwa ndani ya kitabu hicho!

Fatmah binti Muhammad, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Safiyyah! Tendeni amali zitakazompendeza Mwenyezi Mungu! Kwa maana mimi sitawaokoeni na adhabu yake (mpaka mtakapomtii na kumuabudu)!" (Ibn Saad, II, 256; Bukhari, Manaqib, 13-14; Muslim, Iman, 348-353)

"Zingatieni…zingatieni swala!" alisema Mtukufu Mtume ﷺ siku hiyo hiyo. "Watendeeni wema wale walio chini ya uangalizi wenu! Muogopeni Mwenyezi Mungu kuwahusu! Msiapuuze kuwapa mavazi na kuwalisha. Zungumzeni nao kwa upendo!" (Abu Dawud, Adab, 123 124/5156; Ibn Majah, Wasaya, 1)

Siku hiyo Mtukufu Mtume ﷺ alitumia *miswaq* yake kusukutua meno yake kwa hamasa na shauku kubwa. "Ni kana kwamba sikuwahi kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akitumia miswaq yake kwa uzuri zaidi kama siku hiyo", anasema Bibi Aisha ؓ. (Bukhari, Maghazi, 83; Ibn Saad, II, 261)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliweka chombo kidogo cha maji jirani yake. Mara kwa mara, alikuwa akiuingiza mkono wake ndani ya chombo hicho na kuulowanisha uso wake, na kusema, "*La ilaha ill-Allah*…hakika mauti yana uchungu wake." (Bukhari, Maghazi, 83)

Siku hiyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliomba dua ifuatayo:

"Mola wangu…Niingize katika rehma Zako! Nichukue Kwako ewe *Rafiq'ul-A'la*! Ewe Allah, niingize katika rehma Zako! Nijaalie rehma Yako! Nichukue Kwako ewe *Rafiq'ul-A'la*!" (Bukhari, Maghazi, 83; Ahmad, VI, 126)

Wakati mmoja siku hiyo, Mtume wa Rehma ﷺ, alimfariji bintiye Fatimah ؓ aliyekuwa na huzuni nzito, akamwambia: "Usilie, na nikifariki sema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea!" (Ibn Saad, II, 312)

Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia vivyo hivyo Maswahaba, akiwakumbusha aya iliyoteremka wakati wa vita ya Uhud pindi waliponyong'onyezwa na uvumi kuwa 'Muhammad alikuwa ameuawa':

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلاَّ رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىَ عَقِبَيْهِ فَلَن يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakaye geuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanao mshukuru." (Al-i Imran, 144)

Siku hiyo hiyo, Malaika wa Wahyi, Jibril عليه السلام alifika kwa Mtume ﷺ na kusema: "Amani na baraka ziwe juu yako, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hii ni mara yangu ya mwisho kukanyaga ardhini kwa ajili yako!" (Ibn Saad, II, 259)

Maneno yaliyokuwa yametamkwa mapema siku hiyo na Mtukufu Mtume ﷺ sasa yalikuwa yakitimia: "Roho ya mtume haiwezi kuchukuliwa mpaka aoneshwe mafikio yake Peponi! Kisha inabaki kwake sasa kuelekea huko!" (Bukhari, Maghazi, 83, 84; Ahmad, VI, 89)

Muda mfupi baada ya Jibril عليه السلام kuwasili alikuja Malaika ya Mauti عليه السلام. Aliomba idhini ya kuingia kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Baada ya kuruhusiwa, aliingia, akasimama na kusema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ewe Ahmad! Mwenyezi Mungu Mtukufu amenituma kwako, ameniamuru nisikilize kile utakachoniamuru. Ukitaka nitaichukua roho yako; kama la, nitaiacha!"

Jibril عليه السلام, ambaye bado alikuwa amekaa jirani nao wakati huo akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah, Mwenyezi Mungu ana shauku nawe!"

Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia Malaika wa Mauti ambaye alikuwa akisubiri jawabu, "Yaliyo kwa Mwenyezi Mungu ni bora n ani yenye kudumu! Hivyo, Ewe Malaika wa Mauti, fanya uliloamrishwa kufanya; ichukue roho yangu!" (Ibn Saad, II, 259; Haythami, IX, 34-35;Balazuri, I, 565)

Kisha, kwa mara ya mwisho, aliutumbukiza mkono wake ndani ya kile chombo cha maj, akaulowesha uso wake. Sasa alikuwa ameanza safari ya kuelekea kwa Mola wake na kuyaacha maisha yake ya dunia yaliyotawaliwa na kumtumikia Mwenyezi Mungu. Alitamka maneno ya *tawhid*, akasema:

"Mola wangu! Rafiq'ul-A'la! Rafiq'ul-A'la!" na kuikabidhi roho yake tukufu. Mkono ambao alikuwa ameutumia kuulowanisha uso wake ulikuwa umeteremka ndani ya chombo cha maji. (Bukhari, Maghazi, 83)

Aya ılıyoteremka miaka mingi kabla:

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُم مَّيِّتُونَ

"Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa." (az-Zumar, 30) sasa ilikuwa imetimia.

Ewe Mwenyezi Mungu…teremsha rehma na amani kwa Mtukufu Mtume wetu Muhammad Mustafa ﷺ, kizazi chake na Maswahab zake; wajaalie Baraka na amani ya milele!

Mtukufu Mtume ﷺ alipokufa, watu wa familia yake walijikuta wakizama katika mafuriko ya machozi ya huzuni. Wakati huo huo, walisikia sauti yenye simanzi ikiwafariji, licha ya kutomuona mtoaji wa buriani hiyo.

"Amani na Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu", ilisema sauti hiyo.

Baada ya Ahl'ul-Bayt kuitikia, sauti hiyo hiyo ikasikika tena, mara hii ikitoa mwangwi wa aya isemayo:

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَمَن زُحْزِحَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَوَما الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلاَّ مَتَاعُ الْغُرُورِ

"Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu." (Al-i Imran, 185) Mwangwi huo ulifuatiwa na sauti ya faraja ikisema:

"Tambueni kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuna faraja kwa kila msiba, mrithi kwa kila marehemu na malipo kwa kila aliyekufa! Shikamaneni na Mwenyezi Mungu na mtarajie mema kutoka Kwake! Hakika aliyekumbwa na msiba ni Yule aliyekosa thawabu (Akhera)! Amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu!" (Ibn Saad, II, 259)

Ibn Omar ﵁ anathibitisha, "Ahl'ul-Bayt wote, watu waliokuwa msikitini na wale waliokuwa wamesimama mtaani waliiskia sauti hiyo." (Balazuri, I, 564) Ali ﵁ anasema kuwa ilikuwa sauti ya Khidr ﵁. (Ibn Saad, II, 260)

Bibi Fatmah ﵂ alizidiwa na huzuni kutokana na kuondokewa na baba yake kiasi cha kusema, "Kuondoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ni msiba ambao lau ungetupwa juu ya mchana, basi ungegeuka kuwa usiku." (Diyarbakri, II, 173)

Baada ya hapo, bibi Fatimah ﵂ hakuonekana kutabasamu hata kidogo kwa kipindi cha miezi sita aliyoishi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume ﷺ. (Kâmil Mîras, Tecrîd Tercemesi, XI, 25-26)

Baada ya maradhi thakili yaliyodumu kwa siku kumi na tatu baada ya kurejea Madina, siku ya Jumatatu, tarehe 12, mwezi wa Rabiulawwal, mwaka wa 11 wa Hijrah (8 Juni, 632), milango ya mbingu ilifunguliwa kwa ajili ya Mtukufu Mtume ﷺ, kipenzi cha Mwenyezi Mungu, ambaye kwa kupita katika milango hiyo alielekea kwa Rafiki Mkuu Kabisa, Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ingawa hawakuweza kuondokana kabisa na hisia za simanzi, Maswahaba walihisi kuwa sasa maana halisi ya maisha ilikuwa imetoweka. Baada ya siku hiyo, Bilal Habashi ؓ, Muadhini wa Mtume ﷺ, hakuweza tena kutoa adhana kwa sauti ile maridhawa iliyokuwa ikizizma angani. Maswahaba kila walipomsisitiza kufanya hivyo, Bilal ؓ alikuwa akijaribu kuelekea msikitini; lakini anaposhindwa kumuona Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amesimama mbele ya msikiti kama ilivyokuwa kawaida yake, alikuwa akishindwa kustahmili, akipoteza sauti yake, akanyong'onyea na kurudi bila kutoa adhana. Katika kujaribu kuuondosha moto wa upendo moyoni mwake, aliondoka madina akaelekea Damascus, Syria. Siku moja alimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ndotoni.

"Mpaka lini utaendelea kunitenga, ewe Bilal?" alimwambia. "Je, haujafika muda sasa wa kunitembelea?"

Ghafla, Bilal ؓ aliamka akiwa amedhikika. Bila kuchelewa, alifunga safari, mara hii akielekea mjini Madina kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume ﷺ. Wakati akiwa amesimama mbele ya kaburi la Mtume ﷺ huku akilia, mara Hassan na Hussain ؓ waliwasili. Akiwa amefurahi kuwaona wajukuu wapendwa wa Mtukufu Mtume ﷺ, Bilal ؓ aliwakumbatia kwa upendo.

"Ewe Bilal, tungependa kukusikia ukitoa adhana", walimsihi naye akawakubalia ombi lao. Adhana yake iliutikisa mji wa Madina. Alipofika kwenye kipengele cha *Ashadu anna Muhammadan Rasulullah*, wanaume na wanawake wote wa mji huo waliingia mitaani

na kuanza kuwagika msikitini, wakidhani kuwa Mtukufu Mtume ﷺ amefufuka. Tangu kufariki kwa Mtukufu Mtume ﷺ, hakuna siku ambayo wakazi wa Madina walilia sana kama siku hiyo. (Ibn Athir, Usd'ul-Ghabah, I, 244-245; Dhahabi, Siyar, I, 357-358)

Anas ibn Malik رضي الله عنه anasema:

"Sikuwahi kuona siku yenye nuru na maridhawa kuliko siku Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr walipowasili Madina. Vilevile nilishuhudia siku Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyofariki dunia. Sikuwahi kuona siku yenye giza, mbaya na yenye kutisha kama siku hiyo. Kila kitu katika mji wa Madina kilichokuwa na nuru pindi Mtume ﷺ alipowasili Madina kilibadilika na kuwa na giza kwa kifo chake! Tulikuwa na uzito kuuzika mwili wake mtukufu tukiwa hatuamini sana kuwa kweli alikuwa amefariki dunia!" (Ahmad, III, 221, 268, 287; Tirmidhi, Manaqib, 1/3618; Darimi, Muqaddimah, 14)

Shida na masaibu yote ambayo Waislamu wangeenda kukutana nayo yasingekuwa na athari yoyote. Kadhalika Mtukufu Mtume ﷺ anasema, "Waislamu wanapopatwa na shida ya aina moja au nyingine watafakari na watafute faraja katika shida iliyowapata nilipofariki dunia na waendelee kufanya subira." (Muwatta', Janaiz, 41; Darimi, Muqaddimah, 14)

Vile vile, Mtukufu Mtume ﷺ anasema:

"Afya yangu ina manufaa kwenu: mnazungumza nami na ninazungumza nanyi! Kifo change pia kina manufaa kwenu: nitaoneshwa matendo yenu; nitakapoyaona matendo yenu mema humshukuru Mwenyezi Mungu na nitakapoyaona matendo yenu mabaya, nitawaombea maghfira kwa Mwenyezi Mungu." (Haythami, IX, 24)

Bibi Aisha ﵂ anaripoti kuwa Mtukufu Mtume ﷺ aliutumia muda wake wa mwisho katika kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu, kufanya toba na kumshukuru. Mara kwa mara alikuwa akirudiarudia kusoma: "*Subhanallahi wa bi-hamdihi, astaghfirullaha wa atubu ilayh*: Utakasifu na himidi ni za Mwenyezi Mungu, ninamuomba msamaha na kutubia Kwake." (Bukhari, Adhan, 123, 139; Muslim, Salat, 218-220; Ahmad, I, 393; Ibn Saad, II, 192)

Mtume ﷺ alikuwa na alama maalumu katikati ya mabega yake, inayothibitisha utume wake. Maswahaba walikuwa wakitamani sana kuibusu. Baada ya mauti yake, alama hiyo haikubadilika na hivyo Maswahaba wakaanza kuwa na shaka iwapo kweli amefariki dunia. Asma bint Umays ﵂, ambaye alikuwa ndugu wa Mtukufu Mtume ﷺ, aliutazama muhuri huo wa utume. Alipoona kuwa haionekani akaamini kuwa Mtume ﷺ alikuwa amefariki dunia.

Mtukufu Mtume ﷺ hakuacha hata sarafu moja ya dirham au mtumwa. Vitu pekee alivyoviacha ni nyumbu mweupe aliyekuwa akimtumia kwa usafiri, upanga na ardhi katika maeneo ya Khaybar na Fadak, ambayo tayari alikuwa ameshayakabidhi kama amana kwa ajili ya wasafiri.

Mtukufu Mtume ﷺ alifariki dunia siku ya Jumatatu na kuzikwa siku iliyofuata. Maswahaba walimswalia pasipo jamaah, bila imamu. Baadhi walishauri azikwe jirani na *mimbar* ya msikiti. Wengine wakashauri azikwe katika makaburi ya Baqi. Majadiliano yaliisha kwa Abu Bakr ﵁ kusema, "Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema, 'Kila mtume huzikwa mahali alipofia.'" Hivyo wakaanza kuchimba mahali alipofia.

Wakati wakijiandaa kuuosha mwili wa Mtume ﷺ walijaribu kumvua kanzu, wakashtushwa na sauti iliyowaamuru kutomvua kanzu yake! Hivyo walimuosha bila kumvua kanzu.

Abdullah ibn Masud ﷺ anasema:

"Mtume wetu mpendwa alitutaarifu kuhusu kifo chake mwezi mmoja kabla. 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nani atakayeongoza swala yako ya jeneza?' tulimuuliza huku tukibubujikwa na machozi. Naye alianzakububujikwa na machozi, akasema, 'Allah awape rehma Zake Nyote! Awalipe kheri kwa ajili ya Mtume Wake! Baada ya kuniosha na kunivika sanda, mtanilaza kwenye godoro langu pale, jirani na kaburi langu katika nyumba hii! Kisha mtakiacha chumba hiki kwa muda, kwa maana marafiki zangu wawili, Jibril na Mikail ndio watakaoanza kuniswalia; kisha Israfil na Malaika wa Mauti akiwa pamoja na jeshi la malaika pembezoni mwake wataniswalia. Baada ya hapo mtaingia chumbani kwa makundi makundi; niswalieni na mnitakie rehma na amani. Lakini msinisumbue kwa kunisifu au kupiga mayowe na kelele.

Kisha wanaume katika familia yangu wataanza kuniswalia na kisha wanawake. Mnaweza kufanya hivyo baadaye.

Pelekeni salamu kwa Maswahaba zangu ambao hawapo hapa! Pelekeni salamu zangu kwa wale wote watakaonifuata, katika Dini yangu, mpaka Siku ya Mwisho!" (Hayhtami, IX, 25; Ibn Saad, ii, 256-257)

Kila kitu kilifanywa kama ilivyousiwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Ali ﷺ alitangaza, "Mtu yeyote asiwe na shaka kuona kwamba hakuna imam anayeongoza swala ya kumswalia Mtume ﷺ. Yeye ni imamu wenu katika umauti wake, akama alivyokuwa wakati wa uhai wake!" Kisha akasimama mbele ya mwili wa Mtume ﷺ na kusema:

"Rehma, amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!

Ewe Mwenyezi Mungu! Shuhudia kuwa alifikisha yale uliyomteremshia, akaunasihi umma wake na kupigana katika njia Yako mpaka ulipoinyanyua Dini Yako na kutimiza ahadi Yako!

Ewe Allah! Tujaalie kuwa miongoni mwa wale wanaomfuata katika yale Uliyomteremshia! Tupe subira katika njia hii baada yake pia! Tujaalie tuungane naye!" Sauti za *amiin* zilisikikakutoka kwa kundi la waumini alipokuwa akiomba dua hii. (Ibn Saad, II, 291)

Baraka iliyoje kwa ardhi kumhifadhi kiumbe bora kabisa ndani ya tumbo lake.

Dini ikiwa imekamilika na ushuhuda ukiwa umetolewa na Maswahaba wote kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba Mtume Wake alikuwa wametimiza wajibu wake katika kufikisha kile alichotumwa, sasa Mtume ﷺ, Nuru ya Ulimwengu, aliitwa kwenda kwenye ulimwengu wa milele.

Sasa anausubiri Umma wake kwenye Uwanja wa ufufuo, kwenye *sirat*, kwenye Birika la *Kawthar*.

Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, uwe mwombezi wetu!

Aliupa heshima ulimwengu kwa kuzaliwa Siku ya Jumatatu, tarehe 12 ya Rabiulawwal na pia alipewa utume siku ya Jumatatu mwezi kama huo. Abu Qatadah رضي الله عنه anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliulizwa kuhusu kufunga siku ya Jumatatu. Akajibu, 'Hiyo ni siku niliyozaliwa na ndiyo siku niliyotumwa kama mtume.'" (Muslim, Siyam, 197-198)

Vilevile, tarehe 12 ya mwezi wa Rabiulawwal aliwasili Madina na kuweka msingi wa mamlaka ya Kiislamu yatakayodumu mpaka Siku ya mwisho. Hivyo, tarehe 12 ya mwezi wa Rabiulawwal ndipo alipoondoka duniani kuelekea kwenye ulimwengu wa milele, ambapo atakuwa mwombezi kwa ummah wake.

Aziz Mahmud Hudayi –Mwenyezi Mungu amrehemu- anauelezea kwa namna ya ushairi uasi wa watu kwa kumtupa Mtukufu Mtume ﷺ:

Nani atakayetarajia utii wako ilhali wewe ni ulimwengu wa ghururi, je wewe siye?

Je wewe si Ulimwengu uliomchukua Muhammad Mustafa?

Huzuni iliyouteka Ulimwengu Wote

Mtukufu Mtume ﷺ alipofariki dunia, bibi Fatimah رضي الله عنها alilia na kuomboleza sana, akasema huku macho yake yakiwa yamejaa machozi, "Baba yangu kipenzi, ambaye hakuna aliye karibu kwa Mola Wake kama yeye! Baba yangu aliyeitika wito wa Mola wake! Baba yangu kipenzi ambaye nafasi yake ni Pepo ya *Firdaws*! Baba yangu kipenzi ambaye kwa kuondoka kwake tumemtambua Jibril!"

Baada ya Mtume ﷺ kuzikwa, Fatmah رضي الله عنها alimwambia Anas رضي الله عنه:

"Ilikuwaje nyoyo zenu zikawaruhusu kumwaga udongo juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" (Bukhari, Maghazi, 83; Darimi, Muqaddimah, 14)

Kutokana na staha, Anas رضي الله عنه hakujibu; lakini muonekano wa huzuni na majonzi machoni mwake vilieleza, "Hapana, ewe Fatimah, nyoyo zetu hazikuturuhusu, lakini tulizalazimisha nafsi zetu kutekeleza amri ya Mtume ﷺ!" (Kâmil Mîras, Tecrîd Tercemesi, XI, 25)

Waumini walikuwa wamejaa msikitini wakilia, ndipo Omar رضي الله عنه alipofika na kusema, "Sitaruhusu mtu kusema 'Muhammad ﷺ amekufa", alisema kwa sauti iliyojaa hasira, "atakayefanya hivyo nitamkata shingo yake kwa upanga wangu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ amezirai kama ilivyokuwa kwa Musa عليه السلام!" Aliendelea kutoa hotuba yake nzito, kiasi kwamba kinywa chake kilianza kutoa povu.

Mara Abu Bakr رضي الله عنه alipopata taarifa hizi zenye kuhuzunisha, alimpanda farasi wake haraka haraka na kufika Msikitini. Kitu cha

kwanza alichokifanya ni kuufunua uso wa Mtukufu Mtume ﷺ. Aliuinamia mwili wake, akalia na kumbusu kwenye paji la uso, na kisha akasema:

"Ninaapa kwa Allah, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amefariki dunia. Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea (*Inna lillahi wa inna ilayhi rajiun*). Wazazi wangu wawe fidia kwako! Ninashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu hatafanya uonje machungu ya mauti mara mbili! Umekufa mara moja na sasa umeipita hatua ya mauti! Ewe kipenzi change, hutakufa tena…" Kisha aliinama na kuubusu tena wajihi maridhawa wa Mtume ﷺ. Alikiinua tena kichwa chake na kulia, "Ewe rafiki yangu kipenzi!", akambusu tena na tena kwenye paji lake la uso.

"Hakika wewe ni mzuri katika umauti wako kama ulivyokuwa katika uhai wako! Uzuri ulioje, wa uhai na umauti wako!" alisema na kisha akaufunika uso wa Mtukufu Mtume ﷺ, akatoka kuelekea Msikitini. Wakati huo Omar ؓ bado alikuwa akiendelea na hotuba yake akiwataka waumini kukataa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amekufa.

"Ewe Omar, sasa waweza kukaa chini", Abu bakr ؓ alisema kumwambia Omar ؓ.

Kutokana na kutamalakiwa na simanzi nzito, Omar ؓ hakuwa na nia ya kukaa chini. Ni baada ya Abu Bakr ؓ kurudia tena kumshauri mara kadhaa ndipo Omar ؓ alipopata nguvu na kuweza kuketi. Kisha Abu Bakr ؓ akaanza kuzungumza:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu, alikuwa ameshamtaarifu Mtume Wake juu ya kifo akiwa bado yu hai. Naye akawataarifu kuwa muda utakapowadia nyinyi nyote mtakufa pia. Hakuna hata mmoja atakayekwepa kifo. Yule aliyekuwa akimuabudu Muhammad ﷺ atambue kwamba Muhammad ﷺ amekufa! Bali Yule anayemuabu-

du Mwenyezi Mungu, atambue kuwa Mwenyezi Mungu, yu hai, ni wa milele na hapatwi na umauti! Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ
انقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىَ عَقِبَيْهِ فَلَن
يَضُرَّ اللّٰهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللّٰهُ الشَّاكِرِينَ

'Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakaye geuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanao mshukuru." (Al-i Imran, 144)

Baada ya kukumbushwa aya hiyo, watu walianza kuukubali ukweli kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amefariki dunia. Alishtuka sana walipomsikia Abu Bakr ؓ akisoma aya hiyo kana kwamba hawakuwa na habari kwamba iliteremka miaka mingi iliyopita.

Baadaye Omar ؓ alikiri akisema,"Wallah, ilikuwa kana kwamba sikuwahi kuisikia aya hiyo. Nilipomsikia Abu Bakr ؓ akiisoma nilishtuka mno. Miguu yangu haikuweza kuhimili; ghafla magoti yangu yakanyong'onyea, nikaanguka chini!" (Ibn Saad, II, 266-272; Bukhari, Maghazi, 83; Haythami, IX, 32; Abdurrazzaq, V, 436)

Mara baada tu ya hotuba yenye kuumiza ya Abu Bakr ؓ, Omar ؓ aliekekea mahali ulipokuwa mwili wa Mtukufu Mtume ﷺ, akainama na kumbusu kwenye paji la uso. Macho yake yakitirirsha machozi, akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Wazazi wangu wawe fidia kwako! Gogo la mtende, ambalo ulikuwa ukiliegemea, lililia ulipoacha kukaa juu yake na likanyamaa ulipolishika kwa mkono wako… lakini sasa rafiki yako anastahiki kulia na kuhuzunikia utengano wako kuliko lile gogo!

Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wazazi wangu wawe fidia kwa ajili yako! Mola wako alisema:

مَّنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللّٰهَ

'Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Mwenyezi Mungu' (an-Nisa, 80). Amejaalia kukutii wewe kuwa ni sawa na kumtii Yeye, huku akilinyanyua jina lako kwenye daraja ya juu kabisa mbele Zake!

Wazazi wangu wawe fidia kwako, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Licha ya kukutuma kama mtume wa mwisho, aliunyanyua tena ubora wako kwenye daraja ya juu kabisa, kwa kupata kiapo cha utii kutoka kwa mitume wote waliokutangulia, ili wakuamini na kukunusuru!

Wazazi wangu wawe fidia kwako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Watu wa motoni, watakapokuwa wakiadhibiwa, watatamani lau wangekuwa na pamoja na wewe. Watasema:

يَا لَيْتَنَا أَطَعْنَا اللّٰهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا

'…Laiti tungeli mt'ii Mwenyezi Mungu, na tungeli mt'ii Mtume!' (al-Ahzab, 66). Hilo limeinyanyua thamani yako mbele ya Mwenyezi Mungu kwenye daraja ya juu kabisa!" (Kastallani, II, 492)

Akisimulia kumbukumbu zenye kuhuzunisha siku ambayo Mtukufu Mtume ﷺ alifariki dunia, Umm Salama ؓ anasema:

"Siku ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifariki dunia tulijikusanya pembezoni mwa mwili wake huku tukilia. Mwili wake mzuri bado ulikuwa ndani ya nyumba yetu na tulikuwa tukijifariji kwa kumtazama. Tuliposikia sauti za sululu tulianza kulia na kuomboleza; vivyo hivyo umati wa watu waliokuwa wakisubiri msikitini-walilia. Mji wa Madina ulitikiswa na sauti za mayowe. Tuliposikia sauti ya kusikitisha ya Bilal ؓ akitoa adhana na hasa alipofika kwenye *Ashadu anna Muhammadan Rasulullah*, simanzi zetu zilizidi na kuongezeka mara dufu. Watu walipoanza kuıngıa mahali lilipochimbwa kaburi, tuliwafungia mlango wasipate kuingia. Ilikuwa siku yenye uchungu sana! Baadaye ilikuwa kila tunapokuwa tumekumbana na shida nyingine, tulikuwa tukijikumbusha machungu na maumivu tuliyoyapata siku aliyokufa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na hivyo kutohisi kama kuna tabu imetupata." (Ibn Kathir, al-Bidayah, V, 256)

Kwa kuwa Maswahaba walimpenda sana kuliko mtu yeyote na kuliko chochote kile, walipata shida mno kutengana na Mtukufu Mtume ﷺ. Kuna wengi wao ambao hawakutamani kuishi tena bila yeye, kuwa na macho ambayo hayataweza kumuona tena au kuwa na masikio ambayo hayataweza kumsikia tena akizungumza. Kwa hakika Mtukufu Mtume ﷺ miaka mingi kabla alikuwa ameshatabiri ukiwa huu watakaoupata:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi ya Muhammad iko mikoni Mwake, itakuja siku ambayo hamtaniona tena. Mtatamani mno pamoja nanyi, kisha nitakuwa kipenzi kwenu na mwenye thamani machoni mwenu kuliko mtu yeyote katika familia zenu na mali zenu zote!" (Muslim, Fadail,142; Bukhari, Manaqib, 25)

Kila siku walikuwa wakiisubiri kwa hamu kwa matarajio ya kuungana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kufurahia kuwa pamoja naye milele.

Othman ﷺ anasimulia:

"Kama katika Maswahaba kuna mtu aliyeumizwa na kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, bila shaka mtu huyo ni mimi. Ni kweli, wengine nao waliumia sana. Kuna ambao walikumbwa na hali ya wasiwasi mzito baada ya kifo chake. Siku moja nilikuwa nimekaa chini ya mti, Omar ﷺ akapita mahali hapo na kunitolea salamu. Sikujua kabisa kama alikuwa amenitolea salamau, achilia mbali kumuona akipita. Omar alienda kwa Abu Bakr ﷺ na kumwambia, 'nilipita mahali alipokuwa amekaa Othman, nikamsalimia lakini hakunijibu. Je hilo sio jambo la kustaajabisha?'

Baadaye nikawaona wakija. Walinitolea salamu na kisha Abu Bakr akasema, 'Ndugu yako Omar amenijia na kunambia kuwa alikutolea salamu lakini wewe hukujibu. Kwa sababu gani?'

'Sijafanya kitu kama hicho' nilijibu, na hapohapo Omar akasisitiza kwa kusema, 'Wallah ulifanya!'

'Wallah, sikujua kama ulipita wala kunisalimia!' nilisema.

'Othman anasema kweli', Abu Bakr alihitimisha." (Ahmad, I, 6)

Muda mfupi baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kufariki dunia, Omar ﷺ alimshauri Abu Bakr ﷺ wamtembelee Umm Ayman ﷺ, kama Mtume ﷺ alivyokuwa akifanya wakati wa uhai wake. Hivyo wakamtembelea. Alipowaona, Umm Ayman ﷺ akaanza kulia.

"Kwa nini walia?" waliuliza. "Hujui kuwa neema ambazo Mwenyezi Mungu alimuandalia Mtume ﷺ ni bora kuliko dunia?"

"Hiyo sio sababu ya kilio changu", alijibu. "Ninajua kuwa neema na Baraka ambazo Mwenyezi Mungu amemuandalia Mtume

ﷺ ni bora kuliko dunia. Ninalia kwa sababu Ufunuo (Wahyi) umefikia kikomo." Hisia zake hizo ziliwafanya Abu Abakr na Omar ؓ kupatwa na mauimivu mazito, nao wakaanza kulia. (Muslim, Fadhaail'us-Sahabah, 103)

Miaka mingi baadaye, wakati wa ukhalifa wake, Omar ؓ alikuwa akipita katika mitaa ya mji wa Madina. Akaona mshumaa ukitoa mwanga kutoka kwenye nyumba moja. Alipoisogelea, akamuona mwanamke kikongwe ndani ya nyumba, akifuma sufu na wakati huo huo akisoma shairi:

"Amani ya watu wema iwe juu ya Muhammad ؓ…Ewe Muhammad, kwa huruma yako, kila nafsi inakuombea…ulikuwa ukiswali usiku na kulia wakati wa alfajiri…Mauti inazidi kuwakurubia wote siku hadi siku…Nyumba ya Akhera itaniunganisha nawe!"

Omar ؓ alikaa chini na kulia kwa muda. Kisha akagonga mlango.

"Ni nani huyo?" kikongwe huyo aliuliza.

"Ni Omar ibn Khattab."

"Omar anafanya nini usiku huu; anataka nini kwangu?", aliuliza akiwa na wasiwasi.

"Kwa mapenzi yakokwa Mwenyezi Mungu, tafadhali fungua mlango. Usiwe na wasiwasi!" Omar ؓ alimsihi, naye akafungua.

"Nisomee shairi ulililokuwa ukilisoma", alimsisitizia. Akaanza kusoma. Kabla hajafika kwenye msitari wa mwisho, Omar ؓ akamkatiza na kusema, "ninakuomba unijumuishe pia katika ushairi wako pia!"

Alibadilisha msitari wa mwisho ya shairi lake na kusomeka, "Nyumba ya Akhera itaniunganisha nawe mimi na Omar; Ewe Mwenyezi Mungu Mwenye kutoa maghfira, mpe Omar rehma

zako!" Kisha Omar ﷺ akaondoka, akiwa ameliwazika. (Ali al-Muttaqi, XII, 562/35762)

Anas ﷺ alikuwa akisema, "Hakuna hata usiku mmoja uliopita bila kumuona kipenzi changu (Mtume s.a.w) ndotoni", nakisha hulia. (Ibn Saad, VII, 20)

Maswaba walikuwa wakimuita Mtukufu Mtume ﷺ kwa sifa ya *habibi* (kipenzi changu) au *khalili* (rafiki yangu kipenzi), katika kuelezea na kuonesha upendo ghali waliokuwa nao kwake.

Kwa kumtakia rehma na amani Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, walikuwa akionesha upendo wao na mshikamano wao wa dhati kwake; lakini kumkumbuka kwako hakukuishia kwenye suala hilo la kumtakia rehma. Kushikamana kwao na njia yake, kuzitii sunnah zake, kuzitaja na kuzidhukuru mara kwa mara *ahadith* zake wakati wote, pamoja na matendo mengine mengi yaliyo mema, daima vili-udumisha na kuuendeleza upendo wao kwake.

Abu Dharr ﷺ anasema, "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba Mtume ﷺ alipofariki alituacha katika hali ambayo kama ndege angeruka angani na kutikisa mbawa zake angetukumbusha maneno yake. Kwa maana alisema, '…kila kitu kinachoweza kuwakurubisha na pepo na kuwaweka mbali na moto, kimesha-bainishwa.'" (Ahmad, V, 153, 162; Haythami, VIII, 263)

Katika Uislamu ni wajibu kwa Waislamu wote kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ kuliko mtu yeyote na kuliko chochote kile duniani, kuyatangauliza maamrisho yake na makatazo yake kabla ya matamanio yao na kushikamana na maneo na matendo yake yote bila khiyari.

USWAT'UL-HASANAH

Ruwaza bora Iliyokamilika

Katika viumbe vyote, ni mwanadamu pekee aliyepewa heshima ya kuchukua sehemu katika Majina yote ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sambamba na hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia mwanadamu uwezo wa kutenda mazuri na mabaya, mwelekeo na silika ya kuyaelekea mema na maovu.

Hivyo, lengo la dini ni kupunguza sifa hasi kuhusu nafsi ya mwanadamu mpaka kwenye kiwango cha kuziangamiza, jambo litakaloziinua sifa za kimaanawi kwenye kilele chake cha juu kabisa. Lakini ili lengo hilo lifanikiwe, wanadamu wanahitaji mfano halisi wanaoweza kuufuata; *uswat'ul-hasanah*, yaani mfano bora. Miongoni mwa hekma za kuletwa mitume mbalimbali iko katika ukweli kwamba wao ni mfano halisi ambao wanadamu wanaweza kuufuata. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ بِإِذْنِ اللَّهِ

"Na hatukumtuma Mtume yeyote ila at'iiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu…" (an-Nisa: 64)

Sifa hii inaonekana wazi na imepata makazi yake halisi kwa Mtukufu Mtume ﷺ, kama inavyothibitishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللّٰهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن
كَانَ يَرْجُو اللّٰهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللّٰهَ كَثِيراً

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." (Al-Ahzab: 21)

Mtume Muhamad Mustafa ﷺ ndio mtume na binadamu pekee ambaye historia ya maisha yake imeandikwa kwa upana na kwa undani. Kutoka zama hadi zama, kila neno, tendo na hisia za Mtukufu Mtume ﷺ vimeandikwa kwa ukamilifu na kuwa pambo la heshima katika historia. Qur'an Tukufu inatuambia:

وَإِنَّكَ لَعَلى خُلُقٍ عَظِيمٍ

"Na hakika wewe una tabia tukufu." (al-Qalam: 4)

Maisha na tabia tukufu ya Mtume ﷺ ni kilele cha mwenendo wa mwanadamu, hata mwelekeo wa tabia zake za nje zinaweza kueleweka na kujionesha vizuri kwa mwanadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimleta kama mfano bora, ruwaza adhimu kabisa kwa wanadamu wote. Ni kwa sababu hiyo kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfanya aianze safari yake ya maisha kuanzia kwenye hali ya chini kabisa kama yatima, kisha akampitisha katika kila hatua ngumu ya maisha mpaka mwishowe akamnyanyua kwenye kilele cha utawala na mamlaka, kama mtume na kama mkuu wa dola; ili watu waweze kupata mfano kamili kabisa wa menendo kutoka kwake, katika kiwango chochote cha hali ya kijamii watakachokuwamo, na kuufikia kwa uwezo wao wote mfano huo anaoutoa. Jambo hilo laweza kufikiwa tu kwa kumpenda Mtukufu Mtume

ﷺ na kuishi katika ulimwengu wa ukamilifu wake wa kimaanawi na kiroho.

Mtukufu Mtume ﷺ ni kiongozi wa dini na ni mkuu wa dola. Yeye ni mfano halisi kwa wale wanaoingia katika bustani la mapendo ya Mungu, lakini haachi kushukuru na kunyenyekea pale anapojazwa baraka na neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama alivyo mfano wa subira na kumtegemea Mwenyezi Mungu katika nyakati ngumu, ndivyo alivyo mfano wa ukarimu na kujinyima wakati anapopata ngawira. Yeye ni mfano wa huruma kwa familia yake, vivyo hivyo ni mwenye huruma sana kwa watumwa, wanyonge na waliopotea. Ni mwenye roho nzuri na ukarimu mkubwa kwa wale wanaomkosea.

Kama wewe ni tajiri, basi tafakari juu ya unyenyekevu na ukarimu wa Mtume huyo Mtukufu aliyeitawala Arabia yote na akazivuta nyoyo za kila Mwarabu mashuhuri kwa moyo wa upendo…

Kama wewe ni miongoni mwa wanyonge, angalia na jifunze namna Mtukufu Mtume ﷺ alivyoishi mjini Makka chini ya shinikizo la kutisha na ukandamizaji wa waabudu masanamu…

Kama umepata ushindi, fikiria juu ya Mtume mwenye ujasiri na kuridhika ambaye, aliwashinda maadui katika vita vya Badr na Hunayn …

Lakini – Mungu aepushie mbali – kama utakuwa umeshindwa, mkumbuke Mtume ﷺ aliyekuwa akitembea kwa uvumilivu baada ya kujeruhiwa na akiwa amewapoteza masahaba zake katika vita vya Uhud katika kutekeleza maagizo ya Mwenyezi Mungu …

Kama wewe ni mwalimu, mfikirie Mtume ﷺ alivyokuwa laini wa moyo, msikivu na mvumilivu katika kufikisha lulu za moyo wake kwa wanafunzi wa *Suffa* katika msikiti wake (Masjidun – Nabawi)…

Kama wewe ni mwanafunzi, vuta picha ya Mtume ﷺ akiwa amekaa mbele ya Jibril عليه السلام kwa adabu, usikivu na shauku kubwa akiwa amemletea wahyi…

Kama wewe ni mtoa mawaidha au mhubiri unayewaita watu kwenye mambo mema, basi isikilize sauti tamu ya Mtume ﷺ akitoa cheche za hekima kutoka moyoni mwake kwenda kwa masahaba msikitini …

Kama huna mtu wa kukutetea na kukusaidia kueneza neno la haki na kuliinua, basi yatazame maisha ya Mtume ﷺ aliyetangaza neno la haki kwa watu wajinga na kuwaita kwenye uongofu katika kipindi ambacho alikuwa hana msaada wowote mjini Makka…

Kama umeivunja ngome ya maadui, ukawadhoofisha na kuuangamiza uovu kwa lengo la kutangaza haki, basi uvute mbele ya macho yako muonekano wa Mtume ﷺ siku ya ushindi wa Makka akitembea kwa unyenyekevu hali ni mwenye kushukuru, akaingia katika ardhi takatifu ya Makka akiwa juu ya ngamia kana kwamba anataka kusujudu kutokana na kunyenyekea licha ya kuwa ni kamanda aliyekuwa amepata ushindi ….

Kama unamiliki shamba na ukataka kuratibu mambo ya shamba lako, jifunze kwa Mtume ﷺ alipofanya uteuzi makini wa mtu anayeweza kumudu na kuendesha mashamba ya Banu Nadir, Khaybar na Fadak baada ya kuyaweka chini ya himaya yake …

Kama wew ni mpweke, mfikirie yatima huyu aliyekuwa kipenzi cha Abdullah na Aminah …

Kama wewe ni kijana, yatafakari kwa undani maisha ya kijana huyu, aliyetarajiwa kukabidhiwa jukumu la Utume, akichunga kondoo wa Abu Talib mjini Makka …

Kama wewe ni mfanyabiashara unajiandaa kutoka na mizigo ya bidhaa, tafakari juu ya uaminifu wa mtu mtukufu zaidi alivyotoka na msafara wa biashara kuelekea Yemen na Damascus …

Kama wewe ni hakimu, kumbuka uadilifu na busara za Mtume ﷺ katika kuamua kadhia ya kuweka jiwe jeusi kwenye ukingo wa Kaaba na kuepusha mauaji ambayo yangetokea …

Yageuze macho yako tena kwenye historia na mtazame Mtume ﷺ kwa mara nyingine akiwa amekaa katika msikiti wa Madina akitoa hukmu mbalimbali katika namna ya uadilifu wa hali ya juu na kutenda haki sawa baina ya maskini dhaifu na tajiri mwenye kuheshimika …

Kama wewe ni mume, fikiria hisia ya upendo na huruma kubwa aliyokuwa nayo mume mtukufu wa Bibi Khadija na Bibi Aisha رضي الله عنها…

Kama wewe una watoto, jifunze mwenendo mzuri wa baba yake Fatimah, babu wa Hassan na Husayn …

Sifa yoyote utakayokuwa nayo, na mazingira yoyote yale yatakayokukabili, utamkuta Muhammad Mustafa ﷺ akiwa kama mwalimu kamili na muongozo wako mzuri kila wakati na kila mahali.

Ni mwalimu ambaye mtu anaweza kusahihisha makosa yake yote kwa kufuata Sunnah zake na hatimaye akaweza kurejesha kila kitu mahali pake na kurekebisha nguvu na juhudi zilizopotea.

Kwa kufuata nuru ya muongozo wake unaweza kuondoa vizuizi katika njia yako na kujikuta umeifikia milango ya furaha …

Kama wataka kujiokoa dhidi ya kuwa mtumwa wa maada ukataka kuishi maisha ya kiroho, basi angalia mfano wa watu kama Bilal, Yasir na Thawban رضي الله عنهم, ambao walilelewa na Mtukufu Mtume

ﷺ. Suhubiana nao kwa uaminifu ili uweze kupata moyo wenye kiwangocha juu cha hisia, ukuu na wepesi wa kuelewa mambo. Kumbuka kwamba watu wajinga walibadilishwa na kuwa nguzo za uaminifu kupitia muongozo na juhudi za Mtukufu Mtume ﷺ na kuendelea kushikamana naye. Qitmir, mbwa wa as-haabul-Kahf, alipata Baraka kwa kuandamana tu na watu wema. Kwa upande mwingine, muangalie mke wa Nabii Laut عليه السلام na mtoto wa Nabii Nuh عليه السلام, Kanan, walikumbwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuchanganyikana na watenda maovu. Wao pamoja na watu wa mfano wao walizama katika tope la nafsi zao, wakafikwa na mwisho mbaya kama madhalimu waliosuhubiana nao.

Kisha jitahidi kuzitumia siku zako zilizobaki kuwa pamoja na wanafunzi watiifu na wema wa Mtukufu Mtume ﷺ ili usiishie kuwa miongoni mwa majahili.

Maisha yake ni mfano wa bustani iliyopambwa kwa maua mazuri na mawaridi yenye kutoa harufu ya miski. Muonekano wake wa ajabu unaelezea ukamilifu wa ulimwengu wake maridhawa wa kiroho. Thamani na hadhi yake isiyokifani mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inaelezwa ndani ya Qur'an Tukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ. يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

"Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa

kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui." (al-Hujurat: 1-2)

Hivyo, Qur'an Tukufu inawataka Waislamu wote kumheshimu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Licha wa kuwaita mitume wengine wote kwa majina yao, Qur'an Tukufu haimuiti Mtukufu Mtume ﷺ moja kwa moja kwa jina lake, na badala yake inatumia vyeo kama vile '*Nabii*' au '*Rasul*'. Wakati huohuo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaamrisha Waislamu kufanya vivyo hivyo:

لَا تَجْعَلُوا دُعَاءِ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُم بَعْضًا

"Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi…" (an-Nur: 63)

Aya hii inabainisha kuwa ni kinyume na adabu ya Muislamu kumuita Mtukufu Mtume ﷺ kwa kutumia jina lake tu, huku ikisisitiza umuhimu wa kuliambatanisha na sifa zake kuu na adhimu. Hivyo, mtu anapolitamka jina lake anatakiwa kuliambatanisha na vyeo vyake kama, *Nabii*, *Rasul*, *Rasulullah* na *Habibullah* na kwa mujibu wa amri ya aya ya 56 ya Surat al-Ahzab, linapotajwa jina lake tunatakiwa kumtakia rehma. Hili ni eneo muhimu la adabu ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu atataka tuwe nazo kwa Mtume Wake ﷺ na ni amri zinazotakiwa kufuatwa na ummah wake wote. Qur'an Tukufu inasema:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ
آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu." (al-Ahzab, 56)

Mtukufu Mtume ﷺ sio tu kwamba alikuwa mwalimu aliyefundisha Qur'an kwa maneno, bali pia aliishi kwa mujibu wa Qur'an hiyo. Katika *hadith* moja iliyosimuliwa na Jabir ﷺ, anasema, "Mwenyezi Mungu alinituma kuja kukamilisha tabia njema." (Muwatta', Husn'ul-Khuluq)

Vitabu vyote vya Kiislamu vilivyoandikwa kwa zaidi ya miaka1400 iliyopita vimekuwa na lengo moja la kuielezea Qur'an Tukufu, na kumuelezea mtu mmoja tu, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ ni maisha adhimu sana kiasi kwamba hata Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa maisha hayo: لَعَمْرُكَ "Naapa kwa umri wako!" (al-Hijr, 72)

Kuwa karibu na hakika ya Muhammad huwezekana kwa upendo tu, sio kwa akili. Na bila shaka, Hakika hiyo ndiyo inayofichua maajabu yote. Kuchukua fungu katika mfanona ruwaza njema ya Mtukufu Mtume ﷺ, kujiweka mbali na anasa za kupita za nafsi, kudumisha ibada na kushikamana na hekma iliyoficha siri zote za utii; hayo ndiyo yanayompa mtu njia inayoelekea kwenye hiyo Hakika. Mtu anapoanza kupatata sehemu ya Hakika ya Muhammad, huwa kiumbe mwenye kupendeza, ambaye nuru na ukweli wa siri za ishara za Mwenyezi Mungu hufunuka mbele yake.

Siri za Qur'an huwekwa wazi mbele ya moyo wa mtu mpaka kwenye kina cha chini kabisa kwa kuungana na hali ya kiroho ya Mtukufu Mtume ﷺ. Na kuhusu kumtii na kumfuata Mtukufu Mtume ﷺ, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا
وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

"Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu." (al-Hashr, 7)

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ

"Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu." (Muhammad, 33)

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُوْلَـئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم. مِّنَ النَّبِيِّينَ
وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاء وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ. أُولَـئِكَ رَفِيقاً

"Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!" (an-Nisa, 69)

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ
وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ. قُلْ أَطِيعُواْ اللَّهَ وَالرَّسُولَ
فإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنَّ اللَّهَ لاَ يُحِبُّ الْكَافِرِينَ

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu. Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri." (Al-i Imran, 31-32)

وَمَن يُطِعِ اللّٰهَ وَرَسُولَهُ وَيَخْشَ اللّٰهَ وَيَتَّقْهِ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ

"Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu." (an-Nur, 52)

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاء بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللّٰهَ وَرَسُولَهُ أُوْلَـئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللّٰهُ إِنَّ اللّٰهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

"Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima." (at-Tawbah, 71)

مَّنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللّٰهَ وَمَن تَوَلَّى فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظاً

"Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao." (an-Nisa, 80)

أَلَمْ يَعْلَمُواْ أَنَّهُ مَن يُحَادِدِ اللّٰهَ وَرَسُولَهُ فَأَنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِداً فِيهَا ذَلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ

"Je, hawajui ya kwamba anaye shindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi huyo atapata Moto wa Jahannamu adumu humo? Hiyo ndiyo hizaya kubwa." (at-Tawbah, 63)

وَأَطِيعُواْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلاَ تَنَازَعُواْ فَتَفْشَلُواْ وَتَذْهَبَ
رِيحُكُمْ وَاصْبِرُواْ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

"Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri." (al-Anfal, 46)

Kutetemeka na kuhisi shani na haiba inayopatikana kwa kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ na kuanza kuusafisha moyo dhidi ya uchafu wote wa nafsi, ni dalili kuwa Muumini husika ameingia katika njia ya kulipata fungu la upendo wa Mtukufu Mtume ﷺ na maadili yake ya mfano.

Mashujaa wa moyo, ambao, baada ya kulipata fungu lao katika maadili ya Mtukufu Mtume ﷺ waliyozama ndani yake, wameendelea kutoa mifano adhimu, wakionesha maana ya kumpenda Mtume ﷺ. Uhai ndio walioupata katika hakika na dhati ya Mtume ﷺ.

Miongoni mwa mashujaa hao ni Sayyid Ahmad Yasawi, walii mkubwa kutoka Turkistan, ambaye baada ya kufikisha umri wa miaka sitini na tatu, umri aliokuwa nao Mtume ﷺ alipofariki dunia, aliona kuwa haistahili tena 'kutembea juu ya ardhi', akachimba shimo kubwa kama handaki na kuamua kumalizia maisha yaliyobaki huko shimoni.

Uways al-Qarani aliposikia habari kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwahi kuvunjika jino wakati vita ya Uhud, akiwa hajui jino gani hasa, aliamua kutenganisha kila jino kinywani mwake. Alipata faraja baada tu ya kuling'oa kila jino, kwa namna ambayo aliweza kuondokana na utata wa jino husika, ambalo aliliona kuwa linamzuia kuzama ndani ya uhai wa Mtume ﷺ. (Fariduddin Attar, uk. 23)

Imam Malik ﵁ ni shujaa mwingine aliyeishi kila hatua ya maisha yake katika shauku ya kutaka kuungana na Mtukufu Mtume ﷺ. Kamwe hakuwa akipanda farasi akiwa mjini Madina kutokana na kuuheshimu mji huo. Daima İmam huyo alizungumza kwa sauti ya chini anapokuwa katika eneo la *Rawdhah*, eneo lililo baina ya *minbar* na kaburi la Mtukufu Mtume ﷺ. Ndiyo maana Khalifa wa wakati huo, Abu Jafar Mansur, alipoinua sauti yake mahali hapo, Imam hakusita kumuonya:

"Shusha sauti yako katika eneo hili ewe Khalifa. Mwenyezi Mungu aliwahi kuwaonya watu waliokuwa wabora zaidi kuliko wewe!" Kisha akalihitimisha onyo lake kwa kumkumbusha Khalifa aya ifuatayo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ
بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

"Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui." (al-Hujurat, 2)

Siku moja Imam Malik alimsamehe Gavana wa Madina aliyekuwa amemletea shida, akamwambia, "Siku ya Kiyama sitajisikia vizuri kabisa kutaka haki zangu kutoka kwa dhuria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ."

Katika kuelezea jinsi moyo wake ulivyokuwa umejaa upendo wa kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ, Bezm-i Alem Valide Sultan aliandika:

Kutokana na upendo, Muhammad alizaliwa,
Bila Muhammad…upendo utabaki na upweke…

Mwaka 1678, mshairi wa Kiuthmaniyya, Naabi alifanya safari ya hijja akiwa na maafisa kadhaa wa serikali. Walipoukaribia mji wa Madina, shauku na msisimko vilimtamalaki mshairi huyo na kupoteza kabisa usingizi. Wakati huohuo alimuona afisa akiwa amelala bila kujitambua huku akiwa ameinyoosha miguu yake kuelekea upande wa mji wa Madina. Akiwa amehuzunishwa na kitendo hicho, Naabi akaanza kuandika utenzi wake maarufu kwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Msafara wao ulipokuwa umbali mfupi kabisa kutoka Msikiti wa Mtume ﷺ, kwa mshangao mkubwa Naabi akausikia utenzi wake ukisomwa kwa sauti kwenye mnara:

Jizuie na utovu wa adabu kwani hii ni ardhi ya kipenzi cha Allah,

Hili ni eneo linalotazamwa na Allah na ni eneo la Mtume,

Ee Naabi ingia katika eneo hili tukufu kwa sharti la kuchunga adabu,

Hili ni eneo linalotembelewa na watakatifu na mahali panapotukuzwa na Mitume…

Akiwa na msisimko mkubwa kiasi cha kukaribia kutoamini kilichotokea, Naabi alielekea haraka kwa muadhini na kumuuliza alipoutoa utenzi ule.

Akamwambia: "Usiku wa jana tuliona ndoto ambapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituambia, 'Mshairi mmoja katika umma wangu aitwaye Naabi anakuja kunitembelea; ni mtu ambaye amejawa sana na upendo wangu. Hivyo mkaribisheni kwa utenzi wake mwenyewe kutokea kwenye minara ya Msikiti huu'. Hivyo tulikuwa tunatekeleza agizo hili."

Hapo hapo Naabi alilia kwa furaha. "Kwa hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu amenielezea kama mtu katika umma wake",

alisema wakati akilia. "Kwa hiyo amenipokea kuingia katika ummah wake…"

"Ni nuru ya kipekee ambayo hata jua linaizunguka", ni maneno yanayopatikana katika utenzi wa shairi moja la Suleyman Çelebi, mtunzi wa *Mawlid*, ambaye anaona kuwa hata jua linamzunguka Mtukufu Mtume ﷺ, akielezea kuwa hata vitu vinampenda kwa upendo wa ajabu kabisa.

Sultan Suleyman Mkuu, ambaye aliandika mashairi kwa jina la *'Muhibbi'*, anatuma ombi lifuatalo kwa Mtukufu Mtume ﷺ:

Wewe ni nuru ya ulimwengu, Kipenzi cha Mola,
Usiwafukuze, hata kidogo, mlangoni kwako wale wanaokupenda…

Ali رضي الله عنه anasimulia:

"Nilikuwa nikitembea pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mjini Makka. Siku moja tukaenda nje ya mji wa Makka. Kila jiwe na kila mti vilikuwa vikimtolea salamu kwa kusema, 'Baraka na amani ziwe juu yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!'" (Tirmidhi, Manaqib, 6/3626)

Ufuatao ni mfano mwingine unaoonesha kuwa hata vitu vinampenda Mtume ﷺ:

Katika safari moja ya kivita, Mtukufu Mtume ﷺ alimlingania Uislamu Bedui mmoja aliyekutana naye. Bedui akamtaka atoe uthibitisho wa utume wake. Mtukufu Mtume ﷺ akauashiria mti uliokuwa mbele yake, akauita uje mbele yake. Hapo hapo mti ule ukaitikia amri ya Mtume ﷺ, ukaja kwa nguvu na kukita mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kutamka tamko la shahada mara tatu. Bedui alistaajabu sana na aliyoyaona, akabaki mdomo wazi na kusema wakati akijiandaa kwenda kwa watu wa kabila lake, "Watu

wa kabila langu wakinisikiliza, nitawaleta kwako; wasiponisikiliza nitarejea mwenyewe na kuandamana nawe!" (Haythami, VIII, 292)

Sio vitu tu,bali hata wanyama walimtambua Mtume ﷺ na kumtii. Tukio moja linasimulia na jabir ibn Abdullah رضي الله عنه:

"Siku moja tulikuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tukirejea kutoka vitani. Tulipokaribia mabustani ya Ibn'n-Najjar mjini Madina, tulikuta kuna ngamia katika bustani moja ambaye alikuwa akimshambulia kila anayejaribu kuingia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alielezwa kuhusu hali hiyo. Hivyo alienda, akaingia kwenye bustani na kumuita ngamia aliyekuwa akiwashambulia watu. Aliposikia sauti ya Mtume ﷺ, aliinamisha kichwa chake kiasi kwamba mdomo wake ukawa unagusa ardhi, na kwa unyenyekevu mkubwa akatembea kuelekea mahali alipokuwa, akapiga magoti na kukaa.

'Nipeni kamba', alisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Baada ya kumfunga kamba shingoni alimkabidhi mmiliki wake, kisha kasema, 'Tofauti na wanadamu na majini walioasi, viumbe wote mbinguni na ardhini wanatambua kuwa mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.'" (Ahmad, III, 310)

Yatupasa kutafakari na kuitathmini upya ikhlasi ya utii na usikivu wetu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ tukilinganisha hali ya upendo mkubwa waliyo nayo wanyama na vitu kwa Mtume ﷺ...

Tuna haja kubwa sana ya halı yake ya kiroho, hususan katika zama hizi za shida na tabu; tabu inayomsukuma mshairi kumuita Mtukufu Mtume ﷺ: "Inuka, ewe Mwalimu wa Ulimwengu, kwa maana Siku ya Kiyama imekaribia!"

Ukubwa ulioje wa faraja tunayoipata ndani ya *salawat*, salamu tunazomtakia Mtume na ambazo huufanya uhusiano wetu naye kudumu milele ndani ya upendo wetu kwake…

Waislamu makini wenye moyo safi wameichukulia kuwa kuwa karibu na hakika ya Mtume ﷺ kwamba ni baraka kubwa duniani kwa kuziacha nafsi zao zipite katika njia yake ya kiroho; na matokeo yake wakazama katika ladha na shauku kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Shakhsia adhimu ya Mtukufu Mtume ﷺ ambayo tumekuwa tukijaribu kuielezea kwa mukhtasari ndani ya maneno yenye kikomo, ni mionzi tu inayoakisi uelewa wetu kutoka kwa Mtukufu Mtume, Nuru ya Viumbe. Siri ya *wasl ila'Allah*, yaani kufika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, inapatikana kwa kukielewa sana Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume Wake, kwa moyo salama, na kwa kuwapenda wale wanaopendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na kuwachukia wale wanaochukiwa nao. Tofauti kati ya mambo hayo mawili na mfano wa umbali mkubwa uliopo baina ya *a'la-i iliyyin* na *asfal-i safilin*, yaani wa juu zaidi ya waliyo juu na wa chini zaidi ya walio chini. Kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ na kuvichukia vyote anavyovichukia ni kichocheo kikuu kabisa katika kumuweza mtu kunufaika na hali yake ya kiroho.

Waumini, ambao katika kipindi chote cha historia wameweza kufuatisha mfano bora wa Mtukufu Mtume ﷺ, wameweza kufikia kilele cha *iman*; na kwa kuikamilisha silika ya kutenda wema iliyo ndani ya *fitrah*au maumbile yao, wakawa kama nyota zing'arazo katika kutoa mifano inayotakiwa kuigwa na wenzine.

Hiyo ndiyo Hakika au dhati ya Muhammad iliyoelezwa kwa kiwango cha uelewa kinachoweza kubebwa na mwandishi asiye stadi na kustahmiliwa na maneno yenye kikomo…

Lazima tukiri kuwa maneno yaliyotumika katika kitabu hiki kwenye mada zake mbalimbali, zinazojulikana na zisizojulikana, ni mithili ya matone machache kutoka kwenye bahari isiyokuwa na mipaka. Na sasa yamekoma yakiwa yametahayari mbele ya milango ya ukimya usiokuwana kikomo.

Ewe Mwenyezi Mungu…Ifanye juhudi hii ndogo, iliyoelemewa na maneno yenye kikomo, kuwa sababu ya kupata rehma zako tele na utujaalie kupata fungu katika Hakika ya Muhammad! Tujaalie tupate shufaa na uombezi wa Mtume Wako ﷺ, ambaye ni chimbuko na chemichemi ya upendo!

Amiin…

HITIMISHO

Kwa kuwa Uislamu ni dini ya ulimwengu na inayoyatazama na kuyatawala maisha yote, sio tu kwamba ni lazima iwe imebeba kanuni za mafundisho yote kama vile sheria, maadili na uchumi zitakazouongoza mwenendo wa mwanadamu, bali pia ni lazima itakuwa imebeba viwango na mifumo ya juu kabisa, kuanzia ile iliyo rahisi kabisa na thabiti mpakaile yenye kutatanisha na ya kinadharia. Kwa kuwa inajumuisha mambo rahisi yahusuyo maisha ya kila siku, baadhi ya kanuni hizi za Uislamu zinamhusu kila mtu. Hata hivyo, baadhi yana ukweli juu ya mambo ya ndani kabisa yenye uwezo wa kuziacha akili katika mshangao mkubwa. Kwa hiyo, ugumu unaoandamana na ugunduzi wa mambo hayo, hususan katika vitabu vilivyoandikwa kwa lengo la kuyafikisha, huondoka kabisa. Kwa maana nyingine, hiyo inaweza kutofautishwa na jaribio la kutambaa juu ya mlima mrefu, ukijiandaa kukabiliwa na kiu kali na kazi ngumu njiani. Hakika kazi ya kujaribu kuufanya ukweli huo mgumu kuwa rahisi kwa kutumia vipawa vyenye kikomo vya lugha limekuwa jambo zito na gumu kulikamilisaha. Hata hivyo, mafanikio kamili yalinabaki kuwa jambo lenye kutamaniwa daima.

Vyovyote mambo haya yatakavyokuwa nje ya uelewa wa mwanadamu, kanuni ya Uislamu inamtaka mtu asimame imara na asiitelekeze sehemu ya kitu ambacho hakieleweki kwa urahisi. Kwa sababu hiyo, tunawahimiza wasomaji wetu watupatie faida za shaka kwa kutuona kuwa tumetekeleza kanuni hiyo na watusamehe kwa upungufu wa uelewa na maelezo yetu.

Kitu kingine ambacho yatupasa kukikumbuka hapa ni kwamba uelewa wa mwanadamu hujitengeneza wenyewe kutokana na mgandamızo na maono yatokayo kwenye ulimwengu wa akili na uelewa. Hivyo, ugumu wa kuepuka makosa katika kuyatambua na kuyaelezea kikamilifu masuala yenye siri ambayo yamevuka mipaka ya uzoefu wa kibinaadamu ni sawa sawa na ugumu wa kuielewa na kuielezea kikamilifu hakika na dhati ya Mtukufu Mtume ﷺ, muujiza wa uumbaji, na kukielezea kito adhimu, yaani Qur'an Tukufu, dhihirisho kamili la majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Pepo, Moto na taswira nyingine kama hizo ni misemo ambayo imewekwa kulingana na uelewa wetu, lakini uhalisia wake hasa anaujua Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee. Tathmini zote zinazofanywa na akili na moyo salama kuhusu ukweli wa kimaanawi wa Uislamu ni za kweli, japokuwa akili hiyo haiwezi kuzielezea kwa usahihi. Ni za kweli; kwa kiwango tu cha uelewa wetu na kwa kiasi cha maelezo yetu, ambayo yamefungamanishwa na mawazo yatokayo kwenye ulimwengu wa akili. Lakini mawazo yetu hayo hayatoshi, yana upungufu. Tofauti iliyopo baina ya mambo haya ya kimaanawi na taswira inayopatikana katika ulimwengu wa akili ambao ndio msingi wa uelewa wetu, ni kubwa isiyokuwa na kikomo wala mwisho. İli kuuelewa ukweli huu wa kimaanawi, kunahitaji aina nyingine ya uelewa, uwezekano wa wazi na njia sahihi. Kwa mfano, *ruyatullah,* yaani kumuona Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama. Mtu hawezi kufanya lolote zaidi ya kustaajabu iwapo 'kuona' kunatosha kuelezea tukio ambalo Waumini watakutana nalo siku ya Kiyama. Hakika haitoshi, bali ina umuhimu katika kuelezea jambo litakalotokea.

Hivyo, linabaki kuwa jambo lisilowezekana kwa wanadamu kuchukua zaidi ya kile kinachoweza kubebwa na vikombe vyao

kutoka kwenye bahari kubwa ya ukweli, kama ambavyo haiwezekani kuijaza bahari yote ndani ya kikombe. Kikombe hapa ni lugha; ni akili. Jicho ni kikombe kwa upande wa suala la kuona.

Katika aya ifuatayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea Ukuu Wake ambao upo nje ya uwezo wa uelewa wa mwanadamu:

قُل لَّوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لِّكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ
قَبْلَ أَن تَنفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي وَلَوْ جِئْنَا بِمِثْلِهِ مَدَدًا

"Sema: Lau kuwa bahari ndio wino kwa maneno ya Mola wangu Mlezi, basi bahari ingelimalizika kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu Mlezi, hata tungeli ileta mfano wa hiyo kuongezea." (al-Kahf: 109)

Yampasa mtu kutafakari, je kikombe cha mwanadamu kina uwezo gani kulinganisha na ukuu na adhama ya Mweneyzi Mungu isiyokuwa na kikomo?

Sio kama Hakika itajizuia dhidi ya upungufu wa uelewa na ufafanuzi!

Maana ambayo inaweza kubebwa na kila neno inaweza tu kutoa maudhui yanayoendana na uelewa wa mtu anayeilezea. Hivyo, baadhi ya dhana kama vila Mwenyezi Mungu, ulimwengu na roho zina kina na undani usiokuwa na kikomo wala mpaka. Wale wanaozitumia dhana hizo katika mazungumzo na maandishi yao wanaweza tu kuzama ndani ya dhana hizo kwa kile kiwango tu cha uelewa wao. Hilo pia lipo kwa upande wa msikilizaji au msomaji.

Miongoni mwa dhana hizo ambazo maudhui zake zinakwenda nje ya uelewa wa mwanadamu ni majina matukufu ya Mtukufu Mtume ﷺ. Hivyo tunataraji rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu,

na tunamuomba atusamehe kwa upungufu wetu katika ufikishaji wa maudhui ya majina hayo na udhaifu wa wasomaji wetu katika kuyaelewa.

Kwa mara nyingine, hatuna budi kurejea kwenye kimya, kitu ambacho kinashikilia matumaini yetu makubwa ya kushikamana na Haki, na hivyo kuyahitimisha maneno na maelezo yetu.

Hatuna ponyo jingine zaidi ya kuingia katika hali ya kiroho ya Mtume Muhammad Mustafa ﷺ! Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Ponyo halisi la waliokata tamaa…

Dahilak Ya Rasulallah…

YALIYOMO

MWAKA WA KWANZA WA HIJRA / 7

Maisha ya Mtume Aliyebarikiwa ﷺ Katika Mji wa Madina..... 7

Abu Ayyub al-Ansari:
Mbeba bendera wa Mtume Aliyebarikiwa ﷺ..... 9

Anas ibn Malik: Mtumishi wa Mtukufu Mtume ﷺ..... 11

Maridhiano ya Undugu baina ya Muhaajiruun
na Ansaar: Muakhaat..... 14

Ubora wa Muhajiruun na Ansaar..... 18

Ubora wa Muhajiruun na Ansaar..... 31

Tangazo la mji wa Madina kuwa Eneo Takatifu..... 37

Soko la Madina na Udhibiti wa Shughuli za Kibiashara..... 39

Masjid'un-Nabi na Ujenzi wa Nyumba ya Mtume ﷺ 44

Kuhamasisha Swala ya Jamaah 53

Adhana ya Kwanza 59

Suffa: Shule ya Maarifa na Hekima 62

Mtukufu Mtume ﷺ Amuoa Bibi Aisha رضي الله عنها..... 70

Hali ya Mji wa Madina..... 72

Ruhusa ya Kupigana: "Wapigeni wale Wanaokupigeni!"..... 77

Kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu 81

Baadhi ya Harakati ndogo ndogo za Kijeshi 90

MWAKA WA PILI WA HIJRA / 95

Batn'u Nakhlah na Harakati nyingine za Kijeshi 95
Kubadilisha Uelekeo wa Qibla 99
Funga, Zakatul-Fitr na Zaka 104
Itikafu 116
Vita ya Badr Kubwa (17 Ramadhan 2/ 13 Machi 624) 119
Msaaada wa Malaika 139
Simba wa Badr 145
Safari ya kurudi kutoka Badr 151
Muamala kwa Mateka wa vita 153
Hukumu ya Ngawira 166
Kifo cha Kishahidi 169
Zaynab رضي الله عنها Awasili Madina 176
Mayahudi na Vita vya Banu Qaynuqa
(Shawwal, 2/ Aprili, 624) 179
Tukio la Sawiq (Dhil-hijjah, 2/ Mei, 624) 185
Ndoa ya Ali na Bibi Fatimah رضي الله عنهما 186
Ahl'ul-Bayt na kuwapenda 192

MWAKA WA TATU WA HIJRA / 197

Uhud: Vita iliyobeba Hekma na Mazingatio 197
Shauku ya Maswahaba kufa kishahidi 201
Hamza, Bwana wa Mashahidi Wote 207
Saad ibn Rabi': Swahaba aliyefunga Mlango wa Udhuru 221

Mashahidi wa Uhud 222
Tunaipenda Uhud nayo yatupenda..... 230
Mafunzo yanayopatikana katika Vita vya Uhud..... 231
Hamra'ul-Asad (8 Shawwal, 3 / 24 Machi 625)..... 234
Suala la Mirathi 237

MWAKA WA NNE WA HIJRAH / 242

Tukio la Raji (Safar 4 / Julai, 625)..... 242
Tukio la Bi'r Maunah (Safar, 4 / Julai, 625) 248
Njama chafu ya Usaliti wa Banu Nadhir 251
Kuharamishwa Pombe/Vileo na Kamari..... 257
Dhatur-Riqah..... 263
Vita vya Badr Ndogo (Dhilqadah, 4/ Aprili, 626)..... 269

MWAKA WA TANO WA HIJRA / 272

Salman Farisi Aukubali Uislamu na Kuachiwa Huru 272
Kufutwa kwa Desturi ya Kuwaasili Watoto 281
Amri ya Kujisitiri: Hijabu 286
Vita vya Muraythi
(Shaban-Ramadhan, 5 / Januari-Februari, 627) 289
Tayammum..... 292
Tukio la Ifk au Kashfa na Uzushi 294
Hao ni maadui...Tahadhari nao!..... 302
Majaribu Thakili na Mtihani Mzito:
Vita vya Khandaq (Shawwal-Dhilqadah, 5/ Machi, 627)..... 307
Habari Njema Wakati wa Kuchimba Khandaq.....311

Baraka Tele katika Chakula cha Jabir 313
Shida na tabu zilizowafika wakati wa Khandaq..... 317
Misimamo ya Ujasiri katika Vita vya Khandaq..... 321
Vita ni Hadaa..... 326
Kuelekea kwa Banu Quraydha
(23 Dhilqadah, 5/ 15 Aprili, 627)..... 329

MWAKA WA SITA WA HIJRA / 335

Mkataba Wa Hudaybiyah: Msingi Wa Ushindi Wote
Na Kichocheo Muhimu Cha Kurudi Makka 335
Kiapo cha Utii cha Ridh-waan: Tukio lililoridhiwa
na kumfurahisha Mwenyezi Mungu 340
Mkataba wa Hudaybiyah: Awamu Mpya
Kabisa katika Kazi ya ulinganiaji 343
Ushindi wa Wazi: Uwongofu Wenye Kuendelea Milele..... 352

MWAKA WA SABA WA HIJRA / 359

Kuwalingania Wafalme Mbalimbali Kwenye Uislamu 359
Kutupiwa Sihiri na Mayahudi 380
Pigo la Mwisho Dhidi ya Uadui wa Mayahudi: Ufunguzi
wa Khaybar (Safar-Rabiulawwal, 7 / Juni-Julai, 628) 382
Umakini Katika Kuchunga Haki za Wengine 392
Daws awasili Mjini Madina 394
Kurejea kwa Wahamiaji wa Abyssinia..... 395
Njama ya Mayahudi Kumpa Sumu Mtukufu Mtume ﷺ 397
Kadhia ya Ndoa ya Mutah 399
Kurejea Kutoka Khaybar..... 401

Umrat'ul-Qada (Dhilqada, 7 / Machi, 629)..... 404

MWAKA WA NANE WA HIJRA / 410

Kifo cha Zaynab, binti wa Mtukufu Mtume ﷺ 410
Vita vya Mu'ta: Tukio la Kihistoria Lililoandikwa na Maswahaba Wachache (Jamadiyalawwal, 8 / Agosti-Septemba, 629) 411
Umahiri, na Ujasiri wa Khalid ibn Walid kama Kamanda..... 419
Ushindi wa Ufunguzi wa Makka:
Haki Imekuja na Batili Imeondoka 423
Siku ya Usamehevu..... 439
Kiapo cha Utii cha Watu wa Makka 445
Zirejesheni Amana kwa Watu Wake 446
Uaminifu wa Kipekee 451
Vita ya Hunayn (11 Shawwal, 8 / 1 Februari, 630) 453
Vita vya Awtas (Shawwal, 8 / Februari, 630) 459
Kuizingira Taif (Shawwal, 8 / Februari, 630)..... 459
Ugawaji wa Ngawira 462
Adhabu ya Kosa la Kumuua Muislamu..... 472
Kumteua Gavana na Mwalimu wa Makka 476

MWAKA WA TISA WA HIJRAH / 478

Upanga wa Fasihi 478
Chunguzeni Ukweli wa Habari !..... 484
Safari ya Kivita ya Tabuk: Mtihani Mkubwa wa Iman (Rajab, 9 / Septemba-Oktoba, 630) 486
Kushindana Katika Kujitolea 496
as-Saat'ul-Usrah: Nyakati za Shida Ngumu 501

Shahidi Wa Tabuk 510
Khiyana ya Wanafiki na Masjid'ud-Dirar 513
Tumetoka kwenye Jihad Ndogo kwenda
Kwenye Jihad Kubwa 515
Watatu Waliotubu 516
Hazina za Mbingu na Ardhi ni za Mwenyezi Mungu 523
Hakuna Faida kuwa Muislamu bila Ibada 524
Matukio Mengine Baada ya Tabuk 528
Mwaka wa Wajumbe Mbalimbali 531
Hajj: Hijja ya Wajibu 534

MWAKA WA KUMI WA HIJRA / 538

Adiy ibn Hatim aukubali Uislamu 538
Hijja ya Kwanza na ya Mwisho ya Mtukufu Mtume ﷺ:
Hijja ya Kuaga 541
Leo Nimekukamilishieni Dini Yenu 554
Mahali Iliposhuka Adhabu 556

MWAKA WA KUMI NA MOJA WA HIJRA / 562

Muungano na Mtengano Mkubwa: Safari Kuu
ya Kuelekea kwa 'Rafiki wa Juu kabisa' 562
Huzuni iliyouteka Ulimwengu Wote 580

USWAT'UL-HASANAH / 588

Ruwaza bora Iliyokamilika 588

HITIMISHO / 605

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1350 BOOKS IN **60 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org |